**MATENDO**
**MTAALA**

I. **MAELEZO KWA UJUMLA**.
   A. Mwalimu: F.C. DiPalma, Jr.
   B. Mtafsiri: Chris Mwakabanje
   C. Kila darasa linachukua dakika takribani 38.

II. **AINISHO NA MALENGO**.
   A. Kujifunza kwa kina kitabu cha Matendo.
   B. Kuelewa mahali pake na umuhimu wa kitabu katika Agano Jipya.
   C. Kupata maarifa ya matukio ya uongofu katika Matendo.
   D. Kufurahia mambo hayo na kuyatendea kazi yaliyomo ndani ya kitabu kwa kuiga upendo, ukarimu, ujasiri, maswala ya kiroho, na juhudi ya uinjilisti ya Wakristo wa kwanza.
   E. Kupata uelewa wa mpangilio wa kitabu.
   F. Kushukuru kukua kwa kanisa la awali na kuelewa jinsi lilivyokua.
   G. Kuelewa kusudi maalum la matukio mawili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu katika Matendo na kuweza kutofautisha kati ya huo na ule wa maji kwa ajili ya msamaha wa dhambi.

III. **VIFAA VINAVYOHITAJIKA WAKATI WA KUJIFUNZA**.
   A. Unapaswa uwe na:
      1. Biblia (swahili – UV, English – ASV, KJV, NKJV).
      2. Masomo kwa video 66.
      3. Notisi za kozi hii.

   B. Maoni (lakini tunapendekeza mno) fafanuzi (commentary) ya J. W. McGarvey ile ya awali katika Matendo, iliyochapwa mara ya kwanza mwaka 1862. Kuanzia hapo imetolewa na "Gospel Advocate" na "Guardian of True Foundation."

IV. **MAMBO YA KUFANYA KATIKA KOZI HII**:
   A. Usome kitabu chote cha Matendo angalau mara moja.
   B. Angalia kikamilifu katika video masomo yote 66.
   C. Usome kikamilifu notisi zote za darasani.
   D. Kamilisha kazi yote ya kudondoa (maelezo yapo chini).
   E. Wakilisha makala ya muhula (maelezo yapo chini).
   F. Fanya mitihani mitatu.
   G. Sharti uwe na jumla ya wastani wa maksi angalau 70.

V. **KAZI YA KUDONDOA**.
   A. Mistari ya kudodoa lazima iandikwe (au ichapwe) bila kutazamia mahali, kisha itumwe VBI kwa masahihisho. Mistari ni lazima itoke katika UV kama ulivyoonyeshwa katika fomu yako ya maombi ya kujiunga na VBI.

   B. Mistari yote ni sharti iandikwe ama kuchapwa kwa mkao mmoja (mara moja). Unaweza kujifunza zaidi na kuianza upya yote iwapo ulikosea, lakini unatakiwa kuanza upya yote na kuiandikwa katika mkao mmoja.

   C. Kwa kozi hii, mistari ifuatayo inapaswa kudondolewa:
   Matendo 1:8 — Matendo 8:4
   Matendo 2:38 — Matendo 8:38

| | |
|---|---|
| Matendo 2:41, 42 | Matendo 10:34, 35 |
| Matendo 2:47 | Matendo 17:30 |
| Matendo 5:29 | Matendo 17:30 |
| Matendo 5:41 | Matendo 22:16 |

D. Kazi ya kudondoa uiwasilishe VBI wakati unatuma mtihani wako wa tatu.

E. Maoni: Njia bora ya kudondoa ni kuandika mistari katika vijikadi ili kwamba iwe rahisi kwako kuipitia mara kwa mara muda wote unavyoendelea na kozi hii.

**VI. MITIHANI.**

A. Kuna mitihani mitatu ya kujaza (wa kwanza baada ya Matendo 8:4; wa pili baada ya 17, na wa tatu baada ya sura 28).

B. Unapokaribia sura 8 wasiliana nasi na omba mtihani wako wa kwanza. Unapokaribia sura 17, omba mtihani wa pili. Unapokaribia sura 28, omba mtihani wa mwisho.

C. Ukishapokea mtihani, unaruhusiwa kuuangalia na kujifunza.

D. Walakini, unapofanya mtihani, unatakiwa uufanye kikamilifu bila kutazamia kwenye notisi, Biblia, kitabu, n.k.

VII. MAKALA YA MUHULA.

A. Andika makala juu ya hotuba ya Paulo ya Matendo 17:22-31. Haswa, elezea kwa kadiri uwezavyo mambo ambayo tunaweza kujifunza kuhusu Mungu kutokana na mistari hii. Hata hivyo pointi zako ni lazima zitokane na Matendo 17, unaruhusiwa kutumia mistari mingine katika Biblia ili kutilia mkazo pointi zako kuu.

B. Makala inapaswa kuwa na kurasa angalau tano za kuchapwa kuacha nafasi mbili mbili (double spaced). Kama umeandika kwa mkono, makala inapaswa kuwa kurasa saba bila kuruka msitari (single spaced).

C. Makala itatakiwa unapotuma mtihani wako wa mwisho VBI pamoja na dondoa.

VIII. MAKSI.

A. Kazi ya kudondoa, makala ya muhula, na mitihani itasahihishwa tofauti tofauti.

B. Maksi za mwisho zitazingatia juu ya wastani wa kazi zako zote ulizopewa.

C. Unaweza kuomba ili ufafanuliwe na kufikiriwa juu ya maksi, lakini kwa vyovyote vile VBI ndiyo itakuwa na uamuzi wa mwisho.

IX. TUNZO.

A. Tunzo itatolewa, ikiwa ni pamoja na cheti, pale tu utakapokuwa umefanikiwa kumaliza kazi yako kikamilifu, kanda za video umerejeza (kama uliziazima), na ada yote kwa kozi hii umelipa.

B. Mungu na abariki kazi yako ya kujifunza neno lake lililovuviwa!

## MATENDO YA MITUME
## MAELEZO YA KIHITORIA

**KUANGALI KWA UJUMLA  MAELEZO YA KIHISTORIA:**

I. Jina (title).
II. Mwandishi.
III. Tarehe ya uandishi, kimechukua muda gani, na nyakati.
IV. Makusudi dhahiri makuu ya kitabu.
V. Umuhimu na nafasi ya kitabu cha Matendo katika Agano Jipya.
VI. Njia mbalimbali za kukichanganua kitabu cha Matendo.
VII. Vielelezo mbalimbali vya kitabu.

**I. JINA (TITLE):**

A. Hakuna jina la kitabu lililovuviwa – Luka hakutaja jina la kitabu.

B. Hivyo basi, jina lililotumika limetolewa na watu wasiovuviwa.

C. Jina lililozoeleka ni, Matendo ya Mitume – Lakini hili si ndilo jina lililo sahihi zaidi kutokana na sababu mbalimbali:
   1. Maandishi haya hayahusishi matendo ya *kila* mmoja wao.
   2. Yanaondoa matendo *mengi* ya mitume wengine *weng*i.
   3. Kusema ukweli, mbali na orodha ya 1:13, kitabu hiki kinawataja mitume wanne tu wa Kristo – Yakobo na Yohana (12:2) na Petro na Paulo.
   4. Kati ya hawa wanne, mkazo umetiliwa kwa maelezo mengi kwa mitume wawili – Petro na Paulo.

D. Kwa sababu hizi, jina sahihi la kitabu lingekuwa, Matendo ya Mitume Baadhi.
   1. Jina hili linabainisha zaidi kwamba kitabu kina baadhi ya matendo ya mitume wa Kristo.
   2. Kufuatana na hayo, tutakitaja kitabu ama kwa kukiita tu Matendo, Kitabu cha Matendo, au Matendo ya Mitume.

**II. MWANDISHI:**

A. Hakika, mwandishi ni Roho Mtakatifu (2 Pet.1:20,21; 1 Kor.2:9-13).

B. Lakini ni mwanadamu gani ambaye kwa huyo Mungu alifunua kitabu hiki?

C. Hakuna mahali panamwonyesha moja kwa moja ndani ya kitabu mwandishi mwanadamu.

D. Hata hivyo, idadi kubwa ya wanafunzi wa Biblia wanahatimisha kwa kumtaja Luka kuwa ndiye mwanadamu aliyetumiwa kuandika kitabu.
   1. Sababu moja anayopewa Luka kuandika kitabu hiki ni madai ya kwamba aliandika kitabu cha kwanza kwa mtu aliyeitwa Theofilo (1:1).
      a. Luka aliandika kitabu cha kwanza kwa mtu aliyeitwa Theofilo (Lk.1:1-4).
      b. Hii inadhihirisha kwamba Luka aliteuliwa na Mungu kuandika kitabu cha Matendo.
      c. Kwa nyongeza, Matendo kinaanzia pale kitabu cha Injili cha Luka kinapoishia, k.m. mahali alipopaa Kristo kwenda mbinguni (Matendo 1:2; Lk.24:51) na kisha kinatoa kwa mhutasari hatimisho la habari za Injili ya Luka (Matendo 1:2-4).
      d. Basi, vitabu hivi viwili vinaungana pamoja kwa karibu na kutoa ushahidi mkubwa kuwa viliandikwa na mtu mmoja.
      e. Kutokana na sababu hizi, ni wazi kwamba Luka ni mwanadamu aliyetumiwa na Mungu kufunua vitabu vyote hivi viwili.

2. Sababu zingine zinazotusadikisha kwamba Luka ndiye mwanadamu aliyetumiwa na Mungu kuandika Matendo zimeorodheshwa katika 3 na 4 hapo chini.
   a. Kwa nyongeza, kifungu E chini kinajumuisha maeleza ya kufurahisha ambayo yanaonyesha kuwa Luka alikuwa Mmataifa.
3. Sababu ya pili inayotufanya kusadiki kwamba Luka ndiye mwandishi ni muundo (style) na yaliyomo katika vitabu vyote viwili yanalingana na kushabihiana sana, kama inavyodhihirishwa katika pointi zifuatazo:
   a. Vitabu vyote viwili vinaandikwa haswa na Roho Mtakatifu.
      (1) Habari ya Injili ya Luka zinaeleza kile alichofanya Yesu baada ya Roho kushuka juu yake na kumpaka mafuta kwa ajili ya huduma yake (Lk.4:18).
      (2) Matendo inaelezea yale waliyofanya mitume baada ya Roho kushuka juu yao na kuwatia nguvu kwa ajili ya kazi (Mdo.1, 2).
   b. Habari ya Injili ya Luka zinatoa mazingira ya msingi ya Ukristo kuanzia kuzaliwa kwa Yesu hadi kufufuka kwake. Matendo kinatoa historia ya Ukristo kuanzia ufufuo wa Kristo hadi kufungwa kwake Paulo katika mji wa Rumi.
   c. Habari ya Injili ya Luka zinatoa picha jinsi mitume walivyofunzwa. Matendo kinatoa picha ya matokea ya walichojifunza.
   d. Injili ya Luka inahatimisha kwa Agizo Kuu na ahadi ya Roho. Matendo kinaanza kwa pointi hiyo na kuonyesha jinsi ilivyotekelezwa.
4. Ya tatu, kiwakilishi "tu – sisi" baadhi ya sehemu katika Matendo (16:1-17; 20:5-21:18; na 27:1-28:16) kinafunua kwamba mwandishi alikuwa akisafiri kwa karibu pamoja na Paulo. Luka anafaa mahali hapo kuliko mtu mwingine yeyote.
   a. Luka alikuwa pamoja na Paulo akiwa gerezani Rumi (Kol.4:14; Flm.1:24).
   b. Mara ya pili Paulo alipofungwa gerezani Rumi, alisema, "Luka tu yuko hapa pamoja nami." (2 Tim. 4:11).
   c. Hili ni jambo la msingi tunapotambua mwaandishi wa Matendo akiwa na Paulo katika kufungwa kwake mara ya pili Rumi (Mdo. 28:10-16).
   d. Kutokana na ukweli huu, ni dhahiri kusema kwamba kitabu kiliandikwa na Luka.

5. Nne, waandishi na maandishi ya kale yanaonyesha kwamba Luka ndiye mwandishi ambaye alitumiwa na Mungu kufunua kitabu cha Matendo. Baadhi ya mifano ni pamoja na ifuatayo:
   a. Vipande vya Muratoria (the Muratorian fragment).
   b. Kupinga ukengeufu cha Irenaus (Against Heresies).
   c. Na maandishi ya Clement wa Alexandria, Eusebius, Tertullian, Jerome, na Origen.

E. Moja ya jambo la kufurahisha kuhusu Luka – alikuwa pengine Mmataifa.
1. Katika Kol.4:10-14, tunaona yafuatayo:
   a. Katika mst. 10, 11, Paulo anaorodhesha watenda kazi pamoja naye watu wa tohara, i.e., wenye asili ya Kiyahudi.
   b. Katika mst. 12-14, ameorodhesha wafanya kazi wengine.

(1). Lakini tangu kutajwa majina matatu katika mst.10, 11 walikuwa ni wafanya kazi ambao asili yao ni Wayahudi, kisha watenda kazi wengine wameorodheshwa mst. 12-14 lazima hao asili yao ni Mataifa.

(3) Luka ametajwa kama miongoni mwa watenda kazi katika mst. 14.

2. Pia katika Mdo.1:19, Luka anawataja wale walioishi Yerusalem, k.m. wale wenye asili ya Kiyahudi.

a. Kisha, katika kuwataja wenye asili ya Kiyahudi, anasema, "… kwa lugha yao…"
b. Hivyo basi ni kweli, Luka hajihesabu yeye kuwa mwenye asili ya Kiyahudi.
c. Hatimisho pekee ni kusema alikuwa Mmataifa.

3. Kama ni kweli kwamba alikuwa Mmataifa, basi alikuwa ni Mmataifa pekee ambaye Mungu alimtumia kumfunulia sehemu ya Agano Jipya!

F. Mhutasari wa sababu za kuamini kuwa Luka ndiye aliyetumiwa kuandika kama mwanadamu:
1. Maandiko ya awali aliyomwandikia Theofilo.
2. Mtindo wa aundishi unalinga kati ya Luka na Matendo.
3. Mafungu yenye "tu… sisi" yanaonyesha kuwa alikuwa karibu na kusafiri pamoja na Paulo.
4. Waandishi na maandishi ya awali yanathibitisha hilo.

## III. TAREHE YA KUANDIKA, KIPINDI GANI, NA NYAKATI:

A. Kwa hakika, hakuna jibu la uvuvio juu ya swali ni lini kitabu kiliandikwa.

B. Hata hivyo, wengi huamini kuwa kiliandikwa mwaka 62 au 63 B.K. kwa sababu zilizoorodheshwa hapo chini.

1. Kitabu kwa ghafla kinafikia hatima, kikieleza tu kwa ufupi miaka miwili ya kufungwa kwake Paulo Rumi (28:30,31) ambayo iliishia takribani mwaka 62 au 63 B.K.
a. Hakuna jambo linalotajwa juu ya mambo yaliyompata Paulo baada ya haya.
b. Kama kitabu kingekuwa kimekamilika miaka iliyofuata baadaye, ni wazi kusema kwamba Luka angetutaarifu mambo yaliyompata Paulo.
c. Pia, kwa kuwa Luka alikuwa na Paulo (2 Tim.4:11), angekuwa na muda kipindi hiki cha miaka miwili kukusanya na kuhakiki taarifa na kuandika maandiko haya sahihi.

2. Sababu nyingine ya kusadiki tarehe 62 au 63 B.K. ni kwamba hayajatajwa matukio makubwa yaliyotukia baadaye kama vile:
a. Moto mkubwa na mateso ya Wakristo yaliyofanywa na Mfalme Nero mwaka 64 B.K.
b. Kifo cha Paulo (ambacho wengi wanadhania kuwa 68 B.K.).

c. Na, kuanguka kwa Yerusalem mwaka 70 B.K.

d. Ikiwa kitabu kiliandikwa baada ya moja ya matukio haya, hakika yangelitajwa ndani ya kitabu.

3. Ukizingatia ukweli huu, k.m. hatimisho la ghafla na kutokuhusisha taarifa za matukio yaliyotokea baadaye, tunahatimisha kwamba kitabu kiliandikwa takribani 62 au 63 B.K.

C. Kipindi gani kitabu cha Matendo kilichukua kuandikwa:
1. Takribani miaka 29 – 30 kuanzia kupaa kwake Kristo (33 B.K.) hadi mwaka wa pili wa kufungwa kwake Paulo (62 – 63 B.K.).
2. Wafalme wa Rumi waliotawala kipindi hiki walikuwa kama ifuatavyo:
a. Tiberio (14 – 37 B.K.).
b. Kaligula (37 – 41 B.K.).
c. Klaudio (41 – 54 B.K.).
d. Nero (54 – 68 B.K.).

D. Makadirio ya nyakati za kitabu cha Matendo, kama sura zilivyoonyesha katika mabano hapo chini.

| B.K. | | |
|---|---|---|
| | 33 | Kuanzishwa kwa kanisa Yerusalem (1-2). |
| | 35 | Kupigwa mawe kwa Stefano, kutawanyika kwa kanisa (7,8). |
| | 35 | Kuongoka kwa Sauli (9). |
| | 38 | Safari ya Paulo ya kwanza kutembelea Yerusalem baada ya uongofu wake (9). |
| | 39 | Kuongolewa kwa Kornelio Mmataifa (10). |
| | 42 | Kukubaliwa kwa Mataifa kuingia katika kanisa la Antiokia (11). |
| | 44 | Safari ya pili ya Paulo kutembelea Yerusalem (12). |
| | 45-48 | Safari ya kwanza ya uinjilisti (Paulo & Barnaba) (13, 14). |
| | 50 | Mkutano Yerusalem (15). |
| | 50-53 | Safari ya pili ya uinjilisti (Paulo & Sila) (16-18). |
| | 54-57 | Safari ya tatu ya uinjilisti (Paulo) (19,20). |
| | 58 | Kufika kwake Paulo Yerusalem (20-23). |
| | 58-60 | Paulo akiwa Kaisaria (24-26). |
| | 60-61 | Safari ya Paulo kuelekea Rumi (27, 28). |
| | 61-63 | Paulo akiwa Rumi kwa miaka miwili (28). |

## IV. MAKUSUDI DHAHIRI MAKUU YA KITABU CHA MATENDO

A. Moja ya malengo ni kubainisha mifano ya matukio ya uongofu wa wenye dhambi kwa njia ya mahubiri ya Injili.

B. Kusudi lingine lilikuwa ni kubainisha mambo yaliyohusu kanisa la Bwana kama ifuatavyo:
1. Mwanzo wake.
2. Mfumo wake wa uongozi.
3. Siku ya kuabudu na baadhi ya mambo yaliyomo katika ibada.
4. Na, kuenea kwake.

C. Kusudi la tatu lilikuwa ni kutoa picha sahihi ya Wakristo duniani. Watu hawa:
1. Kwa ujumla walijitoa kwa Bwana, kwa hiari wakiacha kila kitu, hata maisha yao wenyewe, k.m. Stefano (sura 7) na Yakobo (sura 12).

2. Waliungana katika mafundisho (2:42; 4:32, n.k.).
3. Walipendana vya kutosha hata kujitoa sadaka na kusaidiana, ukijumuisha mahitaji yao ya kimwili (2:44f; 4:32-37).
4. Walidumu katika uinjilisti (5:28,42; 8:4; 14-21).
5. Walikuwa watu wa sala (2:42; 4:24ff; 12:15,22).
6. Walilipokea neno la Mungu kwa furaha na kujifunza neno la Mungu (2:41; 17:11).
7. Waling'aa kama nuru kwa Bwana (2:47; 4:13; 17:6).
8. Walinena ukweli, hata wakati ulipouma (20:20, 26, 27).
9. Walipendana kiasi cha kutoa machoni mmoja alipoaga (20:37,38).
10. Walimwabudu Mungu katika roho na kweli (2:42; 20:7).
11. Walikuwa na ujasiri wa kumtii Mungu hata wakati palipokuwa na vita (5:29).
12. Walijawa na furaha kwa kuwa Wakristo (2:46; 8:39; 16:23-25).
13. Waliridhika kuitwa Wakristo tu (11:26; 26:28).
14. Walihesabu kuwa furaha kuteseka kwa ajili ya Yesu (5:41; 14:22; 16:23-25).

D. Kusudi la nne ilikuwa kuonyesha kwamba Ukristo ni kwa kila mtu wa kila taifa.
   1. Ukijumuisha katika kusudi hilo lilidhihirisha kwamba Injili ni uweza wa Mungu kuokoa watu toka katika kila kabila, taifa, mazingira, hali ya kijamii, kazi, n.k.

E. Lengo lingine lilikuwa kuwakilisha taarifa muhimu juu ya Roho Mtakatifu.

F. Kusudi la sita lilikuwa kudhihirisha ukweli wa mateso ya Ukristo.
   1. Ukijumuisha mifano iliyotolewa ya tabia na matendo mema mbali na kukabiliana na mateso.

G. Lengo la saba lilikuwa kuonyesha uaminifu wa Mungu na Mwanawe mpendwa jinsi alivyotekeleza ahadi na unabii mwingi.

H. Na mwisho, kusudi ilikuwa kuonyesha kanisa la Bwana likiwa katika mapambano ikiwa ni matokeo ya mahubiri ya Injili.
   1. Kisha kuonyesha kufaulu (triumph), ushindi juu ya vikwazo vyote.
   2. Kumbuka Math. 28:18,19.
   3. Mifano ya mapambano/kufaulu inavyojirudia-rudia katika kitabu cha Matendo:

| | FUNGU: MAPAMBANO | | USHINDI (triumph) |
|---|---|---|---|
| 1. | 1:1-6:7 | Mateso | Kuhubiriwa kwa Injili |
| | | Unafiki | Nidhamu/ Hofu<br>Makutano wanaongezeka |
| | | Ubaguzi | Wanafunzi wakazidi sana/ Makuhani wanazidishwa |
| 2. | 6:8-9:31 | Mateso na Sauli | Amani/ Kuimarishwa/ Kuongezeka |
| 3. | 9:32-12:24 | Herode anamwua Yakobo, kufungwa kwa Petro | Mungu amwua Herode/ anamtoa gerezani Petro/ Neno linaenea na kuzidi sana |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | 12:25-16:5 Wayahudi wenye wivu wanafanya ghasia/ Paulo anapigwa mawe/ Wakristo wenye asili ya Kiyahudi wanajaribu kushurutisha kushika sheria/ Kushindwa kuelewana baina ya Paulo na Barnaba | Kanisa liliimarika ktk imani na kuongezeka katika idadi kila siku. |
| 5. | 16:6-19:20 Paulo na Sila wametiwa gerezani kwa madai ya uongo/ Wayahudi wenye wivu wanafanya ghasia/ Athene: Hekima ya Mungu inashinda hekima ya wanadamu. | Neno la Bwana likazidi sana kuenea na kushinda |
| 6. | 19:21-28:31 Ghasia Efeso/ Paulo anaonywa juu ya hatari Yerusalem/ Wayahudi wanamkamata Paulo ili kumwua/ Paulo kushitakiwa na kuwa Gerezani Kaisaria/ kuvunjikiwa kwa meli na Kuumwa na nyoka/ Paulo gerezani Rumi | Fursa ya Paulo kuihubiri Injili kwa wakuu na askari/ Alihubiri ufalme wa Mungu na Bwana Yesu Kristo, akiwa na ujasiri, pasiwe na mtu wa kumkataza. |

## V. UMUHIMU NA NAFASI YA KITABU CHA MATENDO KTK AGANO JIPYA:

A. Kitabu cha Matendo kinatudhihirishia jinsi mitume wa Kristo walivyotii "agizo kuu" lililotolewa na Kristo.

1. Kwa mfano, angalia Mdo. 2:14ff; 3:12ff; 4:8ff; 5:28, 42; 6:7; 8:4; 12:12; 14-12.

B. Matendo ni kiungo muhimu sana kati ya vitabu vinne vya Injili na nyaraka ishirini na moja.

1. Kiunganisho hicho kati ya habari za Injili, Matendo na Nyaraka tunaweza kukitazama kwa njia mbalimbali:

a. Mosi, katika mpangilio wa Agano Jipya:

| **Maeneo** | **Kitabu Kinachohusika** | **Somo Kwa Ujumla** |
|---|---|---|
| Habari za injili | Mathayo – Yohana | Maisha ya Kristo |
| Historia | Matendo | Jinsi ya kufanyika kuwa Mkristo |
| Nyaraka | Warumi – Yuda | Jinsi ya kuishi kama Mkristo |
| Unabii | Ufunuo | Tumaini la Mkristo |

b. Pili, Matendo kinatumika kama msingi kwa karibu Nyaraka nane

| **Nyaraka** | **Sura yenye Mazingira katika Matendo** |
|---|---|
| Warumi | 2 na 28 |
| 1 na 2 Wakorintho | 18 |
| Wagalatia | 13 na 14 |
| Waefeso | 19 na 20 |
| Wafilipi | 16 |

C. Jambo la tatu muhimu kuhusu Matendo ni kwamba kinatoa ushahidi dhahiri dhidi ya madai ya utume wa Paulo, k.m.,:

1. Kujitokeza kwa Yesu mbele ya Paulo kwa njia ya Miujiza na kumteua ili kuhubiri Injili kwa Mataifa (Sura 9, 22, 26).

2. Miujiza ya ajabu aliyoweza kutenda kwa nguvu za Roho Mtakatifu (k.m. 14:8-10; 19:11, 12; 20:9-12).

3. Mambo yanayoyofanana ya kustaajabisha baina ya maisha ya Petro na Paulo kama yanavyobainishwa hapa chini:

a. **MAISHA YAO:**

| PETRO | | PAULO | |
|---|---|---|---|
| 1. | Hotuba ya kwanza (2) | 1. | Hotuba ya kwanza (13) |
| 2. | Kiwete ameponywa (3) | 2. | Kiwete ameponywa (14:8) |
| 3. | Simoni, mchawi (8) | 3. | Elima, Mchawi (13) |
| 4. | Nguvu ktk kivuli (5) | 4. | Nguvu ktk leso (19) |
| 5. | Kuweka mikono (8) | 5. | Kuweka mikono (19) |
| 6. | Walitaka kumsujudia Petro (10) | 6. | Walitaka kumsujudia Paulo (14) |
| 7. | Tabitha afufuliwa toka kwa wafu (9) | 7. | Eutiko afufuliwa toka kwa wafu (20) |
| 8. | Petro atiwa gerezani (12) | 8. | Paulo atiwa gerezani (28) |

b. **MAFUNDISHO YAO:**

| | | | PETRO | PAULO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ukweli kuhusu Kristo: | | | |
| | a. | Kifo | 2:23, 36; 10:39 | 13:28; 1 Kor.15:3 |
| | b. | Maziko | 2:27,31 | 13:29; 1 Kor.15:4 |
| | c. | Ufufuo | 2:24, 32; 10:20 | 13:30; 1 Kor.15:4 |
| | d. | Kutawala akiwa Mfalme na Bwana | 2:36; 1Pet.3:22 | 17:3; 18:5, 28 |
| 2. | Amri: | | | |
| | a. | Utiifu | 10:34, 35 | 17:30, 31 |
| | b. | Amini | 10:34 | 16:31 |
| | c. | Tubu | 2:38; 3:19 | 17:30, 31 |
| | d. | Ubatizwe | 2:38; 10:48 | 16:33; 18:8 |
| | e. | Uishi kwa utaua | 2:40 | 14:22; Rum.6:4 |
| 3. | Ahadi: | | | |
| | a. | Msamaha | 2:38 | 13:38 |
| 4. | Mataifa: | | | |
| | a. | Watu wote walio mbali | 2:39 | 13:46-48 |

D. Jambo la nne muhimu kuhusu Matendo ni kwamba, kama kilivyo Mwanzo katika Agano la Kale, ni kitabu cha *mwanzo*:

1. Wa Injili kuhubiriwa (2:14ff).

2. Wa kanisa la Bwana (2:1-47).

3. Wa kubatizwa na kupata Roho Mtakatifu (2:1-4; 10:44-46; 5:32).

4. Wa wokovu kupitia Kristo (2:22-47).

5. Wa uinjilisti dunia nzima (8:4).

6. Mateso kwa Wakristo (4 & 5).

7. Wa Ukuu wake Kristo (2:32-36).

E. Umuhimu wa Matendo kwa ufupi na nafasi yake katika Agano Jipya.

1. Kinaonyesha jinsi kanisa la awali lilivyoitikia Agizo Kuu.

2. Ni kiungo muhimu kati ya Injili nne na Nyaraka ishirini na moja.

3. Kinatoa ushahidi mkubwa wa utume wake Paulo.

4. Ni kitabu cha mwanzo (beginnings).

## VI. MTAZAMO TOFAUTI KADHAA WA KITABU CHA MATENDO – NJIA MBALIMBALI ZA KUCHANGANUA MAZINGIRA YA KITABU:

A. Kwa kuandika usitawi:

1. 2:41 – watu 3,000.
2. 4:4 – idadi ya wanaume 5,000.
3. 5:14 – walioamini wakazidi kuongezeka –wengi.
4. 6:7 – hesabu ya wanafunzi ikazidi sana – jamii kubwa ya makuhani wakatii.
5. 9:31 – kanisa … likaendelea na kuongezeka.
6. 12:24 – neno la Mungu likaenea na kuzidi.
7. 16:5 – makanisa … hesabu yao ikaongezeka kila siku.
8. 19:20 – neno la Bwana lilivyozidi na kushinda.

B. Kwa *wahusika* ambao kazi zao zimetajwa zaidi vipindi mbalimbali katika kitabu:

1. Petro – Sura 1-5; 10,11
2. Stefano – Sura 6, 7
3. Barnaba, Filipo, na Sauli 8, 9, 12-28.

C. Kwa kazi ya *Roho Mtakatifu*.

1. Utimilifu wa ahadi ya Baba kwa mitume kuhusu Roho Mtakatifu (sura 1 & 2)
2. Matokeo ya kumwagwa kati ya Wayahudi na Mataifa (sura 3-28).

D. Kijografia (maeneo makuu)

1. Yerusalem
2. Antiokia (sura 13:1-14:26; 15:36-21:15).
3. Paulo Yerusalem, Kaisaria, na Roma (21:16-28:31).

E. Kwa Sehemu sita zikionyesha maendeleo katika kutekeleza *agizo kuu*;

1. 1-6:7 – Kanisa Yerusalem na mahubiri ya Petro. Anahatimisha kwa maneno, “Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalem; jamii kubwa ya makuhani wakatii ile imani.:

2. 6:8-9:31 – Kuenea kwa Ukristo katika Palestina yote; mauaji ya Stefano, na mahubiri katika Samaria. Sehemu hii inahatimishwa kwa maneno, “Basi kanisa likapata raha katika Uyahudi wote na Galilaya na Samaria, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu.”

3. 9:32-12:24 – Kuongolewa kwa Paulo; kukua kwa kanisa la Antiokia; na uongofu wa Kornelio. Muhtasari wake ni, “Neno la Bwana likazidi na kuenea.”

4. 12:25-16:5 – Kuenea kwa kanisa katika Asia ndogo yote na safari ya kwenda kuhubiri Galatia. Inahatimisha, “Makanisa yakatiwa nguvu katika ile imani, hesabu yao ikaongezeka kila siku.”

5. 16:6-19:20 – Kuenea kwa kanisa Ulaya na kazi ya Paulo miji mikuu ya Mataifa kama vile Korintho na Efeso. Muhtasari unasomeka hivi, “Hivyo ndivyo neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu.”

6. 19:21 – 28:31 – Kufika kwa Paulo katika mji wa Rumi na kufungwa kwake huko. Inahatimishwa na Paulo, “Akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo; kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu.

F. Kwa kuendelea katika kutimiza Matendo 1:8 (angalia kwanza mstari huu):

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Darubini | Yerusalem | Yudea & Samaria | | Hata mwisho wa nchi |
| Kumbukumbu | 1:1….3:1……………..8:5 | ………………13:1….. | | 21:17..28:31 |
| Mgawanyiko | Mwanzo wa Kanisa / Kukua kwa Kanisa | Kuzidi kuenea kwa kanisa | Safari tatu za Paulo | Kesi ya Paulo |
| Somo | Wayahudi<br>Petro | Wasamaria<br>Filipo | | Mataifa<br>Paulo |
| Maeneo<br>Muda | Miaka 2<br>B.K. 33-35 | Miaka 13<br>B.K. 35-48 | | Miaka 14<br>B.K. 48-62 |

G. Mhutasari kwa ujumla wa Kitabu cha Matendo
1. Kwa habari za kukua.
2. Kwa wahusika (characters).
3. Kwa kazi za Roho Mtakatifu.
4. Kijiografia
5. Kwa kuendelea kutekeleza agizo kuu.
6. Kwa kuendelea kutekeleza Matendo 1:8.

## VIII. VIELELEZO KADHAA VYA KITABU CHA MATENDO:

## KILELEZO CHA MATENDO (KWA UJUMLA)

I. Sehemu ya kwanza: Kanisa limeanzishwa Yerusalem ……….. 1-7

II. Sehemu ya pili: Kanisa lilitawanyika hadi Judea na Samaria …….. 8-12

III. Sehemu ya tatu: Kanisa limeenea kufikia mwisho wa dunia ………… 13-28

## KIELELEZO CHA MATENDO (KWA UFUPI)

I. Sehemu ya kwanza: Kanisa limeanzishwa Yerusalem ………… 1-7

- A. Kanisa limeanza kwa nguvu ……………………………. 1,2
- B. Kanisa lilienea Yerusalem ……………………………… 3-7

II. Sehemu ya pili: Kanisa lilitawanyika hadi Yudea na Samaria …. 8-12
- A. Kanisa lilitanuka kijiografia …………………………... 8,9
- B. Kanisa lilivuka mipaka ya kitaifa ………………………. 10-12

III. Sehemu ya tatu: Kanisa lilienea hata mwisho wa nchi ………… 13-28
- A. Safari ya kwanza ya uinjilisti (Paulo na Barnaba……….. 13,14
- B. Safari ya pili ya uinjilisti (Paulo na Silas ………………. 15-18:22
- C. Safari ya tatu ya uinjilisti (Paulo) ……………………… 18:23-21:14
- D. Paulo katika mikono ya maadui ………………………. 21:15-28:31

## KIELELEZO CHA MATENDO (MSINGI)

I. Sehemu ya kwanza: Kanisa lilianzishwa Yerusalem …………… 1-7
- A. Kanisa lilianza kwa nguvu ……………………………… 1,2
  1. Kungojea kwa ahadi …………………………… 1
  2. Ahadi imetimizwa na kanisa kuanzishwa …….. 2

- B. Kanisa lilikua Yerusalem ……………………………… 3-7
  1. Miujiza ya Petro na Yohana / Upinzani na Masadukayo … 3:1-4:31
  2. Kukabiliana na tatizo la jamii / uongo wa Anania na Safira… 4:32-5:11
  3. Mafanikio na kuinuka upya kwa upinzani ………………... 5:12-42
  4. Kuchanguliwa kwa watu saba ……………………………. 6:1-7
  5. Stefano anawachukiza Mafarisayo / Kifo cha Stefano ……. 6:8-7:60

II. Sehemu ya pili: Kanisa lilitawanyika hadi Yudea na Samaria …………. 8-12
- A. Kanisa lilitanuka kijiografia ……………………………………. 8,9
  1. Kukua kwa kanisa kutokana na kazi ya Filipo …………. 8:1-40
  2. Kuongolewa kwa Paulo / Petro anamfufua Dorkasi …… 9:1-43

- B. Kanisa linavuka mipaka ya kitaifa …………………………….. 10-12
  1. Mlango unafunguliwa kwa Mataifa …………………… 10:1-11:30
  2. Mateso kutoka ndani ya serikali ………………………. 12

III. Sehemu ya tatu: Kanisa linaenea hadi mwisho wa nchi ………………. 13-28
- A. Safari ya kwanza ya uinjilisti (Saul na Barnaba ………………. 13,14
  1. Kuitwa kwa Barnaba na Sauli ………………………… 13:1-3
  2. Safari ya kwanza ya uinjilisti …………………………. 13:4-14:28

B. Safari ya pili ya uinjilisti (Paulo na Sila) …………………… 15-18:22
1. Mkutano uliofanyika Yerusalem …………………… 15:1-35
2. Safari ya pili ya uinjilisti …………………………… 15:36-18:22

C. Safari ya tatu ya uinjilisti (Paulo) ………………………….. 18:23-21:14

D. Paulo akiwa katika mikono ya maadui …………………… 21:15-28:31
1. Katika Yerusalem ………………………………… 21:15-23:30
2. Katika Kaisaria …………………………………… 23:31-26:32
3. Paulo anakwenda Rumi …………………………… 27:1-28:15
4. Paulo anasubiri miaka miwili kwa Nero …………….. 28:16-31

**KIELELEZO CHA MATENDO (KWA MAPANA)**

I. Sehemu ya kwanza: Kanisa lilianzishwa Yerusalem ……………… 1-7
A. Kanisa lilianza kwa nguvu …………………………………….. 1,2

1. Kungojea ahadi ………………………………………… 1
a. Utangulizi …………………………………… 1:1,2
b. Ahadi imetolewa …………………………….. 1:3-8
c. Kupaa kwa Kristo ……………………………… 1:9-11
d. Mitume Yerusalem ………………………….. 1:12-14
e. Uchaguzi wa Mathiya ………………………….. 1:15-26

2. Ahadi imetimizwa na kanisa limeanzishwa ……………. 2
a. Mitume wamejazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha..2:1-13
b. Roho Mtakatifu (kupitia Petro) anashawishi makutano … 2:14-36
(1) Tafsiri iliyovuviwa ya matukio haya ………… 2:1-13
(2) *Yesu*: Alidhihirishwa na Mungu; akauawa na Wayahudi; Alifufuliwa na Baba ……………………… 2:22-24
(3) *Yesu*: Uthibitisho toka kwa manabii ……… 2:25-32
(4) *Yesu*: Aliinuliwa na kuketishwa kitini …… 2:33-36
c. Jinsi wengine walivyopokea kati ya makutano / masharti ya msamaha yaliyovuviwa ………………………… 2:37-41
d. Kanisa linazidi kusonga mbele ………………….. 2:42-47

B. Kanisa likaenea Yerusalem …………………………………… 3-7
1. Miujiza ya Petro na Yohana / Upinzani wa Masadukayo … 3:1-4:31
a. Petro amponya kiwete ……………………………. 3:1-11
b. Roho Mtakatifu kupitia Petro anashawishi makutano 3:12-26
(1) *Yesu*: Aliuawa na Wayahudi / Alifufuka na kutukuzwa na Mungu ……… 3:12-17
(2) *Yesu*: Alitabiriwa na manabii / Masharti ya msamaha yaliyovuviwa …….. 3:18-26
c. Petro na Yohana wametiwa gerezani ……………. 4:1-4
d. Petro anahubiri mbele ya baraza la Sanhedrin / Wokovu ni katika jina la Yesu pekee …………… 4:5-12
e. Baraza la Sanhedrin linawakataza Petro na Yohana wasihubiri …………………… 4:13-22
f. Mitume wanaomba wawe majasiri ……………… 4:23-31

2. Kupambana na tatizo la jamii / Uongo wa Ananisa na Safira 4:32-5:11

a. Ushirika wa kanisa la awali pasipo uchoyo ……… 4:32-37
b. Anania na Safira wanadanganya na kufa ………… 5:1-11

3. Mafanikio na kuinuka upya kwa upinzani ……………….. 5:12-42
a. Miujiza ya mitume / wengi wakazidishwa ……… 5:12-16
b. Kufungwa kwa mitume / Kufunguliwa kimiujiza / Hotuba 5:17-28
c. Mahubiri ya mitume yalimwinua Yesu katika baraza ……. 5:29-32
d. Ushauri wa Gamalieli kwa baraza ………………… 5:33-39
e. Kupigwa kwa mitume / Furaha / Yesu anahubiriwa .. 5:40-45

4. Kuchaguliwa kwa watu saba ………………………………6:1-7
a. Tatizo ……………………………………………… 6:1
b. Ufumbuzi wake ……………………………………6:2-4
c. Saba wanachaguliwa / Mitume wanawawekea mikono… 6:5,6
d. Neno la Mungu likaenea na watu wakatii ……………. 6:7

5. Mafarisayo wamechukizwa na Stefano / Kifo cha Stefano …… 6:8-7:60
a. Stefano anafanya miujiza …………………………….. 6:8
b. Mashitaka juu ya Stefano ……………………… 6:9-11
c. Stefano analetwa mbele ya baraza ……………. 6:12-15
d. Stefano anajitetea mbele ya baraza …………… 7:1-53
(1) Swali la kuhani mkuu ………………… 7:1
(2) Stefano asimulia historia: Abraham, Isaka, Yakobo na wanawe kumi na wawili …….. 7:2-8
(3) Kukataliwa kwa Yusufu na ndugu zake, lakini Mungu akamwokoa ……………………………… 7:9,10
(4) Yusufu aliokoa nduguze na Israeli ……… 7:11-16
(5) Musa akaja kuwasaidia nduguze utumwani.. 7:17-26
(6) Musa alikataliwa na Israeli ………………. 7:27-29
(7) Mungu akamsimamisha Musa kuwa kiongozi na mwokozi ……………………………… 7:30-37
(8) Musa akakataliwa tena na Israeli ……….. 7:38-40
(9) Israeli ikamkataa Mungu moja kwa moja ... 7:41-43
(10) Mungu hakai katika hekalu zilizofanywa na wanadamu ………………………….. 7:44-50
(11) Stefano anawashutumu wanaomhukumu – walimpinga Roho Mtakatifu; waliwatesa manabii; wakamwua Yesu; na kuikataa Sheria! ….. 7:51-53
e. Jinsi baraza lilivyoitikia – kifo cha Stefano ……… 7:54-60

II. Sehemu ya pili: Kanisa lilitawanyika kutoka Yudea hadi Samaria ……… 8-12
A. Kanisa likatanuka kijiografia ……………………………………. 8,9
1. Kuenea kwa kanisa kutokana na kazi ya Filipi ………… 8:1-40
a. Sauli kulitesa kanisa ……………………………. 8:1-3
b. Matokeo – Injili ilienezwa …………………….. 8:4
c. Filipo akamhubiri Kristo na Ufalme wake Samaria/ watu wengi wakabatizwa, pamoja na Simon mchawi 8:5-13
d. Petro na Yohana wanatumwa kuwawekea mikono Wasamalia na kupewa Roho Mtakatifu ………… 8:14-17
e. Simon ajaribu kununua uwezo huo/ majibu ya Petro 8:18-25
f. Filipo anatumwa kwa towashi Mwethiopia ……… 8:26-34
g. Filipo akamhubiri Kristo (ikiwa ni pamoja na ubatizo)

na Filipo alitii ………………………………… 8:35-40

2. Uongofu wa Sauli / Petro anamfufua Dorcas ……….. 9:1-43
   a. Sauli anaendelea kulitesa kanisa …………… 9:1,2
   b. Yesu anakabiliana na Sauli, aliyeuliza, "Bwana, unataka nifanye nini?" (KJV) …………………… 9:1-9
   c. Anania anatumwa kwa Sauli / Sauli anabatizwa. 9:10-19
   d. Sauli akamhubiri Kristo Dameski …………….. 9:2-23
   e. Sauli anajaribu kuungana na wanafunzi Yerusalem / Barnaba anamsaidia …………………………. 9:24-31
   f. Petro anamsaidia Ainea katika Lida …………. 9:32-35
   g. Petro anamfufua Dorcas Yopa ……………….. 9:36-43

B. Kanisa kuenea katika Mataifa ………………………………. 10-12
1. Mlango umefunguka kwa Mataifa ………………….. 10:1-11:30
   a. Akishaongozwa na malaika, Kornelio anamwita Petro 10:1-8
   b. Petro anaona maono …………………………. 10:9-16
   c. Wajumbe toka kwa Kornelio wanamwita Petro .. 10:17-22
   d. Petro na Kornelio wanakutana ………………… 10:23-29
   e. Kornelio kwa nini alimwita Petro …………….. 10:30-33
   f. Ujumbe wa Petro kwa Kornelio na watu wa nyumbani (10:34-43)
      (1) Mungu hana upendeleo ……………… 10:34,35
      (2) Amani kwa njia ya Yesu – Bwana wa wote. 10:36,37
      (3) *Yesu*: Aliyethibitishwa na Baba kwa njia ya miujiza 10:38
      (4) *Yesu*: Aliyesulubiwa na Wayahudi …… 10:39
      (5) *Yesu*: Aliyefufuliwa na Baba na kudhihirishwa wazi ……………………. 10:40,41
      (6) *Yesu*: Mhukumu wa wote ……………... 10:42
      (7) *Yesu*: Alitabiriwa na manabii – msamaha kupitia yeye …………………………. 10:43
   g. Roho Mtakatifu anashuka juu ya Kornelio na Watu wa nyumbani mwake ………………….. 10:47,48
   h. Petro anaamuru ubatizo wa maji …………….. 10:47,48
   i. Baadhi Yerusalem walishindana na Petro kwa kuwa alikwenda kwa Mataifa …………… 11:1-3
   j. Maelezo ya Petro …………………………….. 11:4-17
      (1) Maono ……………………………….. 11:4-10
      (2) Wajumbe kutoka kwa Kornelio …….. 11:11,12
      (3) Kornelio anaeleza kwa nini alimwita Petro. 11:13,14
      (4) Kushuka kwa Roho Mtakatifu na lengo lake 11:15-17
   k. Majibu ya walioshindana ……………………. 11:18
   l. Kazi ya waliotawanyika …………………………. 11:19-21
   m. Yerusalem inamtuma Barnaba Antiokia ……….. 11:22-24
   n. Barnaba anamleta Sauli kutoka Tarso kwenda Antiokia 11:25,26
   o. Kutabiriwa kwa njaa / Antiokia inatuma kitu Yerusalem kwa mikono ya Barnaba na Sauli …… 11:27-30

2. Mateso kutoka serikali tawala ………………………… 12
   a. Herode anamwua Yakobo …………………….. 12:1,2
   b. Herode anamtia gerezani Petro/ Kanisa linadumu kusali linaomba kwa ajili ya Petro ……………….. 12:6-11
   c. Mungu kimiujiza anamtoa gerezani Petro ……… 12:6-11

d. Petro anakwenda nyumbani kwa Mariam wanakoomba. 12:12-17
e. Kutoroka kwa Petro kunajulikana ……………… 12:18,19
f. Herode anamkufuru Mungu na kufa …………… 12:20-23
g. Neno linaenea / Sauli na Barnaba anarejea Antiokia 12:24,25

III. Kanisa linaenea hadi mwisho wa nchi …………………………………… 13-28
A. Safari ya kwanza ya uinjilisti …………………………………… 13,14
1. Kuitwa kwa Barnaba na Sauli …………………………… 13:1-3
2. Safari ya kwanza ya uinjilisti …………………………… 13:4-14:28
a. Kipro …………………………………………… 13:4-13
(1) Kuhubiri katika masinagogi / Yohana Mark anasaidia ………………………… 13:4,5
(2) Elima (Bar-Yesu) anawapinga Sauli na Barnaba 13:6-8
(3) Sauli (Paulo) anampiga Elima kwa upofu/ Sergio Paulo akaamini ……………….. 13:9-12
(4) Paulo akiwa Perge / Yohana Marko anarejea Yerusalem …………………… 13:13

b. Antiokia ………………………………………. 13:14-50
(1) Ujumbe wa Paulo katika sabato ya kwanza 13:14-43
(a) Israeli kutoka Misri hadi Daudi …. 13:14-43
(b) *Yesu*: Mwokozi kutoka uzao wa Daudi 13:23
(c) *Yesu*: Yohana alihubiri kuja kwake 13:24,25
(d) *Yesu*: Israeli ilimwua, kama ilivyotabiriwa na manabii ………………………… 13:26-29
(e) *Yesu*: Alifufuliwa na Baba, kama ilivyotabiriwa na manabii ………………………… 13:30-37
(f) *Yesu*: msamaha na haki kupitia yeye 13:38-43

(2) Ujumbe wa Paulo sabato ya pili ……….. 13:44-50
(a) Karibu mji mzima umekusanyika / Wayahudi wanakufuru …………………… 13:44,45
(b) Paulo na Barnaba wanawageukia watu wa Mataifa …………………….. 13:48-50

c. Ikonia …………………………………………. 13:51-14:1
(1) Akizungumza akiwa katika Sinagogi …. 13:51-14:1
(8) Ananena kwa ujasiri katika Bwana, bila kujali upinzani ……………………….. 14:2-5

d. Listra …………………………………………. 14:6-20
(1) Paulo na Barnaba wanaondoka Ikonia kwenda Listra na Derbe ……………… 14:6,7
(2) Paulo anamponya kiwete ……………. 14:8-10
(3) Watu wanadhania kuwa Paulo na Barnaba ni miungu …………………………….. 14:11-13
(4) Paulo na Barnaba wanawakataza watu …. 14:14-18
(5) Paulo anapigwa mawe ………………….. 14:19,20

e. Akihubiri wakati akirudi safarini ……………….. 14:21-25

f. Paulo na Barnaba wanatoa ripoti Antiokia ……. 14:26-28

B. Safari ya uinjilisti ya pili (Paulo na Sila ……………….. 15:18-22

1. Kukutana Yerusalem …………………………… 15:1-35
   - a. Paulo na Barnaba wanashindana juu ya tohara / Sheria ya Musa / Swali la wokovu kupelekwa Yerusalem …………………. 15:1-5
   - b. Petro anazungumza …………………….. 15:6-11
   - c. Paulo na Barnaba wanazungumza ……… 15:12
   - d. Yakobo anakubaliana na Petro ……….. 15:13,14
   - e. Yakobo anamnukuu nabii ili kukazia …….. 15:15-17
   - f. Yakobo anahatimisha …………………. 15:18-21
   - g. Paulo, Barnaba, Yuda, na Sila wanatumwa wakiwa na barua kwenda kwa Wakristo wa Mataifa … 15:22-29
   - h. Taarifa kwenda katika kanisa la Antiokia ... 15:30-35

2. Safari ya pili ya uinjilisti ……………………….. 15:36-18:22
   - a. Ugomvi juu ya Yohana Marko …………. 15:36-38
   - b. Paulo/ Sila na Barnaba/ Yohana Marko wanatengana …………………………… 15:39-41
   - c. Derbe / Listra – Timotheo anatahiriwa … 16:1-5
   - d. Troa – Kuitwa Makedonia ……………... 16:6-10
   - e. Filipi …………………………………… 16:11-15
     - (1) Uongofu wa Lidia …………….. 16:11-15
     - (2) Paulo amtoa pepo msichana ….. 16:16-18
     - (3) Bwana zake wanawapiga Paulo na Sila na kuwatia gerezani kwa uongo 16:19-24
     - (4) Mlinzi wa gereza anauliza, "Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?" ……. 16:25-30
     - (5) Mlinzi wa gereza Filipi atii injili …. 16:31-34
     - (6) Paulo na Sila wanaachwa huru toka gerezani ………………………… 16:35-40
   - f. Thesalonike ……………………………… 17:1-9
     - (1) Paulo anamhubiri Yesu katika Sinagogi 17:1-4
     - (2) Wayahudi wanahamasisha watu kufanya ghasia juu ya Wakristo … 17:5-9
   - g. Beroya …………………………………. 17:10-15
     - (1) Waberoya waugwana wanaamini .. 17:10-12
     - (2) Wayahudi wa Thesalonike wanafanya ghasia tena……………………… 17:13-15
   - h. Athene ………………………………….. 17:16-34
     - (1) Paulo anajadili katika Sinagogi/ Wanafalsafa waona shauku na mafundisho yake …17:16-21
     - (2) Paulo anamhubiri "Mungu asiyejulikana" 17:22-31

(a) Anamtambulisha Mungu wanayemwabudu kwa ujinga …………… 17:22,23
(b) Anamwelezea Mungu mmoja wa kweli aliye kinyume na miungu ya uongo 17:24-29
(c) Anataja majukumu ya mwanadam kwa Mungu …………………… 17:30,31

(3) Kuitikia katika mahubiri ya Paulo … 17:32-34

i. Korintho ………………………………… 18:1-17
(1) Paulo akiwa na Akila na Prisila …… 18:1-3
(2) Majadiliano katika Sinagogi – akataliwa na Wayahudi ……………………… 18:4-6
(3) Krispo na Wakorintho wengi wanaongolewa 18:7-11 ……….. 18:7-11
(4) Galio anakataa kukubali madai ya uongo ya Wayahudi kuhusu Paulo …18:12-17
(5) Paulo anarejea Antiokia ………. 18:18-22

C. Safari ya tatu ya (Paulo) ya uinjilisti ……………………….. 18:23-21:14
1. Galatia na Filigia …………………………………… 18:23
2. Efeso ……………………………………………….. 18:24-19:41
a. Akila na Priska …………………………….. 18:24-28
b. Paulo anakutana na wanafunzi 12 waliobatizwa kwa ubatizo wa Yohana ……………………. 19:1-7
c. Paulo anashindana ktk sinagogi na kufundisha shuleni 19:8-10
d. Paulo anatenda miujiza ……………………. 19:11,12
e. Wadanganyifu wanaigiza miujiza na kushindwa 19:13-16
f. Yesu ametukuzwa na baadhi ya Wakristo wanatubu 19:17-20
g. Timotheo na Erasto wanatumwa Makedonia …… 19:21,22
h. Demetrio ahamasisha wafua fedha kufanya ghasia. 19:23-29
h. Paulo anataka kunena na mkutano, bali wanafunzi
i. wanamzuia …………………………………… 19:30-34
j. Karani wa mji ananyamazisha makutano … 19:35-41

3. Makedonia …………………………………………… 20:1-5

4. Troa – Chakula cha Bwana / Eutiko afufuliwa toka ufuni …20:6-12

5. Mileto ……………………………………………….. 20:13-38
a. Safari kwenda Mileto ………………………… 20:13-38
b. Paulo anaita wazee kutoka Efeso ……………. 20:17,18a
c. Anarudia kuwasimulia kazi ………………….. 20:18b-21
d. Kwenda Yerusalem kuhatimisha mbio zake na huduma kwa furaha bila kujali maonyo aliyopewa… 20:22-25
e. Paulo hakuwa na hatia ………………………. 20:26,27; linga. 20:21
f. Aliwaonya wazee juu ya ukengeufu ujao …… 20:28-32
g. Mambo ya kuagana, sala, na huzuni ……….. 20:33-38

6. Tiro – Paulo aonywa asiende Yerusalem …………… 21:1-6

7. Kaisaria – Agabo anamwonya Paulo kuhusu Yerusalem – Majibu yake …………………………… 21:7-14

D. Paulo katika mikono ya maadui ………………………………. 21:15-28:31

1. Yerusalem …………………………………………….. 21:15-23:23
   - a. Paulo awasili Yerusalem & kupokelewa kwa furaha 21:15-17
   - b. Anakutana na Yakobo na wazee …………….. 21:18-20a
   - c. Yakobo anaeleza tatizo kati ya Wayahudi waaminio na Paulo …………………………… 21:20b-22
   - d. Ushauri wa Yakobo …………………………… 21:23-25
   - e. Paulo afuata ushauri wa Yakobo …………….. 21:26
   - f. Wayahudi wamshutumu Paulo na kutaka kumwua 21:27-30
   - g. Maofisa wa Rumi wamkamata Paulo …………. 21:31-36
   - h. Paulo aomba ruhusa kuzungumza na makutano … 21:37-39
   - i. Anapewa ruhusa na kuanza kunena …………….. 21:40-22:21
     - (1) Historia yake katika Waebrania ………… 21:40-22:5
     - (2) Maono yake juu ya Yesu aliyefufuka akiwa njiani kwenda Dameski ………………………………… 22:6-10
     - (3) Anania kumwendea Paulo Dameski na kumweleza yampasayo kufanya ……………………. 22:11-16
     - (4) Maono yake katika Yerusalem …………. 22:17-21

   - j. Mwitikio wa Wayahudi kutokana na hotuba ya Paulo 22:22,23
   - k. Paulo anadai uraia wake wa Kirumi ……………. 22:24-29
   - l. Paulo analetwa mbele ya baraza la Sanhedrin……. 22:30-23:11
     - (1) Anakutana na Kuhani Mkuu …………… 22:30-23:5
     - (2) Anagawanya baraza la Sanhedrin ……… 23:6-9
     - (3) Jemadari wa Rumi anamwokoa na Bwana ananena naye …………………… 23:10,11

   - m. Wayahudi baadhi wapatana kumwua Paulo …….. 23:12-15
   - n. Paulo atambua mapatano hayo na anaomba msaada toka kwa jemadari wa Rumi …………………….. 23:16-22
   - o. Jemadari anapanga kumpeleka Paulo kwa Feliki liwali katika Kaisaria ………………………….. 23:23-30

2. Kaisaria …………………………………………….. 23:31-26:32
   - a. Paulo anapelekwa kwa Feliki ……………… 23:31-35
   - b. Washitaki wa Paulo wanamshitaki mbele ya Feliki 24:1-9
   - c. Paulo anajibu mashitaka …………………… 24:10-21
     - (1) Anadai hawawezi kuthibitisha madai hayo 24:10-13
     - (2) Anatoa kwa ufupi imani na mambo anayofanya 24:14-16
     - (3) Anaeleza kile alichokuwa akifanya Yerusalem walipomshitaki ………………... 24:17-21

   - d. Feliki anaahirisha kikao / Paulo anatoa hoja kwake / Festo anambadili Feliki ………………………… 24:22-27

   - e. Festo anakwenda Yerusalem / Kuwaomba Wayahudi walete mashitaka juu ya Paulo Kaisaria ……………25:1-5

   - f. Paulo anadai kutokuwa na hatia mbele ya Festo na

anaomba kesi iende kwa Kaisari ………………….. 25:6-12

g. Festo anajadili kesi ya Paulo na Agripa ambaye amekubali kuisikiliza ……………………………. 25:13-22

h. Paulo anapelekwa mbele ya Festo na Agripa …… 25:23-27

i. Paulo anajitetea mbele ya Agripa ………………. 26:1-32
   (1) Maisha yake kama Myahudi …………… 26:1-5
   (2) Imani yake ndiyo sababu hasa ya kushitakiwa 26:6-8
   (3) Mwanzo wake akiwatesa Wakristo …….. 26:9-11
   (4) Maono yake juu ya Yesu aliyefufuka akiwa safarini Dameski ………………………... 26:12-18
   (5) Utiifu wake kwa maono yale …………… 26:19-23

j. Festo anaingilia kati / Paulo anamweleza Agripa … 26:24-32

3. Paulo anakwenda Rumi ……………………………… 27:1-28:15
   a. Kusafiri katika upepo wa mbisho kuelekea Bandari Nzuri 27:1-8
   b. Maonyo ya Paulo kuhusu hatari hayajazingatiwa… 27:9-13
   c. Merikebu imechukuliwa na upepo mkali, ukisababisha wengine kukosa matumaini miongoni mwa wasafiri …… 27:14-20
   d. Utabiri wa Paulo kuhusu kuvunjika kwa meli lakini pasipo kupoteza maisha …………………………… 27:21-26
   e. Mabaharia wanajaribu kujiokoa lakini bila mafanikio 27:27-32
   f. Paulo anawataka wote wale chakula, akiwakumbusha kuwa wasingeliangamia …………………………………. 27:33-37
   g. Nchi imeonekana / merikebu ikatua/ wote walikuwa salama nchini (Malta) …………………………………………… 27:38-44
   h. Namna walivyopokelewa na wenyeji / Paulo Anasongwa-songwa na na nyoka ………………… 28:1-6
   i. Wema zaidi umedhihirishwa …………………… 28:7-10
   j. Kusafiri kwenda Rumi, nchi ya Puteoli / ndugu wamekuwepo hapo na katika njia iendayo Rumi …………………… 28:11-15

4. Paulo anahubiri gerezani kwa miaka miwili ………….. 28:16-31
   a. Paulo anawasili Rumi / Ananena na viongozi Wayahudi ambao walipenda kusikia mawazo yake ……………… 28:16-22
   b. Paulo ananena tena, akinukuu Maandiko / Matokeo mchanganyiko ………………………………… 28:23-29
      c. Kwa miaka miwili, Paulo ahubiri Ufalme wa Mungu 28:30-31

## MCHANGANUO - MATENDO

**I. Sehemu ya kwanza: (1-7) KANISA LILIANZA YERUSALEM.**

**A. (1 na 2) KANISA LILIANZA KWA NGUVU**

**1. (1) Wakisubiri ahadi**

**MTAZAMO WA SURA (1) NZIMA**

a. 1:1,2 Utangulizi

b. 1:3-8 Kutolewa kwa ahadi.
c. 1:9-11 Kupaa kwa Kristo.
d. 1:12-14 Mitume wakiwa Yerusalem
e. 1:15-26 Uchaguzi wa Mathiya.

a. (1:1,2) UTUNGULIZI

1)

1. "*Kitabu kile cha kwanza*" ni maelezo yanayolenga kitabu cha injili ya Luka, ambacho ni kitabu juu ya mambo Yesu aliyoanza "*kufanya na kufundisha*."
2. "*Theofilo*" linatokana na maneno mawili ya Kiyunani: θεοσ – Mungu, φιλοσ – kupenda; hivyo basi, upendo wa Mungu!
   a. Katika Lk.1:3 anatajwa kama "*mtukufu*" – pengine ni kuonyesha kuwa alikuwa afisa mwenye cheo serikalini (cf. Mdo.23:26; 24:3; 26:25).
   b. Matendo inawezekana iliandikwa kumwongoa Theofilo, au kuhakiki imani na matendo yake kwa kufanyika kuwa Mkristo.

**2)**

1. Mwisho wa kitabu cha Luka ni siku Yesu aliyopaa kurejea mbinguni (alipochukuliwa).
   a. Luka 24:50,51.
   b. Linga. Mdo.1:9-11.
2. Haya yalitokea baada ya kuwapa amri, kupitia Roho Mtakatifu.
   a. Haswa, walipewa amri!
   b. Hili linarejea "Amri Kuu" au agizo:
      (1) Luka 24:44-48.
      (2) Linga. Mk.16:15,16; Math.28:18-20.
3. Yesu aliwapa amri kuu wanafunzi wake "aliowachagua."
   a. Angalia sifa maalum za mtume wa Kristo – *alipaswa achaguliwe na Kristo*. Hakuna mtu leo ambaye anaweza kuwa na sifa hizo!
   b. Linga. 1:21, 22.
4. Muhtasari wa 1:1,2, utangulizi:
   a. Katika mst. 1 Luka anarejea kitabu chake cha kwanza kama taarifa ya mambo Yesu aliyofanya na kufundisha.
   b. Katika mst. 2 tunajifunza habari iliyoandikwa na Luka ikihatimishwa na matukio mawili:
      (1) Kristo anatoa amri kuu kwa mitume aliowachagua,
      (2) Na kupaa kwake kwenda mbinguni.

**b. (1:3-8) KUTOLEWA KWA AHADI**

**3)**

1. Baada ya kifo cha Yesu, alifufuka toka kwa wafu siku ya tatu kulingana na maandiko (1 Kor.15:4) na kuishi pamoja na mitume aliowachagua.
   a. Tena, alijidhihirisha kufufuka kwake kwa ushahidi mwingi hata ni vigumu kupingwa.
      (1) Bwana aliwatokea wanafunzi wake mara kumi na tatu baada ya kufufuka kwake, kutokea kwingi huku kumeorodheshwa katika 1 Kor.15:5-8.
      (2) "*Aliowadhihirishia*" hapa inamaanisha pasipo udanganyifu na kwamba bila kukosea. Ni jinsi gani ukweli huo uridhihirika?
         (a) Kwanza, mitume hawakutarajia ufufuo (Yoh.20:25; Lk.24:1-4, 19-24). Kwa hiyo, hapakuwa na hila zilizokuwepo za kutarajia kumwona. Kwa maneno mengine, hawakutarajia ufufuo wake kabisa zaidi ya kudhania tu!
         (b) Pili, walimzoea Yesu kikamilifu baada ya kuishi naye kwa miaka mitatu. Hivyo, wasingedanganywa washindwe kumtambua.

(c) Tatu, aliwatokea mitume wote kumi na moja. Hili ni la msingi kwa kuwa inawezekana mmoja au baadhi kudanganyika, lakini haiwezekani kuwadanganya wote kumi na moja kwa wakati huo.
(d) Nne, Yesu alikaa nao kwa siku arobaini baada ya kufufuka kwake. Muda ulikuwepo wa kutosha kujitambulisha kwao, au kubainisha jambo hilo kuwa si kweli.
(e) Na tano, mitume walimwona Yesu maeneo mbalimbali na wakati ambao pasingelikuwa na udanganyifu.

b. Jambo gani lingine lingeweza kubadili tabia za mitume zaidi ya lile la ufufuo wa Yesu baada ya kifo chake?!
(1) Mk.16:9-16
(2) Mdo.5:40-42.

c. Je, si swala la msingi kwa Mkristo kuwa na uhakika huu (k.m. ushahidi thabiti) juu ya ufufuo wa Yesu?!
(1) Flp. 3:10
(2) 1 Pet. 1:3, 4.

2. Si kwamba mitume walimwona Yesu tu, bali pia walimsikia akinena!
   a. Tena somo hili ni lile lililopendwa na Yesu - ufalme wa Mungu.
      (1) Math.4:17.

**4)**

1. Yesu aliwaamuru mitume kusubiri mahali maalum – Yerusalem.
2. Hapo, aliwaambia, kupokea ahadi ya Baba yake ambaye Yesu aliwaahidi hapo nyuma.
3. Ahadi hii ilikuwa kwa mitume kuipokea ili wapate maongozi kufunua Agano Jipya kwa njia ya Roho Mtakatifu.
   a. Luka 24:49.
   b. Katika Yoh.13 –16 tunaona maelezo zaidi maalum kuhusu ahadi hii.
   c. Lakini kabla ya kujifunza maelezo hayo, ni muhimu kufafanua kutoka katika maandiko kwamba ahadi hizi waliahidiwa watu gani.
   d. Mistari ifuatayo inaonyesha kuwa Yesu aliahidi nguvu hizi kwa mitume wake na ni kwa mitume wake pekee:
      (1) Math.26:20,21.
      (2) Yoh.13:1-4,21.
      (3) Yoh.13:6,23,36; 14:5,8,22.
   e. Hivyo basi, kuzingatia ukweli huo, ebu na tujifunze maelezo juu ya ahadi ya Yesu kwa mitume wake kuhusu Roho Mtakatifu:
      (1) Yoh.14:16,17,26.
      (2) Yoh.15:26,27.
      (3) Yoh.16:7-14.

**5)**

1. Yesu alianza kwa kutaja ubatizo wa Yohana. Kuna mambo mengi yanayolenga ubatizo huo:
   a. Uliamuriwa na Mungu (Lk.7:29,30).
   b. Ulifanya kazi ya maandalizi kwa kuja kwake Masihi (Yoh.1:31; Lk.3:3-6).
   c. Mhudumu alikuwa ni Yohana (Mk.1:5).
   d. Waliohusika katika ubatizo huu ni Wayahudi waliotubu (Mk.1:4,5).
   e. Ulikuwa ubatizo wa maji (Yoh.1:26).
   f. Ulikuwa ni wa kuzamisha (Mk.1:10; Yoh.3:23).
   g. Ulibadilishwa na kuwa ubatizo kwa jina (mamlaka) ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu (Mdo.19:1-5).
2. Katika mstari huu kuna ahadi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa kundi dogo la watu.

a. Alisema "*ninyi*" mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu. Lakini, ni watu gani alikuwa akizungumza nao wakati huo?
b. Fungu hili wazi linadhihirisha pasipo shaka kuwa Yesu alikuwa akizungumza na:
   (1) Mitume aliowachagua (1:2).
   (2) Kwa mitume wake *alijidhihirishia* nafsi yake baada ya kufufuka kwake (1:3).
   (3) Kwa mitume wake aliowaamuru wasiondoke Yerusalem na ambao aliwaahidi (1:4).
   (4) Mitume wake ambao walipata ubatizo wa Roho Mtakatifu siku chache tangu Yesu aahidi (1:26-2:4).
   (5) Mitume wake walionena kwa njia ya miujiza neno la Mungu katika lugha ngeni ambazo hawakuwahi kujifunza kabla (2:4,6,11,14,37).

3. Basi, tunajifunza mitume wa Kristo wangepokea ahadi iliyotajwa hapo juu (mst.4) baada ya kubatizwa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.
4. Tunajifunza pia ahadi hii maalum kwa watu hawa maalum ingetekelezwa siku chache toka Yesu apae kwenda juu mbinguni – wala isiwe miaka mingi au maelfu baada ya Yesu kuahidi.
5. Fungu lingine linalolingana juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu ni Math.3:1-12.
   a. Ingawa hatuna muda wa kujifunza fungu hili kwa undani, lakini mambo ya msingi makuu yanapatikana hapa:
      (1) Batizo mbili zimetajwa katika mistari hii.
         (a) Mmoja ni ubatizo wa moto. Huu unawakilisha adhabu ya milele katika mwali wa moto jehanamu kwa wale wote ambao hawatatii amri za Mungu.
         (b) Mwingine ni ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao ulikuwa kwa mitume wa Yesu pekee waliochaguliwa.

      (2) Ni jambo la msingi kutambua kwamba Yesu ndiye angekuwa mhudumu wa batizo hizi mbili.
      (3) Hili linamaanisha kwamba hakuna mtu ambaye ataweza kuhudumu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.
   b. Wale waliochukua notisi zilizoandaliwa kwa kozi hii wataona maelezo mengi yenye kubainisha fungu katika notisi za fungu hili.
   c. Maelezo zaidi kwa mchanganuo ni kama ifuatavyo:
      (1) Mt.3:1-4 Yohana Mbatizaji alihubiri toba na ufalme wa mbinguni kuwa ulikaribia.
      (2) 3:5,6 Wengi waliotubu wakamwendea wakabatizwa na Yohana, wakiziungama dhambi zao.
      (3) 3Z:7-9 Kundi lingine likaja, likiwa pamoja na Mafarisayo na Masadukayo. Yohana alikataa kuwabatiza hao, akiwaita nyoka, na akiwataka watubu.
      (4) 3:10 Yohana alielezea maangamizi ya milele kwa njia mbili kwao wasiotubu.
         (a) Kwanza, aliwakilisha maangamizi ya milele kwa shoka iliyoweka katika shina la miti (husimamia watu wasiotii – kwa hali hii, Wayahudi). Haswa, hili lingepelekea mauti juu ya miti.
         (b) Pili, alielezea miti isiyozaa (tena husimamia watu wasiotii) ikishakatwa na kuchomwa moto (husimamia adhabu katika miali ya moto wa jehanamu).
      (5) Ebu rukia mst. 12 acha mst. 11 kwa muda. Yohana alimwelezea Yesu akitenganisha ngano (husimamia watu wanaotii) toka katika makapi (ikiwakilisha watu wasiotii).
         (a) Ngano zimehifadhiwa ghalani (husimamia thawabu).
         (b) Makapi yamechomwa moto usiozimika (tena husimamia adhabu katika moto wa milele).
      (6) Kwa muhtasari basi, kabla ya kujifunza Mt.3:11, tunaona katika mistari hii, makundi mawili ya watu na hatima mbili za watu zilizobainishwa kwa nadharia:
         (a) Kundi la kwanza ni watu watakaotii amri za Mungu. Watapata thawabu.
         (b) Kundi la pili ni watu wasiotii amri za Mungu. Wataadhibiwa kwa kuchomwa katika moto ambao hautazimwa kamwe.

(7) Tukiwa na mazingira hayo akilini mwetu ebu na tujifunze Mt.3:11:
   (a) Yohana anamtaja aliye na nguvu, ambaye hakustahili hata kufungua gidamu za viatu vyake – kwa hakika yanamlenga Bwana Yesu Kristo.
   (b) Halafu, Yohana alisema Yesu angewabatiza wale waliokuwa wanamsikiliza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto.
   (c) Lakini, kwa kuwa moto unatumika kwa ajili ya adhabu mstari 10 (mstari kabla ya huu) na mstari 12, (mstari baada ya huu) hivyo basi tunapaswa kuona kuwa unasimamia adhabu katika mstari 11 – na hivyo ndivyo ilivyo haswa!
   (d) Kwa hiyo, katika mstari huu, Yohana anataja batizo mbili tofauti; mmoja wa Roho Mtakatifu na mwingine wa moto!
      1. Kwa kuwa Yesu amewahusisha mitume baadaye kama watakaobatizwa kwa Roho Mtakatifu (Mdo.1:2-5), walikuwepo wengine ambao wangekuwa mitume baadaye waliomsikiliza Yohana siku hiyo.
      2. Math.3:11 tunapata ahadi yao ya kwanza kwamba wangebatizwa katika Roho Mtakatifu.
      3. Kwa upande mwingine, kwao wasiotii waliokataa kutubu, Yesu aliahidi wangeadhibiwa katika adhabu kwa kutoshwa motoni – adhabu ya kutisha hiyo!

**6)**

1. Mitume walimwuliza Yesu kama ufalme ungerejezwa kwa Israeli. Jambo hili linalenga mambo angalau mawili:
   a. Kwanza, inaonyesha kuwa mitume hawakujua bado kwamba ufalme au kanisa la Kristo asili yake ni ya kiroho.
      (1) Walitarajia ufalme kuwa wa kimwili ama wa kisiasa (Linga.Math.20:20,21; Yoh.6:15).
      (2) Yesu hakurekebisha makosa ya kutoelewa kwao wakati huu.
   b. Jambo la pili linalenga swali la mitume kuhusu ufalme uliokuwa bado haujaanzishwa – hili ni swala la msingi sana!
      (1) Isaya alitabiri kuanzishwa kwake katika siku za mwisho (Isaya 2:2-4).
      (2) Danieli alitabiri kuanzishwa katika siku za watawala wa Rumi (Dan.2:44).
      (3) Yohana Mbatizaji alisema "umekaribia," au ulikuwa karibu na karne ya kwanza (Math.3:2).
      (4) Hivyo ndivyo alivyofanya pia Yesu (Math.4:17).
      (5) Ulikuwa bado haujafika Yesu alisema katika maneno yaliyoandikwa katika (Mt.16:18, 19).
      (6) Yusufu wa Arimathaya alikuwa akiungojea baada ya kifo cha Yesu (Mk.15:43).
      (7) Na katika mistari hii, baada ya ufufuo wake Kristo, mitume wake walikuwa wakingojea kuanzishwa kwake!
      (8) Ni jambo dhahiri basi, kwamba Yohana hakuanzisha, kwa sababu alikufa kabla ya wakati huo (Math.14:3-12).

**7)**

1. Yesu alilijibu swali lao kwa kuwaeleza kwamba hawakupaswa kujua majira ambayo Mungu angeanzisha ufalme. Muda ulikuwa katika uweza wa Mungu, na ilikuwa kazi yake (Kumb.29:29)!

**8)**

1. Yesu aliwaeleza wanafunzi wake mambo manne muhimu wangejua na walipaswa kujua:
   a. Kwanza, wangepokea nguvu,
   b. Pili, nguvu hizo wangezipata wakati Roho Mtakatifu angewajia juu yao,
   c. Tatu, wangelikuwa mashahidi wake; na

d. Nne, wangeanzia Yerusalem na kisha kuelekea eneo la Uyahudi, Samaria, na hata mwisho wa nchi.

2. Ebu tujadili mambo haya manne kwa mapana zaidi:
   a. Kwanza, mitume wangepokea nguvu.
      (1) δυναμιν – kupewa nguvu au uwezo ili kufanya jambo fulani.
      (2) Katika mazingira haya, huu ni uwezo kwa mitume kutenda miujiza ili kulifanyia kazi agizo kuu ambalo Yesu aliwapa.
      (3) Pia ni pamoja na kufunua neno la Mungu kwa njia ya uvuvio wa Roho Mtakatifu (Yoh.14-16).
      (4) Ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuthibitisha neno kwa miujiza na nguvu za Roho Mtakatifu (Mk.16:17-20; Ebr.2:3,4).
   b. Pili, Yesu alisema nguvu hii ingewajia Roho Mtakatifu atakapokuja juu ya mitume wake maalum aliowachagua.
      (1) Ungelikuwa ni utimilifu wa ahadi ya Baba na ubatizo wa Roho Mtakatifu uliotajwa na Yesu hapo awali (Lk.24:49; Mdo.1:4,5).
      (2) Pia ujio wa nguvu ingekuwa ni alama za ufunguo wa wakati wa kuanzishwa kwa ufalme wa Yesu kama inavyodhihirishwa katika Mk.9:1.
      (3) Kumbuka tulivyojifunza Math.16: 18,19 ambapo tulijifunza Yesu akilitumia neno "kanisa" na "ufalme" akilenga kitu kimoja kiroho.
      (4) Ukiwa na wazo hilo akilini mwako, ebu na tusome na kuchanganua alichosema Yesu katika Mk.9:1.
         (a) Kwanza, Yesu alisema kungelikuwa na wengine waliokuwa wakimsikiliza siku hiyo ambao wasingekufa hata wauone ufalme ukija.
            1. Hili linatueleza bila shaka kwamba isingepita miaka mamia au maelfu hata ufalme (kanisa) wake uanzishwe, kama wengine wanavyofundisha leo!
            2. Na tunaelezwa ungeanzishwa hakika ndani ya miaka 70 au 80 katika kipindi alichokuwa akiongea Yesu, ama mapema kabla ya hapo.
         (b) Pili, Yesu alisema ufalme (kanisa) ungekuja na *nguvu*.
            (1) Neno lililotafsiriwa "nguvu" katika Mk.9:1 ni sawa na lile lililotafsiriwa katika  Mdo.1:8!
            (2) Na *nguvu* ndilo neno la ufunguo linalounganisha, ama kuyaweka pamoja, ufalme (kanisa) katika Mk.9:1 na kujiwa na Roho Mtakatifu mitume wa Kristo katika Mdo.1:8.
         (c) Sasa tunaona tumeona wazo hilo *likibainishwa* wazi, ebu tuhatimishe kwa *maneno* tuliyojifunza kuhusu nguvu hizi na ufalme katika Math.16:18,19; Mk.9:1; Mdo.1:8.
            1. Kwanza, Yesu ametumia maneno "ufalme" na "kanisa" kwa kupokezana (interchangeably) kulenga kitu kimoja cha kiroho (Math.16:18,19).
            2. Pili, ufalme (kanisa) lingeanza kwa *nguvu* (Mk.9:1).
            3. Tatu, nguvu hizo wangezipokea mitume wa Kristo akisha kuwajilia juu yao Roho Mtakatifu (Mdo.1:8).
            4. Ukijumuisha mistari hii, *ufalme* (kanisa) kuja na nguvu na nguvu hizo hizo zingekuja juu yao mitume wa Kristo.
            5. Kwa hiyo, tunatambua kwamba ufalme (kanisa) ungeanzishwa wakati Roho Mtakatifu angewajilia juu yao mitume wa Kristo.
            6. Basi, tunachopaswa kutambua ni lini ufalme (kanisa) ulianzishwa ni kuangalia wakati Roho Mtakatifu alipowajilia mitume wa Kristo.
            7. Na jibu hili litatolewa kwetu katika fungu lijalo katika kitabu hiki!
      c. Jambo la tatu Yesu aliwaambia mitume wake katika 1:8 ni kwamba wangekuwa *mashahidi* wake.
         (1) Shahidi ni mwenye kuona jambo fulani na, kwa msingi huo, anataka kuthibitisha ukweli kama alivyoshuhudia.

(2) Ndiyo sifa nyingine za kuwa mtume wa Kristo, k.m. alitakiwa kumwona Yesu na kuwa tayari kutoa ushahidi wa kile alichokiona haswa.
(3) Katika mst.22 sisitizo zaidi litatolewa juu ya mambo yaliyompasa mtume kuwa *shahidi wa kufufuka kwake Yesu kutoka kwa wafu*.
(4) Tena, ni wazi kabisa kwamba hakuna mtu aliye hai leo ambaye anaweza kuwa na sifa hizi!
(5) Kristo alikuwa amefanya kazi na mitume wake kwa zaidi ya miaka mitatu akiwaandaa kwa kazi hii maalum.
(6) Na alikuwa akihatimisha maandalizi yao maalum kwa kazi hii pekee kwa njia ya uweza wa Roho Mtakatifu ambaye aliwaahidi katika mstari huu:
   (a) Yoh.14:26.
   (b) Yoh.15:26,27.
(7) Mitume walianza kufanya kazi kama mashahidi wa Kristo katika Matendo 2:14ff
(8) Katika fungu hilo, walianza kushuhudia kwa msingi wa mambo waliyoona ambayo Yesu alitenda na kufundisha.
(9) Ni jambo la kufurahisha kuona asili ya neno lililotafsiriwa "mashahidi" (μαρτυρεσ).
   (a) Tunapata neno la Kiingereza "martyr" kutokana na neno hilo.
   (b) "Martyr" ni mtu aliyeona bora kuteseka au kufa kuliko kuiacha imani yake!
   (c) Hivyo ndivyo mitume wa Kristo walivyofanya na ndivyo pia watu wengi kuanzia hapo walifanya.
   (d) Waliamua kufundisha na kumhubiri Yesu, hata kama ingewapelekea kuteseka au kufa kwa ajili ya hilo.
   (e) Linga. Ufu.2:10.

d. Jambo la nne alilowaambia mitume wake katika 1:8, lililenga maswala ya kijiografia ambalo lilikuwa kutekeleza agizo kuu la Kristo. Walikuwa waanzie Yerusalem, kisha waende eneo la Uyahudi, Samaria, hata mwisho wa nchi.
   (1) Yesu alikuwa amewapatia mpango mzima wa kazi katika mistari kama vile Mk.16:15 na Math.28:19.
   (2) Sasa anawapatia maagizo maalum waanzie wapi na kuendelea kufanya kazi kwa ajili yake.
   (3) Pia, kama tulivyoona katika mazingira ya msingi, maagizo ya kijiografia husaidia kutoa kielelezo cha kitabu cha Matendo:
      I. Sehemu ya kwanza: (1-7) Kanisa lilianzishwa Yerusalem.
      II. Sehemu ya pili: (8-12) kanisa lilienea Yudea na Samaria.
      III. Sehemu ya tatu (13-28) kanisa lilienea hadi mwisho wa nchi.
   (4) Tazama ramani kuona agizo hili la kijiografia.
   (5) Lakini, kwa nini Bwana aliagiza kuzingatia agizo la kijiografia? Ndugu J. W. McGarvey katika fafanuzi (commentary) katika Matendo anatoa jibu la kimantiki kama hili:

      "Isidhaniwe kuwa mpangilio huu wa kazi yao uliandikwa kwa ajili ya ubaguzi wa Kiyahudi, ama kupangwa kwa kutimiza unabii tu. Bali ulitabiriwa kupitia manabii, kwa sababu kulikuwa na sababu za msingi. Sababu moja, inayoungwa mkono sana na wengi, kwa kuanzia Yerusalem, kulifaa kubainisha madai ya Yesu katika mji huo huo ambamo alihukumiwa. Lakini sababu inayotawala pasipo shaka ni hii: eneo hili ni lenye kundi la Wayahudi wacha Mungu, sehemu hiyo ambayo ilivutiwa zaidi na mahubiri ya matayarisho ya Yohana na Yesu, daima yalikusanya watu katika sikukuu za kila mwaka, na hivyo basi mwanzo wenye mafanikio ungefanyika hapo. Kutoka hapa, wakazi wa vijijini wa Yudea walijiandaa vema, lakini kwa mvuto huo huo, wa injili; kisha Wasamaria, ambao walikuwa wameona baadhi ya miujiza ya Yesu; na mwisho wa yote, Mataifa. Hivyo basi mpangilio wenye mafanikio ulitoa mwongozo kuanzia eneo moja hadi

lingine, na ikawa hivyo kwa mitume, hata katika nchi za wapangani, ilikuwa kuhubiri injili "kwanza kwa Wayahudi" na kisha "kwa Mataifa." Matokeo yake yanalingana na kanuni hii; Kwa mafanikio makubwa zaidi ya injili yalitokea Yudea, na njia bora zaidi ya kuwafikia Mataifa katika kila jimbo ilikuwa kwa njia ya masinagogi ya Wayahudi."

3. Muhtasari wa 1:3-8, ahadi iliyotolewa:
   a. Katika mst.3 tunaona kwamba Yesu alitoa ushahidi thabiti wa kufufuka kwake kwa kuwatokea baina ya wanafunzi wake kwa siku arobaini:
   b. Katika mst.4 aliwaambia mitume wake kusubiri Yerusalem hata watakapopokea ahadi ya Baba aliyowaahidi mapema.
   c. Katika mst.5 alisema kwamba ahadi ingetimia mara mitume watakapokuwa wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu.
   d. Katika mst.6 mitume walimwuliza Kristo iwapo angeurejesha ufalme kwa Israeli wakati huo.
   e. Katika mst.7 Yesu aliwaambia hawana haja ya kujua jawabu la swali hilo kwa sababu lilikuwa ndani ya maamuzi ya Mungu.
   f. Kisha, katika mst.8, Yesu aliwaambia mambo manne wangejua na walitakiwa kufahamu:
      (1) Wangepata nguvu.
      (2) Nguvu hizo wangezipata wakati Roho Mtakatifu akija juu yao.
      (3) Hivyo basi wangelikuwa mashahidi wake.
      (4) Wangeanzia Yerusalem, na kisha kwenda eneo la Uyahudi, Samaria, na hata mwisho wa nchi.

### c. (1:9-11) KUPAA KWAKE YESU

**9)**

1. Yesu alipaa na kuingia mawinguni mbele ya macho ya mitume.

**10)**

1. Watu wawili wakiwa katika mavazi meupe walisimama mahali waliposimama mitume wakizidi kutazama juu bminguni.
   a. Kuna sababu nyingi wanazodhania watu wengi kuwa watu hawa wawili walikuwa malaika halisi.
      (1) Walileta ujumbe ambao kwa kweli ulitoka kwa Mungu.
      (2) Luka anatumia picha hiyo hiyo katika kitabu chake cha injili (Lk.24:4).
      (3) Lakini, angalia Yohana anawataja watu kama hao (Yoh.20:12).

**11)**

1. Watu wawili (malaika) wanawaita mitume kuwa "*watu wa Galilaya*." Muundo huu wa mitume wa Kristo utakuwa muhimu haswa tutakapofika katika sura 2.
2. Kisha, wakatangaza kuwa Yesu angekuja tena "*jinsi mlivyomwona"* akienda mbinguni.
3. Lakini, kuna jambo gani la msingi kutaja kuja kwake kama alivyoondoka kwenda mbinguni?
   a. Kupaa kwake kulikuwa *dhahiri*, si kwa siri ama kwa kutoeleweka kama watu wengine wanavyofundisha leo (Ufu.1:7).
   b. Akapotelea mawinguni. Pia atarudi mara ya pili na mawingu (Ufu.1:7; 1 Thes.4:16,17).
   c. Malaika walitokea wakati wa kupaa kwake. Pia watatokea wakati wa kuja kwake mara ya pili (Math.25:31; 2 Thes.1:1-9).
   d. Alipaa kwa umbo lenye namna ya mwili. Atarejea tena kwa umbo lenye namna ya mwili, ingawa hatujui kuwa ni mwili wa namna gani atakuwa nao (Flp.3:20,21; 1Yoh.3:2).
4. Wakati tunajifunza mistari hii, ni jambo la maana kutambua umuhimu wa kupaa kwake Kristo kwenda mbinguni. Alipaswa arejee mbinguni ili:
   a. Kumtuma Roho Mtakatifu kwa mitume (Yoh.16:7),

   b. Atawale kama Mfalme katika kiti cha enzi cha ufalme wake wa milele (Dan.7:13,14; Mdo.2:32-36),
   c. Kuwakilisha damu yake ya upatanisho mara moja kwa dhabihu zote za dhambi (Ebr.9:12-14, 24-26), na
   d. Kuwa mpatanishi, mwombezi, mtetezi, wa Mkristo, ili kutupa sisi ujasiri wa kukiingia kiti cha neema (Heb.4:14-16; 1 Tim.2:5; 1 Yoh.2:1,2).
5. Pia, angalia uthabiti wa Yesu kurudi tena mara ya pili:
   a. Yesu alisema angerudi tena (Yoh.14:28).
   b. Malaika walisema angerudi tena (mstari huu).
   c. Mitume walidai angerudi tena (1 Thes.4:16-18; 2 Pet.3:4ff).
6. Muhtasari wa 1:9-11, kupaa kwake Kristo:
   a. Katika mst.9 Yesu alichukuliwa mawinguni, mbele ya macho ya mitume.
   b. Katika mst.10 watu wawili (malaika) wakasimama mbele za mitume walipozidi kutazama mbinguni.
   c. Katika mst.11 malaika walitangaza kuwa Yesu angerudi tena kwa jinsi ile ile alivyopaa kwenda mbinguni.

### d. (1:12-14) MITUME YERUSALEM

1. Mitume walirejea Yerusalem toka mlima wa Mzeituni kama Yesu alivyowaamuru (Lk.24:49; Mdo.1:4).
   a. "Mwendo wa Sabato" – takribani ¾ ya maili.

**13)**

1. Katika mstari huu imetolewa orodha ya nne ya mitume katika Agano Jipya. Tafadhali angalia ukweli kuhusu orodha hizi:
   a. Orodha mbili haziko katika mtiririko mmoja.
   b. Petro ametajwa wa kwanza katika nne zote. Hata hivyo, ukweli huu usitumike kumwinua Petro kuliko mitume wengine.
      (1) Yeye mwenyewe alidai, kuwa mtume wa Kristo, na wala si mkuu wa mitume (1 Pet.1:1).
      (2) Alikuwa mzee mwenzi wao wazee, na wala si mkuu wa wazee (askofu) (1 Pet.5:1).
      (3) Mitume wengine walipewa mamlaka sawa na Petro kufunga na kufungua mapenzi ya Mungu kwa njia ya neno lake (Math.16:18,19; 18:18).
      (4) Aliwaonya waliotenda dhambi kuwa kinyume na Mungu na wala si kinyume chake (Petro) wapate msamaha wa dhambi (Mdo.8:20-22).
      (5) Alikataa watu kumsujudia na kumwabudu (Mdo.10:25,26).
      (6) Paulo alimkemea alipotenda dhambi kwa kumwita mnafiki (Gal.2:11-14).
      (7) Kama ilivyokuwa kwa mitume wengine, alikuwa na haki ya kuoa na ni dhahiri alioa (Math.8:14,15; 1 Kor.9:5).
   c. Filipo ametajwa wa tano katika orodha zote.
   d. Yakobo, mwana wa Alfayo, ametajwa wa tisa katika orodha zote.
   e. Linga. Math.10:2-4; Mk.3:14-21; Lk.6:13-16.

**14)**

1. Mitume hawa walizidi kuungana na kuomba daima wakiwa na baadhi ya wanawake na ndugu zake Bwana!
   a. "Walidumu" – προσκαρτερουντεσ kuwa thabiti, kusimama imara, kushikama pamoja.
   b. "Kwa moyo mmoja"
      (1) ομοθυμαδον – kutoka ομοισ moja, na θυμοσ nia; kwa hiyo, kwa nia moja, ndivyo walivyoungana!
      (2) Linga. Rum.15:6

   c. Kama tunavyoona kupitia kitabu kizima, watu hawa na wakristo wa awali waliomba daima na kwa bidii (Linga. 1 Thes.5:17; Yak.5:16).
   d. Pia, wanawake kama vile Mariam Magdalena, Mariam mama yake Yakobo na Jose, na Yoana, na Suzana mara nyingi wametajwa kama wafuasi waadilifu wa Bwana hadi mwisho (linga. Lk.8:2,3; 23:49,55; 24:10).
   e. Mariamu ametajwa kwa mara ya mwisho hapa, mama yake Yesu.
   f. Angalia ndugu zake Yesu wametajwa wakiwa na mitume.
      (1) Ndugu hao ni Yakobo, Yusufu, Simoni, na Yuda (Math.13:55).
      (2) Hawakumwamini Yesu hapo nyumba (Yoh.7:5).
2. Mhutasari wa 1:12-14, mitume Yerusalem:
   a. Baada ya kupaa kwake Yesu mitume walirejea Yerusalem (mst.12).
   b. Walikwenda orofani walikokuwa wakikaa (mst.13).
   c. Walidumu katika sala na katika umoja (mst.14).

### e. (1:15-26) KUCHAGULIWA KWA MATHIYA

**15)**
1. Petro alianza kuwaeleza watu karibu 120, wanafunzi wa Yesu.

**16)**
1. Petro alisema kwamba Roho Mtakatifu alinena kuhusu Yuda kupitia Daudi, juu ya mwenye kumsaliti Yesu.
   a. Baadaye atafafanua mambo ambayo Daudi alinena yaliyomhusu Yuda.
   b. Amethibitisha kwa kunukuu Zaburi mbili katika mstari 20.
   c. Ni jambo la kufurahisha kuona kwamba Yesu pia alinukuu kutoka katika Zaburi mambo ambayo yalimlenga Yuda:
      (1) Yohana 13:18.
      (2) Zab.41:9.
2. Katika mst.16 tunaona pia nukuu dhahiri juu ya mafundisho ya kweli ya uvuvio wa Biblia.
   a. Petro alisema, "…Roho Mtakatifu alitangulia kunena kwa kinywa cha Daudi…" (haswa ikirejea katika Agano la Kale).
   b. Hili linabainisha kwamba Roho Mtakatifu alimwongoza Daudi (na waandishi wengine wenye kuvuviwa) kunena maneno ya Mungu. Haya si maneno aliyobuni Daudi pasipo msaada wa Mungu.
   c. Kama nabii wa Mungu, Daudi alitiwa nguvu kunena maneno haswa ambayo Mungu alitaka anene kwa kufunua maandiko ambayo Petro ameyanukuu katika mistari hii.
   d. Kwa hiyo, siyo tu dhana au mawazo yanatoka kwa Mungu, bali kila neno kwa asili ya ufunuo lilitoka kwa Mungu, na wala si kwa wanadamu. Jambo hilo ndilo linatajwa kuwa maneno halisi (verbal), kamili (plenary) yenye uvuvio (inspiration).
   e. Linga. 2 Sam.23:2; Yer.1:9; 2 Pet.1:20,21, 2 Tim.3:16.

**17)**
1. Petro alibainisha kwamba Yuda miongoni mwa wale asilia kumi na mbili waliochaguliwa na Yesu mwenyewe kwa ajili ya kazi maalum ya mitume (Lk.6:3-16).

**18,19)**
1. Mistari hii inaonekana kuwa mawazo yaliyovuviwa yaliyoingizwa na Luka, si mwendelezo wa hotuba ya Petro kwa wanafunzi 120.
   a. Sababu moja iliyoleta hatimisho hili ni kwamba mst.19 una maneno, "…*kwa lugha yao, Akeldama, maana yake 'Konde la Damu*.'"
   b. Maneno "*lugha yao*" yanarejea lugha ambayo ilizungumzwa na watu wenye asili ya Kiyahudi na anatoa tafsiri ya neno "*Akeldama*."

(1) Lakini katika mistari miwili iliyotangulia (16,17) Petro, mwenye asili ya Kiyahudi, alikuwa akizungumza kwa watu wenye asili ya Kiyahudi.
(2) Kwa hiyo, asingetaja lugha yake mwenyewe kama, "*lugha yao wenyewe*"!

c. Kwa upande mwingine Luka, ambaye alikuwa Mmataifa na aliyewaandikia watu wenye asili ya Mataifa, angeitaja lugha ya Kiebrania kama lugha yao.
d. Kwa kulinganisha, lisingekuwa jambo la maana kwa Petro, akiwa Myahudi, angeona haja ya kufafanua maana ya maneno "*Akeldama*" kutoka katika lugha yao kwa uma wa Wayahudi.
e. Lakini Luka, akiwa Mmtaifa akiwaandikia Mataifa, angeona haja ya kutafsiri maneno haya ya Kiebrania – anasema maana yake "*Konde la Damu*."
f. Kwa sababu hizi tunahatimisha kwamba mistari 18,19 ni mawazo ambayo Mungu alimwongoza Luka kufunua akiwa na lengo maalum.

2. Katika mistari hii miwili, (18,19), Luka anatueleza mambo mengi kuhusu Yuda:
a. Kwanza, alinunua konde kwa "*ijara ya udhalimu,*" k.m. na fedha alizopokea kwa ajili ya kumsaliti Bwana Yesu.
b. Pili, alikufa kifo kibaya sana, kimeelezwa mwishoni mwa mst.18.
c. Na tatu, konde hilo likajulikana kama Konde la Damu.
(1) Luka anasema jina hili liliteuliwa kwa ajili la konde kwa sababu ya kifo kibaya alichokufa Yuda hapo (18,19).
(2) Mathayo anadai jina hili liliteuliwa kwa sababu ya konde lililonunuliwa na "*fedha za damu*" k.m. fedha alizozipokea kwa kumsaliti Yesu (Math.27:6-8).
(3) Jina hilo pengine lilitokana na mambo mawili yote ya ukweli huo na ni njia sahihi haswa kuliita konde.

3. Wengine wanadai kwamba mst.18,19 Luka anapingana na habari za Mathayo juu ya ukweli huo kama unavyopatikana katika Math.27:3-10. Tutachanganua madai haya sasa na kuthibitisha kwamba ni ya uongo.
a. Kwanza, inadaiwa kuwa Yuda ndiye alinunua konde (18), lakini Mathayo anadai makuhani wakuu walinunua konde (Math.27:6,7).
(1) Kuna kupingana hapa!
(2) Yuda alizirudisha fedha za usaliti kwa makuhani wakuu (Math.27:3-5).
(3) Makuhani wakuu walikataa fedha hiyo isirejeshwe katika hazina kwa sababu ni "*fedha yenye damu*" (Math.27:6).
(4) Badala yake, walizitumia fedha hizo za Yuda kununulia konde (Math.27:7).
(5) Basi, ni vyema kudai Yuda alinunua konde kwa kuwa alizitoa fedha kwa makuhani, ambao walizitumia kununulia konde.
(6) Hii ni njia ya kawaida ya kusema – kile anachofanya mtu anakifanya kupitia wengine, ni kawaida kuzungumza kama yeye mwenyewe anatenda.
(7) Kwa mfano mwingine wa Kibiblia namna hii ya kuzungumza, jifunze Yoh.4:1,2.

b. Pili, inadaiwa kupingana kwa kuwa Mathayo alisema Yuda alijinyonga mwenyewe, wakati Luka anadai kuwa akaanguka kwa kasi akapasuka matumbo yake yote yakatoka.
(1) Tena, hakuna kupingana hapa!
(2) Mathayo amedai kuwa alijinyonga mwenyewe (Math.27:5).
(3) Na Luka alidai Yuda alianguka na kupasuka matumbo (mst.18).
(4) Hata hivyo, si maelezo yanayopingana, bali maelezo aina mbili yenye kuchangia!
(a) Maelezo yenye kutoa mchango ni yale, ambayo pale unapojumuisha pamoja, hutoa maelezo kamili ya mambo jinsi yalivyo.
(b) Ili kufafanua, ebu na tuangalie mfano wa Kibiblia wa michango miwili yenye kuunga mkono maelezo:
1. Math.26:51.
2. Yoh.18:10.
(5) Sasa, ebu na tuone jinsi maelezo ya Mathayo na Luka yenye uvuvio kuhusu kifo cha Yuda yanavyoshabihiana, unapounganisha pamoja.

(a) Yuda alijinyonga mwenyewe kama Mathayo alivyosema.
(b) Kisha, ama tawi alilojinyonga juu yake ama kamba ilikatika.
(c) Lilipotukia jambo hilo, Yuda alidondoka kutoka mtini na kupasuka matumbo katikati ya mwili wake, kama Luka alivyosema.

(6) Hivyo basi, tunazo sababu za maelezo ya msingi za michango hii, maelezo yenye uvuvio na hayawezi kujipinga kamwe.

**20)**

1. Kwanza Petro alinukuu Zab.69:25 na kisha Zab.109:8.
   a. Hii ndiyo mistari Petro anarejea mst.16 wa sura hii kama ilivyonenwa na Roho Mtakatifu kwa kinywa cha Daudi.
   b. Na Petro kwa uvuvio wa Mungu anasema kwamba yaliyonenwa katika Zaburi yalimlenga Yuda. Namna gani ukweli huu?
      (1) Kwanza, katika Zab.69:9 ni moja ya hukumu kwake yeye aliyemsaliti Kristo, na mahali pake msaliti huyo kuwa ukiwa, pasipokaliwa, na kuwa magofu.
         (a) Ni jambo la kufurahisha kuona kwamba maeneo kadhaa katika Zab.69 yamenukuliwa mara kwa mara yakimlenga Masihi.
         (b) Kwa mfano, angalia Zab.69:9 na Yoh.2:17, na Zab.69:21 na Math.27:34,38.
         (c) Basi, ni sahihi kabisa Zaburi 69 pia ina unabii unaomhusu Yuda msaliti wa Masihi!
2. Pili, wazo katika Zab.109:8 ni kwamba Yuda kama msaliti wa Kristo alipoteza ofisi yake kama mtume na kwamba mwingine angechukua nafasi yake.
   (a) Wazo hili, k.m., nafasi ya Yuda kuchukuliwa na mwingine, huonyesha mpango dhahiri wa mistari kadhaa inayofuata.

**21,22)**

1. Petro ametoa sifa mbili muhimu ambazo alipaswa mtu kuwa nazo ili kuchukua nafasi ya Yuda:
   a. Kwanza, mtu huyo ilimpasa awe miongoni mwao mitume wakati "wote" Yesu alipokuwepo na kufanya kazi pamoja nao (mst.21).
      (1) Kipindi chote inajumuisha wakati kuanzia ubatizo wa Yohana hadi kupaa kwake Kristo kwenda mbinguni, k.m., "*siku aliyochukuliwa kwetu kwenda juu*" (mst.22).
      (2) Linga. Yoh.15:26,27.
   b. Pili, nafasi ya Yuda ilitakiwa aichukue mtu aliyemwona Kristo baada ya kufufuka kwake (mst.22).
      (1) Kumbuka somo letu katika maelezo juu ya ushahidi mst.8.
      (2) Shahidi ni mtu mwenye kuona jambo na ambaye kimsingi anatafuta namna ya kuthibitisha ukweli kwa ushuhuda wake.
      (3) Basi, mwenye kuchukua nafasi ya Yuda ni sharti awe amemwona Kristo baada ya kufufuka kwake na awe tayari kuwaeleza wengine kuhusu jambo hilo.
   c. Lakini kwa nini ilikuwa muhimu kwa mtume kuwa shahidi wa ufufuo wa Yesu?
      (1) Ilikuwa ni kuthibitisha kuwa Yesu alikuwa Masihi neno lenye kumaanisha "Kristo" (Yoh.1:41)!
         a. Luka 24:44-48.
         b. Rum.1:4.
      (2) Angalia, ni mitume *tu* waliofanya kazi ya kutoa ushahidi na ona jinsi walivyotoa ushuhuda wa ufufuo wa Yesu:
         (a) 2:32.
         (b) 3:15.
         (c) 5:29-35.
         (d) 10:39-41.
         (e) 13:30,31.

(f) 4:33
(3) Nguvu nyingi za ushahidi wao zimeonekana katika maneno makuu matatu:
(a) Idadi yao: kulikuwa na mashahidi kumi na mbili, wala si mmoja au wawili tu.
(b) Kuafikiana kwao: kwa ujumla mitume wote walikubaliana kabisa.
(c) Maisha yao: walikuwa majasiri bila hofu wakikabiliana na mateso – hata kama walipigwa hadi kufa kwa ajili ya Bwana Yesu.
(4) Leo, tuna maandishi ya mashahidi hao ambao walishuhudia kwa macho ya namna ya kipekee yaliyoandikwa katika Agano Jipya la Bwana wetu na Mwokozi, Yesu Kristo!
(5) Si jambo la ajabu basi ufufuo wa Yesu toka kwa wafu kuwa msingi wa imani ya Ukristo?
(a) 1 Kor.15:17.
(b) Yoh.17:20.
(c) Yoh.20:28,29.
(6) Leo, kwa kuwa hakuna miongoni mwetu anayeweza kuwa "shahidi" neno hilo kwa maana ile ya Biblia, kazi yetu ni kuhubiri na kufundisha neno la Mungu (2 Tim.4:2; Mk.16:15; Math.28:19, 20)!

c. Tena, tunaona hakuna mtu mume au mke anayeishi leo ambaye anaweza kuwa na sifa za kuwa mtume wa Kristo kama zilivyotolewa katika kitabu hiki na vitabu vingine vya Agano Jipya:
(1) Kuchaguliwa moja kwa moja na Mungu (mst.2).
(2) Kuwa shahidi wa Kristo, neno hilo kwa maana ile ya Biblia (mst.8).
(3) Kuwa pamoja na Yesu na mitume wake kuanzia ubatizo wa Yohana hadi kupaa kwake Yesu (mstari huu; Yoh.15:26,27).
(4) Kuwa shahidi wa kufufuka kwake Yesu (mstari huu).
(5) Kupokea nguvu kwa Roho Mtakatifu ili kutenda mambo kadhaa:
(a) Kwanza, kukumbuka pasipo kukosea yote ambayo Yesu mwenyewe aliwaambia (Yoh.14:26).
(b) Pili, kuandika bila ya kukosea ukweli wote, neno la Mungu, amri za Bwana (Yoh.16:13; 1 Kor.14:37).
(c) Tatu, kuthibitisha kwamba ujumbe huo ulitoka kwa Mungu pamoja na miujiza mikubwa (2 Kor.12:12).

**23)**

1. Watu wawili walipendekezwa waliokuwa na sifa hizo maalum zilizowekwa. Mmoja aliitwa Yusufu, aitwaye Barsaba, aliyekuwa na jina la pili Yusto, na mwingine aliitwa Mathiya.

**24,25)**

1. Mitume waliomba mapenzi ya Mungu yatendeke katika kuchagua baina ya hao wawili. Kwa nini walifanya hivyo?
   a. Walitambua wote wawili walikuwa na sifa za kuwa mitume.
   b. Lakini walitambua pia kuwa Mungu anajua mioyo ya wanadamu wote na walipenda mapenzi yake yafanyike!
(1) Mungu angejua kuwa ni nani kati ya hao wawili angefaa zaidi kufanya kazi kama mtume.
(2) "*Ujuaye mioyo*" – καρδιογνωστα haswa ikimaanisha "mwenye kujua moyo."
(3) Mambo ya msingi: ni jambo la busara kutambua ukweli kwamba Mungu anajua yaliyomo ndani ya mioyo yetu!
(4) Tunaweza kuwa wajinga ama kupumbaza wengine, lakini hatuwezi kumdanganya Mungu!
(a) Kulingana na swala hilo, tafadhali angalia mafungu yafuatayo:
1. 1 Nyakati 28:9.
2. Zaburi 139:1-4.

3. Waebrania 4:12,13.
(b) Tukishajua hilo, tunapaswa mimi na wewe tufanye nini basi?
1. Mithali 4:23.
2. 2 Wakorintho 10:5.
3. 2 Wakorintho 7:1.
4. Mathayo 5:8.
5. Wafilipi 4:8.

c. Angalia katika mst.24 mitume walijua kwamba kuchukua nafasi ya mtume aliyeanguka ilikuwa ni kazi ya Mungu pekee mwenye uwezo wa kuteua.
(1) Wakizungumza mbele za Mungu, mitume waliomba, "…*tuonyeshe ni nani uliyemchagua*."
(2) Kama vile Yesu alivyochagua mitume kumi na mbili, wale kumi na moja walitaka Mungu achague mtu atakayembadili Yuda.

d. Pia, angalia maneno yaliyotumika yenye nguvu kuhusu Yuda katika mazingira haya, katika sala, na katika sehemu zinginezo za Biblia.
(1) Alikuwa mtume kama vile mitume wengine kumi na moja walivyokuwa (mst.17).
(2) Walakini, aliwaongoza maadui wa Kristo kumkamata (mst.16).
(3) Alianguka kutoka katika ofisi yake asiwe mtume wa Kristo (mstari huu).
(4) Alianguka katika makosa, k.m., kwa dhambi, ambayo ilivunja sheria ya Mungu (mst. huu; 1 Yoh.3:4).
(5) Alifikia hatima mbaya sana kwa jinsi alivyojinyonga mwenyewe na kuanguka, akapasuka matumbo (mst.18; Math.27:5).
(6) Konde lililonunuliwa kwa fedha ya usaliti liliitwa "Konde la Damu likiwa ukumbusho wa kitendo chake kibaya cha uharibifu (mst.19).
(7) Ametajwa kwa uvuvio kuwa msaliti (Luka 6:16).
(8) Alikuwa mwizi (Yoh.12:6).
(9) Yesu alimwita mwana wa upotevu (yaani kuangamia kabisa, kupotea haswa kwake) (Yoh.17:12).
(10) Yesu alisema ni heri kwake kama asingelizaliwa (Math.26:24).
(11) Pia, alikwenda zake mahali pake mwenyewe (mstari huu).
(12) Je, hapa kuna shaka yoyote kwamba mmoja wa watu wa Mungu anaweza kuanguka kutoka katika neema kwa namna ambayo apoteze wokovu wake (linga. Gal.5:4; 1 Kor.9:27; 2 Pet.2:20-22)?

e. Luka alisema baada ya kuanguka kwake Yuda kwa uasi, alikwenda mahali pake mwenyewe. Tutajadili tutakapofika 2:25-28 mahali ambapo alikwendaYuda.

f. Wengine hudai mistari hii mitume waliomba kwa Yesu na wala si kwa Baba.
(1) Siamini kwamba mitume waliomba kwa Yesu.
(2) Imani hiyo inasimamia juu ya kujifunza kwa makini mistari hii na mafundisho dhahiri ya Agano Jipya kwamba Wakristo wanapaswa kuomba kwa Baba kupitia Mwanawe Yesu (Ebr.7:25).
(3) Maelezo zaidi kujifunza kuhusu ama mitume waliomba kwa Yesu yanapatikana katika notisi zilizoandikwa juu ya mistari hii.

g. Maelezo ya kuchanganua zaidi ya swali juu ya ombi hili kama lilitolewa kwa nani.
(1) Baadhi wanadai mitume walisali kwa Yesu kwa kuwa ndiye aliyechagua mitume asilia kumi na mbili na kwa sababu sala imeelekezwa kwa "Bwana."
(2) Wengine wanadai mitume walisali kwa Baba.
(3) Ili kuliweka bayana swali hili, mambo kadhaa ya uhakika sharti yaangaliwe:
(a) Kwanza, hakuna shaka Yesu mara nyingi ametajwa kuwa "Bwana" (linga. Lk.24:34).
1. Lakini, ni kweli pia kwamba Baba anatajwa kuwa "Bwana" (linga.Ebr.7:21; 8:8,9,10,11; Ufu.4:8; 11:17; 15:3,4; 16:5; 19:6; 21:22

   2. Kwa hiyo, ombi hili kumlenga "Bwana" si ushahidi wa kutosha kudai kuwa lilimlenga Yesu.
   3. Ukweli ni kwamba, inaonekana jambo la msingi kuhusu sala za kwanza mara baada ya kuanzishwa kwa kanisa, mitume walimwomba Baba katika sala wakimwita "Bwana" (Mdo.4:24,29)!

(b) Pili, ni kweli Yesu aliwachagua mitume wa kwanza kumi na mbili (1:2).
   1. Hata hivyo, ukweli huo tu hautoshelezi kudai kuwa sala hiyo ilikuwa kwa Yesu.
   2. Jambo hili tu ni kweli sala ingetolewa kwa Yesu ingekuwa kinyume na mapenzi ya Baba, kama tutakavyojadili muda mchache.
   3. Kwa nyongeza, Yesu alipokuwa duniani, mambo aliyofanya (ukijumlisha kuchagua mitume kumi na mbili) yalifanyika kwa mamlaka ya Baba (Math.28:18; Yoh.17:1,2).
   4. Kwa hiyo, baada ya Yesu kuondoka duniani, ingelikuwa jambo la kawaida kutarajia kwamba mambo aliyoyafanya alipokuwa hapa (kama vile kuchagua mitume) yangefanywa na Baba.

(c) Tatu, ni kweli kwamba Yesu alitambua mioyo ya watu (Yoh.2:24,25; 6:64; Ufu.2:19).
   1. Kumbuka kwamba ombi hili aliombwa yeye ajuaye mioyo ya wote (mst.24).
   2. Lakini Baba pia mara nyingi ametajwa kuwa anayejua mioyo ya watu (1 Nya.28:9; Zab.139:1-4, n.k.).
   3. Kusema ukweli, ulinganifu bayana wa nafasi ya Yuda kupewa mtu mwingine unapatikana katika 1 Sam.16
      a. Mst.1 Mungu alimkataa Sauli asitawale juu ya Israeli na akamtuma Samweli kwa Yese kumtafuta mtu ambaye angechukua nafasi kati ya wanawe.
      b. Mst.2,3 Samweli alimwomba Bwana ampatie uthabiti wa jambo hilo; hivyo Bwana akamwaahidi Samweli angemwonyesha ambaye angemtia mafuta kuwa mfalme.
      c. Mst.4,5 Samweli alikwenda Bethlehem na akamwita Yese na wanawe.
      d. Mst.6 Samweli akamwaangalia Eliabu na kuamini kuwa ndiye mtu ambaye angechukua nafasi na huyo ndiye aliyemchagua Mungu.
      e. Mst.7 Bwana alimwambia Samweli asiangalie umbo la nje.
      f. Mst.12 Bwana alimchagua Daudi kama mtu atakayejaza nafasi iliyoachwa na Sauli.
   4. Ukweli ni kwamba tukio hilo lilitendeka kabla ya Yesu kuja duniani kama Mwana wa Mungu.
   5. Lakini, inawezekana pengine mitume walikuwa na tukio hilo akilini mwao na walikuwa wakimwita Baba katika njia ile Samweli alifanya katika tukio lile.
   6. Kwa hiyo, tunaona kwa namna nyingine ukweli kwamba ombi limeelekezwa kwa "Bwana" huo si ushahidi wa kutosha kudai lilielekezwa kwa Yesu.

(d) Mwisho, Mungu ametoa maagizo bayana katika Agano Jipya kwamba tunapaswa kuomba kwake, kupitia Mwanawe Yesu na wala si moja kwa moja kwa Yesu.

(e) Hiyo ndiyo amri na kielelezo ambacho ametupatia tukifuate katika mafungu kama yafuatayo:
   1. Kitabu cha Matendo – 4:24, 29; 12:5; 16:25; 27:35.
   2. Mathayo 6:6, 9.
   3. Yohana 16:23,24 (linga.14:13,14; 15:16).
   4. Waefeso 5:20.
   5. Waebrania 7:25.

**26)**

1. Mitume walitafuta mapenzi ya Mungu katika kupiga kura, na Mathiya alichaguliwa kuchukua nafasi ya Yuda.
   a. Kupiga kura juu ya mambo muhimu na magumu ilikuwa jambo la kawaida kwa Wayahudi katika kipindi cha Agano la Kale.
   b. Baadhi ya mifano ya kupiga kura katika Agano la Kale ilijumuisha mambo yafuatayo:
      (1) Daudi aliwagawa makuhani kwa kupiga kura (1 Nya.24:5).
      (2) Nchi ya Kanaani iligawanywa kwa kupiga kura (Hes.26:55; Yosh.15-17).
      (3) Akani alitambuliwa kwa kupiga kura (Yosh.7:16-18).
   c. Katika kupiga kura, Wayahudi walisihi wapate maamuzi kutoka kwa Mungu. Jambo hili halikuwa swala la kuteua au kuchagua (Mith.16:33).
   d. Haijafunuliwa ni namna gani mitume walifanya kupiga kura hii.
   e. Hata hivyo, kanuni kadhaa zilizoandikwa zilizotumika na Wayahudi zinaweza kupatikana katika maandishi kwa ajili ya mstari huu.
      (1) Richard Lenski na watoa maoni wengine kadhaa wanatambua kanuni zifuatazo:
         (a) Nembo mbili, kila moja ikiwa na jina juu yake, iliwekwa chomboni.
         (b) Chombo kilitikishwa kwa nguvu hata kufanya nembo moja ianguke chini.
         (c) Nembo hiyo ilionyesha uchaguzi wa Mungu alioufanya.
      (2) Albert Barnes, maoni yake katika Matendo anafafanua kanuni nyingine kama ifuatavyo:
         (a) Majina ya watu yaliandikwa katika vipande vya mawe, vimbao, n.k. na kuwekwa chomboni.
         (b) Majina ya ofisi, maeneo ya nchi, n.k. yaliwekwa katika chombo kingine.
         (c) Nembo moja ingeandikwa bila mpangilio katika chombo kilicho na majina na nyingine katika chombo kilicho na ofisi, n.k.
         (d) Majina yangeshabihiana na ofisi hiyo, n.k.
         (e) Hatua hii ingeendelea hadi kila jina kuwa sambamba na ofisi, eneo la nchi, n.k.
      (3) Inaonekana kuwa hatua iliyofanyika hapa na mitume inafanana na maoni aliyotoa Lenski.
   f. Lakini, kwa hali yoyote ile, ni muhumi kutilia mkazo kwamba hatua hii haikuwa kuchangua kwa kupiga kura!
   g. Ni muhimu pia kusisitiza kwamba kupiga kura hakujatokea tena katika Agano Jipya.
   h. Sababu kadhaa tunaweza kuzitoa kwa nini hatua hii ilitumika katika jambo hili na ni katika jambo hili pekee:
      (1) Mitume walikuwa katika kipindi cha mpito kati ya kupaa kwake Kristo na ujio wa Roho Mtakatifu.
         (a) Yesu alikuwa amerejea mbinguni; kwa hiyo, hakuwepo ili mitume wamwulize moja kwa moja wapate maongozi yake kama walivyofanya hapo nyuma.
         (b) Mitume walikuwa bado kubatizwa kwa Roho Mtakatifu kuwaongoza katika kweli yote, neno la Mungu.
         (c) Hawakuwa na Agano Jipya kujifunza na kulitumia kutoa maamuzi.
      (2) Kwa hiyo, swala hili lina mambo ya kipekee ambayo hatuna siku zetu hizi.
      (3) Kuanzia muda huo, Yesu alimtuma Roho Mtakatifu aliyeahidi kuwaongoza mitume kufunua Agano Jipya, ambalo:
         (a) Lina mambo yote yapasayo uzima na utauwa (2 Pet.1:3,4).
         (b) Linafaa kwa mambo mengi, ukijumuisha na kutukamilisha kiroho, kukamilika katika mambo yote tayari kutenda kila tendo jema (2 Tim.3:16,17).
         (c) Linaweza kutufanya tuwe na hekima (2 Tim.3:15).
         (d) Litatusaidia kuwa na nia ya Kristo na kutenda mambo yote anayotaka sisi tufanye kupitia yeye mwenye kututia nguvu (Flp.2:5; 4:13)
         (e) Kupiga kura si njia tunazotumia siku hizi. Badala yake, tunatambua mapenzi ya Mungu kwa njia ya kujifunza, kutafakari Maandiko, kulitendea kazi neno la Mungu, na kwa kusali sana.

2. Kabla ya kuondoka mistari 15-26, mambo muhimu ya kuyatendea kazi katika mistari hii ni kuchanganua madai ya baadhi ya watu katika dini za ulimwengu wa leo.
   a. Wengine hudai wana mitume.
   b. Wengine hudai wana mamlaka maalum ama moja kwa moja au vinginevyo kutoka kwa mitume wa Kristo.
      (1) Wanadai kwamba wana mamlaka ya kufunua na/au kutafsiri maandiko, au,
      (2) Kutawala wengine mahali ambapo Agano Jipya halijaamuru.
   c. Mambo haya yote tunaweza kuhatimisha kwa kichwa, "kurithi utume."
3. Majibu kwa ufupi yametolewa katika kujibu madai haya.
   a. Kwanza, hakuna mitume au watu wengine leo ambao wananena, fundisha, au amuru kwa mamlaka ya Mungu kama mitume wa Kristo walivyofanya kwa kuwa hakuna mwanadamu mwenye sifa leo za kufanya hivyo (angalia maelezo yetu ya 1:3,21,22)!
   b. Pili, Agano Jipya ni ufunuo wa mwisho wa mapenzi ya Mungu kwa mwanadam; kwa hiyo, hakuna mtu mwenye mamlaka kufunua maandiko mengine leo (Yuda 3).
   c. Tatu, kila Mkristo ni kuhani na Mungu ametuonya kuwaangalia wanaojaribu kutafsiri maandiko kwetu (1 Pet.2:5; 2 Tim.2:15; Math.7:15).
   d. Nne, mfumo wa uongozi wa kanisa ni rahisi:
      (1) Kristo ni kichwa pekee cha kanisa lake (Kol.1:18).
      (2) Wazee wengi wenye sifa maalum katika kila kusanyiko linalojitegema la kanisa la Bwana (Mdo.14:23; 1 Pet.5:1,2).
      (3) Mashemasi kuhudumu katika kila kusanyiko (1 Tim.3:8-12).
      (4) Wahubiri kuhubiri injili (Rum.10:14,15).
      (5) Nafasi nyingine yoyote mbali na hizo iliyoanzishwa na wanadam kutawala haijaamuriwa na Mungu na hivyo basi ni dhambi (Math.20:20-28)!
4. Kwa wote wanaopenda maelezo mengi juu ya madai haya wanaweza kuona katika notisi zilizochapwa.
   a. Kwanza, je tuna mitume leo wanaonena, fundisha, na wenye mamlaka ya Mungu, kama mitume wa Kristo walivyofanya?
      (1) Biblia inajibu swali hili, jibu ni hapana kabisa!
      (2) Kama tulivyojadili mara nyingi, hakuna mtu anayeishi leo mwenye sifa za kuwa mtume kama zilivyoorodheshwa katika masomo yetu ya 1:21,22.
      (3) Lakini, mtu mwingine anasema, "Je, unaonaje mtume Paulo?"
         (a) Kulikuwa na sifa moja tu ambayo Paulo hakuwa nayo. Hakuwa pamoja na Yesu, tangu ubatizo wa Yohana.
         (b) Lakini, Paulo alikuwa na sifa zingine zote! Je, kuna mtu yeyote anayeishi siku hizi anayeweza kudai madai hayo? Hakika kabisa hakuna!!
         (c) Mbali na hivyo, Paulo alikuwa mtu pekee, mwenye sababu maalum:
            1. 1 Kor.15:8-11.
            2. Mdo.9:3-6.
            3. Mdo.26:15-18.
            4. Je, kuna mtu yeyote ambaye anaweza kudai hivi? Hakika hakuna!
      (4) Hivyo basi, hatimisho pekee ambalo tunaweza kutoa kiuhakika ni kwamba hakuna mitume leo wanaonena, fundisha, na kuamuru kwa mamlaka ya Mungu, kama vile mitume wa Kristo walivyofanya.
   b. Pili, je, kuna watu ambao wanaishi sasa ambao wana mamlaka ambayo waliyapokea kutoka kwa mitume moja kwa moja au kwa njia nyingine (indirectly) kutoka kwa mitume wa Kristo kufunua na/au kutafsiri maandiko?
      (1) Mungu anabainisha wazi katika maneno yake ya Agano Jipya kuwa ndio ufunuo wa mwisho wa mapenzi yake kwa mwanadamu. Kwa hiyo, mtu yeyote anayedai kufunuliwa zaidi maandiko anapingana na Mungu, na hivyo basi ni mwongo!
         (a) Yohana 16:13.
         (b) 2 Petro 1:3.

(c) Yuda 3.
(d) Ufunuo 22:18-19.

(2) Tena, hakuna mamlaka ndani ya maandiko "kurithi" nafasi za mitume wa Kristo.
(a) "Mrithi" ni mtu ambaye anafuata nyuma ili kukalia ofisi, cheo, n.k.
(b) Katika Agano Jipya, Yuda ni mtume pekee ambaye ndiye alilirithiwa, na swala lake lilikuwa la kipekee kwa njia zifuatazo:
1. Yuda alipaswa abadilishwe kwa kuwa alianguka kutoka katika ofisi kutokana na dhambi zake (1:25) na wala si kwa sababu alikufa na mtume mwingine alihitajika kumrithi!
2. Kwa nyongeza, maamuzi ya nani achukue nafasi ya Yuda haikufanywa na wenye hekima, washiriki wenzake, au mtu yeyote kama inavyofanyika katika ulimwengu wa dini siku hizi.
a. Badala yake, mitume wa Kristo waliomba kwa Mungu ili aamue kwa mikoni yake (mst.24,25).
b. Na wakapiga kura kama taratibu zilizojulikana za kutafuta maongozi ya Mungu (mst.26).
c. Basi, uteuzi wa kubadilisha aliachiwa Mungu ambaye anajua mioyo ya watu – siyo kupiga kura na wanadamu dhaifu wasiojua mioyo ya wengine!
3. Tazama pia Petro alitumia maandiko maalum ya Agano la Kale ambayo yalitabiri usaliti wa Yuda kama mamlaka ya kuchukua hatua hiyo (mst.20).
a. Katika moja ya mistari hii, (Zab.109:8), ilitabiriwa kuwa mwingine angelitwaa ofisi yake yeye alifanya makosa (Yuda).
b. Kwa msingi wa unabii huo maalum katika maandiko, Petro anahatimisha kwamba Yuda ofisi yake angeichukua mtu mwingine ("basi", mst.21).
c. Kwa hiyo, badala ya kuanzisha mfumo wa kutumia kurithisha mitume siku zijazo, kurithi mahali pa Yuda lilikuwa tukio la mara moja.
d. Lilikuwa jambo la kipekee hata maamuzi ya kumrithi Yuda yalifanywa kwa sababu Mungu alitabiri nafasi yake kuchukuliwa na mwingine hapo nyuma katika neno lake.

(c) Walakini katika somo la "urithi wa utume", wawili tu ndio waliochaguliwa baada ya wale wa kwanza kumi na mbili walioteuliwa na Kristo.
1. Matukio yote mawili ni ya kipekee, ukijumuisha Mungu kuhusika na kadhalika kukubali, haswa yalikusudiwa na Mungu na wala hayakurudiwa.
2. Tukio la kwanza lilikuwa la Yuda, ambalo tumejifunza tayari.
3. Tukio la pili lilikuwa la Paulo ambalo tumejifunza mapema. Utakumbuka swala lake lilikuwa la kipekee kwa kuwa:
a. Ni mmoja "aliyezaliwa kabla ya majira yake" na alikuwa wa mwisho kumwona Bwana (1 Kor.15:8).
b. Alikabiliana moja kwa moja na Yesu katika maono, na mashahidi waliokuwepo (Mdo.9:3-6).
c. Alichaguliwa moja kwa moja na Kristo kwa kazi maalum (Mdo.26:15-18).

(d) Ni jambo la msingi kutambua kwamba kifo cha mtume mmoja tu kimeandikwa katika Agano Jipya – Yakobo, nduguye Yohana (Mdo.12:2).
1. Ni jambo muhimu sana kutambua kwamba mtu yeyote hakuchaguliwa kurithi mahali pa Yakobo kama mtume.
2. Swala hili linafanana na hoja zetu kwamba nafasi ya Yuda kuchukuliwa na mtu mwingine na kuchaguliwa kwa Paulo kimiujiza ni ya aina yake, tukio lililofanyika mara moja, na wala halikurudiwa tena.
3. Njia nyingine ya kuhatimisha ni kuonyesha kwamba "urithi wa mitume" siyo fundisho la kibiblia ama linalokubalika na Mungu!

c. Tatu, ebu na tujibu swali kwamba kuna yeyote aliyepewa mamlaka na Kristo au mitume wake

kutawala wengine mahali ambapo Agano Jipya haliamuru kwa njia ya uwezo wao wa kufunua na kutafsiri maandiko.

(1) Ni wazi kwamba kila Mkristo ni kuhani, ambaye Mungu amempa majukumu juu yake kujifunza maandiko ili kutambua mapenzi yake Mungu. Zaidi sana, ametuonya juu ya hao wanaotafsiri maandiko kwetu.
  (a) 1 Petro 2:5.
  (b) Matendo 17:11.
  (c) 2 Timotheo 2:15.
  (d) Wakolosai 2:8.
  (e) Mathayo 7:15.

(2) Ni wazi pia kuona mfumo rahisi wa uongozi wa kanisa, hapana mtu mmoja aliyetawala juu ya wengine na kukubaliwa na Mungu!
  (a) Wakolosai 1:18.
  (b) Wafilipi 1:1.
  (c) Matendo 14:23.
  (d) Tito 1:5-7.
  (e) 1 Tim.3:8-12.
  (f) Warumi 10:14,15.
  (g) Mathayo 20:20-28.
  (h) Mathayo 23:8-12.
  (i) Kuchunguza kwa makini Agano Jipya kunafunua kwamba hakuna vyeo vikubwa, nafasi za juu za mamlaka kama vile papa, kardinali, askofu mkuu, raisi, sinodi, vikao, n.k.!
  (j) Nafasi hizo zimebuniwa na wanadamu, kinyume na mapenzi ya Mungu. Ni mafundisho na maagizo ya wanadamu ambayo Yesu alidai huifanya ibada ionekane kuwa ya bure (Math.15:9)!

3. Muhtasari wa 1:15-26, uteuzi wa Mathiya:
   a. Katika mst.15,16 Petro alianza sehemu hii kwa kurejea katika maandiko ya Agano la Kale ambayo yalihusu unabii wa usaliti wa Yuda kwa Yesu.
   b. Katika mst.17 amebainisha kwama Yuda alikuwa miongoni wa mitume asilia kumi na mbili waliochaguliwa na Yesu mwenyewe.
   c. Katika 18,19 Luka anaingiza taarifa kwamba:
      (1) Yuda alinunua konde kwa fedha za usaliti.
      (2) Alikufa kifo kibaya sana.
      (3) Na, konde likaitwa Konde la Damu.
   d. Katika mst.20 Petro alinukuu kutoka Zab.69:25 na 109:8 kuonyesha kwamba:
      (1) Makazi ya Yuda yasingekaliwa.
      (2) Mwingine angechukua nafasi yake.
   e. Katika mst.21,22 Petro alitoa sifa aina mbili muhimu ambazo mtu alipaswa kuwa nazo kuchukua nafasi ya Yuda kama mtume wa Kristo:
      (1) Alitakiwa kuwa pamoja nao mitume wakati wote Yesu akiishi na kufanya kazi nao.
      (2) Alipaswa kuwa shahidi wa kufufuka kwake.
   f. Katika mst.23 watu wawili walitambulishwa wenye sifa – Yusufu na Mathiya.
   g. Katika mst.24,25 mitume waliomba mapenzi ya Mungu kufanyika katika kuchagua hao wawili.
   h. Katika mst.26 mitume walitafuta mwongozo wa Bwana kwa kupiga kura na Mathiya alichaguliwa kuchukua nafasi ya Yuda kama mtume.

4. Muhtasari wa sura 1, kugonjea kwa ahadi:
   a. 1:1,2 Utangulizi.
   b. 1:3-8 Kutolewa kwa ahadi.
   c. 1:9-11 Kupaa kwake Kristo.
   d. 1:12-14 Mitume wakiwa Yerusalemu.

e. 1:15-26 Kuchaguliwa kwa Mathiya.

**2. AHADI IMETEKELEZWA NA KANISA LIMEANZISHWA**:

**MTAZAMO KWA UJUMLA WA SURA 2**

a. 2:1-3 Mitume wamejazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine.
b. 2:14-36 Roho Mtakatifu (kupitia Petro) anawathibitishia makutano juu ya dhambi, haki, na hukumu.
   (1) 2:14-21 Tafsiri yenye uvuvio ya matukio haya.
   (2) 2:22-24 *Yesu*: Aliyedhihirishwa na Mungu; aliuawa na Wayahudi, alifufuliwa na Baba.
   (3) 2:25-32 *Yesu*: Uthibitisho toka kwa unabii.
   (4) 2:33-36 *Yesu*: aliinuliwa na kuketishwa katika kiti cha enzi.
c. 2:37-41 Mwitikio wa baadhi miongoni mwa makutano/ majibu yenye uvuvio ya jinsi ya kupata msamaha.
d. 2:42-47 Kanisa lilidumu kwa kusimama imara.

**a. (2:1-13) MITUME WALIJAZWA ROHO MTAKATIFU NA KUNENA KWA LUGHA.**

**2:1)**
1. Mitume walikusanyika pamoja siku ya Pentekoste.
2. Pentekoste ilikuwa moja ya sikukuu tatu za mwaka ambazo kila mtu mwenye umri wakutosha wa kiume alitakiwa awepo Yerusalem (Kut.23:14-17; Kumb.16:16). Sikukuu hizi zilikuwa kama ifuatavyo:
   a. Pasaka (Law.23:5,6).
   b. Pentekoste, iliyojulikana pia kama Sikukuu ya Majuma, na Sikukuu ya Mavuno, ambapo malimbuko ya mavuno yao yalitolewa kwa Bwana (Law.23:15-17; Hes.34:22,23; Kut.23:16).
   c. Vibanda (Law.23:34-44).
3. "Pentekoste" kwa Kiyunani inamaanisha "ya hamsini" (fiftieth).
4. Hilo ni jina sahihi kwa kuwa Sikukuu ya Pentekoste ilifanyika siku ya hamsini baada ya Pasaka (Law.23:15,16).
   a. Basi, kulingana na mistari hii, kuhesabu siku hamsini kulianza siku baada ya Sabato ya ya Sikukuu ya Pasaka.
   b. Sabato ilikuwa siku ya saba ya juma, ama Jumamosi kama tunavyoitambua.
   c. Kwa hiyo, kuhesabu kulianza Jumapili, ambayo ni siku ya kwanza ya juma.
   d. Kuanzia siku hiyo wangehesabu Sabato saba (Jumamosi) ikiwa ni jumla ya siku arobaini na tisa (juma saba).
   e. Kisha siku ya pili, siku iliyofuata baada ya Sabato ya saba ingelikuwa siku ya hamsini, au Siku ya Pentekoste.
   f. Na kwa kuwa ilikuwa siku moja baada ya Jumamosi ya saba, wakati wote iliangukia Jumapili, siku ya kwanza ya juma.
5. Ni jambo la msingi kuona kwamba hukumu na kifo cha Yesu kilitokea baada ya kipindi cha sikukuu kubwa ya mwaka ambayo ni Pasaka (Math.26:17-27:62).
   a. Basi, siku hamsini baadaye, wakati watu toka ulimwenguni kote wangekusanyika pamoja Yerusalem, Mungu alichagua siku ya Pentekoste kwa kusudi maalum.
   b. Kusudi hilo lilikuwa kuwaonyesha wote, ushindi wa Mwanawe mpendwa na kulianzisha kanisa kale!
   c. Pia, kama tulivyotangulia kuona, tukio hili lilitukia Jumapili, siku ya kwanza ya juma.
   d. Kuna mambo kadhaa mengi ambayo yanahusika na siku ya kwanza ya juma katika Agano Jipya ambayo ina maana:

a. Marko 16:9.
b. Matendo 20:7; 1 Kor.16:2.

6. "Ilipotimia" (had fully come).
   a. Siku ya Kiebrania ilianza wakati wa machweo – takribani 12:00 (6:00p.m.).
   b. Kwa hiyo, sehemu ya kwanza ya siku hii ilijaa giza, ambayo isingelifaa kwa matukio muhimu ya siku hiyo.
   c. Hivyo basi, kwa kusudi hili, siku ilitimia (fully come) ilipokuwa mchana!
7. "*Walikuwako* wote mahali pamoja." Eng. "…with one accord…" Ni watu gani hawa walikuwa wote mahali pamoja kwa nia moja?
   a. Kumbuka mafungu ya asili ya Biblia hayakugawanywa katika sura na mistari.
   b. Basi, hapakuwa na mgawanyiko kati ya tunachojua kama 1:26 na 2:1.
   c. Soma mistari hii pasipo kutulia.
   d. Ukishafanya hivyo, ni wazi "*walikuwa*" hao ni mitume kumi na mbili!
   e. Swala hili linalingana na sheria za sarufi (grammar).
      (1) Kanuni ni hii, neno au tungo ambalo kiwakilishi (kama vile 'wao' walikuwako) kinalenga kikirejea nyuma kwa ile nomino ya karibu kabisa ama kiwakilishi ambacho kinakubalina kwa kiwango, n.k.
      (2) Katika swala hili, kiwakilishi 'wao' walikuwako katika 2:1 dhahiri kinarejea nyuma kwa nomino "mitume" katika 1:26 – wala si wanafunzi 120 nyuma kabisa 1:15!
   f. Tutakapojifunza 2:4, tutatambua kwa maelezo zaidi kwamba ililenga mitume wa Kristo, na mitume wake pekee waliokusanyika pamoja.

**2:2)**

1. Uvumi wa nguvu ukaijaza nyumba waliyokuwemo mitume.
2. Angalia uvumi umetajwa "*kama*" uvumi wa upepo wa nguvu.
3. Ndiyo kusema, haukuwa upepo haswa, lakini kama uvumi wa upepo.

**2:3)**

1. Maono makubwa yaliyohusisha ndimi zilizogawanyikana kama ndimi za moto zilizowakalia mitume.
2. Tena, haukuwa moto halisi, bali ulionekana "*kama*" moto.
3. Ndimi zikamkalia kila mtume.

**2:4)**

1. Mitume walijazwa Roho Mtakatifu.
2. Jambo hili kwa hakika lilikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao Yesu aliwaahidi (1:4,5,8).
3. Lilipotukia hili, walipokea nguvu za kimiujiza kunena lugha zingine kama Roho Mtakatifu alivyowawezesha kufanya hivyo.
4. "Lugha zingine" – ετεραισ γλωσαισ.
   a. ετεραισ – nyingine ya aina tofauti.
   b. γλωσαισ – lugha.
      (1) Kamusi (Vine's Expository Dictionary of Old and New Testament Words) – karama ya miujiza kunena kwa lugha nyingine bila kujifunza."
      (2) (Thayer's Greek English Lexicon – "lugha, k.m. lugha waliyoitumia watu ukitofautisha na ile ambayo ilitumika na mataifa mengine; kuzungumza na watu wengine wasio wenyeji, i.e. lugha za kigeni, Mdo.2:4 linga.6-11; kunena kwa lugha mpya ambayo mnenaji hakujifunza hapo kabla, Mk.16:17."
   c. Basi, ni wazi kutokana na maana ya maneno katika Kiyunani kwamba uwezo huu wa kimiujiza kunena "*katika lugha zingine*" ulikuwa uwezo wa kuzungumza lugha ambazo mitume hawakuwahi kujifunza kabla.

   d. Kwa nyongeza, maana ya maneno ya Kiyunani, mazingira pia yanadhihirisha wazi kuwa lugha zilikuwa ni za kigeni ambazo mitume hawakuwahi kujifunza kabla.
   e. Tutajifunza mazingira punde.
5. Muujiza huu wa kumwagwa Roho Mtakatifu au ubatizo wa Roho Mtakatifu ni uthibitisho zaidi kuonyesha kwamba ni mitume wa Kristo na mitume wake pekee ambao walikusanyika pamoja ili kupokea nguvu hii – si wanafunzi 120 ama wengineo wowote! Hatimisho hilo limewekwa bayana kutokana na maandiko yafuatayo:
   a. Mdo. 1:2-5:Yesu alisema ahadi ingetimia wakati mitume wangebatizwa kwa Roho Mtakatifu.
   b. Mdo.1:8: Yesu alisema kwamba Roho Mtakatifu atakapowajia mitume, wangepokea nguvu na wangelikuwa mashahidi wa Kristo.
   c. Mdo.2:7:Wanenao kwa lugha kwa uwezo wa Roho Mtakatifu walikuwa *Wagalilaya.* Mdo.1:11 Mitume walikuwa Wagalilaya.
   d. Mdo.2:14: Petro akasimama pamoja na wale kumi na moja (mitume) kunena na makutano.
   e. Mdo.2:37: Miongoni mwa watu katika kundi hilo walimwomba Petro na mitume wengine kitu cha kufanya juu ya hali yao ya hatia.
   f. Mdo.2:42: Wakristo wa awali walidumu katika mafundisho ya mitume.
   g. Mdo.2:43: Ishara na maajabu mengi yalifanywa na mitume.
   h. Mdo.3:6,7: Kiwete aliponywa kwa muujiza na mtume Petro.
   i. Mdo.4:33: Mitume walishuhudia kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi.
   j. Mdo.5:12: Kwa mikono ya mitume, ishara na maajabu mengi yalifanywa.
   k. Je, unashaka lolote kwamba ni mitume wa Kristo, na mitume wake pekee waliobatizwa kwa Roho Mtakatifu katika tukio hili?
6. Tukiwa bado katika somo hili, ni muhimu kuangalia pointi zifuatazo kuhusu ubatizo kwa Roho Mtakatifu:
   (1) Ilikuwa ni ahadi (Lk.24:49; Mdo.1:5,8; 2:33).
   (2) Mhudumu ni Kristo (Math.3:11; Mdo.2:32,33).
   (3) Aliyetumika (element) ni Roho Mtakatifu (Mdo.1:5, 8).
   (4) Kusudi lilikuwa si kupokea msamaha wa dhambi, bali:
      (a) Kuwatia nguvu mitume kwa ajili ya kazi maalum ya kufunua na kuthibitisha neno la Mungu (Mdo.1:8; 2:1-4; Yoh.16:13).
      (b) Kuthibitisha kwamba Mungu amewakubali watu wa Mataifa (Mdo.11:15-18).
   (5) Ilijumuishwa pamoja na karama za kimiujiza za Roho Mtakatifu (Mdo.2:1-4; 10:46).
   (6) Ilitukia mara mbili tu (Matendo sura 2 na 10).
   (7) Ilitajwa kwa maneno yenye kuonyesha mipaka, k.m, kwa mitume wa Kristo (Mdo.1:2,3,4, 26; 2:1-4).
7. Tutakapojifunza 2:38 tutakuwa na fursa ya kulinganisha ubatizo kwa Roho Mtakatifu na ubatizo wa maji ili kupata msamaha wa dhambi.
8. Mambo ya mwisho mst.4, tafadhali rejea mafunzo yetu 1:8.
   a. Katika mafunzo hayo tuliunganisha mafundisho katika Math.16:18,19; Mk.9:1; na Mdo.1:8.
   b. Katika mistari hiyo Mungu anafundisha kwamba ufalme (kanisa) ungekuja kwa nguvu na kwamba nguvu wangepewa mitume wake Kristo wakati Roho Mtakatifu angewajilia.
   c. Sasa, katika 2:4, tunaona Roho Mtakatifu akiwajilia mitume wa Kristo na kuwajaza nguvu za kuweza kunena lugha zingine.
   d. Kwa hiyo, ni lazima kuhatimisha ufalme (kanisa) wa Bwana wetu ulianzishwa siku ya Pentekoste, kama vile Yesu alivyoahidi kutokea.
   e. Na katika 2:47 tunaona kanisa likitajwa katika wakati uliopo timilifu kwa mara ya kwanza. Lilikuwepo siku hii maalum na likadumu kuwepo kuanzia hapo.

**2:5-8)**

1. Katika mst.5 tunajifunza kwamba walikuwepo Yerusalem Wayahudi wataua kutoka kila pande za dunia wakati huo.
   a. Kumbuka hii ilikuwa Sikukuu ya Pentekoste (linga. mst.1).
   b. "Wataua" ευλαβεισ – wenye bidii wasiopenda kumkosea Mungu; walio makini kushika amri zake, watu wa dini.
   c. Maeneo ambayo watu hawa walitoka yametajwa haswa mst.9-11.
2. Katika mst.6 makutano hawa walikutanika pamoja na walishikwa na butwaa.
   a. Walishikwa na butwaa kwa kuwa mitume walinena lugha za wasikilizaji wao.
   b. Hivyo basi, waliotembelea Yerusalem walishikwa na butwaa kwa sababu hawakutegemea kusikia mitume wakizungumza kwa lugha nyingi za watu duniani.
   c. Zingatia mitume walizungumza katika lugha ambazo zilielewaka – wala si katika maneno ya siri yasiyoeleweka ama sauti isiyoweza kueleweka.
3. Katika mst.7,8 Luka ametaja makutano kama ndio waliostaajabu na kushangaa kwa kile walichokiona na kusikia.
   a. Walistaajabu kwa kuwa walionena ni Wagalilaya, walakini makutano walisikia wakinena kwa lugha ambazo walizaliwa nazo (makutano).
      (1) Angalia kwamba makutano wanawatambua wazungumzaji kama Wagalilaya.
      (2) Na hivyo ndivyo haswa malaika walivyowatambua mitume katika 1:11 – "*enyi watu wa Galilaya*" (Linga. Lk.22:58.59)!
      (3) Kama tulivyoona katika masomo yetu katika 2:4, hii ni namna nyingine ya kujua kwamba watu ambao wangepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu ni mitume wa Kristo, wala si 120 ama kundi lolote lile la watu.
   b. Kwa nini makutano walishangaa kwamba Wagalilaya waliweza kunena lugha zingine?
      (1) Wagalilaya walitazamwa kama watu wajinga, washenzi, wasio wastaarabu (Yoh.1:46; 7:52).
      (2) Rafudhi zao zilitazamwa kama zisizoundwa vizuri na zilizoharibika, kwa hiyo ingekuwa jambo la kushangaza kuona wanajua rafudhi na lugha zingine (Mk14:70; Math.26:73).
      (3) Uhakika huo ungetoa ushahidi zaidi kwa makutano kwamba mitume walikuwa wakinena lugha hizi kwa nguvu za miujiza!

**1:9-11**)
1. Katika mistari hii tunaorodha ya maeneo na nchi walikotoka makutano walikuwa pamoja kuwakiliza mitume.
   a. "*Waongofu*" (mst.10) – watu katika mataifa ya nje ambao walibadilisha dini na kuwa Wayahudi (Math.23:15).
2. Watu waliwasikia Mitume wakinena mambo makuu ya Mungu, na makutano walisikia hayo yakinenwa katika lugha zao wenyewe, wala si kwa lugha za mitume kama ambavyo wangetarajia.
3. Wataalamu wanadai kwamba lugha kubwa zilizozungumzwa maeneo haya zilikuwa kati ya saba au nane, pamoja na rafudhi mbalimbali zilizokuwepo.
   a. Mifano ya lugha kuu ni pamoja na Kiajemi (Persian), Kishamu (Syriac), Kikaldayo (Chaldee), Kiyunani, Kilatini, na Kiarabu.

**2:12,13)**
1. Luka ametaja makutano wakiwa na mambo wawili kama matokeo ya nguvu hizi za miujiza ambazo Roho Mtakatifu aliruhusu mitume waitumie:
   a. Wengi walistaajabu na kutokujua, wasiwasi au kuchanganyikiwa wasijue maana ya jambo hili.
   b. Wengine waliwadhihaki (kudharau au kufanya mzaha) mitume, wakiwashutumu kuwa walikuwa wamelewa.

2. “*Dhihaki*” – διαχλευαξω – kutumia namna ya fedhuli na mzaha kwa kutweza na kumwenyesha mtu mwingine kuwa duni na asiye na thamani.
3. “*Mvinyo mpya*” - γλευκουσ – haswa, mvinyo mtamu.
   a. Kulingana na Kamusi ya Smith ya Biblia na zingine zilizokubalika, mvinyo mtamu ulitengenezwa na kutambulikana kama juisi bora ya mizabibu.
      (1) Juisi ilitiririka kutoka katika zabibu zilizoiva kabla ya watu hawajaanza kuzikanyaga ili kukamua juisi iliyobaki katika matunda.
      (2) Maelezo yafuatayo kuhusu mvinyo mtamu ni muhtasari kutoka katika kamusi ya Smith: “Walakini fafanuzi za kale za watoa maoni yanataja kuwa utamu wake ulikuwa bora sana, wala si sawa na jinsi ilivyo sasa, bali matokeo yake ya utengenezaji hata kuwa juisi bora sana ya mizabibu:?
      (3) Kwa maneno mengine, ukizingatia maana ya neno katika Kiyunani **gleukous**, mvinyo huu haukuwa mpya, k.m. uliotengenezwa karibuni.
      (4) Ukweli kwamba mvinyo haukutengenezwa karibuni unaendana na ukweli wa kwamba miezi nane ilikuwa imepita tangu mavuno ya mizabibu na Sikukuu ya Pentekoste.
      (5) Badala ya kutengenezwa karibuni, mvinyo huu, haswa ulitengenezwa kuwa juisi bora ya mizabibu.
      (6) Basi, “mvinyo mtamu” ni tafsiri bora kuliko mvinyo mpya.
   b. Zaidi, matumizi ya neno hili la Kiyunani katika Biblia na makala mengine inaelezea kinywaji chenye chachu na kilicholevya.
      (1) Linga. Ayu.32:19 katika tafsiri ya Septuagint.
      (2) Hakika wenye kudhihaki hawa walitumia neno kuonyesha kuwa mitume walikuwa wamelewa.
      (3) Ukweli kama ulivyo, Petro ndivyo haswa alivyoelewa washitaki wao alipojibu, kuanzia mstari unaofuata.
4. Wakati ni sahihi neno kutafsiriwa “mvinyo mpya” katika mstari huu mara nyingi inarejea kwa ule wenye chachu, kinywaji cha kulevya, si sababu kila mara tunaposoma neno “mvinyo” katika Biblia halihusu chachu, kinywaji chenye kulevya!
5. Ingawa maelezo ya kina kujifunza somo hili ni nje na lengo la somo hili, maelezo yafuatayo yanathibitisha kuonyesha tafsiri za maneno “divai” wakati wote hayalengi chachu, kinywaji chenye kulevya. Maelezo haya yanatoka kwa W.D. Jeffcoat katika kitabu chake (The Bible and “Social” Drinking, kilichochapishwa na Robinson Typesetting, Corinth, MS, USA).
   a. “Muhtasari wa matokeo ya uchunguzi wa maneno juu ya mvinyo katika Biblia unafunua yafuatayo:
      (1) Kuna maneno tisa katika Agano la Kale na matatu katika Agano Jipya ambayo yametafsiriwa ‘divai’ ama katika umoja au kwa kuunganishwa na maneno mengine.
      (2) Kuna maneno mengine kumi katika Agano la Kale na mawili katika Agano Jipya ambayo yanalenga juisi ama mazao yatokanayo na mizabibu au matunda mengine.
      (3) Kuna jumla ya maneno ishirini ya nne katika Biblia ambayo yanatumika kulenga mazao yatokanayo na mizabibu au juisi ya matunda mengine.
      (4) Kati ya maneno ishirini na nne, manne hayahusu kwa namna yoyote ile mazao yatokanoayo na mizabibu au juisi ya matunda mengine.
      (5) Kuhusu maneno ishirini yanayobakia na tungo ambazo zinazohusu juisi za matunda, maneno matatu ya Kiebrania ‘yayin,’ ‘shekar,’ na ‘chemar’ na maneno matatu ya Kiyunani, ‘oinos,’ ‘gluekous,’ na ‘sikera’ ni ya jamii moja.
      (6) Jina moja la Kiebrania, ‘chomets’ na moja la Kiyunani, ‘oxos,’ yanalenga divai ambayo imefikia hakua ya kuwa kali yenye chachu (siki).
      (7) Maneno matatu ya Kiebrania, ‘mesek,’ ‘minsak’ na ‘mezeg’ yanalenga ama divai iliyochachu au isiyochachu, iliyo na dawa za kulevya au iliyozimuliwa.
      (8) Maneno matano ya Kiebrania, ‘tirosh,’ dam-anabim,’ ‘dam-enab,’ ‘mishrath-anabim,’ na ‘mamtaqqim’ yanalenga namna fulani ya mizabibu au juisi zinginezo.

(9) Mbali na neno moja la Kiebrania, 'sobe,' hakuna neno lingine katika Biblia ambalo linaonyeshe kinywaji cha kulevywa.
(10) Kwa upande mwingine, kuna maneno nane, 'shemanim,' 'dam-anabim,' 'dam-enab,' 'mishrath-anabim,' 'ashishah,' 'anabim,' 'yekeb,' na 'mamtaqqim,' ambayo yanahusu kitu kisicholevya.
(11) Maneno mengine kumi, 'yayin,' 'tirosh,' 'shekar,' 'asis,' 'chemar,' 'chamar,' 'mesek,' 'mimsak,' 'mezeg,' na 'oinos,' jambo la msingi zaidi na mara nyingi lenye faida ni kuyatumia, kuruhusu watu kutambua kwa kuchunguza mazingira au hali, kama kinacholengwa ni kilevi. Watu kwa kufikiri tu wasihatimishe kuwa na ukweli pasipo kuchunguza mazingira."

b. Angalia mazingira yafuatayo ambapo "divai" imetafsiriwa, lakini ni kweli kwamba kinacholengwa ni kitu kisicho na chachu:
   (1) Hes.18:12,13 (Linga. Neh.10:37).
   (2) Isa.16:10.
   (3) Isa.62:8,9.
   (4) Isa.65:8.
c. Kutokana na maandiko haya, kadhalika kujifunza maneno yaliyotafsiriwa "divai" katika Biblia, ni dhahiri kuwa maneno haya moja kwa moja hayahusu chachu, kinywaji chenye kulevya.
   (1) Badala yake, maneno haya yanahusu mizabibu na juisi za mizabibu isiyochachu.
   (2) Kwa hiyo, kabla ya mtu kufikia hatimisho, kujifunza mazingira kwa makini ni lazima kufanywe ili kutambua jinsi Mungu alivyokusudia neno litumike.
   (3) Ndugu Jeffcoat, katika kitabu kilichotajwa hapo juu anachanganua somo la unywaji wa pombe kikamilifu.
   (4) Anahatimisha kuwa mazoea haya ni dhambi mbele za macho ya Mungu na lazima yakomeshwe na wote wanaopenda kumpendeza Bwana.
   (5) Kwa wale wenye notisi za kozi hii, maelezo ya nyongeza kuhusu dhambi ya kileo inapatikana katika mwishoni mwa notisi za makala A.

6. Muhtasari wa 2:1-13, mitume walijazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine:
   a. Katika mst.1 mitume walikuwa wote pamoja siku ya Pentekoste.
   b. Mst.2 uvumi kama uvumi wa nguvu uliijaza nyumba waliyokuwamo.
   c. Mst.3 ndimi kama za moto ziliwatokea mitume na kuwakalia kila mmoja wao.
   d. Mst.4 mitume walijazwa Roho Mtakatifu ambaye aliwawezesha kunena lugha zingine ambazo hawakujifunza hapo nyuma.
   e. Mst.5 Wayahudi wataua kutoka kila pande za dunia walikuwepo Yerusalem.
   f. Mst.6-12 walistaajabu na kushangaa waliposikia mitume (ambao walikuwa Wagalilaya) wakinena kwa lugha ngeni ambazo hakuwahi kujifunza hapo kwanza.
   g. Mst.13 wengine walipokea kinyume kwa kuwadhihaki mitume, wakiwashutumu kulewa.

## b. (2:14-36) ROHO MTAKATIFU (KUPITIA PETRO) ANATHIBITISHIA UMATI JUU YA HATIA, HAKI, NA HUKUMU.

### (1) (2:14-21) TAFSIRI ILIYOVUVIWA YA MATUKIO.

**2:14,15)**

1. Petro alijibu kwamba yeye na mitume wengine hawakulewa kama walivyoshutumiwa na baadhi katika umati.
2. Alitoa sababu kwa nini mitume hawakulewa kwamba ilikuwa saa tatu za mchana.
   a. Saa tatu za mchana ni saa tatu za asubuhi (9:00 a.m.).
   b. Kuna sababu kadhaa zinazomfanya Petro ataje muda huo ili kuonyesha kuwa watu hao hawajalewa:
      (1) Ilikuwa saa ya ibada ya asubuhi na ya kutoa dhabihu.

   (2) Lilikuwa jambo lisilo la kawaida hata kwa walevi kulewa muda wa mchana (1 Thes.5:7).
   (3) Kufuatana na Albert Barnea kwa maoni (commentary) yake katika kitabu cha Matendo, ilikuwa kawaida kwa Wayahudi kutokula ama kunywa chochote hadi baada ya saa tatu za mchana.
   (4) Hivyo ndivyo ilivyokuwa haswa siku ya Sabato na wakati wote wa sikukuu (kama vile Pentekoste).
3. Ushahidi mwingine wa Petro kudhihirisha kuwa yeye na mitume wengine hawakulewa ni hotuba ya nguvu aliyokuwa yu karibu na kuihutubu.
4. Angalia mst.14 Petro anawaasa makutano wasikilize kwa makini sana mambo atakayosema.
   a. Kwa hiyo, Roho Mtakatifu, kupitia Petro, alikuwa akizungumza na umati kwa maneno aliyozungumza Petro.
   b. Ukweli huu ni muhimu kuukumbuka tutakapofika 2:37.

**2:16)**
1. Katika mstari huu Petro anaeleza kwa uvuvio mambo ambayo makutano walisikia na kuyaona na sababu iliyomfanya yeye na mitume wengine waweza kunena kwa lugha.
2. Akipinga madai ya kwamba mitume walikuwa wamelewa, bali utimilifu wa unabii ambao nabii Yoeli alinena hapo nyuma.
3. Petro anabainisha kwamba kilichokuwa kikitendeka siku ya Pentekoste ni kile Yoeli alitabiri katika Agano la Kale.

**2:17,18)**
1. Katika mistari hii na inayofuata Petro kwa uvuvio anabainisha unabii maalum kwa kunukuu Yoeli 2:28-32.
2. Katika mistari hiyo Yoeli alitabiri wakati ambao Mungu angemwaga Roho yake kwa watu wote" (KJV – all flesh).
3. Matokeo yake ni kwamba watu mbalimbali wangetabiri, ona maono, kuota ndoto.
4. Tena, mambo haya yangetokea katika "*siku za mwisho*."
   a. Lakini Petro akasema kwa uvuvio kwamba mambo yaliyokuwa yakitendeka siku ya Pentekoste ndio utimilifu wa yale aliyosema Yoeli kuwa yangetokea siku za mwisho.
   b. Basi, tunaweza kuhatimisha kuwa siku za mwisho zilianza siku ya Pentekoste ya Matendo 2 wakati mitume walipomwagiwa Roho Mtakatifu.
   c. Tena, kama tulivyojifunza hapo nyuma, tukio hili lilitukia wakati kanisa la Masihi lilipoanza.
   d. Na kwa kuwa ni siku za "mwisho," zinasimamia kipindi cha mwisho wa nyakati.
   e. Hivyo basi, kipindi tangu kuanzishwa kwa kanisa lililojengwa na Masihi hadi kufikia kuja kwake mara ya pili mwisho wa dunia, kama tujuavyo.
   f. Basi, mwanadamu amekuwa katika siku za mwisho takribani kwa miaka 2,000!
   g. Na hakuna mtu ajuaye siku za mwisho zitafikia hatima lini (Math.24:36-44)!
5. Katika unabii huu ulionukuriwa na kutafsiriwa na Petro, Mungu alisema angemwaga Roho wake juu ya "watu wote" (all flesh).
   a. Ni muhimu sana kuelewa kusudi la Mungu kusema "watu wote" (all flesh).
   b. Kwa mfano, je, alimaanisha kwamba kila mtu mmoja angepokea uwezo wa kimiujiza kutoka kwa Roho Mtakatifu?
   c. Katika kujibu swali hili, ni muhimu kuelewa kwamba neno "wote" kama lilivyotumika katika Biblia si kwamba kila mtu mmoja.
   d. Linga. Yoh.12:32.
   e. Ukiwa na hili akilini, inawezekana kabisa kwamba ahadi hii ya kumwagwa Roho Mtakatifu *iliwekewa mipaka* na Mungu kwa watu wachache kuliko kudai kwa kila mtu.
   f. Ili uelewe jinsi Mungu alivyoiwekea mipaka ahadi hii, maswali kadhaa yanapaswa kuulizwa na kisha kupatiwa majibu.

(1) Kwanza, je, “watu wote” (all flesh) ni pamoja na wanadamu na wanyama (KJV)?
    (a) Hakika, wote watakubali kwamba Mungu hakumwaga Roho yake juu ya wanyama, samaki, na ndege!
    (b) Kwa ulinganifu wa muundo kama huu angalia Isa.66:23.
    (c) Basi, lazima tuhatimishe kwamba Mungu aliweka mipaka ahadi hii “*watu wote*” katika mst.17!
(2) Pili, je, “*watu wote*” inajumuisha wanadamu wote?
    (a) Tena, ukweli ni kwamba wote wanakubaliana kuwa Mungu asingemwaga Roho wake juu ya waasi wote wenye dhambi ambao hawajamtii yeye!
    (b) Zaidi sana, katika mst.18, Mungu anatenganisha ambao wangemwagiwa Roho wake kama *watumishi wake* wa “kiume” na “kike.”
    (c) Basi, lazima tuhatimishe Mungu aliwekea mipaka ahadi hii kwa hao ambao ni watumishi wake.
(3) Tatu, je, “*watu wote*” ni jumla ya Wakristo wote?
    (a) Jambo muhimu linalotakiwa kujibu swali hili ni kutambua kama watu wote katika kanisa la awali waliweza kutenda miujiza kwa mfano: kutabiri, kuona maono kwa njia ya miujiza, n.k.
    (b) 1 Wakorintho 12:29,30.

g. Lakini ikiwa Mungu aliiwekea mipaka ahadi hii, “watu wote” inamaanisha nini katika mstari huu?
    (1) Inamaanisha kwamba karama za miujiza za Roho Mtakatifu zilizokuwepo karne ya kwanza zingetolewa na Mungu kwa kundi fulani la watu wake.
    (2) Waandishi wa Biblia mara nyingi waliigawa dunia katika makundi makubwa ya jamii za watu (linga. Gal.3:28).
    (3) Ukiwa na wazo hili akilini mwako, zingatia jinsi Mungu alivyogawa Roho Mtakatifu juu ya “watu wote” katika karne ya kwanza wakati miujiza ilipotendeka:
        (a) Kwa Wayahudi (katika sura hii) na kwa mataifa (sura 10).
        (b) Kwa wanaume (wana wenu) na wanawake (binti zenu) (linga. Mdo.21:9 pamoja na 1 Kor.14:34).
        (c) Kwa wenye umri mkubwa (wazee wenu) na kwa wenye umri mdogo (vijana wenu).
        (d) Basi, Mungu aliposema angemwaga Roho Mtakatifu kwa “watu wote,” alimaanisha kundi fulani la watu wake.

6. Kabla ya kuondoka katika mistari hii miwili, ni muhimu kuangalia mahali pengine katika Agano Jipya, Mungu aliweka mipaka kwa kipindi cha muda fulani angeruhusu karama hizi za miujiza kutumika.
    a. 1 Kor.13:8-10.
    b. Kwa hiyo, karama hizi za miujiza za Roho Mtakatifu zilifikia kikomo katika karne ya kwanza wakati Mungu alipokamilisha kufunua ufunuo wake wa Agano Jipya.

**2:19,20**

1. Mistari hii ni mwendelezo wa unabii wa Yoeli, mistari hii haswa inapatikana Yoeli 2:30,31.
2. Alitabiri muda ambao Mungu angetoa ishara kubwa na maajabu mbinguni na duniani.
3. Maajabu haya ni pamoja na vitu kama damu, moto, moshi, ambavyo vimetumika kama mfano wa vita na maafa mengine.
    a. Ni jambo la kufurahisha kutambua kwamba mwanahistoria Josephus alitaja mambo haya wakati wa maafa ya Yerusalem na Warumi katika mwaka 70 B.K.
    b. Kwa mfano, alitaja kimwondo (meteors) kikali, upanga wenye moto ulioning’inia angani, na nyota yenye mkia (comet). (Bales, Hub of the Bible, p. 72).
    c. Wanahistoria wengine waliandika nguzo za moshi ziliendelea kupaa juu angani kutoka katika masinagogi, majumbani, n.k. wakati wa maangamizi hayo.

4. Majabu mengine yaliyotabiriwa na Yoeli ni pamoja na kutiwa giza kwa jua, kwa mfano mwezi kugeuka kuwa damu.
   a. Hii ni lugha ya mfano ambayo manabii waliitumia kutabiri maangamizi ya watu wanaompinga Mungu.
      (1) Isaya 13:1, 9-13.
      (2) Isaya 29:1,6.
      (3) Ezekieli 32:2, 6-8.
   b. Kwa nyongeza, Bwana Yesu alitumia lugha kama hiyo kuelezea majilio ya maangamizi ya Yerusalem (Math.24:15-29; Lk.21:20-26).
   c. Zaidi sana, matukio yanayolingana na haya yalitokea kabla na baada ya kusulubishwa Kristo katika siku za nyuma kabla ya hii ya Pentekoste.
      (1) Mathayo 27:45, 50-54.
      (2) Kusema ukweli, Tertulian alitaarifu kuwa Pontius Pilato alimwandikia Mfalme Tiberio kwamba, "Mwezi, uligeuka kuwa kama damu, haukuangaza usiku mzima, ingawaje ulionekana kuwa mzima." (Ante-Nicene Fathers, Pilate to Tiberias, Vol.III, p. 463).
5. Angalia nabii Yoeli alisema kwamba maajabu haya na ishara zingetukia wakati fulani kabla ya "*siku kubwa na yenye kutisha ya Bwana*."
   a. Katika Agano la Kale, tungo "siku ya Bwana" ilitumika wakati Mungu alipoleta ghadhabu yake juu ya waasi.
   b. Pia, ilitumika kuonyesha kuanguka kwa taifa lililoasi.
   c. Kwa nyongeza, kwa mistari iliyotumika hapo kuhusu Babeli, Yerusalem, na Misri, uichunguze tafadhali ifuatayo:
      (1) Obadia 15.
      (2) Amosi 5:18-20.
   d. Katika Agano Jipya tungo "siku ya Bwana" inalenga siku ya hukumu mwisho wa dunia.
   e. Katika siku hiyo Mungu ataleta hukumu ya mwisho ya ghadhabu yake kwao wasiomtii.
      (1) 2 Petro 3:10.
      (2) Linga.1 Kor.5:5; 2 Kor.1:14; 1 Thes.5:2.
   f. Ni imani yangu "siku kubwa na yenye kutisha ya Bwana" anayotabiri Yoeli katika mistari hii ililenga maangamizi ya Yerusalem mwaka 70 B.K.
      (1) Hilo lingelingana na matumizi ya maneno hayo katika Agano la Kale, kipindi ambacho Yoeli alitabiri.
      (2) Katika maafa ya Yerusalem, Mungu alileta ghadhabu yake juu ya taifa lililoasi la Israeli.
      (3) Alikuwa amewavumiliwa na kuwarehemu kwa miaka mingi, lakini walizidi kuwa waasi kinyume chake.
      (4) Ishara ambazo Yoeli amezitabiri zingetukia kabla ya siku hiyo hakika zilishuhudiwa mbinguni na duniani kipindi cha kuanguka kwa Yerusalem.
      (5) Kwa nyongeza, lugha aliyotumia Yoeli inalingana kabisa na ile ya Yesu alipotabiri kuhusu Yerusalem katika Math.24 na Lk.21.
      (6) Mwisho, wakati wa maangamizi ya Yerusalem, Mungu alimwaga Roho wake juu ya "watu wote," Wayahudi/Mataifa, waume/wanawake, n.k.
      (7) Basi, shughuli ambayo inatawala maangamizi ya Yerusalem hakika inalingana na unabii wa Yoeli kabisa!
   g. Inawezekana kabisa pia kwamba "siku kubwa na yenye kutisha ya Bwana" Yoeli aliyoitabiri ni siku ya hukumu.
      (1) Hakika hiyo pia inalingana na matumizi ya maneno hayo katika Agano Jipya.
      (2) Tahadhari moja lazima ingechukuliwa iwapo mtazamo huu ni sahihi.
      (3) Tahadhari hiyo ni kuwaonya kwamba ishara katika mst.19,20 haziwezi kutumika kama ishara za mwisho wa dunia.

(a) Kama tulivyoona, ishara zinazofanana na hizo zimewakilishwa mara nyingi katika historia ya ulimwengu.
(b) Basi, ishara hizi siyo ndiyo ushahidi tosha kuonyesha mwisho wa dunia na Siku ya Hukumu imekaribia.
(c) Mungu anachosema katika unabii ni kwamba wakati fulani kabla ya "siku kubwa na yenye kutisha ya Bwana" ishara hizi zingetukia.
(d) Kwa kuwa ishara hizi zimetukia tayari mara kadhaa katika historia, wewe na mimi tunatakiwa kujiandaa kwa ajili ya hukumu kila iitwapo leo!
(e) Kumbuka maneno ya Mwokozi wetu katika Math.24:36-44.
(f) Katika kila hali, Mungu anabainisha wazi katika Agano Jipya kwamba Siku ya Hukumu ni hakika ambayo watu wote wenye akili watakabiliana nayo (linga. Rum.14:12; 2 Kor.5:10,11).

**2:21)**

1. Mungu kupitia Yoeli alitabiri kwamba katika siku za mwisho watu "*watakaoliitia jina la Bwana*" wataokoka.
2. Kumbuka siku za mwisho zilianza katika huduma yake Yesu na zitadumu hadi Siku ya Hukumu.
3. Lakini, nini maana ya kuliitia jina la Bwana?
   a. Kuna njia kadhaa kutambua jibu la Mungu kulingana na swali hili.
   b. Njia mojawapo ni kujifunza jambo ambalo Bwana hamaanishi katika maneno haya.
   c. Hakika hana maana kuliitia jina la Bwana na kusali, kwa namna inavyofanyika katika ulimwengu wa madhehebu siku hizi.
      (1) Luka 6:46.
      (2) Mathayo 7:21-23.
   d. Njia nyingine ya kujifunza maana ya maneno haya ni kujifunza matumizi yake katika mazingira ya Matendo sura 2.
      (1) Yoeli alitabiri mambo ambayo yangetokea katika siku za mwisho (2:17).
      (2) Kati ya mambo hayo ni kuliitia jina la Bwana ili kuokoka (mstari huo).
      (3) Lakini, Petro alisema kwa uvuvio kwamba yaliyotukia siku ya Pentekoste ulikuwa mwanzo wa utimilifu wa unabii wa Yoeli.
      (4) Kwa maana hiyo, tungetegemea kuona watu wakiliitia jina la Bwana ili waokolewe katik siku ya Pentekoste.
      (5) Kwa hiyo, ikiwa tutawatambua waliokoka siku hiyo na jinsi gani waliokolewa, tutakuwa na jibu lenye uvuvia juu ya swala la kuliitia jina la Bwana.
      (6) Wale waliokuwa wameokolewa siku ya Pentekoste walikuwa ni wale:
         (a) Walisikia injili (22-36).
         (b) Waliamini injili na kujutia dhambi zao (2:37).
         (c) Walitubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi zao (2:38;41).
         (d) Walidumu katika mafundisho ya mitume, ikiwa ni pamoja na ibada sahihi (mst.42).
         (e) Na, walizidishwa katika kanisa la Bwana (mst.47).
      (7) Kutokana na uvuvio huo, tunahatimisha kwamba kuliitia jina la Bwana ni kwa njia ya uaminifu na upendo kutii amri zake (ukijumuisha ubatizo), mahali ambapo msamaha hupokelewa kwa njia ya rehema na neema zake Mungu.
   e. Jambo la tatu la kujua maana ya kulitia jina la Bwana ni kujifunza mazingira ya mafungu mengine ambayo maneno haya hupatikana.
      (1) Matendo 22:16.
      (2) Warumi 10:13-17.
         (a) Muhtasari:
            1. Mtu alitumwa kuhubiri/fundisha injili (mst.15).
            2. Kusikia injili huunda imani (mst.14,17).

3. Mwamini Bwana (mst.14).
4. Tii injili, kwa hiyo kuliitia jina la Bwana (mst.16,13).

(b) Kutokana na habari hizi zenye uvuvio, tunahatimisha kama tulivyohatimisha katika mistari mingine miwili:

1. Kuliitia jina la Bwana ni kutii injili kwa uaminifu kabisa na upendo.
2. Hili ni pamoja na kubatizwa ili kupata ondoleo la dhambi (kuoshwa dhambi).

4. Muhtasari wa 2:14-21, tafsiri yenye uvuvio za matukio haya.
   a. Katika mst.14,15 Petro alikataa pamoja na mitume wengine kuwa walikuwa wamelewa kama walivyoshutumiwa.
   b. Katika mst.16 Petro alisema kwamba yaliyokuwa yakitukia ni utimilifu wa unabii uliofunenwa na Yoeli 2:28-30.
   c. Katika unabii huo Mungu angemwaga Roho wake kwa makundi aina zote za watu wake (mst.17,18).
   d. Watu wake wangewezeshwa kutabiri, kuota ndoto, na kuona maono kimiujiza kwa nguvu za Roho Mtakatifu (mst.17,18).
   e. Kwa nyongeza, muda fulani kabla ya siku ya Bwana, Mungu angeonyesha ishara kubwa na maajabu mbinguni na duniani (19,20).
   f. Katika siku za mwisho wale watakaloliitia jina la Bwana (kutii injili kwa uaminifu kabisa na upendo) wataokoka (mst.21).
5. Mtazamo kwa ufupi wa sura 2, ahadi ilitimia na kanisa lilianzishwa:
   a. (2:1-13) Mitume wakajazwa na Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine.
   b. (2:14-36) Roho Mtakatifu (kupitia Petro) aliuthibitishia umati juu ya dhambi, haki, na hukumu
      (1) (2:14-21) Tafsiri yenye uvuvio juu ya matukio haya.

**2. (2:22-24) Yesu: Aliyedhihirishwa na Mungu; Akauawa na Wayahudi; Alifufuliwa na Baba.**

**2:22)**

1. Katika mstari huu Petro alianza kuhubiri kuhusu Yesu Kristo aliyesulubiwa kwa uwezo na hekima zake Mungu (linga. 1 Kor.1:18, 23-2:2).
2. Alifanya hivyo kwa kutoa mambo sita, yenye kugusa moyo, na kushangaza.
3. Jambo lake la kwanza lilikuwa uthibitisho wa Mungu Baba kama ilivyodhihirika kwa miujiza ya uweza wake ambayo Mungu aliifanya kupitia Yesu.
   a. Angalia kwamba hawa watu hawakuwa waigizaji, wafuata mkumbo, au wenye kutenda miujiza ya uongo iliyofanywa na wazushi.
   b. Badala yake, ilikuwa miujiza bayana, halisi, kweli iliyofanywa na Mungu Mwenyezi kupitia Mwanawe mpendwa!
4. Wala si hivyo tu, lakini jambo lake la pili ni kwamba miujiza hiyo ilifanyika katikati ya Wayahudi; basi, waliitambua waziwazi miujiza hiyo.
5. Waliijua miujiza iliyotendeka na wala wasingelipinga kuwa haikuwa halisi, sahihi, miujiza ya kweli.
6. Basi, hata adui mkubwa kabisa wa Yesu asingeweza kukataa uthabiti wa miujiza aliyoitenda!

**2:23)**

1. Likiwa jambo lake la tatu, alilotaja kwamba Yesu alitolewa kwa shauri la Mungu Baba akisha tangulia kujua hilo.
   a. Maana yake rahisi ni Mungu alitangulia kupanga muda wa kufa Yesu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.
      (1) Ufunuo 13:8.
      (2) Wagalatia 4:4.

b. Wayahudi walimtoa Yesu kwa sababu ya wivu, lakini Mungu alimtoa Mwanawe wa pekee kwa ajili ya dhambi za kila mmoja wetu!
   (1) Mathayo 27:18.
   (2) Warumi 4:25.
   (3) Warumi 8:32.
c. Basi, sababu ya msingi ya kutolewa Yesu si kwa sababu ya udhaifu wake ama kushindwa kujiokoa mwenyewe, wala si wivu wa Wayahudi.
d. Kinyume chake, sababu ya msingi ilikuwa mpango wa Mungu kumtoa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu.
e. Walakini, ukweli kwamba Mungu alitangulia kufahamu kuwa matukio haya yangetokea, haingilii uhuru wa mtu kuchagua!
f. Kulingana na mipango ya Mungu akimshughulikia mwanadamu tangu mwanzo, kila mhusika katika mpango huu wenye kuvutia, ukijumuisha Yesu, kwa hiari yao walichagua kutenda waliyoyafanya.
   (1) Yoshua 24:15.
   (2) Ufunuo 22:17.
   (3) Yohana 10:17,18.

2. Kama jambo lake la nne, Petro anawawajibisha Wayahudi (ninyi) kwa kumsulibisha na kumwua Yesu.
   a. Ebu tafakari Wayahudi wasikilizaji waliitikiaje maelezo haya yenye uvuvio, haswa kwa jinsi Petro alivyobainisha:
      (1) Mungu alimdhihirisha Yesu kwa miujiza aliyoifanya.
      (2) Miujiza hii ilitendeka katikati ya Wayahudi namna ambayo ilikuwa vigumu kukataa.
      (3) Yesu alitolewa kwa mashauri ya Mungu yaliyokusudiwa naye.
      (4) Hata hivyo, Wayahudi walimsulibisha na kumwua Yesu.
3. Tazama Wayahudi walimsulibisha Yesu "kwa mikono mibaya" (by lawless hands).
   a. Inaonekana maneno haya yanarejea kwa maofisa na askari wa Rumi walichukua hatua ya kumsulibisha Yesu.
   b. Maneno yanamaanisha "watu wasio na sheria," ambayo yangerejea kwa Mataifa, ukijumuisha Warumi ambao hawakuwa na sheria za Musa (linga.Rum.2:14).
   c. Jambo hili linalingana na mambo halisi yaliyotukia (Math.27:1,2,26,27).

**24)**

1. Petro hakutaka apoteze muda mwingi kuthibitisha kusulibisha na kifo chake Yesu. Mambo hayo yalikuwa dhahiri na kusadikiwa na wote.
2. Bali alipaswa atumie muda mwingi kuthibitisha ufufuo wake Kristo kwa wale walio waaminifu wenye mioyo mizuri tayari kuamini ukweli huo.
3. Basi, kama jambo lake la nne, Petro alizungumzia ufufuo wake Kristo. Zingatia mtiririko wa hoja zake, katika sehemu hii:
   a. Mungu alimdhihirisha Yesu kwa miujiza ambayo hakuna mtu angeipinga (mst.22).
   b. Walakini, Wayahudi kwa mikono mibaya, walimsulibisha na kumwua Yesu (mstari wa mwisho).
   c. Hivyo basi, walitoa hukumu ya kifo.
   d. Lakini Mungu anaigeuza hukumu ya kifo hiyo isiyo na haki na kudhihirisha tena Uungu wake kwa kumfufua mwanawe wa pekee kutoka kwa wafu.
4. Katika kufanya hivyo Mungu "alifungua uchungu wa mauti."
   a. "Kufungua" λυσασ – kinyume cha kufungwa au kuunganishwa pamoja kwa kamba. Inamaanisha kufunguliwa, kuachiliwa au kuwa huru.
   b. Basi, kwa kumfufua Yesu kutoka kwa wafu kaburini, Mungu alimweka huru Yesu mbali na mauti alionja kwa ajili ya kila mwanadamu (Ebr.2:9).

5. Kama pointi yake ya sita, Petro alisema Yesu alifufuka toka kwa wafu kwa sababu isingewezekana kwake yeye kuweka chini ya mauti baada ya siku tatu zilizoamuliwa na Mungu (linga. Lk.24:46).
6. Umuhimu wa ufufuo wa Yesu toka kwa wafu unaweza kuonekana katika maandiko mengine kadhaa:
   a. 1 Wakorintho 15:17.
   b. Warumi 4:25.
   c. Warumi 1:4.
7. Kwa sababu ya umuhimu wake, Petro alitumia muda wake kwa mistari kumi na moja kujadili somo la ufufuo.
8. Muhtasari wa 2:22-24, *Yesu*: aliyedhihirishwa na Mungu; aliyeuawa na Wayahudi; aliyefufuliwa na Baba. Katika sehemu hii muhimu, tumeona Petro akihubiri mambo sita ya nguvu, yenye kugusa nyoyo, na kustaajabisha:
   a. Kwanza, Mungu alidhihirisha wazi wazi kumkubali Yesu kwa nguvu za miujiza alizoitenda kupitia Yesu (mst.22).
   b. Pili, miujiza halisi hiyo ilijulikana na ukweli huo usingepingwa, ama na Wayahudi au watu wengine wowote (mst.22).
   c. Tatu, kinyume na Wayahudi walivyofikiri, Mungu alimtoa Mwanawe wa pekee kwao kwa mashauri lake alilokusudia na kwa kutangulia kujua kwake tangu mwanzo (mst.23).
   d. Nne, mbali na Baba kumdhihirisha Mwanawe, Wayahudi walimsulibisha na kumwua kwa mikono mibaya (mst.23).
   e. Tano, Mungu aligeuza hukumu yao isiyo haki ya kifo kwa kufumfua Yesu kutoka kwa wafu (mst.24).
   f. Na sita, haikuwezekana Yesu kuwa mtumwa wa mauti baada ya siku tatu zilizoamuriwa na Mungu (mst.24).
9. Mtazamo kwa ufupi wa sura 2, ahadi imetimizwa na kanisa kuanzishwa:
   a. 2:1-13 Mitume walijazwa Roho Mtakatifu na kunena lugha zingine.
   b. 2:14-36 RohoMtakatifu (kupitia Petro) alithibitisha dhambi ya makutano, haki na hukumu.
      (1) 2:14-21 Tafsiri iliyovuviwa ya matukio haya.
      (2) 2:22-24 Yesu: Alidhihirishwa na Mungu, Aliuawa na Wayahudi; Alifufuliwa na Baba.

**2:25-28)**

1. Katika mistari hii Petro alianza na ufufuo wake Yesu kwa kunukuu kutoka katika maandiko ya Agano la Kale, ambayo wasilizaji waliyaamini.
2. Zingatia mst.25 unaanza na neno la ufunguo "Maana" (for).
   a. Neno "maana" linaeleza muunganiko kati ya yaliyotangulia kusemwa mwishoni mwa mst.24 na kile kinachosemwa katika mistari hii.
   b. Mwishoni mwa mst.24 Petro alisema haikuwezekana Yesu kushikwa chini ya utumwa wa mauti.
   c. Katika mst.25-28 anafafanua kwa nini haikuwa hivyo.
   d. Alisema haikuwezekana Yesu kushikwa chini ya utumwa wa mauti kwa sababu Mungu alitabiri ufufuo wa Kristo, Masihi kupitia kwa Daudi katika Agano la Kale.
3. Fungu maalum alilolinukuu Petro ni Zab.16:8-11.
   a. Tutajifunza maana iliyovuviwa ya Zaburi, kama ilivyoelezwa na Petro katika mst.29-32 ya sura hii.
   b. Lakini kwanza tuone ni nani Petro alidai Daudi alimzungumzia katika Zab.16:8-11.
   c. Kisha tutachanganua kilichozungumzwa katika Zaburi.
4. Kwanza, Petro alisema kwa uvuvio katika mst.25 kwamba Daudi alizungumza mambo yaliyopo katika Zab.16:8-11 "ataja habari zake."
   a. Lakini, ni habari za "nani"?

    b. Hakika, Petro alikuwa akirejea kwa Yesu, ambaye asingeshikwa na mauti (mst.24).
5. Katika kusoma Zaburi hii, inaonekana kama Daudi alikuwa akizungumza juu yake mwenyewe.
    a. Lakini, Petro alibainisha wazi katika kufunua sehemu hii ya Zaburi 16, Daudi hakujitaja mwenyewe kama mtu ambaye angenena baadaye maneno haya.
    b. Hakika, Petro angeonyesha katika mst.29-32 ya sura hii kwamba sehemu hii ya Zaburi 16 haikumlenga Daudi.
    c. Badala yake, kwa uvuvio wa Mungu, Daudi alikuwa akitabiri kuhusu Masihi aliyekuwa akisubiriwa kwa muda mrefu!
    d. Masihi ndiye mpakwa mafuta, mfalme ajaye, Kristo ambaye angelikuwa Mwokozi wa mwanadamu.
    e. Kwa hiyo, katika Zab.16, Daudi alikuwa akitabiri mambo kuhusu Masihi ajaye, Kristo, Mwokozi.
    f. Lakini mtume mwenye kuvuviwa Petro alisema Daudi alinena mambo haya kuhusu Yesu (habari zake).
    g. Wewe nami tunapaswa kuhatimisha kama hivyo!
6. Nusu ya sehemu ya mwisho ya mst.25 na sehemu ya kwanza ya mst.26, Masihi huyu alitabiriwa akimwona Bwana Mungu, akimwangalia, na kumwokoa katika matatizo.
    a. Hili lingempatia Masihi ujasiri na furaha.
    b. Na pia lingedhihirisha uhakikisho wa Mungu kama ndiye aliyemwita Masihi.
7. Katika nusu ya sehemu ya mwisho ya mst.26 na katika mst.27,28, tunaona Daudi pia akitabiri mambo yafuatayojuu ya Masihi:
    a. Mwili wake ungekaa katika matumaini (mst.26).
    b. Jambo hilo ni kweli kwa kuwa Mungu asingeacha nafsi yake (roho) kuzimu (mst.27a).
        (1) Kama tutakavyo jifunza, kuzimu ndipo mahali roho zetu huenda tunapokufa kimwili.
        (2) Hilo linatufahamisha kuwa Masihi angekufa kimwili, lakini Mungu asingeruhusu nafsi yake kubakia kuzimu.
    c. Wala Mungu asingeruhusu mwili wa Masihi kuona uharibifu (i.e., kuchakaa na kurudia mavumbi kama itakavyokuwa kwa miili yetu) (mst.27b).
    d. Kinyume chake, Masihi angeishi tena baada ya kufa (mst.28a).
    e. Basi, angekuwa mshindi juu ya mauti.
    f. Na baada ya ufufuo wa ushindi, Masihi angefurahia wakati wa kupaa kwake kwenda mbinguni kuwepo pamoja na Mungu (mst.28b.)
    g. Hii ilikuwa namna nyingine kuonyesha kusulibiwa kwake Mwokozi kulikuwa mipango ya Mungu kinyume na kudai ilikuwa laana yake!
8. Pia katika mst.27 angalia Daudi ametaja Masihi kama “Mtakatifu.”
    a. Petro anamtambua huyu “Mtakatifu” kuwa ni Bwana Yesu (3:13-15).
    b. Stefano anatambua kuwa huyo ni Bwana Yesu (7:52)!
    c. Na Paulo anamtambua Mtakatifu kuwa Bwana Yesu (13:33-37)!
9. Ni unabii wa kustaajabisha huu juu ya Masihi, Kristo! Unastaajabisha kwa sababu kadhaa:
    a. Kwanza, ulitolewa miaka mingi kabla ya Masihi kuja na kufa.
    b. Pili, Mungu alitabiri mambo mengi ya kushangaza kuhusu Masihi ambayo mwanadamu asingetabiri.
    c. Tatu, unabii unaujumbe sahihi wa ajabu na maelezo sahihi ambayo mwanadamu wa kawaida asingeweza kubahatisha au kuota.
    d. Kama tulivyoona, maelezo haya yanajumuisha mambo yafuatayo:
        (1) Angekuja na kuishi katika mwili na pia angekufa.
        (2) Walakini roho yake isingeachwa kuzimu na wala mwili wake usingeona uharibifu kaburini.
        (3) Basi, angekuwa mshindi juu ya mauti kwa kufufuka kutoka kwa wafu.
        (4) Na baada ya ufufuo wenye utukufu, angepaa kwenda mbinguni, akirejea katika furaha za mahali hapo pazuri ajabu.

(5) Je, kuna shaka yoyote kwamba Yesu ndiye Masihi aliyegonjewa kwa muda mrefu?!
(6) Alitimiza kila jambo la unabii huu wa ajabu kwa ukamilifu na barabara kabisa!
(7) Tena, je kuna shaka lolote kwamba Biblia, na unabii wake sahihi wa kushangaza, ni neno la Mungu?!

10. Kabla ya kuondoka mst.25-28 kuna jambo lingine ambalo linastahili kujadiliwa zaidi.
    a. Mst.27, kulingana na tafsiri (version) ya kale ya "King James", Mungu asingeiacha roho ya Masihi "jehanamu" (hell).
    b. Tafsiri za ASV na NKJV zinaonyesha kwamba Mungu asingeacha nafsi (soul) ya Masihi kuzimu (hades).
    c. Kuna tofauti yoyote kati ya maneno mawili haya "jehanamu" (hell) na "kuzimu" (hades)? Kama ipo, ni ya namna gani?
    d. Kuna tofauti na tafsiri sahihi ya mstari huu ni kuzimu (hades).
    e. Ukweli ni kwamba, neno halisi la Kiyunani linalopatikana hapa na katika mistari kadhaa ya Agano Jipya.
    f. Kuna tofauti kubwa ya neno la Kiyunani linalotafsiriwa jehanamu (hell) "γεεννα" ambalo halipo katika mstari huu.
        (1) Neno lililotafsiriwa ahera (hell) linaelezea mahali waovu wataadhibiwa milele.
        (2) Linga. Mk.9:43,44.
    g. Kwa upande mwingine, neno kuzimu "hades" linalenga ulimwengu usionekana ambako roho zetu za kibinadamu hukaa kwa muda zinapoondoka katika miili yetu wakati tunakufa kimwili.
        (1) Katika ulimwengu au eneo hili kuna sehemu mbili.
        (2) Kadhalika kuna eneo kubwa linalotenganisha sehemu hizi mbili.
        (3) Wakati wa kufa kimwili kifo cha kila mtu mwenye haki huenda mojawapo ya sehemu hizi za kuzimu, na roho ya kila mtu asiye haki inakwenda sehemu pengine.
        (4) Roho zilizopo mahali pa wasio haki haziwezi kuvuka kuingia eneo la wenye haki kadhalika.
    h. Kuelewa hili vema, tunatakiwa kujifunza mafungu kadhaa ya maandiko.
        (1) 1 Thes.5:23.
        (2) Yak.2:26.
        (3) Mhu.12:7.
        (4) Lk.16:19-31.
        (5) Lk.23:43.
        (6) Ufu.20:12-15.
    i. Kuna ndugu waaminifu, wasomi, wema wanaoamini kuwa sehemu ya kuzimu ya paradiso iko mbinguni.
        (1) Ingawa somo juu ya imani hiyo ni nje na kozi hii, imeandikwa vyema, na kutafakari kwa usahihi kwa uchunguzi wa mtu binafsi.
        (2) Mimi binafsi naamini kwamba sababu ya eneo la paradiso kuwa mbinguni ni swala pana zaidi.
        (3) Wale wote walipata notisi za kozi hii watapata nyongeza ya maelezo katika somo hili mwishoni mwa notisi (appendix B) hizi.

**2:29)**

1. Hapa, Petro anabainisha wazi kuwa Zab.16:8-11 haikumhusu Daudi; basi, Daudi alikuwa akitabiri kuhusu mtu fulani na wala si yeye mwenyewe.
2. Petro anadai kwamba Zaburi haikumlenga Daudi kwa sababu alikuwa amekufa na kuzikwa, na kaburi lake lilikuwepo Yerusalem.
3. Kwa maneno mengine, kinyume na mtu aliyetafsiriwa katika Zaburi, mwili wa Daudi ulionja kuoza kwa kawaida na kuharibika wakati huo.
    a. Linga. 13:36 ambapo aliyevuviwa mtume Paulo alisema mwili wa Daudi uliona uharibifu kaburini!

4. Basi, mwili wa Daudi haukufufuka kutoka kwa wafu kama wa huyo aliyetabiriwa katika Zaburi hii.
5. Hatimisho pekee ambalo tunaweza kuhatimisha ni kwamba Zaburi ilimlenga mtu mwingine na wala si Daudi.
6. Petro angeondoa shaka zote kuhusu mtu huyo kuwa ni yupi katika mistari inayofuata kadhaa.
7. Lakini kbla ya hapo, angalia Petro anamtaja Daudi kama "baba" (patriarch).
   a. Baba (patriarch) ni kichwa au kiongozi wa familia.
   b. Hakika, neno limetumika kumlenga Daudi kama kichwa cha familia ambayo kwa huyo Masihi angetokea (linga. Math.1:1).

**2:30,31)**

1. Katika mistari hii Petro alitoa maana iliyovuviwa ya Zab.16:8-11.
2. Amefanya hivyo kwa kuelezea mambo makubwa manne.
   a. Kwanza, alisema kwamba katika Zab.16 Daudi alikuwa akisema kama nabii wa Mungu, k.m. kama mtu aliyenena neno la Mungu.
   b. Pili, Petro alisema kwa kunena maneno haya, Daudi akakumbuka ahadi ya Mungu kumwinua Kristo kukaa katika kiti cha enzi cha Daudi.
   c. Tatu, Daudi alinena haya kuhusu kumwinua Kristo kukaa katika kiti cha enzi cha Daudi kama unabii wenye uvuvio wa ufufuko wake Kristo, Masihi.
   d. Mwisho, Petro alieleza mambo ya kweli muhimu kuhusu ufufuo wa kipekee wa Kristo.
      (1) Nafsi yake haikuachwa kuzimu,
      (2) Na mwili wake usingeona uharibifu kaburini.
3. Ukishaweka akilini mwako hizo pointi nne muhimu, ebu na tujifunze maelezo muhimu kadhaa yanayopatikana katika mistari hii miwili.
4. Mst.30 Petro alisema Daudi alipotoa unabii katika Zabu.16:8-11, alikuwa anajua ahadi ya Mungu aliyoitoa hapo nyuma.
   a. Kadhalika, ahadi ya Mungu kwa Daudi ilimlenga mmoja katika uzao wake (k.m., "uzao wa viuno vyake").
   b. Kubainisha zaidi, Mungu aliahidi kwamba Kristo, Masihi angetoka katika familia ya Daudi.
   c. Na aliahidi Kristo angefufuka kutoka kwa wafu kuketi katika kiti cha enzi.
      (1) Ni wazi kwamba Mungu hakuwa anamaanisha kuwa Kristo angetawala katika kiti cha duniani, cha kimwili cha Daudi.
      (2) Kinyume chake, kuketi katika kiti cha Daudi, maana yake kutawala, kuongoza, kuwa na mamlaka kama mfalme juu ya ufalme wake.
      (3) Linga. Lk.1:31-33.
   d. Ahadi hii ya Mungu kwa Daudis inapatikana katika 2 Sam.7:12-16 (linga. Zab.132:11; 89:3,4).
5. Mst.31 Petro anatoa muda haswa wa utimilifu wa unabii huu.
   a. Haukutimia miaka mamia, au hata maelfu baada ya karne ya kwanza.
   b. Kinyume chake, Petro alisema kwa uvuvio kwamba ahadi ya Mungu kwa Daudi ilitimia kwa ufufuo wa Kristo, karne ya kwanza.
   c. Basi, Kristo alipofufuka kwa ushindi toka ufuni karne ya kwanza, alifufuka kutawala kama mfalme juu ya kiti cha Daudi!
   d. Alifufuka ili atawale na kuwa na mamlaka katika ufalme wake.
   e. Mambo haya yote yalitendeka karne ya kwanza, na wala si tarehe mbali ya baadaye!
   f. Ni muhimu sana kutambua ukweli huo kwa sababu ya mafundisho ya uongo ya utawala wa miaka elfu (premillennialism) ambayo yanafundishwa sehemu kubwa katika ulimwengu wa dini siku hizi.
   g. Tutajifunza fundisho hilo na kuona kwa nini ni uongo mwishoni mwa sura hii.
   h. Hadi hapo, tafadhali weka sawasawa akilini mwako wazo hili.

(1) Kristo alifufuka toka kwa wafu karne ya kwanza kutawala kama mfalme juu ya kiti cha kiroho cha enzi cha Daudi.

**2:32)**

1. Petro kwa ujasiri alihubiri kwamba Yesu ambaye mitume walimtangaza ndiye aliyetimiza ahadi ya Mungu kwa Daudi!
2. Angalia jinsi kwa hakika Yesu alivyotimiza ahdi kwa Daudi:
   a. Alitoka uzao wa Daudi (linga. Math.1:1; Ufu.22:16).
   b. Mungu hakuiacha roho yake kuzimu.
   c. Baba hakuacha roho yake ione uharibifu kaburini.
   d. Na Mungu akamfufua toka kwa wafu ili atawale akiwa Mfalme juu ya kiti cha enzi cha Daudi.
   e. Kwa hiyo, kuna hatimisho moja tu lenye uhakika.
   f. Hatimisho hilo ni kwamba Yesu ni Kristo, Masihi, Mwokozi wa mwanadamu, Mfalme juu ya ufalme wake!
   g. Hoja za Petro za msingi kabisa zinaweza kufupishwa kama ifuatavyo:
      (1) Mungu alitabiri angemfufua Kristo, Masihi atoke kwa wafu; nafsi yake isingeachwa kuzimu; na mwili wake usingeona uharibifu kaburini.
      (2) Mungu alifufua Kristo toka kwa wafu; nafsi yake haikuachwa kuzimu; na mwili wake haukuona uharibifu kaburini.
      (3) Kwa hiyo, Yesu ndiye Kristo, Masihi aliyetabiriwa!
   h. Unaonaje mvuto wa ujumbe huo kwa wasikilizaji siku hiyo?!
   i. Unaweza kushukuru ujumbe huo unavyopaswa kutushawishi katika maisha haya leo?!
3. Lakini, Petro hakuhakikisha tu ukweli huo kutoka katika maandiko na kuhubiri kwa ujasiri namna hii.
4. Pia aliwahakikishia wasikilizaji kwamba yeye na mitume wengine walikuwa mashahidi wa ukweli wa Mungu kumfufua Yesu toka kwa wafu.
   a. Kumbuka, Yesu aliwaambia mitume kwamba wangekuwa mashahidi wake (Joh.15:27; Mdo.1:8).
   b. Ukweli ni kwamba, walipaswa wawe mashahidi wa ufufuo wake ili kuwa mitume wa Kristo (Mdo.1:21,22).
   c. Walikuwa wameona na kumsikia akitoaa uthibitisha usiopingika wa ufufuo wake baada ya kifo na maziko yake (1:3).
   d. Siyo tu hilo, lakini pia walikula pamoja naye, na kumgusa; pamoja na makovu katika mikono na ubavu wake (Lk.24:36-43; Yoh.20:26-29; 1Yoh.1:4)!
   e. Na walimwona akipaa kwenda mbinguni (Mdo.1:9-11).
   f. Basi, ushuhuda wao usingefanikiwa kwa kupingwa.
5. Kabla ya kuondoka katika mistari hii, ni muhimu kutambua kwamba kuna mafungu mengine yenye uvuvio kuhusu ahadi ya Mungu kwa Daudi. Na mafungu yote mawili yanathibitisha ahadi kutimilika katika Yesu Kristo!
   a. Katika Mdo.13:32-39 (haswa mst.34,35), Paulo aliyatumia mafungu mawili yote Zaburi 16 na 2 Sam. 7:12ff na alidai ahadi hizi za Mungu kwa Daudi ilitimizwa na Yesu.
   b. Na Ebr.1:1-5 (hasa mst.5), mwandishi aliyevuviwa wa Waebrania ananukuu 2 Sam.12ff na kusema ahadi ya Mungu kwa Daudi ilitimia katika Yesu.
   c. Basi, kuna mafungu matatu mbalimbali katika Agano Jipya kwa ahadi hii ya Agano la Kale na mafungu yote yanahatimisha kwa maana moja, pasipo makosa wala kupingana.
   d. Hatimisho kadhaa tunaweza kueleza kutokana na ukweli huu:
      (1) Kwanza, inatoa ushahidi mkubwa kwamba Yesu ndiye Kristo ambaye Mungu alimtabiri kuwa angemfufua kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi.
      (2) Na pili, inaonyesha umoja wa kustaajabisha na mapatano (harmony) ya Biblia. Huu ni moja ya ushahidi mkubwa kwamba kitabu hiki kitakatifu asili yake ni Mungu, na wala si mwanadamu!

6. Muhtasari wa 2:25-32, Yesu: uhakiki toka katika unabii.
   a. Mst. 25 Petro alithibitisha mambo kadhaa kwa kunukuu toka Zab.16:8-11.
      (1) Kwanza, alithibitisha madai yake kwamba isingewezekana kwa Yesu kushikwa na mauti.
      (2) Na pili, alithibitisha ufufuo wa Kristo toka kwa wafu kama ule uliotabiriwa na Daudi katika Zaburi hii.
      (3) Tatu, alithibitisha kwamba ufufuo wa Kristo toka kwa wafu ulihakiki yeye kuwa ni Masihi ambaye Waisraeli walikuwa wakimgojea kwa muda mrefu!
   b. Pia mst. 25 Petro alisema ingawa maneno ya Zaburi 16:8-11 yaliandikwa na Daudi, hayakumlenga Daudi. Badala yake, yalimlenga Yesu.
   c. Katika Zaburi mwenye kuvuviwa Daudi alitabiri mambo yafuatayo yenye kustaajabisha kuhusu Masihi (mst.25-28).
      (1) Bwana angekuwepo daima mbele ya Masihi, akimwangalia, na kumwokoa atoke katika taabu (mst.25).
      (2) Ukweli huo ungempatia Masihi faraja, ujasiri, na furaha (mst.26).
      (3) Siyo tu hivyo, bali Masihi angejaa matumaini (mst.26).
      (4) Swala hilo ni kweli kwa kuwa Masihi angekufa kimwili, Mungu asingeiacha nafsi ya Masihi kuzimu (mst.27).
      (5) Wala Mungu asingeacha mwili wake uone uharibifu kaburini (mst.27).
      (6) Badala yake, Masihi angeshinda kifo kwa kufufuka toka kwa wafu na kuishi tena (mst.28).
      (7) Na, baada ya ufufuo wa ushindi, Masihi angepaa kwenda mbinguni na kufurahia kuwepo kwake mbele za Mungu mbinguni (mst.28).
   d. Tena, mst. 29, Petro alitangaza kwamba maneno ya Zaburi hayakumlenga Daudi kwa kuwa alikufa na mwili wake uliona uharibifu kaburini Yerusalem.
   e. Mst.30,31 Petro alieleza mambo makuu yafuatayo katika kutoa maana yenye uvuvio ya Zaburi 16:8-11:
      (1) Kwanza, katika Zaburi hiyo, Daudi alinena neno la Mungu akiwa mmoja wa manabii wake.
      (2) Pili, katika kunena maneno haya, Daudi akakumbuka ahadi ya Mungu kumwinuaKristo aketi juu ya kiti cha enzi cha Daudi.
      (3) Tatu, ahadi hiyo ya kumwinua Kristo kuketi katika kiti cha enzi cha Daudi ilikuwa unabii uliotabiri ufufuo wa Kristo, Masihi.
      (4) Nne, mambo ya kipekee katika ufufuo huo ni ukweli kwamba nafsi ya Kristo isingelibakia kuzimu na mwili wake usingeliona uharibifu kaburini.
      (5) Tano, Petro alisema kwa uvuvio kwamba ahadi ya Mungu kwa Daudi ilitimia katika ufufuo wa Kristo karne ya kwanza.
   f. Mst. 32 Petro kwa ujasiri alisema Yesu alitimiliza ahadi ya Mungu kwa Daudi!
      (1) Mungu Baba alimfufua Yesu kutoka kwa wafu kama ilivyotabiriwa.
      (2) Nafsi ya Yesu haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu kaburini.
      (3) Kwa hiyo, Yesu ndiye Kristo, Masihi, Mwokozi, Mfalme, ambaye Daudi alimtabiri.
      (4) Na wala si tu Petro alithibitisha ukweli huu wa ajabu wa maandiko,
      (5) Bali mitume pia walikuwa mashahidi kwa ufufuo dhhiri ambao ingelikuwa vigumu kuupinga!
   g. Basi, katika sehemu hii ya kustaajabisha, Petro, kwa uvuvio wa Mungu, alithibitisha kwamba Yesu alikuwa ndiye Masihi aliyegonjewa kwa muda mrefu, Kristo, Mwokozi.
      (1) Alifanya hivyo kwa kunukuu katika maandiko ya Agano la Kale ambayo wasikilizaji wake Wayahudi waliyajua.
      (2) Na alithibitisha mambo hayo kwa ushahidi thabiti wa mitume kumi na mbili kwamba Mungu alimfufua Yesu toka kwa wafu, kama ilivyotabiriwa
      (3) Hata ingawa habari hii ilithibitishwa, Petro na mitume walitoa ushuhuda zaidi wa kukazia madai yao kwamba Yesu ndiye Kristo.

(4) Tutaona ushahidi huo katika mst.33-36.
7. Mtazamo kwa ufupi wa sura 2, Ahadi ilitimizwa na kuanzishwa kwa kanisa.
   a. 2:1-13 Mitume walijazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine.
   b. 2:22-24 *Yesu*: Alidhihirishwa na Mungu; aliuawa na Wayahudi; alifufuliwa na Baba.
   c. 2:25-32 *Yesu*: Uthibitisho kutoka katika unabii.

### 4. **(2:33-36) YESU: ALIINULIWA NA KUKETISHWA JUU YA KITI CHA ENZI**

**2:33)**
1. Mst. 25-31 Petro alinukuu na kufafanua Zaburi 16:8-11.
2. Alifanya hivyo ili kuthibitisha kwamba Kristo angefufuka kutoka kwa wafu kutawala kama Mfalme juu ya kiti cha enzi cha Daudi.
   a. Pia alitoa ushuhuda wa mitume kumi na mbili kwamba Mungu alimfufua Yesu, Kristo, toka ufuni katika kutimiza Zaburi hiyo.
   b. Swali la kawaida lingezuka: "Yesu alienda wapi baada ya kufufuka toka ufuni?"
   c. Petro alijibu swali hilo katika mstari huu.
3. Katika kufanya hivyo, alitoa madai mazito na muhimu sana kuhusu Yesu. Alimhubiri Yesu:
   a. Ameinuliwa na kuketishwa mkono wa kuume wa Mungu,
   b. Alipokea ahadi ya Roho Mtakatifu kutoka kwa Baba, na
   c. Alimwaga matendo ya miujiza ambayo yalitukia siku ya kustaajabu ya Pentekoste ile.
4. Ebu na tuchanganue madai hayo kwa maelezo zaidi.
5. Kwanza, dai la kwamba ameinuliwa na kuketi mkono wa kuume wa Baba.
   a. Hakika, hili linamaanisha Yesu alikuwa mbinguni pamoja na Baba.
      (1) Dhahiri kabisa, Baba alidhihirisha kumkubali Yesu kwa kumfufua toka ufuni na kwenda mbinguni.
   b. "Alimpandisha" - υψωθεισ - kuinuliwa juu; kutukuzwa.
      (1) Basi, Baba alimwinua Mwanawe kwa kumpandisha kwenda juu mbinguni (linga. Flp.2:9; Ebr.2:9; Efe.1:20ff).
      (2) Ni jambo linalofurahisha kulinganisha matumizi ya neno hili hili katika mafungu mengine ya maandiko:
         (a) Yoh.8:28.
         (b) Linga. Yoh.3:14; 12:32,33.
   c. Tena, wala si tu Yesu kuinuliwa, lakini alipandishwa "kuketi katika mkono wa kuume wa Mungu."
      (1) Katika Biblia mkono wa kuume, hasa kuketi mkono wa kuume wa Mungu, ni mahali pa mamlaka na nguvu (Linga. Ayu.40:14; Zab.17:7; 18:35).
      (2) Yesu, tena, alitukuzwa na Baba kwa kupandishwa mbinguni katika nafasi ya mamlaka na nguvu.
      (3) Kwa hiyo, Yesu alikuwa akitawala kama Masihi, Mfalme, mbinguni, kama alivyotabiriwa katika Zabu.16:8-11!
      (4) Tena, Yesu kutawala kama Mfalme alianza karne ya kwanza – wala si miaka mamia au maelfu baadaye kama viongozi wengine wa dini wanavyodai leo!
      (5) Hili linalingana kabisa na yale Mungu anayofundisha katika mafungu mengine kuhusu Yesu Kristo muda alipoanza kutawala:
         (a) Ilikuwa baada ya kufanya utakaso wa dhambi (Ebr.1:13ff).
         (b) Ilikuwa baada ya ufufuo wake toka kwa wafu (2:30-32).
         (c) Alipopaa na kurejea kwake mbinguni (Linga. Dan.7:13,14).
      (6) Fungu lingine linalothibitisha Yesu kuinuliwa na kuketishwa mkono wa kuume wa Mungu karne ya kwanza ni Efe. 1:19ff.
      (7) Linga. Rum.8:34; Kol.3:1; Ebr.12:2; 1 Pet.3:22.
   d. Kutokana na mambo haya, tunaweza kuona kwamba Petro alipodai Yesu kuinuliwa na kuketishwa mkono wa kuume wa Mungu, alibainisha mambo muhimu mno!

6. Pili, Petro alidai huko mbinguni, Yesu alipokea ahadi ya Roho Mtakatifu toka kwa Baba.
   a. Kama tulivyojifunza awali, ahadi ilikuwa kutumwa kwa Roho Mtakatifu kwa mitume ili kuwapatia uwezo wa kimiujiza, pamoja na uwezo wa kufunua Agano Jipya la Kristo.
   b. Tafadhali angalia maelezo yetu katika 1:4 kwa kuthibitisha zaidi.
   c. Tafadhali kumbuka pia Yesu alisema asingeweza kumtuma Roho Mtakatifu kwa mitume hadi atakaporejea tena kwa Baba mbinguni (Yoh.16:5-7).
   d. Yohana pia alidai kwamba Roho Mtakatifu angetolewa baada ya kutukuzwa kwanza Yesu (Yoh.7:39)!
   e. Basi, ukweli wa kwamba ahadi hii ilitimizwa siku hiyo ni ushahidi tosha kuthibitisha Yesu kuwa alirejea mbinguni na kutukuzwa!
7. Tatu, Petro alidai kuwa Yesu alimwaga matukio hayo ya miujiza ambayo wasikilizaji wenyewe waliona na kusikia siku hiyo. Jambo hili linalenga mambo kadhaa:
   a. Kwanza, kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya mitume (2:1-4);
   b. Pili, uwezo wa miujiza wa mitume kunena lugha zingine ambazo hawakuwahi kujifunza hapo kabla (2:4-13).
   c. Na tatu, uwezo wa miujiza wa mitume kufunua ukweli, neno la Mungu na kutafsiri unabii (2:14ff).
8. Angalia jinsi Petro alivyokabiliana na shutuma kwanza kabisa za baadhi ya wasikilizaji siku ile kuwa mitume walikuwa wamelewa mvinyo mpya (2:13).
   a. Mst.16-21 kwanza alibainisha kwamba miujiza hii ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ilitabiriwa na Bwana katika maandiko.
   b. Tena katika mst.22-31 alithibitisha kwamba ufufuo wa Yesu ulitabiriwa pia katika maandiko.
   c. Katika mst.32 alionyesha kwamba mitume walikuwa ni mashahidi wa ufufuo wake.
   d. Katika mstari huo amerejea ahadi ya Yesu kumtuma Roho Mtakatifu kwa mitume.
9. Mambo yote haya ya kweli yasiyopingika yanasaidia kuthibitisha kwamba Petro na mitume wengine walikuwa wakinena kwa mamlaka na nguvu za Mungu mwenyenzi!

**2:34,35)**

1. Petro tena anabainisha kwa wasikilizaji wake kwamba Daudi hakupaa mbinguni.
   a. Sababu moja inayompelekea Petro kusema hivyo ili kuonyesha kwamba maelezo ya mstari wa mwisho hayakumlenga kabisa Daudi.
   b. Bila shaka kabisa yalimlenga Yesu Kristo, kama Petro alivyodai kwa uvuvio mstari wa mwisho.
   c. Kwa nyongeza, Petro alikuwa akionyesha kwamba Zaburi aliyoinukuu haikumlenga Daudi kabisa.
2. Tena Petro alimnukuu Daudi, kama ilivyoandikwa katika Zaburi 110:1.
   a. Katika Zaburi hiyo, Bwana (haswa, Yehovah) alinena kwa mmoja aliyetajwa na Daudi kuwa "Bwana wangu."
      (1) Kwa kuwa Daudi alimtaja mtu huyo kuwa Bwana, hivyo basi alikuwa mkuu kuliko Daudi.
      (2) Hakika, Wayahudi waliitambua Zaburi hii kama iliyomtabiri mambo yalihusu Masihi, Kristo (linga. Math.22:41-46; Lk.20:41-44).
      (3) Kwa hiyo, katika Zaburi hii, Mungu Baba alikuwa akizungumza na Bwana wa Daudi, ambaye alikuwa Kristo, Masihi.
   b. Alichosema Baba kuhusu Kristo katika Zaburi hiyo ni muhimu pia.
      (1) Alimweleza Kristo kuketi (k.m. upande wa Baba yake) mkono wa kuume.
         (a) Kama tulivyojifunza mapema, mkono wa kuume wa Baba ni nafasi ya nguvu na mamlaka.
         (b) Hili linaonyesha kuwa mmoja akitawala kama Mfalme mwenye mamlaka makubwa.

(c) Basi, Baba alikuwa akitabiri Kristo akitawala kama Mfalme mkono wa kuume wa Baba mbinguni.
(d) Lakini Petro alikuwa amethibitisha kikamilifu matumizi ya Zaburi 16:8-11 kwamba Yesu alikuwa Kristo, Masihi.
(e) Na katika mstari wa mwisho, Petro alidai kwa uvuvio kwamba Yesu, "*amepandishwa mkono wa kuume wa Mungu*."
(f) Kwa hiyo, Petro alikuwa akitumia Zaburi 110:1 kama nyongeza ya maandiko kuthibitisha kuwa Yesu ndiye Kristo aliyetabiriwa, Masihi! Mchanganuo wake wa kimaatiki ni kama ifuatavyo:
1. Yesu ameinuliwa na kuketi upande wa kuume wa Mungu (mst.33).
2. Lakini Daudi alitabiri tayari kwamba Kristo angeketi mkono wa kuume wa Mungu (mst.34, 35; Zab.110:1).
3. Kwa hiyo, Yesu alikuwa ndiye Kristo aliyetimiza unabii huo!
(g) Hatimisho sahihi pekee ambalo linaweza kutolewa ni kwamba Yesu, Kristo alikuwa mbinguni mkono wa kuume wa Mungu akitimiza unabii.
(h) Na akikaa mahali pa mamlaka na nguvu, akitawala kama Mfalme katika ufalme wake.
(i) Na tena, utawala wake ulianza karne ya kwanza, wala si miaka mamia au maelfu baadaye.
(j) Kadhalika, amekuwa akitawala kama mfalme juu ya utawala wake tangu hapo!
(k) Ni jambo la kufurahisha kuona kwamba mwandishi aliyevuviwa wa Waebrania anataja pia kifungu hiki kuhusu Yesu kama Kristo (Ebr.1:13)!

(2) Katika Zab.110:1 Baba pia alimwambia Masihi angetawala muda gani uliopangwa!
(a) Mungu alisema Masihi angetawala hata awaweke maadui zake Masihi chini ya miguu yake.
(b) Hii ni njia nyingine ya kusema Masihi angetawala hadi madui zake wote wangewekwa chini ya miguu yake; walioshindwa na kuangushwa.
(c) Kwa njia pekee ya kutumia Zaburi 110:1 ulinganifu na uvuvio mtume Paulo anabainisha adui wa mwisho kuwa ni:
1. 1 Kor. 15:23-26.

**2:36)**

1. Mungu, kupitia Petro, alitaja hatimisho sahihi la hoja yake.
2. Petro anaanza hatimisho lake kwa kutumia neno "Basi" na kuhatimisha kwa Waisraeli wote.
3. Alisema wangejua kwa uhakika, pasipo shaka, kwamba hatimisho hilo lilikuwa sahihi kabisa.
4. Kabla ya kujifunza hatimisho hilo, angalia jinsi Mungu alivyothibitisha swala lake kupitia Petro:
    a. Petro alikuwa amehubiri yafuatayo kuhusu Yesu:
    (1) Maisha yake yalidhihirishwa na Mungu, kwa nguvu nyingi, miujiza ya wazi aliyoitenda (mst.22).
    (2) Kusulibishwa kwake na kifo kwa mikono ya watu wabaya (mst.23).
    (3) Maziko yake, ingawa mwili wake haukuona uharibifu (mst.27,31).
    (4) Kufufuka kwake toka ufuni, kama ilivyotabiriwa juu ya Masihi (mst.30-32).
    (5) Kupaa kwake kwenda mbinguni (mst.33).
    (6) Kuinuliwa kwake kuwa Mfalme juu ya kiti cha enzi cha Daudi kuketishwa mkono wa kuume wa Mungu mbinguni. (mst.33-35).
    (7) Na kupokea kwake ahadi kutoka kwa Baba ya Roho Mtakatifu na kumwagwa kwa matukio ya miujiza siku hiyo (mst.33).
    b. Kadhalika, Petro aliyevuviwa alithibitisha kwamba alimhubiri Kristo kwa ushahidi mwingi sana:
    (1) Miujiza Yesu aliyoitenda, na hiyo iliyofanywa na Petro pamoja na mitume wengine siku hiyo iliyotajwa mst. 4-22.

(2) Unabii wa pekee uliobainisha kuhusu Kristo, alioutimiza Yesu kabisa, ukijumuisha na Zaburi 16:8-11 pamoja na 110:1 kama ilivyotabiriwa katika mst.25-35.
(3) Uchanganuzi kimantiki, kama ulivyoonyeshwa kwamba unabii haukumhusu Daudi kama inavyoonekana katika mst. 29,34.
(4) Na ushahidi wa mitume kumi na mbili walioona ni ukweli usiopingika (mst.32).

c. Tukitafakari hayo yote, hakuna shaka Petro alijua kwamba Israeli ingetambua hatimisho hilo la hoja yake pasipo shaka kabisa!
d. Basi, ni dhahiri ndiyo sababu wasikilizaji wengi walisadiki pasipo shaka.
e. Ndiyo sababu watu wengi hata leo wanasadiki kwa ushahidi mwingi juu ya Bwana na Mwokozi, Yesu Kristo!

5. Hatimisho sahihi kabisa ya hoja za Mungu ilimhusu Yesu huyo huyo aliyesulibishwa na Wayahudi.
6. Kinagaubaga zaidi, Baba alimfufua Yesu toka ufuni na kumweka mkono wake wa kuume, basi kumfanya Yesu kuwa "Bwana" na "Kristo." Hayo ni maneno mawili muhimu sana!
   a. "Bwana" – κυριοσ.
      (1) Neno linaonyesha mwenye nguvu, cheo na mamlaka makubwa; aliye juu ya wengine wote; mmiliki; na mwalimu ambaye anatumikiwa kwa kila hali.
      (2) Basi, Baba amemfanya Yesu kiongozi mkuu; aliye juu ya wote; na ambaye anatumikiwa kuzingatia kifo chake, ufufuo, na kupandishwa kwake juu.
      (3) Linga. Flp.2:8-11.
   b. "Kristo" – χριστοσ.
      (1) Neno hili linamaanisha mpakwa mafuta, neno ambalo mara nyingi linahusisha wafalme.
      (2) Katika Agano Jipya, lilitumika kumrejea Masihi, Mfalme ambaye Wayahudi walimtarajia kuwa mwokozi wa taifa lao.
      (3) Basi, Baba alimfanya Yesu kuwa Masihi, Mwokozi, aliye juu ya wafalme wote.
   c. Tunapounganisha pamoja maneno Bwana na Kristo na maana ya maneno hayo, matokeo yake ni makubwa sana!
      (1) Baba alimfanya Yesu kuwa Bwana (k.m. mwalimu "master" mwenye nguvu, cheo, na mamlaka makubwa).
      (2) Tena, alimfanya Yesu kuwa Kristo (k.m. Masihi, Mwokozi, na mkuu kuliko wafalme wote)!
      (3) Matokeo yake, Baba alikuwa akisema kuwa Yesu ni Mungu, ni mmoja katika Uungu, Mtakatifu, ndiye Mtawala ambaye sisi tunapaswa kumtii!
      (4) Hakika, yeye ni Bwana wa mabwana na mfalme wa wafalme (Ufu.17:14)!
   d. Basi, wasikilizaji walikuwa na hatia ya kumsulibisha Yesu, yeye ambaye Baba alimfufua ili atawale kama Bwana na Kristo juu ya wanadamu.
   e. Unafikiri wasikilizaji walijisikia nini kutokana na ukweli huo mioyoni mwao kwa kadiri walivyoruhusu maneno haya yenye uvuvio kupenye akilini mwao.
   f. Tutajifunza nini kilifuata baada ya maneno haya yenye uvuvio sehemu inayofuatana ya sura hii.
7. Kabla ya kufanya hivyo, tafadhali tulia kidogo ili kuyatendea kazi mambo ya mstari huu wenye mvuto mkubwa.
   a. Waza "mimi" kuhusu unachomaanisha ninaposema, "Yesu ni Bwana wangu na Kristo wangu."?
   b. Je, umetafakari unamaanisha nini unapotamka hivyo?
   c. Je, tusingekuwa wote Wakristo bora kama tungefikia mara kwa mara kuhusu "Yesu ni Bwana wangu na Kristo wangu?"
8. Pia, kabla ya kutoa mhutasari wa sehemu hii, tafadhali angalia matumizi makubwa Petro anatumia unabii wa Agano la Kale na hatimisho sahihi lililotokana na unabii huo.
   a. Petro alionyesha kwa uvuvio wa Mungu kwamba:
      (1) 2:29-32 Yesu alikuwa ni Kristo ambaye alitimiza unabii katika Zab.16:8-11.

(2) 2:33-36 Yesu alikuwa ni Kristo aliyetimiza unabii katika Zab.110:1.

b. Tafadhali chunguza hatimisho kadhaa ambazo zimetokana na unabii na utimilifu wake:

(1) Kwa kuwa ilitabiriwa kuwa Kristo angefufuka na kuketi katika kiti cha enzi cha Daudi (2:30,31),
Na kwa kuwa Yesu Kristo alifufuka na kuketi mkono wa kuume wa Mungu mbinguni ili kutimiliza unabii huo.
Kwa hiyo, kiti cha enzi cha Daudi kipo mkono wa kuume wa Mungu mbinguni, wala si mahali popote duniani!
Katika kuhatimisha basi, Yesu alifufuka toka ufuni karne ya kwanza kutawala mbinguni kama Kristo, Mfalme (2:29-33; Efe.1"19-23).

(2) Kwa kuwa Yesu ambaye ndiye Kristo anatawala mbinguni atakuwepo hadi madui wake wote washindwe (2:34,35).
Na kwa kuwa adui wa mwisho ni mauti (1 Kor.15:26),
Kwa hiyo, Yesu atatawala kama Mfalme mbinguni hadi mauti itakaposhindwa hapo mwisho, atakapokuja mara ya pili (1 Kor.15:23-26).

c. Tutajifunza zaidi hatimisho hili tutakapojadili kwa ufupi somo juu ya utawala wa miaka elfu (premillennialism) mwishoni mwa sura hii.

9. Muhtasari wa 2:33-36, *Yesu*: aliinuliwa na kuketishwa katika kiti cha enzi.

a. Mst.33 Petro alitoa hoja za nguvu tatu kuhusu Yesu.

(1) Kwanza, aliinuliwa na kuketi mkono wa kuume wa Mungu mbinguni.
(2) Pili, Yesu alipokea ahadi ya Roho Mtakatifu kutoka kwa Baba.
(3) Tatu, Yesu alimwaga matukio ya miujiza yaliyotokea siku ya Pentekoste.

b. Mst.34 Petro alinukuu Zaburi 110:1, Zaburi ya Kimasihi, kama ilivyotimizwa na Yesu.

(1) Katika Zaburi hiyo, Baba alimwambia Masihi kutawala mahali pa nguvu na mamlaka mkono wa kuume wake mbinguni.
(2) Na Masihi angetawala mbinguni hata maadui zake wote washindwe.
(3) Kwa hiyo, kama Kristo, Yesu alikuwa atawale kama Mfalme mbinguni karne ya kwanza na ataendelea kufanya hivyo hadi maadui zake wote washindwe, adui wa mwisho ni mauti.

c. Mst.36 Petro kwa uhakika alihatimisha hoja za Mungu kwa kueleza kuwa Baba amemfanya Yesu kuwa Bwana na Kristo.

(1) "Bwana" ikionyesha kuwa Yesu ni mwalimu (master) ambaye ana nguvu, cheo, na mamlaka yote.
(2) Na "Kristo" likionyesha Yesu ni Masihi, Mwokozi, na mfalme mkuu juu ya wafalme wote.

10. Mtazamo kwa ufupi wa sura 2, Ahadi imetekelezwa na kanisa kuanzishwa.

a. 2:1-13 mitume walijazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine.

b. 2:14-36 Roho Mtakatifu (kupitia kwa Petro) alithibitishia makutano makosa, haki, na hukumu.

(1) 2:14-21 Tafsiri iliyovuviwa ya matukio haya.
(2) 2:22-24 *Yesu*: Alidhihirishwa na Mungu; aliuawa na Wayahudi; akafufuliwa na Baba.
(3) 2: 25-32 *Yesu*: uthibitisho kutoka katika unabii.
(4) 2:33-36 *Yesu*: Aliyepandishwa na kuketishwa kitini pa enzi.

**c. (2:37-47) BAADHI YAO WALIVYOPOKEA KATIKA UMATI / MASHARTI YENYE UVUVIO YA JINSI YA KUPOKEA MSAMAHA**.

**2:37)**

1. Hapa tunaona jinsi wengine walivyopokea katika wasikilizaji ambao walikuwa na mioyo adilifu na safi.
2. Angalia kwa makini jinsi wasikilizaji walivyopokea ni baada ya "waliposikia", k.m. maneno yaliyonenwa na Petro.

3. Hakika watu hawa waliamini maneno yaliyovuviwa aliyonena Petro kuhusu Yesu. Kumbuka, Petro aliwaeleza wasikilizaji:
   a. Walikuwa na hatia ya kumsulibisha Yesu, Masihi.
   b. Baba aligeuza hukumu yao ya kifo isiyohaki kwa kumfufua Yesu toka ufuni.
   c. Wala si tu Yesu alikuwa hai, bali alikuwa akitawala kama Bwana na Kristo mkono wa kuume wa Baba.
4. Maneno hayo yaliyovuviwa "yalichoma mioyo yao" wasikilizaji hao!
   a. "kuchomwa" – κατενυγησαν – umiza au penyeza ndani kwa kitu chenye incha kali; kuumiza sana; kuumia kwa huzuni nyingi ama maumivu na uchungu mwingi.
   b. Petro aliwachoma mioyo kwa kutumia upanga wa Roho, neno la Mungu, ambalo ni kali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili (linga. Efe.6:17; Ebr.4:12).
   c. Na kwa upanga huo mkali, aliwashawishi na mioyoni mwao kuleta huzuni kubwa, maumizu makali sana, kuwa na majuto haswa kwa ajili ya dhambi zao.
5. Kama matokeo ya dhambi zao, walimwuliza Petro na mitume wengine swali la miaka yote.
   a. Waliuliza ni jambo gani walipaswa kufanya.
   b. Swali linaonyesha walitambua kuwa walikuwa na hatia ya dhambi.
   c. Na inaonyesha walitaka kujua nini cha kufanya kupokea msamaha wa dhambi zao.
   d. Kwa maneno mengine, waliuliza, "Tufanye nini ili tuokoke kutoka katika dhambi zetu?" (Linga. Mdo.16:30)!
6. Sasa, ebu na tutoe kwa mhutasari masharti ya hao waliouliza swali hili muhimu siku hiyo.
   a. Walikuwa na hatia ya dhambi.
   b. Waliamini waneno yaliyovuviwa aliyohubiri Petro kuhusu Yesu Kristo.
   c. Na walipata huzuni kubwa na uchungu mwingi mioyoni mwao kutokana na dhambi zao.
7. Kabla ya kuacha mstari huu, ni muhimu kwamba tunatoa jambo moja la msingi lililofunuliwa hapa.
   a. Jambo hilo ni swali la jinsi gani Roho Mtakatifu anafanya kazi akilini mwa watu katika kuwashawishi kufanya jambo lolote.
      (1) Swala hili hufundishwa maeneo mengi ulimwenguni katika dini leo kwamba Roho Mtakatifu hufanya kazi akilini mwa watu, pasipo kutumia chombo au ujumbe wowote.
      (2) Mara nyingi hili hutajwa na watu wakidai Roho Mtakatifu amewaongoza kufanya, au kusema haya na yale.
      (3) Inamaanisha kuwa, na kwa kawaida, Roho Mtakatifu amemwongoza mtu huyu kwa kufanya kazi moja kwa moja akilini mwao.
      (4) Tabia hii pia imeonekana katika imani kwamba mtu amepotea jumla haiwezekani kwa mtu huyo kuwa na imani hata Roho Mtakatifu atakapofanya kazi moja kwa moja akilini mwake.
   b. Katika kujifunza swali hii, ni lazima tuchanganue bayana maana ya jambo hili.
      (1) Swala si kwamba Roho Mtakatifu anaongoza, au kusababisha imani ndani ya watu.
      (2) Bali, swala ni kwamba jinsi gani Roho Mtakatifu anaongoza, anaelekeza, na kusababisha imani ndani ya watu!
   c. Bila shaka Roho Mtakatifu anafanya mambo yafuatayo:
      (1) Anawalinda na kuongoza watu (linga. Rum.8:14; Gal.5:18). Hakika aliwaongoza watu waende kwa Kristo katika sura hii.
      (2) Anasababisha imani ndani ya watu. Tena, alifanya hivyo katika tukio hili.
   d. Swala ni kwamba, jinsi gani Roho Mtakatifu anafanya mambo haya?
   e. Tunaamini hapa na mazingira mengine katika kitabu cha Matendo jibu lililovuviwa ambalo litatatua tatizo.
   f. Ili kuona kwa nini tunaamini hivi, tafadhali angalia mambo yafuatayo:
      (1) Math.28:18-20; Mk.16:15,16.
      (2) Yoh.16:13; 17:17.
      (3) Mdo.2:1-4.

(4) Katika siku hiyo, lilikuwa jambo la wazi Roho Mtakatifu akifanya kazi kimiujiza. Kwa mfano:
  (a) 2:1-11.
  (b) 2:16-21, 25-32, 33-36.
  (c) 2:22-36.
(5) Basi, hapana shaka Roho Mtakatifu alikuwepo siku hiyo na kwamba alifanya kazi kimiujiza.
(6) Lakini swala hili ni: jinsi gani Roho Mtakatifu anaongoza, kuelekeza, na kuumba imani kwa hao waliouliza swali, "Tutendeje"?
(7) Njia bora kutambua jinsi gani Roho Mtakatifu alivyofanya kazi ni kuchanganua kwa makini ulinganifu wa matukio ya siku ile.
  (a) Tunapofanya hivyo, inadhihirika wazi Roho Mtakatifu alitenda kazi waliziona na kusikia siku hiyo 2:2-13:
    1. Mst. 2.
    2. Mst. 3
    3. Mst. 4-13.
  (b) Lakini angalia jinsi makutano walivyopokea ishara hizo za miujiza:
    1. Mst. 6-12.
    2. Mst. 12.
    3. Mst. 13.
  (c) Kwa nyongeza katika mambo waliofanya makutano, tafadhali angalia walichoshindwa kufanya katika mistari 2-13:
    1. Wanaonyesha kuwa hawakuamini katika Yesu kama Kristo.
    2. Hawakuonyesha ishara yoyote kwamba walikuwa na hatia au kujutia dhambi zao.
    3. Na wala hawakuuliza cha kufanya ili waokoke kutoka katika dhambi zao.
  (d) Tunaona hapa, ingawa Roho Mtakatifu alidhihirika na kusikika bayana katika mistari 2-13, wasikilizaji walishindwa kuonyesha imani, majuto kwa dhambi zao, na kutambua kwamba walitakiwa waokolewe.
  (e) Lakini katika mst.14 Petro akasimama pamoja na mitume wengine na kuwaonya wasikilizaji kutilia manani maneno ambayo alikuwa ayanene, kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu.
  (f) Kisha Petro, kwa uwezo wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu alianza kuhubiri injili kama Yesu alivyomwamuru, akijumuisha yafuatayo:
    1. Mst.15-21 Petro alitoa ujumbe ili kufafanua maana iliyovuviwa ya matukio hayo kama utimilifu wa unabii wa Yoeli.
    2. Katika mst.22-24 Petro alitoa ujumbe kufundisha kwamba Yesu alidhihirishwa na Mungu, aliuawa na Israeli, na kufuliwa na Baba.
    3. Katika mst.25-32 Petro alitumia maneno kufundisha kwamba Yesu alitimiza unabii kuhusu Kristo.
    4. Katika mst.33-36 Petro alitumia ujumbe kuonyesha kwamba Yesu aliinuliwa na kuketishwa kitini pa enzi na Baba, kama ilivyotabiriwa.
    5. Mst.38 aliweza kutumia maneno kubainisha cha kufanya ili wapate msamaha.
    6. Mst.39 alitumia maneno kuwaeleza kuhusu ahadi.
    7. Mst.40 alitumia maneno kuwahamashisha ili waweze kujiokoa wenyewe.
    8. Na mst. 41 waliolipokea neno kwa furaha walibatizwa.
  (g) Katika mst.37 baada ya wengine "kusikia" maneno hayo waliyapokea kwa furaha ujumbe huo wa injili.
    1. Hakika waliamini ujumbe huo.
    2. Walichomwa mioyo yao wakiwa na huzuni mioyoni mwao kwa sababu ya dhambi zao.
    3. Na wakauliza cha kufanya ili wapate kuokolewa.

(h) Basi, kati ya mst.14 na mst.36, Roho Mtakatifu kupitia Petro:
    1. Aliwashawishi kubadilika akilini mwao.
    2. Aliwaongoza waende kwa Yesu ambaye ndiye Kristo.
    3. Na akaumba imani mioyoni mwao.

(i) Tena, kama tulivyoona, Roho Mtakatifu alifanya hivyo kupitia neno la Mungu ambalo Yesu alimtuma kumwongoza Petro na mitume wengine:
    1. Basi, ingawa miujiza iliyoonekana wazi ilitendeka karne ya kwanza, Roho Mtakatifu hakufanya kazi moja kwa moja na kwa njia ya kimiujiza katika mioyo ya watu hao.
    2. Ni kweli kwamba alikuwa na uwezo wa kufanya miujiza moja kwa moja mioyoni mwa watu lakini hakuamua kufanya hivyo.
    3. Kinyume chake, alitumia mjumbe (Petro) na chombo chake (neno la Mungu) kuongoza na kuumba imani ndani ya watu hao.
    4. Ndiyo sababu Roho Mtakatifu ameiitwa Roho wa Kweli – kwa sababu alifunua ukweli, ulio neno Mungu (Yoh.16:13; 17:17).
    5. Na Yesu alimtuma kuwaongoza mitume (na watu wengine waliovuviwa) katika neno lote la Mungu karne ya kwanza (Yoh.16:13).
    6. Roho Mtakatifu alikamilisha ufunuo wa neno la Mungu karne ya kwanza na Mungu akakataza kuongeza chochote katika hilo (Gal.1:6-9).
    7. Kwa hiyo, leo, Roho Mtakatifu hatumii wajumbe wanadamu kufunua zaidi maandiko yake kama alivyofanya katika karne ya kwanza.
    8. Hata hivyo, bado tuna chombo chake, neno la Mungu lililovuviwa kulitumia kwa kusudi la kuongoza, kuelekeza, na kuumba imani akilini mwa watu.
    9. Hivyo neno la Mungu ni chombo cha Roho Mtakatifu kuongoza, kuelekeza, na kuumba imani imedhihirika hivyo na ukweli kwamba neno la Mungu ni "upanga wa Roho" (Efe.6:17).
    10. Na Wakristo wanapaswa kuuchukua upanga huo wa Roho na kuutumia kama moja ya silaha ya Mungu (Efe.6:10-17)!

(j) Njia zingine tunazojua neno la Mungu kuwa ni chombo cha Roho Mtakatifu huonekana kwa namna watu walivyoitikia kwa hiari zao kabisa. Ukweli huu pia ulikuwa dhahiri kipindi cha miujiza cha karne ya kwanza.
    1. Roho Mtakatifu hakuwashurutisha watu kupokea ujumbe moja kwa moja (directly) akilini mwao kwa namna ambayo wasingeweza kupinga.
    2. Badala yake, maneno yalinenwa kwa watu "wote" (mst.14); kwa "nyumba yote ya Israeli" (mst.36); na kwa "kila mmoja" wao (mst.38).
    3. Lakini ni hakika kwao tu waliohiari kuchagua "kulipokea kwa furaha" neno hilo la Mungu (mst.41)!
    4. Tena, kama tulivyoona katika mafungu mengine ya kitabu cha Matendo, wengine walichagua kinyume chake, kukufuru, kupinga, na kulikana neno la Mungu, wakijihukumu wenyewe kuwa "hawakustahili uzima wa milele" (13:45,46)!

(k) Ukweli kwamba Roho Mtakatifu anatumia neno la Mungu kama kifaa chake leo kuongoza, kuelekeza, na kuumba  imani ndani ya watu imedhihirika pia katika mafungu yafuatayo:
    1. Ni neno, injili ambayo ilihubiriwa na kusikiwa ambayo ingeumba imani (Rum.10:8-17).
        a. Ukweli ni kwamba, neno limeandikwa ili kwamba tuamini (Yoh.20:30,31).
        b. Na wengine watachangua kuamini neno, wakati wengine wataamua kutoliamini (Rum.10:16).
    2. Kadhalika, ni neno la Mungu huleta matokeo ndani ya mioyo ya watu wanaochagua kuamini (1 Thes.2:13).

3. Ni neno la kweli la injili ambalo linafanya kazi mioyoni hata kuzaa matunda ya Roho (Kol.1:5,6; Gal.5:22,23).
4. Ni neno ambalo hutuangazia wakati tunasafiri katika maisha (Zab.19:8; 119:105, 130). Kwa hiyo, hatupaswi "kuangaziwa" na Roho Mtakatifu kwa njia zingine za siri na za kimiujiza kuelewa neno.
5. Ni neno linalotiwa mioyoni mwetu na tunaliruhusu kukaa mioyoni mwetu, ambalo hututia nguvu na kutujenga (Zab.119:11; 1 Yoh.2:14; Mdo.20:32).
6. Ni neno linatupa uzima tukilitii kwa uaminifu na kupenda (Yoh.6:63; 1 Pet.1:23; Flp.2:16).
7. Ni neno lenye nguvu ya kutosha kuokoa roho zetu ikiwa tutalipanda akilini mwetu, kusimama katika hilo, kushikamana nalo kwa thabiti (Rum.1:16; Yak.1:21; 1 Kor.5:1,2).
8. Ndiyo sababu Bwana anatueleza kuwa makini sana na tunachosikia (Mk.4:24; Lk.8:18).
9. Na anaonya kwa ukali, "Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa" (kwa kifaa chake, neno) (Ufu.2:29).
10. Ndiyo maana tunaonywa kuwa tusimhuzunishe Roho Mtakatifu (kwa kukataa kifaa chake, neno) (Efe.4:30)!
11. Na ndiyo maana tunatakiwa kuwa makini tusijaribu kumpinga Roho Mtakatifu (kwa kukataa kifaa chake, neno) (Mdo.7:51).

(l) Hata hivyo, ukweli wa kwamba Roho Mtakatifu anatumia neno la Mungu kama kifaa chake kuongoza, kuelekeza, na kuumba imani katika watu kinyume na madai ya kuongoza moja kwa moja (directly) mioyoni pengine imekuwa dhahiri zaidi katika kitabu cha Matendo kuliko mahali pengine katika Biblia.
1. Tutapata fursa zingine kadhaa kuhakiki ukweli huu kwa kiina kadri tunavyojifunza kitabu hiki muhimu.

**2:38)**

1. Huyu ni Petro na majibu yake yaliyovuviwa juu ya swali, "Tutendeje?" (mst.37).
   a. Katika kujifunza mstari huu, tutachambua zaidi juu ya Petro alichosema hapa.
   b. Kisha tutajifunza mambo kadhaa kwa kiina.
2. Kumbuka kutoka 2:37 hali ya kiroho ya hao waliouliza swali hili:
   a. Walitambua kuwa wana hatia ya dhambi.
   b. Waliamini maneno yaliyovuviwa ambayo Petro alihubiri kuhusu Yesu kuwa ni Kristo.
   c. Walihuzunika na machungu mengi mioyoni mwao kwa sababu ya dhambi zao.
   d. Na walitaka kujua cha kufanya ili wapokee msamaha wa dhambi zao.
3. Basi, wakiwa akilini mwao na hali hiyo kiroho, majibu ya Petro yana masharti kadhaa ya kiroho ambayo wenye imani wenye kujutia dhambi zao lazima wafanye ili kupata msamaha wa dhambi zao.
4. Angalia Petro anatoa masharti mawili ambayo ni lazima wenye imani hawa kujutia makosa yao ya nyuma. Walipaswa kutubu na kisha kubatizwa.
5. U kweli kwamba toba na ubatizo vimeungana pamoja na kiunganishi "na" inatujulisha kwamba masharti yote mawili lazima yatendwe ili kupokea matokeo Mungu ameyaahidi.
6. Hivyo basi, masharti yote mawili, toba na ubatizo, yana uzito sawa ili kupata matokea yaliyokusudiwa.
7. Matokeo yaliyoahidiwa na Mungu kwa wenye imani na kujuta makosa wanaopenda kutubu na hubatizwa ili kupata msamaha au ondoleo la dhambi.
8. Kadhalika, wale wanaotenda masharti haya yaliyovuviwa wangepokea pia kipawa (gift) cha Roho Mtakatifu.
9. Kwa mtazamo mpana wa mstari huu akilini, ebu na tujadili mambo kadhaa kwa maelezo zaidi.

10. Kwanza kabisa, Petro alisema kwa uvuvio kwamba sharti la kwanza kwa wenye imani waliojutia makosa walipaswa kufanya ili kupata msamaha wa dhambi ilikuwa ni kutubu.
   a. Kumbuka, watu hawa walikuwa tayari wamechomwa mioyo yao na ujumbe wa injili, k.m. walikuwa na huzuni kubwa na maumivu makali mioyoni mwao kwa sababu ya dhambi zao.
   b. Hili linabanisha kwamba toba si kusikitikia dhambi kama inavyofundisha katika ulimwengu wa dini siku hizi!
   c. Watu hawa walijutia sana dhambi zao na Petro alitambua hilo kutokana na swali lao.
   d. Lakini hata hivyo, Petro aliwaeleza walihitajika kutubu, ikiwa ni nyongeza ya kujutia dhambi zao.
   e. Sasa toba ni nini?
      (1) Njia mojawapo ya kujua maana ya toba ni kutoa maelezo ya neno ambalo limetafsiriwa "tubuni" katika mstari huu (μετανοησατε).
         (a) Kuzingatia wasomi wa Kiyunani kama vile Vine, Thayer, Arndt, na Gingrich, neno kama lilivyotumika katika Biblia linamaanisha mtu kubadili akili, ikilenga kimsingi haswa juu ya dhambi.
         (b) Hivyo basi, kufutia maana ya neno Kibiblia, kutubu maana yake ni kubadili akili juu ya maswala ya dhambi.
      (2) Njia nyingine za kutambua kutubu kuna maanisha nini ni kujifunza mafungu kadhaa ya ufunguo ambamo neno au wazo linapatikana.
         (a) 2 Kor.7:9,10.
         (b) Mdo.26:18-20; 1 Thes.1:9.
         (c) Math.3:7,8.
      (3) Tunapojumuisha maelezo hayo yote, toba Kibiblia linaweza kutafsiriwa kama ifuatavyo:
         (a) Toba ni badiliko la akili.
         (b) Badiliko hili la akili hutendeka kutokana na kupondeka, kuwa na huzuni juu ya dhambi za nyuma.
         (c) Kwa nyongeza, badiliko hili la akili hupelekea kubadili tabia, ikiwa ni pamoja na kukaa mbali na dhambi kisha kumtumikia Mungu aliye hai.
   f. Mistari mingine inayoonyesha kuwa toba ni muhimu kwa wokovu toka dhambini ni Lk.13:3,5.
11. Pili, Petro alisema kwa uvuvio kwamba wenye huzuni hawa walioamini walipaswa kutubu na kubatizwa ili kupata ondoleo la dhambi zao.
   a. Mstari huu daima unathibitisha kwamba ili mtu kwanza apate msamaha wa dhambi, kila mtu mwenye akili lazima abatizwe.
   b. Basi, ubatizo ni muhimu kwa wokovu, kinyume na jinsi ulimwengu unavyofundisha katika dini za siku hizi.
   c. Mistari mingine inayoonyesha kwamba ni muhimu kubatizwa ili kupata wokovu toka dhambini ni pamoja na ifuatayo:
      (1) Mk.16:15, 16.
      (2) Mdo.22:16.
      (3) Rum.6:3,4.
      (4) 1 Kor.12:13 pamoja na Efe.5:23.
      (5) Gal.3:27.
      (6) Col.2:12,13.
      (7) 1 Pet.3:20,21.
   d. Kadhalika, neno lililotafsiriwa "batizwa" βαπτισθητω, muundo wa βαπτιζω linamaanisha kutoswa, kuzamishwa au kudidimizwa
      (1) Basi, ubatizo ambao Mungu anaamuru ni wa kuzamisha majini, si kumwagiwa au kunyunyiziwa maji kama unavyofanywa na watu wa dini siku hizi.

(2) Ukweli kwamba ubatizo wa kimaandiko ni kuzamishwa majini imedhihirishwa bayana katika maandiko yafuatayo:
   (a) Matendo 8:35-39.
   (b) Warumi 6:3,4 (linga. Kol.2:12).
(3) Jambo lingine la kufurahisha kwamba ubatizo wa kimaandiko ni kuzamishwa majini unatokana na watafiti wa mambo ya kale (archaeology).
   (a) "Archaeology" ni elimu ya sayansi ya maisha na utamaduni wa watu wa kale kwa kuchimba miji na vitu vya kihistoria.
   (b) Mfano bora wa ugunduzi wa mambo ya kale (archaeological discoveries) umethibitisha ukweli kwamba ubatizo kimaandiko ni wa kuzamishwa majini umeonekana katika nukuu kwa video.
      1. Wakati uchambuzi wa kiina wa elimu ya mambo ya kale ni nje na kozi hii, tumejumuisha nakala ya makala hii mwishoni mwa notisi hizi (Appenix C).
      2. Kwa nyongeza, ingawa hatuna muda wa kutosha kuchanganua zaidi haya mambo yaliyopatikana, mambo yafuatayo na nukuu zinavutia:
         a. Katika kitabu cha Matendo, Luka anataja nchi 32, miji 54, visiwa 9 vya Mediterania, na watu 95 (62 ambao hawajatajwa mahali popote katika Agano Jipya).
         b. Sir William Ramsey alianza kwa kujaribu kuthibitisha makosa katika kitabu cha Matendo kwa uchunguzi wake binafsi. Baada ya utafiti wake, alisema, Luka, "alipaswa kuwa miongoni mwa wanahistoria bora sana."
         c. Mtafiti maarufu (archaeologist), Dr. Nelson Gleuck alisema: (ANGALIA VIDEO – kozi hii kwa Kiingereza).
(4) Kwa ufupi basi, Mungu anaamuru ubatizo wa kuzamishwa majini. Tumeona hivyo kutokana na yafuatayo:
   (a) Kutokana na maana ya neno la Kiyunani.
   (b) Kutokana na mifano ya Agano Jipya kama vile Matendo 8:35-39.
   (c) Kutokana na maelekezo yaliyovuviwa juu ya ubatizo ukiwa ni maziko.
   (d) Na kutokana na ushahidi wa vitu vilivyopatikana vya mambo ya kale (archaeological).
(5) Kwa kuwa Mungu anaamuru ubatizo wa kuzamishwa majini, ubatizo mwingine wowote, kama vile kummwagia maji mtu au kumnyunyizia ni dhambi.
   (a) Kunyunyiza na kummwagia maji mtu havilingani kabisa na kumzamisha mtu majini.
   (b) Basi ni dhahiri, kubatiza kwa kunyunyiza au kumwagia ni kukataa namna ile ya ubatizo ambao Mungu anaamuru
   (c) Kufanya hivi ni kutokumtii Mungu, kuvunja maneno ya Mungu, na hivyo ni dhambi (1 Yoh.3:4).

d. Tungali bado katika somo la ubatizo, lazima tujadili ubatizo wa watoto wadogo.
(1) Jambo hili ni muhimu kwa sababu kubatiza watoto kumeenea ulimwengu kote katika ulimwengu wa madhehebu.
(2) Katika notisi za kozi hii, tumeambanisha orodha kubwa ya ukweli wa maandiko juu ya somo hili.
(3) Wakati hatuna muda wa kutosha kujadili ukweli huo kwa maelezo zaidi, inadhihirisha wazi kwamba watoto wachanga hawastahili kubatizwa kimaandiko kwa sababu zifuatazo:
   (a) Hakuna mfano hata mmoja wa ubatizo wa watoto katika Agano Jipya.
   (b) Hakuna sababu za kuwabatiza watoto kwa kuwa hawana dhambi (Mt.18:1-3).
   (c) Mtoto hawezi kutekeleza masharti ambayo ni lazima yafanywe kabla ya mtu kubatizwa kimaandiko, k.m. kusikia, imani, toba, na kukiri.
(4) Kwa kuwa ubatizo wa watoto ni dhambi ya kuongeza katika neno la Mungu, tunawasihi kwa upendo wote wanaotenda kuacha kufanya hivyo (Ufu.22:18,19)!

(5) Ikiwa unapenda kujifunza somo hili zaidi, tafadhali angalia notisi zilizoandikwa kwa ajili ya mstari huu.

e. Tafadhali angalia watu siku ya Pentekoste walikuwa na uwezo kufanya yafuatayo kabla ya kustahili kubatizwa kimaandiko:
   (1) Walisikia injili kuhusu Yesu, Kristo (2:22-36).
   (2) Waliamini ujumbe wa injili (kuzingatia swali mst. 37).
   (3) Hakika, kwa furaha walipokea injili (mst.41).
   (4) Walichomwa mioyoni mwao na injili (ikidhihirisha imani na huzuni kubwa kwa dhambi zao) (mst.37).
   (5) Waliamuriwa kutubu dhambi zao za kale (mst.37).
   (6) Kwa hiyo, tunaweza kuhatimisha kutokana na mfano mmoja huu ili mtu astahili ubatizo wa kimaandiko, mtu huyo sharti awe na uwezo wa kusikia, kuamini, na kuipokea injili kwa furaha, kadhalika kuitikia ujumbe unaookoa akiwa na huzuni na toba.
   (7) Zaidi sana, mfano huu katika kitabu cha Matendo sio pekee.
   (8) Kujifunza mafungu mengine ambapo ubatizo umetajwa hufunua matendo yafuatayo ambayo watu walikuwa na akili na uwezo wa kutenda ili wapate kubatizwa kimaandiko (linga. Mk.16:15,16; Mdo.8:12,13, 30-39; 10:44-48; 16:14, 15, 30; 18:8; 19:1-5):
      (a) Kusikia, kuelewa, na kuamini injili,
      (b) Kuuliza na kujibu maswali, kusikiliza kwa makini mambo ambayo yalinenwa na wengine, na kutii amri.
      (c) Kumwabudu Mungu, na
      (d) Kumkiri Kristo kwa kinywa.
   (9) Hatimisho sahihi kutokana na ukweli huu ni kwamba watoto hawastahili kubatizwa kufuatana na maandiko. Hatimisho hili linalingana na mambo yafuatayo:
      (a) Hakuna mfano hata mmoja wa ubatizo wa watoto katika Agano Jipya.
      (b) Hakuna haja ya kubatiza watoto kwa kuwa hawana hatia ya dhambi (Math.18:8).
      (c) Mtoto hawezi kutenda masharti ambayo mtu ni lazima atende kabla ya kubatizwa kimaandiko:
         1. Kuisikia injili (kwa jinsi ya kuweza kuamini injili) (Mdo.18:8).
         2. Kuamini injili (Mk.16:15,16).
         3. Kutubu dhambi zao za nyuma (2 Kor.7:9,10).
         4. Kumkiri Yesu kuwa ni Bwana kwa vinywa vyao (Rum.10:9,10).

12. Kwa ufupi, kufikia hapa katika somo letu mst.38, tumeona kuwa Petro aliwajibu swali lao wasikilizaji juu ya mambo waliyopaswa kutenda, kwa kuwaeleza kutubu na kubatizwa:
13. Kama swala lingine linalofuata, tunatambua kuwa Petro aliwaeleza kufanya hivyo, “katika jina la Yesu Kristo.”
   a. Haswa, Petro aliwaambia kutubu na kubatizwa katika (on) au kwa (upon) jina la Yesu Kristo.
   b. Kubatizwa katika (on) au kwa (upon) jina la Yesu Kristo inamaanisha kubatizwa kutegemea au kutumainia juu ya jina lake.
   c. Inamaanisha kuwa jina la Yesu Kristo ndilo msingi wa ubatizo.
   d. Kipindi cha Biblia, jina la mtu mara nyingi lilitumika kulenga sifa, nguvu, mamlaka, heshima, kazi, n.k.
   e. Kwa mfano mzuri, jaribu kuangalia majina yanayoambana na Yesu:
      (1) Yesu – maana yake Mwokozi (Math.1:21).
      (2) Bwana – linamaanisha mwalimu (master), Mmiliki, Kiongozi (kutambua mamlaka na nguvu zake)
      (3) Kristo – linamaanisha Mpakwa Mafuta, Mfalme.

f. Basi, kubatizwa kwa jina la Yesu Kristo inamaanisha kubatizwa kutegemea au kutumainia juu ya ukweli wa kwamba yeye ni Bwana wetu, Mwalimu (Master), Kiongozi, na Mfalme!
g. Mtu anapobatizwa sawasawa, basi, anatambua Yesu kuwa ni Mwokozi, Mwalimu, Mtawala, Mfalme wa maisha yao.

14. Tena, Petro aliwaambia wasikilizaji walitakiwa kutubu na kubatizwa kwa (upon) jina la Yesu Kristo "*ili kupata msamaha w dhambi*."
    a. Jambo hili linatubanishia kusudi la Mungu juu ya toba na ubatizo kwa waumini wenye huzuni.
    b. Kusudi ni "kwa ajili ya" (for) (KJV, NKJV) au kwa (unto) (ASV) ondoleo la dhambi au msamaha wa dhambi.
    c. Neno lililotafsiriwa mpate (for) au kwa ajili ya (unto) (εισ) likimaanisha ili kupata; kupokea, hatimaye au kusudi upokee.
        (1) Basi, kwa matumizi ya neno hili, Roho Mtakatifu kupitia Petro alikuwa akisema waumini hawa wenye huzuni (na wote tangu hapo) lazima watubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi zao za kale.
        (2) Au alisema kwa njia nyingine, "hatimaye au kusudi ili kupata" kwa muumini aliyehuzunika ambaye hutubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi.
    d. Mbali na uwazi wa lugha hii, kuna hoja mbili ambazo hutumiwa na baadhi kupinga kwamba mstari huu haufundishi kuwa ubatizo unahitajika ili mtu kupata msamaha wa dhambi.
    e. Hoja hizi mbili zimeelezwa na kuonekana kuwa ni uongo katika notisi zilizoandikwa katika kozi hii.
    f. Kama ungependa kujifunza jambo hili, tafadhali rejea katika notisi hizo.
        (1) Hoja ya kwanza kubwa ambayo wengine huitumia ni kwamba neno lililotafsiriwa "mpate" (for) linamaanisha "kwa sababu ya" (because of) au "kwa habari ya" (on account of).
            (a) Wanadai kwamba mtu angebatizwa kwa sababu dhambi zake tayari zimesamehewa *kabla* ya ubatizo.
            (b) Kwa maneno mengine, watu hawa wanasema hilo kinyume na ubatizo kuwa *kwa ajili ya* (for) ondoleo la dhambi, haswa ni kwa sababu amesamehewa dhambi *kabla* ya ubatizo.
            (c) Tafadhali chunguza kwa makini sababu zifuatazo kuona fundisho hili ni uongo:
                1. Bila hata ya kujifunza maana ya neno la Kiyunani, ni wazi kwamba mafundisho haya huharibu mazingira ya mst.37,38.
                    a. Waumini hawa wenye huzuni waliuuliza nini wangefanya ili kupokea msamaha wa dhambi (mst.37).
                    b. Majibu ya Petro yenye uvuvio kwa swali lao lilikuwa kwamba walipaswa kutubu na kubatizwa (mst.38).
                    c. Basi, kama tungo hili, "mpate ondoleo la dhambi" lisingetajwa katika mst. 38, tungejua kuwa mawili yote toba na ubatizo yanahitajika ili kupata msamaha wa dhambi.
                    d. Tungejua hivyo kwa sababu mambo hayo ndiyo masharti Petro alitoa kujibu swali lao walilouliza wafanye nini ili wapate msamaha wa dhambi.
                2. Alama ya pili ya neno lililotafsiriwa "mpate" halipaswi kutafsiriwa "kwa sababu ya" hilo halijatafsiriwa katika Biblia yoyote inayotambulika.
                3. Alama ya tatu ni wingi wa kamusi nyingi za Kiyunani – Kiingereza zilizotafsiri neno "kwa ajili ya" (for), "kwa" (unto) , "ili kupata ", n.k.
                4. Kwa nyongeza, ndugu Thomas Warren alifanya uchunguzi wa neno lililotafsiriwa "for" ambapo alinukuu kutoka wataalam wa lugha ya Kiyunani ishirini.

a. Kila mmoja wa wasomi hao alithibitisha kwamba neno linamaanisha "kwa ajili (for), "ili kupata", n.k.
b. Neno linalenga kutazamia kitu fulani mbele ili kukipata, wala si kuangali nyuma kitu fulani ambacho tayari umepata.
c. Ni jambo la maana pia kutambua kwamba wengi wa watalaam hawa ni washiriki wa madhehebu yanayopinga umuhimu wa kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi!
d. Uchunguzi mkamilifu wa ndugu Warren, unajumuisha maoni mazuri ya wsomi hao yameambatanishwa mwishoni mwa notisi (appendix D) zilizoandikwa kwa Kiingereza.

5. Kuna njia nyingine ya kutambua neno lililotafsiriwa "kwa ajili ya" (for) halistahili kutafsiriwa "kwa sababu ya" ni kujifunza mafungu yanayolingana (Math.26:28).
   a. Katika fungu hili, Yesu alisema damu yake ilimwagika kwa ajili ya wengi, "kwa ondoleo la dhambi."
   b. Mafungu haya yanafanana, kama yalivyoonyeshwa hapo chini.
      (1) Mdo.2:38 – "Tubuni mkabatizwe … mpate ondoleo la dhambi."
      (2) Math.26:28 – "Damu yangu … imwagikayo … kwa ondoleo la dhambi."
   c. Kwa nyongeza kwa ulinganifu katika Kiingereza, neno lilo hilo lililotafsiriwa "mpate" (for) katika Mdo.2:38 linapatikana pia katika Math.26:28 ambapo pia limetafsiriwa "kwa" (for).
   d. Ili kulinganisha, wanaoshikilia mtazamo huo wa uongo wangepaswa kuingiza "kwa sababu ya" (because of) mahali pa "kwa ajili ya" (for) katika Math.26:28, kama vile wafanyavyo katika Mdo.2:38.
   e. Watakapofanya hivyo angalia matokeo:
      (1) Math.26:28 – "Damu yangu … iliyomwagika … kwa sababu ya ondoleo la dhambi."
      (2) Tunatambua kwamba Yesu hakumwaga damu yake kwa sababu ya ondoleo la dhambi.
      (3) Hivyo basi, hakumwaga damu kwa sababu dhambi zilikuwa tayari zimesamehewa.
      (4) Kinyume chake, alimwaga damu yake ili msamaha wa dhambi upatikane (Ebr.9:22; Efe.1:7).
      (5) Kwa hiyo, ni wazi kwamba neno lililotafsiriwa "kwa ajili ya" (for) au "kwa" halina maana "kwa sababu ya"!

(2) Jambo la pili kubwa wanalotumia watu wengine kupinga mstari huu unafundisha kwamba ubatizo unahitajika ili kupata msamaha wa dhambi unaweza kubainishwa kama ifuatavyo:
Tungo "kwa ondoleo la dhambi" haiwezi kufafanua (modify) vitenzi vyote viwili, "tubu" na "kubatizwa."
   (a) Kwa maneno mengine, watu hawa wanadai kwamba tungo "kwa ondoleo la dhambi" inalenga tu kwa toba na wala si kwa ubatizo.
   (b) Basi, wanahatimisha kuwa toba ni muhimu ili kupata msamaha wa dhambi, lakini ubatizo hautakiwi ili kupata msamaha.
   (c) Kuna sababu kadhaa kwa nini madai haya ni uongo:
      1. Kwanza, kama tulivyojifunza mapema, mtazamo huo huharibu mazingira ya mst.37,38 ambapo Petro alijibu swali lao la nini walichopaswa kufanya ili kupata msamaha wa dhambi kwa kuwaeleza mambo mawili yote yakiwa muhimu toba na ubatizo.

2. Sababu ya pili kwa nini madai haya ni uongo ni kwamba yanavuruga mafungu mengine kadhaa ya maandiko ambamo Mungu anasema kwamba mtu ni lazima abatizwe ili kupokea msamaha wa dhambi:
    a. Mk.16:16.
    b. Mdo.22:16
    c. Rum.6:3,4.
    d. Kol.2:12,13.
    e. Gal.3:26,27.
    f. 1 Pet.3:20,21.
3. Sababu ya tatu kwa nini dai hilo ni uongo ushahidi ni mwingi wa wasomi wa Kiyunani.
    a. Kwa mfano, katika rejea ya awali, ndugu Warren aliorodhesha nukuu kutoka kwa watalaam kumi na sita wa Kiyunani.
    b. Kila mmoja wa watu hawa walieleza kuwa siyo tu inawezekana kwamba tungo "kwa ondoleo la dhambi" hufafanua (modify) vitenzi vyote viwili "tubu" na "kubatizwa", lakini ni dhahiri kwamba hufafanua vitenzi vyote viwili!
    c. Tena, zaidi ya hawa wote walikuwa washiriki wa madhehebu ambayo yanapinga umuhimu wa ubatizo kwa ajili ya kupokea msamaha wa dhambi.

(3) Basi, tumejifunza hoja mbili ambazo wengine wanazitumia kupinga kuwa mstari huu unafundisha umuhimu wa kubatizwa ili kupokea msamaha wa dhambi.
- (a) Na tumetambua kuwa hoja zote mbili ni za uongo!
- (b) Kwa hiyo, tunahatimisha wazi Mungu anafundisha katika mstari huu kuwa aliyeamini mwenye huzuni sharti atubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi.

15. Kwa ufupi, katika kujifunza kwetu mst.38, tumeona Petro akijibu kama ifuatavyo swali, "Yatupasa kufanya nini?"
    a. Aliwaamuru watubu.
    b. Aliwaamuru kubatizwa.
    c. Alisema kwamba ilipaswa kufanyika hivyo kwa kutengemea jina la Yesu Kristo.
    d. Na, alisema kuwa kusudi la kutubu na kubatizwa ni kupata msamaha wa dhambi.
16. Kama swala letu linalofuata, angalia Petro alivyoahidi kuwa walioamini wenye huzuni ambao walitubu na walibatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi wangepokea, "kipawa cha Roho Mtakatifu."
    a. Tungo hili, "kipawa cha Roho Mtakatifu", imekuwa somo kubwa la mjadala kati ya ndugu kwa miaka mingi.
    b. Uchunguzi mwingi unahitajika kwa sababu ya tofauti kadhaa, hatimisho zenye kuleta maana kubainisha fungu.
    c. Ingawa ndugu wamefikia hatimisho zinazotofautiana kuhusu maana haswa ya kipawa cha Roho Mtakatifu, wamefanya mijadala katika somo hili kwa upendo na amani.
    d. Kadhalika, ni lengo letu kuingia somo hili tukiwa na tabia ya namna hiyo.
17. Kabla ya kuanza maelezo mengi ya uchambuzi wa kipawa cha Roho Mtakatifu, tunataka kutoa mambo mawili ya utangulizi.
    a. Kwanza, kwa sababu ya matatizo na hatimisho mbalimbali zilizofikiwa, tutatoa kwa ufupi hatimisho hizo.
        - (1) Tunasikitika kuwa hivi ndivyo itakavyokuwa, lakini hakuna muda wa kujifunza kila hatimisho kikamilifu.
        - (2) Kwa hao wenye kupenda kujifunza baadhi ya hatimisho hizo kwa kiina, notisi za ziada zimeambatanishwa mwishoni mwa kozi hii (kozi ya kiingereza).

b. Pili, kabla ya kusonga mbele, ni muhimu sana kuelewa kwamba Mungu anabainisha bayana kuwa karama za miujiza za Roho Mtakatifu zilikoma kipindi Agano Jipya lilipokamilika karibia mwishoni mwa karne ya kwanza.
    (1) Tuliona ukweli huo katika somo kwa nini Yesu alimtuma Roho Mtakatifu na uweza wa miujiza kwa mitume wake na watu wengine waliovuviwa karne ya kwanza.
        (a) Yoh.16:13.
        (b) Waebrania 2:3,4.
    (2) Kwa nguvu hizo alizotoa Mungu, watu hawa walifunua katika karne ya kwanza:
        (a) 2 Pet.1:3.
        (b) Yuda 3.
        (c) Yak.1:25.
        (d) Gal.1:6-9; Ufu.22:18,19.
    (3) Maandiko haya na mengine yanatueleza kwamba neno la Mungu *lilifunuliwa* na *kuthibitishwa* karne ya kwanza.
    (4) Basi, kusudi la Mungu kuleta karama za miujiza lilitimia.
    (5) Ni jambo la mantiki kabisa kwamba litakapotia kusudi la Mungu, karama za miujiza kadhalika zingekoma pia.
    (6) Si kwamba ni mantiki tu, bali ndivyo haswa Mungu alivyopanga, kama tulivyojifunza hapo nyuma 1 Kor.13:8-10!
    (7) Na kwa kuwa Mungu alipendelea kuziondoa karama za rohoni za Roho Mtakatifu karne ya kwanza, karama hizo za miujiza hazipo leo!
    (8) Kwa hiyo, bila kujali "kipawa cha Roho Mtakatifu" kilichopo katika mstari huu, tunajua hakijumuilishi uwezo wa kutenda miujiza siku hizi!
    (9) Kwa nyongeza, Roho Mtakatifu haongozi wala kushawishi sisi leo ama kufanya chochote kwa namna ya siri (mysterious), ushawishi wa moja kwa moja akilini mwetu.
    (10) Kinyume chake, kama tulivyoona katika somo letu mst.37, Roho Mtakatifu anaongoza tu na kuelekeza akili za watu kwa kutumia chombo chake, neno la Mungu.
    (11) Tukikubaliana katika mambo haya yanayofundishwa wazi wazi katika maandiko, hatuamini maoni tofauti tofauti juu ya kipawa cha Roho Mtakatifu hata kuwa sababu ya kutoshirikiana baina ya ndugu.

18. Ukiwa na maelezo hayo ya msingi akilini mwako, ebu na tujadili kipawa cha Roho Mtakatifu.
19. Kuzingatia sarufi (grammar) ya Kiyunani, tungo, "kipawa cha Roho Mtakatifu" inaweza kumaanisha mambo mawili yote:
    a. Karama zilitolewa na Roho Mtakatifu,
    b. Au, Roho Mtakatifu mwenyewe kuwa kipawa.
    c. Mazingira, ama ya karibu au mbali, ni sharti kujifunza ili kugundua ni nini kati ya hayo mawili Mungu alikusudia katika mstari huu.
    d. Tutajifunza mazingira hayo zaidi hapo baadaye.
20. Lakini, kabla ya kujifunza mazingira, tunaona tunalazimika kuorodheshwa hatimisho kadhaa ambazo ndugu hufikia juu ya kipawa cha Roho Mtakatifu.
21. Kwanza, ndugu wanaoamini kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu ni kipawa kilichotolewa na Roho Mtakatifu huleta hoja mbalimbali kuwa ni kipawa cha jinsi gani hicho.
22. Hoja hizo ni pamoja na zifuatazo:
    a. Wengine hudhani kuwa kipawa hicho ni baraka za kiroho, ikiwa ni pamoja na wokovu na uzima wa milele.
    b. Wengine huamini kuwa karama ilikuwa nguvu za miujiza kwa kuwekewa mkono na mitume karne ya kwanza.
    c. Na wengine hufikiri kipawa ni neno la Mungu, lililofunuliwa na Roho Mtakatifu karne ya kwanza.

23. Ingawa tunawastahi kweli wanaofikia hatimisho hizo, lakini siamini kuwa ni hatimisho sahihi, ukizingatia ushahidi wa Kibiblia uliopo.
    a. Kama tulivyoeleza awali, hatuna muda wa kujifunza kwa nini hatimisho hizo si sahihi.
    b. Hata hivyo, ninyi mlio na notisi zilizoandikwa kwa kozi hii mtaona maelezo zaidi mwishoni mwa notisi hizi (katika kozi ya Kiingereza).
    c. Pia, utaona maelezo ya nyongeza juu ya somo hili katika maelezo ya mwisho wa notisi hizi (Appendix E).
24. Ebu kwa ufupi tuchanganue hatimisho hizi, moja baada ya nyingine.
    a. Kwanza, je kipawa cha Roho Mtakatifu ni baraka za rohoni, ikiwa ni pamoja na wokovu na uzima wa milele?
        (1) Hatusadiki kuwa hivyo!
        (2) Kama tulivyoona katika somo letu mst.38, Petro aliwapatia amri waumini hao waliohuzunika zenye masharti katika kujibu swali lao.
        (3) Alisema kuwa wakitubu na kubatizwa, wangepata msamaha wa dhambi zao.
        (4) Neno "na" (and) katikati ya maneno "tubuni" na "mkabatizwe" yanatueleza kuwa kuna masharti mawili tofauti.
        (5) Masharti haya mawili ni toba na kubatizwa kwa jina la Yesu Kristo.
        (6) Basi, msamaha wao ulitengemea kutekeleza kwao masharti ya Mungu ya toba na ubatizo.
        (7) Baada ya kuonyesha kuwa msamaha wa dhambi ungetokana na kutii amri hizo zenye masharti, Petro aliongeza nyingine "na" kabla ya kutoa ahadi ya kipawa cha Roho Mtakatifu.
        (8) Kwa maneno mengine, Petro alikuwa anasema kuwa watakaotubu na kubatizwa wangepokea kitu kingine cha nyongeza katika msamaha wa dhambi.
        (9) Aliwaahidi wangepokea kipawa cha Roho Mtakatifu katika msamaha.
        (10) Kwa hiyo tunahatimisha kipawa cha Roho Mtakatifu ni mbali, na ni nyongeza katika msamaha wa dhambi.
        (11) Zaidi sana, haionekani kuwa kipawa (gift) cha Roho Mtakatifu si uzima wa milele.
            (a) Kama tulivyoona, Petro aliahidi karama ya Roho Mtakatifu kwa hao waliotubu na kubatizwa kupata msamaha wa dhambi.
            (b) Kama kipawa cha Roho Mtakatifu ilikuwa uzima wa milele,
            (c) Basi, maana yake, Petro aliahidi uzima wa milele kwa kila mmoja anayetubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi.
            (d) Lakini tunajua kuwa ni zaidi ya toba, ubatizo na msamaha wa kwanza ili mtu kupata uzima wa milele.
            (e) Kwa mfano, ili kupata uzima wa milele, mtu anapaswa:
                1. Kudumu kuenenda katika nuru ya neno la Mungu ili kuzidi kupokea msamaha wa dhambi (1 Yoh.1:7).
                2. Vumilia hadi mwisho (Math.10:22).
                3. Kubakia mwaminifu hata kifo kikikufika (Ufu.2:10).
            (f) Kwa hiyo, tunahatimisha kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu si uzima wa milele!
            (g) Jambo hili linaweza kufupishwa kama ifuatayo:
                1. Petro aliahidi Roho Mtakatifu kwao waliotubu na kubatizwa kwa ajili ya msamaha wa dhambi.
                2. Lakini, ili kupata uzima wa milele, ni zaidi ya toba na ubatizo ili kupata msamaha wa dhambi.
                3. Kwa hiyo, kipawa cha Roho Mtakatifu si uzima wa milele!
    b. Pili, je kipawa cha Roho Mtakatifu kilikuwa uwezo wa miujiza uliopatikana kwa kuwekewa mikono ya mitume karne ya kwanza?

(1) Kwa heshima na upendo wote kwao wanaoamini maoni haya, hatuamini kipawa cha Roho Mtakatifu kinahusu uwezo wa miujiza katika mstari huu, ama iwe kwa wakati ule au sasa.

(2) Kuna sababu nyingi kwa nini ninaamini kipawa cha Roho Mtakatifu katika mstari huu hakina maana uwezo wa miujiza.

(a) Kwanza, tafadhali chunguza ukweli ufuatayo:

1. Kama maoni haya ni kweli, kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu kinalenga uwezo wa miujiza kwa kuwekewa mikono ya mitume, basi kulikuwa na watu 3,000 waliopokea siku ya Pentekoste uwezo wa kutenda miujiza (2:41).
2. Kufikia wakati 4:4 walikuwa 5,000 wanaume waliokuwa na uwezo wa miujiza.
3. Katika 5:14 tunajifunza kwamba makutano walizidishwa katika kundi.
4. Na katika 6:17 tunaona kuwa idadi ya wanafunzi ilizidi kuwa wengi sana!
5. Basi, kulingana na mawazo haya, kulikuwa na waumini waliotubu maelfu ambao walizamishwa majini ili kupata msamaha wa dhambi ambao wangeweza kutenda miujiza kwa kuwa mitume waliwawekea mikono juu yao ili kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu.
6. Kama haya ni kweli, tungetarajia kuona taarifa za kutenda miujiza angalau kwa baadhi yao Wakristo hao.
7. Hata hivyo, tunapojifunza kwa makini sura za kwanza tano za kitabu cha Matendo, hakuna hata taarifa kama hiyo kutaja miujiza ikitendwa na yeyote isipokuwa mitume wa Kristo!
8. Tafadhali chunguza mafungu yafuatayo kama uthibitisho wa ukweli kwamba taarifa pekee tulizonazo za mtu yeyote kutenda miujiza ni za mitume wa Kristo tu mwanzoni.
   a. 2:43 – Ajabu nyingi na ishara zikafanywa na *mitume*.
   b. 3:1-11; 4:13-16 – Petro na Yohana walimponya kiwete kwa namna ambayo hakuna mtu yeyote angepinga.
   c. 4:33 – Kwa nguvu nyingi mitume wakatoa ushuhuda mwingi wa kufufuka kwake Yesu.
   d. 5:12 – Na kwa mikono ya mitume zikafanyika ishara na maajabu mengi katika watu.
9. Kufikia hapa, ebu tupitie tuliyojifunza kuhusu maoni juu ya kipawa cha Roho Mtakatifu.
   a. Mtazamo wa kwamba ahadi iliyoahidiwa ya kipawa cha Roho Mtakatifu ilikuwa ni uwezo wa miujiza kwa kuwekewa mikono ya mitume.
   b. Kulingana na maoni hayo, kungelikuwa na maelfu ya Wakristo mbali na mitume ambao wangekuwa wakitenda miujiza.
   c. Lakini, kulingana na maandiko yaliyovuviwa kwa sura tano za awali za Matendo, hapakuwa na maelfu wakitenda miujiza isipokuwa mitume.
   d. Ukweli ni kwamba, taarifa tulizonazo tu ni mitume wa Kristo ndio pekee waliokuwa wakifanya miujiza.
   e. Kwa hiyo, kwa kuwa mtazamo huu unapingwa moja kwa moja kwa ushahidi mwingi wa sura tano ya kwanza za Matendo, tunahatimisha kuwa mtazamo huo ni uongo!
10. Hatimisho hili linatiwa nguvu tunapokwenda hatua moja zaidi na kujifunza Matendo 6:5 (angalia hatimisho katika 11c chini).
11. Kwa kuhatimisha basi, alama ya kwanza kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu katika Mdo.2:38 si uwezo wa miujiza ushahidi ni mwingi wa sura sita za kwanza za Matendo ambamo tumeona yafuatayo:

a. Hapakuwa na Wakristo maelfu waliokuwa wakifanya miujiza kama matokeo ya kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu baada ya kutubu na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao.
b. Badala yake, kila rejeo (reference) kwa miujiza na uwezo wa kimiujiza katika sura hizi inarejea kwa mitume pekee wa Kristo.
c. Kabla ya mitume kuweka mikono yao juu ya Stefano, Filipo, na wengine katika sura 6, watu walitajwa kuwa wenye kujaa imani na Roho Mtakatifu" (6:3,5).
   (1) "Wenye kujaa Roho Mtakatifu" hakika haina maana kuwa waliweza kutenda miujiza, kwa sababu mitume tu ndio walikuwa wakifanya kufikia hapa.
   (2) Hivyo basi, tungo hii hakika inaonekana kumaanisha ukweli kwamba Roho Mtakatifu alikaa ndani yao bila kufanya au njia yoyote ile miujiza.
   (3) Kwa hakika, walipokea "kipawa cha Roho Mtakatifu" walichoahidiwa na Petro kama matokea ya imani yao, toba, na ubatizo kwa ondoleo la dhambi.
   (4) Lakini hawakuwa na uwezo kutenda miujiza, hata ingawa Roho Mtakatifu alikaa ndani yao.

(b) Kwa alama ya pili kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu si uwezo wa miujiza waliopata kwa kuwekewa mikono ya mitume, tafadhali tafakari maelezo yafuatayo.
1. Kama tulivyojifunza nyuma, kanisa likaongezeka katika idadi na kuenea kijiografia kwa haraka.
2. Ukweli ni kwamba, mateso yalipoibuka, watu wote isipokuwa mitume walitawanyika kutoka Yerusalem na kwenda kila mahali wakihubiri neno (8:4).
3. Kwa mfano, walikwenda Samaria (8), Kaisaria (10), Antiokia, Foinike, na Kipro (11), na maeneo mengine mengi (13-21).
4. Kadri walivyokwenda maeneo haya wakihubiri neno, wengi waliamini, walitubu, wakabatizwa, na kupokea msamaha wa dhambi.
5. Waliotii injili kwa namna hii pia walipokea kipawa cha Roho Mtakatifu.
6. Lakini, kufuatana na mtazamo huu wa kipawa cha Roho Mtakatifu, ilikuwa jambo muhimu kwa mitume kuwawekea mikono juu yao Wakristo hawa ili kwamba wapate kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu.
7. Hivyo basi, waumini hawa wangepokea msamaha wa dhambi walipobatizwa, lakini walikuwa wasubiri hata mitume kuwajia na kuwawekea mikono juu yao ili kupokea karama za Roho Mtakatifu.
8. Je, hilo linalingana na lile ambalo Petro aliahidi katika mstari huu?
9. Zaidi sana, hata aje mtume na kuweka mikono yake juu yao, hao waliobatizwa hawakuwa na Roho ya Kristo ikikaa ndani yao, basi, hawakuwa mali yake (Rum.8:9-11).
   a. Waliingia ndani ya Kristo na kumvaa kwa njia ya ubatizo (Gal.3:27).
   b. Walinunuliwa kwa gharama ya damu ya thamani ya Kristo (1 Kor.6:19,20; 1 Pet.1:18,19).
   c. Walikuwa wamepata baraka zote za rohoni katika yeye (Efe.1:3).
   d. Walakini, hawakuwa mali yake na hawakuwa na Roho wake akikaa ndani yao hata mtume alipowajia na kuweka mikono yake juu yao.
   e. Hakika, haliwezekani hili kuwa kweli!
10. Kwa nyongeza, fikiria ni maeneo mangapi mitume wangelipaswa kwenda na jinsi gani ingewalazimu kusafiri haraka mahali ili kuweka mikono juu ya kila Mkristo ili kumpatia kipawa cha Roho Mtakatifu?

11. Unapotafakari ukweli huu, ni wazi kwamba mitume wasingeliweza kuwawekea mikono Wakristo hao wote.
12. Hili kimazingira haliwezekani, tena, ndiyo sababu ya pili inayotupelekea tusiamini kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu si nguvu za miujiza ziliyopatikana kwa kuwekewa mikono ya mitume.

(c) Sababu ya tatu kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu si uwezo wa kimiujiza kwa kuwekewa mikono na mitume, tafadhali chunguza yafuatayo.
1. Kipawa cha Roho Mtakatifu waliahidiwa waumini wote wenye huzuni ambao wangetubia dhambi na kubatizwa kwa ondoleo la dhambi zao.
2. Kwa hiyo, kulingana na maoni haya, wote waliotubu dhambi zao na kubatizwa walipaswa kupokea kipawa kwa kuwekewa mikono ya mitume.
3. Lakini, hata katika karne ya kwanza wakati karama za miujiza zilikuwepo, si Wakristo wote waliweza kutenda miujiza (1 Kor.12:29).
4. Basi, kuna tofauti baina ya mtazamo wa maoni haya ya kipawa cha Roho Mtakatifu kilichohitajika na ni nini hasa kilitendeka.
5. Kwa kadri nijuavyo, kuna maoni aina mbili kutokana na utata huu:
   a. Ama Mungu alishindwa kuwapa kipawa cha Roho Mtakatifu ambaye kwa uaminifu aliahidi kwao wenye imani, toba, na kubatizwa kwa ondoleo la dhambi zao.
   b. Au, kipawa cha Roho Mtakatifu katika mstari huu si uwezo wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu uliotajwa katika 1 Kor.12-14 na mafungu mengine.
6. Tunajua kwamba Mungu asingeshindwa kutekeleza ahadi yake!
7. Kwa hiyo, ni lazima tuhatimishe kipawa cha Roho Mtakatifu katika mstari huu si nguvu ya kutenda miujiza kwa kuwekewa mikono na mitume.

(d) Alama ya mwisho kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu si nguvu za kimiujiza zilizopokelewa kwa kuwekewa mikono ya mitume imedhihirika katika ukweli ufuatao.
1. Kulingana na 2:29, ahadi hii ya kipawa cha Roho Mtakatifu ilikuwa hata "*na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie*."
2. Lakini Mungu aliita watu na tena anaita leo watu kwa njia ya injili ya Kristo (2 Thes.2:14).
3. Kwa hiyo, ikiwa kipawa cha Roho Mtakatifu ilikuwa nguvu za miujiza, basi wote waliotii mwito wa injili wakati ule na hata leo wanaotii wapokee uwezo wa kimiujiza.
4. Kama tulivyojifunza, tunajua kwamba hakika si kweli kabisa!
5. Kwa hiyo, hii ni alama nyingine tena kwamba maoni ya kipawa cha Roho Mtakatifu kuwa ni nguvu za kimiujiza zilizopatikana kwa kuwekewa mikono na mitume si sahihi.

c. Mtazamo wa tatu juu ya kipawa cha Roho Mtakatifu katika mstari huu ni kwamba kipawa ni neno la Mungu lililofunuliwa na Roho Mtakatifu karne ya kwanza.
(1) Ndugu wema kabisa wanaoshikilia mtazamo huu wanaamini kipawa cha Roho Mtakatifu kuwa ni neno la Mungu na kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Mkristo kupitia neno la Mungu na kwa njia ya neno pekee.
(2) Hakuna shaka kwamba Roho Mtakatifu alifunua na kuthibitisha neno la Mungu kupitia mitume na watu wengine waliovuviwa karne ya kwanza (Yoh.16:13; Ebr.2:3,4).
(3) Na wala hakuna shaka kwamba Roho Mtakatifu anatumia neno la Mungu kama upanga wake kushawishi akili zetu leo (Efe.6:17) kinyume na njia zingine zozote za moja kwa moja, ushawishi wa siri (mysterious).
(4) Kwa nyongeza, hakuna shaka neno la Mungu ni zawadi bora yenye thamani kubwa (Zab.119:97, 127).
(5) Lakini mimi binafsi nina mashaka makubwa kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu katika mstari huu ni neno la Mungu.

(6) Mashaka hayo yanasimamia uchunguzi wangu wa kiina wa mazingira ya mstari huu kuhusu kipawa cha Roho Mtakatifu kuwa ni neno la Mungu.
(7) Katika mazingira haya, tafadhali angalia watu hawa waliopokea neno la Mungu kabla ya kuzamishwa majini ili kupata ondoleo la dhambi.
    (a) 2:37 Walichomwa mioyo yao na neno la Mungu.
    (b) 2:38 Kwa neno la Mungu, Petro aliwaambia jambo la kufanya ili kupokea msamaha wa dhambi.
    (c) 2:40 Kwa neno la Mungu, Petro aliwasihi waokoke.
    (d) 2:41 Walilipokea neno la Mungu kwa furaha.
    (e) 2:41 Tena si hivyo tu, walibatizwa ili kupata ondoleo la dhambi zao.
(8) Basi, katika mazingira haya, ni dhahiri watu hawa walilipokea neno la Mungu kabla ya kubatizwa na kuingizwa katika Kristo kwa ondoleo la dhambi.
(9) Lakini katika mstari huu Petro aliwaahidi watu hawa kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu baada ya kutubu na kubatizwa kwa ondoleo la dhambi.
(10) Kwa hiyo, tunahatimisha kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu si neno la Mungu.
(11) Hoja hii inaweza kuhatimishwa kama ifuatavyo:
    (a) Kipawa cha Roho Mtakatifu kilipokelewa baada ya mtu kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi.
    (b) Ni sharti mtu alipokee neno la Mungu kabla ya kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi.
    (c) Kwa hiyo, kipawa cha Roho Mtakatifu katika mstari huu si neno la Mungu.

25. Ni imani yangu binafsi kipawa cha Roho Mtakatifu katika mstari huu ni Roho Mtakatifu mwenyewe akiwa kama zawadi.
    a. Kubainisha zaidi, kipawa cha Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu mwenyewe akikaa ndani ya Mkristo kwa njia ile ambayo hamwezeshi Mkristo kutenda miujiza au kupokea mwongozo wa moja kwa moja, kuelekeza, au ushawishi toka kwa Roho Mtakatifu.
    b. Imani hii husimamia katika kujifunza sarufi (grammar), mstari huu wenyewe, mazingira yanayozunguka mstari huu, na mazingira ya mbali ya Agano Jipya.
    c. Kuna sababu kubwa mbili kwa nini ninaamini kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu katika Mdo.2:38 ni Roho Mtakatifu mwenyewe.
        (1) Kwa kuwa hatuna muda wa kutosha kujifunza kwa kiina sababu hizi mbili kubwa, ningependa kuzitaja kwa ufupi.
            (a) Sababu ya kwanza ni matumizi ya tungo kama hilo, "kipawa cha Roho Mtakatifu" katika Mdo.10:44-47.
            (b) Pili ni mazingira ya sehemu nyingine ya Agano Jipya juu ya somo hili.
            (c) Notisi zilizochapwa kwa Kiingereza zina maelezo zaidi juu ya sababu hizi mbili.
    d. Natoa changamoto usome notisi hizo na kuchunguza maandiko kwa makini ili kutambua kama hili hatimisho ni sahihi (Mdo.17:11).
    e. Tafadhali weka akilini mwako imani yangu kuwa Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Mkristo kwa vyovyote vile hakubadili yale tuliyojifunza awali juu ya masomo mawili muhimu.
        (1) Kwanza, maandiko wazi kabisa yanafundisha kwamba karama za Roho Mtakatifu vilikoma karibia na mwishoni mwa karne ya kwanza.
            (a) Hali hii ilikuwepo wakati Agano Jipya lilipokuwa likifunuliwa na kuthibitishwa.
            (b) Kwa hiyo, hakuna karama za Roho Mtakatifu leo!
            (c) Notisi nilizozitaja hapo awali zina maelezo zaidi kuthibitisha kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu hakikuhusika na hakihusiki na uwezo wa kimiujiza.
        (2) Pili, njia pekee ambayo Roho Mtakatifu anaongoza na kutuelekeza ni kwa neno la Mungu, upanga wa Roho.
            (a) Hatuongozi, wala kutuelekeza au kutushawishi kupitia hisia kwa siri, hisia kali (hunches), sauti za usiku, ndoto, maono, au aina yoyote ile ya moja kwa moja kugusa akili zetu!

(b) Sasa, hakuna mtu yeyote anayeheshimu neno la Mungu atakayekataa kwamba Mungu hufanya kazi kwa majaliwa (providence), k.m. katika kuhakiki watoto wake waaminifu wanapata mahitaji yao wanayohitaji ili kuishi (Math.6:33; Flp.4:19).
(c) Na hakuna mtu atakayekataa kwamba Mungu anatawala ufalme wa wanadamu (Dan.4:17, 25, 32).
(d) Hata hivyo, katika mambo haya yote, Mungu angali anaachilia uhuru wetu wa kuamua. Tunaweza kuchagua tunachotaka, kusema, na kutenda (Yosh.24:15; Ufu.22:17).
(e) Basi, wala si Baba wala Roho Mtakatifu anayeshawishi moja kwa moja au kutia nguvu akili zetu, kutuongoza kwa namna fulani ya moja kwa moja.
(f) Badala yake, anaongoza, anaelekeza, na kutushawishi kwa njia ya chombo chake, neno lililovuviwa la Mungu.

26. Kwa mawazo ya utangulizi haya na kuwa na tahadhari akilini, tafadhali fikiria sababu mbili za msingi za kuamini kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu kilichotajwa katika mstari huu ni Roho Mtakatifu akikaa ndani ya Mkristo kwa namna ambayo si ya kimiujiza.
   a. Sababu ya kwanza ni matumizi ya tungo, "kipawa cha Roho Mtakatifu" katika Mdo.10:44-47.
      (1) Kama tulivyojifunza awali, kuzingatia sarufi (grammar), tungo hii inaweza kumaanisha moja ya hayo mambo mawili:
         (a) Pengine humaanisha kitu fulani ambacho Roho Mtakatifu anatoa.
         (b) Au, pengine humaanisha Roho Mtakatifu mwenyewe kama zawadi.
      (2) Watalaam wa lugha wanatueleza kuwa maana halisi hutegemea mazingira.
      (3) Kuna kiashiria kidogo katika Mdo.2:38 ambazo zinaonyesha kati ya maana hizi mbili ni ipi iliyo sahihi ambayo Mungu alikusudia katika mstari huu.
      (4) Walakini, tungo kama hiyo, "kipawa cha Roho Mtakatifu" imepatikana pia katika Mdo.10:45.
      (5) Basi, kujifunza mazingira (10:44-47) ni muhimu sana katika kutusaidia kutambua maana ya kipawa cha Roho Mtakatifu.
         (a) Mst.44 Roho Mtakatifu aliwashukia waliosikia neno.
         (b) Mst.45 hurejea hapa kama kipawa cha Roho Mtakatifu.
         (c) Mst. 47 Petro kwa uvuvio aliwaambia waliopokea kipawa hiki ni Roho Mtakatifu mwenyewe.
         (d) Kulingana na mazingira haya hivyo, ni wazi kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu mwenyewe kama kipawa.
            1. Roho Mtakatifu aliwashukia juu yao (mst.44).
            2. Roho Mtakatifu waliyempokea (mst.47).
      (6) Sasa, ebu na tutoe muhtasari na kuhatimisha kulingana na jinsi tulivyoona katika mazingira haya.
         (a) Tungo, "kipawa cha Roho Mtakatifu" inapatikana katika Mdo.10:44-47.
         (b) Katika mazingira hayo, kipawa cha Roho Mtakatifu kilikuwa Roho Mtakatifu mwenyewe kama zawadi.
         (c) Mahali pengine pekee ambapo pana tungo kama hilo ni katika Mdo.2:38.
         (d) Basi, inawezekana kabisa kipawa cha Roho Mtakatifu kilichoahidiwa katika Mdo.2:38 ni Roho Mtakatifu kama zawadi.
         (e) Msimamo huo utakuwa na nguvu zaidi kama tunapata msaada kwa mtazamo huu katika mazingira ya mstari huu.
      (7) Kabla ya kuondoka 10:44-47, ni muhimu kuangalia tofauti moja kubwa baina ya mazingira haya na 2:38.
         (a) Katika Mdo.10, ni wazi kwamba Kornelio na watu wa nyumbani mwake walipokea uwezo wa kimiujiza au udhihirisho wa Roho Mtakatifu.

1. Mst.46 – Walipopata Roho Mtakatifu, Mungu aliwapatia uwezo wa kimiujiza wa kunena kwa lugha zingine ambazo hawakuwahi kujifunza.
2. Walakini, Mungu alibainisha wazi kwamba kupokea kwao uwezo wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu ilikuwa kwa kusudi maalum la kipekee.
3. 11:17,18 – Kusudi hilo la kipekee ni Mungu kuonyesha kuwakubali Mataifa kupata wokovu kwa njia ya kutii injili, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi asilia.

(b) Walakini, maandiko yanafundisha wazi kwamba inawezekana kwa Roho Mtakatifu kukaa ndani ya mtu bila ya kumwezesha mtu huyo kutenda miujiza.
   1. Lk.1:15 – Yohana Mbatizaji alijaa Roho Mtakatifu toka tomboni mwa mamaye.
   2. Yoh.10:41 – Walakini Yohana hakutenda miujiza ya aina yoyote kwa uwezo wa Roho Mtaktifu.

(c) Basi, si jambo la kushangaza kama kipawa cha Roho Mtakatifu katika Mdo.2 ni ahadi ya Roho Mtakatifu kukaa ndani ya Wakristo kwa njia ya kutokutenda miujiza au kwa kujidhihirisha.

(d) Ukweli ni kwamba, kuna njia kadhaa ambazo tunaweza kuona kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu katika Mdo.2:38 hakihusishi wala hakilengi uwezo wa kutenda miujiza.
   1. Kwanza, Mungu aliahidi kwamba wote watakaotubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi watapokea kipawa cha Roho Mtakatifu (2:38).
      a. Basi, kama kipawa cha Roho Mtakatifu kinahusu nguvu za kutenda miujiza, wote waliotubu na kubatizwa wangekuwa na uwezo wa kutenda miujiza.
      b. Lakini, kila mtu aliyetubu na kubatizwa hakupata nguvu za kutenda miujiza, hata karne ya kwanza ambapo miujiza ilitendeka kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (1 Kor.12:29,30).
      c. Kwa hiyo, kipawa cha Roho Mtakatifu si Roho Mtakatifu kukaa ndani ya mtu kwa namna ya kumwezesha kutenda miujiza.
   2. Pili, ahadi ya kipawa cha Roho Mtakatifu kwa ajili ya wote Bwana atakaowaita (2:39).
      a. Hivyo, kama kipawa cha Roho Mtakatifu kinahusu uwezo wa kutenda miujiza, wote aliowaita Bwana wangekuwa na uwezo wa kutenda miujiza.
      b. Mungu aliwaita watu wakati huo na anaita sasa kwa njia ya injili ya Kristo (2 Thes.2:14).
      c. Lakini, wote wenye kutii wito wa injili hawapati nguvu za kutenda miujiza (1 Kor.12:29,30).
      d. Kwa hiyo, kipawa cha Roho Mtakatifu si Roho Mtakatifu akikaa ndani ya mtu kwa njia ya kumwezesha kutenda miujiza.
   3. Na tatu, wote waliopata kipawa cha Roho Mtakatifu kwa kipimo cha miujiza katika Matendo 10 walidhihirisha uwezo wa miujiza mara moja kwa kunena kwa lugha ambayo hawakujifunza kabla.
      a. Kwa ulinganifu makini, waliopokea kipawa cha Roho Mtakatifu katika Mdo.2 hawakudhihirisha uwezo kama huo wa kimiujiza.
      b. Kusema kweli, taarifa pekee tulizonazo zinaonyesha mitume pekee wa Kristo wakifanya miujiza kipindi chote cha sura tano za kwanza za Matendo (linga. 2:43; 3:1-11; 4:13-16; 4:33; 5:12).
      c. Habari za kwanza mtu kutenda miujiza mbali na mitume ni Stefano (6:8).
      d. Lakini hili lilitendeka kwa sababu mitume wa Kristo walimwekea mikono juu yake kumwezesha kutenda miujiza, wala si kwa sababu kipawa cha Roho Mtakatifu kilimwezesha kutenda miujiza (6:6; 8:17-19).

e. Kwa hiyo, maelfu ya watu walitubu, walibatizwa, na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu kwa kipindi kinachochukua sura 2-5.
f. Walakini, hakuna hata mmoja wao aliyeweza kutenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
g. Hatimisho pekee sahihi ambalo tunaweza kufikia ni kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu hakihusishi uwezo wa kimiujiza, hata kipindi cha miujiza karne ya kwanza!

(8) Kukamilisha somo letu katika tungo hili, "kipawa cha Roho Mtakatifu" katika Mdo.10:44-47, tunafikia hatimisho lifuatalo.
(a) Kipawa cha RohoMtakatifu ni Roho Mtakatifu mwenyewe kama zawadi.
(b) Kornelio na watu wa nyumbani mwake walipokea Roho Mtakatifu kwa kiwango cha miujiza katika tukio hili pekee kuonyesha Mungu kuwakubali watu wa Mataifa ili kupata wokovu.
(c) Walakini, mazingira ya Matendo 2 yanabainisha kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu katika Mdo.2:38 hakikuhusisha wala hakihusishi uwezo wa kimiujiza.
(d) Kinyume chake, ilikuwa ahadi kwa kila mwuumini mwenye huzuni ambaye:
1. Angeitika wito wa Mungu uliotolewa katika injili (mst.39).
2. Angetii injili ukijumulisha kutubu na kubabatizwa kwa ondoleo la dhambi (2:38).
(e) Si kila mtu aliyetekeleza masharti hayo karne ya kwanza angeweza kutenda miujiza.
(f) Zaidi sana, hakuna mtu leo atakayetekeleza masharti hayo atatenda miujiza.
(g) Basi, kipawa cha Roho Mtakatifu kilichoahidiwa na Petro kwa watu ambao watatekeleza masharti hayo ni Roho Mtakatifu akikaa ndani ya Mkristo bila uwezo wa kutenda miujiza.

b. Sababu ya pili ya kuamini kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu kilichoahidiwa katika Matendo 2:38 ni Roho Mtakatifu mwenyewe akikaa ndani ya Mkristo kwa njia isiyo ya kutenda miujiza ni ushahidi wa sehemu zingine za Agano Jipya (mazingira).
(1) Ikiwa mtazamo huu wa kipawa cha Roho Mtakatifu ni kweli, basi italingana na madai katika sehemu zingine za Agano Jipya.
(2) Ikiwa mtazamo huu ni uongo, itapingana na jinsi sehemu zingine za Agano Jipya zinavyodai.
(3) Ukiwa na ukweli huo akilini, ebu tufanye uchunguzi ya jinsi sehemu zingine za Agano Jipya zinavyosema.
(a) Yoh.7:39 – Yohana alithibitisha kuwa Yesu aliahidi Roho Mtakatifu kwa hao waliomwamini. Roho Mtakatifu asingetolewa hata Yesu atakapotukuzwa.
(b) Mdo.2:38 pamoja na Mdo.3:19 – Angalia ulinganifu:

| <u>MATENDO 2:38</u> | <u>MATENDO 3:19</u> |
|---|---|
| Tubuni ……………………………… | Tubuni |
| Mkabatizwe ………………………… | Mrejee (be converted) |
| Ondoleo la dhambi …………………. | Ili dhambi zenu zifutwe |
| Kipawa cha Roho Mtakatifu ……….. | zipate kuja nyakati za kuburudika kwa kuwapo kwake Bwana |

Kwa hiyo, kulingana na mistari hii inayofanana, tunaweza kwa uhakika kuhatimisha kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu ni kuwepo kwake Bwana kwa Mkristo mwaminifu.
(c) Mdo.2:38 na Mdo5:32 – Angalia ulinganifu:

| <u>MATENDO 2:38</u> | <u>MATENDO 5:32</u> |
|---|---|
| Kipawa cha Roho Mtakatifu ……………… kwa hao: | Roho Mtakatifu walipewa hao: |

Wenye kutubu na kubatizwa ……………… Wamtiio Bwana

Kwa hiyo, kutokana na mistari hii miwili, tunaweza kuhatimisha kisahihi kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu mwenyewe aliyetolewa kwa kila mtu mwenye kumtii Bwana, ikiwa ni pamoja na kutubu na kubatizwa.

(d) Rum.8:9,11 –

Roho wa Mungu anakaa ndani yenu.
Ikiwa mtu hana Roho wa Kristo, huyo sio wake.
Roho hukaa ndani yenu.
Roho wake anakaa ndani yenu.

(e) 1 Kor.6:19 – Mwili wa Mkristo ni hekalu la Roho Mtakatifu.

Hekalu – ναοσ – mahali halisi akaapo Mungu.

(f) Gal.3:26,27 pamoja na 4:6 –

Wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo.
Kubatizwa kuingia katika (into) Kristo, mmemvaa Kristo.
Kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wake mioyoni mwenu.

(4) Sasa, ebu tukamilishe na kuhatimisha kwa usahihi kutokana na somo letu la mafungu haya;
   (a) Kipawa cha Roho Mtakatifu kilichoahidiwa kwa mwuumini mwenye huzuni anayetubu na kubatizwa ili kupata ondoleo la dhambi (2:38).
   (b) Kipawa cha Roho Mtakatifu ni sawa na kurejea zije nyakati za kuburudika kwa kuwepo kwake Bwana ambaye wameahidiwa watakaotubu na kuondolewa dhambi zao hata zipate kufutwa (2:38 na 3:19).
   (c) Roho Mtakatifu wameahidiwa hao watakaomtii Mungu (5:32). Angalia ulinganifu huu wa kushangaza:
      1. Kipawa cha Roho Mtakatifu waliahidiwa hao ambao wanamtii Mungu (kwa kuamini, kutubu, na kubatizwa ili kupata msamaha) (2:38).
      2. Roho Mtakatifu wamepewa hao wenye kumtii Mungu (5:32).
      3. Basi, kipawa cha Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu mwenyewe, Mungu alimpatia mtu alipotii injili na kupata msamaha wa dhamba!
   (d) Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Mkristo (Rum.8:9-11).
   (e) Mwili wa Mkristo ni hekalu la Roho Mtakatifu (mahali halisi pa kukaa), ambaye yuko ndani ya Mkristo (1 Kor.6:19).
   (f) Mtu anapofanyika kuwa mwana wa Mungu kwa njia ya imani na ubatizo, Mungu humtuma Roho Mtakatifu kuingia ndani ya moyo wa mtu huyo (Gal.3:26,27; 4:6).
   (g) Tunaamini kwamba maandiko haya yanaweka bayana kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu mwenyewe akikaa kabisa ndani ya Mkristo kwa namna ambayo hamwezeshi mtu huyo kutenda miujiza.

27. Swali la kawaida linalozuka kuhusu kipawa cha Roho Mtakatifu linaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo:
   a. "Ikiwa kukaa kwa Roho Mtakatifu ndani ya Mkristo hakumwezeshi Mkristo kutenda miujiza au kupokea mwongozo wa moja kwa moja au ushawishi, nini kusudi la kukaa kwake basi?"
   b. Swali hili ni zuri, ambalo majibu mbalimbali yamefunuliwa katika maandiko.
      (1) Kwanza, katika Efe.1:13,14.
         (a) "kutiwa muhuri" - εσφραγισθητε.
            1. Alama ya kumiliki.
            2. Basi hivyo, Roho Mtakatifu kukaa ndani ya Mkristo ni alama ya mwana wa Mungu kumilikiwa na Mungu (linga. 1 Kor.6:19,20)!

(b) “dhamana” (guarantee – NKJV), arabuni (earnest – KJV, ASV) - αρραβων.
1. Malipo ya awali (down payment), rehani, au kutoa uhakika (assurance) kwamba baraka kamili itatolewa mbeleni.
2. Baraka za mbeleni zinatajwa kama “urithi wetu” katika mst.14.
3. Basi, Roho Mtakatifu kukaa ndani ya Mkristo ni arabuni ya Mungu au uhakikisho wa urithi wa Mkristo, ambao ni uzima wa milele mbinguni (1 Pet.1:3,4).
4. Hakika, arabuni ya Mungu ya urithi huu ina masharti!
5. Wakristo watapokea urithi huo wa uzima wa milele kama watamtumikia Mungu kwa uaminifu hata kufa (Ufu.2:10)!

(2) Pili, katika 1 Kor.6:19, 20.
(3) Tatu, katika Rum.8:26,27.

28. Kuna ndugu wema, waaminifu, wenye juhudi kujifunza wanaopinga mtazamo huu wa kipawa cha Roho Mtakatifu.
    a. Ingawa hatuna muda wa kujifunza kupinga kwao, ninaamini kumechanganuliwa barabara mwishoni mwa notisi (Appendix E) katika kozi ya Kiingereza.
29. Tukitazama nyuma kila kitu tulichojifunza katika mst.38, tunaona kuwa Petro aliwaambia wauumini mwenye huzuni mambo yafuatayo:
    a. Walitakiwa kutubu na kubatizwa.
    b. Walitakiwa kufanya hivyo kwa (upon) jina la Yesu Kristo.
    c. Walitakiwa wachukua uamuzi huo ili wapate msamaha wa dhambi.
    d. Na, wangepokea kipawa cha Roho Mtakatifu.
30. Kabla ya kuondoka katika mstari huu, ninyi mliopata notisi zilizochapwa za kozi hii mtaona jedwali mwishoni wa notisi (Appendix F) ambalo linatoa picha za batizo tano katika Agano Jipya: wa Yohana, Mateso, Roho Mtakatifu, Moto, na wa Agizo Kuu.
31. Mwisho, tunataka kujifunza jedwali muhimu sana kuhusu batizo hizo mbili.
    a. Jedwali hili linatofautisha ubatizo wa maji kama amri katika mstari huu na mingine na ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao tulijifunza katika 1:5.
    b. Jifunze jedwali katika video (katika Kiingereza).

**2:39)**

1. Katika mtazamo huu Petro alibainisha wazi ahadi hii ya kipawa cha Roho Mtakatifu kilikuwa kwa watu wa aina zote watakaotekeleza masharti ya Mungu ili kupata msamaha wa dhambi.
2. Hivyo, wote wanaosikia injili, na kuiamini, kutubu dhambi zao, kumkiri Kristo, na wamebatizwa majini kwa ondoleo la dhambi hupokea kipawa cha Roho Mtakatifu, ambacho ni Roho Mtakatifu mwenyewe akikaa ndani yao pasipo kutenda miujiza.
3. Ametaja makundi yote ya watu katika makundi mbalimbali kama ifuatavyo:
    a. “ninyi” = Watu wa Israeli ambao walikuwa na hatia ya kumsulibisha Bwana (2:22,36).
    b. “watoto wenu” = uzao wa taifa hilo la Israeli.
    c. “na wote walio mbali” = Mataifa (linga. Efe.2:11-17).
    d. “na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu” = yeyote ambaye angeitika kwa kutii wito wa Mungu ulitolewa kwa wanadamu wote kwa njia ya injili ya Kristo (2 Thes.2:14).

**2:40)**

1. Petro aliwasihi wasikilizaji kwa maneno mengine mengi ili kujiokoa wenyewe.
2. Dhahiri hili linaeleweka kuwa kinyume na wanavyofundisha katika ulimwengu wa dini leo, mtu sharti afanye kitu fulani ili aokolewe (linga. Flp.2:12)!
    a. Ni kweli kabisa mtu hawezi kuokoka bila ya upendo, rehema, na neema ambazo Baba ametoa kwa kila mmoja wetu kupitia Mwanawe mpendwa (Efe.2:4,5).
    b. Hata hivyo, upendo wa Mungu, rehema, na neema haviondoi wajibu wetu wa kumtii Mwokozi ili tuokolewa (Ebr.5:8,9)!

c. Ukweli ni kwamba, lazima tuwe na imani hai, yenye kutenda kazi, na utiifu ambao unatenda kazi kwa upendo ili kuokolewa au kuhesabiwa haki (Yak.2:14-26; Gal.5:6).
d. Na, kama tulivyoona, imani hii yenye utiifu ni pamoja na ubatizo kwa ondoleo la dhambi.
e. Zaidi, tunaweza kubakia sisi wenyewe katika upendo wa Mungu ikiwa tunataraji kupokea rehema za Mungu (Yuda 21).
f. Tena, tunapaswa kujitajidi kudumu katika neema yake (Mdo.13:43).
g. Mwisho, tunapaswa kuwa waaminifu hata kufa ikiwa tunataka kupokea taji ya uzima wa milele (Ufu.2:10).

**2:41).**

1. Hakika walikuwepo miongoni mwa wasikilizaji waliofurahia maneno yenye uvuvio yaliyonenwa na Petro siku hiyo kuu.
2. Walifurahia kujifunza mambo ya kufanya ili kupata msamaha wa dhambi zao!
3. Hawakufurahi tu katika kusikia habari njema hizo, bali pia waliitikia kwa kutii kwa njia ya kubatizwa kama Petro alivyoamuru!
4. Idadi ya waliotii kutoka mioyoni mwao siku ile ni 3,000.
5. Kabla ya kuuacha mstari huu, tafadhali angalia jambo fulani muhimu:
   a. Mst.40 Petro aliwasihi "wajiokoe wenyewe"
   b. *Swali* – Walifanya nini watu hawa "kujiokoa wenyewe"?
   c. *Jibu* – Mstari huu unatueleza kwamba walibatizwa, kama Petro alivyowaamuru kufanya katika mst. 38.
   d. *Swali* – Kulingana na Mungu, je ni muhimu kubatizwa ili kuokolewa?
6. Muhtasari wa 2:37-41, Kukubali kwa baadhi katika makutano / Masharti yaliyovuviwa juu ya msamaha.
   a. Katika mst.37 baadhi ya walioamini wenye huzuni waliitikia maneno ya Petro yenye uvuvio kuhusu kusulibishwa na kupandishwa kwa Yesu kwa kuuliza nini walitakiwa kufanya ili kuokolewa toka katika dhambi zao.
   b. Katika mst.38 Petro aliwaambia kutubu na kubatizwa.
      (1) Jambo hili lilikuwa lifanyike kwa (upon) jina la Yesu Kristo.
      (2) Lilikuwa kwa kusudi la kupokea msamaha wa dhambi zao.
      (3) Na ni pamoja na ahadi ya kipawa cha Roho Mtakatifu.
   c. Katika mst.39 ahadi hiyo ilitolewa kwa ajili ya watu wote ambao wangetii wito wa injili, ukijumulisha Waisraeli, kizazi chao, na Mataifa.
   d. Katika mst.40 Petro aliwasihi wasikilizaji kujiokoa wenyewe.
   e. Na mst.41 tunajifunza kulikuwa na watu 3,000 walioyapokea maneno hayo kwa furaha na wakabatizwa wapate kuokolewa.
7. Mtazamo kwa ufupi wa sura 2, ahadi ilitimizwa na kanisa likaanzishwa.
   a. 2:1-13 Mitume walijazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine.
   b. 2:14-36 Roho Mtakatifu (kupitia Petro) alithibitishia makutano makosa, haki na hukumu.
      (1) 2:14-21 Tafsiri yenye uvuvio ya matukio haya.
      (2) 2:22-24 *Yesu*: alidhihirishwa na Mungu; akauawa na Wayahudi; akafufuliwa na Baba.
      (3) 2:25-32 *Yesu*: Uthibitisho kutokana na unabiii.
      (4) 2:33-36 *Yesu*: Aliinuliwa na kuketishwa kitini pa enzi.
   c. 2:37-41 Jinsi wengine walivyoitikia kati ya makutano / masharti yaliyovuviwa ya jinsi ya kupata msamaha.

### d. (2:42-47) KANISA LINAZIDI KUSONGA MBELE

**2:42)**

1. Kama tulivyoona katika mst.41, watu walioyapokea masharti yaliyovuviwa ya jinsi ya kupata msamaha walibatizwa ili kumtii Bwana.

2. Hata hivyo, katika mstari huu tunajifunza kwamba utiifu wao haikuishia katika maji ya ubatizo tu!
3. Wakristo wa kwanza walidumu (haswa, kuvumilia, kuendelea) katika mambo kadhaa yafuatayo:
   a. Kwanza, walidumu katika mafundisho ya mitume.
      (1) "mafundisho" – διδαχη – mafundisho, maagizo.
      (2) Hivyo, walidumu katika mafundisho ya mitume, ambayo tunayo hata siku hizi kama Agano Jipya la Kristo.
      (3) Kwa maneno mengine, Wakristo hawa wapya walidumu kuenenda katika nuru ya neno la Mungu na walitaka kuwa waangalifu wasije wakapotoka mbali na mafundisho ya Kristo (1 Yoh.1:7; 2 Yoh.9-11).
      (4) Je, tunaweza kupunguza masharti kidogo siku hizi na tubakie kumpendeza Bwana aliyetufia?
   b. Pili, walidumu katika ushirika.
      (1) Neno hili κοινωνια linaweza kutafsiriwa kwa namna mbili:
         (a) Kwanza, maana pana inalenga uhusiano baina ya watu wenye mapenzi, furaha, matakwa, matumaini, thamani ya aina moja, n.k.
            1. Ni pamoja na kusaidiana wao kwa wao, kuguswa haswa na kushirikiana katika mambo wanayopenda, furaha, matakwa, matarajio, thamani, n.k.
            2. Ni pamoja na wazo la urafiki wa karibu, jamii, umoja, kushikamana pamoja, n.k.
            3. Linga. 1 Yoh.1:3,7.
            4. Linga. Kol.2:2.
            5. Hivyo basi, Wakristo hawa wa awali waliungana, jamii iliyoshikamana pamoja ya watu walioshiriki wote katika fursa za kila mmoja na majukumu ya maisha ya Ukristo!
      (2) Maana ya pili ya neno lililotafsiriwa "ushirika" ni changizo au kutoa mali, pesa, au misaada mingine.
         (a) Mchango au kutoa huko kulitokana na kupenda kushirikiana na wengine baraka za maisha ya Ukristo.
         (b) Linga. Rum.15:26.
   c. Tatu, walidumu katika kumega mkate.
      (1) Jambo hili linarejea kukumbuka kifo cha Bwana kwa kushiriki mkate na matunda ya mzabibu kila siku ya kwanza ya juma.
      (2) Ninaamini ndiyo haswa inayolengwa kwa sababu hizi mbili:
         (a) Kwanza, mazingira ya karibu ya mstari huu.
            1. Mstari unajumuisha mambo mengine ya ibada: mafundisho ya neno la Mungu, changizo, na sala.
            2. Basi, ni mantiki pekee kwamba kumega mkate katika mstari huu kulilenga hilo ambalo ni sehemu ya ibada ya Ukristo kila siku ya kwanza ya juma (linga. 1 Kor. 11:23ff).
         (b) Pili, mazingira ya sehemu zingine za Agano Jipya.
            1. Linga. 1 Kor. 10:16.
   d. Jambo la nne ambalo Wakristo hawa wa awali walidumu nalo ni sala.
      (1) Hakika, hili ni jambo lingine kati ya matano ya ibada yaliyoamuriwa na Mungu katika Agano Jipya.
      (2) Kama tulivyoona katika somo letu mambo ya historia katika kozi hii, Wakristo wa awali walikuwa watu walioamini katika nguvu za sala!
      (3) Wazo la kulitendea kazi: ikiwa tutasali kama walivyosali, na kufanya kazi kama walivyofanya, tutafikia hatua ambayo walifikia!

    e. Hivyo kwa ufupi, katika kubainisha mambo yaliyofanywa na Wakristo wa awali hao, Bwana alitaja mambo manne kati ya matano yanayokubalika katika ibada ya Agano Jipya:
        (1) Kufundisha na kuhubiri neno la Mungu.
        (2) Kuchanga fedha kwa Bwana kwa ajili ya kazi yake.
        (3) Kukumbuka kifo cha Bwana katika kushiriki Chakula cha Bwana.
        (4) Na kusali.

**2:43)**

1. Hapa tunajifunza kwamba mitume wa Kristo walitenda miujiza mingi ("maajabu na ishara").
2. Bila shaka walitenda miujiza hiyo kwa uwezo wa Roho Mtaktifu ambaye Yesu alimwaahidi kumtuma juu yao.
3. Matokeo ya miujiza hiyo ilikuwa kuleta hofu mioyoni mwa hao walioiona na kuisikia.
4. Bila shaka wakati huo, watu walipoona na kuusikia ukweli, miujiza ya Kibiblia, walitambua kuwa hao waliotenda miujiza walifanya hivyo kwa uwezo wa Mungu Mwenyenzi.

**2:44,45)**

1. Katika mistari hii Luka alitoa picha nzuri ya ushirika uliokuwepo katika kanisa la karne ya kwanza.
2. Aliwafafanua Wakristo hao wa awali kwa namna mbalimbali:
    a. Kwanza, walikuwa "*pamoja*."
        (1) Waliungana katika nia na matendo (linga.15:6).
        (2) Inawezekana wengi wao waliishi pamoja katika makazi ya dharura au katika nyumba za Wakristo wa Yerusalem.
    b. Pili, "*na kuwa na vitu vyote shirika*."
        (1) Hawakuona mali yao kimwili kuwa ni mali zao wenyewe.
        (2) Walipenda kushirikiana mali hizo na ndugu (linga. 4:32).
    c. Na tatu, walipenda hata kuuza walichonacho na kutoa kwa kuwagawia wale waliokuwa na mahitaji.
        (1) "*mali*" (possessions) – vitu kama vile ardhi, nyumba, mashamba ya mizabibu, n.k.
        (2) "*vitu*" (goods) – pengine inarejea vitu vyao binafsi vyenye kuhamishika.
3. Wengine wanadai kwamba mistari hii miwili, pamoja na 4:32-37 na 5:1-10, inafundisha ukommunisti (communism).
4. Ninapinga kwa sababu zifuatazo, siamini kuwa ujamaa umefundishwa katika mistari hii:
    a. Kwanza kabisa, ni wazi jambo hili lilikuwa la muda mfupi ili kufikia mahitaji katika kanisa la Yerusalem.
        (1) 2:5-11 – Makutano hawa waliokwenda Yerusalem toka kila taifa chini ya mbingu kwa ajili ya sikukuu hii maalum ya Pentekoste.
        (2) 2:37-41 – Baada ya kuwasili kwao, waliongolewa katika Ukristo.
        (3) Bila shaka, jambo hili liliwafanya wakae muda mrefu Yerusalem mbali na jinsi walivyokuwa wamepanga.
        (4) Wakiwa nchi ya ugenini kwa muda mrefu zaidi ya walivyopanga, wakakabiliwa na mahitaji bila kutarajia kama vile chakula.
        (5) Mambo hayo ya kipekee, mahitaji maalum yalipelekea fursa kwa Wakristo kuonyesha upendo wao kwa kushirikiana pamoja.
        (6) Hivyo basi, badala ya kufundisha ujamaa, mistari hii inatoa mifano sahihi ya upendo usio na unafiki wa Wakristo wakishirikiana pamoja kukabili mahitaji ya dharura, maalum katika kanisa la Yerusalem.
    b. Pili, imani kwamba zoezi la kuwa na vitu vyote shirika lilikuwa la muda mfupi kukabili mahitaji ya mara moja maalum linatiwa nguvu tunapotambua kuwa hakuna kanisa nje na Yerusalem lililofanya kama hivi.

(1) Mdo.9:36 – Dorkasi alifanya kazi ya kusaidia Yopa yeye binafsi. Hili lisingewezekana ikiwa kila mmoja aliweka katika mfuko wa pamoja.
(2) Mdo.11:29 – Waliokuwa Antiokia walituma misaada yao kwa wengine, kwa kadri ya uwezo wao. Lisingewezekana hili kama kila mmoja aliweka katika mfuko wa pamoja.
(3) 1 Kor.16:2 – Wakristo Korintho (na wengine wote) waliamuriwa kutoa kwa kadri ya kufanikiwa kwao. Hivyo basi, watu binafsi walimiliki mali zao wenyewe.

c. Tatu, kufuatana na maana ya neno ukommunisti (communism), vitu vyote humilikiwa na serikali.
(1) Walakini, katika mazingira halisi haya, ni wazi kwamba Wakristo walikuwa na haki ya kumiliki vitu vyao binafsi.
(2) Linga. 2:46 – "*nyumba kwa nyumba*."
(3) Tena, mafungu mengine kati ya haya katika kitabu cha Matendo ambapo Wakristo walishirikiana vitu vyao, haki ya kumiliki mali binafsi imedhihirika wazi.
(4) Linga. Mdo.5:4.

d. Na mwisho kabisa, kulingana na maana ya ujamaa, kuna uwiano wa mgawanyo wa mapato yaliyovunwa na wote.
(1) Uwiano wa karibu kabisa, katika mst.45, ni wazi kwamba kilichofuata mauzo ya vitu vyao viligawanywa "kulingana na mahitaji ya kila mmoja"!
(2) Kwa maneno mengine, kusudi la michango hiyo ilikuwa kusaidia mahitaji ya haraka ya ndugu waliohitaji, si kuhakikisha kuwa kila mtu alikuwa na uwiano sawa (Yak.2:15,16).

5. Kwa sababu hizo nne, hatuamini kwamba ujamaa umefundishwa katika mistari hii au kwingine kokote katika maandiko.
6. Tunachokiona katika mistari hii ni aina ya upendo wa kusaidiana pasipo unafiki jambo ambalo Yesu alisema lingetambulisha wanafunzi wake.
   a. Linga. Yoh.13:34, 35.

**2:46,47)**

1. Hapa tuna mtiririko wa maelezo mazuri Luka akiwaelezea Wakristo wa kwanza.
2. Angalia mambo anayoyataja sita.

a. Kwanza, walidumu kila siku katika shughuli zao kwa ajili ya Bwana.
(1) Haswa, walivumilia na kustahimili katika shughuli hizo.
(2) Kwa nyongeza, Ukristo wao ulidhihirika kila siku na wala si katika siku ya kwanza ya juma tu.
(3) Bila shaka, waliamini barabara mafungu kama Flp.1:20,21 na Kol.3:3, 4!

b. Pili, walikuwa pamoja "*kwa moyo moja*."
(1) Ndiyo kusema, waliungana na kupatana kuwa kundi moja.
(2) Kuchunguza zaidi Agano Jipya kunaonyesha waliungana kwa sababu ya:
(a) 1 Kor.1:10.
(b) Flp.3:16.
(c) Flp.2:2.
(d) Flp.2:3.
(e) Flp.2:5.
(f) 1 Pet.4:11.

c. Tatu, walikusanyika pamoja muda uliopangwa katika hekalu.
(1) Hekalu palikuwa mahali ambapo walimwabudu Mungu na ambapo walipatumia kama kituo cha kuanzia kazi.
(2) Bila shaka, waliendelea kukutanika hapo kwa muda fulani.
(3) Ni jambo la kufurahisha kuona kuwa hawakuacha kukusanyika pamoja (Ebr.10:25).

d. Nne, waliutumia muda wakiwa pamoja, ikiwa ni pamoja na kula chakula pamoja manyumbani.

(1) Zingatia tungo, "*kumega mkate*" katika mst.46.
(2) Kuna tofauti kubwa kati ya matumizi ya tungo la maneno hili hapa na lile la mst.42.
(3) Katika mazingira haya, ni wazi kwamba inarejea kula chakula cha kawaida, mbali na kushiriki Chakula cha Bwana.
(4) Ni kweli hilo kwa sababu katika mstari uo huu, Luka *anataja "walishiriki chakula chao wenyewe*."
(5) Pia, hili ni swala walilolifanya kila siku mbali na siku ya Bwana ambayo Bwana anaamuru kushiriki Chakula cha Bwana (linga. 20:7).

e. Tano, waliyatenda mambo haya yote wakiwa na mambo mawili muhimu – "*kwa furaha* (gladness) *na weupe wa moyo* (simplicity).
  (1) "*furaha*" – αγγλλιασει.
    (a) Neno hili linamaanisha shangwe (exultation), furaha kubwa au kupendezwa mno.
    (b) Hivyo basi, watu hawa, ilikuwa furaha kubwa kuwa Mkristo na kuishi kama Mkristo!
    (c) Kinyume na kununa kwa chuki, walikuwa wanyenyekevu wenye shukrani!
    (d) Flp.4:4.
    (e) Gal.5:22,23.
  (2) "*weupe wa moyo*" (simplicity of heart – NKJV); moyo mmoja (singleness – KJV, ASV) – αφελοτητι καρδιασ.
    (a) Neno lililotafsiriwa "*weupe wa moyo*" (simplicity) au "moyo mmoja" haswa inamaanisha weupe wa moyo na uwazi usio wa kidunia.
    (b) Kwa maneno mengine, hawakuwa na mapenzi na vitu (material) vya dunia hii (I Yoh.2:15-17).
    (c) Math.6:24.
    (d) Flp.4:11-13.
    (e) Ebr.13:5,6.

f. Jambo la sita walidumu nalo ilikuwa kumsifu Mungu.
  (1) Hili ni jambo ambalo Wakristo wanapaswa daima kujitahidi kulifanya!
  (2) Linga. 1 Pet.2:9,10.
  (3) Ebr.2:12.

g. Kama matokeo ya jinsi Wakristo wa kwanza walivyoenenda, walitazamwa na kukubaliwa na watu wa Yerusalem.
  (1) Math.5:16.
  (2) Flp.2:15,16.

h. Ni kielelezo na utaratibu gani Wakristo wa kwanza walituachia ili tuige!
  (1) Sikiliza muhtasari wa maelezo ya Mungu juu yao.
    (a) Walidumu kufanya kazi kila siku kwa ajili ya Bwana.
    (b) Waliungana, kundi lililopatana pamoja.
    (c) Walikusanyika pamoja na kuabudu hekaluni.
    (d) Walifurahia kuutumia muda wao pamoja, ikiwa ni pamoja na kula chakula pamoja majumbani mwao.
    (e) Walionyesha tabia njema ajabu katika maisha yao ya kila siku.
      1. Ikiwa ni pamoja na wingi wa furaha na kupendezewa na kuishi maisha kama Wakristo.
      2. Kwa nyongeza, kinyume na kupenda vitu vya dunia vya dunia, msingi wa mapenzi yao yalikuwa kumtumikia mwalimu (master) wao, Bwana Yesu Kristo.
    (f) Walimsifu Mungu.
    (g) Na kwa sababu ya kuwa na mwenendo wa namna hiyo, walitazamwa na kukubaliwa na watu wa Yerusalem.

3. Mwishoni mwa mst.47 tunaona ukweli muhimu sana kwamba Bwana alilizidisha kanisa kila siku kwa hao waliokuwa wakiokolewa.

4. Kuna mambo kadhaa ambayo ni muhimu juu ya ukweli huu.
   a. Kwanza, tafadhali angalia Bwana anamzidisha mtu katika kanisa wakati mtu huo anapokuwa ameokoka.
      (1) Inamaanisha watu hawana mamlaka toka kwa Mungu kumzidisha mtu katika kanisa la Bwana, wala si kwa kuwapiga kura kuingia kanisani ama kwa njia nyingineyo yoyote ile.
      (2) Badala yake, mtu akishafanya masharti ya Mungu ya jinsi ya kuokoka, Bwana (siyo wanadamu) anamzidisha mtu huyo katika kanisa la Bwana.
      (3) Ndio kusema kwamba mtu hawezi kutoka nje na "kujiunga na kanisa la hiari yake" na akubaliwe na Mungu!
      (4) Tena, tukishafanya masharti ili tuokolewe, anatuzidisha katika kanisa lake, wala si katika madhehebu yaliyoundwa na wanadamu.
   b. Pili, tafadhali chunguza Bwana pekee ndiye anawazidisha katika kanisa lake wale waliokolewa kutoka katika dhambi zao.
      (1) Maana yake ni kwamba kanisa la Bwana linaundwa na hao waliokolewa toka katika dhambi zao.
      (2) Hilo linalingana na ukweli kwamba Bwana alilinunua kanisa lake kwa damu yake ya thamani yenye uwezo wa kutosha kuosha dhambi (Mdo.20:28).
      (3) Lakini, ni watu gani waliokolewa na kuzidishwa na Bwana katika kanisa lake katika sura hii?
      (4) Kama tutatambua walichofanya, tunaweza kujua mambo anayopaswa mtu kufanya ili aokolewe na kuzidishwa katika kanisa la Bwana.
      (5) Kama tulivyojifunza, waliokuwa wameokolewa na kuzidishwa katika kanisa la Bwana siku hiyo ni wale waliofanya:
         (a) Mst. 22-36.
         (b) Mst. 41.
         (c) Mst. 37
         (d) Mst.38, 47.
         (e) Katika mafungu mengine, Mungu anatueleza kwamba kabla ya watu kuweza kubatizwa kiusahihi, wanapaswa kuikiri imani yao katika Yesu kuwa ni Kristo (Mdo.8:37; Rum.10:9,10).
      (6) Hivyo basi, watu wanapotekeleza masharti haya, wameokolewa na kuzidishwa na Bwana katika kanisa lake.
5. Jambo la tatu muhimu sana kuhusu mstari huu ni kwamba ni mahali pa kwanza katika Agano Jipya ambapo kanisa limetajwa kama limekuwepo kwa wakati uliopo (present tense)!
   a. Ebu kumbuka somo letu katika 1:6-8, mahali mitume wa Yesu walipomwuliza kama angerejesha ufalme kwa Israeli mitume watakapobatizwa kwa Roho Mtakatifu.
   b. Katika somo hili, tuliona mambo kadhaa:
      (1) Isa.2:2-4 – Isaya alitabiri mwanzo wa kanisa la Bwana katika Yerusalem siku za mwisho.
         (a) Mdo.2:16, 17 – Petro alisema kwamba walikuwa katika siku za mwisho siku ya Pentekoste.
         (b) Kusema ukweli, angalia ulinganifu mkubwa kati ya Isa.2:2-4 na Matendo 2 kama ilivyoonyeshwa katika jedwali katika video (Kiingereza).
      (2) Dan.2:44.
      (3) Math.3:2
      (4) Math.4:17.
      (5) Math.16:18,19.
      (6) Mk.9:1.
      (7) Matendo 1:8.
      (8) Kutokana na maandiko haya, tunahatimisha kuwa ufalme (kanisa) ungeanzishwa wakati Roho Mtakatifu amewajia mitume wa Kristo.

c. Lakini, katika somo letu la 2:1-4, tumeona Roho Mtakatifu akiwashukia mitume wa Kristo na kuwajalia nguvu siku ya Pentekoste siku chache baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni.
d. Kwa hiyo, tungetarajia ufalme (kanisa) ambao Yesu aliahidi kuanzishwa siku hiyo.
e. Matarajio hayo yametimia tunapofika 2:47 na kuona Mungu akilitaja kanisa kama lilikuwa tayari lipo kwa wakati uliopo (present tense) kwa mara ya kwanza.
f. Basi, ufalme (kanisa) lilianzishwa karne ya kwanza, katika mji wa Yerusalem, kama vile Mungu alivyotabiri.
g. Baada ya siku hiyo, ufalme (kanisa) ulitajwa kama upo tayari.
   (1) Kol.1:13.
   (2) Ufu.1:9.
   (3) Mdo.11:15.

6. Lakini kwa nini ni muhimu sana kutambua na kuandika ufalme (kanisa) ulivyoanza?
   a. Sababu ya kwanza ni kulitambua kanisa la kweli moja la Bwana na kulitofautisha na madhehebu katika ulimwengu wa dini siku hizi.
      (1) Efe.4:4.
      (2) Hili ni jambo muhimu sana kwa sababu, kulingana na 2:47, Bwana huwazidisha hao waliokoka katika kanisa moja hilo.
      (3) Hilo moja lilianzishwa na Bwana mwenyewe siku ya Pentekoste, katika mji wa Yerusalem, kama ilivyoandikwa katika sura hii.
      (4) Makanisa mengine yote yaliyoanzishwa baada ya siku hiyo yalianzishwa na wanadamu na hayakubaliki na Mungu (Math.15:13).
   b. Sababu ya pili ni muhimu kuandika lini ufalme (kanisa) wa Bwana ulianzishwa ili kuyafunua mafundisho ya utawala wa miaka elfu (premillennialism).
7. Wakati hatuna muda wa kutosha kujifunza fundisho hilo kwa kiina, tunapaswa kulijadili kwa kifupi kwa sababu sehemu kubwa ulimwengu linasadikika katika dini siku hizi.
8. Ebu na tuanze kwa kutoa maana kwa ufupi na fafanuzi za utawala huo (premillennialism).
   a. Kwanza, neno "premillennialism" ni muungano wa mashina matatu ya maneno.
      (1) Pre – kabla.
      (2) Millennium = miaka 1,000.
      (3) Ism = fundisho, dhana, mpango.
      (4) Ukiunganisha sehemu hizo pamoja, neno hili linaweza kufafanuliwa kama fundisho linalohusu kipindi cha miaka 1,000.
      (5) Kwa ubainifu zaidi, "premillennialism" ni fundisho linalohusu kuja kwa Bwana kabla ya kipindi cha miaka 1,000.
   b. Ukiwa na maelezo haya kichwani, ningependa kufafanua baadhi ya mambo muhimu kuhusiana na fundisho hili.
      (1) Linafundishwa na hao wanaoamini fundisho kuwa Yesu alikuja mara ya kwanza kuanzisha ufalme wake.
      (2) Walakini, Wayahudi walimkataa na kumsulibisha.
      (3) Kwa hiyo, Yesu hakuanzisha ufalme wake kama alivyopanga.
      (4) Hata hivyo, Yesu atarudi tena kuanzishwa ufalme wake.
      (5) Atarudi kimwili katika mji wa Yerusalem.
      (6) Na atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi Yerusalem kwa miaka 1,000.
   c. Kwenda hatua moja mbele, mambo haya muhimu ya mafundiso ya "premillennialism" yanaweza kufafanuliwa kwa maneno mawili ya ufunguo.
      (1) Kwanza, kwamba Kristo alishindwa kuanzisha ufalme wake kama alivyopanga alipokuja duniani mara ya kwanza.
      (2) Na pili, katika kuja kwake mara ya pili, Yesu atarejea Yerusalem kuanzisha ufalme wake na kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi kwa miaka 1,000.
      (3) Sasa, ebu na tuchanganue mambo hayo ya ufungua moja baada ya jingine.

9. Kwanza, je Kristo alishindwa kuanzisha ufalme wake Wayahudi walipomkataa karne ya kwanza?
   a. Tumeona wazi katika somo letu Matendo 1 na 2 kwamba Kristo hakika hakushindwa kuanzisha ufalme wake karne ya kwanza!
   b. Badala yake, tumejifunza kwa maelezo mengi jinsi alivyoanzisha ufalme wake kwa muda ule aliopanga na mahali sahihi, na kwa namna ya kipekee ambayo yeye na watu wengine waliovuviwa walitabiri.
   c. Kwa nyongeza, baadhi ya unabii huo ulitolewa miaka mingi mamia kabla.
   d. Basi, hayakuwa matukio ya bahati nasibu au dharura!
   e. Unabii huo ulibainishwa wazi na kupatana vyema pasipo makosa, wala si kwa nasibu, au uongo!
   f. Ufalme wa Yesu ulianzishwa siku ya Pentekoste, kama ilivyoandikwa katika kitabu hiki cha Matendo.
   g. Tena, kama tulivyojifuza awali, kuanzia siku hiyo na kuendelea, ufalme umetajwa kama upo.
   h. Kwa ushahidi mwingi huu wa maandiko, hakuna shaka kabisa kwamba Yesu alianzisha ufalme wake karne ya kwanza mbali na kukataliwa kwake na Wayahudi.
   i. Kwa hiyo, kwa kuwa fundisho la "premillenniasm" linapinga ushahidi huu mwingi, fundisho hilo ni la uongo na lazima lipingwe.
10. Tungali katika somo la kuanzishwa kwa ufalme wa Kristo, wengine hudai yafuatayo:
    a. Kwa kuwa Yesu alishindwa kuanzisha ufalme wake, badala yake alianzisha kanisa kama kitu mbadala.
    b. Hili linamaanisha Mungu hakukusudia kuanzisha kanisa.
    c. Basi, Yesu alipokataliwa, alicheleweshsa kuanzisha ufalme na akaweka kanisa kama kitu mbadala.
11. Madai haya ni ya uongo kwa sababu tatu kubwa:
    a. Kwanza, kama tulivyojifunza, Yesu alisema ufalme na kanisa ni kitu kimoja (Mt.16:18,19).
       (1) Kwa hiyo, Mungu hakika hakuchelewa uanzishwaji wa ufalme na kuweka kanisa badala yake.
       (2) Kinyume chake, kama tulivyoona, kanisa lilianza muda mmoja ambao ufalme ulianzishwa kwa sababu maneno hayo mawili yanalenga kitu kimoja.
    b. Pili, ni wazi kutokana na maandiko kwamba kanisa lilikuwemo katika makusudi ya Mungu milele.
       (1) Hivyo ni kusema dhahiri kwamba kanisa halikutokea dakika za mwisho, si kitu kilichopangwa mbadala kwa kuahirisha ufalme!
       (2) Linga. Efe.3:9-11.
    c. Tatu, Yesu alisema angejenga kanisa lake na hili lilikuwa kabla ya kukataliwa kwake na Wayahudi.
       (1) Linga. Mt.16:18.
       (2) Hivyo basi, badala ya kanisa kutokea dakika za mwisho kwa ajili ya ufalme, wazo la kuanzisha kanisa lake lilikuwemo akilini mwa Kristo kabla hata ya kukataliwa na Wayahudi.
    d. Kufuatia mafungu ya maandiko ya wazi kabisa haya, ni dhahiri kwamba kanisa ni makusudi ya Mungu ya milele.
    e. Hivyo, si wazo mbadala lililokuwemo akilini mwa Mungu kwa sababu Yesu alikataliwa na Wayahudi.
12. Kwa ufupi basi, jambo la ufunguo la "premillennialism" ni kwamba Yesu alishindwa kuanzisha ufalme wake alipokuja mara ya kwanza hapa duniani.
    a. Tumeona kwamba jambo lao hilo la ufunguo ni uongo bila shaka.
    b. Ni uongo kwa sababu linapinga mafungu mengine yaliyowazi kama hayo tuliyojifunza.

c. Kwa kuwa jambo hiyo la ufunguo la kwanza ni uongo, basi fundisho lote ni uongo na lazima lipingwe na hao wanaompenda Bwana na neno lake.

13. Jambo la pili la ufunguo la "premillennialism" ni kwamba Yesu atakaporejea tena, atakwenda Yerusalem kuanzisha ufalme wake na kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi kwa miaka 1,000.
14. Jambo la pili la ufunguo la "premillennialism" nalo ni uongo kwa sababu kadhaa kama zifuatavyo:
    a. Kwanza, ni uongo kwa sababu tumekwisha jifunza tayari, Yesu Kristo alianzisha ufalme wake karne ya kwanza.
        (1) Kwa kuwa ufalme ni wa milele (Dan.2:44), umekuwepo tangu mwanzo wake siku ya Pentekoste.
        (2) Na utadumu milele (Dan.2:44).
        (3) Kwa hiyo, Kristo haji tena kuanzisha ufalme; alifanya hivyo tayari karne ya kwanza!
    b. Pili, jambo hili la ufunguo la "premillenialism" ni uongo kwa kuwa Yesu haji tena kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi Yerusalem kwa miaka 1,000.
        (1) Kama tulivyojifunza katika 2:29-36, Yesu alifufuka toka ufuni karne ya kwanza ili kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi.
            (a) Na kiti hicho cha enzi kipo mbinguni, hakipo duniani!
            (b) Kwa hiyo, Yesu hapaswi aje Yerusalem kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi.
            (c) Amekuwa akifanya hivyo tayari kwa takribani miaka 2,000 sasa!
        (2) Tunaweza kuthibitisha hili hatimisho kwa ufupi kwa kurudia somo letu la 2:29-36.
        (3) Katika sehemu hiyo, utakumbuka Petro alitumia kwa nguvu maandiko ya Agano la Kale kuthibitisha mambo mawili yafuatayo:
            (a) Kwanza, Yesu ndiye Kristo alitimiza unabii katika Zab.16:8-11.
                1. Alifanya hivyo kwa kufufuka toka ufuni karne ya kwanza ili kutawala kama Mfalme juu ya ufalme katika kiti cha enzi cha Daudi (2:29-32).
            (b) Pili, Yesu ndiye Kristo alitimiza unabii wa Zab.110:1.
                1. Alifanya hivyo kwa kuinuliwa na kuketishwa mkono wa kuume wa Mungu mbinguni ili kutawala huko hata atakapokuwa amemwangamiza adui wake wa mwisho (2:33-36).
        (4) Kufuatia mafungu hayo, hatimisho sahihi kadhaa tunaweza kutoa kama ifuatavyo:
            (a) Kwa kuwa ilitabiriwa kwamba Kristo angefufuliwa na kuketishwa katika kiti cha enzi cha Daudi (2:30,31),
            Na kwa kuwa Yesu Kristo alitimiza unabii huu kwa kufufuliwa na kuketishwa katika kiti cha enzi cha Daudi (2:33),
            Hivyo basi, kiti cha Daudi kipo mkono wa kuume wa Mungu mbinguni, na wala si mahali popote duniani!
            Kwa hiyo, Yesu alifufuliwa kutoka kwa wafu karne ya kwanza kutawala mbinguni kama Kristo, mfalme (2:29-33; Efe.1:19-23).
            (b) Kwa kuwa utawala wa Yesu Kristo kama mfalme mbinguni atadumu milele hata maadui wote watakaposhindwa (2:34,35).
            Na kwa kuwa adui wa mwisho ni mauti (1 Kor.15:26).
            Hivyo basi, Yesu atatawala kama mfalme mbinguni hata mauti ipate kushindwa, katika kuja kwake (1 Kor.15:23-26).
            Wakati huo, ataukabidhi ufalme kwa Baba yake mbinguni, wala si Yerusalem ama mahali popote pale duniani (1 Kor.15:24).
    c. Tatu, jambo hili la ufunguo la "premillennialism" ni uongo kwa sababu Kristo haji tena kutawala mahali popote pale duniani.
        (1) 1 Thes.4:13-17.
15. Kwa ufupi basi, tumejifunza fundisho la "premillennialism" na kuona kwamba ni la uongo kwa sababu linapingana na mafungu mengi yaliyo wazi ya maandiko.

16. Maelezo ya nyongeza yanaonyesha kuwa "premillennialism" ni fundisho la uongo tunaweza kuona katika WVBS kozi ya *Mwanzo*, na *Historia ya Agano la Kale*.
17. Muhtasari wa 2:42-47, kanisa linasonga mbele.
    a. Katika mst.42 tunaona kwamba Wakristo wa kwanza walidumu katika mafundisho ya mitume, ushirika, kumega mkate, na katika sala.
    b. Mst. 43 tunaelezwa kwamba mitume wa Kristo walifanya miujiza mingi na kwamba watu waliingiwa na hofu nyingi.
    c. Mst.44 na 45 Mungu anaelezea upendo waliokuwa nao Wakristo wa kwanza kati yao kwa kusema:
        (1) Walikuwa pamoja,
        (2) Walikuwa na vitu vyote shirika, na
        (3) Kwa hiari yao waliuza mali na kuwagawia vitu vyao kwa watu ambao waliokuwa na mahitaji.
    d. Katika mst.46 na 47 Mungu alibainisha zaidi kuhusu Wakristo hawa kwa kusema kwamba:
        (1) Waliendelea kila siku katika kazi kwa ajili ya Bwana.
        (2) Waliungana pamoja, kundi lenye kupatana.
        (3) Walikusanyika pamoja kufanya kazi na kuabudu hekaluni.
        (4) Walifurahia muda wao kuutumia pamoja, na kula chakula kwa pamoja majumbani mwao.
        (5) Walikuwa na mwenendo mwema sana katika maisha yao ya kila siku.
            (a) Tabia hii ilileta furaha nyingi kwa kuwa Wakristo na kuishi kama Wakristo.
            (b) Na, ikiwa ni pamoja na nia yao ya msingi ya kutaka kumtumikia Bwana kinyume na kutumikia mali (material).
        (6) Walimsifu Mungu.
        (7) Kwa sababu ya mienendo yao walitazamwa na watu na kukubaliwa na jamii ya Yerusalem.
    e. Mwisho, mstari wa 47 mwishoni, tunajifunza kwamba Bwana alilizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa kadri walivyoitii injili.
18. Mtazamo kwa ufupi wa sura 1 na 2:
    1. Sehemu ya kwanza: (1-7) Kanisa lilianzishwa Yerusalem.
        A. (1 na 2) Kanisa lilianza kwa nguvu.
            (1) Sura 1, wakisubiri ahadi.
                (a) Mst. 1,2 Utangulizi.
                (b) Mst. 3-8 Ahadi imetolewa.
                (c) Mst. 9-11 Kupaa kwake Kristo.
                (d) Mst. 12-14 Mitume wakiwa Yerusalem.
                (e) Mst.15-26 Kuchaguliwa kwa Mathiya.
            (2) Sura 2, Ahadi imetekelezwa na kanisa limeanzishwa.
                (a) 1-13 Mitume wamejazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha zingine.
                (b) 14-36 Roho Mtakatifu (kupitia Petro) alithibitishia makutano dhambi, haki, na hukumu.
                    (1) 14-21 Tafsiri yenye uvuvio ya matukio haya.
                    (2) 22-24 *Yesu*: alidhihirishwa na Mungu; akauawa na Wayahudi; akafufuliwa na Baba.
                    (3) 25-32 *Yesu*: Uthibitisho kutoka katika unabii.
                    (4) 33-36 *Yesu*: Aliinuliwa na kuketisha kitini pa enzi.
                (c) 37-41 Jinsi baadhi walivyoitika kati ya makutano / Masharti yenye uvuvio juu ya msamaha.
                (d) 42-47 Kanisa lilisonga mbele.
19. Mtazamo kwa ufupi sehemu IB katika kielelezo chetu:
        B. (3-7) Kanisa likazidi kukua Yerusalem.

(1) 3:1-4:31 Miujiza ya Petro na Yohana / Upinzani wa Masadukayo.
(2) 4:32-5:11 Kukabiliana na mambo ya kijamii / Anania na Safira wanadanganya.
(3) 5:12-42 Mafanikio na upinzani kuinuka upya.
(4) 6:1-7 Kuchaguliwa kwa wale saba.
(5) 6:8-7:60 Mafarisayo wanamwinukia Stefano / Kifo cha Stefano.

20. Mtazamo kwa ufupi wa sehemu IB1 – Muujiza wa Petro na Yohana / Upinzani wa Masadukayo (3:1-4:31).
    a. 3:1-11 Petro amponya kiwete.
    b. 3:12-26 Roho Mtakatifu (kupitia Petro) anaushawishi mkutano mwingine.
        (1) 3:12-17 *Yesu*: Aliuawa na Wayaudi / alifufuliwa na kuinuliwa na Baba.
        (2) 3:18-26 *Yesu*: Alitabiriwa na manabii / masharti ya jinsi ya kusamehewa yaliyovuviwa.
    c. 4:1-4 Petro na Yohana wanatiwa gerezani.
    d. 4:5-12 Petro anahubiri mbele ya Sanhedrin – wokovu ni katika jina la Yesu tu.
    e. 4:13-22 Baraza (sanhedrin) linaamuru Petro na Yohana wasihubiri.
    f. 4:23-31 Sala ya mitume ili wawe majasiri.

**B. (3-7) KUKUA KWA KANISA YERUSALEM**

**1. (3:1-4:31) PETRO NA YOHANA / UPINZANI WA MASADUKAYO**

**a. (3:1-11) PETRO AMPONYA KIWETE.**

**3:1-5)**

1. Mst. 1 Petro na Yohana walikwenda hekaluni “saa tisa.”
    a. “Saa tisa” (ninth hour) = takribani 9 alasiri (3 p.m.) ambao ulikuwa muda wa sala za jioni.
    b. Idadi kubwa ya watu ingelikwenda kusali hekaluni katika muda huo.
2. Mst.2 kiwete alichukuliwa na kuwekwa katika mlango Mzuri wa hekalu. Kiwete alitajwa kama ifuatayo:
    a. “*Aliyekuwa kiwete toka tumboni mwa mamaye*”
        (1) Hakuwahi kutembea hata mara moja.
        (2) Hakuna udanganyifu hapa.
    b. Aliwekwa daima katika mlango huu.
        (1) Watu wangemtambua kwa sababu walimwona mara kwa mara.
        (2) Ukweli kwamba watu walimtambua ni njia nyingine ya kuthibitisha kuwa pasingelikuwa na udanganyifu hapa!
    c. “*Akiomba sadaka*” kwa watu ambao walikuwa wakiingia hekaluni (mst.3).
        (1) Sadaka (alms) ilikuwa namna nyingine ya upendo, rehema, au kuonyesha huruma kwa watu wenye mahitaji maalum.
        (2) Kiwete huyu alikuwa aombe ili kupata mahitaji kwa ajili ya maisha.
3. Mst.3 Kiwete alimwomba Petro na Yohana sadaka (alms).
4. Mst.4 Petro alimwambia kiwete amtazame yeye.
5. Mst.5 Kiwete alitamzama kwa makini Petro na Yohana kwa sababu alitarajia kupata kitu kwao.

**2:6-8)**.

1. Katika mst.6 Petro alijibu kwamba alikuwa hana fedha kwa ajili ya kiwete huyo.
    a. Walakini, Petro alitoa kile alichokuwa nacho – uwezo wa kumwezesha mtu huyo kutembea.
    b. Zingatia, Petro aliahidi kufanya hivyo katika “jina la (au mamlaka ya) Yesu Kristo wa Nazareti.
    c. Basi, badala ya kujipendekeza mwenyewe, Petro alikuwa akimpa sifa Yesu Kristo kutokana na miujiza aliyokaribia kuitenda.

2. Katika mst.7 tunaona Petro akimwinua kiwete, miguu na fundo zake zikapata nguvu mara!
3. Si tu hivyo, katika mst.8 kiwete aliinuka juu na kwenda hekaluni, akiruka-ruka na kumsifu Mungu.
4. Hivyo basi, tulichonacho kilichoandikwa katika mistari hii ni uponyaji wa mara moja na kamili juu ya mtu ambaye alikuwa kiwete maisha yake yote!

**3:9-11)**

1. Katika mistari hii tunaona matokeo ya watu walivyomwona kiwete akitembea na akimsifu Mungu.
2. Matokeo yake yalikuwa kama ifuatavyo:
   a. Walimtambua kuwa alikuwa kiwete aliyeomba katika mlango wa hekaluni kila siku.
   b. Walishikwa na fadhaa kubwa na mshangao wa mambo yaliyotokea kwake.
   c. Walikimbilia eneo la ukumbi wa Sulemani hekaluni.
3. Kabla ya kuondoka katika mistari hii, tafadhali angalia tofauti ya ajabu kati ya miujiza hii ya kweli na miujiza ya bandia ambayo watu wanadai leo:
   a. Kwanza, kiwete alikuwa ni kiwete kweli, mwenye ulemavu toka kuzaliwa kwake na ukweli huo ulijulikana barabara na walioona miujiza. Ugonjwa huu haukuwa wa kujifanya au uliotokana na kuumia.
   b. Pili, watu walioona miujiza walimtambua mtu huyo kiwete kwa sababu walimwona hekaluni mara kwa mara.
   c. Tatu, mitume hawakupanga kumkuta kiwete pale; ilitukiwa tu wakati Petro na Yohana walipowasili hekaluni.
   d. Nne, kinyume na kuwa na imani kubwa, kiwete alikuwa akiomba na kutarajia msaada wa mali kutoka kwa mitume.
      (1) Ukweli ni kwamba, hata Petro alipomwambia kiwete kusimama na kwenda, hakufanya hivyo (mst.6,7).
      (2) Kinyume chake, Petro akainama na kumwinua kiwete kabla ya kuamini kuwa alikuwa ameponywa (mst.7).
      (3) Hivyo basi, hakumwamini Yesu au uwezo wa Petro wa uponyaji hadi alipoona kuwa anauwezo wa kusimama na kutembea.
      (4) Hili linathitisha bila shaka kabisa kwamba ilikuwa si lazima kwa mwenye kuponywa kuwa na imani.
      (5) Linga. Yoh.11:38-44 (Lazaro).
   e. Tano, badala ya kijitukuza yeye mwenyewe, Petro alimpa sifa Yesu aliyetukuka.
   f. Sita, kiwete aliponywa mara moja, kama tabia ya miujiza ya kweli ya Biblia.
   g. Saba, kiwete aliponywa kikamilifu, wala si kwa sehemu; akitembea na kuruka-ruka.
   h. Nane, watu waliomtambua kiwete waliamini kuwa aliponywa kweli kweli. Walijaa "*ushangao wakastaajabia mambo yale yaliyompata*."
   i. Tisa, hata maadui wa Kristo hawakuweza kupinga miujiza ya ajabu iliyotendeka (linga.4:14).
   j. Na kumi, ajabu na mshangao wa makutano ilikuwa ni ishara tosha kwamba hakuna mtu angeweza kutenda miujiza pasipo msaada wa Mungu.

b. **(3:12-26) ROHO MTAKATIFU (KUPITIA PETRO) ANATHIBITISHIA MKUTANO MWINGINE MAKOSA**.

**(1) (3:12-17) Yesu: Aliuawa na Wayahudi / Alifufuliwa na Kutukuzwa na Baba**.

**3:12)**

1. Petro alipoona makutano wamekusanyika pamoja, aliwauliza kwa nini walimtazama yeye na Yohana kama ndio waliofanya miujiza kwa nguvu zao wenyewe.

2. Kwa maneno mengine, aliwakemea makutano kwa kutomhusisha Mungu moja kwa moja kuwa ndiye aliyetenda miujiza hiyo.

**3:13-15)**

1. Katika mistari hii alithibitishia makutano makosa, kama vile alivyofanya siku ya Pentekoste (linga. 2:22-24,36).
2. Zingatia tofauti za kushangaza alizodhihirisha kati ya mambo ya taifa la Israeli na yale ya Mungu mwenyezi katika mistari hii:

| **ISRAELI** | **MUNGU** |
|---|---|
| Walimtoa Yesu ahukumiwe. | |
| Mlimkana mbele ya pilato, ingawa Pilato alitaka kumwachia huru Yesu. | Alimtukuza Mtumishi wake Yesu. |
| Walimkana yule Mtakatifu na Mwenye Haki. | |
| Mkataka mpewe mwuaji mahali pa Yesu. | |
| Mkamwua Mkuu wa uzima. | Ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. |

3. Kama tulivyoona tayari, na tutaendelea kuona katika kitabu cha Matendo, mahubiri ya mitume yalikuwa na ujasiri na kuthibitishia watu makosa yao!
   a. Ebr. 4:12; Efe.6:17; Mdo.2:37.
   b. Gal.4:16.
   c. Efe.4:15.
   d. Tunahitaji mahubiri kama hayo leo!
4. Pia, tafadhali angalia maneno mazuri anayotumia Petro kumtaja Bwana Yesu Kristo:
   a. Mst. 13 – "*Mtumishi wake*."
      (1) Hapa ni marejeo dhahiri muhimu, Mtumishi mwenye mateso huyo aliyetabiriwa kuja na kuwa Mwokozi wa mwanadamu!
      (2) Linga. Isa. 42:1-9; 52:13-53:12.
   b. Mst.14 – "Mtakatifu."
      (1) Maelezo bora na sahihi juu ya Yesu, alitengwa na mambo ya ulimwengu na kuwa wakfu kwa ajili ya Bwana!
      (2) Maneno haya yalitumika pia kwa ajili ya Masihi (Zab.16:10; Mdo.2:27).
   c. Mst. 14 – "*Mwenye haki*" – δικαιον.
      (1) Neno hili maana yake; mwenye adili; asiye na hatia; aliyembali na dhambi kabisa.
      (2) Ni jinsi gani maelezo haya hubainisha ukamilifu wa Yesu… asiye na hatia kabisa, yeye ambaye hakuwahi kutenda dhambi yoyote (linga.4:15; 1 Pet.2:22).
      (3) Basi, Israeli ilikuwa na hatia ya kumkana yeye asiye na dhambi Yesu na kumwomba mwuaji Baraba mahali pake!
   d. Mst. 15 "*Mkuu wa uzima*" – αροχηγον.
      (1) Neno lililotafsiriwa "Mkuu" linamaanisha aliyechimbuko, mwanzilishi, au chanzo.
      (2) Hivyo, Petro aliposema Yesu ndiye "Mkuu wa uzima", alikuwa akimaanisha kuwa Yesu ndiye chimbuko aliyechanzo cha uzima (Linga. Yoha.1:3,4; 5:26; 1 Kor.15:45).
      (3) Ukiwa na maana hiyo akilini, angalia jinsi Petro alivyowashitaki Waisraeli kuhusu:
         (a) Walimpeleka Yesu kwa Pilato ambaye alitaka aachiwe huru (mst.13).
         (b) Walimkana mtakatifu asiye na hatia Yesu (mst.14).
         (c) Waliomba wapewe Baraba mwuaji badala ya Yesu (mst.15).
         (d) Siyo hivyo tu, bali walimwua Yesu, aliyechimbuko na chanzo cha uzima (mst.15).
   e. Mungu mwenyezi angefanya nini kwa tendo hilo lisilo la haki?

        (1) Alimfufua kutoka kwa wafu (mst.15).
        (2) Alimtukuza Mtumishi wake Mtakatifu, Yesu (mst.13).
    f. Ebu fikiria jinsi walivyojisikia vibaya kutokana na makosa wasikilizaji waliyoyafanya kwa wale wenye mioyo safi na minyoofu.
5. Mwisho mwa mst. 15 Petro tena alitoa ushahidi zaidi juu ya kuona kwao mitume ili kuthibitisha kwamba Baba alimfufua Mwanawe toka ufuni (linga.2:32).

**3:16)**

1. Katika mstari huu Petro alimpa Yesu sifa kwa muujiza huu.
    a. Petro alisema kuwa jina la Yesu, kwa imani katika jina lake, amemfanya kiwete huyu kuwa na nguvu.
    b. Kumbuka katika somo letu 2:38, jina la mtu mara nyingi liliwakilisha mhusika, nguvu, na mamlaka ya mtu huyo.
    c. Hivyo basi, Petro alikuwa akisema kuwa miujiza hiyo ilitendwa kwa nguvu na mamlaka ya Yesu.
2. Lakini, Petro alikusudia nini aliposema miujiza hii ilifanyika "kwa imani" katika jina la Yesu? Alikuwa akiizungumzia imani ya nani?
    a. Kama tulivyoona mst.9-11 ni wazi kuwa haikuwa imani ya kiwete huyo!
        (1) Kinyume na kuwa na imani katika Kristo, aliomba na kutarajia msaada wa mali kutoka kwa mitume.
    b. Njia pekee nyingine ni imani ya mitume katika Kristo iliyowawezesha kufanya miujiza hii ya ajabu.
    c. Hili linalingana na ukweli kwamba kipindi cha miujiza, imani upande wa mtendaji miujiza ilikuwa lazima kabisa.
        (1) Lk.17:6.
        (2) Math.14:28-31.
        (3) Math.17:14-20.
    d. Kwa hiyo, mtu anapodai kuwa na nguvu ya kutenda miujiza leo anaposhindwa kufanya miujiza, tunajua kwamba ni laghai!
3. Mwisho, Petro alisisitiza uhakika na usahihi wa miujiza hiyo kwa kufafanua tabia bayana zifuatazo:
    a. Wasikilizaji wote waliweza "kuona" ushahidi dhahiri kwa macho yao wenyewe.
    b. Walimjua kiwete huyo na kasoro zake binafsi.
    c. Waliweza kuona "kabisa" (kamili) uponyaji wake wazi wazi.
    d. Na miujiza hii ya kustaajabisha ilitendeka mbele ya watu wote waliokuwepo.

**3:17)**

1. Akishatumia upanga wa Roho kuthibitishia umati makosa yao, Petro kwa huruma na upendo, na kwa wema aliwasihi wasikilizaji kama "ndugu" zake".
2. Pili, alitambua kwamba walimsulibisha Bwana Yesu kwa ujinga, k.m. walikuwa hawajui ukweli kwamba alikuwa ndiye Masihi aliyetabiriwa.
    a. Hao na wakuu wao hawakujua hekima ya Mungu iliyofunuliwa katika maandiko (linga. 1 Kor.2:8).
    b. Ingawa Petro alitambua ujinga wao, ni wazi kwamba kutokujua kwao si sabau ya kutokuwa na hatia!
        (1) Hili ni kweli kwa sababu Petro alishakwisha wathibitishia makosa yao kwa kumwua Yesu (mst.13-15)
        (2) Kwa nyongeza, katika mst.19-21, aliwasihi watubu na kuongolewa ili dhambi zao zipate kufutwa!
    c. Hili kabisa linalingana haswa na kanuni muhimu ya Biblia.
        (1) Lk. 12:47, 48.
3. Muhtasari wa 3:12-17, Yesu: Aliuawa na Wayahudi / Alifufuliwa na kutukuzwa na Baba.

a. Mst.12 Petro aliwauliza makutano kwa nini walimkazia macho yeye na Yohana kama ndiyo wao waliofanyia miujiza kiwete huyo kwa uwezo wao.
b. Mst.13-15 Petro alithibitishia makutano makosa yao kwa kufafanua kuwa:
   (1) Walimtoa Yesu na kumkana mbele ya Pilato, ingawa Pilato alitaka Yesu aachiwe huru;
   (2) Walimkana Yesu, ambaye ni mtakatifu ambaye hakuwa na hatia kabisa;
   (3) Walimwomba aachiwe huru mwuaji badala ya Yesu, na
   (4) Wakamwua Mkuu wa uzima.
c. Kinyume chake kabisa cha matendo haya mabaya, Petro alisema kwamba Mungu Baba:
   (1) Alimfufua kutoka kwa wafu, na
   (2) Alimtukuza Yesu kama Mtumwa mwenye mateso ambaye alitabiriwa na Agano la Kale.
d. Mst.16 Petro alibainisha imani ya yeye na Yohana katika Yesu ndiyo ilifanya miujiza hii ya ajabu ya uponyaji.
e. Mst.17 Petro alitambua kwamba Israeli ilifanya hivyo kwa kutokujua.

### (3) **(3:18-26) YESU: ALITABIRIWA NA MANABII / MASHARTI YENYE UVUVIO YA JINSI YA KUPATA MSAMAHA**

**3:18)**
1. Petro alithibitisha mateso aliyopitia Yesu akiwa ni Kristo aliyetabiriwa na Mungu na manabii wa Agano la Kale (linga. Lk.24:44-46).
   a. Hivyo basi, Waisraeli walifanya mambo hayo wakitumia uhuru wao wa kuchagua na kudhania kuwa walikuwa wakifanya mapenzi yao kwa kumwangamiza Yesu.
   b. Walakini, pamoja na hayo yote, Mungu alikuwa ametabiri mambo hayo kutokea kwa utukufu wake na huyo Mwanawe mpendwa Yesu, pia kwa wokovu wa mwanadamu!
   c. Linga. Rum.11:33-36.
2. Ukweli kwamba unabii wote ulitimizwa na Yesu kama Kristo ni ishara nyingine zaidi ya uovu mbaya wa Israeli kwa kumsulibisha Yesu!
3. Walimwua yeye aliyekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea!

**3:19-21)**
1. Petro alikuwa ameuthibitishia umati makosa yao ya kumwua Yesu.
2. Katika mistari hii walielezwa mambo ya kufanya ili kupata msamaha wa dhambi zao.
3. Kwanza, katika mst.19, aliwaeleza kwamba walihitaji kutubu.
   a. Kama tulivyojifunza katika 2:38, toba ni badiliko la akili.
   b. Badiliko hili la akili kwa huzuni iliyo ya jinsi ya Mungu kutokana na dhambi zao za hapo nyuma.
   c. Hupelekea mabadiliko katika mwenendo au tabia ya mtu anayetubu.
   d. Hivyo basi, Petro alikuwa akiueleza mkutano huo walihitajika wabadilike akilini kutokana na huzuni ya jinsi ya Mungu ambayo hupelekea badiliko katika tabia.
4. Tena, pia katika mst.19, Petro aliwaeleza walipaswa "kuongoka" (be converted - KJV, NKJV), au "kurejea upya" (turn again – ASV).
   a. Neno lililotafsiriwa "kuongolewa" au "kugeuka upya" (επιστρεφατε) haswa lenye maana kurejea upya; linamaanisha kugeuka toka dhambini; kurekebisha.
   b. Kwa hiyo, ni wazi kwamba anachoamuru Petro aliposema warejee upya ni kubadili *tabia* au *mwenendo*.
      (1) Basi, alipowaambia watubu, aliwaamuru kubadilika katika akili zao.
      (2) Na alipowaambia kurejea upya, aliwaamuru wabadili tabia zao.
   c. Hakika, kubadili tabia zao kungeanzia mahali fulani.
   d. Na jambo hilo lingetokea mara baada ya kutubu kwao.
   e. Tunaporudi 2:38, mstari unaolingana na huu, ni dhahiri kwamba baada ya toba, mabadiko ya tabia ya mtu inajumuisha na ubatizo majini ili kupata msamaha wa dhambi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Matendo 3:19 | TUBUNI | | DHAMBI ZIPATE KUFUTWA |
| Matendo 2:38 | TUBUNI | | ONDOLEO LA DHAMBI |
| Matendo 3:19 | TUBUNI | **REJEA** | DHAMBI ZIPATE KUFUTWA |
| Matendo 2:38 | TUBUNI | **KUBATIZWA** | ONDOLEO LA DHAMBI |

   f. Kufuatana na ulinganifu wa mistari hii, tunaweza kuhatimisha kwamba mtu hugeuka toka dhambini na kumwelekea Mungu inajumuisha na ubatizo majini ili kupata msamaha wa dhambi!
5. Bado tungali katika mst. 19, Petro aliorodhesha baraka aina mbili ambazo zitapokelewa na kila mtu ambaye atatubu na kurejea kutoka dhambini na kumwelekea Bwana.
   a. Kwanza, dhambi zao "zitafutwa" – εξαλειφηναι.
      (1) Neno hili linamaanisha kuoshwa kabisa; kuondoa au kufuta; kufutia mbali (obliterate).
      (2) Lilitumika hilo kuonyesha kufuta taarifa zote za deni alilodaiwa mtu.
      (3) Hivyo basi, Mungu anaahidi kufutilia mbali kabisa taarifa zote za dhambi za nyuma zilizotendwa na hao wenye kutubu, kurejea toka katika dhambi zao, na kumgeukia Bwana, ukijumuisha na ubatizo majini.
      (4) Ni jambo la ajabu na wazo lenye kufariji (Ebr.8:12)!!
   b. Baraka ya pili iliyoahidiwa katika mst. 19 ni, "*ili zije nyakati za kuburudika kwa kuwapo kwake Bwana*"
      (1) Zingatia baraka hii inatokea tu baada ya mtu kutubu, kurejea, na dhambi zake kufutwa.
      (2) Kila anayefanya hivyo anapata kuburudika kwa kuwapo kwake Bwana.
      (3) Lakini, ina maana gani kwa kuwepo kwake Bwana?
      (4) Tena, ukweli kwamba mstari huu na 2:38 inafanana hutupa majibu yenye uvuvio kwa swali la nini maana ya kuwepo kwake Bwana.

**MATENDO 2:38 …………………………………………….. MATENDO 3:19**

TUBUNI …………………………………………………………. TUBUNI

MKABATIZWE …………………………………………………. MREJEE

MSAMAHA WA DHAMBI …………………………………DHAMBI ZIPATE KUFUTWA

**KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU ………… KUBURUDIKA KWA KUWEPO KWAKE BWANA**

      (5) Hivyo Basi, mtu anapotii injili kwa uaminifu na kwa hiari yake, hupokea msamaha wa dhambi, Mungu hukaa ndani ya mwanawe (hakuna miujiza, wala uongozi au ushawishi wa moja kwa moja).
      (6) Ni burudani kwa mwana wa Mungu mwaminifu kutambua ukweli kuwa dhambi zake amesamehewa na kwamba, kama matokeo, Mungu anakaa ndani yake!

**3:20,21)**
1. Mst. 20 tunaona sababu nyingine kwa nini Petro aliamuru wasikilizaji wake watubu na kurejea.
2. Sababu hiyo ilikuwa Baba angelimtuma Yesu kwao.
   a. Kutumwa kwa Yesu Kristo ni marejeo ya wazi yakilenga kuja kwake Kristo mara ya pili.

   b. Wakati huo, waliokufa katika Kristo na hao waliohai na kubakia waaminifu kwake watanyakuliwa mawinguni na hivyo kukaa na Bwana milele mbinguni (1 Thes.4:13-17).
   c. Watachukuliwa kuishi milele mbinguni (1 Kor.15:24).
   d. Sasa ni dhahiri kwamba Mungu anataka wanadamu wote kwa idadi yao kutii injili kwa unyenyekevu (1 Tim.2:4; 2 Pet.3:9).
   e. Lakini, mwanadamu ana hiari ya kuchagua ama kutii injili au la (Ebr.5:9).
   f. Kwa sababu hizo, Petro alitoa maonyo yaliyovuviwa kwa watu wote kutubu na kurejea kumwendea Bwana ili amtume Yesu kuwachukua waaminifu wengi kwenda kwake!
3. Basi, mst.21, Petro alieleza kuwa Yesu sharti abakie mbinguni "hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote."
   a. Maneno haya yanafurahisha na kuleta changamoto!
   b. Ni changamoto kutambua haswa maana yake tungo hii "zamani za kufanywa upya vitu vyote."
      (1) Wala si tu ni changamoto kutambua nini maana yake tungo hili, kadhalika ni muhimu sana!
      (2) Ni muhimu sana kwanza kabisa kwa sababu tunataka kuelewa neno la Mungu!
      (3) Lakini pia ni muhimu kwa kuwa "premillennialism" wanatumia vibaya mstari huu kufundisha mafundisho yao.
      (4) Tafadhali kumbuka tumejifunza tayari katika somo letu la 2:47 kwamba fundisho la "premillennialism" ni la uongo na hivyo, lazima lipingwe.
         (a) Katika somo hilo, tunaona kwamba Kristo alianzisha ufalme (kanisa) wake karne ya kwanza.
         (b) Kwa hiyo, harudi tena duniani kuanzisha ufalme wake.
         (c) Kinyume chake, anakuja kukutana na watu wake mawinguni na kuukabidhi ufalme kwa Baba aliye mbinguni.
   c. Ukiwa na msingi huo akilini, inastaajabisha kujifunza kwamba "premillennialism" wanafundisha fungu hili linaahidi kufanywa upya kwa vitu vyote duniani.
      (1) Na wanadai kuwa kufanywa upya vitu vyote itakuwa wakati Kristo atakaporudi duniani kuanzisha ufalme wake.
4. Ukweli kabisa, wala si mstari huu ama mazingira haya yanaahidi kitu chochote kama hicho.
   a. Tunajua hili kwa sababu tumeona kwamba Yesu haji duniani kuanzisha ufalme wake!
   b. Tutaona pia mstari huu hauna ahadi yoyote kama hii kupitia mchanganuo wetu dhahiri wa maana ya maneno.
5. Njia moja ya kuelewa changamoto ya maneno haya ni kuunganisha na maneno yanayofuata baada ya mstari huu (k.m., mazingira ya karibu).
   a. Sehemu ya kwanza Petro anazungumzia kuhusu kufanywa upya kwa "vitu vyote."
   b. Lakini sehemu ya kwanza ya mstari haitengani bali inaungana na sehemu nyingine inayofuata!
   c. Hivyo basi, "vitu vyote" sehemu ya kwanza ya mstari inaungana na yaliyosemwa sehemu iliyotangulia.
   d. Sehemu ya mwisho Petro alirejea kwa vitu "*vilivyonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu*."
   e. "Vitu vyote" inarejea katika vitu ambavyo Mungu alinena kwa kinywa cha manabii wake.
   f. Kwa hiyo, Yesu sharti abakie mbinguni hata vitu vyote vifanywe upya ambavyo Mungu alivinena kupitia manabii wake.
6. Lakini ufunguo mwingine unaoendana kwa kuelewa vyema na changamoto ya maneno haya ni maana ya neno lililotafsiriwa "kufanywa upya" (restoration) "αποκαταστασεωσ".
   a. Neno hili linaweza kumaanisha kufanywa upya kwa vitu katika hali au namna yake ya kwanza.
   b. Lakini pia linaweza kumaanisha ukamilifu au kujalizia kitu fulani.

c. Ukweli ni kwamba, ninaamini kwamba maana yake ambayo Mungu alikusudia kwa kutafsiriwa ya neno "restoration" katika fungu hili.
d. Ikiwa "ukamilifu" ndiyo maana haswa ya neno lililotafsiriwa "restoration," hivyo tunaweza kuweka neno "ukamilifu" badala yake katika tungo na lisibadili maana yake, wala lisipingane na fungu lingine lolote lile la maandiko.
e. Ebu na tusome mst.21 pamoja na neno "ukamilifu" (completion) badala ya neno "kufanywa upya" (restoration), na kuona hakuna mabadiliko ya maana katika mstari.
f. Hivyo basi, tunahatimisha maana ya mst.21 ni kwamba Yesu sharti abakie mbinguni hata vitu vyote ambavyo Mungu alinena kupitia manabii wake vimetekelezwa, vimekamilika, vimetimia.
g. Lakini hatimisho hilo linalingana na mafungu mengine ya Agano Jipya? Ili kujibu swali hilo tafadhali chunguza yafuatayo:
   (1) 1 Kor.15:23,24.
   (2) Math.25:31-46.
   (3) 1 Kor.15:24.
   (4) 1 Thes.4:17.
h. Kufuatana na mafungu hayo ya maandiko, ni dhahiri hatimisho letu ni sahihi – hivyo ni kusema kwamba, Mungu anafundisha katika mstari huu kwamba Yesu atabakia mbinguni hata vitu vyote alivyonena Mungu kupitia manabii wake vimekamilika.
   (1) Wakati huo Yesu atarejea kuwachukua hao walio katika ufalme wake kwenda mbinguni, ambako wataishi milele.
   (2) Hivyo, fundisho la "premillennialism" kwamba mstari huu unaahidi kurejeshwa upya vitu vya dunia baada ya Yesu kurejea kwake mara ya pili ni uongo kabisa!

**3:22,23)**

1. Mwishoni mwa mstari uliotangulia, Petro anarejea "*…vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake…*"
2. Sasa basi, katika mistari hii miwili, Petro ananukuu kutoka kwa nabii mkubwa katika Agano la Kale, Musa, kama inavyoonekana katika Kumb.18:15-20.
   a. Ukweli ni kwamba wasikilizaji wake Petro, Wayahudi walimstahi na kumwamini Musa kuwa mmoja wa manabii wakuu wa Mungu.
   b. Walitambua na kukubali ukweli wa kwamba Musa alinena kwa uweza wa Mungu mwenyezi.
   c. Hivyo basi, kwa kumnukuu Musa, Petro aliwakumbusha wasikilizaji wake Wayahudi walipaswa kumsadiki na kumtii Musa jinsi alivyosema katika Kumb.18:15-20 kama walitaka kumpendeza Mungu.
3. Lakini, ni kitu gani alisema Musa katika Kumb.18:15-20?
4. Petro alitoa muhtasari wa unabii wa Musa kama ifuatavyo:
   a. Kwanza, Mungu "angemwinua" nabii kwa mafano wa Musa kutoka katika Israeli.
   b. Pili, watu watapaswa kumsikiliza na kumtii nabii huyo.
   c. Na tatu, kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake.
5. Mambo hayo yakiwa akilini , ebu na tuchanganue kwa kiina zaidi.
   a. Kwanza, hapakuwa na shaka kwamba Yesu alitokea Israeli (k.m., alikuwa miongoni mwao "*katika ndugu zenu*" kama Musa alivyotabiri kwa Israeli) [Linga. Math.1:1-17; Rum.1:3].
   b. Pili, lakini jinsi gani Yesu alikuwa kama Musa? Kuna ulinganifu kadhaa, bali tutazingatia katika mambo mawili muhimu zaidi.
      (1) Kwanza, Musa ndiye aliyetoa sheria awali (k.m. Mungu alimtumia yeye kulichukua Agano la Kale kwa taifa la Israeli).
         (a) Ni dhahiri, Yesu pia ndiye aliyetoa sheria. Alitoa sheria za Kristo, ambazo ni za Agano lililo bora (Gal.6:2; Ebr.8:6).

(2) Pili, Musa aliliokoa taifa la Israeli toka kifungoni (utumwani) katika taifa la Misri (Mdo.7:35,36).
   (a) Hakika, Yesu ni mwokozi bora zaidi. Anawaokoa wote wanaomtii kutoka katika utumwa wa dhambi na mauti (Rum.7:22-25; Ebr.2:14, 15; 1 Kor.15:54ff).

6. Tunapotafakari ukweli huo toka katika maandiko, ni dhahiri kwamba Petro alikuwa akisema kwamba Yesu Kristo ndiye aliyeutimiza unabii huo wa Musa katika Kumb.18:15-20.
   a. Yesu alikuwa nabii kwa mfano wa Musa.
   b. Alikuwa nabiii aliyetoka katika taifa la Israeli.
   c. Basi hivyo, Yesu alikuwa nabii ambaye watu walilazimika kumsikia na kumtii.
   d. Na kila mtu asiyemsikiliza na kumtii Yesu ataangamizwa kabisa!
   e. Lakini, alikuwa amethibitisha tayari kuwa taifa la Israeli lilimwua nabii mkuu, "Mkuu wa uzima" (mst.15)!
   f. Ebu fikiria machungu na hatia walivyopata wasikilizaji siku hiyo!
   g. Tena, mahubiri ya mitume yalichoma mioyo yao walioyasikiliza!

**3:24,25**)

1. Mst. 24 Petro alisema kwamba wala si nabii Musa pekee aliyetabiri siku za Masihi, Kristo.
2. Samweli na manabii wengine walitabiri kuhusu siku hizo.
3. Mst. 25 Petro aliwaeleza Wayahudi wasikilizaji hao kuzingatia mambo mawili:
   a. Kwanza, kutokana na mahusiano yao na manabii.
      (1) Walikuwa "watoto" wa manabii (wazao) wa manabii, kwa hiyo
      (2) Walipaswa wasikilize na kuwatii manabii hao.
   b. Pili, kuzingatia mahusiano katika ahadi za Mungu alizotoa kwa Abraham.
      (1) Wayahudi walimtazama Abraham kama baba wa taifa la Israeli (mst.13).
      (2) Hakika, Mungu alimtambua Abraham kama baba kwao waliowaaminifu (Rum.4:11,12).
      (3) Basi, kwa kurejea ahadi za Mungu kwa Abraham, Petro kwa mara nyingine aliwasihi kwa kuwakumbusha mtu mwenye nafasi ya juu kabisa katika akili zao Wayahudi!
4. Petro aliitambulisha ahadi hiyo kama moja ya ahadi ambazo Mungu aliahidi kwamba mataifa yote duniani wangebarikiwa kupitia ukoo ("uzao") wa Abraham.
   a. Ahadi hii toka kwa Mungu kwenda kwa Abraham inapatikana Mwa.12:3; 18:18; na 22:18.
   b. Tutaizungumzia zaidi ahadi katika somo lijalo mstari unaofuata.

**3:26)**

1. Katika mstari huu Petro alitoa hatimisho lenye uvuvio na la kusisimua kwa hoja yake.
2. Alifanya hivyo kwa kubainisha mambo yafuatayo:
   a. Kwanza, Yesu alikuwa nabii mkuu ambaye Musa alimtabiri katika Kumb.18:15-20.
      (1) Tunajua hivyo kutokana na mstari huu kwa sababu Yesu ndiye ambaye Baba alimwinua aliye mfano wa Musa (linga.22,23).
      (2) Basi, Yesu ndiye ambaye wote walipaswa kumsikiliza na kumtii.
      (3) Na kila asiyemsikiliza na kumtii Yesu, Baba aliahidi kumkatilia mbali kabisa mtu huyo!
   b. Pili, Petro alisema Yesu ndiye haswa ambaye Baba alimtuma ili awabariki watu wote.
      (1) Hakika, hili linamaanisha Yesu alikuwa "mzao" aliyetimiza ahadi ya Baba kwa Abraham "kuwabariki" mataifa yote duniani (mst.25).
      (2) Gal.3:16.
      (3) Lakini, jinsi gani Yesu alibariki na anabariki watu wote duniani?
   c. Jibu la swali hilo ndilo Petro anaeleza jambo la tatu katika mstari huu. Alisema Yesu angefanya hivyo "kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu yake."
      (1) Je hilo linamaanisha Yesu angemwepusha na anawaepusa watu na maovu yao kana kwamba hawana uhuru wa kuchagua katika mambo hayo?

(2) Ukweli ni kwamba, lazima tuliendee Agano Jipya ili kupata jibu la swali hilo!
(3) Kwanza, ebu na tuangalie mazingira ambamo maelezo haya hupatikana.
(a) 3:19.
(b) 3:22, 23.
(4) Pili, mafundisho mengine ya Agano Jipya yanasemaje?
(a) Tito 2:11-14.
(b) Efe.1:3.
(c) 2 Kor.5:14,15.
(d) Ufu.22:14.

d. Jambo la nne, Petro alisema Baba alimtuma Mwanawe kwa taifa la Israeli "kwanza" ("kwenu kwanza").
(1) Hili si kwamba Mungu alionyesha upendeleo kwa Wayahudi (Rum.2:11; Mdo.10:34;35).
(2) Kinyume chake, ilikuwa kwa sababu Wayahudi walipaswa wao kupokea injili haswa.
(3) Ni ukweli huo kwa sababu Mungu alifunua unabii mwingi kuhusu Yesu Kristo katika Agano la Kale, ambalo Wayahudi walikuwa nalo (Rum.3:1,2; Lk.24:44-46).

3. Muhtasari wa 3:18-26, *Yesu*: alitabiriwa na manabii / masharti yaliyovuviwa ya jinsi ya kupata msamaha.
a. Mst.18 Petro alisema mateso ambayo Yesu aliyapata kama Kristo yalitabiriwa na Mungu kupitia kwa manabii wake.
b. Mst. 19 Petro aliwaeleza wasikilizaji walitakiwa kutubu (k.m., kugeuka akilini) na kuongoka (k.m. kubadilika kitabia, kunakoanzia na ubatizo).
c. Pia mst.19 Petro alisema kungekuwa na matokeo aina mbili kutokana na kutubu na kuongoka kwao:
(1) Kwanza, dhambi zao zingefutwa kabisa, na
(2) Pili, nyakati za kuburudika zingekuja kwa kuwepo kwake Bwana.
d. Mst.20 sababu nyingine inayotolewa kutokana na kutubu na kuongoka – ili Baba amtume Yesu tena.
e. Mst.21 Yesu lazima abakie mbinguni hata mambo yote yaliyotabiriwa na manabii yakamilike.
f. Mst.22,23 Unabii wa Musa toka katika Kumb.18:15-20 ulijumuishwa katika mambo makubwa matatu:
(1) Mungu "*angemwinua*" nabii kwa mfano wa Musa kutoka katika Israeli.
(2) Watu walipaswa kumsikiliza na kumtii nabii huyo.
(3) Asiyemsikiliza na kutomtii nabii huyo angeangamizwa kabisa.
g. Mst.24 Wala si Musa tu, bali Samweli na manabii wengine walitabiri siku hizi za Masihi, Kristo.
h. Mst.25 Wasraeli walikuwa watoto wa manabii wenye ahadi maalum aliyoifanya Mungu kwa baba mkuu Abraham.
(1) Ahadi hiyo ilikuwa kwamba watu wote wa duniani wangebarikiwa kupitia uzao wa Abraham.
i. Mst.26 Yesu Kristo alitimiza unabii huo wote na ule wa ahadi ya Mungu kwa Abraham.
(1) Alikuwa nabii mkuu kwa mfano wa Musa ambaye Mungu alimwinua kutoka katika Israeli.
(2) Na alikuwa uzao wa Abraham alitumwa na Baba kuwabariki watu wote duniani.
(3) Yesu angekuwa baraka kwa kuwageuza watu toka katika dhambi zao.
(a) Angefanya hivyo kupitia sadaka kwa hiari yake mwenyewe, na
(b) Kupitia injili yake, ambayo lazima mtu aitii ili kupokea baraka hii.
(4) Baba alimtuma Mwanawe kwa Israeli kwanza.

4. Mtazamo kwa ufupi wa sura 3:
a. 3:1-11 Petro anamponya kiwete.
b. 3:12-26 Roho Mtakatifu (kupitia Petro) anathibitishi umati mwingine makosa yao.

(1) 3:12-17 *Yesu*: Aliuawa na Wayahudi / Alifufuliwa na kutukuzwa na Baba.
(2) 3:18-26 *Yesu*: Alitabiriwa na manabii / Masharti yenye uvuvio ya msamaha.

### c. (4:1-4) PETRO NA YOHANA WANATIWA NDANI

**4:1-3)**

1. Baadhi ya viongozi wa Kiyahudi wanamvamia Petro alipokuwa akizungumza.
2. Miongoni mwa viongozi hao baadhi walikuwa Masadukayo.
   a. Masadukayo ni kundi la dini (madhehebu) ya Kiyahudi.
   b. Hawakuamini katika ufufuo wa wafu, au katika malaika, au katika roho na nafsi ya mwanadamu (Mdo.23:8; Math.22:23).
3. Viongozi hawa wa dini walishikwa na fadhaa kwa mambo aliyokuwa akifundisha.
   a. Mitume walifundisha ufufuo wa wafu.
   b. Wala si hivyo tu, bali walikuwa wakithibitisha hoja zao kwa kutoa ushahidi wa kufufuka kwake Yesu toka ufuni.
4. Kama matokeo, viongozi hawa wa dini waliwatia ndani mitume hao hadi siku iliyofuata.

**4:4)**

1. Mbali na kuingiliwa na viongozi hawa wa dini ya Kiyahudi, kanisa lilizidi kukua!
2. Watu wengi waliosikia neno la Mungu waliamini ujumbe wa injili.
3. Ukweli ni kwamba, kanisa lilizidi kukua kuanzia watu 3,000 siku ya Pentekoste hadi watu 5,000 kwa muda mfupi uliofuata!
4. Kama tulivyojifunza katika maelezo ya historia, hili linadhihirisha uweza wa neno la Mungu kama likihubiriwa, kufundishwa, na Wakristo kuishi kwalo!

### d. (4:5-12) PETRO ANAHUBIRIA BARAZA – WOKOVU NI KATIKA JINA LA KRISTO PEKEE

**4:5-7)**

1. Siku iliyofuata, wakuu, wazee, waandishi, wakuu wa makuhani, na jamii kuhani mkuu walikusanyika pamoja Yerusalem.
2. Mkutano huo ulikuwa wa Sanhedrin.
   a. Baraza hili lilikuwa ndilo kuu katika kushurutisha Sheria za Musa kwa Wayahudi.
   b. Lilikuwa na wajumbe 71, ukijumuisha pamoja na kuhani mkuu, aliyetumika kama raisi.
   c. Sanhedrin lilikuwa na uwezo juu ya maisha au mauti (Math.26:3,4).
   d. Walakini, hawakuweza kutoa hukumu ya kifo. Hiyo ilikuwa ni jukumu la serikali ya Rumi (Yoh.18:31).
   e. Kesi ya Yesu ilisikilizwa mbele ya Sanhedrin (Math.26:59).
   f. Kama ilivyosikilizwa kesi ya Petro na Yohana (sura hii).
   g. Stefano (Mdo.6:12).
   h. Kadhalika pia Paulo (Mdo.22:30).
3. Mst.7 tunajifunza wakuu wa Sanhedrin waliwaweka Petro na Yohana katikati ya baraza.
4. Kisha wakuu waliuliza kwa mamlaka au jina la nani walifanya "haya."
5. Sanhedrin walipowauliza Petro na Yohana kwa mamlaka na jina gani walifanya mambo hayo, ni wazi kwamba walikuwa wakiuliza kwa mamlaka gani walikuwa wakitenda mambo hayo.
6. Kwa maneno mengine, waliwauliza Petro na Yohana walitenda mambo hayo kwa mamlaka yao wenyewe au kwa (upon) mamlaka ya mtu mwingine.

**4:8-10)**

1. Petro kwa ujasiri alisema kuwa kiwete aliponywa kwa jina (mamlaka) la Yesu Kristo.
2. Mst.3:6 na 16 Petro alisema miujiza hii ilitendwa kwa mamlaka ya Bwana Yesu.
3. Angalia, Petro alibainisha mambo ya kweli kadhaa kwa wakuu hao kuhusu Yesu.

a. Kwanza, Yesu huyo ndiye Kristo. Hivyo, alikuwa ndiye Masihi, Mwokozi, Mfalme.
b. Pili, kwamba alitoka Nazareth. Hivyo basi, pasiwepo na shaka katika kumtambua.
c. Tatu, kwamba wakuu hawa walimsulibisha Yesu. Petro aliwatwisha mzigo Waisraeli kwa kifo cha Yesu (2:23; 3:14,15).
d. Na nne, kwamba Baba alimfufua toka ufuni.

**4:11,12)**

1. Mst.11 Petro alisema Yesu huyo ambaye viongozi wa Kiyahudi walimkana kwa kumsulibisha ndiye aliye jiwe kuu la pembeni la jengo la Bwana.
2. Petro alinukuu toka katika Zab.118:22 na Isa.28:16.
3. Math.21:42.
   a. Rum.9:33; Efe.2:20.
   b. 1 Pet.2:4-7.
4. Basi, Yesu, Petro, na Paulo kila mmoja walidai kwa uvuvio kuwa Yesu ndiye mjenzi na msingi wa kanisa la Bwana, hekalu la kiroho la Mungu (1 Kor.3:11,16,17)!!
5. Hata hivyo, Wayahudi hawa walimkana na kumsulibisha Yesu!
6. Lakini Petro aliendelea kufafanua zaidi!
7. Mst.12 alidai hakuna njia nyingine ya mtu kuokoka isipokuwa kwa njia ya Yesu.
   a. Basi, kwa kumkana Yesu, Kristo, wakuu hawa waliikataa njia pekee ambayo Mungu aliitoa kwa ajili ya wokovu wetu toka dhambini!
   b. Linalingana kabisa hili na mafungu mengine yaliyo dhahiri katika maandiko:
      (1) Lk.19:10; Math.1:21.
      (2) Yoh.14:6.
8. Ukirudi nyuma katika mst.8-12 tumeona mfululizo wa simulizi zifuatazo:
   a. (mst.8-10) – Petro alianza kwa kusema yeye na Yohana walimponya kiwete yule kwa mamlaka ya Yesu.
   b. Mst.10 Alibainisha kwamba Yesu ndiye Kristo.
   c. Mst.10 Aliwashutumu wakuu hao wa Kiyahudi kwa kuhusika katika kumsulibisha Yesu.
   d. Mst.10 Walakini, Mungu Baba alimfufua kwa ushindi Yesu toka ufuni.
   e. Mst.11 Pia Yesu ndiye aliyetabiriwa kuwa jiwe kuu la pembeni la jengo la Bwana.
   f. Mst.11 Walakini, wakuu wa makuhani walimkana.
   g. Mst.12 Muhimu zaidi, Yesu ndiye pekee na katika yeye wokovu wa kiroho toka dhambini unaweza kupatikana!
9. Kweli, mahubiri ya mitume yalijaa ujasiri na yalimwinua Yesu kuwa ndiye Kristo!
   a. Watu hawa wakiwa katikati ya umati uliokuwa mkali kwao na kusudi lao.
   b. Walakini, walinena ukweli pasipo hofu!

**e. (4:13-22) Sanhedrin wanaamuru Petro na Yohana wasihubiri**

**4:13)**

1. Wajumbe wa baraza la Sanhedrin walistaajabia kwa sababu ya ujasiri wa Petro na Yohana.
2. Walistaajabu sana kwa sababu walimwona Petro na Yohana kutokuwa na elimu kubwa na wala hawakujifunza ujuzi wa kuzungumza mbele ya halaiki.
3. Hata hivyo, mbali na kutokuwa na elimu na ujuzi hapo nyuma, walinena neno la Mungu kwa ujasiri na kwa kujiamini sana.
4. Angalia jinsi Sanhedrin ilivyohatimisha kuhusu wapi ujasiri wa Petro na Yohana ulitoka.
5. Walitambua kwamba mitume hawa "*walikuwa pamoja na Yesu*"
   a. Ndiyo kusema kwamba, wajumbe wa Sanhedrin walimwona dhahiri Yesu kuwa na ushawishi mkubwa kwao.
   b. Yesu alikuwa na ushawishi dhahiri jinsi mitume walivyofikiri, nena, na kutenda!
6. Mambo ya kuyafanyika kazi:
   a. Tunajua kwamba hatuwezi kuwa na Yesu kwa mfano ambao hawa walivyokuwa naye.
   b. Walakini, tunaweza kuwa na Yesu kwa kujifunza na kutafakari maneno yake (Kol.3:16).

   c. Na kwa kujitahidi kufuata kielelezo alichotuachia (1 Pet.2:21; 1 Yoh.2:6).
   d. Tunapofanya mambo haya kwa kuzidi na zaidi, tunakuza nia zetu juu ya Kristo (Flp.2:5).

**4:14)**
1. Ushahidi dhahiri usiopingika ambao Petro na Yohana walitoa kwa kufanya muujiza kwa jina la Yesu ulidhihirika mbele ya macho ya baraza.
2. Waliweza kumshuhudia kiwete aliyekuwa kiwete tangu tumboni mwa mamaye akisimama mbele yao akiwa mzima kabisa.
3. Tena, tunaona ukweli na uwazi dhahiri wa miujiza ya Biblia (angalia somo letu 3:9-11, 16).

**4:15-18)**
1. Mst.15 Petro na Yohana waliamuriwa kuondoka katika baraza ili wajumbe wa Sanhedrin waweze kujadili swala hilo wao binafsi.
2. Mst.16 tunaona walijadili namna ya kuwatenda mitume.
   a. Sanhedrin walitambua kukabiliwa na shida kubwa!
   b. Walitaka kuwatenda kitu fulani mitume.
   c. Walakini, walitambua Yerusalem yote ilijua miujiza ya ajabu ambayo mitume waliitenda.
   d. Na Sanhedrin walitambua wasingeliweza kupinga ukweli wa miujiza hiyo.
3. Mst.17 Wajumbe wa baraza waliamua kutoa onyo kali mitume wasinene tena kwa yeyote kwa mamlaka ya Kristo ("katika jina lake").
   a. Kusudi lao katika kutoa vitisho hivi vikali ilikuwa kuzuia ushawishi na mafundisho ya Ukristo yasienee katika watu.
4. Mst.18 Sanhedrin waliwaita tena mitume ndani na kuwaamuru wasinene tena kwa mamlaka ya Yesu.

**4:19,20)**
1. Petro na Yohana tena walijibu kwa ujasiri mkubwa na kwa kupinga dhahiri agizo hilo lisilo la haki ambalo Sanhedrin ilikuwa imetoa.
2. Kubainisha zaidi, katika mst.19, Petro na Yohana waliuliza baraza ikiwa ni haki mbele za Mungu kwa mitume kuwasikiliza wao zaidi kuliko Mungu.
   a. Kwa maneno mengine, mitume walikuwa wakisema Mungu aliwaamuru kwenda na kuhubiri kwa mamlaka ya Mwanawe mpendwa, Yesu.
   b. Lakini Sanhedrin waliamuru wasinene au kufundisha tena kwa mamlaka ya Yesu.
   c. Hivyo basi, Petro na Yohana walijibu dhahiri kwamba ni heri kumsikiliza Mungu (kuliko baraza) kwa kuendelea kunena na kufundisha kwa mamlaka ya Kristo.
3. Basi, katika mst.20, Petro na Yohana walifanya zaidi ya kuhusisha tu!
   a. Walidai kuwa wangelisema mambo yale tu ambayo walisikia na kuyaona.
   b. Ndiyo kusema, walijua walikuwa na wajibu kutaarifu matendo na maneno ya Mungu mwenyezi na Mwanawe mpendwa, Yesu Kristo.
   c. Na hakuna mtu ambaye kisheria angeweza kuwazuia kufanya hivyo!
4. Kabla ya kuondoka mst.19,20 ebu tuone matumizi yake.
   a. Ni jinsi gani Petro na Yohana waliamua kuchukua uamuzi huo katika swala hilo?
      (1) Ni dhahiri kwamba walikuwa na uhuru wa kuamua katika swala hili!
      (2) Lakini, walichukuaje uamuzi wa namna hiyo?
      (3) Kulingana na mst.19, mitume walitaka kuamua jambo "lililo haki mbele za Mungu"!
      (4) Moyo wa ujasiri ajabu!
      (5) Je, mimi nina moyo wa jinsi hii?
      (6) Wewe je, una moyo gani?
      (7) Linga. 2Kor.5:9-11.

**4:21,22**
1. Katika mistari hii miwili kuna mambo ya msingi ya ufunguo kadhaa yamebainishwa:

   a. Sanhedrin iliwatishia Petro na Yohana kwa mara nyingine tena.
   b. Lakini baada ya vitisho hivyo, waliwaachilia huru mitume waondoke.
   c. Wajumbe wa Sanhedrin waliogopa kuwaadhibu mitume kwa kuwa walitambua wangewakasirisha watu.
   d. Jambo hilo ni kweli kwa kuwa watu walimtukuza Mungu kwa miujiza ya uponyaji iliyotendeka juu ya kiwete.
   e. Miujiza hiyo ilikuwa ya kustaajabisha mno kwa kuwa kiwete huyo alikuwa katika hali hiyo kwa miaka arobaini.
2. Muhtasari wa 4:13-22, Sanhedrin inawashurutisha Petro na Yohana wasihubiri.
   a. Mst.13 Sanhedrin ilistaajabia ujasiri wa Petro na Yohana.
      (1) Walistaajabu kwa kuwa Petro na Yohana hawakusoma hapo nyuma hata kuwa na umahiri wa kusema hadharani.
      (2) Hatimisho la Sanhedrin lilikuwa Petro na Yohana "*walikuwa pamoja na Yesu*"!
   b. Mst.14 kiwete aliyeponywa alikuwa akisimama mbele ya Baraza uthibitisho usiopingika kwamba Petro na Yohana walitenda muujiza kwa mamlaka ya Yesu.
   c. Mst.15 Petro na Yohana waliamuriwa kuondoka katika Baraza ili kwamba wajadili swala hilo kwa siri.
   d. Mst.16 Sanhedrin walitaka kuwatenda jambo fulani mitume, lakini walitambua kwamba Yerusalem yote iliona muujiza ambao ilikuwa vigumu kuukana.
   e. Mst.17,18 Sanhedrin waliwatishia mitume wasinene tena katika jina la Yesu ili kwamba Ukristo usienee.
   f. Mst.19 Petro na Yohana waliuliza Baraza ikiwa ni haki kwao kulitii Baraza kuliko kumtii Mungu.
   g. Mst.20 Petro na Yohana walilieleza Baraza wangezungumza tu mambo waliyoyaona na kuyasikia.
   h. Mst.21,22 Sahendrin waliwatishia mitume tena, lakini waliwaacha waondoke huru.
      (1) Baraza liliongopa juu ya kuwatenda mitume jambo lolote kinyume, wangewakasirisha watu.
      (2) Ni kwa sababu watu walimtukuza Mungu kwa ajili ya miujiza hiyo.

### f. (4:23-31) SALA YA MITUME KUPATA UJASIRI

**4:23,24)**

1. Baada ya Baraza kuwaachilia Petro na Yohana, walirejea na kuwa na mitume wenzao.
2. Waliporejea, waliwaeleza mambo yote ambayo Sanhedrin iliwaagiza.
3. Katika mst.24 tunaona wakisali mbele za Mungu:
4. Tafadhali angalia mambo kadhaa kuhusu sala yao:
   a. Kwanza, waliomba kwa "*moyo mmoja*."
      (1) Kama tulivyotangulia kuona awali, watu hawa waliungana katika mawazo, matendo, na katika sala!
   b. Pili, mitume walimwendea Mungu kwa heshima nyingi, wenye mioyo ya kicho.
      (1) Walimtaja kuwa ni "Bwana."
         (a) Lakini neno la asili la Kiyunani lililotumiwa na Roho Mtakatifu katika swala hili ni tofauti (δεστιοτησ) kama lilivyotumika kwa kawaida.
         (b) Neno hili linamtaja kiongozi mwenye mamlaka na nguvu nyingi.
         (c) Basi, kwa staha walitambua uwezo wa Mungu mwenyezi na wakimwita ili aweze kuwasaidia ujasiri.
      (2) Na pia walitaja uweza mkuu wa Mungu walipomtambua kuwa ndiye Muumba wa "mbingu na nchi na bahari, na vyote vilivyomo ndani yake."

**4:25-28)**

1. Katika mst.25,26 mitume walimnukuu Mungu kama alivyonena kwa kinywa cha Daudi.

a. Hii ni ishara nyingine ya uvuvio kamili wa Biblia wa kunena moja kwa moja!
b. Nukuu hii inatoka Zab.2:1,2.
c. Katika fungu hili la Zaburi Daudi aliuliza kwa nini wakuu na watu wa mataifa waliasi juu ya Mungu na Kristo wake, k.m. Mpakwa mafuta wake.

2. Katika mst.27 Petro alitoa tafsiri iliyovuviwa ya Zaburi hii.
   a. Alisema Zaburi hii ilikuwa unabii wa kukataliwa kwake Kristo, Masihi na wakuu pamoja na mataifa ya ulimwengu.
   b. Petro alibainisha baadhi ya walioasi kuwa ni Herode, Pilato, Mataifa, na taifa la Israeli.
   c. Alimtambulisha huyo waliyeasi juu yake kama mtumishi Mtakatifu wa Baba, Yesu, ambaye Baba "amempaka mafuta" (k.m. aliyewekwa kuwa Mfalme).
3. Katika mst.28 Petro alibainisha kwamba, ingawa watu hawa waliasi juu ya Yesu, wakitekeleza hasa mashauri ya Mungu aliyokusudia kufanya tangu mwanzo.
   a. Baba alikusudia Mwanawe kuteseka na kufa ili kwamba wanadamu waweze kupata faida ya dhabihu ya pekee yenye uwezo wa kutoa msamaha wa dhambi (Ebr.10:1-18).
   b. Kwa hiyo, watu waasi hawa walikuwa na jambo moja akilini mwao walipomkana na kumwua Yesu.
   c. Na, Mungu aliruhusu wafanye kulingana na uhuru wa mapenzi yao.
   d. Lakini mapenzi ya Baba yalitimia katika kifo cha Mwanawe mpendwa ili kuwezesha ukombozi na msamaha wa dhambi!
   e. Linga. somo letu la 2:33 na 3:18.

**4:29-31)**

1. Katika mistari hii mitume kwanza walitaja "vitisho" vya Baraza (Sanhedrin).
2. Vitisho hivyo vikiwa akilini, ni jambo la kufurahisha kuona sababu ya mitume kusali!
3. Wangeweza kusali kwa ajili ya usalama na afya zao, au kwa ajili ya maangamizi ya maadui yao.
4. Lakini, hawakufanya hivyo!
5. Kinyume chake, mitume walimwomba Mungu awasaidie kunena neno lake kwa ujasiri.
   a. Kwao, kazi yao ya kuhubiri, kufundisha, na kuishi katika neno la Mungu ndilo jambo waliloliwekea kipaumbele.
   b. Linga. Efe.6:18-20.
   c. Linga. 2Thes.3:1.
6. Katika mst.30 mitume walirejea katika karama za Roho Mtakatifu kama vile uponyaji, ishara, na ajabu.
   a. Kama tulivyoona, karama hizi za miujiza zilikuwa sambamba na neno la Mungu.
   b. Kubainisaha zaidi, zilitumika kufunua na kuthibitisha neno hilo karne ya kwanza (Linga. Ebr.2:3,4; Mk.16:20).
   c. Miujiza hii ilikuwa ifanywe kwa mamlaka ya mtumishi Mtakatifu wa Baba -Yesu.
7. Katika mst.31 tunaona Mungu akijibu maombi yenye bidii, kicho, yafaayo kwa mitume.
8. Kujibu kwake Mungu maombi ya mitume kumeelezwa kwa njia nyingi.
   a. Kwanza, mahali walipokuwepo mitume palitikisika.
      (1) Neno lililo tafsiriwa "palitikisika" linamaanisha mtikisiko bila mpangilio.
      (2) Pengine hili linamaanisha tetemeko la namna fulani lilitukia.
   b. Pili, mitume hawa wote walijazwa na Roho Mtakatifu.
   c. Tatu, mitume wakanena neno la Mungu kwa ujasiri, ambalo ndilo swala haswa waliloliomba!
9. Ingawa kilichotukia hapa kinalingana na kile kilichotukia siku ya Pentekoste, haionyeshi hapa kuwa ni ubatizo mwingine wa Roho Mtakatifu.
10. Tafadhali niruhusu nikuelezee kwa nini nashikilia msimamo huu kwa kutoa sababu mbili:
   a. Kwanza, mitume walikuwa tayari wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu mara moja, katika kutekeleza ahadi zake Yesu kwao (linga. Mdo.1:5,8; 2:1-4).

(1) Baada ya hapo, sehemu mbalimbali zimetajwa kwamba mitume waliweza kutenda miujiza (2:4-13; 14-36, 43; 3:1-11).
(2) Basi, hapakuwa na umuhimu kwa mitume kubatizwa katika Roho Mtakatifu tena kwa kuwa tayari walikuwa na uwezo wa kutenda miujiza.
(3) Siyo tu hivyo, bali ingeonekana kuwa marudio juu ya uwezo mkubwa wa Mungu kama kulikuwa na haja ya mitume kubatizwa kwa Roho Mtakatifu tena baada ya siku ya Pentekoste.

b. Sababu ya pili ni maoni kwamba hili siyo tukio la pili la ubatizo wa Roho Mtakatifu kama tunavyoona katika Mdo.11:15-17.

11. Muhtasari wa 4:23-31, sala ya mitume kwa ajili ya kupata ujasiri.
    a. Mst.23 Petro na Yohana walirejea na kuwa pamoja na mitume wenzao na kuwataarifu yote waliyoelezwa na Baraza (Sanhedrin).
    b. Mst. 24 waliomba kwa Mungu mwenye uweza wote.
    c. Mst.25,26 Mitume walinukuu kutoka katika Zab.2:1,2, unabii juu ya kukataliwa kwake Kristo wa Mungu (mpakwa mafuta) na wakuu pamoja na mataifa.
    d. Mst.27,28 mitume walitoa tafsiri iliyovuviwa ya Zaburi hiyo.
       (1) Herode, Pilato, Mataifa, na taifa la Israeli waliasi.
       (2) Waliasi juu ya Mtumishi Mtakatifu wa Mungu Yesu ambaye Mungu alimtia mafuta kuwa Mfalme.
       (3) Wakisha kutenda kwa uhuru wa mapenzi yao, kusudi la Mungu lilijulikana kwa kumruhusu Mwanawe ajitoe mwenyewe kama sadaka kwa ajili ya dhambi.
    e. Mst.29 Mitume walimwomba Mungu kuwasaidia kulinena neno lake kwa ujasiri.
    f. Mst.30 Mitume walitaja karama za miujiza za Roho Mtakatifu ambazo zilikwenda sambamba na ufunuo pamoja na kuthibitisha neno la Mungu karne la kwanza.
    g. Mst.31 Mungu alijibu sala ya mitume kwa njia mbalimbali.
       (1) Mahali walipokusanyika palitikisika.
       (2) Mitume wote wakajazwa Roho Mtakatifu.
       (3) Na mitume wakalinena neno la Mungu kwa ujasiri.
12. Mtazamo kwa ufupi wa 3:1-4:31, Miujiza ya Petro na Yohana / Upinzani wa Masadukayo.
    a. 3:1-13 Petro amemponya kiwete.
    b. 3:12-26 Roho Mtakatifu (kupitia Petro) alithibitishia makutano makosa.
       (1) 3:12-17 *Yesu*: Aliuawa na Wayahudi / Alifufuliwa na kuinuliwa na Baba.
       (2) 3:18-26 *Yesu*: Alitabiriwa na manabii / masharti yenye uvuvio ya jinsi ya kupata msamaha.
    c. 4:1-4 Petro na Yohana walitiwa kizuizini.
    d. 4:5-12 Petro alihubiri mbele ya Sanhedrin – wokovu ni katika jina la Kristo tu.
    e. 4:13-22 Sanhedrin aliwaamuru Petro na Yohana wasihubiri.
    f. 4:23-31 Sala ya mitume ya kuwa majasiri.
13. Mtazamo kwa ufupi wa 4:32-5:11, kupambana na matatizo ya jamii / Anania na Safira wanadanganya.
    a. 4:32-4:37 Kanisa la awali lilishirikiana bila uchoyo.
    b. 5:1-11 Anania na Safira wanadanganya na kufa.

## 2. (4:32-5:11) KUPAMBANA NA MATATIZO YA JAMII / ANANIA NA SAFIRA WANADANGANYA.

### a. (4:32-37) KANISA LA AWALI LILISONGA MBELE

**4:32)**

1. Luka tena alielezea kanisa la awali kuwa liliungana (“moyo mmoja na roho moja”).
2. Na walikuwa wakishirikiana pamoja mali zao za duniani ndugu wote.

3. Ndugu hawa walimpenda Bwana kweli na kila mmoja wao na waliudhihirisha upendo huo kwa kutokuwa wachoyo kabisa (Math.16:24).
4. Angalia somo letu la 2:44, 45.

**4:33)**

1. Kama tulivyoona, mitume walinena wakishawishi na kutenda miujiza ya nguvu ili kuthibitisha neno walilolinena.
2. Kama tulivyoona, somo lao kubwa walilonena ni ufufuo wa Bwana Yesu.
   a. (Linga. somo letu la 1:22 na 2:32 umuhimu wa ufufuo).
3. Kama matokeo ya maisha yao yaliyojaa upendo pasipo unafiki na mahubiri mengi na miujiza ya mitume, "*neema nyingi ikawa juu yao wote*."
   a. Neno lililotafsiriwa "neema" linaweza pia kutafsiriwa "pendeza" (favor) au "mapenzi mema" (good-will).
   b. Hakika kabisa, linarejea hili ukweli kwamba watu wengi katika Yerusalem waliwatazama Wakristo wa karne ya kwanza na kuwakubaliwa au kupendezwa nao.
   c. Walipendezwa kweli kweli na kuvutiwa na maneno na matendo ya kanisa.
      (1) Angalia somo letu katika 2:47.

**4:34,35)**

1. Tena tunaona upendo, usio na ubinafsi, matendo ya ukarimu ya Wakristo wa awali!
2. Wenye viwanja au nyumba waliuza na kutoa mapato mbele ya mitume.
3. Kadhalika, mitume waligawanya mali hizo "*kwa kadiri ya hitaji la kila mmoja*."
4. Matokeo yake, hakuna hata mmoja aliyekuwa na hitaji la maisha.
5. Wakristo wa kwanza hawa walikuwa familia iliyoshikamana kwa karibu walitambua miongoni mwao aliyekuwa na hitaji.
6. Siyo tu hivyo, bali waliokuwa na vitu vyao walivitoa kwa hiari ili kusaidia kwa hao walio vihitaji!
7. Hakika walimjali kila mtu!
8. Mfano wa ajabu kwetu sisi wa kuiga!
9. Linga. Mith.28:27; Yak.2:15,16; 1 Yoh.3:17.
10. Ili kuona kwa nini swala hili si ujamaa (communism), tafadhali jifunze notisi zetu katika 2:44,45.

**4:36,37)**

1. Katika mistari hii, Barnaba alitoa mfano wa ukarimu, roho ya upendo ya Wakristo wa awali.
2. Aliuza kiwanja chake na kutoa fedha kwa mitume.
3. Angalia mambo mengine kadhaa yanayonenwa kuhusu Mkristo huyu mkarimu:
   a. Kwanza, mitume walimpatia jina la "Barnaba."
      (1) Likimaanishwa haswa "mwana wa mafunzo au faraja."
      (2) Kama tutakavyoona katika somo letu katika kitabu cha Matendo, maelezo hayo ni sahihi kabisa kwa huyu mtu asiyemchoyo mtumishi wa Bwana (linga. Mdo.9:27; 11:19-30; 13-15 n.k.)!
   b. Pili, alikuwa Mlawi.
      (1) Alitokana na Lawi, mmoja wa wana wa Yakobo.
      (2) Walawi ndio walihudumu katika mambo ya dini mbele za Bwana (Kut.32:26-29; Hes.3:9, 11-13; 8:16-18).
      (3) Walawi walitoka katika familia ya Haruni walitumika kama makuhani chini ya sheria ya Musa (Kut.28:1).
   c. Tatu, Barnaba alitoka katika Kisiwa cha Kipro.
4. Muhtasari kwa ufupi wa 4:32-37, Kanisa lilishirikiana pasipo choyo.
   a. Mst.32 Wakristo wa awali waliungana na kuwa vitu vyote shirika.

b. Mst.33 Mitume walishuhudia ufufuo wa Kristo kwa nguvu nyingi na kanisa likakubalika mno.
c. Mst.34,35 Waliokuwa na viwanja na nyumba waliuza na kutoa fedha kwa mitume.
   (1) Mitume wakawagawia waliokuwa wahitaji.
   (2) Matokeo yake, hawakuwepo Wakristo waliohitaji chochote ili kuishi.
d. Mst.36,37 Barnaba aliuza kiwanja chake na kutoa fedha mbele za mitume.

## b. (5:1-11) ANANIA NA SAFIRA WANADANGANYA NA KUFA

**5:1,2)**
1. Anania na Safira waliuza moja ya mali zao.
2. Walizuia sehemu ya thamani na kutoa fungu mbele za mitume.
3. Kama matokeo yake, ni dhahiri kwamba Anania na Safira walificha kwa siri sehemu ya thamani wakati huo wakijifanya kutoa thamani yote mbele za mitume.

**5:3,4)**
1. Katika mst.3 Petro alimweleza Anania kuwa alimdanganya Roho Mtakatifu na kuzuia sehemu ya thamani ya bei ya kiwanja.
2. Katika mst.4 tunajifunza mambo mengi ya kufurahisha:
   a. Kwanza, kabla ya Anania kuuza kiwanja, ilikuwa juu yake kufanya vyovyote alivyofikiri kuwa vyema ("haikuwa mali yako").
      (1) Jambo hili linadhihirisha kuwa Wakristo walikuwa na haki ya kumiliki mali zao binafsi.
      (2) Na pia linatueleza kuwa kuuza kwa mali zao ilikuwa swala la hiari yao wenyewe.
      (3) Ni jambo la kweli Wakristo wa karne ya kwanza Yerusalem "wakawa na vitu vyote shirika" waliuza mali na vitu vyao ili kwasaidia Wakristo waliokuwa wana mahitaji (4:32-37; linga. 2:44,45).
      (4) Hivyo basi, Wakristo siku hizi wana haki ya kumiliki mali zao binafsi!
   b. Pili, baada ya Anania kuuza kiwanja, alikuwa huru kufanya sawasawa na jinsi alivyotaka na kiwango ("haikuwa katika uwezo wako?").
      (1) Kwa kuwa thamani ilikuwa katika uwezo wao, wangeweza kuzuia yote au sehemu ya thamani yake.
      (2) Hili hapa linatueleza dhambi ya Anania na Safira si kuzuia sehemu ya thamani kwa ajili yao.
      (3) Hatimisho pekee tunaloweza kutoa ni dhambi ya kujifanya kutoa thamani yote ya kiwanja wakati walitoa haswa sehemu yake.
   c. Jambo la tatu la kufurahisha katika mst.4 ni kwamba Petro alisema Anania aliwajibika kwa kuamua kudanganya ("Ilikuwaje hata ukaweka neno hili moyoni mwako?").
      (1) Hata hivyo, katika mst.3, Petro alisema Shetani alimjaza Anania kusema uongo mbele ya Roho Mtakatifu.
      (2) Hili pekee linatuonyesha kuwa Shetani ana fungu katika uamuzi huu, na hivyo ndivyo alivyofanya Anania.
      (3) Math.4:3-11; 2 Kor.4:3,4; 11:3, 13-15; Yoh.8:44; 2 Kor.2:11.
      (4) 1 Pet.5:8.
      (5) Lakini, hawezi kumlazimisha mtu afanye kitu chochote. Kama tulivyojifunza awali, mwanadamu ana uhuru wa kuchagua!
         (a) Yakobo 4:7,8.
         (b) Waefeso 4:27.
         (c) Waefeso 6:10-13.
      (6) Basi, Shetani alimjaribu Anania kupitia njia (agents) zake.

(a) Lakini Anania alikuwa angali na uamuzi wa mwisho ama kumtii Mungu au Shetani.
(b) Na akahiari mwenyewe kuchagua kumtii Shetani na kumtenda Mungu dhambi.
(c) Kwa hiyo, Anania alikuwa awajibike kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe!

d. Jambo la nne la kufurahisha katika mst.4 ni Petro alivyomshutumu Anania kwa kumdanganya Mungu, na wala si wanadamu.
  (1) Basi, Anania si tu aliwadanganya wanadamu (k.m. mitume), bali pia alimdanganya Mungu.
  (2) Lakini, ni jinsi gani alimdanganya Mungu!
    (a) Anania alichanga fedha hizi kwa Bwana kwa ajili ya kazi ya kanisa.
    (b) Kwa kujifanya kutoa thamani yote kwa Bwana wakati haswa alitoa tu sehemu yake, alimdanganya Mungu!
    (c) Matokeo yake, alikuwa na hatia ya kujaribu kumdanganya Mungu.
  (3) Angalia pia katika mst.3 Petro alimshutumu Anania kwa kumdanganya Roho Mtakatifu.
    (a) Walakini, katika mst.4 Petro alimshutumu Anania kwa kumdanganya Mungu.
    (b) Kwa hiyo, tunahatimisha kuwa Roho Mtakatifu ni Mungu, k.m. yeye ni Mungu, Mtakatifu.
    (c) Linga. Math.28:19; 2 Kor.13:14.

**5:5,6)**

1. Anania aliposikia mashutumu ya kweli toka kwa Petro, akafa mara moja!
   a. Hatuoni kitu chochote kwamba Petro alihusika katika kifo hiki.
   b. Basi, inadhihirika kuwa Mungu alitumia kitu chochote kile kusababisha kifo cha Anania kutokana na dhambi yake mbaya ya kumdanganya Mungu.
   c. Kwa hiyo, hii ni taarifa ya kwanza juu ya nidhamu ya kanisa.
   d. Na lilitendwa na Mungu mwenyezi kwa jinsi ya ajabu na kudhihirika!
2. Matokeo yalikuwa wote waliosikia tukio hili waliingiwa na hofu.
3. Baada ya kufa Anania vijana kadhaa walimzika.

**5:7-11)**

1. Katika mst.7 tunajifunza Safira alikwenda mahali walipokuwepo mitume saa tatu baadaye baada ya kifo cha mumewe.
2. Pia, fungu linasema hakujua nini kilitokea juu ya mumewe.
3. Katika mst.8 Petro alimwuliza Safira iwapo waliuza kiwanja kwa kiasi gani.
   a. Kweli, Petro alimwuliza ikiwa kiwanja waliunza kwa kiasi alichodai Anania.
   b. Inaonekana kuwa Petro alikuwa akitoa fursa ili Safira aeleze ukweli kwa kutaja kiwango haswa walichouzia kiwanja kinyume na kile walichobuni kuwa ndicho.
   c. Safira alijibu kwa kutaja kiasi ambacho Petro aliuliza kuwa ndicho kiasi sahihi.
4. Katika mst.9,10 Petro alimjibu Safira kwa kuzidi kudanganya.
   a. Alimwuliza Safira kwa nini yeye na Anania walikubaliana kumjaribu Roho Mtakatifu.
     (1) Lakini ni jinsi gani Anania na Safira walimjaribu Roho Mtakatifu?
       (a) Kama tulivyoona, walijaribu kuwadanganya mitume juu ya thamani waliyouzia kiwanja.
       (b) Na mitume walikuwa wakifunua neno la Mungu na kutenda miujiza kwa uweza wa Roho Mtakatifu (linga. 2:1-13; 3:1-11, n.k.).
       (c) 1 Kor. 12:10.
       (d) Basi, kama Anania na Safira wangefanikiwa kuwadanganya mitume, wangelifanikiwa kumdanganya Roho Mtakatifu!
       (e) Hilo ndilo kosa lao la kumjaribu Roho Mtakatifu!
   b. Petro pia alimweleza Safira juu ya watu waliomzika mumewe walikuwa wakisimama hapo na walikuwa wamtoe nje.

(1) Maelezo haya ni dhahiri kwamba Safira alikuwa anakwenda kufa.
(2) Na katika mst.10 Safira alikufa mara moja, akabebwa nje, akazikwa karibu na mumewe.

5. Katika mst.5 tunaona matokeo yake ni nidhamu ya kwanza kabisa kuandikwa ambayo Mungu mwenyezi aliifanya.
   a. Waliokuwemo katika kanisa la Bwana wakaigiwa na hofu kubwa.
   b. Siyo tu waliokuwa ndani ya kanisa, bali pia wale wote waliokuwa nje na kusikia habari hizi waliigiwa na hofu kubwa.
   c. Waliona uwezo wa kimiujiza wa mitume wa kuweza kuona ndani ya moyo wa mtu na kutambua unafiki na uongo.
   d. Waliona jinsi Mungu alivyotenda kwa uweza mara moja juu ya dhambi, ambayo ililinajisi kanisa lililonunuliwa kwa damu ya Mwanawe mpendwa.
   e. Fungu hili na mengine mengi yanatufundisha kuwa na kicho hai, heshima, na hofu mbele za Mungu Mwenyezi (linga.10:34,35; Rum.3:18).
   f. Tunaelezwa umuhimu aliouweka Mungu juu ya usafi wa kanisa (linga. Efe.5:25-27)?
   g. Tunafundishwa kuhusu umuhimu wa nidhamu ya kanisa (linga. 1 Kor.5; 2 Thes.3:6, 14, 15)?
6. Mtazamo kwa ujumla wa 5:1-11, Anania na Safira wanadanganya na kufa.
   a. Mst.1 -Anania na Safira waliuza kiwanja chao.
   b. Mst.2 – Walitoa sehemu ya thamani yake kwa mitume na kuzuia sehemu ya thamani yake kwa ajili yao wenyewe.
   c. Mst.3 Petro aliwashutumu Anania na Safira kwa kumdanganya Roho Mtakatifu kwa hila wakizuia sehemu ya thamani kwa ajili yao.
   d. Mst.4 Petro alitoa mambo manne muhimu:
      (1) Kabla ya Anania kuuza kiwanja, kilikuwa katika uwezo wake kukifanya lolote.
      (2) Baada ya Anania kuuza kiwanja, alikuwa huru kufanya lolote kwa thamani yake.
      (3) Anania aliwajibika kutokana na udanganyifu huo.
      (4) Tena Anania alikuwa na hatia ya kumdanganya Mungu, na wala si wanadamu tu.
   e. Mst.5,6 Anania akafa na kuzikwa, watu waliosikia kifo chake wakaigiwa na hofu kubwa mno.
   f. Mst.7 Safira alifika mbele za mitume saa tatu baada ya kifo cha mumewe, hata hivyo hakujua kilichokuwa kimetukia.
   g. Mst.8 Petro alimhoji Safira iwapo waliuza kiwanja kwa thamani hiyo na Safira akajibu ndiyo, waliuza kwa thamani hiyo.
   h. Mst.9 Petro alimshutumu Safira kwa kukubaliana na Anania ili kumjaribu Roho Mtakatifu kupitia uongo wao.
   i. Mst.10 Safira akafa papo hapo na kuzikwa.
   j. Mst. 11 Waliokuwemo kanisani na wale wa nje waliosikia jambo hili waliingiwa na hofu kubwa.
7. Mtazamo kwa ufupi wa somo letu la Matendo na kuangalia sehemu tatu zifuatazo za kielelezo chetu:
   I. (1-7) Sehemu ya Kwanza: Kuanzishwa kwa kanisa Yerusalem.
      A. (1 na 2) Kuanzishwa kwa kanisa kwa nguvu nyingi.
         1. (1) Kungojea kwa ahadi.
         2. (2) Ahadi imetimizwa na kuanzishwa kwa kanisa.
      B. (3-7) Kanisa lilizidi kukua Yerusalem.
         1. 3:1-4:31 Muujiza wa Petro na Yohana / Upinzani wa Masadukayo.
         2. 4:32-5:11 Kupambana na matatizo ya jamii / Anania na Safira wanadanganya na kufa.
            a. 4:32-37 Kanisa la awali lilishirikiana pasipo choyo.
            b. 5:1-11 Ananania na Safira wanadanganya na kufa.
         3. 5:12-42 Mafanikio na upinzani kuinuka upya.

   4. 6:1-7 Kuchaguliwa kwa saba.
8. Mtazamo kwa ujumla wa 5:12-42, Mafanikio na kuinuka upya kwa upinzani.
   a. 5:12-16 Miujiza ya mitume / Watu wengi wanazidi kuongezeka.
   b. 5:17-28 Mitume kuwekwa gerezani / kutolewa ndani kimiujiza / mahubiri.
   c. 5:29-32 Mitume wanamhubiri Yesu aliyeinuliwa mbele ya baraza.
   d. 5:40-42 Kupigwa kwa mitume / kufurahi / Yesu ahubiriwa.

### 3. (5:12-42) MAFANIKIO NA UPINZANI KUINUKA UPYA

#### a. (5:12-16) MIUJIZA YA MITUME / WATU WANAZIDI KUONGEZEKA

**5:12,13**)
1. Tena madai kwamba mitume walifanya miujiza mingi kati ya watu.
   a. Maelezo haya yanathibitisha zaidi kuwa ni mitume tu wa Kristo na ni hao pekee mitume wa Kristo waliobatizwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste.
   b. Walikuwa hao tu walioweza kufanya miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu hadi kufikia hapa wakati huu.
   c. Linga. somo letu katika 2:4, 43, 3:1-11.
2. Luka pia alirudia ukweli kwamba mitume waliungana pamoja ("kwa nia moja").
   a. Hii ilikuwa moja ya picha nzuri ya tabia za kanisa la awali!
   b. Linga. 2:1, 42, 44, 46; 4:32.
3. Katika mst.12 Luka alibainisha kuwa hakuna mtu aliyethubutu miongoni mwa Wakristo kuambatana na mitume.
   a. Baada ya kuona uweza wa miujiza mikubwa ya mitume, kubainika kwa udanganyifu na unafiki, na kuhubiri neno la Mungu kwa ujasiri mkubwa, watu wakawahofu mitume wa Kristo.
   b. Ni kwamba, walikuwa na staha kubwa kwa mitume na kuhofu na kuwaheshimu kama watu ambao Mungu alifanya kazi kubwa kupitia wao.
   c. Kutokana na hofu hiyo kubwa, watu walionyesha heshima zao kwa mitume kama watu ambao hawakujulikana kuwa kama hivi hapo nyuma.

**5:14)**
1. Mara nyingine tena tunaona kukua kwa kanisa la awali kwa kushangaza ("walioamini wakazidi kuongezeka", "wengi."
2. Kama tulivyoona hapo nyuma, haya ni matokeo ya ukweli mwingi:
   a. Mahubiri ya nguvu, mafundisho, na kuishi kwa injili yenye utukufu wa Kristo.
   b. Miujiza ya nguvu ya mitume.
   c. Na sasa, kifo cha kushangaza cha Anania na Safira kwa dhambi yao mbaya juu ya Mungu.

**5:15,16**)
1. Mistari hii miwili inarejea nyuma katika mst.12 ambapo panasema mitume walitenda miujiza mingi sana kati ya ndugu.
2. Watu wa mji wa Yerusalem na nje ya Yerusalem waliletwa mbele ya mitume ili waweze kuponywa.
3. Hili linajumuisha wagonjwa na hao waliteswa na pepo wachafu (mapepo).
4. Mwishoni mwa mst.16 tafadhali angalia tofauti nyingine kubwa kati ya miujiza ya kweli ya kibiblia na miujiza ya leo ya kuiga.
   a. Tofauti ni kwamba mitume walipofanya miujiza ya uponyaji kwa "*wote waliponywa magonjwa yao*."
   b. Tafadhali linganisha taarifa hiyo na wanaodai kutenda miujiza leo inapojulikana kuwa watu wote hawakuponywa!

   c. Tunalinganisha hivyo, tunaona kwamba watu wa leo wanaodai kufanya miujiza ni uongo kabisa!
   d. Tafadhali angalia maelezo katika 3:9-11 kwa uthibitisho zaidi kuhusu ukweli huu.
5. Mtazao kwa ufupi wa 5:12-16, Miujiza ya mitume / Watu wengi walizidishwa.
   a. Mst.12 Mitume walitenda miujiza mingi na kanisa liliungana pamoja.
   b. Mst.13 Wakristo wengine walikuwa na kicho hai, staha, na mitume wakaheshimiwa.
   c. Mst.14 Kanisa likakua kwa haraka, watu wengi wakiongezeka.
   d. Mst.15,16 Mitume waliwaponya watu wote wakiwajia kutoka ndani na nje ya Yerusalem.

### b. (5:17-28) MITUME KUTIWA NDANI / KUACHIWA HURU KIMIUJIZA / MAHUBIRI

**5:17-21)**
1. Katika mst.17,18 kuhani mkuu na Masadukayo wengine, wakajaa wivu na kuwakamata mitume na kuwatia gerezani.
   a. Kumbuka vitisho vya baraza (Sanhedrin) katika mst.4:17-21.
2. Katika mst.19,20 malaika kutoka mbinguni kimiujiza aliwatoa gerezani mitume.
   a. Malaika aliwaagiza mitume kwenda hekaluni na kunena maneno yenye uzima kwa watu.
3. Mst.21 Mambo mawili yalibainishwa:
   a. Kwanza, mitume wakaingia hekaluni asubuhi na mapema na kufundisha, kama vile malaika alivyowaamuru kufanya.
   b. Pili, wakati huo huo, kuhani mkuu aliita mkutano wa Sanhedrin na kutuma gerezani ili mitume waletwe mbele ya baraza.
4. Kabla ya kuondoka katika mistari hii, tafadhali angalia jinsi Luka alivyoeleza ujumbe waliohubiri mitume hekaluni – "maneno yote ya uzima huu" (mst.20).
   a. Jinsi ilivyo ajabu kufundisha injili ya Kristo yenye kuokoa roho, kutoa uzima, kubadilisha maisha.
   b. Linga. Yoh.6:68.

**5:22,23)**
1. Waliotumwa kwenda kuwaleta mitume walirejea wakiwa na ujumbe huu:
   a. Gereza lilikuwa limefungwa salama kabisa kama vile hapakuwa na jambo baya lolote lililotokea.
   b. Kuingia ndani pengine walichokuwa wakifikiri, tafadhali chunguza mambo yafuatayo ili kuona kilichotokea:
      (1) Mitume hawakujali mamlaka ya baraza (Sanhedrin).
      (2) Basi, Sanhedrin waliwatia gerezani mitume.
      (3) Lakini, Mungu aligeuza hukumu ya Sanhedrin na kuwaachia huru mitume kwa njia ya miujiza ya ajabu.
      (4) Na mafundisho ya mitume yalienea mji mzima.
      (5) Basi, juhudi ya Sanhedrin ilikuwa bure.
2. Katika mst.25 mtu alitoa taarifa kwa Sanhedrin kwamba mitume walikuwa wakifundisha wazi wazi hekaluni.
3. Katika mst.26, 27 tunajifunza kuwa mkuu wa gereza na maofisa wengine kadhaa walikwenda kuwakamata mitume hekaluni.
   a. Angalia kwamba walikuwa makini ili kwamba wasije wakasababisha ghasia yoyote juu ya mitume.
      (1) Maofisa hao walikuwa makini wasije wakaleta vurugu kwa sababu waliogopa watu wangewapiga mawe ikiwa wangewatendea mabaya mitume.
      (2) Hivyo basi ni dhahiri, watu wa kawaida waliona mafundisho ya mitume na miujiza na kuhatimisha kuwa walikuwa watu wa Mungu.
      (3) Waliwastahi na kuwaheshimu mitume (linga. 4:21).

        (4) Kwa nini viongozi wakuu na maofisa hawa wasifikie waamuzi kama hayo?
    b. Maofisa wa Kiyahudi waliwaleta mitume mbele ya Sanhedrin.
4. Katika mst.28 kuhani mkuu alieleza mambo yafuatayo katika kuzungumza na mitume mbele ya baraza:
    a. Kwanza, aliwauliza mitume iwapo Sanhedrin haikuwakataza mitume wasifundishe katika jina (mamlaka) la Kristo.
        (1) Hakika, baraza liliamuru mitume wasinene katika jina la Yesu (4:18).
    b. Pili, kuhani mkuu alitambua kwamba mitume waliujaza Yerusalem na mafundisho (elimu) ya Yesu Kristo.
        (1) Basi, mitume hawakutii amri ya Sanhedrin!
        (2) Ni sifa ya ajabu juu ya mitume kwa kuhani mkuu kusema kwamba mji ulijaa mafundisho ya Yesu!
    c. Tatu, kuhani mkuu aliwashutumu mitume kwa kujaribu kuleta damu ya Yesu juu ya baraza.
        (1) Hili ni sawa na kusema kwamba mitume walikuwa wanasema kwamba baraza lilikuwa na hatia ya kumhukumu mtu asiye na hatia.
        (2) Kusema ukweli, mitume hawakuwaeleza watu kwamba Sanhedrin ilikuwa na hatia.
        (3) Bali, mitume walilieleza baraza moja kwa moja wao wenyewe kuwa na hatia (linga.4:10)!
5. Mtazamo kwa ufupi wa 5:17-28, Mitume kutiwa gerezani / kuachiwa huru kimiujiza / mahubiri.
    a. Mst.17,18 Masadukayo wakajaa wivu, wakawatia mitume gerezani.
    b. Mst.19,20 Malaika kimiujiza anawatoa mitume gerezani.
        (1) Malaika aliwaamuru kunena neno la uzima hekaluni.
    c. Mst.21 Mitume walifundisha neno, kama walivyoamuriwa.
        (1) Sanhedrin walituma watu gerezani ili mitume waletwe mbele ya baraza.
    d. Mst.22,23 Maofisa waliokwenda kuwachukua mitume hawakuwaona mitume gerezani.
        (1) Mbali na ukweli kwamba gereza lilikuwa limefungwa salama salimini.
        (2) Na kwamba walinzi walikuwa mbele ya lango kama ilivyotakiwa.
    e. Mst.24 Wakuu wa baraza walichanganyikiwa kwa taarifa hizo za mitume kutoka gerezani.
    f. Mst.25 Mtu akatoa taarifa kwa Sanhedrin kwamba mitume wanafundisha hekaluni.
    g. Mst.26, 27 jemedari na watumishi walikwena kuwakamata mitume.
        (1) Wakawa makini wasije wakasababisha ghasia yoyote ile.
        (2) Hilo lilitokea kwa kuogopa watu kuwapiga mawe iwapo wangewajeruhi mitume.
    h. Mst.28 Kuhani mkuu aliwaambia mitume mambo kadhaa:
        (1) Aliwauliza iwapo hawakukatazwa kunena mambo yoyote katika jina la Yesu.
        (2) Alitambua kwamba mitume walikuwa wameujaza Yerusalem na mafundisho ya Yesu.
        (3) Aliwashutumu kwa madai kuwa baraza lililikuwa na hatia ya kumsulibisha Yesu.

### c. (5:29-32) MITUME WALIMHUBIRI YESU ALIYEINULIWA MBELE YA BARAZA.

**5:29)**

1. Katika mst.28 kuhani mkuu alitoa shutuma aina mbili za msingi juu ya mitume:
    a. Kwanza, hawakutii amri ya Sanhedrin ya kutokufundisha yeyote tena katika jina la Yesu.
    b. Na pili, mitume walikuwa wakiwashawishi watu kwamba Sanhedrin ilikuwa na kosa la kumwua mtu asiye na hatia (Yesu).
2. Katika mstari huu Petro alijibu shitaka la kwanza kwamba mitume hawakutii Sanhedrin.
    a. Jibu la Petro lilikuwa walilazimika ("Ilipasa"), ("lazima") kumtii Mungu kuliko kuwatii wanadamu.

b. Kumbuka jinsi tulivyojifunza 4:19,20 ambapo tuliona mambo mawili:
   (1) Sanhedrin waliamuru mitume wasizungumze au kufundisha katika jina la Yesu tena.
   (2) Lakini Mungu aliwaamuru mitume kunena na kufundisha katika jina la Yesu.
c. Kwa kuwa kulikuwa na ugomvi baina ya Mungu alivyoamuru na watu (Sanhedrin), mitume walilazimika kumtii Mungu kuliko kuwatii wanadamu.
d. Na ndivyo walivyofanya mitume! Walizidi kufundisha na kuhubiri katika jina la Kristo!
e. Basi, hawakutii amri ya Sanhedrin bali wakatii amri ya aliye juu mno Mungu!
f. Kwa ujumla hii ni kanuni muhimu sana kwetu sisi sote leo.
g. Ndiyo kusema, panapokuwa na ugomvi baina ya amri za wanadamu na amri za Mungu juu ya neno lake, tunapaswa kumtii Mungu kuliko wanadam.
h. Ni sharti tumweke Mungu, Mwanawe, ufalme wake, na neno lake kwanza katika maisha yetu (Math.6:33; 10:28-39).
i. Kanuni hii inaweza na lazima itumike katika mahusiano yetu ya kila siku. Kwa mfano:
   (1) Kazini (mwajili / mwajiliwa).
   (2) Nyumbani (mume / mke).
   (3) Kwa serikali tawala.
   (4) Kanisani.

**5:30,31)**

1. Katika mistari hii miwili Petro alijibu shitaka la pili kwamba mitume walikuwa wakiwaeleza watu kuwa Sanhedrin ilikuwa na makosa kwa kumwua Yesu, ambalo halikuwa na hatia.
2. Kumbuka somo letu la mst.28 tulipoelezea mambo yafuatayo:
   a. Kwanza, mitume walikuwa na hatia ya kujaribu kuwashawishi watu kwamba Sanhedrin ilikuwa na hatia ya kumwua Yesu.
   b. Pili, mitume waliwaeleza moja kwa moja Sanhedrin kuwa walikuwa na hatia (linga. 4:10).
3. Katika mistari hii, mitume moja kwa moja waliishutumu Sanhedrin kwa makosa kama ifuatavyo:
   a. Kwanza, Mungu wa baba zao Waisraeli alimfufua Yesu kutoka kwa wafu.
      (1) Tena, mitume walihubiri ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu kama walivyofanya kila mara (linga. 2:24, 30-32; 3:15; 4:10).
      (2) Ufufuo wa Yesu pengine ulitajwa kwa sababu kadhaa:
         (a) Kwa kuwa ulikuwa utimilifu wa unabii ambao Wayahudi wangekuwa na habari nao (linga. Lk.24:44-46; Mdo.2:24-32).
         (b) Kwa sababu ufufuo wa Yesu toka ufuni ni ishara kubwa ya Baba kudhihirika juu ya Mwanawe mpendwa (linga. Rum.1:4).
         (c) Na kwa sababu ya ufufuo huo aligeuza mara moja hukumu yao isiyo haki waliyoitoa kwa kumwua Yesu iliyofanywa na watu wabaya kama vile Sanhedrin (linga. 2:22-24, 36; 3:13-15; 4:10).
   b. Maana ya pili waliyoitoa mitume ni kwamba Sanhedrin ilimwua Yesu kwa kumtundika mtini.
      (1) Tena, badala ya kuwaambia watu makosa ya Sanhedrin, mitume moja kwa moja wanawaambia Sanhedrin makosa yao.
      (2) Kweli, watu hawa wenye uvuvio walinena neno la Mungu kwa ujasiri na upendo kuwathibitishia dhambi zao!
      (3) Kwa bahati mbaya, ebu kumbuka kwamba kutundikwa mtini kulitazamwa na Wayahudi kama aliyelaaniwa na Mungu (Gal.3:13; Kumb.21:23).
      (4) Oh ni jinsi gani Baba na Mwanawe mpendwa walivyotupenda!
   c. Jambo la tatu ambalo mitume walieleza ni kwamba Baba alimwinua Yesu kuketi mkono wa kuume wa Baba.
      (1) Baba asingemwaachilia Mwanawe mpendwa kushikwa na mauti (2:24ff).

(2) Kinyume chake, alimfufua ukiwa ni ushindi juu ya kifo na kumtukuza kwa kumketisha upande wa kuume wa Baba na kumpatia mamlaka na nguvu (linga. 2:33; 3:13).
(3) Basi, Wayahudi (ukijumuisha Sanhedrin) walimwua Yesu, bali Baba alimfufua na kumtukuza kwa kumpatia mamlaka na nguvu!

d. Jambo la nne, ebu angalia sababu kadhaa kwa nini Baba alimwinua Yesu hata kuketi mkono wake wa kuume.
(1) Kwanza, ili awe mkuu (prince) na mwenye mamlaka.
(a) Mkuu (prince) ni mtawala mwenye nguvu na mamlaka.
1. Hili ni wazi kumhusu Yesu akishafufuka toka ufuni ili kutawala katika ufalme wake kama Mfalme, Masihi, Kristo.
2. Linga. 2:30-32.
(b) Pia, Yesu aliinuliwa na kuwa Mwokozi wa mwanadamu.
1. Hiyo ndiyo sababu iliyomfanya aje duniani (Lk.19:10; Math.1:21; 1 Tim.1:15).
2. Na angeweza tu kumaliza kazi yake akiwa Mwokozi baada tu ya kwenda yeye mwenyewe mbele ya Baba mbinguni akiwa dhabihu iliyotolewa mara moja kwa wakati wote kwa ajili ya dhambi (Ebr.9:11-14; Rum.4:25).
3. Ebr.5:9.
(2) Sababu ya pili kwa nini Yesu aliinuliwa na kuketishwa mkono wa kuume wa Baba ni "*awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi*."
(a) Lakini, ni jinsi gani Yesu "awape" toba na msamaha wa dhambi Waisraeli?
(b) Kama tulivyojifunza, kila mtu mwenye kuwajibika ana uhuru wa kuchagua.
1. Hilo linamaanisha kuwa kila mmoja wetu anaweza kuchagua kutubu ama kukataa kutubu.
2. Mungu hawezi kumlazimisha mtu yeyote yule kufanya hivyo!
3. Linga. Lk.13:3; Mdo.17:30,31.
(c) Basi ni jinsi gani Yesu alitoa njia ya toba na msamaha wa dhambi alivyoinuliwa na kuketishwa mkono wa kuume wa Mungu?
1. Upendo mwingi sana uliwatia (na sisi) msukumo mkubwa wa kuhutubu (2 Kor.5:14, 15).
2. Neno lake, lililofunuliwa na Roho Mtakatifu kupitia mitume na manabii waalivyoeleza (na sisi) juu ya hitaji na matokeo ya kutubu (2 Kor.7:9,10).
a. Na Roho Mtakatifu hakutumwa hadi baada ya Yesu alipoinuliwa na kuketishwa mkono wa kuume wa Baba (2:33).
3. Na damu yake ilitolewa kwa Baba ndiyo kitu pekee ambacho kingetoa msamaha wa dhambi uwezekane (Ebr.9:12-14, 22).
4. Lakini, ili kupokea msamaha wa upendo huo, neno hilo, na damu hiyo, mtu ni lazima kutii injili, ukijumuisha ubatizo majini, ili kupata msamaha wa dhambi kama zawadi toka kwa Mungu (cf. 2:37, 38; Rum.6:23).
5. Hivyo ndivyo Yesu alitoa njia ya toba na msamaha wa dhambi, sambamba na uhuru wa mtu wa kuchagua!

**5:32)**

1. Mitume walirejea ukweli wa kwamba ni "mashahidi" juu ya mambo ambayo Baba alifanya kwa njia ya Mwanawe.
2. Kusema ukweli, kuwa shahidi ni sifa kubwa kwa kazi ya mtume wa Kristo (1:8, 21, 22; 2:32; 3:15).
3. Kwa nyongeza, mitume walisema kuwa Roho Mtakatifu pia ni shahidi wa mambo hayo.
4. Na mwisho, mitume walieleza kuwa Roho Mtakatifu walipewa wote waliomtii.
5. Kwa sababu ya mafundisho mengine yanayofanana, ninaamini kuwa hapa ni dhahiri inalenga Roho Mtakatifu kukaa kwa hali ya kawaida. Kwa mfano:

a. Kukaa huko kwa kawaida kunafanyika tu mtu anapoiamini injili, kutubu dhambi, na kuzamishwa majini, basi hupokea msamaha wa dhambi (2:37,38).
b. Inatendeka hilo kwa mtu anapomtii Bwana kwa kutubu na kuwa mbali na dhambi zake na kurejea kwa Bwana, hivyo basi dhambi zake hufutwa (3:19).
c. Na inatokea tu baada ya mtu kumtii Bwana kwa kuamini na kubatizwa ili kuingizwa katika Kristo (Gal.3:26, 27; 4:6).
d. Tafadhali kumbuka kutoka katika somo la 2:38 hivyo kukaa kwa kawaida kwa Roho Mtakatifu hakuhusishi mambo mawili yafuatayo:
   (1) Karama za miujiza za Roho Mtakatifu zilizokoma karne ya kwanza.
   (2) Mwongozo wowote wa moja kwa moja, maelekezo, au ushawishi wa Roho Mtakatifu akilini mwetu.

6. Mtazamo kwa ufupi wa 5:29-32, mitume walihubiri Yesu aliyeinuliwa kwa baraza.
   a. Mst.29 Petro alijibu shitaka la kwanza la kuhani mkuu kwa ujasiri akisema kwamba imetupasa kumtii Mungu kuliko kuwatii wanadamu.
   b. Mst. 30,31 Petro alijibu shitaka la pili kwa kutoa pointi mbalimbali:
      (1) Baba alimfufua Yesu kutoka kwa wafu.
      (2) Hilo lilikuwa baada ya Wayahudi kumtundika mtini Yesu.
      (3) Baba alimwinua pia Yesu kumketisha mkono wa kuume katika nafasi ya nguvu na mamlaka.
         (a) Katika nafasi hiyo, Yesu alikuwa mkuu (prince) – anayetawala kama mfalme.
         (b) Yeye ni Mwokozi wa mwanadamu.
         (c) Na, alitoa msukumo kwa Israeli na wanadamu wote kutubu na akafanya uwezekano wa watu wote kupokea wa dhambi kwa njia ya kutii injili yake.

### d. (5:33-39) USHAURI WA GAMALIELI KWA BARAZA.

**5:33)**

1. Sanhedrin ilichomwa mioyoni mwao kwa yale yaliyonenwa na mitume.
2. Ukweli ni kwamba, walichukizwa mno hata kutaka kuwaua mitume.

**5:34-39)**

1. Katika mst.34 Gamalieli, ambaye ni mmoja wa wajumbe wa Sanhedrin, akasimama kuzungumza nao.
2. Angalia mambo kadhaa ya kufurahisha:
   a. Alikuwa Farisayo.
      (1) Kundi hili lilikuwa la Wayahudi wenye msimamo mkali (Mdo.26:5).
   b. Alikuwa mwalimu pia mtafsiri wa Sheria ya Musa ambaye aliheshimiwa na watu wote.
   c. Inawezekana kabisa kuwa ndiye mtu aliyemfundisha Paulo Sheria ya Musa (22:3).
3. Gamalieli aliamuru mitume kutolewa nje ya baraza ili kwamba Sanhedrin wajadili hili wenyewe.
4. Katika mst.36,37 Gamalieli alionya baraza kuwa makini jinsi watakavyowatenda mitume.
5. Katika mst.36,37 Gamalieli aliwataja watu wawili walioongoza uasi juu ya Uyahudi siku za nyuma.
   a. Alibainisha kwamba wote wawili walikufa na wafuasi wao walitawanyika viongozi wao walipokufa.
   b. Kwa maneno mengine uasi huo juu ya Uyahudi ulikoma wenyewe, bila kuathiri kabisa Uyahudi.
6. Katika mst.38,39 Gamalieli alishawishi baraza kuwachia huru mitume, kwa sababu mbili zifuatazo:
   a. Ikiwa kazi yao ni ya wanadamu (k.m. pasipo kukubaliwa na Mungu) haitafanikiwa.
      (1) Ingeangamia kama vile mifano miwili ambayo Gamalieli alikuwa tayari ameitaja.
   b. Ikiwa kazi ya mitume ilitoka kwa Mungu, Sanhedrin isingeliweza kuzuia na kushinda.

(1) Na iwapo watapinga kazi iliyokubaliwa na Mungu, watakuwa na hatia ya kupingana na Mungu.

### e. (5:40-42) MITUME WAPIGWA / WAFURAHI / WAHUBIRI KRISTO

**5:40)**

1. Sanhedrin walikubaliana na ushauri wa Gamalieli, lakini waliamua kuwapiga mitume na kuwaamuru walinene kwa jina la Yesu.
2. Neno lililotafsiriwa "wakawapiga" (δειραντεσ) ni neno linalobainisha bayana!
   a. Linamaanisha kuchana-chana ngozi kutokana na kupiga mijeredi!
   b. Hivyo basi, mitume walipigwa vibaya sana, sawa na kupigwa kwa mijeredi kwa Yesu alikopigwa kwa ajili yetu.
   c. Yesu alitabiri kuwa mitume wake wangepelekwa katika baraza na kupigwa (Math.10:17).
   d. Katika matukio kama hayo kwa kawaida Wayahudi walipiga mapigo 39 ili kuzuia kuzidisha kiwango kilichowekwa cha 40 na Sheria ya Musa (Kumb.25:3; 2 Kor.11:24).

**5:41)**

1. Mbali na kupokea mapigo makali kama hayo, mitume waliondoka katika baraza wakifurahi!
2. Walifurahia kwa kuwa walihesabu kuwa ni heri (na Sanhedrin) kuteswa kwa aibu kwa ajili ya Kristo.
3. Ni moyo wa ajabu mitume walikuwa nao!
4. Jinsi gani imani ilivyodhihirika na upendo katika Bwana!
5. Je, imani na upendo wangu ungekuwa kwa jinsi hii baada ya kupata adhabu isiyo na haki? Wewe je?
6. Tafadhali angalia mafungu yafuatayo katika somo la Mkristo na mateso:
   a. 2 Tim.3:12; Flp.1:29.
   b. Yak.1:2-4.
   c. Rum.5:3-5.
   d. 1 Pet.1:5-9.
   e. 1 Pet.4:12-19.
   f. Rum.8:17.
   g. 2 Tim.2:12.
   h. Hivyo ndivyo wafuasi wa awali wa Bwana waliweza kufurahi kuona ni heri kuteseka aibu kwa ajili ya Yesu!

**5:42)**

1. Mitume hawakuacha kufurahi katika mateso kwa ajili ya Yesu!
2. Kadhalika waliendelea kufundisha kuhusu Yesu, wakidharau wazi agizo la Sanhedrin.
3. Je, watu hawa waliamini kuwa Yesu ndiye Kristo, Mwokozi wa mwanadamu?
   a. Je, waliamini kuwa injili yake ilikuwa uwezo wa Mungu iokoayo roho za wanadamu?
   b. Je, walimpenda Yesu kuliko mtu yeyote au kitu chochote, hata kutokupenda maisha yao wenyewe?!
   c. Katika kujibu maswali haya, tafadhali angalia vikwazo ambavyo Sanhedrin waliviweka mbele ya mitume kujaribu kuwazuia.
      (1) 4:18 Waliamuru mitume wasihubiri katika jina la Yesu.
      (2) 4:17,21 Walitishia kwa ukali mitume.
      (3) 5:18 Wakawatia gerezani.
      (4) 5:33 Walitaka kuwaua mitume.
      (5) 5:40 Waliwapiga mitume na kuwaamuru wasinene.
4. Tafadhali angalia maelezo mazuri ya maamuzi yao kwa kuhubiri na kufundisha injili, bila ya kuwa na hofu:
   a. "kila siku."

(1) Walikuwa kila siku ya juma wakitenda kazi ya Bwana.
(2) Walikuwa wajumbe wa habari njema wasingeweza kusubiri na wala hawakusubiri kuwapa habari hiyo yenye baraka ya wokovu!

b. "katika hekalu."
(1) Mahali ambapo walizoea kumwabudu Mungu na kujifunza neno lake.

c. "na nyumba kwa nyumba."
(1) Mitume na Wakristo wa awali hawakuridhika kuhubiri na kufundisha mahali tu pa ibada.
(2) Hawakusubiri watu kuwajia wao mahali pa ibada.
(3) Kinyume chake, waliwaendea watu majumbani mwao wakikutana nao humo.
(4) Hakika, walimpenda Bwana, neno lake, na roho za thamani za wanadamu!
(5) Waliamini Mk.8:36!

d. "hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu Kristo."
(1) Walidumu kuwafundisha watu kuwa Yesu ni Kristo, Masihi, Mwokozi.
(2) Ujumbe huo wa wokovu ulikuwa ndani ya mioyo yao mfano wa moto na walipaswa kuwaeleza watu juu yake (Yer.20:9).
(3) Vitisho, kutiwa gerezani, kupigwa visingeweza kuwazuia kuhubiri Yesu Kristo na kusulimbiwa kwake kama nguvu na hekima ya Mungu (1 Kor.1:18-2:2)!

e. Ndio maana hivyo kanisa la awali likakua haraka sana?!
(1) Ni kielelezo cha ajabu kiasi gani watu hawa walikifuata!
(2) Tunaporejea katika mfano wa juhudi, upendo, malengo, ujasiri, na kuenea sehemu kubwa, tutakuwa na mfanikio kama yao!

5. Mtazamo kwa ufupi wa 5:33-39, Ushauri wa Gamalieli kwa baraza.
5:40-42 Kupigwa kwa mitume / kufurahi / Yesu anahubiriwa.
a. Mst.33 Sanhedrin ilichukizwa mno na ujumbe wa mitume hata wakataka kuwaua.
b. Mst.34, 35 Gamalieli alilionya baraza kuwa waangalifu na mambo ya kuwatenda mitume.
c. Mst.36,37 Gamalieli alitoa mifano ya waasi wawili waliasi juu ya Uyahudi ambao ulishindwa hapo nyuma.
d. Mst.38,39 Gamalieli alilishauri baraza kuwaachia huru mitume.
(1) Ikiwa kazi hii ni ya kibinadamu pasipo Mungu kuikubali, isingefanikiwa.
(2) Ikiwa ilikuwa kazi ya Mungu, wasingeliweza kuishinda.
(3) Ikiwa ilikuwa kazi ya Mungu nao wanapambana nayo, wangelikuwa na hatia ya kupambana na Mungu.

e. Mst.40 Baraza lilikubalia ushauri wa Gamalieli lakini waliamua kufanya mambo mawili:
(1) Waliwapinga mitume vibaya mno.
(2) Wakawaamuru wasinene katika jina la Yesu.

f. Mst.41 Mitume walifurahia kwamba ni heri kuteswa kwa ajili ya Yesu.
g. Mst.42 Mitume waliendelea kufundisha Yesu kuwa ni Kristo.

6. Mtazamo kwa ufupi ya 5:12-42, Mafaniki na upinzani kuinuka upya.
a. 5:12-16 Miujiza ya mitume / wengi wanaongezeka.
b. 5:17-28 Kutiwa gerezani kwa mitume / kuachiwa kimiujiza / Yesu anahubiriwa.
c. 5:29-32 Mitume wanahubiri Yesu aliyeinuliwa mbele ya baraza.
d. 5:33-39 Ushauri wa Gamalieli mbele ya baraza.
e. 5:40-42 Kupigwa kwa mitume / kufurahi / Yesu anahubiriwa.

7. Mtazamo kwa ufupi wa sehemu ya kielelezo kinachofuata – 6:1-7, kuchaguliwa kwa saba.
a. 6:1 Tatizo.
b. 6:2-4 Suluhisho.
c. 6:5,6 Kuchaguliwa kwa saba / mitume wanaweka mikono juu yao.
d. 6:7 Neno la Mungu lilienea na watu kulitii.

## 4. (6:1-7) KUCHAGULIWA KWA SABA

### a. (6:1) TATIZO

**6:1)**

1. Tena, kukua kwa kanisa kulifafanuliwa ("idadi ya wanafunzi ikaongezeka").
2. Mara nyingi, panapotokea kuongezeka kwa haraka, matatizo hutokea, kama walivyofanya katika kanisa la Yerusalem ilivyotajwa katika mstari huu.
3. Katika swala hili, "Wayahudi wenye asili ya Kiyunani" (Hellenists) walinung'unika au kulalamika juu ya "Waebrania" kwa kuwa wajane wao walisahaulika katika mahitaji ya kila siku.
4. Kugawia vitu ilikuwa jambo wazi kuwasaidia waliokuwa wahitaji na vilitoka katika thamani ya viwanja na vitu vilivyouzwa (2:44,45; 4:34-37).
5. (Hellenists) pengine inarejea kwa Wakristo wa Kiyahudi wenye asili ya kuongea Kiyunani na walifuata tamaduni na tabia za Kiyunani.
6. "Waebrania" pengine inarejea kwa Wakristo wa Kiyahudi asilia ambao hawakufuata tamaduni na tabia za Kiyunani, ingawa pengine walizungumza Kiyunani.
7. Tatizo hili lilileta changamoto kubwa kwa kanisa la Bwana Yerusalem.

**b. (6:2-4) SULUHISHO**.

1. "Thenashara" = mitume wa Kristo (wale wa asili kumi na mmoja na Mathiya).
2. Angalia jinsi mitume mara moja walivyolitatua tatizo hili kanisani!
3. Waliwaita ndugu pamoja ili kujadili hali hiyo.
4. Mwishoni mwa mst.2 mitume walionyesha haikuwa vizuri kwao kuacha kazi yao ya awali ya kuhubiri neno la Mungu na badala yake "kuhudumu mezani."
   a. "Kuhudumia mezani" inamaanisha kuwa kushiriki kugawa chakula na mahitaji mengine ili kukidhi mahitaji.
   b. Basi, mitume walikuwa wakisema kazi yao muhimu zaidi ilikuwa ni kuhubiri neno la Mungu na walitaka kuutumia muda wao wote kufanya kazi hiyo.
   c. Ni wazi mitume hawakujiona wao wenyewe kuwa ni bora hata wasifanye kazi za mikono, kama tunavyoona katika swala la mtume Paulo (18:1-3; 20:34).
   d. Hata hivyo, walikuwa haswa kwa ajili ya kufunua na kulithibitisha neno la Mungu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na walipaswa wajitoe kwa muda wote kuifanya kazi hiyo.
5. Katika mst.3 mitume waliwaeleza watu wawachague watu saba kutoka kati yao kuteuliwa kwa ajili ya kazi hiyo ya kuhudumu mezani kila siku.
6. Mitume waliorodhesha sifa tatu kubwa kwa watu hao saba:
   a. Kwanza, watu hawa saba walitakiwa wawe "walioshuhudiwa kuwa wema."
      (1) Hawa walikuwa watu ambao walijulikana kwa tabia zao njema na uadilifu.
      (2) Kwa kuwa kugawa vitu kungeweza kuleta majaribu kufuatana na hali yenyewe, watu pekee wenye msimamo na maadili mema wangechanguliwa.
   b. Pili, watu hawa saba walipaswa "wenye kujawa Roho Mtakatifu."
      (1) Hakuna shaka kabisa kwamba, karne ya kwanza, maneno haya yangerejea uwezo wa kutenda miujiza wa Roho Mtakatifu (linga.2:4,5; 4:8).
      (2) Hata hivyo, karne ya kwanza wakati miujiza ilikuwa ingali ikitendeka, maneno hayo yalitumika kurejea maswala ambayo hayakuhusisha uwezo wa kutenda miujiza.
         (a) Kwa mifano mingi tafadhali angalia maelezo ya mwisho (Appendix G) ya notisi za kozi hii.
      (3) Haswa katika fungu hili ni wazi kwangu kwamba maneno haya yanarejea kwa jambo ambalo halihusiani na miujiza.
      (4) Tafadhali angalia sababu zifuatazo kwa nini ninaamini maneno haya hayahusu uwezo wa kutenda miujiza:
         (a) Sababu ya kwanza ni, sifa hizi zimeambatanishwa na zingine ambazo si za kimiujiza, k.m. "wenye kushuhudiwa kuwa wema" na "waliojawa na hekima."

(b) Sababu ya pili ni, uwezo wa kimiujiza haukuhitaji kutenda kazi za watu hawa saba.

(c) Sababu ya tatu ni, kabla ya kufikia hapa katika Matendo, hakuna maandishi kwamba watu wowote wale isipokuwa mitume wa Kristo walitenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

1. Kusema ukweli, inaonekana Luka alitoa jambo muhimu kuonyesha mitume pekee ndio walitenda miujiza kabla ya muda huu.
2. Kwa mfano, mitume wametajwa wakifanya miujiza katika 2:1-13; 2:14-36 (tafsiri iliyovuviwa ya maandiko); 2:43; 3:1-11; 4:14-16; 4:33; 5:12,15,16).
3. Nje na kumbukumbu (reference) haya nane yanayohusu mitume kutenda miujiza, hakuna marejeo kwa mtu mwingine yeyote akitenda miujiza.
4. Hatimisho ambayo nahatimisha juu ya msingi huo wa kweli ni kwamba hakuna mtu mwingine isipokuwa mitume wa Kristo walikuwa na uwezo wa kimiujiza kabla ya hapo.
5. Basi, maneno "waliojawa na Roho Mtakatifu" haulengi uwezo wa kutenda miujiza katika mstari huu.
6. Kwa vyovyote vile, tuna uhakika mstari huu hauna maana uwezo wa kimiujiza leo kwa kuwa hakuna mtu aliye na uwezo huo.

(5) Swali la kawaida linaloibuka maneno haya "waliojawa Roho Mtakatifu" yanamaanisha nini?

(6) Ninaamini kuna mambo kadhaa yenye kulenga maana ya maneno hayo yenye kufurahisha:

(a) Kwanza, haya ni marejeo kwa kukaa hali ya kawaida kwa Roho Mtakatifu.

1. Kama tulivyoona katika somo letu, kukaa huku kunaanzia mtu anapotii injili, na hivyo kufanyika kuwa mwana wa Mungu.
2. Ukijumuisha kuamini injili, kutubu, na kuzamishwa kwa ajili ya msamaha wa dhambi (2:38; 3:19; 5:32; Gal.3:26,27; 4:6).
3. Roho Mtakatifu anapokaa au kuishi ndani ya mtu, Roho Mtakatifu humjaa mtu huyu!
4. Kama tulivyojifunza, siku hizi kujazwa au kukaa kwa Roho Mtakatifu hakumwezeshi mtu kufanya miujiza, kuongozwa moja kwa moja, n.k.!
5. Hivyo, sifa ya "kujawa na Roho Mtakatifu" katika mstari huu watu hawa walipaswa kuwa watoto wa Mungu, Wakristo!

(b) Pili, maneno haya ni kiwango cha Mkristo kumruhusu Roho Mtakatifu amshawishi maishani mwake kupitia kifaa chake, upanga wa Roho ambalo ni neno la Mungu (Efe.6:17).

1. Efe.5:18.
2. Gal.5:22,23.
3. 1 Thes.2:13.
4. Kol.1:5, 6.
5. Tukishaunganisha mafungu haya pamoja, tunahatimisha kwamba sifa za "kujawa Roho Mtakatifu" katika mstari huu inamaanisha Mkristo anayeishi maisha ya utaua na mfano kulingana na Upanga wa Roho Mtakatifu, neno la Mungu!

(7) Hatimisho la maneno haya "kujawa na Roho Mtakatifu" katika mstari huu hairejei katika maana ya karama za kimiujiza tutatilia mkazo tunapojifunza 6:6 na 8.

c. Sifa ya tatu ya watu hawa ni kwamba walikuwa "waliojawa na hekima."

(1) Watu hawa walipaswa kutumia maarifa kwa kadiri iwezekanavyo.

(2) Walitakiwa wawe na maamuzi sahihi.

7. Katika mst.4 mitume walionyesha wangeendelea kujitoa wenyewe kwa ajili ya sala na kuhubiri na kufundisha neno la Mungu.

a. Tena, hii ndiyo ilikuwa kazi yao ya msingi na muhimu.

### c. (6:5,6) SABA WACHAGULIWA / MITUME WAWAWEKEA MIKONO

1. Katika mst.5 tunajifunza kwamba maoni ya mitume yalikubaliwa na ndugu.
2. Ndugu wakachagua watu saba wenye sifa maalum zilitajwa na mitume katika mst.3.
3. Watu wawili miongoni mwao, Stefano na Filipo, watahusika sehemu kubwa katika sura kadhaa zinazofuata za Matendo.
4. Watu hao saba walipelekwa mbele ya mitume, ambao waliwaombea na kuweka mikono yao juu yao.
5. Mara kwa mara watu wameuliza kwa nini mitume wawawekee mikono juu yao hao watu saba.
6. Katika Agano Jipya kuwekewa mikono kulihusisha mambo mawili:
   a. Kwanza, hii ilikuwa njia ya kuwatuma watu waende safari, au kuwatenga watu kwa makusudi ya kazi maalum (ling.13:1-3).
   b. Pili, kama tutakavyojifunza katika 8:12-19, mitume wa Kristo walipomwekea mikono mtu, mara nyingi ilikuwa sababu ya kumwezesha kutenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
   c. Katika fungu hili, inaonekana kuwa kusudi haswa la mitume kuwawekea mikono hawa ilikuwa kuwawezesha kutenda miujiza.
   d. Sababu ya kushikilia msimamo huu itabainishwa wazi katika somo letu katika mst.8.

### d. (6:7) NENO LA MUNGU LIKAENEA NA WATU WAKATII

1. Maelezo mazuri mengine ya kukua kwa kanisa la awali na kwa nini walikua!
2. Tafadhali angalia hatua zilizoelezwa katika mstari huu:
   a. Kwanza, neno la Mungu lilienea (tena, lilihubiriwa, likafundishwa na watu kuishi kwalo.
   b. Pili, idadi ya wanafunzi ikazidi kuongezeka kwa haraka.
   c. Na tatu, hata idadi kubwa ya makuhani walitii injili ya Kristo.
      (1) Makuhani walikuwa miongoni mwa watu waliompinga vikali Yesu na lengo lake (lang. 4:1ff).
      (2) Kwa hiyo, kwa idadi hiyo kubwa ya walioongolewa ilikuwa utimilifu wa kazi kubwa.
      (3) Hili linadhihirisha uwezo mkubwa wa injili ya Kristo (linga.1:16; Yak.1:21)!
3. Kabla ya kuondoka 6:1-7 tunapenda kuelezea kwamba je, hawa watu saba walikuwa ndio mashemasi wa kwanza?
   a. Wengine hudai kwamba watu hawa walikuwa mashemasi wa kwanza.
      (1) Hutoa maelezo kuwa neno lilitafsiriwa “mgawo” au “huduma” katika mst.1 ni muundo wa neno lililotafsiriwa “shemasi”.
      (2) Pia hudai watu hawa saba walikuwa wakifanya kazi kama watumishi, ambayo hiyo ni majukumu ya mashemasi.
   b. Kwa sababu zifuatazo, siamini watu hawa walikuwa mashemasi.
      (1) Kwanza, ni kweli neno lililotafsiriwa “mgawo” au “huduma” katika mstari wa kwanza ni muundo wa neno lililotafsiriwa “shemasi.”
         (a) Walakini, neno lililotafsiriwa “kulihudumia” katika mst.4 pia ni muundo wa neno lililotafsiriwa “shemasi”, lakini linahusu mitume katika mstari huo, wala si mashemasi.
         (b) Basi, matumizi ya muundo wa neno lililotafsiriwa “shemasi” kurejea kazi ya watu hawa saba si ushahidi wa kutosha kwamba walikuwa mashemasi.
         (c) Kusema ukweli, neno lililotafsiriwa “shemasi” linaweza kumaanisha mambo mengi mbalimbali, kama vile:
            1. Kutumikia (ministering) (Math.27:55).
            2. Tumika (serve)Hudumia (Lk.22:26)
            3. Itumikia (administered) (2 Kor.8:19,20)

4. Msaada (relief) (Mdo.11:29).
5. Huduma (ministry) (Mdo.1:17,25).
6. Utumishi (office) (Rum.11:13).
7. Huduma (service) (Ufu.2:19).
8. Mtumishi (servant) (Yoh.12:26).
9. Shemasi (deacon) (1 Tim.3:8,10,12,13; Flp.1:1).

(d) Haswa, watu hawa saba hawajawahi kutajwa kama mashemasi katika fungu hili ama kwingine kokote kule.
(e) Zaidi sana, katika marejeo mengine yanayowahusu watu hawa nje na fungu hili, wametajwa kama "watu saba", na wala si mashemasi!
(f) Kwa hiyo, tunahatimisha kwa kusema kwamba matumizi ya muundo wa neno lililotafsiriwa "shemasi" kuhusu kazi ya watu hawa saba hayataji kuwa walikuwa mashemasi.

(2) Sababu ya pili ya mimi kutokuamini kuwa hawakuwa mashemasi ni kwa sababu sifa za kutumika kwao si sawa na sifa za mashemasi 1 Tim.3:8-13.
(3) Kwa sababu hizi mbili, ninaamini kuwa ni sahihi zaidi na salama kuwataja watu hawa kama "saba" kuliko kuwaita mashemasi.

4. Mtazamo kwa ufupi wa 6:1-7, Kuchaguliwa kwa watu saba.
   a. Mst.1 Wayahudi wa asili ya Kiyunani (Hellenists) walinung'unika kwa sababu walidhania kuwa wajane wao walisahauriwa katika huduma ya kila siku.
   b. Mst.2 Mitume waliwaeleza kuwa si vyema kwao kutumia muda wao wa kuhubiri neno na kuutumia kuhudumu kwa mkate wa kila siku.
   c. Mst.3 Mitume waliwaeleza ndugu kuwachagua watu saba walioshuhudiwa kwa mema wenye kujawa Roho Mtakatifu na hekima ili kuhudumu katika hili.
   d. Mst.4 mitume walionyesha kuwa wangeendelea katika sala na kufundisha neno la Mungu.
   e. Mst.5 Ndugu walichagua watu saba wenye sifa zilizotakiwa.
   f. Mst.6 Watu hawa saba walipelekwa mbele za mitume ambao wakawaombea na kuwawekea mikono juu yao.
   g. Mst.7 Neno la Mungu likazidi kuenea na kanisa likakua zaidi.
5. Mtazamo kwa ujumla wa kielelezo cha sehemu inayofuata – 6:8-7:60, Mafarisayo wakasirishwa na Stefano / kifo cha Stefano.
   a. 6:8 Stefano alifanya miujiza.
   b. 6:9-11 Mashitaka juu ya Stefano.
   c. 6:12-15 Stefano alipelekwa mbele ya baraza.
   d. 7:1-53 Stefano anajitetea mbele ya baraza.
   e. 7:54-60 Jinsi baraza lilipokea ujumbe – kifo cha Stefano.

## 5. (6:8-7:60) MAFARISAYO WAKASIRISHWA NA STEFANO / KIFO CHA STEFANO

### a. (6:8) STEFANO ANAFANYA MUUJIZA

1. Stefano ametajwa kuwa mtu aliyejaa imani na uwezo na kutenda miujiza mikubwa.
2. Hapa ni mara ya kwanza mtu mwingine mbali na mitume akitenda miujiza.
3. Ni wazi kwamba Stefano alipokea uwezo huu wa muujiza kutoka kwa mitume wa Kristo walipomwekea mikono juu yake (mst.6).
   a. Kabla ya mitume kuweka mikono juu yake na juu ya wengine wale sita, hakuna taarifa yoyote ile isipokuwa mtume wa Kristo akifanya miujiza.
   b. Kisha mitume wakaweka mikono juu ya wale saba (mst.6).
   c. Kisha, mara tu baada ya hapo, tunaona Stefano akitenda miujiza.
   d. Baadaye, kuna taarifa ya Filipo akifanya miujiza pia (8:6,7).

e. Hatimisho: Stefano na watu wengine sita walipata uwezo wa kutenda miujiza kwa njia ya kuwekewa mikono ya mitume.
f. Ukweli wa hatimisho hili utatiliwa mkazo tutakapojifunza swala la Simoni mchawi katika 8:14-19.

b. (6:9-11) MASHITAKA JUU YA STEFANO

1. Katika mst.9 baadhi ya Wayahudi walianza kushindana (haswa kubisha, kujadili) na Stefano.
2. Walakini, katika mst.10 tunajifunza wapinzani wa Stefano hawakuweza kuthibisha kwa uongo mambo Stefani aliyasema.
3. Hivyo basi, katika mst.11 upinzani kwa siri ulishawishi watu kudanganya kuhusu Stefano kwa kusema alinena maovu, matusi ("kufuru") juu ya Mungu na Musa.

**c. (6:12-15) STEFANO ANAPELEKWA MBELE YA BARAZA**

1. Katika mst.12 Wayahudi hawa wakawataharakisha viongozi na watu, Stefano akamatwe, na kuletwa mbele ya baraza (Sanhedrin).
2. Katika mst.13,14 Wayahudi walikuwa na mashahidi wa uongo ili kutoa mashitaka mengine mawili juu ya Stefano.
   a. Kwanza, alinena maneno mabaya juu ya "mahali hapa" (hekaluni).
      (1) Kulingana na washitaki wake Stefano, alikuwa na hatia hii wakati aliposema kwamba Yesu alisema angelivunja hekalu.
   b. Mashitaka ya pili juu ya Stefano ni kwamba aliinenea vibaya Sheria.
      (1) Kulingana na washitaki wake Stefano, alikuwa na hatia aliposema kuwa Yesu alisema angebadilisha kawaida hizi za Musa zilizotolewa kwa Israeli.
3. Tunatambua kuwa madai haya juu ya Stefano ni ya uongo kwa kuwa Luka alisema walikuwa waongo kwa kuwa alikuwa akinena kwa uvuvio ("mashahidi wa uongo") (mst.13).
4. Katika mst.15 tunajifunza kuwa baraza zima likamkazia macho Stefano.
   a. Walipofanya hivyo, walitambua kuwa sura ya Stefano ilionekana kama vile ya malaika.
   b. Hakika, inamaanisha kwamba Stefano alitazama kwa makini, bila hofu, kwa utulivu, adhima, na mwenye kumtumainia Mungu.
   c. Ni mfano wa ajabu wa ujasiri na upendo kwa Bwana!
   d. Stefano alikuwa ameshutumiwa kwa uongo kwa mashitaka yafuatayo:
      (1) Kufuru juu ya Musa.
      (2) Kufuru juu ya Mungu.
      (3) Kufuru juu ya hekalu.
      (4) Kufuru juu ya Sheria ya Musa.
   e. Walakini, alitulia kimya, mwenye matumaini mbele ya kundi lenye nguvu!
5. Wakati kuna Yesu mmoja tu na Yesu pekee, tafadhali angalia ulinganifu wa kufurahisha kati ya Stefano na Yesu:
   a. Stefano alikuwa akisimama mahali ambapo Yesu alisimama alipohukumiwa.
   b. Alipelekwa mbele ya baraza kwa mashitaka yanayolingana (linga. Mk.14:56-64).
   c. Alikuwa na washitaki wale wale (Sanhedrin).
   d. Alitambua walikusanyika pamoja ili kumhukumu, wala si kumpatia haki.
   e. Alitambua kwamba alikuwa katika muda mwafaka mno katika maisha yake.
   f. Aliomba rehema kwa washitaki wake (linga.7:60).

**d. (7:1-53) STEFANO ANAJITETEA MBELE YA BARAZA**

**(1) (7:1) SWALI LA KUHANI MKUU**

**7:1)**

1. Kuhani mkuu alimwuliza Stefano kama mashitaka juu yake yalikuwa ya kweli.

### (2) (7:2-8) STEFANO ATOA HISTORIA: ABRAHAM, ISAKA, YAKOBO NA WANAWE KUMI NA MBILI

**7:2-8)**

1. Angalia katika mst.2 Stefano alimtaja Mungu kama "Mungu wa utukufu."
   a. Je, maneno hayo yanalingana na mtu ambaye alikuwa na hatia ya kumkufuru Mungu kama Stefano alivyoshitakiwa?!
   b. Kwa hakika hapana!
2. Pili, Stefano alitoa historia ya Israeli kwa kutaja wahusika wakuu wafuatayo:
   a. Abraham.
   b. Isaka.
   c. Yakobo.
   d. Mababa (patriarchs) kumi na mbili (watoto kumi na mbili wa Yakobo au Israeli, ikiwa pamoja na Yusufu).
3. Wengine wamedai kumekuwa na kupingana kati ya kipindi cha miaka 400 kinachopatikana katika 7:6 na miaka 430 inayopatikana katika Kut.12:40,41.
   a. Haswa, hakuna kupingana kabisa!
   b. Kwa maelezo, tafadhali angalia mwishoni mwa notisi (Appendix H) zilizoandikwa.

### (3) (9,10) YUSUFU ALIKATALIWA NA NDUGU ZAKE

**7:9,10)**

1. Mambo yafuatayo yalibainishwa:
   a. Kwa sababu ya wivu, ndugu zake Yusufu wakamwuza Misri. Hivyo basi, walimkana Yusufu!
   b. Walakini, Mungu alikuwa pamoja na Yusufu na kumwokoa katika shida.
   c. Zaidi sana, Yusufu akapata kibali mbele za Mungu na hekima kwa Farao, Mfalme wa Misri.
   d. Ukweli ni kwamba, Farao akamfanya Yusufu kuwa liwali juu ya Misri na nyumba yake.

### (4) (11-16) YUSUFU ALIWAOKOA NDUGU ZAKE NA ISRAELI

**7:11-16)**

1. Katika nafasi yake ya mamlaka Misri, Yusufu aliweza kuokoa ndugu zake na Waisraeli wengine wote kutokana na njaa kubwa.
2. Ni muhimu kuangalia kielelezo katika mistari hii ambacho kitarudiwa mara kadhaa katika hotuba yake Stefano.
3. Katika mst.14 madai mengine ni kutofautiana idadi ya watu anaowataja Stefano waliongia Misri (75) na idadi ambayo Musa alisema walikwenda Misri (70) katika fungu kama vile Mwa.46:26, 27.
   a. Haswa, hakuna kukingana kabisa!
   b. Kwa maelezo kadhaa sahihi yanayowezekana ya tofauti hii katika idadi, tafadhali angalia mwisho wa notisi (Appendix I) zilizochapwa.

### (5) (7:17-26) MUSA ALIKWENDA KUSAIDIA ISRAELI KUTOKA UTUMWANI

**7:17-26)**

1. Musa alilelewa na binti wa Farao mwenye hekima na akawa hodari katika maneno na matendo.

2. Akiwa na umri wa mika arobaini, Musa akaamua kuwatembelea watu wake, Waisraeli.
3. Lengo lake ilikuwa kuokoa Israeli kutoka katika utumwa wao Misri.

### (6) (7:27-29) MUSA ALIKATALIWA NA ISRAELI

**7:30-37)**

1. Mbali na Musa kukataliwa na Israeli, Mungu akamtuma Misri kuokoa Israeli kutoka katika utumwa huko (mst.34).
2. Siyo tu hilo, lakini Mungu akamfanya Musa kuwa kiongozi na mkombozi (mst.35).
   a. Ni jambo la kufurahisha kuona kuwa neno lililotafsiriwa "mkombozi" (λυτρωτησ) linamaanisha mtetezi fidia (redeemer), mtu anaweka huru.
3. Mungu alimwezesha Musa kuwakomboa Waisraeli kutoka utumwa mwa Misri (mst.36).
4. Zaidi sana, Mungu alimwezesha Musa kutenda miujiza Misri, Bahari ya Shamu, na jangwani (mst.36).
5. Musa huyo huyo ndiye aliyetabiri kuja kwake Nabii Mkuu ambaye Mungu angemwinua kutoka katika ndugu zake Musa (mst.37).
   a. Na, kama tulivyoona katika somo letu 3:22, 23, Yesu Kristo alikuwa Nabii Mkuu aliyetimiza unabii huu!
   b. Alikuwa ni Mkombozi ambaye alikuja kuwakomboa watu katika utumwa wa dhambi.
   c. Alitenda miujiza kudhihirisha kwamba alinena kwa mamlaka ya Baba.
   d. Lakini hata hivyo Waisraeli walimkana na kumwua!

### (8) (7:38-40) MUSA AKAKATALIWA NA ISRAELI TENA

**7:38-40)**

1. Katika mistari hii Stefano alirudia jinsi Israeli ilivyomkana Musa kipindi cha kutangatanga jangwani.
2. Israeli ilimkana Musa mbali na mambo mengi ya msingi:
   a. Kwanza, alitenda miujiza mingi kwa uwezo wa Mungu mwenyenzi (mst.36).
   b. Na pili, alipokea neno la Mungu kutoka kwa Mungu mlimani Sinai (mst.38).
3. Angalia jinsi Mungu alivyoelezea jinsi Israeli ilivyofanya mbali na kwamba Mungu alimthibitisha Musa (mst.39, 40).
   a. Hawakumwamini.
   b. Walimkana Musa.
   c. Waligeuka na kwelekea Misri mioyoni mwao.
   d. Walimwomba Haruni atengeneze miungu ya kuwaongoza.
4. Tafadhali kumbuka Stefano alishitakiwa kunena mabaya juu ya Musa (linga.6:11).
   a. Walakini, tunaweza kuona wazi kwamba katika kusema mambo haya, Stefano alikuwa haneni mabaya juu ya Musa.
   b. Kinyume chake, alikuwa akitoa maelezo sahihi ya mambo maovu ambayo Israeli ilitenda juu ya Musa!

### (9) (7:41-43) ISRAELI ILIMKANA MUNGU MOJA KWA MOJA

**7:41-43)**

1. Katika mistari hii Stefano alikumbusha jinsi Israeli ilivyomkana Mungu moja kwa moja.
2. Walifanya hivyo kwa kufanya ndama kwa mikono yao na kisha kumwabudu kama sanamu, k.m. sanamu iliyowakilisha mungu wa uongo.
3. Kama matokeo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao wenyewe na waliabudu miungu mingine ya uongo!
4. Stefano alithibitisha swala lake kwa kunukuu Amosi 5:25-27 na Yer.19:9-12.

### (10) (7:44-50) MUNGU HAKAI KATIKA MAHEKALU YALIYOFANYWA KWA MIKONO

**7:44-50)**

1. Katika mst.44 Stefano aliwakumbusha juu ya Hema alilomwamuru Musa kulijenga jangwani kwa mfano ule Mungu aliowapa.
2. Katika mst.45,46 Stefano alieleza kwamba Hema lililetwa nchi ya Kanaan na kutumika kipindi chote cha Daudi.
3. Kwa nyongeza Daudi alitaka kujenga mahali pa kudumu kwa ajili ya Mungu.
4. Mungu hakumruhusu Daudi kujenga Hekalu, lakini alimruhusu mwanawe Daudi, Sulemani kujenga Hekalu.
5. Tena, tunatakiwa kumkumbuka Stefano alishitakiwa kwa kukufuru juu ya Hekalu
   a. Walakini, katika mistari hii tunaona Stefano alikuwa anajua vyema historia ya Hema na Hekalu na kuzungumza kwa adabu kuhusu hayo.
   b. Hivyo basi, hakuwa na hatia ya hayo au juu ya mashitaka mengine waliomshitaki.
6. Katika mst.48 Stefano alibainisha kwamba Mungu mwenyezi hahitaji hekalu zilizojengwa kwa mikono wa wanadamu ambamo ndani yake akae.
   a. Ukweli ni kwamba, wanadamu wasingelijenga hekalu kubwa vya kutosha kuweza kukaa Mungu wetu aliye juu!
   b. Lakini Stefano hakutosheka kwa kutoa maelezo haya tu!
   c. Kama alivyofanya katika mst.42,43 alitia nguvu hoja yake kwa kunukuu maandiko katika Agano la Kale ambayo wasikilizaji wake walidai kuyapenda na kuyatetea.
   d. Alinukuu kutoka katika Isa.66:1,2 ambamo Mungu aliwauliza Israeli ni nyumba gani wangeweza kujenga kwa ajili yake kwa kuwa mbingu ni kiti chake cha enzi na dunia ni mahali alipoweka miguu yake!
   e. Katika matumizi ya maandiko kupitia hotuba yake yote, Stefano alionyesha kwamba mashitaka ya kwamba aliinena maneno mabaya juu ya Sheria ilikuwa ni uongo, kama vile madai mengine yalivyokuwa uongo.
7. Sasa hivyo Stefano alikuwa amekabiliana vyema na mashitaka ya uongo juu yake kwa kutoa historia ya Israeli, alielezea baadhi ya mambo mazito sana na ya kweli juu washitaki wake!

**(11) (7:51-53) STEFANO ASHUTUMU WALIOMSHITAKI – WALIMPINGA ROHO MTAKATIFU; WALIWATESA MANABII; WALIMWUA YESU; NA KUKATAA SHERIA!**

**7:51-53)**

1. Katika mst.51 Stefano aliwaelezea Waisraeli kama wenye ukaidi na wasiopenda kuwa chini ya sheria ya Mungu ("wenye shingo ngumu…").
   a. Alisema daima walimpinga Roho Mtakatifu kama vile baba zao walivyofanya.
   b. Hakika, walifanya hivyo walivyopinga neno la Mungu lililofunuliwa na Roho Mtakatifu.
2. Katika mst.52 Stefano alibainisha kuwa baba za Israeli waliwatesa na kuwaua manabii wa Mungu.
   a. Kwa kufanya hivyo, Israeli ilikuwa inawapinga wale waliotabiri kuja kwa Masihi ("yule Mwenye Haki").
   b. Hili lilikuwa baya vya kutosha, lakini Sanhedrin na Waisraeli wengine walioishi kipindi cha Stefano walikuwa na hatia ya kitu kibaya zaidi!
   c. Haswa walimkana huyo aliyetabiriwa Masihi kwa kumtesa na kumwua!
3. Katika mst.53 Stefano alisema jambo hili ni kweli ingawa watu hawa walipata fursa ya kupokea Sheria ya Musa.
   a. Mbali na fursa hiyo ya pekee, pia waliamua kukataa sheria kwa kutoituza!
4. Basi, Stefano kwa ujasiri aliyageuza mashitaka waliyomshutumu yeye.
   a. Kumbuka, Stefano alikuwa ameshitakiwa kwa uongo kutukana juu ya:
      (1) Musa.
      (2) Mungu.
      (3) Hekalu.
      (4) Sheria ya Musa.

b. Stefano alithibitisha kuwa mashitaka hayo yalikuwa ni ya uongo.
c. Wala si hivyo tu, bali alishitaki Israeli, pamoja na washitaki wake, juu ya yafuatayo:
   (1) Kumpinga Roho Mtakatifu.
   (2) Kuwatesa na kuwaua manabii waliotabiri kuja kwake Masihi.
   (3) Kumsaliti na kumwua Masihi. Yesu Kristo.
   (4) Kuipinga Sheria ya Musa.
5. Ebu tafakari matokeo aliyoleta na Stefano kwa hao Sanhedrin!

**e. (7:54-60) MAUTI YA STEFANO**

1. Wajumbe wa Sanhedrin walichukizwa sana kwa sababu ya ukweli wa maneno ya Stefano hata wakasaga meno kwa hasira ("wakamsaga meno…").
2. Katika mst.55,56 tunajifunza Stefano akatazama mbinguni na kuona mambo mawili:
   a. Utukufu wa Mungu.
   b. Yesu akisimama mkono wa kuume wa Baba.
3. Hakika, Mungu aliruhusu Stefano kuona maono kumtia moyo na wengine ambao wangekufa katika Bwana siku zijazo.
4. Wengine wamekeungeusha ukweli wa Yesu alionekana akisimama mkono wa kuume wa Baba badala ya kuketi wakijaribu kuunga mkono mafundisho ya "premillennialism."
   a. Tumeona tayari jinsi fundisho la "premillennialism" ni uongo.
   b. Kwa njia hiyo hiyo, kujaribu kutumia ukweli wa kwamba Yesu alionekana akisimama kuunga mkono "premilleniasm" ni uongo pia.
   c. Kwa maelezo mengi juu ukweli huo, tafadhali angalia "Appendix J" katika notisi zilizochapwa.
5. Katika mst.57-59 tunaona jinsi Sanhedrin ilivyomjibu Stefano kwa maono aliona ya mbinguni. Wakafanya yafuatayo:
   a. Wakapinga kelele kwa sauti kuu.
   b. Wakaziba masikio yao.
   c. Wakamrukia kwa nia moja.
   d. Wakamtoa nje ya mji.
   e. Wakampiga kwa mawe (linga. Law.24:16).
6. Katika mst.58 kijana Sauli alitambulishwa kama mtu aliyeshika nguo za hao mashahidi wa uongo waliompiga mawe Stefano.
7. Alivyopigwa mawe Stefano, alifanya mambo mawili:
   a. Alimwita Yesu kupokea roho yake.
   b. Alimwomba Mungu asiwahesabie watu hao dhambi hiyo ya kumwua.
      (1) Luka 23:34.
8. Baada ya Stefano kutoa maelezo haya, alikufa ("akalala usingizi").
9. Ingawa watu wengine wanaamini kuwa Stefano alimwomba Yesu katika tukio hili, siamini kuwa ni kweli.
   a. Tafadhali angalia somo letu la 1:24,25.
   b. Maelezo ya nyongeza katika somo hili ni mwishoni mwa notisi (Appendix K) zilizochapwa.
10. Tunapoangalia hotuba ya kustaajabisha ya Stefano, tunaona akiishutumu Israeli ya kale na sehemu ya uasi wa Israeli ya wakati huo kwa kukana mambo yafuatayo:
   a. Yusufu.
   b. Musa.
   c. Mungu.
   d. Roho Mtakatifu.
   e. Manabii.
   f. Yesu, Nabii Mkuu, Masihi, na
   g. Neno la Mungu.

11. Jambo la huzuni, watu hawa wote, viumbe hai, au vitu vilikuwa na uhusiano wa Israeli katika ama kwa maana ya kimwili au kiroho.
12. Kuangalia kwa mapana, ni mfano wa kusisimua na wenye kutuimarisha alioonyesha Stefano kwetu sisi katika kifo chake!
    a. Ni ujasiri ajabu kukabiliana na umati unaokutishia.
    b. Ni imani na upendo mkubwa kwa Bwana.
    c. Ni kujitoa kiasi gani na kuwa wakfu kwa ajili la Yesu.
    d. Ni moyo mkubwa kiasi gani kunena ukweli kwa gharama zozote.
    e. Ni upendo wa jinsi gani kwa wasikilizaji, kama ulivyodhihirika katika kupenda kwake kunena ukweli kwao.
    f. Ni amani na raha ya jinsi gani kufia katika Bwana (Ufu.14:13)!
    g. Kama Paulo, Stefano aliona kuwa faida na "bora zaidi" kwa Mkristo mwaminifu kufa na kuwa pamoja na Kristo (Flp.1:21-23)!
    h. Hakika, Kristo alitukuzwa katika mwili wa Stefano kwa ujasiri wa maisha ya Stefano na kifo chake (Flp.1:21).
    i. Ni jambo jema hata kwetu sisi sote ikawa hivyo.
13. Muhtasari wa 6:8-7:60, Mafarisayo wakasirishwa na Stefano / kifo cha Stefano.
    a. 6:8 Stefano alitenda miujiza.
    b. 6:9-11 Mashitaka juu ya Stefano.
    c. 6:12-15 Stefano aliletwa mbele ya baraza.
    d. 7:1-53 Stefano anajitetea mbele ya baraza.
        (1) 7:1 Swali la kuhani mkuu.
        (2) 7:2-8 Stefano kwa mara nyingine alisimulia historia: Abraham, Isaka, Yakobo, na wana wake kumi na mbili.
        (3) 7:9,10 Yusufu alikataliwa na ndugu zake, bali Mungu alimwokoa.
        (4) 7:11-16 Yusufu aliokoa ndugu zake na Israeli.
        (5) 7:17-26 Musa akaja kuwaokoa Israeli katika utumwa.
        (6) 7:27-29 Musa alikataliwa na Israeli.
        (7) 7:30-37 Mungu alimsimamisha Musa kama kiongozi na mkombozi.
        (8) 7:38-40 Musa alikataliwa na Israeli tena.
        (9) 7:41-43 Israeli ilimkana Mungu moja kwa moja.
        (10) 7:44-50 Mungu hakai katika mahekalu yaliyojengwa katika mikono ya wanadamu.
        (11) 7:51-53 Stefano aliwashutumu washitaki wake – walimpinga Roho Mtakatifu; waliwaudhi manabii; walimwua Yesu; na kuikataa Sheria!
    e. 7:54-60 Matokeo ya baraza – kifo cha Stefano.

4. Mtazamo kwa ujumla wa sehemu ifuatayo – Sura 8-12, kanisa lilitawanyika Yudea na Samaria.

A. 8 na 9 Kanisa lilienea kijiografia.
B. 10-12 Kanisa lilitanuka kimataifa.

A. 8 na 9 Kanisa lilienea kijiografia.
    1. 8:1-40 Kuenea kwa kanisa kutokana na kazi ya Filipo.
        a. 8:1-3 Sauli alilitesa kanisa.
        b. 8:4 Matokeo – Injili ilienea.
        c. 8:5-13 Filipo alimhubiri Kristo na ufalme wake katika Samaria / wengi walibatizwa, ukijumuisha na Simon mchawi.
        d. 8:14-17 Petro na Yohana alitumwa kuweka mikono juu ya Wasamaria na kuwagawia Roho Mtakatifu.
        e. 8:18-25 Simon alijaribu kununua uwezo huo.
        f. 8:26-34 Filipo alitumwa kwa Mwethiopia towashi.
        g. 8:35-40 Filipo alimhubiri Kristo na towashi akatii.

## II. SEHEMU YA PILI: (8:12) KANISA LILITAWANYIKA KWENDA YUDEA NA SAMARIA

### A. (8,9) KANISA LILIENEA KIJIOGRAFIA
#### 1. (8:1-40) KUSAMBAA KWA KANISA KUTOKANA NA KAZI YA FILIPO
##### a. (8:1-3) SAULI ALITESA KANISA

**8:1-3)**

1. Sauli "alikuwa akiona vema" kwa kuuawa kwake Stefano.
   a. "alikuwa akiona vema" – σονενδοκεω - kuridhia na watu wengine katika kila kitu; kukubalia, kuunga mkono.
   b. Baadaye katika maisha ya Sauli (Paulo) alisikitikia sana jambo hili na mengine (linga. 1 Kor.15:9; Gal.1:13, 14, 23).
   c. Pia baadaye katika maisha, angekuwa mhubiri mwenye toba, sala, nguvu za neno la Mungu.
   d. Lakini kwanza, lazima tumwone kuwa ndiye mtesi wa muda mrefu!
2. Mateso makubwa yakainuka juu ya kanisa Yerusalem.
   a. Kama matokeo, watu wakatawanyika isipokuwa mitume katika eneo lote la Uyahudi na Samaria.
   b. Angalia agizo ya Yesu katika 1:8!
3. Watu wataua walimzika Stefano na kulikuwa na huzuni kubwa na maombolezo juu ya kupotelewa na mtu huyu mwema!
   a. Hii ni ishara nyingine ya upendo mkubwa ambao Wakristo wa awali walikuwa nao kwa kila mmoja!
4. Katika mst.3 tunajifunza kwamba Sauli "akaliharibu" kanisa la Bwana.
   a. "akaliharibu" – ελυμιαινετο.
      (1) Neno hili lililotumika kufafanua uharibifu wa kuathiri uliosababishwa na wanyama mwitu wakali.
      (2) Kwa maneno mengine, Paulo kwa ukali akaliharibu kanisa kwa nia ya kuangamiza kabisa.
   b. Angalia jinsi Mungu alivyoielezea juhudi ya uovu wa Sauli:
      (1) "akiingia kila nyumba" – mbinu, mipango, juhudi kubwa kuangamiza kanisa!
      (2) "akiwaburuta wanaume na wanawake" – kuwalazimisha wanaume na wanawake wache nyumba zao na mahali pa ibada.
      (3) "kuwatupa gerezani" – Kumbuka 2 Tim.3:12!
5. Basi, tunaona mateso mabaya na makali juu ya kanisa la Bwana wetu.

##### b. (8:4) MATOKEO – INJILI ILIENENA

1. Mbali na jitihada kubwa ya kuliharibu kanisa, mwisho wake ilikuwa kinyume!
2. Kama matokeo ya mateso juu ya kanisa la Yerusalem, Wakristo kila mmoja wakaenda kila mahali wakihubiri neno!
   a. Lazima tutie mkazo kuwa ilikuwa kwa kila Mkristo. Wakristo walibakia Yerusalem!
   b. Wafuasi hawa imara wa Yesu hawakuzuiwa na vitisho, kupigwa, kutupwa gerezani; hata kwa mauti!
   c. Ni kiasi gani walimpenda Bwana, neno lake, na kanisa lake!
   d. Tunahitaji watu kama hao leo! Ni pamoja nami na inajumuisha wewe!
3. Kama tulivyoona wakati mwingi katika somo letu la Matendod, mateso hayakuwazuia Wakristo waliojitoa wakfu kwa Yesu.
4. Badala yake, yalisababisha kukua kwao na kuwa jitihada ya kuwafundisha watu wengine, kama vile ilivyofanyika kwa Wakristo hawa!

**c. (8:5-13) FILIPO ALIMHUBIRI KRISTO NA UFALME WAKE SAMARIA / WENGI WAKABATIZWA, PAMOJA NA SIMONI MCHAWI**

**8:5-8)**

1. Katika mst.5 Filipo aliteremkia mji wa Samaria na kumhubiri Kristo kwao.
    a. Kumbuka Filipo alikuwa mmoja wa wale saba waliochaguliwa pamoja na Stefano katika 6:5 kuhudumia mahitaji ya kila siku.
    b. Pia, kumbuka Yesu aliwaamuru mitume wake kuanza kuhubiri Yerusalem, kisha katika eneo la Yudea, kisha katika eneo la Samaria (1:8).
    c. Kwa nyongeza, tafadhali kumbuka kwamba Wayahudi na Wasamaria walichukiana (linga. Yoh.4:9).
    d. Ujumbe aliohubiri Filipo ulikuwa Yesu, Kristo yeye aliyesulibishwa!
    e. Tutazungumzia zaidi kuhusu jinsi ya kumhubiri Kristo tutakapokuwa tunajifunza mst.12 na sehemu zingine za sura hii.
2. Watu wengi waliamini alichohubiri Filipo.
    a. Waliamini kile walichosikia – injili ya Kristo.
    b. Na kile walichoona – miujiza aliyoitenda Filipo.
    c. Kuhusu miujiza hiyo, ni muhimu kukumbuka kwamba Petro na Yohana waliweka mikono yao juu ya watu saba ukijumuisha Filipo, hivyo basi kuwawezesha kuwa na nguvu hizo (6:6-8).
3. Katika mst.7 tunajifuza aina mbalimbali ya miujiza aliyofanya Filipo.
    a. Kwanza, alitoa pepo wachafu (mashetani) wakiwatoa watu waliopagawa na mapepo.
    b. Pili, aliwaponya waliopoza na viwete.
    c. Ingawa hatuna muda wa kujadili somo linalohusu mapepo kwa maelezo mengi, tungependa kutoa maelezo yafuatayo kuhusu mapepo na kukuomba ujifunza zaidi:
        (1) Mapepo ni viumbe vya roho ambavyo Mungu aliruhusu kuishi ndani ya wanadamu, wanawake, na watoto katika karne ya kwanza.
        (2) Walikuwa na akili na kuweza kuzungumza.
        (3) Mapepo walimtambua Bwana Yesu kuwa ni Masihi, walimstahi yeye na uwezo wake, na walitambua baadaye angewatia katika mateso ya milele.
        (4) Mapepo ni roho chafu ambao si maradhi, bali mara nyingi walihushwa na maradhi na mateso mengine.
        (5) Kwa hakika, Mungu aliachilia mapepo kuishi ndani ya watu katika karne ya kwanza ili Mwanawe mpendwa aweze kudhihirisha uwezo wake juu ya nguvu za Ibilisi.
        (6) Mapepo hawa wangeondolewa ndani ya watu kwa njia ya uwezo wa kimiujiza kutoka kwa Mungu.
        (7) Mungu hakuruhusu mapepo kuwakalia watu tangu mwishoni mwa karne ya kwanza wakati karama za miujiza za Roho Mtakatifu zilipokoma.
        (8) Basi, kupagawa na mapepo hakupo siku hizi!
        (9) Hata hivyo, roho wachafu leo wapo lakini na hujaribu kutushawishi si moja kwa moja, pasipo kuishi ndani ya watu (Efe.6:12).
        (10) Ingawa roho hawa wachafu wana nguvu, mwana mwaminifu wa Mungu huweza kuwashinda kwa msaada wa Mungu.
        (11) Msaada wa Mungu ni pamoja na silaha za Mungu, ikiwa ni pamoja na upanga wa Roho, neno la Mungu (Efe.6:10-18).
    d. Maandiko ya nyongeza na maelezo juu ya somo hili yanaweza kupatikana mwishoni mwa notisi (Appendix L) zilizochapwa.
4. Mwisho, katika mst.8 imebainishwa kuwa kulikuwa na furaha kubwa katika mji wa Samaria ikiwa ni matokeo ya kuhubiri injili yenye utukufu ya Kristo.
    a. Moyo wenye uaminifu pia mwema hufurahia kuwepo kwa mahubiri ya habari njema za wokovu kwa njia ya Yesu Kristo (linga.24)!

**8:9-11)**

1. Simoni ametambulishwa na kuelezewa kama ifuatavyo:
   a. Awali alifanya kazi ya uchawi, akifanya kuwa na uwezo mkubwa wa uganga, uwezo wa kutabiri mambo yajayo, au kuponya magonjwa kusema maneno ya kichawi.
   b. Aliwashangaza watu wa Samaria kwa uchawi wake.
   c. Alijisifu kuwa ni mtu mkubwa.
   d. Watu wakamsikiliza, wakidhania kuwa "ni uwezo mkubwa wa Mungu", k.m. kwamba alikuwa na nguvu na siri fulani kubwa kutoka kwa Mungu.
2. Watu wa Samaria walikuwa chini ya ushawishi wa Simoni kwa kipindi cha muda mrefu.

**8:12,13)**

1. Mbali na ushawishi wa Simon, Wasamaria walimwamini Filipo waliposikia injili yenye mvuto aliyoihubiri.
   a. Hili linadhihirisha uwezo wa injili ya Kristo inapohubiriwa kiusahihi!
      (1) Wasamaria awali walimwaamini Simoni mwongo na uchawi wake.
      (2) Baadaye, waliposikia ukweli wa injili, walitambua ilikuwa ina nguvu zaidi na kwamba ilitoka kwa Mungu!
   b. Ni jambo la kufurahisha pia kuona kwamba katika mst.5 Filipo akamhubiri Kristo.
      (1) Bali, katika mst. 12, tunaona baadhi ya vitu katika kumhubiri Kristo ni kufundisha juu ya ufalme, kanisa la Mungu!
      (2) Basi, bila kujali watu wengine wanavyodai leo, hauwezi kutenganisha Yesu na kanisa lake!
      (3) Yeye ni kichwa na Mwokozi wa mwili, ambao ndilo kanisa (Efe.5:23).
      (4) Hivyo basi, ikiwa mtu anapenda kuokolewa, ni lazima wawe ndani yake na katika kanisa lake. Hauwezi kutenganisha hivyo viwili (linga. 2:47)!
   c. Mwisho, katika mst.12 ni muhimu sana kutambua walichofanya hao waumini baada ya kuamini injili.
      (1) Mungu anasema walibatizwa!
      (2) Lakini, jinsi gani walijua kuwa walihitajika kubatizwa?
      (3) Haya yote walitajwa katika mst.5 na 12 ni kwamba Filipo alimhubiri Kristo na mambo yanayohusu ufalme (kanisa) wa Mungu.
      (4) Ni dhahiri basi, umuhimu wa ubatizo umejumuishwa katika kumhubiri Kristo na mambo yahusuyo ufalme (kanisa) wa Mungu.
2. Katika mst.13 tunaona hata alama kubwa ya uwezo wa injili.
   a. Neno hilo lilikuwa na nguvu kiasi cha kumshawishi Simoni mchawi kuliamini.
   b. Imani yake ilimshawishi kutii injili kwa kubatizwa, kama vile Wasamaria wengine walivyofanya!
   c. Siyo tu hilo, bali aliendelea kuwa pamoja na Filipo na kustaajabia miujiza aliyoitenda Filipo.
3. Basi, hakuna shaka kabisa kwamba Simoni aliongolewa kwa Bwana!

### d. 8:14-17) PETRO NA YOHANA WALITUMWA KUWAWEKEA MIKONO WASAMARIA ILI KUWAPA VIPAWA VYA ROHO MTAKATIFU

1. Mitume wakamtuma Petro na Yohana Samaria walipotambua kwamba Samaria ilikuwa imelipokea kwa utiifu neno la Mungu.
   a. Kwa bahati, ni jambo la kufurahisha kuona kwamba mawazo ya kumtuma Petro na Yohana ni wazo ambalo waliungana mitume wote.
   b. Kama kundi, waliamua kumtuma Petro na Yohana.
   c. Hilo ni muhimu kwa sababu linatubainishia kuona kwamba Petro hakufanya uamuzi huo yeye mwenyewe, kama "Papa" akitawala juu ya mitume wengine.
   d. Zaidi sana, si yeye alikuwa akituma mitume kama kiongozi wao na mtume mkuu.
   e. Badala yake, alikuwa mmoja wa hao walitumwa na mitume wengine.

   f. Jambo hili na mengine ya kweli kutoka katika maandiko yanapaswa kutusaidia kuona kuwa madai ya kanisa la "Roman Catholic" kwamba Petro alikuwa "Papa" wa kwanza ni uongo!
2. Petro na Yohana walipowasili, wakasali ili baadhi ya Wasamaria kuweza kupokea Roho Mtakatifu.
3. Sehemu ya kwanza mst.16 imebainishwa kwamba Roho Mtakatifu "hajawashukia" hata Mkristo yeyote Msamaria. a.
   a. Maelezo kwamba Roho Mtakatifu "hajawashukia" hata Mkristo mmoja Msamaria ni jambo la msingi sana!
   b. Ninaweza kuona wazo hili la Roho Mtakatifu "kushuka juu ya" mtu sehemu mbili katika Agano Jipya.
   c. Sehemu hizo ni Matendo 10:44 na 11:15.
   d. Katika mazingira hayo mawili, Mungu alitumia maneno "kushukiwa" akirejea kwa watu waliopokea Roho Mtakatifu katika namna ambayo ni kutenda miujiza!
   e. Hivyo basi, ninahatimisha kuwa Mungu aliposema katika mstari huu Roho Mtakatifu "hajawashukia bado" yeyote kati Wakristo wa Samaria, alikuwa akibainisha kwamba hakuna hata mmoja aliyekuwa na uwezo wa kimuujiza wakati huo.
   f. Hatimisho hilo litatiwa nguvu kadiri tunavyoendelea na somo letu juu ya mistari hii.
4. Sehemu ya mwisho ya mst.16, pamesema kuwa Wakristo hawa Wasamaria walikuwa tu wamebatizwa katika jina la Bwana Yesu (k.m. kwa mamlaka yake).
   a. Haya ni marejeo ya wazi kulingana na kusikia kwao injili, kuiamini, na kubatizwa kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao (linga.8:12,13).
   b. Lakini, Mungu alikuwa ameahidi kupitia Petro kwamba kila aliyeamini mwenye kutuba na kubatizwa katika jina la Yesu wangepata msamaha wa dhambi, kadhalika kipawa cha Roho Mtakatifu (2:38).
   c. Na tumeona kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu kinalenga kukaa kwa kawaida Roho Mtakatifu ndani ya Mkristo (2:38; 3:19; 5:32).
   d. Kadhalika, tumejifunza kwamba kukaa huku kwa kawaida hakumwezeshi Mkristo kufanya miujiza au kuongozwa moja kwa moja au ushawishi toka kwa Roho Mtakatifu.
   e. Basi, Wakristo Wasamaria walipokea ukaaji wa kawaida wa Roho Mtakatifu walipokuwa wamebatizwa kwa mamlaka ya Yesu.
   f. Walakini, hawakupata uwezo wa kutenda miujiza, k.m., Roho Mtakatifu alikuwa "hajawashukia" juu yao kuwapa nguvu za kutenda miujiza!
5. Katika mst.17 tunajifunza nitume Petro na Yohana waliweka mikono yao juu ya baadhi ya Wakristo Wasamaria, na kama matokeo, Wakristo hao "wakapokea Roho Mtakatifu."
   a. Kama tulivyoona tayari, Wakristo hawa "wakampokea Roho Mtakatifu."
   b. Hivyo basi, tunaposoma katika mstari huu kwamba "wakampokea Roho Mtakatifu" ikiwa ni matokeo ya kuwekewa mikono na mitume juu yao, ni wazi kwamba kuna jambo zaidi ya maana ya Roho Mtakatifu kukaa ndani yao.
   c. Hatimisho halali pekee ni kwamba mitume walipoweka mikono juu yao Wakristo, walipokea uwezo wa kutenda miujiza kwa njia ya Roho Mtakatifu.
   d. Hatimisho hili linabainishwa na kutiwa nguvu tunapotambua jambo kama hili lilivyotokea katika Matendo 6.
      (1) Katika 6:5,6 utakumbuka wale saba, ikiwa ni pamoja na Stefano na Filipo walipelekwa mbele ya mitume, waliowaombea na kuwawekea mikono juu yao.
      (2) Kisha katika mst.8 Stefano alikuwa mtu wa kwanza ukiacha mitume wa Kristo alitenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
      (3) Baadaye, katika 8:6, 13 Filipo pia alitenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
      (4) Ni wapi hawa watu wawili walipata uwezo huo wa miujiza?
      (5) Hakika, walipokea uwezo wa kutenda miujiza mitume wa Kristo walipowawekea mikono juu yao.

(6) Na ndivyo haswa Wakristo wa Samaria hawa walivyopokea wakati Petro na Yohana walipowawekea mikono juu yao.
(7) Ndiyo kusema, walipokea Roho Mtakatifu kwa namna ambayo waliwezeshwa kutenda miujiza!

6. Ukiwa na ukweli huo akilini mwako, tunataka kutafakari swali muhimu sana.
   a. Kama tulivyoona, kusudi kubwa la mitume kwenda Samaria lilikuwa kuwawekea mikono baadhi ya Wakristo Wasamaria.
   b. Na kusudi la kuwawekea mikono juu ya Wasamaria ili kwamba waweze kupokea Roho Mtakatifu kwa namna ambayo ingewawezesha kutenda miujiza.
   c. Lakini, Filipo alikuwa tayari amepokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono na mitume (6:5,6).
   d. Na hilo la kuwekewa mikono na mitume lilimwezesha Filipo kutenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (8:6,7,13).
   e. Kwa nini basi Filipo asingeweka mikono yake juu ya Wakristo Wasamaria hawa ili kupokea Roho Mtakatifu kwa namna ambayo ingewafanya kutenda miujiza?
   f. Kwa nini kulikuwa na lazima kwa Petro na Yohana kusafiri mwendo mrefu toka Yerusalem hadi Samaria kuweka mikono yao juu ya Wakristo?
   g. Hatimisho sahihi pekee ni kwamba ingawa Filipo alikuwa na uwezo wa kutenda miujiza, hakuwa na uwezo wa kuwapatia wengine uwezo huo!
   h. Basi, ni wazi kwamba mitume wa Kristo pekee ndio walikuwa na uwezo kuwawekea mikono wengine, kuwawezesha kupokea Roho Mtakatifu kwa njia ambayo wangefanya miujiza.
   i. Hatimisho hili litabainishwa na kutiwa nguvu katika sehemu ifuatayo katika mistari kadhaa.
7. Mwisho, tunapaswa kujadili jambo lingine muhimu zaidi kabla ya kuacha mistari hii.
   a. Wasamaria hawa walisikia injili, waliiamini, na wakabatizwa (8:6,12,13).
   b. Kisha, kulingana na Mungu, wakapokea msamaha wa dhambi, waliokoka, wakapata Roho Mtakatifu akikaa ndani yao kwa njia ya kawaida, na Bwana akawazidisha katika kanisa lake (2:38,41,47; 3:19; Mk.16:16).
   c. Walipokea baraka zote hizo za ajabu kabla ya kuwekewa mikono na mitume ili kuwawezesha kutenda miujiza kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu (8:17).
   d. Hili linafafanua kwamba hata wakati huo, miujiza ilipofanywa, mtu hakutakiwa kuwa na uwezo wakutenda miujiza ili apate kuokoka.
   e. Badala yake, waliokolewa walipotekeleza masharti ya Mungu: kusikia, kuamini, kutubu, kumkiri Yesu, na kuzamishwa majini ili kupata msamaha wa dhambi.
   f. Leo, kama tulivyojifunza, hakuna uwezo wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu.
   g. Walakini, watu wangali wakiokolewa kwa njia ya kusikia, kuamini, kutubu, kumkiri Yesu, na kuzamishwa majini kwa ajili ya ondoleo la dhambi.
   h. Hakuna anayeokolewa kwa madai yake ya kutenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu!
8. Mtazamo kwa ufupi juu ya kile tulichohatimisha katika 8:1-40. Kuenea kwa kanisa kupitia kazi ya Filipo:
   a. 8:1-3 Sauli alilitesa kanisa.
   b. 8:4 Matokeo yake – injili ilisambaa!
   c. 8:5-13 Filipo alimhubiri Kristo na ufalme wake Samaria / wengi wakabatizwa, ikiwa ni pamoja na Simoni mchawi.
   d. 8:14-17 Petro na Yohana walitumwa kuwawekea mikono Wasamaria ili kupokea Roho Mtakatifu.

**e. (8:18-25) SIMONI ALIJARIBU KUNUNUA UWEZA HUO / MAJIBU YA PETRO**

**8:18,19)**

1. Tafadhali angalia, Simoni aliona jambo fulani ambalo lilimshawishi kuwa kupitia mitume kuweka mikono yao Roho Mtakatifu walipewa watu kwa namna ambayo waliweza kutenda miujiza.
   a. Kwa maneno mengine, kwa hakika jambo fulani lilitukia mtiume walipoweka mikono yao juu ya Wakristo.
   b. Simoni aliona kwamba kwa mitume kuweka mikono yao juu ya Wakristo hao, waliweza kufanya kitu ambacho hawakuwahi kukifanya hapo nyuma.
   c. Tunahatimisha kuwa Wakristo hao waliweza kufanya kitu fulani kimiujiza, kama vile kunena katika lugha ngeni ambazo hawakuwahi kujifunza kabla.
   d. Linathibitisha hili hatimisho letu kwamba mitume waliweka mikono yao juu ya Wasamaria Wakristo kwa kusudi la kuwawezesha kutenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
2. Pia, angalia Simoni alibainisha wazi kwamba ilikuwa ni kwa njia ya mitume tu wa Kristo walioweza kuweka mikono juu ya wengine ili kuwapatia nguvu za kutenda miujiza.
   a. Hili linaleta hatimisho sawa na lile tulilohatimisha katika mst.14-17.
   b. Ndiyo maana Filipo hakuweka mikono yake juu ya Wasamaria kuwapa uwezo wa kutenda miujiza, ingawa alikuwa na uwezo wa kutenda miujiza yeye mwenyewe.
   c. Filipo hakuwa mtume wa Kristo, basi hakuwa na uwezo wa kuwawekea wengine mikono ili kuweza kutenda miujiza.
3. Hili linatupeleka katika swali ambalo ni la kufurahisha sana – Kifo cha mtume wa Kristo wa mwisho kilileta matokeo gani juu ya uwezo wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu?
   a. Tumeona kwamba kupitia kwa mitume wa Kristo tu ambao waliweza kuweka mikono juu ya wengine kuwapa uweza wa kutenda miujiza.
   b. Kwa hiyo, mtume wa mwisho alipokufa, uwezo wa kugawa kwa mtu mwingine karama hizi za miujiza kwa  mitume kuweka mikono haukuwepo tena.
   c. Hakuna shaka kwamba walikuwepo waliobakia ambao waliwekewa mikono na mitume ambao waliweza kutenda miujiza.
   d. Walakini, kama Filipo kwa habari hii, hawakuwa na uwezo wa kuwagawia watu wengine uwezo huu.
   e. Hivyo basi, mtume wa mwisho alipokufa, na mtu wa mwisho aliyewekewa mikono na mitume alipokufa, karama za kimiujiza za Roho Mtakatifu zikakoma.
   f. Njia pekee nyingine ambayo mtu angeweza kupokea karama za Roho Mtakatifu karne ya kwanza ilikuwa kwa njia ya ubatizo wa Roho Mtakatifu.
      (1) Hata hivyo, kama tulivyoona katika somo letu sura 2, ubatizo wa Roho Mtakatifu ulitukia mara mbili tu.
      (2) Basi, wakati Paulo alipoandika waraka kwa Waefeso, angeweza kusema kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu kwamba kulikuwa na ubatizo mmoja tu (Efe.4;5)!
      (3) Pia, kama tulivyojifunza, ubatizo huo mmoja ni kuzamishwa majini kwa ajili ya ondoleo la dhambi, wala si ubatizo wa Roho Mtakatifu.
   g. Basi, uwezo wa kutenda miujiza usipopatikana kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu au kwa kuwekewa mikono na mitume, Mungu aliondoa karama hizo za miujiza za Roho Mtakatifu karibia na mwisho wa karne ya kwanza.
   h. Hakika, kwa wakati huo, Mungu alisababisha karama hizo "kubatilika, kukoma, kutoweka, na kuondoka" kama alivyotabiri kuwa ingetokea (1 Kor.13:8-13)!
4. Kwa bahati mbaya, Simoni alipowaona mitume kuwa na uweza huo, alijaribu kununua huo uwezo kwa fedha.
   a. Alitaka awe na uwezo wa kuwekea watu wengine mikono ili kwamba waweze kutenda miujiza.
   b. Hakika, alitaka kuwa na uwezo wa kufanya hivi kama njia ya kuwa na nguvu juu ya wengine na kutengeneza faida.
   c. Bila shaka, swala hili lilikuwa si sawa, na nia yenye uovu juu ya Simoni mchawi!

**8:20,21)**

1. Petro alimjibu Simoni kwa ukali na hasira yenye haki.
2. Kwa kufanya hivyo, Petro alimwaambia mambo yafuatayo Simoni.
   a. (mst.20) – apotelee mbali na feDha zake kwa kadiri alivyofikiri kuwa angeweza kununua karama ya Mungu kwa fedha.
   b. (mst.21) Moyo wake haukuwa mnyoofu mbele za Mungu. Ilikuwa imejaa tamaa ya kutukuka na fedha.
   c. (mst.23) aliruhusu yeye mwenyewe kuwa na sumu ya uchungu wa moyo na kuwa katika kifungo au utumwa wa dhambi.
3. Katika mst.22 Petro alitoa kwa Simoni masharti yenye uvuvio yanayohusu toba na kwa Wakristo wengine wanaoanguka katika dhambi.
   a. Ni muhimu sana kutambua kwamba Simoni alikuwa ametii injili tayari, na kwamba alikwisha pokea msamaha wa dhambi wa awali na kufanyika kuwa mwana wa Mungu.
   b. Kwa uvuvio Luka alisema kwamba Simoni aliiamini injili na akabatizwa (8:13).
   c. Basi, masharti ya msamaha kwa ajili ya dhambi yaliyotolewa katika mstari huu ni kwa hao waliotii injili tayari, ukijumuisha kubatizwa kuingia katika Kristo ili kupata msamaha wa dhambi.
   d. Ninatambua kwamba watu wengine wanadai kuwa Simoni hakuwa Mkristo haswa kwa kuwa alianguka ghafula kabisa.
   e. Lakini watu hao wanapingana na Luka aliyenena kwa uvuvio na kusema Simoni akaiamini injili na kubatizwa.
   f. Simoni alipofanya hivyo, alipokea msamaha wa dhambi na kufanyika kuwa Mkristo, mwana wa Mungu.
   g. Kusema ukweli, kama sisi sote, hakuwa mkamilifu kwa kufanyika tu kuwa Mkristo.
   h. Kama vile mimi na wewe alihitaji kufanya kazi ili kuondoa tabia mbaya na kuzidisha tabia njema badala yake (Kol.3:1-17; Rum.6:6-13).
   i. Hata hivyo, Simoni alikuwa angali Mkristo, mwana wa Mungu, na mambo aliyoambia na Petro kufanya yanamlenga tu mtu ambaye ameshafanyika kuwa Mkristo kwa kutii injili, ikiwa ni pamoja na kuzamishwa majini.
4. Ikiwa na tahadhali hizo akilini, Petro alimwambia Simoni afanye nini ili apate msamaha wa dhambi?
   a. Kwanza, Petro alimwaambia kutubia uovu wake.
      (1) Kama tulivyoona katika somo letu la 2:38, toba ni badiliko la akili.
      (2) Kubadilika huko kwa akili hutegemea huzuni ya jinsi ya Mungu kwa dhambi, na hupelekea mtu kubadili tabia.
   b. Pili, Petro alimwaambia Simoni amwombe Mungu ili apate msamaha.
5. Hivyo basi, Mkristo kupata msamaha wa dhambi, hahitajiki kubatizwa mara ya pili.
   a. Badala yake, ni lazima watubu dhambi zao na kukiri dhambi hizo kwa Mungu, wakiomba msamaha wake.
   b. Mtu Yohana aliyevuviwa aliongeza kwamba Mkristo ni lazima "aenende nuruni", k.m., kujitahidi kuishi kulingana na neno la Mungu, ambalo ni taa ya miguu yetu na mwanga wa njia zetu (1 Yoh.1:7-9; Zab.119:105).

**8:24)**

1. Simoni alijibu shutuma kali za Petro kwa kuomba Petro kumwombea kwa Mungu ili kwamba mambo hayo aliyoyanena yasimpate Simoni.
   a. Hii ni alama bora ya maneno ya Petro yenye uvuvio yalikuwa na matokeo yaliyokusudiwa kwa Simoni.
   b. Hatuna maelezo yenye uvuvio kuonyesha alichofanya Simoni katika maisha yake yote yaliyobakia.
2. Wazo la kuamsha fikra na swali makini linapaswa kuulizwa kufikia hapa.

a. Ikiwa Petro alikuwa “Papa” wa kwanza kama inavyodaiwa na marafiki wetu wa Roman Catholic, basi kwa nini “asisamehe” tu au kutoa msamaha kwa dhambi ya Simoni moja kwa moja?
   (1) Kwanza, Petro hakuwa “Papa” wa kwanza!
   (2) Pili, kwa sababu njia pekee ambayo Petro na mitume wengine kusamehe dhambi ilikuwa ni kwa njia isiyo ya moja kwa moja kupitia mahubiri na mafundisho ya neno la Mungu, ambalo linatueleza nini cha kufanya ili kupata msamaha wa dhambi.
   (3) Na hivyo ndivyo hasa Petro alifanya – alihubiri masharti ya Mungu juu ya msamaha.
b. Zaidi sana, Petro hakumweleza Simoni kumwomba yeye (Petro) ili kupata msamaha.
c. Kinyume chake, Petro alimweleza Simoni kumwomba Mungu ili apate msamaha!

**8:26)**
1. Katika msitari huu tunaona mwanzo wa mojawapo ya habari muhimu zilizoandikwa katika kitabu cha Matendo, ikitueleza mambo ya kufanya ili kuokoka.
2. Picha ilianza kwa kuhusika moja kwa moja kwa malaika wa Bwana.
   a. Walakini, ni muhimu sana kutambua kwamba malaika hakuzungumza na mtu ambaye alihitaji kusikia ujumbe wa Mungu wenye wokovu!
   b. Badala yake, malaika akanena na Filipo ambaye alikuwa mhubiri wa neno la Mungu.
   c. Basi, hata karne ya kwanza wakati miujiza ilipofanyika, Mungu hakutumia malaika kupeleka ujumbe wa wokovu moja kwa moja kwa hao walio dhambini.
3. Malaika alimweleza Filipo kwenda katika njia iliyotoka Yerusalem kueleka Gaza.
4. Kwa bahati, ni muhimu pia kutambua kwamba tangu mwisho wa karne ya kwanza Mungu alipobatilisha karama za miujiza za Roho Mtakatifu, pia hatumii njia ya kuwasioliana na wahubiri kupitia malaika kama alivyofanya katika tukio hili.
   a. Kipindi cha Filipo, hawakuwa na Agano Jipya lililokuwa katika muundi wa maandishi.
   b. Hivyo basi, Mungu alichagua kuwasiliana na baadhi ya watu waliovuviwa kupitia malaika au Roho Mtakatifu.
   c. Leo, tuna ufunuo wote wa Agano Jipya, ambao kwa huo Mungu anawasiliana kwa watu wanaotaka kusikiliza (Ebr.1:1; 2:1-4).

**8:27,28)**
1. Filipo alikwenda katika njia ile na kukutana na Mwethiopia towashi.
2. Mtu huyo mwenye busara alitajwa kama ifuatavyo:
   a. Alikuwa mtu mwenye cheo kikubwa chini ya Malkia wa Ethiopia.
   b. Aliwekwa juu ya hazina ya malkia – nafasi ya kuaminiwa na majukumu.
   c. Alikwenda Yerusalem kumwabudu Mungu na alikuwa akirejea nyumbani basi, kwa hakika alikuwa Myahudi au aliyeongolewa katika imani ya Kiyahudi.
   d. Na, alikuwa akisoma kitabu cha Isaya.
3. Kutokana na maelezo, tunaweza kuona Mwethiopia alikuwa mcha Mungu ambaye alikua akitafuta hakika mapenzi ya Bwana.
4. Alikuwa akitafuta mapenzi ya Mungu mahali sahihi, k.m., katika neno lake, Biblia!

**8:29)**
1. Sasa tunaona kuhusika kwa Roho Mtakatifu katika habari inayovutia ya uongofu wa mtu aliyekuwa akitafuta mapenzi ya Bwana.
2. Kulingana na jinsi ulimwengu wa dini unavyofundisha leo, tungetegemea Roho Mtakatifu akifanya kazi moja kwa moja, kwa siri, na kimiujiza katika moyo wa Mwethiopia.
3. Tunasema hivyo tu kwa sababu watu wengi wanafundisha kwamba Roho Mtakatifu sharti aongoze moja kwa moja ndani ya moyo au akili za mtu kabla mtu hajaweza hata kumwamini Bwana.
4. Siamini hata kidogo fundisho la uongo hilo, kwa kuwa linapingana na maandiko yaliyo dhahiri, kama tulivyoona katika katika somo letu sura 2.

5. Walakini, kama fundisho hilo lilikuwa kweli, pasingelikuwa na fursa bora kuliko hii hapa kwa Bwana kumwonyesha mwanadamu ni kweli.
   a. Siwezi kufikiria mahali pengine zaidi ya sura hii kwa ajili ya Bwana kuonyesha kwamba ni muhimu kwa Bwana kufanya kazi moja kwa moja na kwa siri katika akili ya mtu kumwezesha kutii.
   b. Ni kweli hilo ni kwa sababu, kama tulivyotangulia kuona katika somo letu katika Matendo, watu waliweza wazi wazi na dhahiri kutenda miujiza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
   c. Kwa nyongeza, katika tukio hili haswa, kulikuwa na kuhusika kwa moja kwa moja kwa malaika wa Bwana.
   d. Siyo tu hivyo, bali kulikuwa na kuhusika moja kwa moja kwa Roho Mtakatifu.
   e. Hivyo basi, vitu vyote vinavyohitajika vilikuwepo siku hiyo katika njia ya Gaza.
   f. Ambacho Bwana alipaswa kutueleza sisi katika habari hii ni kwamba Roho Mtakatifu alitenda kazi moja kwa moja na kwa siri katika akili ya Mwethiopia kumwezesha kuamini.
6. Lakini, kama unavyoweza kuona kwa wazi, kile ambacho Bwana hajatueleza sisi, ama katika mst.29, katika mazingira haya, au kwingineko kokote kule katika Biblia!
7. Badala ya kufanya kazi moja kwa moja na kwa siri katika akili za Mwethiopia, Roho Mtakatifu alimweleza Filipo mwinjilisti kusogelea gari la Mwethiopia, kwa hakika kwa lengo la kumfundisha injili!
8. Sasa, ukiwa na ukweli huo muhimu sana akilini mwako, ebu tuone jinsi habari hii ya ajabu ya wokovu inavyozidi kufunuliwa.

**8:30-34)**
1. Angalia shauku kubwa aliyokuwa nayo Filipo ya kumfundisha Mwethiopia. Akamkimbilia!
   a. Mfano wa ajabu huu kwangu na kwako kuiga leo – nia na shauku kubwa ya kufundisha wengine kuhusu Bwana na Mwokozi!
2. Filipo alimsikia Mwethiopia akisoma Isaya na akamwuliza iwapo alielewa aliyokuwa akisoma.
3. Mwethiopia alimwomba Filipo amsaidie kuelewa fungu hilo.
   a. Hili tu linatueleza kuwa mtu huyu alikuwa na njaa na kiu ya haki (Mt.5:6)!
4. Katika mst.32, 33 tunajifunza Mwethiopia alikuwa akisoma mahali tunapotambua kama Isaya 53:7,8.
5. Katika mst.34 Mwethiopia alimwuliza Filipo ikiwa nabii huyu alinena juu yake mwenyewe au juu ya mtu mwingine katika mistari hii.
   a. Kusema ukweli, tunatambua kuwa fungu kuanzia Isa.52:13-53:12 ulikuwa unabii juu ya Kristo, Masihi, Mwokozi.
   b. Kusema ukweli, ni moja ya unabii mkubwa na uliobainishwa Mungu akitabiri kuja kwa Mwanawe mpendwa kama Mtumishi mwenye Mateso, ambaye juu yake Bwana akamtwika maovu yetu yote.

### g. (8:35-40) FILIPO ALIHUBIRI KRISTO NA TOWASHI ALITII

**8:35)**
1. Katika kujibu swali la Mwethiopia juu ya nani Isaya alikuwa akimzungumzia, Filipo akaanza kwa andiko lilo hilo na akamhubiri Yesu.
2. Kwa maneno mengine, Filipo alikuwa akisema kwa uvuvio kuwa unabii wa Isa.53 ulitimilika katika Yesu Bwana.
3. Ingawa inabainishwa katika mstari huu kwamba Filipo "akamhubiri Yesu", hii ni zaidi ya kutamka tu jina la Yesu, kama tulivyoona awali katika sura hii, na kama tutakavyoona katika katika mistari kadhaa inayofuata.

**8:36-39)**

1. Wakawa wakiendelea njiani Filipo na Mwethiopia, wakafika mahali penye maji kisha Mwethiopia akauliza nini kilimzuia asiweze kubatizwa.
2. Lakini, kwa nini Mwethiopia aliuliza juu ya ubatizo? Ni wapi alijifunza juu ya hitaji la kubatizwa?
   a. Katika mst.35 tulichoelezwa tu ni kwamba Filipo akamhubiri Yesu kwa Mwethiopia.
   b. Mwethiopia alikaribia kwenye maji, akauliza nini kilikuwa kinamzuia asibatizwe.
   c. Hivyo basi, tunahatimisha kwamba kumhubiri Yesu ni pamoja na kuhubiri hitaji la kubatizwa majini ili kupokea msamaha wa dhambi!
   d. Tafadhali angalia somo letu katika 8:5 na mst.12.
3. Katika mst.37 Filipo alimwambia Mwethiopia kuwa akiamini kwa moyo wake wote, ingewezekana kubatizwa.
4. Mwetheopia alijibu na kukiri kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.
   a. Kwa bahati mbaya, wasomi wengi hawaamini kuwa mst.37 ilikuwepo katika maandishi ya asili ya Agano Jipya.
   b. Swali hili linajadiliwa kwa upekuzi wa mafungu (textual criticism), ambalo ni nje na kusudi la kozi hii.
   c. Hata hivyo, hata ingawa mstari huu haukuwepo katika maandishi ya asili, zoezi la kumkiri Kristo mbele za watu kabla ya kubatizwa imeandikwa vyema katika Agano Jipya.
   d. Kwa mfano, tafadhali angalia Mt.10:32,33; Rum.10:9,10; 1 Tim.6:13.
5. Baada ya kukiri bayana kwake Mkushi huyo, aliamuru gari lisimame.
6. Wote wawili wakatelemka kuingia majini, na Filipo akambatiza Mkushi.
7. Na Filipo alipokwisha kumbatiza Mkushi, “wote walili walipanda kutoka majini.”
8. Kama tulivyoeleza katika somo letu la 2:38, habari hii ya ubatizo wa Mkushi unadhihirisha bila shaka ubatizo wa kuzamishwa majini, wala si kumwagiwa au kunyunyiziwa maji.
   a. Tafadhali chunguza notisi zetu katika 2:38, kwa ushahidi zaidi ubatizo mmoja ulioamuriwa na Mungu leo ni kuzamishwa majini kwa ajili ya ondoleo la dhambi.
9. Pia, tafadhali angalia alichofanya Mkushi baada ya kuzamishwa. Aliondoka akifurahi!
10. Lakini, kwa nini alifurahi?
   a. Ni wazi alitambua kwamba kupitia utiifu wenye uadilifu na upendo kwa injili, alikuwa amepokea baraka kubwa za upendo wa Mungu, rehemu, na neema.
   b. Alitambua kuwa alikuwa amebatizwa kuingia katika Kristo ambamo hupatikana baraka zote za rohoni, ikiwa ni pamoja na msamaha, ukombozi, upatanisho, kufanyika mwana wa Mungu, amani, tumaini, furaha, n.k.!
11. Baada ya ubatizo huu, Roho Mtakatifu alimnyakua Filipo.
   a. Baadaye alionekana Azoto, mji ambao Wayahudi waliuita Ashdodi.
   b. Alihubiri katika miji mingi hata baadaye akafika mji wa Kaisaria.
   c. Hatutasoma tena kuhusu Filipo hata 21:8 ambapo alionekana katika mji uo huo wa Kaisaria.
12. Ukirejea nyuma katika sura 8, tumeisha kujifunza habari tatu za jinsi gani ya watu walifanya ili kuokolewa katika siku ambazo mitume na wengine walihubiri kwa uvuvio.
   a. Katika mst.5-12 Wasamaria walisikia injili, waliiamini, na wakabatizwa.
   b. Katika mst.13 Simoni mchawi walisikia injili, akaiamini, na akabatizwa.
   c. Na katika mst.30-39 Mkushi afisa alisikia injili, akaiamini, akamkiri Yesu, na kubatizwa.
13. Kuangalia kwa ufupi 8:1-40, kuenea kwa kanisa kupitia kazi ya Filipo.
   a. 8:1-3 Sauli aliliharibu kanisa.
   b. 8:4 Matokeo – injili ikazidi kuenea!
   c. 8:5-13 Filipo alimhubiri Kristo na ufalme wake katika Samaria / wengi wakabarizwa, ikiwa ni pamoja na Simoni mchawi.
   d. 8:14-17 Petro na Yohana walitumwa kuwawekea mikono Wasamaria na kuwapa Roho Mtakatifu.

    e. 8:18-25 Simoni alijaribu kununua uwezo huu.
    f. 8:26-34 Filipo alitumwa kumwona Mkushi towashi.
    g. 8:35-40 Filipo alimhubiri Kristo na towashi akatii.
14. Mtazamo kwa ujumla wa 9:1-43, Uongofu wa Sauli / Petro amfufua Dorkasi.
    a. 9:1,2 Sauli aliendelea kulitesa kanisa.
    b. 9:3-9 Yesu alimkabili Sauli, ambaye aliuliza, "Bwana unataka nifanye nini?" (KJV)
    c. 9:10-19 Anania alimtuma Sauli / Sauli alibatizwa.
    d. 9:20-23 Sauli alihubiri Kristo katika Dameski.
    e. 9:24-31 Sauli alijaribu kujiunga na wanafunzi Yerusalem / Barnaba alimsaidia.
    f. 9:32-35 Petro alimponya Ainea huko Lida.
    g. 9:39-43 Petro amfufua Dorkasi huko Yafa.

### 2. (9:1-43) UONGOFU WA SAULI / PETRO AMFUFUA DORKASI
### a. (9:1,2) SAULI AZIDI KULITESA KANISA

1. Sauli aliendelea kudhihirisha chuki yake juu ya Wakristo kwa kwawatishia, ikiwa ni pamoja na mauaji.
2. Hata akaomba kibali toka kwa kuhani mkuu ili kuwafunga Wakristo toka Dameski na kuwaleta Yerusalem kushitakiwa.

### b. (9:3-9) YESU ANAKABILIANA NA SAULI, ALIYEULIZA, "BWANA, UNINITAKA NIFANYE NINI?" (KJV)

**9:3-6)**

1. Sauli alivyokabili Damaski, alizingirwa na mwanga mkali kutoka mbinguni.
2. Sauli akaanguka chini na Yesu akamwuliza kwa nini alikuwa akimwudhi Yesu.
    a. Tafadhali angalia kwamba Sauli alikuwa akiwatesa Wakristo.
    b. Lakini Yesu alisema kwamba Sauli alikuwa akimtesa yeye!
    c. Basi, mtu akiwatesa Wakristo, wanamtesa Yesu! Lakini, kwa nini ni hivyo?
    d. Ni kwa sababu ni kichwa cha mwili wake wa kiroho, kanisa, na Wakristo mmoja mmoja ni viungo vya mwili (Efe.1:22,23; 5:30).
3. Sauli, alitetemeka kwa hofu na kustaajabia, akimwuliza Bwana ni nini alichotaka Sauli afanye.
4. Yesu alimwambia Sauli angie mjini, ambamo angeelezwa yampasayo kutenda ("upasayo" kutenda).

**9:7-9)**

1. Wale waliokuwa pamoja na Sauli walistaajabia kwa sababu walisikia sauti lakini hawakumwona mtu yeyote.
2. Aliponyanyuka Sauli alikuwa kipofu na aliongozwa kwa kushikwa mkono kuingia Dameski.
3. Katika Dameski Sauli aliyepofuka macho alishinda siku tatu bila kula na kunywa.
    a. Hivyo basi, Sauli bila shaka alimwamini Bwana na kutubu dhambi zake juu ya Bwana na kanisa lake.
    b. Walakini, hakusamehewa dhambi zake.
    c. Alikuwa bado hajaelezwa mambo yaliyompasa kufanya ili kupokea msamaha wa dhambi.
    d. Hivyo basi, ni bayana Sauli hakuokolewa akiwa njiani kuelekea Dameski kama baadhi wanavyodai leo!

### c. (9:10-19) ANANIA ATUMWA KWA SAULI / SAULI ABATIZWA

**9:10-12)**

1. Anania ametajwa kuwa mwanafunzi wa Yesu aliyeishi Dameski.
2. Bwana akamtokea Anania katika maono na kumweleza kwenda kwa Sauli, aliyekuwa akiomba.
   a. Angalia, Sauli alikuwa akiomba.
   b. Si tu alikuwa hajala chakula na kutokunywa maji kwa siku tatu, inadhihirisha imani na toba aliyokuwa nayo.
   c. Alikuwa akiomba pia.
   d. Kulingana na watu wengi katika dini siku hizi, Sauli alikuwa bila shaka ameokoka kutoka dhambini.
   e. Walakini, kulingana na Mungu, mtu huyu mwenye kuamini na kutubu, aliyekuwa akiomba hakuokoka bado.
   f. Alikuwa angali dhambini na alitakiwa aelezwe yapasayo kufanya ili kupokea msamaha.
   g. Basi, wale wote wanaofundisha leo kwamba anachopaswa mtu kufanya leo ili aokoke ni kumwamini Bwana, kutubu dhambi zake, na kuomba "sala ya toba" wanafundisha fundisho la uongo!
3. Bwana alimweleza Anania kwamba Sauli pia alikuwa na maono, ambamo alimwona Anania akiweka mikono juu ya Sauli ili aweze kuona tena.

**9:13-16)**
1. Katika mst.13,14 Anania alipinga kwenda kwa Sauli kwa sababu ya madhara aliyosababisha juu ya Wakristo.
2. Hata hivyo, Bwana akarudia agizo lake kwa Anania kwenda kwa Sauli.
   a. Bwana pia akamhakikishia Anania kwamba Sauli alikuwa chombo chake cha kuchukua ujumbe wake kwa Mataifa, Wafalme, na Waisraeli.
   b. Katika mst.16 Bwana akamwambia Anania kwamba Sauli angeteseka mambo mengi kwa ajili ya kazi ya Bwana.

**9:17-19)**
1. Katika mst.17 tunajifunza Anania alikwenda kwa Sauli kama Bwana alivyomwamuru.
2. Alimweleza Sauli alitumwa na Bwana kwa mambo mawili:
   a. Ili Sauli aweze kuona tena.
   b. Na kwamba Sauli aweze kujazwa Roho Mtakatifu.
3. Katika mst.18 Sauli alipata kuona tena.
4. Baada ya hapo, aliinuka na kubatizwa.
5. Baada ya kubatizwa hatimaye Sauli alikula chakula na kupata nguvu.
6. Kisha akawa na Wakristo wenzake Dameski kwa siku kadhaa.
7. Kabla ya kuendelea, tunapaswa kujadili kwa maelezo kidogo mambo kadhaa yanayoonekana katika mistari hii.
8. Kwanza katika mst.17 Anania alimtaja Sauli kuwa "ndugu Sauli" kabla ya Sauli kubatizwa kuingizwa katika familia ya Mungu.
   a. Kuzingatia ukweli huo, wengine wamedai kuwa Sauli alikuwa Mkristo, mwana wa Mungu, kabla ya kubatizwa.
   b. Walakini, madai hayo ni ya uongo.
   c. Madai hayo ni ya uongo, katika nyongeza kwa matumizi yake katika Ukristo, neno "ndugu" lilikuwa neno lililotumika kwa hao walikuwa Wayahudi kwa asili, hata ingawa mtu hakuwa Mkristo bado.
      (1) Kwa mfano, mapema katika kitabu hiki, Petro alifanya hivi katika kuwataja waliokuwa Wayahudi kwa asili ambao hawakutii injili bado (linga. 2:29; 3:17).
      (2) Pia, Paulo aliwataja "kwa ajili ya ndugu zangu katika mwili", k.m. uhusiano wake kwa wenye asili ya Kiyahudi kama "ndugu" zake, hata ingawa hawakutii injili.
      (3) Kwa kufanya hivyo, watu hawa waliovuviwa, kama vile Anania katika tukio hili, yalikuwa yakirejea kwa watu wenye asili ya Kiyahudi kwa kawaida au uzao huo.

(4) Hawakurejea kwa wasikilizaji kama ndugu katika Kristo kabla hawajabatizwa kuingia katika Kristo!
(5) Hilo ni kweli kwa sababu mtu hafanyiki mwana wa Mungu na hivyo kuitwa ndugu katika Kristo hata imani imemsukuma na kubatizwa kuingia katika Kristo (Gal.3:26,27).

9. Pili, wengine huuliza ni wapi Anania alipata uwezo wa kimiujiza kumponya Sauli upofu wake.
   a. Kama tulivyoona, kulikuwa na njia mbili tu za kupokea uwezo wa kimiujiza karne ya kwanza.
   b. Njia hizo mbili zilikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu na ile ya kuwekewa mikono na mitume.
   c. Kuna matukio mawili tu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na Anania hajakuwemo hata mojawapo ha hayo.
   d. Hivyo basi, tunahatimisha kuwa Anania alipokea uwezo wa kimiujiza kwa njia ya kuwekewa mikono na mitume wa Kristo.
10. Tatu, moja ya sababu Bwana alimtuma Anania kwa Sauli ili "ajazwe Roho Mtakatifu" (mst.17).
   a. Tunapaswa kutambua ama, katika tukio hili, maneno "ajazwe Roho Mtakatifu" yanarejea kupokea Paulo uwezo wa kutenda miujiza, au kitu kingine tofauti.
      (1) Kwanza, katika somo letu la 6:2-4 tunaona maneno haya dhahiri yakilenga kukaa kwa hali ya kawaida kwa Roho Mtakatifu kwa namna ambayo si ya kutenda miujiza.
         (a) Kusema ukweli, tulihatimisha namna hiyo kutokana na matumizi ya maneno yaliyokuwa yakirejea kwa wale saba katika sura 6, ikiwa ni pamoja na Stefano na Filipo.
         (b) Pia utakumbuka kwamba kukaa huku kwa kawaida, au kujawa Roho Mtakatifu kulianza wakati mtu alipotii injili, ikiwa ni pamoja na kuzamishwa majini kwa ajili ya kupokea msamaha wa dhambi (2:38; 3:19; 5:32).
         (c) Basi, inawezekana kuwa Anania kumwendea Sauli ili aweze "ajazwe Roho Mtakatifu" ilirejea kukaa kwa hali ya kawaida kwa Roho Mtakatifu.
         (d) Na Sauli kupokea hali ya kawaida ya kukaa Roho Mtakatifu ingeanza pale ambapo angebatizwa kuingia katika Kristo.
      (2) Pili, ukiwa na msingi huo wa maelezo akilini mwako, tunapojifunza mazingira, ni wazi kwamba maneno haya yalirejea hali ya kawaida ya Paulo kupokea Roho Mtakatifu ambaye alimpokea wakati alipobatizwa kuingia katika Kristo.
         (a) Mst.17 – Anania alitumwa kwa Sauli ili kwamba aweze (1) kupata kuona tena, na (2) ajazwe Roho Mtakatifu.
         (b) Mst.18 – Anania alipofika kwa Sauli, Sauli alipata (1) alipata kuona, na (2) akabatizwa (mst.18).
         (c) Tukijumuisha mistari hiyo miwili basi, tunapata ukweli ufuatao:
            1. Anania alitumwa ili kwamba Sauli apate kuona tena (mst.17), na Sauli akapata kuona tena (mst.18).
            2. Anania alitumwa kwa Sauli apate kujazwa Roho Mtakatifu (mst.17), na Sauli akabatizwa (mst.18).
         (d) Hatimisho sahihi pekee ni kwamba Sauli alibatizwa, akajazwa Roho Mtakatifu.
         (e) Hivyo ni kwamba, alipokea Roho Mtakatifu akikaa kwa hali ya kawaida ambaye hupokelewa na waumini wote ambao hutubu na kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi (2:38; 3:19; 5:32).
      (3) Tatu, njia nyingine kwa maneno haya yanayorejea kukaa Roho Mtakatifu kwa hali ya kawaida katika swala hili ni kuhusu Sauli kupokea karama za Kimiujiza za Roho Mtakatifu.
         (a) Walakini, kama tulivyoona, kulikuwa na njia mbili tu ambazo kwa hizo uwezo wa kimiujiza ungepatikana.

(b) Njia hizo mbili zilikuwa ni kwa njia ya ubatizo wa Roho Mtakatifu na kwa kuwekewa mikono na mitume.
(c) Ni dhahiri kwamba Sauli hakubatizwa kwa Roho Mtakatifu katika tukio hili.
(d) Ni dhahiri pia kwamba Anania hakuwa mtume wa Kristo.
(e) Hivyo basi, Anania hakuwa na uwezo wa kimiujiza kumwekea mikono Sauli kwa namna ya kupokea karama ya miujiza ya Roho Mtakatifu.
(f) Basi, alichopokea Sauli siku hiyo haikuwa karama ya miujiza ya Roho Mtakatifu.
(g) Hii ni njia moja ya kutambua kwamba alichopata Sauli siku hiyo ilikuwa hali ya kawaida ya kukaa Roho Mtakatifu ikiwa ni matokeo ya ubatizo wake kuingia katika Kristo!

**d. (9:20-23) SAULI ALIHUBIRI KRISTO DAMESKI**

**9:24,25)**

1. Sauli alitambua mipango ya Wayahudi ya kutaka kumwua, na Wayahudi wenzake walimsaidia kutoroka katika kapu kwa njia ya ukuta.

**9:26,27)**

1. Sauli alikwenda Yerusalem na kujaribu kujiunga na Wakristo, lakini walimwogopa kuona kwamba hakuwa mwanafunzi wa kweli wa Yesu.
2. Barnaba aliwathibitishia habari za Sauli kukabiliwa na Yesu na ujasiri wake wa kumhubiri Yesu katika Dameski.

**9:28-30)**

1. Sauli alifanya kazi kwa ushujaa katika kanisa la Yerusalem, akimhubiri Yesu na akishindana na Wayahudi wa Kiyunani.
2. Kama matokeo, Wayahudi wa Kiyunani walijaribu kumwua.
3. Wakristo wenzake Sauli walitambua nia ya Wayahudi wa Kiyunani, wakamchukua na kumchukua Kaisaria, kisha wakampeleka aende Tarso.

**9:31)**

1. Baada ya kipindi hiki cha mateso, kanisa likafurahia amani na likaimarishwa (likajengwa, likatiwa nguvu).
2. Kanisa limetajwa kama likienenda (kuishi) katika mambo mawili:
   a. Kicho cha Bwana (heshima, staha, unyenyekevu juu ya Mungu na amri zake) (linga.10:35).
   b. Na katika faraja ya Roho Mtakatifu.
      (1) Faraja iliyotokana na neno la Mungu, kama lilivyofunuliwa na Roho Mtakatifu na kuandikwa katika Biblia (linga. Rum.15:4).
      (2) Faraja iliyopatikana katika kutambua kuwa Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Wakristo kama muhuri wa kukubaliwa na Mungu na arabuni ya malipo yake juu ya urithi wetu wa milele (linga. Efe.1:13,14).
3. Wakristo wa karne ya kwanza hawakuishi tu katika kicho cha Bwana na faraja ya Roho Mtakatifu.
4. Walikuwa pia wakiongezeka katika idadi ("kuongezeka").
5. Katika mazingira yanayofuata mhusika anabadilika kutoka Sauli na kuwa Paulo.
6. Lakini kabla ya kumwacha Sauli kwa kitambo kidogo, tunataka kuhatimisha yale tuliyojifunza juu ya uongofu wake kwa Bwana.
   a. Mst.4,5 Bwana akamtokea Sauli katika maono akiwa njiani kwenda Dameski.
   b. Mst.6 Sauli alimwuliza Bwana alimtaka Sauli afanye nini.
   c. Mst.6 Bwana akamwambia Sauli aingie Dameski, ambamo angeambia "yaliyompasa" kutenda.
   d. Mst.7 Ktika Dameski Sauli alikaa siku tatu bila kula wala kunywa.

(1) Hii ilidhihirisha imani yake katika Bwana, huzuni juu ya dhambi zake, na toba.
e. Mst.11 Wakati huo alikuwa akisali.
   (1) Walakini, alikuwa hajaokolewa bado kutoka dhambini kwa sababu alikuwa hajaelezwa mambo yaliyompasa kutenda.
f. Mst.17,18 Bwana alimtuma Anania kwa Sauli na akambatiza.
   (1) Kama matokeo ya imani, toba, na ubatizo, Sauli alimpokea Roho Mtakatifu katika hali yake ya kukaa kwa kawaida ("ukajazwe Roho Mtakatifu").
   (2) Hali hii ya Roho Mtakatifu kukaa kwa kawaida hutokea mtu anapoamini na kutubu na kuzamishwa majini ili kupata msamaha wa dhambi (2:38).
   (3) Inatokea tu mara mtu anapotubu na kuongolewa (ikiwa ni pamoja na ubatizo) ili dhambi zake zipate kufutwa (3:19).
   (4) Inatokea tu baada ya mtu kumtii Bwana (5:32).

7. Kutokana na ukweli huo wa Biblia tunaweza kuhatimisha mambo sahihi yafuatayo:
   a. Sauli hakuongolewa na kuokoka toka dhambini akiwa njiani kwenda Dameski alipopata maono kutoka mbinguni.
   b. Sauli hakuongolewa na kuokoka mara tu alipoamini katika Bwana.
   c. Sauli hakuongoka na kuokoka alionyesha huzuni na toba kwa kukaa bila kula na kunywa kwa siku tatu.
   d. Sauli hakuongoka na kuokoka alipoomba baada ya kufanya mambo mengine hayo yote.
   e. Sauli aliongoka na kuokoka tu baada ya kufanya mambo hayo yote na akabatizwa kuingia katika Kristo ili kupata msamaha wa dhambi!
8. Kwa bahati nzuri, kuna habari sehemu zingine mbili juu ya uongofu wa Sauli katika kitabu hiki.
   a. Moja inapatikana katika sura 22, na nyingine iko sura 26.
   b. Habari katika 22:16 imebainisha zaidi juu ya somo hili jinsi Sauli alivyookoka toka dhambini.
   c. Ni kweli hilo kwa sababu ya yale Bwana alimtuma Anania kumweleza Sauli alichopaswa kufanya.
   d. Kumbuka kwamba jambo hili lilikuwa baada ya Sauli kuona maono, alimwamini Bwana, alitubu, na kuomba.
   e. Walakini, baada ya kufanya mambo hayo yote, alikuwa angali dhambini!
   f. Tafadhali soma mstari huo kutambua Mungu alichomwambia msemaji wake Anania kumweleza Sauli kufanya "uoshe dhambi zako"!
   g. Hivyo basi, kama tulivyojifunza awali, mstari huu wenye uvuvio unathibitisha kwamba kulingana na Mungu ni muhimu kubatizwa ili kuosha dhambi!

### f. (9:32-35) PETRO AMPONYA AINEA LIDA

**9:36)**

1. Petro alitelemka kuelekea kwa Wakristo walioishi Lida.
   a. Katika mst.32 angalia jinsi Luka alivyowaita Wakristo kwa uvuvio.
   b. Aliwaita "watakatifu."
      (1) Neno hili linamaanisha aliyejitenga na dhambi na kujiweka wakfu, kujitakasa, waliojitoa kwa Mungu.
      (2) Basi, katika kipindi cha Agano Jipya, neno hili lilitumika kuelezea kila Mkristo.
      (3) Ni dhahiri basi, vikundi vinavyotumia leo neno hilo kwa kuhifadhi neno "mtakatifu" kwa watu maalum watakatifu waliokubaliwa au kupigiwa kura na baraza au viongozi wa dini si jambo la kimaandiko!
2. Katika Lida, Petro alimkuta mtu aliyepooza ambaye alikuwa kitandani kwa muda wa miaka nane.
3. Petro akamponya mtu huyo kwa jina la Yesu Kristo.
   a. Tena, ni muhimu kutambua kuwa mtu huyo aliyepooza akanyanyuka mara moja!
4. Watu wengi katika eneo hilo waliponywa na wakaitikia kwa kumgeukia Bwana.

## g. (9:36-43) PETRO ALIMFUFUA DORKASI KATIKA YAFA

**9:36)**

1. Katika mst. 36 mwelekeo ulihamia Yafa.
2. Mwanamke Mkristo kwa jina Tabitha aliishi katika mji huo.
   a. "Tabitha" limetafsiriwa "Dorkasi" lenye maana "paa" au "swala".
3. Dorkasi alikuwa Mkristo mwaminifu aliyetumika kama mfano bora kwetu leo.
   a. Ametajwa kama mwanamke "aliyejaa matendo mema na sadaka alizozitoa"!
   b. Hakika, mwanamke huyu Mkristo safi alikuwa miongoni mwa "wenye juhudi katika kutenda matendo mema" (Tit.2:14; 3:1,14)!

**9:37-39)**

1. Dorkasi akaugua na kisha kufa.
2. Wakristo walimwendea Petro katika Lida, wakimsihi aende huko haraka.
3. Petro akapanda juu orofani ambamo waliulaza mwili wa Dorkasi.
4. Angalia baadhi ya wajane walikuwa wakilia kwa sababu ya kumpoteza Mkristo huyu mwema.
5. Wajane pia walimwonyesha Petro nguo ambazo Dorkasi aliwatengenezea kwa sababu ya upendo wake kwao.
6. Linga. Ufu.14:13.

**9:40,41)**

1. Petro akawatoa watu hao chumbani, akamfufua Dorkasi kutoka kwa wafu, na kupeleka kwao akiwa hai.
2. Hii ni mara ya kwanza habari kuandikwa mitume wakimfufua mtu toka kwa wafu.
3. Kama matokeo ya maajabu hayo wengi wakamwamini Bwana.
4. Petro akakaa Yafa katika nyumba ya Simon, ambaye alikuwa mtengeneza ngozi.
5. Mtazamo kwa ujumla wa sura ya 8 na 9, Kanisa liliongezeka kijiografia.
   1. 8:1-40 Kukua kwa kanisa kufuatia kazi ya Filipo.
      a. 8:1-3 Sauli aliliudhi kanisa.
      b. 8:4 Matokeo – injili ikazidi kuenea!
      c. 8:5-13 Filipo akamhubiri Kristo na ufalme wake Samaria / wangi wakabatizwa, ikiwa ni pamoja na Simon mchawi.
      d. 8:14-17 Petro na Yohana walitumwa kuwawekea mikono Wasamaria ili kupokea Roho Mtakatifu.
      e. 8:18-25 Simoni alijaribu kununua uwezo huo.
      f. 8:26-34 Filipo alitumwa kwa towashi Mkushi.
      g. 8:35-40 Filipo alimhubiri Kristo na towashi akatii.
   2. 9:1-43 Uongofu wa Sauli / Petro amfufua Dorkasi.
      a. 9:1,2 Sauli akazidi kuliharibu kanisa.
      b. 9:3-9 Yesu akabiliana na Sauli, ambaye aliuliza, "Bwana, unataka nifanye nini?" (KJV).
      c. 9:10-19 Anania alitumwa kwa Sauli / Sauli akabatizwa.
      d. 9:20-23 Sauli akamhubiri Kristo Dameski.
      e. 9:24-31 Sauli alijaribu kujiunga na wanafunzi Yerusalem / Barnaba amsaidia.
      f. 9:32-35 Petro amponya Ainea katika Lida.
      g. 9:36-43 Petro alimfufua Dorkasi Yafa.
6. Mtazamo kwa mfupi wa sura 10-12, kanisa likatanuka kijiografia.
   1. 10:1-11:30 Mlango kufunguka kwa Mataifa .
   2. 12:1-25 Mateso kutoka katika serikali iliyokuwepo.
      a. 10:1-11:30 Mlango unafunguka kwa Mataifa.
         (1) 10:1-8 Aliongozwa na malaika, Kornelio alitumwa kwa Petro.

(2) 10:9-16 Petro aliona maono.
(3) 10:17-22 Wajumbe toka kwa Kornelio walimtaka Petro.
(4) 10:23-29 Petro na Kornelio walikutana.
(5) 10:30-33 Kornelio alimweleza sababu ya kutumwa kwake Petro.
(6) 10:34-43 Ujumbe wa Petro kwa Kornelio na watu wa nyumbani kwake.
(a) 10:34,35 Mungu hana upendeleo.
(b) 10:36,37 Amani kwa njia ya Yesu, Bwana wa wote.
(c) 10:38 Yesu: Alidhihirishwa na Baba kwa njia ya miujiza.
(d) 10:39 Yesu: Alisulibishwa na Wayahudi.
(e) 10:40,41 Yesu: Alifufuliwa na Baba na kuonekana dhahiri.
(f) 10:42 Yesu: Mhukumu wa watu wote.
(g) 10:43 Yesu: Alitabiriwa na manabii – msamaha kwa njia ya yeye.

h. 10:44-46 Roho Mtakatifu alimshukia Kornelio na watu wa nyumbani mwake.
i. 10:47,48 Petro aliamuru ubatizo wa maji.
j. 11:1-3 Watu wengine Yerusalem walishindana na Petro kwa kuwa alikwenda kwa watu wa Mataifa.
k. 11:4-17 Maelezo ya Petro.
(1) 11:4-10 Maono.
(2) 11:11,12 Wajumbe kutoka kwa Kornelia.
(3) 11:13,14 Kornelio alimweleza sababu ya kutumwa Petro kwake.
(4) 11:15-17 Kushuka kwa Roho Mtakatifu na kusudi lake.

l. 11:18 Majibu ya walioshindana na Petro.
m. 11:19-21 Kazi ya waliotawanyika (8:4) katika Antiokia.
n. 11:22-24 Yerusalem ikamtuma Barnaba Antiokia.
o. 11:25,26 Barnaba alimleta Sauli kutoka Tarso.
p. 11:27-30 Mwanamke atabiri / Antiokia ikatuma msaada Yerusalem kwa mkono wa Barnaba na Sauli.

**B. (10-12) KANISA LILIENEA KIMATAIFA**
**1. (10:1-11:30) MLANGO UNAFUNGUKA KWA MATAIFA**

**a. (10:1-8) ALIONGOZWA NA MALAIKA, PETRO ALITUMWA KWA KORNELIO**

10:1,2)

1. Karnelio ametambulishwa kuwa ni askari wa Rumi aliyeishi Kaisaria.
   a. Alikuwa "akida" – kamanda katika jeshi la Rumi, mwenye kusimamia askari 100.
2. Ni dhahiri kutokana na mazingira kuwa Kornelio alikuwa Mmataifa, wala si Myahudi (linga. 11:1-3).
3. Ukweli kwamba Kornelio alikuwa mcha Mungu na imedhihirika wazi katika maelezo ya mst.2.
4. Ukizingatia hayo, tafadhali angalia mambo matano ambayo Mungu anamwelezea mtu huyu:
   a. "mtaua" – mwenye mawazo na hisia kali juu ya dini.
   b. "mwenye kumcha Mungu" – alikuwa mwenye heshima kubwa, kicho, hofu yenye afya juu ya Mungu mmoja wa kweli na aliye hai.
   c. "pamoja na nyumba yake yote" –
      (1) Neno lililotafsiriwa "watu wa nyumbani" inawezekana kujumuisha si familia yake tu, bali pia watumishi na wafanya kazi wake.
      (2) Basi, Kornelio alikuwa na ushawishi katika familia yake, watumishi, n.k. kufuata maongozi yake katika kumcha Mungu.
      (3) Hakika, hapa si watoto wachanga na wale ambao hakuwa na umri wa kutosha kumcha Mungu!

   d. "yeye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi" – alikuwa mwema katika kusaidia watu walikuwa wahitaji.
   e. "na kumwomba Mungu daima" – alikuwa mtu wa sala.
5. Tunapojifunza maelezo ya Mungu kuhusu Kornelio, ni dhahiri alikuwa mtu mwema sana, aliyekuwa anatafuta kujifunza na kuyatenda mapenzi ya Mungu.
6. Walikini, kama vile mfano wa Sauli, Kornelio alihitaji mtu kumwendea na kunena, "maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote" (11:14).
7. Hivyo basi, Kornelio hakuokolewa kwa kuwa mwema, mtauwa mwenye kumcha Mung, aliyesaidia watu, na kumwomba Mungu daima!
8. Mambo hayo yote yalikuwa mazuri, lakini hayakutosha!
9. Kornelio na watu wa nyumbani mwake walihitaji kusikia maneno yakueleza mambo yaliyowapasa kufanya ili wapate kuokoka!

**10:3-8)**

1. Kornelio aliona maono ndani yake alimwona malaika wa Mungu akimjia.
2. Malaika alimweleza Kornelio kuwa sala na sadaka zake zilifika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu (k.m., Mungu alikuwa amesikia sala zake – mst.31).
3. Katika mst.5,6 malaika alimweleza Kornelio atume watu kumwita Petro atakayemweleza "yakupasayo kufanya".
   a. Hivyo basi, habari ya Kornelio inalingana na ile ya Mkushi mwenye cheo tuliyojifunza katika sura 8.
   b. Katika kila tukio kulikuwa na mtu mwema, mcha Mungu, aliyekuwa akitafuta mapenzi ya Mungu.
   c. Katika kila tukio kuna kuhusika kwa malaika wa Mungu.
   d. Walakini, katika matukio yote mawili, malaika hawakueleza hao watu nini cha kufanya ili waokolewe.
   e. Kama vile katika swala la Sauli, Bwana hakumweleza yaliyompasa kufanya ili kuokoka.
   f. Kinyume chake, katika swala la Mkushi, malaika alimweleza Filipo kwemwendea na kuzungumza na Mkushi.
   g. Katika swala la Kornelio malaika alimweleza Kornelio kutuma watu kumwita Petro ambaye angemweleza yapasayo kufanya.
   h. Na katika swala la Sauli Bwana alimweleza Sauli kwenda Dameski ambako angeelezwa yaliyompasa kufanya.
   i. Hivyo basi, hata kipindi cha miujiza cha karne ya kwanza, Mungu hakuwaeleza watu moja kwa moja au kupitia malaika mambo yaliyowapasa kufanya ili waokoke.
   j. Badala yake, Bwana alimtumia wanadamu kama wasemaji wake kuwaeleza watu mambo yaliyowapasa kufanya ili waokoke.
   k. Kama ilikuwa hivyo kipindi cha miujiza, je tutarajie mambo tofauti siku zetu hizi ambapo miujiza haitendeki tena?!
4. Kornelia mara moja aliitika kwa malaika kwa kuwatuma watumishi wawili na askari kwa Petro.

### f. (10:9-16) PETRO ALIONA MAONO

1. Petro alipokuwa akisali, aliangukia katika hali karibia na kuzimia ("trance") na akaona maono.
2. Katika maono hayo aliona chombo kama nguo kubwa ikishuka toka mbinguni.
3. Na katika nguo hiyo kulikuwa na aina zote za wanyama na ndege.
4. Bwana akanena na Petro na kumweleza kuchinja na kula wanyama.
5. Petro alikataa kula wanyama, akisema hajawahi kula chochote kilicho "kichafu au najisi".
6. Bwana akajibu kwa kusema alichokitakasa yeye, Petro asikiite kichafu au najisi.
7. Jambo hili lilitendeka mara tatu na kisha nguo kubwa nyeupe ilichukuliwa kwenda mbinguni.

8. Ili kuelewa maono haya sawasawa, ni muhimu kukumbuka mambo fulani ya kweli kutoka katika Agano la Kale.
    a. Katika Agano la Kale hilo, Mungu alitoa tofauti ya wanyama hao, ukijumuisha wanyama, waliokuwa watakatifu (safi) na vitu ambavyo vilikuwa visivyo safi (vichafu na najisi) (Law.11:2-27; Kumb.4:3-20).
    b. Vitu vilivyokuwa vitakatifu na safi vilikubalika kwa matumizi au kwa kula , wakati vitu visivyo safi, vichafu na najisi vilikatazwa katika matumizi na kula.
    c. Hivyo basi, Petro alipoelezwa kula wanyama alitambua kuwa wachafu au najisi, alikataa kufanya hivyo.
    d. Kwa nyongeza, Wayahudi waliwatambua watu wa Mataifa kama Kornelio na wale wa nyumbani mwake kama wasio safi, wachafu au najisi.
    e. Kwa hiyo, walijizuia kutokutana na Mataifa (linga.28).
    f. Lakini, Petro alielezwa katika maono haya kwamba alichokitasa Mungu, Petro asikiite kichafu au najisi.
9. Kama tutakavyoona katika sehemu inayofuata Petro kahuelewa maana ya maono hayo.
10. Walakini, baadaye, alielewa kwamba maono yalimaanisha kwamba Mungu alihitaji injili kuhubiriwa kwa Mataifa, kama vile kwa walio wa asili ya Kiyahudi (linga.10:28).
11. Kwa maono haya Mungu alibainisha kwa Petro kwamba aliwaona watu wa Mataifa kuwa wanastahili kupokea ujumbe wa wokovu.
12. Maono haya makubwa sana yalikuwa muhimu kwa sababu kufikia wakati huu mitume na watu wengine hawakuwa wamehubiri injili kwa Mataifa.
13. Hili halikufanyika mbali na agizo la Bwana kwenda kuhubiri injili katika dunia nzima na kwa kila kiumbe (Mt.28:18-20; Mk.16:15,16; Mdo.1:8).

### g. (10:17-22) WAJUMBE KUTOKA KWA KORNELIO WAMWITA PETRO

1. Wakati Petro alikuwa akitafakari nini maana ya maono hayo, wajumbe watatu kutoka kwa Kornelio walifika mahali alipoishi Petro.
2. Katika mst.19,20 Roho Mtakatifu alimweleza Petro kwenda pamoja na watu hao watatu kwa sababu Roho Mtakatifu aliwatuma hao kwenda kwa Petro.
3. Kisha Petro alitelemka huko na kuuliza kwa nini wajumbe walimjia.
4. Walimjibu Kornelio kuwa aliongozwa Kimungu kwa njia ya malaika kumwita Petro kwenda nyumbani "kusikia maneno" kutoka kwa Petro.

### h. (10:23-29) PETRO NA KORNELIO WAKUTANA

**10:23,24)**
1. Petro akaondoka pamoja na wajumbe na baadhi ya ndugu kwenda Yafa.
2. Walipofika nyumbani kwa Kornelio alikuwa akiwasubiri.
3. Siyo hivyo tu, lakini Kornelio aliwakusanya ndugu zake na marafiki wa karibu kusikia neno la Mungu pamoja naye!
4. Mtu huyo alikuwa na shauku ya kusikia ujumbe wa wokovu na alitaka ndugu zake na marafiki wake kufanya hivyo pia!
5. Mfano wa ajabu mzuri kwetu sisi!

**10:25,26)**
1. Kornelio alipomwona Petro akaanguka chini na kumwabudu.
2. Lakini Petro alikataa kukubali ibada hiyo, alidai kuwa alikuwa mwanadamu kama vile Kornelio.
3. Swali – ikiwa Petro alikuwa ni "Papa" wa kwanza kama inavyodaiwa na marafiki wetu Wakatoliki, basi kwa nini alikataa kuabudiwa na Kornelio?!
    a. Wengi wetu tumeona pengine picha ya "Papa" akipokea ibada ya wengine, kama mwakilishi wa Mungu duniani.

b. Walakini, Mungu anabainisha wazi kwamba hatupaswi kuabudu wanadamu. Kinyume chake tunapaswa kumwabudu Mungu na yeye pekee, kama Mungu wa kweli aliye hai (linga. Ufu.4:10; 14:7; 19:9,10).
c. Mistari kama hii inabainisha dhahiri kabisa jinsi ilivyo kinyume na maandiko na isiyo jambo la Kimungu mwanadamu mfu kukubali aabudiwe!
d. Sambamba na hayo, tafadhali kumbuka somo letu katika 8:24.
   (1) Katika mstari huo tuliona tofauti kubwa kati ya Roman Catholic na Ukristo safi, wa kweli wa Agano Jipya.
   (2) Katika mazingira hayo Petro alikataa kusamehe dhambi ya Simoni.
      (a) Kinyume chake, alimweleza Simoni masharti ya Mungu jinsi ya kupata msamaha kwa dhambi ya Mkristo.
      (b) Masharti hayo ni toba na kukiri dhambi hizo mbele za Mungu.
   (3) Kwa nyongeza, badala ya kumweleza Simoni aombe kupitia au kwa Petro kama "Papa" ili kupata msamaha, Petro alimweleza Simoni kumwomba Mungu!
e. Sasa katika mistari hii sura 10, tunaona tofauti nyingine kubwa kati ya Roman Catolic na Ukristo safi, na wa kweli wa Agano Jipya.
f. Inavunja moyo hasa kuona kwamba watu wameliacha kanisa la Agano Jipya kwa jinsi hiyo (1 Tim.4:1-3; 2 Thes.2:1-10).
g. Kwa imani na upendo wote, tunawasihi watu waachane vikundi hivyo vinavyopingana na maandiko vilivyobuniwa na wanadamu.
h. Tunatoa ombi hilo kwa sababu Bwana wetu Yesu alisema madhehebu kama hayo na watu wa jinsi hiyo walio ndani yake mwisho wao ni kutengwa na Mungu milele (Mt.15:8-13)!

**10:27-29)**

1. Petro alitoa mambo manne kwa watu waliokusanyika nyumbani kwa Kornelio.
   a. Haikuwa haki kwa mtu wa Kiyahudi kuwa karibu na watu wa mataifa mengine (kama vile Kornelio na watu wa nyumbani mwake) (linga. Law.18:24-30; Kumb.7:3-12; Yoh.4:9).
   b. Walakini, Mungu alimdhihirishia asimwite mtu yeyote mchafu au najisi. (Mungu alifanya hivyo katika maono).
   c. Kwa uhakika huo kutoka kwa Mungu, Petro alikwenda kwa Kornelio mara moja na bila kipingamizi.
   d. Tena, Petro alimwuliza Kornelio kwa nini alituma watu wamwite Petro.

### e. (10:30-33) KORNELIO AELEZA SABABU YA KUMWITA PETRO
### (1) (10:34,35) MUNGU HANA UPENDELEO

**10:34,35)**

1. Petro akahubiri kuwa Mungu hana upendeleo.
2. Hakika, Mungu hana upendeleo kiasi kwamba anamkubali kila mtu katika kila taifa anayefanya masharti ya Mungu.
3. Petro aliyataja masharti hayo kwa namna ya jumla kwa kueleza yafuatayo:
   a. "mtu amchaye" – wote walio na hofu hai, heshima, na staha kwa Mungu.
   b. "kutenda haki"
      (1) Wanaofanya mambo ambayo Mungu anayataja kuwa ni haki.
      (2) Bali amri zote za Mungu ni haki (Zab.119:172).
      (3) Kwa hiyo, kutenda haki maana yake kutenda amri za Mungu.
      (4) Kwa maneno mengine, mtu ni lazima ajitahidi kumtii Mungu kwa nguvu zake zote ili akubaliwe na Mungu (linga. Ebr.5:8,9).
      (5) Utiifu huo lazima utiririke kutoka katika moyo wenye imani na upendo kwa Bwana (Gal.5:6; Yoh.14:15).

4. Hivyo basi, mtu yeyote katika taifa lolote anayemcha Mungu na daima kujitahidi kumtii anakubaliwa na Mungu!
5. Kwa hiyo, kwa uvuvio, Petro alifungua mlango kwa Kornelio, watu wa nyumbani mwake, Mataifa yote, na yeyote atakayemcha Mungu na kutii mwenyezi Mungu.
6. Hakika kufikia hatua hii Petro alielewa vyema maono ambayo Mungu alimfunulia hapo mapema!

**(2) (10:36,37) AMANI KWA NJIA YA YESU – BWANA WA WOTE**
**(3) (10:38) YESU: ALIDHIHIRISHWA NA BABA KWA NJIA YA MIUJIZA**

**10:36-38)**
1. Katika mistari hii Petro alizungumzia kuhusu ujumbe ambao Mungu aliutuma kwa taifa la Israeli.
2. Tafadhali zingatia sehemu mbalimbali za ujumbe uliotajwa na Petro:
   a. “akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo”
      (1) Inarejea amani baina ya Mungu na mwanadamu, na matokeo ya amani ya ndani ambayo mtu anafurahia.
      (2) Amani hiyo ilitabiriwa Agano la Kale na ilijumuisha habari za kuja kwake Masihi (Isa.9:6; 53:5).
      (3) Na amani hiyo iliwezeshwa tu kwa damu ya thamani ya msalabani ya Kristo (Kol.2:1:20; Rum.5:1-11).
   b. “Ndiye Bwana wa wote”
      (1) Yesu anatawala malaika na wanadamu wote akiwa Mfalme (linga. Yoh.17:2; Mt.28:18; Efe.1:20-23).
      (2) Linga. 2:36.
   c. “neno …lililoenea Uyahudi wote…”
      (1) Ujumbe huo mwenye kuokoa ulihubiriwa kwa sehemu kubwa (linga.10:15-18).
      (2) Basi, walikuwa hawana udhuru wa kutokujua ujumbe!
   d. “jinsi Mungu alivyomtia mafuta Yesu kwa Roho Mtakatifu na nguvu,”
      (1) Baba alimtuma Mwanawe mpendwa aondoke akafanye kazi yake, pamoja na uwezo wa kufanya miujiza kwa njia ya Roho Mtakatifu.
      (2) Baba alionyesha kumkubali kwake Yesu kwa miujiza ambayo aliweza kuitenda (linga.2:22).
   e. “akitenda kazi njema.”
      (1) Fafanuzi ya ajabu juu ya maisha kwa ufupi ya Bwana wetu!
      (2) Alikuwa mtu alijitoa wakfu katika kutenda mambo ambayo Baba aliyaona kuwa mema (linga.Yoh.4:34; 6:38).
      (3) Je, si jambo jema ikiwa mambo hayo yatasemwa kwetu sisi sote!
   f. “na kuponya wote walioonewa na Ibilisi.”
      (1) Kati ya miujiza aliyotenda Yesu ilikuwa kuondoa pepo katika wale watu waliowapagawa.
      (2) Kama tulivyojifunza awali, hili linadhihirisha uwezo wa Yesu juu ya Ibilisi na uwezo wake.
   g. Tena, Baba alidhihirisha kumkubali Yesu kwa miujiza aliyoitenda.

**(3) (10:39) YESU ASULIBIWA NA WAYAHUDI**
**(4) (10:40,41) YESU: ALIFUFULIWA NA BABA NA KUONEKANA BAYANA**

**10:39-41)**
1. Petro alirejea ukweli kwamba mitume walikuwa mashahidi wenye kuona mambo ambayo Yesu aliyafanya bayana kati ya Wayahudi (linga. 1:8; 3:15; 4:33).

2. Walakini, mbali na ukweli wa Baba kumkubali Mwanawe, Wayahudi walimwua Yesu kwa njia ya ukatili na laana kwa kumtundika mtini (kumsulibisha).
3. Bali Baba alihifadhi hukumu hiyo ya kifo kisicho cha haki kwa kumfufua toka kwa wafu siku ya tatu.
4. Siyo tu hivyo, lakini baada ya ufufuo, alimwonyesha Yesu bayana mbele ya mashahidi, ikiwa ni pamoja na mitume waliokula na kunywa pamoja naye baada ya ufufuo wake.
5. Kwa hiyo, hapakuwa na udanganyifu wa kufufuka kwake kwenye utukufu kutoka kwa wafu!

**(5) (10:42) YESU: ALIYEHUKUMIWA NA WOTE**
**(6) (10:43) YESU: ALIYETABIRIWA NA MANABII – MSAMAHA KWA NJIA YAKE**

**10:42,43)**

1. Baada ya ufufuo wake aliwaamuru mitume wake kuhubiri injili, ikiwa ni pamoja na ukweli kwamba angekuwa mhukumu wa wanadamu wote (linga. 17:30,31; 2 Kor.5:10).
2. Si mitume tu waliomshuhudia Yesu.
3. Manabii wa Mungu wa kipindi cha Agano la Kale pia walitabiri kuja kwake Yesu na msamaha wa dhambi ambao angewezesha.
4. Kufupisha ujumbe wa Petro kwa Kornelio, tafadhali zingatia pointi zifuatazo:
   a. Mst.34, 35 Mungu hana upendeleo – anawakubali wote wanaomcha na kutenda haki.
   b. Mst.36,37 Amani kwa njia ya Yesu, ambaye ni Bwana wa wote.
   c. Mst.38 Yesu: Alidhihirishwa na Baba kwa njia ya miujiza.
   d. Mst.39 Yesu: Alisulibiwa na Wayahudi.
   e. Mst.40,41 Yesu: Baba alifufua kumwonyesha wazi wazi.
   f. Mst.42 Yesu: Hakimu wa watu wote.
   g. Mst.43 Yesu: Alitabiriwa na manabii kama atayeleta msamaha wa dhambi.

**g.(10:44-46) ROHO MTAKATIFU ALISHUKA JUU YA KORNELIO NA WALIOMO NYUMBANI MWAKE**

1. Katika mst.44 Roho Mtakatifu aliwashukia Kornelio na watu wa nyumbani mwake.
   a. Tafadhali angalia katika mstari huu Luka alisema Roho Mtakatifu alishuka “Petro alipokuwa akisema.”
   b. Katika 11:15 Luka alibainisha zaidi na hapo alimnukuu Petro akisema, “Ikawa nilipoanza kunene, Roho Mtakatifu akawashukia…”
   c. Roho Mtakatifu alishuka juu ya Kornelio mwanzoni kabisa wakati Petro alipoanza kutoa maneno Kornelio pamoja na watu wa nyumbani mwake.
   d. Tafadhali kumbuka, imani huundwa ndani ya moyo wa mtu mwaminifu anaposikia ushuhuda unavyobainishwa kwa neno la Mungu (Rum.10:17; Ebr.11:1).
   e. Kwa kuwa Roho Mtakatifu alishuka juu ya Kornelio na watu wa nyumbani mwake kabla ya Petro hajaanza kunena nao kuhusu Yesu, basi Kornelio hakumwamini Yesu wakati huo.
   f. Kwa hiyo, Roho Mtakatifu alishuka juu ya Kornelio na watu wa nyumbani mwake kabla hawajamwamini Yesu.
   g. Hivyo, wanaodai kuwa Kornelia na watu wa nyumbani mwake waliokolewa wakati Roho Mtakatifu wangeokolewa kabla ya kumwamini Yesu!
   h. Hakika, hakuna anayekubali hilo kuwa ni kweli!
   i. Tutakapofika mst.47, 48 tutaona njia nyingine Kornelio na watu wa nyumbani mwake hawakuokoka kwa kumwagiwa Roho Mtakatifu.
2. Katika mst.45 Wakristo wa asili ya Kiyahudi walioungana pamoja na Petro kustaajabu.
   a. Walistaajabu kwa kuwa Roho Mtakatifu alishuka juu ya “Mataifa pia.”

b. Ndiyo kusema, Roho Mtakatifu alishuka juu ya Kornelio na watu wa nyumbani mwake waliokuwa Mataifa, kama vile alivyoshuka juu ya Petro na mitume wengine walikuwa wa asili ya Kiyahudi.
c. Walistaajabu kwa kuwa hawakutarajia baraka kama hiyo kupokea watu wa Mataifa.
d. Pia tafadhali angalia Luka alivyomtaja Roho Mtakatifu akishuka juu ya Kornelio na watu wa nyumbani mwake kama kupokea "kipawa cha Roho Mtakatifu."
e. Itakuwa muhimu kukumbuka ukweli huu tunapojifunza mst.47.

3. Katika mst.46 tunajifunza ndugu walitambua kuwa Kornelio na watu wa nyumbani mwake walipokea Roho Mtakatifu kwa njia ambayo aliwawezesha kutenda miujiza.
   a. Ndugu walitambua kwa sababu Kornelio na watu wa nyumbani mwake walinena katika lugha ya kigeni ambayo hawakuwahi kujifunza hapo kabla ("tongues").

### h. (10:47,48) PETRO ANAAMURU UBATIZO WA MAJI

1. Petro aliwauliza wale waliokuwa pamoja naye ikiwa palikuwa na mtu mwenye kuzuia ubatizo wa maji kwa Kornelio na watu wa nyumbani mwake.
   a. Zaidi ya yote, Petro aliunganisha mambo mawili ya kweli.
      (1) Ukweli wa kwanza ni, Kornelio na watu wa nyumbani mwake walipokea Roho Mtakatifu kama alivyopokea Petro na mitume wengine.
      (2) Ukweli wa pili ni, Kornelio na watu wa nyumbani mwake walipaswa kuonwa kama wenye kustahili ubatizo wa maji.
   b. Lakini kulikuwa na uhusiano gani baina ya ukweli huu aina mbili?
   c. Kujibu swali hili tafadhali fikiria ulinganifu wa matukio katika sura hii.
      (1) Kornelio na watu wa nyumbani mwake walikuwa Mataifa (10:45; 11:1-4).
      (2) Injili hakuhubiriwa katika Mataifa hata kufikia wakati huu.
      (3) Hilo lilikuwa ni kwa sababu walikuwa wenye asili ya Kiyahudi walifikiri ni dhambi kwa Myahudi kwenda kwa watu wa mataifa mengine (10:28).
      (4) Waliwadhania watu wa mataifa mengine, k.m. Mataifa, kuwa wachafu, najisi, au wasio safi, na hivyo basi wasiostahili kupokea ujumbe wenye wokovu wa Mungu.
      (5) Kuondoa fikra hizi akilini mwa Petro, Mungu alimfunulia maono na kumweleza kuwa asimwite mtu yeyote kuwa mchafu na najisi (10:28,34,35).
      (6) Na ili kuondoa fikra hizo potofu ndani ya hao waliokuwa wakisikilza siku hiyo, na kwa vizazi vyote, Mungu alimmwaga Roho Mtakatifu juu ya Mataifa, kama alivyofanya juu ya Petro na mitume wengine siku ya Pentekoste.
      (7) Kumwagwa huku kwa Roho Mtakatifu kulifanya kwa namna hii ya kipekee kwa mara moja tu Mungu kuonyesha kuwa aliwakubali watu wa Mataifa kupokea ujumbe wa wokovu.
      (8) Ndiyo sababu Petro alirejea kumwagwa huku kwa Roho Mtakatifu alipouliza iwapo palikuwa na yeyote mwenye kuzuia Kornelio na watu wa nyumbani mwake wasibatizwe majini.
      (9) Alitambua kuwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya Mataifa ilikuwa isahara ya Mungu kwa watu wote kwamba Mataifa walistahili kupokea ujumbe wake wa wokovu, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi.
      (10) Na alitambua kwamba hao wasikilizaji wenye asili ya Kiyahudi siku hiyo wangeunganisha hilo, ama kuhatimisha namna hiyo, alipouliza swali hilo.
   d. Lakini, maelezo hayo ni maelezo yangu tu, au hayo ni ya mtu mwingine?
      (1) Kwa bahati nzuri, jibu ni hapana – haya si maelezo ya mtu fulani tu!
      (2) Ni jibu la Mungu, lililotolewa na mtume Petro aliyevuviwa katika 11:17,18!
   e. Kuzingatia swali la Petro, walikuwa wanasikiliza siku hiyo walisadiki kwamba Kornelio na nyumba yake walipaswa kukubaliwa kubatizwa majini.
2. Tena, katika mst.48 Petro alimwamuru Kornelio na watu wa nyumbani mwake kubatizwa majini katika jina la Bwana, k.m., kwa mamlaka ya Bwana.

3. Lakini kwa nini Petro aliwaamuru kuwabatiza majini?
4. Jibu la swali hili linaweza kupatikana kwa kukumbuka kwa nini Petro alitumwa kwa Kornelio hapo awali.
5. Tafadhali kumbuka kwamba Petro walitumwa kwa Kornelio kufanya yafuatayo:
   a. 10:6 Kumweleza mambo gani alipaswa kufanya!
   b. 10:22 Kunena maneno mbele yake.
   c. 10:32,33 Kumweleza "maneno yote uliyoamuriwa na Mungu"!
   d. 11:14 Kumweleza "maneno ambayo yatakuokoa wewe na nyumba yao yote."
6. Ukijumuisha mambo haya yote pamoja tunahatimisha kwamba Petro alitumwa kwa Kornelio kumweleza yampasayo kutenda ili kuokoka, k.m. alichoamuru Mungu kufanya ili kuoko toka dhambini.
7. Lakini ni kitu gani Petro alimwamuru Kornelio na nyumba yake wafanye?
8. Aliamuru wabatizwe katika maji!
9. Hivyo basi, ni muhimu Kornelio na nyumba yake kubatizwa majini kwa kusudi la kuokoka toka katika dhambi zao!
10. Hivyo ni kweli, hawakuokoka kabla ya kubatizwa majini.
11. Hili kweli kabisa hata ingawa Roho Mtakatifu aliwashukia juu yao kabla ya kubatizwa majini, hawakuokoka bado.
    a. Kwa hiyo, ni dhahiri Roho Mtakatifu hakuwashukia ili kuwaokoa toka dhambini.
       (1) Kinyume chake Mungu alikuwa na kusudi lingine katika kuwamwagia Roho Mtakatifu juu yao.
       (2) Badala ya kufanya hivyo kuwaokoa kutoka katika dhambi zao, Mungu alifanya kumwonyesha Petro na wanadamu wote kuwa Mataifa wanastahili kupokea ujumbe wa wokovu.
       (3) Basi, baada ya Roho Mtakatifu kumwagwa juu ya Kornelio na nyumba yake, walisikia na kutii ujumbe wa wokovu.
       (4) Na ujumbe wa wokovu unajumuisha amri ya kuzamishwa maijini ili kupata wokovu toka katika dhambi zao.
    b. Basi, madai ya baadhi ya vikundi vya dini kusema kwamba Kornelio waliokolewa kwa kumwagiwa Roho Mtakatifu inadhihirika kwa ni uongo kabisa!
12. Tunapojifunza mazingira haya, sehemu yote iliyobaki ya Matendo, na sehemu yote iliyobaki ya Agano Jipya, ni dhahiri kwamba kitu kimoja kikubwa kuhusu swala la Kornelio lilikuwan la kipekee na halikurudiwa tena.
    a. Tumeona kwamba Roho Mtakatifu alimwagwa juu ya Kornelio na watu wa nyumbani mwake.
    b. Na jambo hili lilitendeka kabla hawajasikia na kutii ujumbe wa wokovu.
    c. Walakini, Mungu alikuwa na malengo maalum katika kumwaga Roho Mtakatifu juu ya Mmataifa huyu na nyumba yake kabla ya kuokolewa.
    d. Kusudi hilo ilikuwa kuwaonyesha watu wote kwamba Mataifa walipaswa kupokea ujumbe wa wokovu, kama ilivyokuwa kwa Waisraeli.
    e. Mungu alipokamilisha kusudi hilo hakurudia tena kutenda tukio hili.
    f. Basi, kuanzia wakati huo hadi kufikia sasa, Mungu hamwagi Roho wake juu ya watu kudhihirisha kuwa wanastahili kupokea wokovu.
    g. Mara Petro, na mitume wengine, na Wakristo wengine walipoelewa injili kuwa ni kwa ajili ya watu wote, hapakuwa na umuhimu wa kwa Mungu kuonyesha kibali chake kwa kundi la watu kama alivyofanya katika swala la Kornelio.
    h. Wakati huo walielewa, basi tunapaswa kuelewa kwamba ni fursa yetu na majukumu kuhubiri na kufundisha injili kwa mataifa yote na kwa kila kiumbe chini ya mbingu (Mt.28:18-20; Mk.16:15,16)!
13. Pia, tafadhali angalia ukweli ufuatao ambao Luka aliuandika kwa uvuvio kuhusu kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika sehemu hii.
    a. Mst.44 Roho Mtakatifu alishuka juu ya hao waliosikia neno la Mungu.

b. Mst.45 Luka alirejea kupokea Roho kwa Mataifa hawa kama kupokea “kipawa cha Roho Mtakatifu.”
c. Mst.47 Petro alitaja kumwagwa huku kwa Roho Mtakatifu kama Mataifa kupokea “Roho Mtakatifu”
d. Kutokana na ukweli huu, tunahatimisha kuwa “kipawa cha Roho Mtakatifu” katika mazingira haya ilikuwa Roho Mtakatifu kama zawadi.
e. Hivyo basi, Roho Mtakatifu aliposhuka juu ya Kornelio na nyumba yake, walipokea kipawa cha Roho Mtakatifu, k.m., Roho Mtakatifu kama zawadi toka kwa Mungu.
f. Maelezo ya nyongeza kuhusu somo hili yanapatikana katika notisi za 2:38 na masomo maalum yanayolingana.

14. Ni muhimu pia kuelezea kabla ya kuondoka mistari hii kwamba Petro hakuweka mikono yake juu ya Kornelio na nyumba yake ili kuwapatia uwezo wa kimiujiza.
    a. Basi, kilichotokea kwa Kornelio na nyumba yake ni tofauti na yaliyotokea sura 8.
    b. Hilo ni kweli kwa sababu katika sura hiyo, Petro na Yohana waliweka mikono yao juu ya Wakristo Wasamaria kuwawezesha kutenda miujiza.
    c. Hivyo basi, kwa kuwa Kornelio na nyumba yake hawakupokea uwezo wa kimiujiza kwa kuwekewa mikono na mitume, huo lazima basi ulikuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu walioupata.
    d. Ilitendwa kutoka mbinguni na Bwana Yesu Kristo mwenyewe, ambaye ni yeye pekee aliyehudumu kubatiza kwa Roho Mtakatifu (Mt.3:11).
    e. Ukweli ni kwamba Petro, kwa uvuvio wa Mungu, aliutaja huu kuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu katika 11:15-17.
    f. Kama tutakavyojifunza zaidi katika mazingira hayo, hii ilikuwa mara ya pili pekee ubatizo wa Roho Mtakatifu ukitukia, na ilikuwa mara ya mwisho!
15. Tena, tafadhali kumbuka somo letu katika 2:16ff, tulibainisha kuwa Mungu aliahidi kumwaga Roho yake juu ya “watu wote.”
    a. Tulijifunza “watu wote” yenye maana aina zote za watu wa Mungu.
    b. Hakika, miongoni mwa watu hao wa Mungu ni Wayahudi na Mataifa.
    c. Kama tulivyoona katika sura 2 Mungu alimwaga Roho wake juu ya mitume, wenye asili ya Kiyahudi.
    d. Sasa, katika sura 10, tunaona Mungu akimwaga Roho yake juu ya Kornelio na nyumba yake, ambao walikuwa Mataifa.
    e. Basi, Mungu bila shaka, alikuwa akitimiza unabii wake ulioandikwa katika Yoeli, sura 2!
    f. Na mwishoni mwa karne ya kwanza alitimiza kikamilifu unabii huu na kusababisha karama za miujiza kukoma, kubatilika, na kutoweka!
16. Mwisho, kabla ya kuondoka katika fungu hili la maandiko, tunapenda kutilia mkazo jambo moja muhimu sana kwa mara nyingine.
    a. Hakuna shaka kwamba Kornelio na watu wa nyumbani mwake walibatizwa kwa Roho Mtakatifu.
    b. Walakini, hata ingawa walibatizwa kwa Roho Mtakatifu, hawakuokolewa bado toka katika dhambi zao!
    c. Ni kweli hilo kwa sababu walimwitaji Petro awaeleze maneno ambayo yangewaokoa.
    d. Petro alinena maneno hayo ya wokovu baada ya Kornelio na nyumba yake kubatizwa kwa Roho Mtakatifu.
    e. Na Petro aliponena maneno hayo ya wokovu, aliamuru wabatizwe ubatizo mwingine, na wala si ubatizo wa Roho Mtakatifu.
    f. Ili Kornelio na nyumba yake waokoke kutoka katika dhambi zao, Petro akaamuru wabatizwe majini!
    g. Kama tulivyoona, ni kweli jambo hilo kwa sababu ubatizo majini ili kupata msamaha wa dhambi ni ubatizo mmoja ambao Yesu ameamuru wafuasi wake watende hadi mwisho wa wakati kama tujuavyo!
17. Mtazamo kwa ufupi wa sura 10.

a. 10:1-8 Iliongozwa na malaika, Kornelio alituma watu kumwita Petro.
b. 10:9 –16 Petro aliona maono.
c. 10:17-22 Wajumbe kutoka kwa Kornelio walimwita Petro.
d. 10:23-29 Petro na Kornelio wakutana.
e. 10:30-33 Kornelia aeleza sababu ya kumwita Petro.
f. 10:34-43 Ujumbe wa Petro kwa Kornelio na nyumba yake.
g. 10:47,48 Petro aliamuru wabatizwe majini.

**i. (11:1-3) BAADHI YERUSALEM WAKASHINDANA NA PETRO KWA SABABU ALIINGIA KWA MATAIFA**

1. Petro aliporejea Yerusalem, wenye asili ya Kiyahudi ("wale wa tohara") wakashindana naye.
2. Walipingana naye kwa sababu alikwenda nyumbani kwa Kornelio kwa watu wa Mataifa ("wasiotahiriwa").

**j. (11:4-17) MAELEZO YA PETRO**
**(1) (11:4-10) MAONO**
**(2) (11:11,12) WAJUMBE KUTOKA KWA KORNELIO**
**(3) (11:13,14) KORNELIO AELEZA SABABU YA KUMWITA PETRO**
**(4) (11:15-17) KUSHUKA KWA ROHO MTAKATIFU NA MAANA YAKE**

**11:4-17)**
1. Petro alianza kuelezea sababu ya kwenda kwa Kornelio na nyumba yake akiwa na ujumbe wenye wokovu.
2. Zingatia haswa katika sura hii kwamba Petro alieleza kilichotendeka "alianza kwa taratibu."
3. Kwa maneno mengine, Petro alikuwa atoe maelezo maalum kulingana na matukio, akianza na jambo lililotokea kwanza.
4. Kwa kuwa mambo aliyosema Petro katika maelezo ni marudio ya somo letu lililopita katika sura 10, tutatoa muhtasari wa maelezo yake kwa sehemu ya maandiko isipokuwa kama kuna jambo jipya la msingi litakalopatikana katika sehemu maalum.
5. Katika mst.5-10 Petro alibainisha maono ambayo Mungu alimwezesha kuona.
6. Katika mst.11,12 Petro alisimulia jinsi Kornelio alivyotuma wajumbe kwa Petro kumwomba aje kwa Kornelio.
7. Katika mst.13,14 Petro alieleza jinsi Kornelio alivyoeleza kusudi la kumwita Petro kwake.
8. Katika mst.15-17 Petro alitoa sehemu muhimu ya maelezo yake. Tunapenda kujifunza sehemu hiyo kwa maelezo zaidi.
   a. Tafadhali angalia katika mst.15 kwamba Petro alisema kwamba Roho Mtakatifu alishuka juu ya Mataifa mara Petro alipoanza kunena!
      (1) Basi, kama tulivyoona mapema, Roho Mtakatifu alishuka juu ya Kornelio na nyumba yake kabla ya kupata hata fursa ya kuikuza imani yake katika Kristo juu ya msingi wa ushuhuda wa neno la Mungu.
      (2) Tafadhali angalia notisi zetu katika 10:44-46 kwa maelezo zaidi juu ya somo hili muhimu la kweli.
   b. Lakini kuna jambo lingine muhimu sana lenye kufunua ukweli katika mst.15 na 16!
      (1) Ukweli ni kwamba, Petro alisema Roho Mtakatifu alishuka juu ya Kornelio na nyumba yake, "kama alivyotushukia sisi mwanzo."
      (2) Na alipoona hilo Petro akakumbuka maneno ya ahadi ya Yesu kwamba mitume wangebatizwa kwa Roho Mtakatifu (liga.Mt.3:11).

(3) Dhahiri Petro alikuwa akisema kwamba Kornelio na watu wa nyumbani mwake walibatizwa katika Roho Mtakatifu kama vile walivyobatizwa Petro na mitume wengine hapo mwanzo wa kanisa la Bwana, kama ilivyoandikwa katika sura 2.
(4) Lakini ulikuwa ulipita muda tangu mitume wabatizwe katika Roho Mtakatifu.
(5) Kama ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa ukitukia mara kwa mara kama baadhi ya watu wanavyodai siku hizi, kwa nini basi Petro alilazimika kurejea nyuma kabisa katika mwanzo wa kanisa kulinganisha na tukio la Kornelio?
(6) Jibu ni dhahiri! Ubatizo wa Roho Mtakatifu haukutokea mara kwa mara!
(7) Ndiyo sababu Petro alirejea nyuma kabisa katika siku ya Pentekoste ya sura ya pili kulinganisha na tukio lingine la ubatizo wa Roho Mtakatifu.
(8) Ni dhahiri basi, kulikuwa na matukio aina mbili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu yaliyoandikwa katika Agano Jipya kufikia wakati huu.
(9) Matukio hayo ni mitume katika sura ya pili na Kornelio na nyumba yake katika sura ya kumi.
(10) Na katika kila tukio mojawapo, Mungu alikuwa na kusudi maalum kwa ajili ya kuruhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu.
  (a) Katika tukio la mitume, ilikuwa ni kuwatia nguvu ili kuwawezesha kufunua na kuthibitisha neno la Mungu pasipo makosa (Yoh.14-16).
  (b) Katika tukio la Kornelio na nyumba yake, ilikuwa ni kuonyesha ulimwengu kukubaliwa kwa Mataifa kupokea ujumbe wa Mungu wenye wokovu (linga. mst.17,18).
(11) Kadhalika, tunaweza kuchunguza Agano Jipya kutoka mwanzo hadi mwisho hata tusiweze kupata mfano mwingine wowote wa ubatizo wa Roho Mtakatifu.
(12) Jambo hili linalingana kabisa na ukweli tuliouona katika somo letu la Matendo.
  (a) Ukweli ni kwamba ubatizo mmoja ambao Yesu ameamuru kwa wafuasi wake hadi mwisho wa dunia ni wa maji ili kupata msamaha wa dhambi!
  (b) Ubatizo huo mmoja si ubatizo wa Roho Mtakatifu!
  (c) Hakika, ubatizo wa Roho Mtakatifu uliondolewa na Mungu mwenyezi wakati alipofunua Efe.4:5 karne ya kwanza!

c. Katika mst.17 Petro aliwauliza ndugu wenye asili ya Kiyahudi angempingaje Mungu, kwa kuwa Mungu amemwagia Roho Mtakatifu juu ya Kornelio na nyumba yake kama alivyofanya juu ya mitume.
  (1) Kwa maneno mengine, Petro alisema kuwa Mungu alikuwa na makusudi maalum kwa kuruhusu Kornelio na nyumba yake kubatizwa katika Roho Mtakatifu.
  (2) Na kusudi hilo maalum ilikuwa kumshawishi Petro na wengine kwamba Mungu alitaka Mataifa kupokea ujumbe wenye wokovu.
  (3) Kumbuka, hao watu wa Yerusalem walimshutumu Petro kwa kufanya makosa ya kumtembelea Kornelio na nyumba yake kwa sababu walikuwa Mataifa (mst.1-3).
  (4) Kwa kuonyesha ushahidi kama alivyofanya katika sura hii, Petro alibainisha dhahiri kwamba kitendo cha kwenda kwa Kornelio kilikuwa sahihi!
  (5) Kilikuwa sahihi kwa sababu Mungu aliongoza matendo ya Petro na kwa sababu alimmwaga Roho Mtakatifu juu ya Mataifa kama alivyofanya kwa mitume.
  (6) Hivyo basi, Petro asingeliweza kutokwenda kwa Kornelio pasipo kumpinga Mungu mwenyezi (kutomtii, kushindana naye)!
  (7) Ndiyo sababu Petro aliwauliza wasikilizaji wake jinsi gani angeliweza kumpinga Mungu mbele ya wasikilizaji wake.
  (8) Alitambua kuwa wasikilizaji wake walikuwa na mioyo minyofu na waaminifu wangekubaliana na kila alichosema Petro kuwa ni sahihi kwa kuhubiri injili kwa Mataifa!

**k. (11:18) MAJIBU YA WALIOSHINDA NAYE**

1. Katika mstari huu tunaona Petro alifanikiwa katika kuwashawishi wasikilizaji wake kwamba alichofanya kilikuwa sahihi kwa sababu yalikuwa mapenzi ya Mungu!
2. Tafadhali angalia majibu ya wasikilizaji kutokana na ushuhuda na swali lake:
   a. "wakanyamaza" – walitambua kuwa wasingeliweza kupinga jambo alilofanya Petro lilikuwa sahihi.
   b. "wakamtukuza Mungu."
      (1) Walifanya hivyo kwa kuwa walitambua maana ya jambo lililotokea.
      (2) Walitambua kuwa tukio hilo la pekee, Mungu alilionyesha kwa wanadamu wote alitaka Mataifa kupokea ujumbe wa wokovu, ukijumuisha "toba liletalo uzima".
      (3) Na, kama tulivyoona, ukijumuisha katika ujumbe huo wa injili unahitajika kwa kila mwanadamu kutubu dhambi za nyuma (2:38; 3:19).
      (4) Na toba hiyo ni (to life) k.m., "inaleta uzima."
         (a) Hilo ni kweli kwa sababu toba ya kibiblia huongoza kuzamishwa majini ili kupata msamaha wa dhambi (2:38; 3:19).
         (b) Na kuzamishwa huko majini kunamfanya mtu afufuke toka majini ili kwenenda katika upya wa uzima kwa sababu wamekuwa viumbe vipya, wamezaliwa upyua kwa njia ya utiifu wao kwa neno la Mungu (Rum.6:3,4; 2 Kor.5:17; 1 Pet.1:22, 23).
         (c) Na mtu akibakia mwaminifu hat kufa, watapata uzima wa milele (Ufu.2:10).
3. Kwa hatari ya kurudia-rudia, ni lazima nikazie mkazo jambo moja muhimu sana kwa mara nyingine tena kabla ya kuondoka mst.15-18.
   a. Jambo hilo ni, kwamba ni dhahiri kabisa kwamba Mungu alikuwa na kusudi maalum katika kumruhusu Kornelio na nyumba yake wabatizwe katika Roho Mtakatifu.
   b. Na kusudi hili ilikuwa kuonyesha nia yake kwa Mataifa kupokea ujumbe wa wokovu.
      (1) Petro alitambua kusudi hili maalum (10:28).
      (2) Wote waliokuwa na Petro walitambua kusudi hilo maalum (10:45-48).
      (3) Walioshindana na Petro Yerusalem walilitambua (11:15-18).
      (4) Nasi leo tunapaswa kulitambua kusudi hilo!
   c. Kumbuka ilikuwa muhimu kwa Mungu kuonyesha nia yake kwa namna ya maajabu hii, wala isirudiwe tena, kwa sababu mitume na watu wengine walishindwa kuipeleka injili kwa Mataifa.
   d. Mungu alipotekeleza kusudi lake kwa kuonyesha kuwa Mataifa wanapokea injili, Mungu hakurudia tena ubatizo wa Roho Mtakatifu!
   e. Kadhalika, kama tulivyoona, Mungu alichagua kutokurudia tena ubatizo wa Roho Mtakatifu tena, kwa kuwa si ubatizo mmoja aliouamuru!

### f. (11:19-21) KAZI YAO WALIOTAWANYIKA KATIKA ANTIOKIA

1. Waliotawanyika kutoka Yerusalem mara baada ya kifo cha Stefano walisafiri kwenda Foinike, Kipro, na Antiokia.
   a. Kumbuka ilibainishwa kuwa watu hawa walikwenda kotekote wakihubiri neno la Mungu (8:4).
   b. Katika mst.19 tunaelezwa kuwa walihubiri neno kwa Wayahudi tu.
2. Walakini, katika mst.20 tunajifunza kuwa baadhi ya watu hao wakafika Antiokia na wakamhubiri Bwana Yesu kwa Wayunani (ASV), (k.m., kwa Mataifa).
3. Bwana akaibariki kazi ya watu hawa.
4. Kwa nyongeza, watu wengi wakaamini injili na kumgeukia Bwana.
5. Kama tulivyoona katika somo mapema, kumgeukia Bwana huku baada ya kuamini kunajumuisha toba na kumtii Bwana, ikiwa ni pamoja na kuzamishwa majini kwa ajili ya ondoleo la dhambi (2:38; 3:19).

### m. (11:22-24) YERUSALEM YAMTUMA BARNABA ANTIOKIA

1. Barnaba alipofika Antiokia alifurahishwa na mambo aliyoyakuta miongoni mwa Wakristo hao wapya.
2. Zaidi sana, aliwahamasisha kudumu mioyoni mwao kuzidi kumtumikia Bwana, k.m., kubakia waaminifu kwake bila kujali chochote kitakachotokea.
3. Angali picha nzuri aliyotajwa juu ya Barnaba katika mst.24:
   a. "alikuwa mtu mwema."
      (1) Ni sifa za ajabu!
      (2) Nid dhahiri Barnaba alikuwa kama Yesu katika hili alikuwa akitena mema (10:38)!
   b. "mwenye kujaa Roho Mtakatifu".
      (1) Tafadhali angalia notisi zetu katika 6:2-4 kwa maelezo zaidi ya maana ya maneno haya.
      (2) Katika somo letu katika mistari hiyo tulijifunza maneno haya kuwa mara nyingi yalimaanisha Mkristo aliyemruhusu Roho Mtakatifu kutia ushawishi mkubwa juu yake kwa njia ya upanga wa Roho, neno la Mungu.
   c. "mwenye kujaa imani".
      (1) Barnaba alikuwa na imani kubwa katika Bwana!
4. Ikiwa ni matokeo ya kuhubiri, kufundisha, na maisha ya watu kama Barnaba kanisa likazidi kukua ("idadi kubwa ya watu walizidi kuongezeka katika Bwana").
5. Kwa bahati nzuri, ni dhahiri kwamba wote "waliozidishwa kwa Bwana" walifanya mambo yaliyofanana ili kuongezwa kama vile katika sura 2 waliokolewa na ambao Bwana "aliwazidisha katika kanisa". Hakika walifanya mambo yafuatayo:
   a. Walisikia injili na kupokea kwa furaha ujumbe wa wokovu (2:14-36, 41).
   b. Waliamini injili na kujutia dhambi zao (2:37).
   c. Walitubu dhambi zao na kuzamishwa majini ili kupata msamaha wa dhambi zao (2:38).

### n. (11:25,26) BARNABA AMLETA SAULI KUTOKA TARSO KWENDA ANTIOKIA

1. Angalia kipindi cha mwaka mzima ambacho Sauli na Barnaba walikuwa Antiokia, walikusanyika pamoja na kanisa.
   a. Walipenda kukusanyika pamoja na Wakristo wengine kuabudu na kutumia muda wao pamoja!
2. Wala si hivyo tu, walifundisha injili pia kwa watu wengi. Walikuwa na moyo wa uinjilisti!
3. Katika mst.26 tunaona njia mbili ambazo wafuasi wa Bwana walitajwa zamani hizo ambapo tunapaswa hata sisi kutajwa.
   a. Kwanza, walitajwa kuwa "wanafunzi".
      (1) Mfuasi (disciple) ni mwanafunzi (learner), (pupil), mfuasi wa mtu mwingine.
      (2) Wala si tu mwanafunzi anajifunza kuhusu mtu mwingine, bali pia anajitahidi kuiga na kumtii huyo mtu mwingine.
      (3) Hakika basi wafuasi wa Yesu ni hao wanaojibidiisha kujifunza mafundisho na maisha yake wenye juhudi katika kuiga na kumtii yeye!
   b. Pili, wafuasi hawa katika Antiokia ndio wa kwanza kutiwa "Wakristo".
      (1) Kusema ukweli jina hilo zuri linaonyesha anayeamini na kumfuata Bwana Yesu Kristo.
      (2) Ni dhahiri kutokana na maandiko kwamba jina hili maalum na la kipekee lilitolewa na Mungu.
         a. Linga. Isa.62:2.
4. Pia, angalia kwamba Wakristo hawa wa kwanza hawakuwa na jina lingine mbele au lililokuja baada ya Mkristo.
   a. Yaani, hawakuwa Wakristo wa madhehebu "X" au "Y"!
   b. Walikuwa wakristo tu!
   c. Ndivyo anavyotutaka Bwana kila mmoja wetu tuwe!

**o. (11:27-30) NJAA ILITABIRIWA / ANTIOKIA WALITUMA MSAADA YERUSALEM KWA MKONO WA BARNABA NA SAULI**

1. Agabo kutoka Yerusalem alifika Antiokia na kutabiri njaa kubwa.
2. Wakristo wa Antiokia waliposikia kuhusu njaa kubwa waliamua kutuma msaada kwa ndugu wa Uyahudi.
    a. Tafadhali angalia kila mtu aliyetuma msaada "kila mtu kwa kadiri alivyofanikiwa."
    b. Kama tulivyoona katika sura 2, hili linabainisha kuwa kila Mkristo alikuwa na uwezo na sasa pia anao uwezo wa kumiliki mali yake binafsi!
    c. Hakika, baadhi walikuwa na mali yao binafsi hata kuwawezesha kutuma misaada na wengine hakuwa na uwezo huo.
    d. Kwa vyovyote vile, hii ni namna nyingine ya upendo kumiminika toka kwa kundi moja la Wakristo kwenda kwa kundi lingine katika kanisa la karne ya kwanza.
    e. Ni jambo wazi pia kukumbuka kwamba hao waliotuma misaada walikuwa asilia ni Mataifa (hao wa Antiokia), wakati waliopokea walikuwa asilia ni Wayahudi (hao wa Uyahudi).
    f. Basi, upendo wa Wakristo huvuka vizuizi, kama vile utaifa asilia, kabila, lugha, rangi ya ngozi, n.k.!
3. Hao wa Antiokia waliowatuma Sauli na Barnaba kupeleka msaada kwa wazee wa Yerusalem.
4. Kwa nasibu, hii ni mara ya kwanza ofisi ya wazee kutajwa katika kitabu cha Matendo.
5. Tutakuwa na maelezo zaidi kuhusu somo hili tutakapofika sura 14.
6. Mtazamo kwa ufupi wa 10:1-11:30, Mlango kufunguka kwa Mataifa.
    a. 10:1-8 Maongozi ya malaika, Kornelio atuma watu kumwita Petro.
    b. 10:9-16 Petro aliona maono.
    c. 10:17-22 Wajumbe kutoka kwa Kornelio wanamwita Petro.
    d. 10:23-29 Petro na Kornelio wakutana.
    e. 10:30-33 Kornelio alieleza sababu ya kumwita Petro.
    f. 10:34-43 Ujumbe wa Petro kwa Kornelio na nyumba yake.
    g. 10:44-46 Roho Mtakatifu ashuka juu ya Kornelio na nyumba yake.
    h. 10:47,48 Petro aliamuru ubatizo wa maji.
    i. 11:1-3 Baadhi Yerusalem walishindana na Petro kwa sababu alikwenda kwa Mataifa.
    j. 11:4-17 Maelezo ya Petro.
    k. 11:18 Majibu ya hao walioshindana naye.
    l. 11:19-21 Kazi ya watu waliotawanyika (8:4) Antiokia.
    m. 11:22-24 Yerusalem yamtuma Barnaba Antiokia.
    n. 11:25,26 Barnaba alimleta Sauli kutoka Tarso kwenda Antiokia.
    o. 11:27-30 Njaa yatabiriwa / Antiokia watuma msaada Yerusalem kwa mkono wa Barnaba na Paulo.
7. Mtazamo kwa ufupi wa 12:1-25, Mateso kutoka serikali ya ndani.
    a. Mst.1,2 Herode amwua Yakobo.
    b. Mst.3-5 Herode amtia gerezani Petro / kanisa likadumu kumwombea Petro.
    c. Mst.6-11 Mungu kimiujiza alimtoa Petro kutoka gerezani.
    d. Mst.12-17 Petro awasili nyumbani kwa Mariam ambamo walikuwa wakiomba.
    e. Mst.18,19 Kuondoka gerezani kwa Petro kwajulikana.
    f. Mst.20-23 Herode alishindwa kumpa utukufu Mungu na akafa.
    g. Mst.24,25 Neno lilienea zaidi / Sauli na Barnaba walirejea Antiokia.

**2. (12) MATESO KUTOKA SERIKALI YA NDANI**

**a. (mst.1,2) HERODE AMWUA YAKOBO**

1. Mfalme Herode alilitesa kanisa, ikiwa ni pamoja na kumwua mtume Yakobo kwa upanga.
2. Hizi ni habari za kwanza kuandikwa juu ya kifo cha mtume.
3. Awali mateso ya Wakristo yalitoka haswa kwa watumishi wa dini ya Kiyahudi.
4. Kwa kifo cha Yakobo tunaona mwanzo wa mateso kutoka maofisa wa serikali ya ndani.

**b. (mst.3-5) HERODE AMTIA GEREZANI PETRO / KANISA LIKADUMU KUMWOMBEA PETRO**

1. Herode alipoona swala la kumwua Yakobo lingewapendeza Wayahudi, pia akamkamata Petro na kumtia gerezani.
2. Ni dhahiri kwamba alitaka pia kumwua Petro, lakini alichelewa kufanya uamuzi huo wake hata sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu na Pasaka.
3. Kwa nasibu, tafsiri ya kale ya “King James” imelitafsiri neno “Passover” katika mst. 4 kama “”Easter”.
   a. Hiyo ni bahati mbaya ya kutafsiri neno vibaya!
   b. Neno hili linapatikana mara 28 nyingine katika Agano la Jipya na limetafsiriwa kiusahihi kama Pasaka katika kila mahali!
   c. Basi, kuna ushahidi mwingi kwamba tafsiri kama ASV na NKJV ni sahihi zaidi katika mstari huu kwa kutafsiri neno kama “Pasaka” kuliko “Easter”!
4. Pia, katika tafsiri ya kale “KJV” na “ASV”, vinadai kuwa alipelekwa “akamtia mikononi mwa vikosi vinne vya askari wanne wanne”
   a. “quaternions” – kikosi cha askari wanne.
   b. Basi, Petro aliwekwa chini ya ulinzi wa askari wanne wanne, au idadi ya askari kumi na sita.
5. Katikati ya hali hii ngumu tumepewa picha nzuri juu ya Wakristo hawa wa awali katika mst.5.
   a. Kanisa nzima lilikusanyika daima kusali kwa Mungu kwa ajili ya ndugu yao mpendwa Petro!
      (1) Tafadhali tafakari juu ya hatari ambayo Petro, Wakristo hawa, na kanisa lilikabiliwa.
      (2) Yakobo alikuwa tayari ameuawa, na Petro alikuwa gerezani bila shaka akisubiri kuuawa.
      (3) Wangejaribu kufanya vurungu ili kumwokoa Petro aliyekuwa gerezani na kujilinda wao wenyewe.
      (4) Walakini, hawakufanya hivyo!
      (5) Kinyume chake, walimwendea Mungu mwenyezi katika sala!
   b. Kama tulivyoona tayari mara nyingi katika somo letu katika Matendo, watu hawa waliamini 1 Thes.5:17 na Yak.5:16!

**c. (mst.6-11) KWA MIUJIZA PETRO ATOLEWA GEREZANI**

**12:6-8)**

1. Kabla tu ya Herode kutekeleza mipango yake ya kumwua Petro, Bwana akatuma malaika kumwokoa.
   a. Hapa ni moja ya sehemu zinazotudhihirishia kwamba Mungu anajibu sala tunapokwenda sawasawa na masharti yake na kama ni sawa na mapenzi yake (1 Pet.3:11,12; 1 Yoh.3:22; 5:14!
2. Angalia katika mst.6 jinsi gani walivyomlinda Petro kikamilifu!
3. Walakini, malaika wa Bwana alimwondoa Petro na kumweleza atoke pamoja naye.

**12:9-11)**

1. Petro alimfuata malaika lakini hakujua kilichokuwa kikiendelea kama ni kitu halisi ama maono.

2. Katika mst.10 mlango wa nje ulifunguka wenyewe, Petro na malaika wakatoka huru!
3. Kadiri walivyozidi kwenda mitaani malaika wa Bwana akamwacha Petro.
4. Ndipo alipogundua jambo hilo lilikuwa kweli na kwamba Mungu alimwokoa kutoka katika mkono wa Herode na Wayahudi kwa njia ya malaika.

**d. (12:12-17) PETRO ALIKUJA NYUMBANI KWA MARIAM WALIPOKUWA WAKIOMBA**

1. Petro akafika nyumbani kwa Mariam, mamaye Yohana Marko.
   a. Tutamwona Yohana Marko tena katika sura hii.
   b. Hata hivyo, angalia kuna Wakristo wengi waliokusanyika pamoja katika nyumba ya Mariam na walikuwa wakimwomba Mungu!
2. Petro alipobisha mlangoni msichana aliyefungua malango alifurahi mno kumwona yeye na akaenda kwa mbio kuwaeleza wengine na kusahau kufungua mlango.
3. Katika mst.15 waliokuwemo ndani ya nyumba walishituka mno, walidhania kuwa msichana alikuwa hakika amekosea.
   a. Ukweli ni kwamba, walikuwa na uhakika kuwa Petro alishakufa na kwamba aliyemwona alikuwa malaika wa Petro!
4. Wakati huo huo Petro alizidi kugonga mlangoni hata wakafungua mlango.
5. Walipofungua mlango walistaajabu kumwona Petro hapo.
6. Kisha, katika mst.17 Petro aliwaeleza jinsi Bwana alivyomwokoa kutoka gerezani.
7. Pia aliwaeleza Wakristo kwenda kumweleza Yakobo na ndugu yaliyotendeka.
   a. Kwa kuwa Herode alimwua Yakobo mtume tayari, Yakobo aliyetajwa katika mstari huu alikuwa Yakobo mwingine.
   b. Inaonekana kuwa alikuwa Yakobo nduguye Bwana, aliyekuwa kiongozi katika kanisa la Yerusalem (linga. 15:13; Gal.1:19).
8. Baada ya kutoa maagizo hayo Petro alikwenda mahali pengine!

**e. (12:18,19) KUTOROKA KWA PETRO KWATAMBULIWA**

1. Asubuhi kulikuwa na vurugu kubwa askari walipogundua kuwa Petro alikuwa hayupo.
2. Herode aliposhindwa kumpata Petro, aliamuru walinzi kuuawa.
3. Baada ya jambo hilo Herode aliondoka Yudea akielekea Kaisaria.

**f. (12:20-23) HERODE ASHINDWA KUMPATIA MUNGU UTUKUFU NA AKAFA**

1. Kwa sababu isiyoeleweka Herode aliwachukia watu wa Tiro na Sidon, watu hao walimwendea Herode kumwomba amani.
2. Katika kuwajibu, Herode, alivaa nguo za fahari, za kifalme, akanena na watu wa Tiro na Sidon.
3. Watu wakasema kuwa Herode alikuwa mungu, na wala si mwanadamu.
4. Ni wazi Herode alitambua watu hawa walikosea kwa kusema alikuwa mungu, walakini hakufanya lolote kuwarekebisha.
5. Kwa kufanya hivyo Herode alishindwa kumtukuza Mungu na alipata hatia ya kujiinua bure.
6. Na, kwa kuwa Herode hakumtukuza Mungu wa kweli aliye hai, Bwana alimtuma malaika kumpiga Herode.
7. Kama matokeo Herode alikufa kifo kibaya akishaliwa na chango.
8. Hakika, kila mmoja wetu anaweza kujifunza somo zuri kutokana na picha hii ya ajabu ya kifo cha Herode.
   a. Somo ni kwamba watu wote wanaojivuna bure na kushindwa kumpatia Mungu utukufu, hatimaye wataangamizwa na Mungu iwapo hawatatubu (Linga. Mith.16:18; 1 Pet.5:5, 6).
   b. Kila mmoja wetu basi na ajitahidi kunyenyekea na kumpa Mungu utukufu ambao anastahili sana!

### g. (12:24,25) NENO LIKAZIDI KUENEA / SAULI NA BARNABA WAREJEA ANTIOKIA

1. Mbali na kifo cha Yakobo na kutiwa gerezani kwa Petro, kanisa likazidi kukua kadiri neno la la Mungu zuri ajabu lilivyozidi kuenezwa.
    a. Kama tulivyoona, hili ni tukio linalotukia mara kwa mara katika kitabu cha Matendo.
    b. Ndiyo kusema, kanisa limeteswa, walakini lilizidi kukua kadiri Wakristo walioteswa waliendelea kuhubiri, kufundisha, na kuishi kulingana na neno, kadhalika katika kumwomba Mungu.
2. Katika mst.25 mara picha imehamia kwa Sauli na Barnaba.
    a. Baada ya kuchukua msaada kutoka Antiokia kwenda Yerusalem, wakarejea Antiokia.
    b. Waliporejea, wakamchukua Yohana Marko pamoja nao.
3. Mtazamo kwa ufupi wa 12:1-25, Mateso kutoka serikali ya ndani.
    a. Mst.1,2 Herode amwua Yakobo.
    b. Mst.3-5 Herode alimtia gerezani Petro / kanisa likazidi kuomba daima kwa ajili ya Petro.
    c. Mst.6-11 Mungu alimtoa Petro kimiujiza toka gerezani.
    d. Mst.12-17 Petro alikwenda nyumbani kwa Mariam walimokuwa wakiomba.
    e. Mst.18,19 Kutoroka gerezani kwa Petro kwagundulika.
    f. Mst.20-23 Herode alishindwa kumpa utukufu Mungu na akafa.
    g. Mst.24,25 neno likazidi kuenea / Sauli na Barnaba warejea Antiokia.
4. Hili linahatimisha sehemu kubwa ya pili ya kielelezo chetu:
    a. 1-7 Kanisa lilianzishwa Yerusalem.
    b. 8-12 Kanisa lilitawanyika kwenda Yudea na Samaria.
    c. 13-28 Kanisa lilienea hata mwisho wa dahari.
        (1) 13,14 Safari ya kwanza ya umisionari (Sauli na Barnaba).
        (2) 15-18:12 Safari ya pili ya umisionari (Paulo na Sila).
        (3) 18:23-21:14 Safari ya tatu ya umisionari (Paulo).
        (4) 21:15-28:21 Paulo mikononi mwa maadui.
    d. 13,14 Safari ya kwanza ya umisionari (Sauli na Barnaba).
        (1) 13:1-3 Kuitwa kwa Barnaba na Sauli.
        (2) 13:4-14:28 Safari ya kwanza ya umisionari (Sauli na Barnaba).
            (a) 13:4-13 Katika Kipro.
            (b) 13:14-50 Katika Antiokia Pisidia.
            (c) 13:51-14:5 Katika Ikonia.
            (d) 14:6-20 Katika Listra.
            (e) 14:26-28 Paulo na Barnaba alitaarifu kwa ndugu Antikia.

## III. (13-18) KANISA LILIENEA KWENDA MWISHO WA DAHARI

### A. (13,14) SAFARI YA KWANZA YA UMISIONARI / SAULI NA BARNABA

#### 1. (13:1-3) KUITWA KWA BARNABA NA SAULI

1. Katika mistari hii picha imerejea katika kanisa la Antiokia.
2. Tafadhali kumbuka mambo yafuatayo ya kweli kuhusu kusanyiko hili la Wakristo.
    a. Mst.11:19 Walitawanyika baada ya kifo cha Stefano walikwenda Antiokia na wakahubiri neno kwa Wayahudi.
    b. 11:20 Baadhi ya watu hao walihubiri injili kwa Mataifa pia.
    c. 11:21 Kama matokeo wengi walimwamini na kumtii Bwana.
    d. 11:22-24 Yerusalem ikampeleka Barnaba kuwatia moyo na kufanya kazi na kanisa.
    e. 11:25 Barnaba alimpeleka Sauli kutoka Tarso kwenda Antiokia.
    f. 11:26 Barnaba na Sauli walifanya kazi kwa mwaka na kufundisha watu wengi.
    g. 11:26 Wanafunzi waliitwa “Wakristo” kwanza hapo Antiokia.

h. 11:27-30 Wakristo hawa safi walituma misaada kwa ndugu zao Yudea ambao waliokuwa wanateseka na njaa.

3. Kwa taarifa hizo za msingi akilini tunajifunza mst.1 Barnaba na Sauli walikuwa miongoni mwa Wakristo waliohudumu katika Bwana kama manabii na waalimu.
4. Roho Mtakatifu alibainisha kuwa alimwitaji Barnaba na Sauli kutengwa kwa kazi maalum.
5. Wakafunga na kuomba, wakaweka mikono juu ya Barnaba na Sauli, na kuwatuma.
   a. Kama tulivyojifunza nyuma, kuwekewa huku mikono ilikuwa swala la kuwatenga Barnaba na Sauli na kuwatuma kwa kazi yao mpya.
   b. Halikuwa jambo la kuwapatia uwezo wa kutenda miujiza.
   c. Aina hiyo ya kuwekewa mikono ingetendwa na mitume tu (linga.8:14-19; 19:6; 2 Tim.1:6).
6. Kabla ya kuondoka katika mistari hii tunapenda kuelezea mambo kadhaa.
   a. Kwanza, angalia mst.2 na 3 kwamba Wakristo hawa wa awali "walifunga."
      (1) Kufunga ni kuhiari binafsi kukana chakula kwa kipindi fulani.
      (2) Yesu alisema wanafunzi wake wangefunga wakati akiondoka duniani (Mt.9:15).
      (3) Kufunga ni njia ya kujinyenyekeza wenyewe mbele ya mwenyezi Mungu (Ezr.8:21).
      (4) Ni njia pia ya kuonyesha toba, kama tulivyoona katika swala la Sauli (9:9).
      (5) Kuomba na kufunga vinaambatana kwa pamoja.
      (6) Wakristo wa awali waliona kufunga na kuomba nyakati muhimu sana, kama huu wakuwatuma Wakristo wenzao katika kazi mpya na kuchagua wazee (linga.14:23).
      (7) Ingawa hatujaamuriwa kufunga, tunakwaalika kujifunza maadiko haya kutambua iwapo kuna haja ya kujitolea kufunga zaidi!
      (8) Wale wanaopenda kuhiari kufunga wanapaswa kukumbuka maonyo ya Bwana na ahadi zake zinazopatikana katika Mt.6:16-18!
   b. Pili, ni jambo la msingi kuelewa tofauti jinsi Sauli na Barnaba walivyoitwa na kutengwa karne ya kwanza na jinsi tunavyofanya hivyo.
      (1) Kama tunavyoona mst.2 Sauli na Barnaba waliitwa na kutengwa kwa ajili ya kazi maalum moja kwa moja na Roho Mtakatifu.
      (2) Walakini, tunapaswa kukumbuka haya yalikuwa kipindi cha miujiza karne ya kwanza.
      (3) Kinyume chake, Mungu anaita watu leo kwa njia ya injiliiliyofunuliwa kwa Roho Mtakatifu karne ya kwanza (2 Thes.2:14).
      (4) Baada ya kutii injili, ndugu Wakristo wanafundishwa kwamba wanapaswa kwenda na kufundisha wengine injili tukufu hiyo ya injili (Mt.28:19,20).
      (5) Roho Mtakatifu haiti na kuwatenga watu kwa ajili ya kazi maalum moja kwa moja leo tena!
      (6) Badala yake, anafanya hivyo kupitia upanga wa Roho, neno la Mungu!

### 2. (13:4-14:28) SAFARI YA KWANZA YA UMISIONARI

#### a. (13:4-13) KATIKA KIPRO

##### (1) (13:4,5) MAHUBIRI KATIKA MASINAGOGI / YOHANA MARKO ASAIDIA

**13:4,5)**

1. Kama ilivyoamuriwa na Roho Mtakatifu, Barnaba na Sauli walipanda mashua kuelekea Kipro, ambako utakumbuka ni nyumbani kwa Barnaba (linga.4:36).
2. Walihubiri neno la Mungu katika sinagogi ambamo watu walizoelea maandiko ya Agano la Kale.
3. Kwa nyongeza, Barnaba na Sauli walikuwa pamoja na Yohana Marko akiwasaidia.

##### (2) (13:6-8) ELIMA (BAR-YESU) AWAPINGA SAULI NA BARNABA

**13:6-8)**

1. Walivyosafiri katika kisiwa cha Kipro walimkuta nabii wa uongo wa Kiyahudi ambaye jina lake aliitwa Bar-Yesu au Elima.
2. Elima alikuwa akimfundisha afisa wa Kirumi aliyeitwa Sergio Paulo, ambaye ametajwa kuwa mtu mwenye akili.
3. Sergio Paulo pia aliwaita Sauli na Barnaba ili aweze kusikia neno la Mungu.
4. Walakini, Elima alimpinga Barnaba na Sauli na kujaribu kumgeuza Sergio Paulo asisikie injili ya Kristo.
5. Kwa bahari nzuri, ni jambo la kufurahisha kuona njia tofauti injili imeelezwa katika fungu hili.
6. Kwa mfano, katika mst.5-12 injili imebuniwa kwa njia nne zifuatazo:
   a. Mst.5.
   b. Mst.8.
   c. Mst.10.
   d. Mst.12.

### (3) (13:9-12) SAULI (PAULO) AMPIGA KWA UPOFU ELIMA / SERGIO PAULO AAMINI

**13:9-12)**

1. Katika mst.9 tunajifunza kwa mara ya kwanza kwamba Sauli aliitwa pia Paulo.
2. Paulo alimkazia macho Elima kwa makini na kuanza kuzungumza naye.
3. Tunaona alama njema za tabia ya Mungu kwa waalimu wa uongo tunapochanganua mambo manne katika maelezo ya Paulo kwa Elima.
   a. "mwenye kujaa hila na uovu wote".
      (1) Hila na uovu ndizo mbinu ambazo waalimu wa uongo wanatumia.
      (2) Linga. 2 Kor.11:13-15; Efe.6:11; 2 Kor.2:11.
   b. "mwana wa Ibilisi".
      (1) Ni wazo la busara kwetu kutambua kuwa mwenyezi Mungu anawataja waalimu wa uongo kama watoto wa Ibilisi!
      (2) Linga. Yoh.8:44.
   c. "adui wa haki yote".
      (1) Shetani na waalimu wake wa uongo hupinga kila kilicho cha haki, ukijumuisha amri za Mungu, ambazo ni za haki (Zab.119:172).
      (2) Hakika, Shetani ni adui wetu mwenye kufisha (1 Petr.5:8)!
   d. "huachi kuzipotoa njia za Bwana zilizonyooka".
      (1) Kupotosha ni haribu maana (distort), badilisha, au geuza kuwa kitu kingine kinyume na kilivyo.
      (2) Waalimu wa uongo hupotosha na kuharibu maana ya maandiko na kugeuza maana kuwa kitu kingine mbali na Mungu alivyokusudia (2 Pet.3:16).
      (3) Na kulingana na mstari huu, wanapofanya hivyo, wanajiletea maangamizi yao wenyewe, kadhalika hao wanaosikia na kuwaamini hao (2 Pet.3:17)!
   e. Tunapotafakari mambo haya kuhusu manabii wa uongo, haistaajabishi kuona kwamba ahadi za Mungu kwao ni mbaya sana, adhabu ya milele kwao (linga. Gal.1:8,9; 2 Pet.2:1-18).
4. Katika mst.11 Paulo alimweleza Elima kwamba Mungu ("mkono wa Bwana") ungeenda kumpinga kwa upofu kwa kitambo ("kwa muda").
   a. Hii ni miujiza ya pekee kufanywa na mtume ambayo ilisababisha kumwumiza mtu.
   b. Kwa nini Mungu aliruhusu miujiza hii kufanyika kwa namna ambayo Elima akawa kipofu?
      (1) Sergio Paulo alikuwa akisikiliza mafundisho ya uongo ya Elima.
      (2) Sergio Paulo pia alitaka kusikia ukweli wa neno la Mungu kutoka kwa Paulo na Barnaba.

(3) Lakini Elima aliwapinga Sauli na Barnaba na kujaribu kumgeuza Sergio Paulo kuwa mbali na imani.
(4) Basi, Sergio Paulo alikuwa akisikia ujumbe aina mbili wa ujumbe toka katika aina mbili za viini vyema mvuto.
(5) Njia pekee ya kushawishi zaidi ambayo Mungu angeweza kudhihirisha ukweli wa neno lililonenwa na wajumbe wake na makosa ya Elima ilikuwa kumtuhusu Paulo kutenda miujiza hii.
(6) Sergio Paulo alipomwona Elima amepigwa na upofu na si lolote kama vile Paulo alivyodai angekuwa kipofu kwa muda, alitambu kuwa Mungu yu kinyume na Elima na alikuwa pamoja na Paulo na Barnaba.

5. Katika mst.12 tunajifunza Sergio Paulo aliamini injili kutokana na mambo ya msingi mawili:
   a. Miujiza iliyotendeka katika kumtia upofu Elima, na
   b. Mafundisho ya kustaajabisha ya Bwana.

**(4) (13:13) PAULO AKIWA PERGA / YOHANA MARKO AREJEA YERUSALEM**

**13:13)**

1. Paulo pamoja na watu aliokuwa nao waliondoka Pafo katika kisiwa cha Kipro na kwenda Perga katika eneo la Pamfilia.
2. Luka pia alitaja kuwa Yohana Marko aliwaacha na kurejea Yerusalem.
3. Ingawa Luka haelezi kwa nini Yohana Marko aliondoka, tutajifunza baadaye kwamba Paulo aliona kwamba Yohana Marko alifanya makosa kwa sababu aliiacha kazi ambayo alijitolea kuifanya pamoja na Paulo na Barnaba (15:38).

**b. (13:14-50) KATIKA ANTIOKIA YA PISIDIA**

**(1) (13:14-43) UJUMBE WA PAULO SIKU YA KWANZA YA SABATO**

**(a) (13:14-22) ISRAELI KUTOKA MISRI HADI DAUDI**

**13:14,15)**

1. Tena, wakaondoka Perga na kwenda Antiokia katika eneo la Pisidia.
2. Katika Antiokia waliingia katika sinagogi na wakuu wa sinagogi wakawapatia nafasi ya kunena na watu.
3. Ni dhahiri kuwa Paulo na Barnaba hawakuingia katika sinagogi kwa sababu walikuwa wakifanya mambo ya Kiyahudi
4. Basi kwa nini wanaingina katika sinagogi? Tunaweza kutoa sababu kadhaa.
   a. Mst.16 Kulikuwa na Wayahudi waliomcha Mungu wengi huko.
   b. Mst.43 Kulikuwa na watu wengi waliokuwa waongofu hapo.
   c. Mst.15 Watu hawa walisoma na kufahamu vyema maandiko ya Agano la Kale, ambalo lina unabii mwingi kuhusu Masihi.

**13:16-22)**

1. Paulo alianza kusema kwa kuwataja wasikilizaji kwa kufurahisha kama, "enyi waume wa Israeli, nanyi mnaomcha Mungu" (mst.16).
2. Kisha akawasihi wasikilize alichokuwa anakwenda kusema kama historia fupi ya Israeli.
3. Kwa kufanya hivyo Paulo alitaka wamsikilize kwa karibu akiwasihi kwa mambo ya historia ambayo walijivunia – historia yao, ukijumuisha ukweli wa kwanba Mungu aliwajali.
4. Ingawa hatuna muda kujifunza historia hii kwa maelezo zaidi, tunakuomba upitie kozi katika vitabu vitano vya Musa (pentateuch) na historia ya Agano la Kale na "World Video Bible School."
5. Katika mst.22 Paulo alimtambulisha mfalme Daudi kama mtu aliyekuwa na moyo wa Mungu, katika ukweli wa kwamba alimtii Mungu.

6. Hakika, Waisraeli walimheshimu Daudi kama nabii wa Mungu na mfalme na kupitia kwake Masihi angetokea.

### (b) (13:23) YESU: MWOKOZI KUPITIA UZAO WA DAUDI
### (c) (13:24,25) YESU: YOHANA ALIHUBIRI KUJA KWAKE

**13:23,24)**

1. Katika mst.23 Paulo kwa ujasiri alidai kwa uvuvio kwamba Yesu ndiye Masihi aliyetabiriwa, wa ukoo wa Daudi, ambaye Baba alimfufua kuwa Mwokozi!
2. Kwa kufanya hivyo Paulo alikuwa akirejea katika unabii wa Agano la Kale kama vile Isa.11:1 na Zab.132:11.
   a. Alitambua kwamba Wayahudi waliukubali unabii huo kuwa wenye mamlaka kwa sababu walitambua kuwa ni unabii wa Mungu uliovuviwa juu ya Masihi.
   b. Kama tulivyoona kwa masomo yetu kwa maelezo mengi ya unabii kama huu katika sura 2 na 3, Petro alidhihirisha kupitia maandiko kuwa Yesu ni Kristo kwa sababu alitimiza unabii huu wa ajabu bayana na sahihi.
   c. Sasa, katika sura hii, Paulo alikuwa akitumia mbinu sawa ya kuthibitisha kuwa Yesu ni Kristo, Masihi, mwokozi aliyesubiriwa kwa muda mrefu!
3. Na katika mst.24,25 Paulo aliongeza ushuhuda wa Yohana Mbatizaji kwamba Yesu ndiye Kristo ambaye Waisraeli walingojea.
   a. Watu wa Israeli pia walimwona Yohana kuwa nabii muhimu na mtu wa Mungu.
   b. Basi, katika kuonyesha Yohana alivyodai hakuwa Masihi, lakini Yesu ndiye, Paulo alikuwa akitoa ushahidi zaidi na nguvu ya madai yake kwamba Yesu ndiye Masihi!
   c. Na ushahidi huu na mamlaka vilikuwa na nguvu kiwango cha mtu yeyote aliye mwaminifu na moyo mnyofu angekubali – wakati huo na sasa!

### (d) (13:26-29) YESU: ISRAELI WALIMWUA KAMA ILIVYOTABIRIWA NA MANABII

**13:26-29)**

1. Angalia katika mst.26 njia bora ambayo Paulo amewakilisha ujumbe wake aliohubiri kwa wasikilizaji wake – "neno la wokovu huu"!
2. Kama Petro katika sura 2 na 3, Paulo alibainisha kwamba Baba aligeuza hukumu yao isiyo na haki ya kifo juu ya Yesu kwa kumfufua toka kwa wafu.
3. Zaidi sana, katika mst.31, Paulo alisema kwamba Yesu alijidhihirisha mara nyingi baada ya kufufuka kwake mbele ya mashahidi wengi, akithibitisha kuwa ufufuo wake si jambo la uongo.
4. Katika mst.32,33 Paulo alihubiri baadhi ya mambo mema ("habari njema"), k.m. Injili!
5. Habari njema hizo ziliambatana na "ahadi" alitoa Mungu kwa baba zao wa taifa la Israeli.
   a. Ahadi hiyo ni kwamba Mungu angewabariki jamii zote za dunia kupitia uzao wa Abraham (Mwa.12:1-3; 22:18).
   b. Tunatambua kutokana na somo letu kwamba Yesu Kristo ndiye aliye uzao aliyetimiza ahadi (Gal.3:16, 19).
   c. Tena, tunajifunza kwamba baraka ingewafikia hao ambao wangeruhusu upendo wa Baba na Mwanawe Yesu kuwavuta na kugeuka mbali na dhambi zao (linga. somo letu la 3:25,26).
6. Katika mst.33 Paulo alieleza kuwa Mungu alitimiza unabii kwa kumfufua Yesu Kristo kutoka kwa wafu.
7. Basi, mwishoni mwa mst.33, Paulo alinukuu kutoka katika Zab.2:7 kuthibitisha alichosema. "Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa."
   a. Kwa maneno mengine, Paulo alisema kwa uvuvio kwamba Zab.2:7 ilitabiri ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu, kama Masihi, Kristo.
   b. Katika Zaburi hiyo, Baba anarejea siku ambayo atathibitisha kikamilifu kabisa kudhihirisha kuwa Yesu ni Mwanawe pekee.

c. Siku hiyo ni siku aliyomfufua kutoka katika wafu hata uzima wa milele.
d. Linga. Rum.1:4.
e. Linga. somo letu la 2:30-36.
f. Lakini, kuna uhusiano gani wa ufufuo wa Yesu na habari njema, baraka kwa jamii zote za dunia, wokovu wa mwanadamu? Tafakari maandiko yafuatayo tuliyojifunza kabla:
   (1) Rum.4:25.
   (2) Ebr.2:17,18.
   (3) 1 Kor.15:54-57.

**13:34-37)**

1. Katika 34,35 Paulo aliendelea kunukuu maandiko kuthibitisha Mungu alitabiri kuwa angemfufua Yesu, Masihi kutoka kwa wafu na wala asiuache mwili wake uharibike ("asipate kurudi uaharibifu").
   a. Katika mst.34 alirejea Isa.55:3 na 2 Sam.7:15,16 kuhusu "Nitawapa ninyi mambo matakatifu ya Daudi yalioyo amini".
   b. Kwa uvuvio aliunganisha maneno hayo kwa ufufuo wa Yesu.
   c. Na katika mst.35 Paulo alinukuu Zab.16:10, ambayo ni maneno dhahiri ya ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu akiwa Masihi (linga. somo letu katika sura 2).
2. Katika mst.36 alionyesha kwamba Zab.16:8-11 isingemhusu Daudi kwa sababu mwili wake ulikuwa kaburini ukiharibika.
   a. Utakumbuka kwamba Petro alitoa maelezo kama haya katika 2:29-31.
3. Basi, katika mst.37 Paulo alitoa tofauti kubwa kati ya Daudi na Yesu.
   a. Tofauti hiyo ni kwamba mwili wa Daudi iliharibika kaburini, bali Baba alimfufua Yesu kutoka kwa wafu na mwili wake haukuona uharibifu.
4. Kusema kweli, katika kutoa tofauti hizo ilikuwa ni kubainisha kuwa Zab.16:10 si unabii kuhusu Daudi.
5. Kinyume chake, ulikuwa unabii wa ajabu kuhusu ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu ukiwa ni uthibitisho kuwa yeye ni Masihi.
6. Hivyo basi, kuanzia mst.23, Paulo kwa ufupi, lakini kikamilifu alithibitisha kwamba Yesu ndiye Kristo, Masihi, Mwokozi.
7. Angalia hoja za nguvu za ajabu za Paulo kwamba Yesu ndiye Masihi. Nguvu hizo zimeonekana kwa nukuu zake kama mamlaka ifuatavyo:
   a. Mst.23 Yesu ndiye Masihi aliyetabiriwa.
   b. Mst.24,25 Nabii na mtu mkubwa wa Mungu, Yohana Mbatizaji alimtambua Yesu kama Kristo.
   c. Mst.27-29 Manabii walitabiri kuwa Yesu ni Masihi – hata kukataliwa na kifo chake mikononi mwa Waisraeli.
   d. Mst.30 Baba aligeuza hukumu hiyo isiyo ya haki.
   e. Mst.31 Baada ya ufufuo wake wenye utukufu, Yesu alitokea mbele ya mashahidi wengi.
   f. Mst.32,33 Yesu ndiye aliyeitimiza ahadi ya Mungu kwa baba zao Israeli.
   g. Mst.33 Ahadi hiyo ilitimia kwa ufufuo wake Yesu kutoka kwa wafu.
   h. Mst.33 Ufufuo ulikuwa ni unabii katika Zab.2:7.
   i. Mst.34 Alitabiri nabii mkubwa Isaya katika Isa.53:3.
   j. Mst.35 Alitabiri Daudi katika Zab.16:10.
8. Ni nguvu kiasi gani ujumbe huo wenye ushahidi mwingi ulipata ndani ya mioyo ya wasikilizaji siku hiyo?
   a. Hakika, wenye mioyo minyofu na safi siku hiyo waliamini kwamba Yesu ndiye Kristo, Masihi, Mwokozi!
   b. Kama inavyopaswa kwangu na kwako kutumia ushahidi mwingi huu wa neno la Mungu kuwashawishi wengine kutii na kumfuata Bwana Yesu Kristo!

**(f) (13:38-43) MSAMAHA NA KUHESABIWA HAKI KUPITIA KWAKE**

**13:38,39)**

1. Sasa Paulo huyo alipothibitisha kwamba Yesu ndiye Masihi na kwamba ndiye tunapaswa kumtii, alitoa habari zingine njema kwa wasikilizaji wake.
2. Habari hizo njema ni ujumbe kwamba wangeweze kupokea msamaha wa dhambi kupitia mtu huyo Yesu!
3. Hakika kabisa, alisema kwamba yeyote amwaminiye angeweza kuhesabiwa haki katika kila jambo ambalo ni vigumu kuhesabiwa haki kwa njia ya Sheria ya Musa.
   a. Kuhesabiwa haki maana yake kutangazwa kuwa huna hatia; kuwa huru mbali na hatia ya dhambi, kuonekana una haki mbele ya macho ya Mungu.
   b. Kwa maneno mengine, kwa njia ya kumwamini Yesu kama ndiye Kristo, isingeliwezekana wakati huo na hata sasa kwa watu wote kupata msamaha wa dhambi na kutangazwa kuwa hana hatia ya dhambi zake za nyuma.
4. Ni ujumbe wa ajabu kiasi gani kwa watu hao kusikia siku hiyo!
   a. Ni jambo njema kwetu sisi kama Wakristo siku hizi kufurahi ziku zote (linga. Zab.51:12)!
   b. Ni jambo la kuvutia kuwa na uwezo wa kuhubiri maneno mazuri ajabu ya wokovu kwa wengine!
5. Hakika, lazima tukumbuke katika somo lililotangulia juu ya aina ya imani inayookoa au yenye kuhesabia haki.
   a. Imani hiyo si imani pekee!
   b. Kinyume chake, ni imani ya kumtii Mungu kutoka katika moyo uliojaa upendo kwake na Mwanawe mpendwa aliyetufia!

**13:40,41)**

1. Ni dhahiri, Paulo aligundua baadhi ya wasikilizaji wake walikuwa karibu na kuasi juu ya ujumbe wa msamaha wa dhambi kwa njia ya Yesu.
2. Hivyo basi, aliwaonya akinukuu kutoka kwa nabii Habakuki (Hab.1:5).
   a. Aliwaonya wasidharau na kutoamini kazi kubwa Baba aliyoifanya (k.m., kutoa njia ya wokovu kwa njia ya Mwanawe, Yesu).
   b. Kazi ya wokovu kupitia Kristo ilibainishwa wazi mbele yao na Paulo na wazungumzaji wengine waliovuviwa.
   c. Na Mungu alisema ikiwa walichagua kudharau na kutoamini ujumbe huo wa wokovu, Mungu alisema "wangeangamia"!

**13:42,43)**

1. Paulo alipomaliza kunena, Wayahudi wakatoa nje ya sinagogi.
2. Kwa nyongeza, Mataifa waliwasihi Paulo na Barnaba kuwahubiri tena sabato nyingine.
3. Zaidi sana, Wayahudi wengi na wale waliokuwa waongofu wakawafuata Paulo na Barnabas, ambao waliwashawishi kudumu katika neema ya Mungu.

(2) (13:44-50) UJUMBE WA PAULO SABATO YA PILI
  (a) (13:44,45) KARIBU MJI MZIMA ULIKUSANYIKA / WAYAHUDI WAKUFURU
  (b) (13:48-50) PAULO NA BARNABA WAWAGEUKIA MATAIFA

**13:44-47)**

1. Mahubiri ya Paulo na Barnaba yalikuwa ya nguvu kiasi cha mji mzima kukusanyika pamoja kusikia neno la Mungu sabato iliyofuata.
2. Walakini, Wayahudi wakajaa wivu na kumpinga mnenaji wa Mungu.
3. Kwa ujasiri mkubwa, Paulo na Barnaba waliwakemea Wayahudi wenye wivu kwa mambo matano yafuatayo:
   a. Ilikuwa muhimu kuhubiri injili kwa Wayahudi kwanza (linga. somo letu katika 3:26).

b. Walakini, walimkataa Yesu na injili yake.
c. Kwa kufanya hivyo, walijihukumu wenyewe kwamba hawakustahili uzima wa milele!
d. Matokea yake Paulo na Barnaba walikuwa waende wakahubiri kwa Mataifa.
e. Kwa kufanya hivyo Paulo na Barnaba walikuwa wakitii amri ya Mungu.
   (1) Ili kuunga mkono swala hilo, Paulo na Barnaba walinukuu Isa.42:6 na 49:6.
   (2) Katika mafungu hayo Mungu alitabiri wakati ambao watu wake wangekuwa nuru kwa Mataifa na wokovu utakapopatikana hata mwisho wa dunia.

**13:48-50)**

1. Mataifa walifurahi sana kusikia ujumbe huo wa wokovu, waliuamini na kutukuza neno la Bwana.
2. Katika mst.49 tunaona maelezo mazuri ya kwamba neno la Bwana likaenea eneo zima hilo.
3. Walakini, Wayahudi wenye wivu walihamasisha kuwaudhi Paulo na Barnaba na kuwatoa nje na eneo hilo.
4. Kabla ya kuondoka katika mistari hiyo tunapaswa kujadili maneno yenye kufurahisha katika mst.48.
5. Katika mstari huu, panasema "nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini".
6. Watu wengi katika ulimwengu wa dini wanatumia mstari huu kufundisha kwamba kabla ya ulimwengu, Mungu kwa kupenda kwake pasipo masharti alichagua au kukusudia watu wengine kupokea uzima wa milele, na wengine hukumu ya milele.
7. Hii ni sehemu ya mafundisho yanayojulikana kama "Calvinism."
8. Hatuna muda kwa sasa kujifunza fundisho hili, ili tunakutaka urejee kozi kutoka "World Video Bible School" katika mafundisho ya madhehebu, ambamo imebainishwa zaidi.
9. Walakini, bila hata kujifunza kwa maelezo mengi Ukalvin, tunaweza kutambua kuwa mstari huu haufundishi kwamba Mungu kwa kupenda kwake pasipo masharti aliwachagua Mataifa siku hiyo, au watu wengine wowote kwa wakati wowote, kupokea uzima milele!
10. Tunaweza kutambua hili kutokana na kujifunza mazingira!
11. Kwanza, ebu tuone mazingira ya karibu (the immediate context).
    a. Katika mst.46 Paulo aliwakemea Wayahudi na kusema kwamba walikuwa na hatia ya kulikataa neno la Mungu.
       (1) Kwa maneno mengine, Wayahudi walikuwa wawajibike kutokana na makosa yao ya kulikataa neno la Mungu.
       (2) Ni kweli jambo hilo kwa sababu Wayahudi walikuwa na hiari ya kulikubali ama kulikataa neno la Bwana (linga. 1 Fal.18:21; Yosh.24:15).
       (3) Walipochagua kwa hiari yao kulikataa neno la Mungu, "walijihukumu wao wenyewe kutokustahili uzima wa milele."
       (4) Kwa hiyo, tunaweza kuona bayana kuwa Mungu kwa kupenda kwake pasipo masharti hakuwachagua Wayahudi hao waende katika hukumu ya milele.
       (5) Kinyume chake, waliamua wao wenyewe na Mungu kupitia Paulo wawajibike kutokana na uchaguzi wao mbaya.
    b. Kwa jinsi hiyo hiyo Mataifa katika mst.48 walikuwa na hiari ya kuchagua walipolisikia neno la Mungu.
       (1) Nao walikuwa na hiari ya kukubali ama kukataa.
       (2) Kwa bahati nzuri, walifurahia kusikia neno hilo na wakaamua kuliamini, na kulitukuza.
       (3) Hata wakasihi wasikilize zaidi neno la Mungu!
       (4) Basi, kinyume na Wayahudi katika mst.46, Mataifa hawa walilipokea neno la Mungu kuliko kulikataa!
       (5) Tena, kama tulivyotangulia kuona katika somo letu, kupokea neno la Mungu maana yake ni kulitii (Ebr.5:8,9).
       (6) Mataifa walipoamua kuchagua hivyo, walichaguliwa kwa ajili ya uzima wa milele, kadiri walivyobakia kuwa waaminifu kwa Bwana hata kifo (Ufu.2:10).

c. Kutokana na mistari hii miwili katika mazingira haya, tunaweza kuona dhahiri kwamba Mungu kwa kupenda kwake pasipo masharti hakuchagua Mataifa kupokea uzima wa milele.
   (1) Badala yake, Mataifa kwa hiari yao walichagua kupokea neno la Mungu.
   (2) Matoke ya uchaguzi wao ni uzima wa milele, kwa masharti ya kubakia waaminifu hata kifo.
d. Kwa upande mwingine, Wayahudi waliotajwa katika mst.46 kwa hiari walichagua kukataa neno la Mungu.
   (1) Matokeo ya kutokutii kwao ni hukumu ya milele, isipokuwa kama walitubu na kumtii Bwana kabla hawajafa.

12. Ikiwa maana hii ya mst.46 na 48 ni sahihi, basi ni sharti ilingane na mazingira ya sehemu zingine zilizobakia za Biblia.
   a. Tumeona tayari kwa kiina katika somo letu juu ya mazingira ya kitabu cha Matendo kwamba Mungu amempatia mwanadamu uhuru wa kuchagua ama kutii au kulikataa neno lake (2:40,41).
   b. Ukweli huo huo unapatikana katika mazingira ya sehemu zingine zote za Agano Jipya katika mafungu kama Flp.2:12; 1 Tim.4:16; Mt.11:28-30; na Ufu.22:17.
   c. Kwa hiyo, ukweli kwamba katika mst.46 na 48, Mungu anafundisha uhuru wa mtu wa kuchagua na Ukalvini haulingani kabisa na sehemu zingine zote za Biblia.
   d. Kwa sababu hiyo, msimamo wa Ukalvini katika mst.48 unafundisha kwa kupenda kwake Mungu pasipo masharti anachagua watu wengine kwa ajili ya adhabu ya milele!

### c. (13:51-14:5) KATIKA IKONIO

#### (1) (13:51-14:1) AKIZUNGUMZA KATIKA SINAGOGI

**13:51,52)**

1. Kutokana na kufukuzwa kwao eneo hilo karibu na Antiokia, Paulo na Barnaba "Nao wakakung'uta mavumbi ya miguu yao" wakaenda Ikonio.
   a. Kufuatia Mk.6:11, Bwana aliwaeleza wanafunzi wake kukung'uta mavumbi ya miguu yao juu yao ambao hawatasikia na kupokea neno.
   b. Jambo hilo lilikuwa ushuhuda juu yao wasiodikia neno la Mungu na onyo kali la hukumu inayokuja!
   c. Kulingana na Lk.10:16, hao waliowakataa wajumbe wa Bwana Yesu walimkataa Yesu na Baba aliyemtuma.
   d. Ni dhahiri basi, kuwakataa wajumbe wa Mungu ambao kwa uaminifu hunena neno lake ni kosa kubwa lenye madhara ya milele!
2. Mbali na mateso na kufukuzwa kwa mitume, Wakristo wa Antiokia walijaa furaha na Roho Mtakatifu.
   a. Jambo hili linadhihirisha furaha ya Mkristo katika Bwana haitegemei hali au mazingira ya nje.
   b. Mkristo mwaminifu anaweza kufurahi katika Bwana daima na mahali popote na hali yoyote ile (Flp.4:4)!
   c. Sehemu ya furaha ya Mkristo inatokana na ukweli kwamba ana Roho Mtakatifu akiishi ndani yake (si katika hali ya kuwezeshwa kutenda miujiza leo).

#### (2) (14:2-5) AKIZUNGUMZA KWA UJASIRI KATIKA BWANA, BILA KUJALI UPINZANI

**14:1-5)**

1. Katika Ikonio Paulo na Barnaba walinena kwa ujasiri hata kundi kubwa la Wayahudi na Wayunani wakaiamini injili (mst.1).
   a. Ni muhimu sana kubainisha jinsi imani ilivyoundwa ndani ya mioyo ya Wayahudi na Wayunani hawa.

b. Ingawa Roho Mtakatifu alikuwa akitenda miujiza siku hizo, hakuunda imani ndani ya watu hao kimiujiza akifanya kazi ndani ya mioyo yao!
c. Badala yake, alifanya hivyo kupitia upanga wa Roho, neno la Mungu!
d. Ndiyo kusema, alifanya hivyo kwa njia ya maneno ambayo Paulo na Barnaba walizungumza – ("na kwa vile walivyonena… wakaamini")!
e. Linga. somo letu la 3:37.
f. Linga. Rum.10:17 na Yoh.20:30,31.
g. Kama ilivyo kweli, Roho Mtakatifu haundi imani ndani ya mioyo ya watu leo kwa njia ya siri, miujiza akifanya kazi mioyoni mwao!
h. Angali anatumia upanga wa Roho, neno la Mungu!

2. Ndani ya mafanikio haya Wayahudi wasioamini walijishughulisha sana kutia sumu akili za Mataifa juu ya ndugu!
3. Mbali na upinzani huo Paulo na Barnaba walikaa huko muda mrefu na kunena neno la Bwana kwa ujasiri.
4. Kwa nyongeza, Bwana alithibitisha kwamba walinena kwa mamlaka yake akiwawezesha kufanya miujiza.
5. Matokeo yake kuhubiri kwa mitume na upinzani wa Wayahudi, mji ukagawanyika kati ya waliowaunga mkono mitume na hao waliowaunga mkono Wayahudi.
   a. Mahubiri ya injili, hata inapohubiriwa kwa roho na nia njema, mara nyingi hugawanya marafiki na familia (linga. Mt.10:34-42).
   b. Pia, ni jambo la kufurahisha kwamba Paulo na Barnaba walitajwa kama mitume.
   c. Tunatambua Paulo alikuwa miongoni mwa hao waliochaguliwa moja kwa moja na Bwana Yesu kumtumia yeye kama mtume.
   d. Lakini, imekuwaje kwa Barnaba?
   e. Hakika hatuna maandishi yoyote juu ya Barnaba kuchanguliwa na Bwana kama vile kumi na mbili, Mathiya, na Paulo.
   f. Basi ni jinsi gani Barnaba aliweza kuitwa kihalali mtume?
   g. Ufunguo wa kujibu swali hili ni kutambua kwamba neno lililotafsiriwa "mtume" (αποστολοισ) katika Agano Jipya lilitumika kwa namna mbalimbali.
   h. Neno linamaanisha haswa, aliyetumwa, mwenye kutumwa kwenda.
      (1) Kwa hali ya kawaida ni pamoja na wazo kwamba mtu ametumwa kwa kusudi au lengo maalum.
   i. Ukiwa na maana hiyo akilini mwako, ebu na tuchunguze njia mbalimbali ambazo kwazo neno limetumika katika Agano Jipya.
      (1) Lk.6:13- Kurejea hao maalum waliochaguliwa na Bwana kufanya kazi maalum ya mitume (ni pamoja na kumi na mbili na Mathiya).
      (2) 1 Kor.9:1; 15:8-11 – Kurejea kwa Paulo kama asiyezaliwa kwa majira yake, lakini aliyemwona Bwana Yesu.
      (3) Neno lilitumika pia kwa maana ya jumla likimaanisha hao waliotumwa na kanisa kwa kazi maalum ya namna fulani. Angalia mifano ifuatayo:
         (a) 2 Kor.8:23 Neno lililotafsiriwa "wajumbe" katika fungu hili, "mitume wa makanisa" ni sawa na neno lililotafsiriwa "mitume" katika sehemu zingine.
         (b) Flp.2:25 Epafradito, kama mjumbe wa Wafilipi (tena, neno lilo hilo lililotafsiriwa "mitume" mahali pengine).
         (c) Rum.16:6,7 Adroniko na Junias.
         (d) 2 Kor.11:13 Hata limetumika kwa mitume wa uongo.
      (4) Ninaamini neno limetumika kwa maana hii pana "mtume" likirejea kwa Paulo na Barnaba katika mstari huu.
         (a) Ndiyo kusema, walikuwa wajumbe maalum waliotumwa na kanisa Antiokia kwenda kuhubiri injili ya Kristo (linga.13:2,3).
6. Mwisho, katika mst.5 shambulio lilijaribu kuinuka lililofanywa na baadhi ya Mataifa na Wayahudi kuwatenda jeuri na kuwapiga mawe Paulo na Barnaba.

### d. (14:6-20) KATIKA LISTRA

#### (1) (14:6,7) PAULO NA BARNABA WAONDOKA IKONIA KUELEKEA LISTRA NA DERBE

**14:6,7)**

1. Waligundua jaribu la kutaka kuwapiga mawe, Paulo na Barnaba wakaelekea Listra na Derbe, ambayo ni miji ya majimbo ya Likaonia.
2. Kama kawaida, walipofika huko, wakahubiri injili yenye utukufu ya Kristo!

(2) (14:8-10) PAULO AMPONYA KIWETE

**14:8-10)**

1. Katika Listra Paulo alimponya mtu ambaye hakuwahi kutembea kamwe.
2. Angalia tena kwamba miujiza hii ya uponyaji ilitendeka mara moja ("akasimama upesi na kwenda").
3. Kabla ya kujifunza mistari inayofuata, tunapaswa kuangalia kwa karibu zaidi mst.9,10.
4. Katika mistari hiyo inadai kwamba Paulo alimwona mtu huyo akiwa na imani ya kuponywa na Paulo akamponya.
   a. Baadhi ya watu katika ulimwengu wa dini wanaodai kutenda miujiza leo hutumia vibaya maelezo haya.
   b. Hutumia vibaya kwa kusema kwamba mtu lazima awe na imani ili aweze kupokea uponyaji.
   c. Inaposhindikana miujiza kutendeka, anayedai kutenda miujiza hukazia bila ushahidi kuwa miujiza haikutendeka kwa kuwa mtu huyo hakuwa na imani, au imani yake ni dhaifu sana.
   d. Kama tulivyoona katika somo letu la 3:9-11, haikuwa muhimu kwa mtu kuwa na imani ili aoponywe!
      (1) Ni dhahiri, kiwete katika sura hiyo hakuwa na imani katika Yesu, Petro, au Yohana.
      (2) Ukweli ni kwamba, alitarajia zawadi fulani ya kimwili kutoka kwa mitume.
      (3) Walikini, mbali na kutokuwa na imani kwake, Petro na Yohana walimponya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
   e. Katika somo letu katika mistari hii, tunarejea pia kwa Yesu alivyomponya Lazaro toka kwa wafu (Yoh.11).
      (1) Kwa kuwa Lazaro alikuwa amefariki, hakika hakuwa na imani ya kufufuka toka kwa wafu!
      (2) Walakini, Bwana Yesu alimfufua toka kwa wafu.
   f. Kutokana na mifano miwili hii, ni dhahiri kabisa kwamba watu hawakupaswa kuwa na imani ili wapokee uponyaji wakati wa karne ya kwanza miujiza ilipotendeka
5. Swali la kawaida litaibuka, "Kwa nini sasa imetajwa kuwa mtu huyu kiwete alikuwa na imani ya kuponywa?"
   a. Jibu linalowezekana ni, imani ya mtu huyu imetajwa kuonyesha kwamba uponyaji wa Paulo kwake ilikuwa zawaidi kwa ajili ya imani kubwa ya mtu huyo!
   b. Sababu ya kutoa jibu hilo inadhihirika kwamba moja ya sababu ilimsukuma Yesu kumponya mtumishi wa akida aliyepoza (Mt.8:5-13).

#### (3) (14:11-13) WATU WADHANI PAULO NA BARNABA NI MIUNGU

**14:11-13)**

1. Watu wa Listra walipoona miujiza walidhania kuwa Paulo na Barnaba walikuwa ni miungu wa Kinyunani Zeu (Zeus) na Herme (Mercury).
2. Ukweli ni kwamba, hata wakataka kutoa dhabihu kwa Barnaba na Sauli!

#### (4) (14:14-18) PAULO NA BARNABA WAWAKATAZA WATU

**14:14-18)**

1. Paulo na Barnaba walipoona watu wanataka kuwaabudu waliogopa sana na kujitahidi kuwashawishi wasifanye hivyo.
2. Paulo na Barnaba walisema mambo yafuatayo kujaribu kuwashawishi watu wasiwaabudu:
   a. Mst.15 Paulo na Barnaba walikuwa ni wanadamu tu asili sawa na watu wa Listra, k.m. hawakuwa miungu.
   b. Mst.15 Ujumbe wao kwa watu wa Listra ulikuwa kwamba walipaswa kugeuka kutoka kuabudu vitu vitupu kama sanamu na wanadamu na kumrejea Mungu wa kweli na aliye hai (linga. 1 Thes.1:9).
   c. Mst.15 Walimtaja Mungu huyo Mungu mmoja aliye hai kama muumba wa mbingu, nchi, bahari, na vyote vilivyomo (linga. Rum.1:18-25).
   d. Mst.16 Mungu aliruhusu wanadamu wawe huru kuchagua jinsi ya kuishi na nani wa kumwabudu.
   e. Mst.17 Walakini, Mungu hakujiacha pasipo ushuhuda mwingi kuwa yeye ndiye Mungu wa kweli aliye hai ambaye alipaswa (anapaswa) kuabudiwa na wanadamu.
   f. Mst.17 Ushuhuda huo ni pamoja na:
      (1) Alitenda mema.
      (2) Alinyesha mvua kutoka mbinguni na nyakati za mavuno.
      (3) Kwa baraka hizo njema aliwashibisha mioyo ya wanadamu kwa chakula na furaha!
3. Pamoja na hoja hizo za nguvu Paulo na Barnaba walizotoa, lakini ilikuwa kazi kubwa kuzuia mkutano usitolee dhabihu!

### (5) (14:19,20) PAULO APIGWA MAWE

**14:19,20)**

1. Kwa bahati mbaya Wayahudi toka Ikonio na Antiokia waliwashawishi makutano kumpiga mawe Paulo.
2. Walimburuta nje ya mji na kumwacha hapo, wakidhania kuwa amefariki.
3. Walakini, Wakristo wenzake walipofika hapo, Paulo kimiujiza alinyanyuka.
4. Na siku iliyofuata yeye na Barnaba wakasafiri kwenda Derbe; wakikusudia kumtumikia Bwana huko na kuhubiri neno leke lenye wokovu, bila kujali kilichotokea!
5. Tafadhali ebu tulia kidogo na utafakari mambo yaliyowapata Paulo na Barnaba katika safari hii.
   a. 13:45-50 Wayahudi kwa ukali waliwapinga, waliwatesa, na kuwataka waondoke Antiokia ya Pisidia.
   b. 14:2-5 Katika Ikonio Wayahudi walitia akili za watu wa Mataifa sumu juu yao, kujaribu kufanya shambulio kuwatesa na kuwapiga mawe.
   c. 14:19 Katika Listra Wayahudi waliwashawishi makutano kumpiga mawe Paulo na kumtoa nje akiwa amekufa.
6. Kutokana na habari hizi tunaona watu hawa walimpenda Bwana sana, walijitoa jumla kwake na kazi yake yenye utukufu, na kuhesabu gharama kuwa wafuasi wake (Lk.14:25-35)!
   a. Linga. 2 Kor.11:23-33.
   b. Linga. Gal.6:14,17.
   c. Kumbuka ahadi ya Bwana kwa Paulo katika 9:15,16!

### e. (14:1-25) WAKIHUBIRI WAKATI WAKIRUDI KATIKA SAFARI YAO

1. Paulo na Barnaba walihubiri injili katika Derbe na wengi wakaongolewa ikiwa ni matokeo yake.
2. Kisha Paulo na Barnaba wakaamua kutembelea miji ambayo walitembelea mapema, ikiwa ni pamoja na Listra, Ikonio, na Antikia ya Pisidia.
3. Walipofanya hivyo, imetajwa kuwa walifanya mambo matatu kama ifuatavyo:
   a. Waliimarisha roho za wanafunzi (k.m., Wakristo).
   b. Waliwaonya kukae katika imani, injili ya Kristo, Ukristo.

(1) Je, kungekuwa na haja ya kuwaonya kama mtu hawezi kuanguka toka katika neema?
c. Waliwaeleza (nasi pia) ni kwa njia pekee kwa dhiki nyingi tutaweza kuingia katika ufalme wa mbinguni.

4. Wazo hili la kuingia katika ufalme kwa njia ya dhiki nyingi ni la kufurahisha!
   a. Tuliona katika somo letu katika sura 2 kwamba neno "ufalme" na "kanisa" ni maneno mawili yenye kulenga kitu kimoja (the same institution) (k.m. Mt.16:18,19).
   b. Hivyo basi, kuingia katika ufalme ni kuingia katika kanisa.
   c. Na tumejifunza kuwa mtu huingia katika ufalme (kanisa) anaposikia injili, anaiamini, anatubu dhambi zake, anamkiri Yesu kwa kinywa chake, na kuzamishwa majini kuingia katika Kristo, na hivyo basi kupokea msamaha wa dhambi.
   d. Lakini kwa hao ambao Paulo na Barnaba walikuwa wakizungumza nao walikuwa tayari ndani ya ufalme (kanisa).
      (1) Walifanya hivyo walipotii injili, hivyo basi wakawa Wakristo (linga. 2:38, 41, 47).
   e. Tunajuaje kuwa walikuwa Wakristo?
      (1) Mst.22 Luka, kwa uvivuo wa Mungu walitajwa kama "wanafunzi" ambalo tumeliona kuwa ni neno lenye maana ya Wakristo.
      (2) Mst.22 Paulo na Barnaba waliwaonya watu hao "wakae katika imani" ambayo tumeiona kuwa ni mpango (system) wa imani, injili, unaowakilisha Ukristo.
   f. Lakini, kama watu hawa walikuwa tayari wameingia katika ufalme (kanisa) kwa njia ya utiifu wao kwa injili, kwa nini Paulo na Barnaba wanaweleza kuwa ni kwa dhiki nyingi pekee mtu angeweza kuingia katika ufalme?
   g. Ninaamini jibu linapatikana katika kutambua kwamba katika Agano Jipya, neno "ufalme" limetumika kulenga kanisa kwa maana mbili, kama ifuatavyo:
      (1) Kanisa la Bwana kabla ya siku ya hukumu.
         (a) Tulijifunza matumizi ya neno hilo katika sura 2.
         (b) Kol.1:13; 1 Thes.2:12; 1 Thes.2:12; Ebr.12:28; Ufu.1:9.
      (2) Maana ya pili neno "falme" limetumika likilenga kanisa la Bwana baada ya siku ya hukumu.
         (a) 1 Kor.15:23,24.
         (b) Ni kwa maana hiyo ufalme (kanisa) ambao wataingia watu baada ya dhiki nyingi kwa njia maisha ya upendo na juhudi ya kumtumikia Bwana.
         (c) Linga. 2 Pet.1:8-12.
5. Katika mst.23 tunajifunza Paulo na Barnaba waliwachagua wazee katika kila kanisa.
6. Angalia ni uwingi (k.m., zaidi ya mtu mmoja) wa wazee walichaguliwa katika kila kanisa.
   a. Ukweli huo ni dhahiri katika fungu kama vile Flp.1:1 na 1 Pet.5:1, ambapo uwingi wa wazee umebainishwa.
   b. Basi, mfumo wa madhehebu wa kuwa na mtu mmoja akitawala juu ya kusanyiko ama makusanyiko kadhaa ni wazi kwamba si la kimaandiko na, kwa hiyo ni dhambi mbele za Mungu!
   c. Kwa maelezo ya nyongeza kuhusu wazee tafadhali chunguza kozi zingine za "World Bible School" katika Mambo ya Msingi (Fundamentals of the Faith), na kanisa la Agano Jipya.
7. Baada ya kuwachagua wazee Paulo na Barnaba walisafiri kuelekea jimbo la Pamfilia.
8. Katika mji huo walihubiri neno katika miji ya Perga na Atalia.

### f. (14:26-28) PAULO NA BARNABA WATOA TAARIFA ANTIOKIA

1. Kumbuka kwamba kanisa la Antiokia liliwatuma Paulo na Barnaba katika safari za umisionari (linga. 13:2,3).
2. Sasa walirejea kutoa taarifa kwa ndugu zao Antiokia.
3. Mambo mawili ya kuangalia hapa kuhusu taarifa yao kwa ndugu.
   a. Walimtukuza Mungu kwa mambo yaliyotendeka ("mambo yote aliyofanya Mungu").

   b. Walitambua kuwa kupitia juhudi yao, Mungu alifungua mlango mkubwa wa imani kwa Mataifa.
4. Baada ya taarifa yao Paulo na Barnaba walikaa pamoja na ndugu zao hapo Antiokia kwa muda mrefu.
5. Mtazamo kwa ufupi wa 13 na 14, Safari ya kwanza ya umisionari.
   1. 13:1-3 Kuitwa kwa Barnaba na Sauli.
   2. 13:4-14:28 Safari ya kwanza ya umisionari.
      a. 13:4-13 Katika Kipro
         (1) 13:4,5 Mahubiri katika sinagogi/Yohana Marko aliwasaidia
         (2) 13:6-8 Elima (Bar-Yesu) anashindana na Sauli na Barnaba.
         (3) 13:9-12 Sauli (Paulo) ampiga upofu Elima/Sergio Paulo aamini.
         (4) 13:13 Paulo aenda Perga/Yohana Marko arejea Yerusalem.
      b. 13:14-50 Antiokia
      c. 13:51-14:5 Ikonio.
         (1) 13:51-14:1 Kuzungumza katika sinagogi.
         (2) 14:2-5 Kuzungumza kwa ujasiri katika Bwana, bila kujali upinzani.
      d. 14:6-20 Listra.
         (1) 14:6,7 Paulo na Barnaba waondoka Ikonio na kwenda Listra na Derbe.
         (2) 14:8-10 Paulo amponya kiwete.
         (3) 14:11-13 Watu wadhani Paulo na Barnaba ni miungu.
         (4) 14:14-18 Paulo na Barnaba wawazuia watu.
         (5) 14:19,20 Paulo apigwa mawe.
      e. 14:21-25 Wahubiri wakati wakurejea safari.
      f. 14:26-28 Paulo na Barnaba watoa taarifa kwa ndugu Antiokia.
6. Mtazao kwa ufupi wa 15-18:22, Safari ya pili ya umisionari.
   a. 15:1-35 Mkutano Yerusalem.
   b. 15:36-18:22 Safari ya pili ya umisionari.
      (1) 15:36-38 Ungomvi juu ya Yohana Marko.
      (2) 15:39-41 Paulo/Sila na Barnaba/Yohana Marko wanatengana.
      (3) 16:1-5 Derbe/Listra – Timotheo atahiriwa.
      (4) 16:6-10 Katika Troa – Wito Makedonia.
      (5) 16:11-40 Katika Filipi.
      (6) 17:1-9 Katika Thesalonike.
      (7) 17:10-15 Katika Beroya.
      (8) 17:16-34 Katika Athene.
      (9) 18:1-17 Katika Korintho.
      (10) 18:18-20 Paulo arejea Antiokia.

**B. (15:18-22) SAFARI YA PILI YA UMISIONARI (PAULO NA SILA)**

**1. (15:1-35) MKUTANO YERUSALEM**

**a. (15:1-5) PAULO NA BARNABA WACHUKUA TOHARA / SHERIA YA MUSA / SWALI LA WOKOVU YERUSALEM**

1. Katika mistari hii tatizo kubwa liliibuka ndani ya kanisa.
2. Watu kadhaa waliotoka Uyahudi walifika Antiokia na kuleta shida miongoni mwa Wakristo.
3. Haswa, walikuwa wakifundisha ni lazima kwa Wakristo wenye asili ya Mataifa kutahiriwa kulingana na Sheria ya Musa.
4. Walifundisha hivyo kwamba ni lazima kwao kufanya hivyo ili wapate kuokolewa!
5. Zaidi sana, tutajifunza katika mst.5, na 24 walimu hawa wa uongo pia walifundisha ni lazima kwa Wakristo hawa kushita Sheria ya Musa!
6. Katika mst.2 Paulo na Barnaba walikabiliana na walimu hawa wa uongo na uamuzi ulifanywa kwenda Yerusalem kujadili jambo hilo pamoja na mitume na wazee.

7. Wakiwa njiani kwenda Yerusalem, Paulo na Barnaba walitoa taarifa za uongofu wa Mataifa.
   a. Taarifa hii ya wokovu za roho zenye thamani zilileta furaha mioyoni mwa watu waliosikia!
8. Kuwasiri kwao Yerusalem, Paulo na Barnaba walipokelewa vyema na kanisa, ikiwa ni pamoja na mitume na wazee.
9. Walakini, baadhi ya Wakristo ambao walitoka madhehebu ya Mafarisayo kabla ya kuongolewa kwao ("Mafarisayo wenye kuamini") walisema kwamba ni lazima kwa hao Wakristo wa Mataifa kufanya vitu viwili:
   a. Kutahiriwa, na
   b. Kushika Sheria ya Musa.
10. Hakika, upinzani huu kwa watu ambao walitokea madhehebu ya Mafarisayo kabla waliahirisha mkutano huo wakati mwingine.
11. Kufuatana na haya, Mungu, kupitia Paulo, alifunua maelezo ya nyongeza katika tukio hili katika Gal.2:1-10.
12. Katika fungu hili, maelezo yafuatayo yenye kufurahisha yanabainisha mambo yaliyotokea.
    a. 2:4 Paulo alisema kwa uvuvio kwamba hao waliokuwa wakifundisha hitaji la kutahiri na kushika Sheria ya Musa walikuwa "ndugu za uongo."
       (1) Waliingia kanisani kwa njia ya udanganyifu.
       (2) Walifanya hivyo kama wapelelezi wakichunguza uhuru walionao Wakristo.
       (3) Na walifanya hivyo kwa kuuleta Ukristo katika "utumwa", k.m.., kurejea katika utumwa wa Sheria ya kale ya Musa (linga. Gal.5:1-4).
    b. 2:2 Paulo na Barnaba walikwenda Yerusalem kwa sababu ya ufunuo toka kwa Mungu.
    c. 2:1 Walimchukua Tito pamoja nao.
    d. 2:2,9 Hakika baada ya mkutano wa kwanza wa kanisa, Paulo na Barnaba walikutana kwa siri na Yakobo, Petro na Yohana, ambao walikuwa viongozi miongoni mwa mitume.
    e. 2:6-9 Baada ya majadiliano yao ya siri, Yakobo, Petro na Yohana waliwapa mkono wa shirika Paulo na Barnaba (k.m. walikubali mafundisho na kazi yao).

**b. (15:6-11) PETRO ANAZUNGUMZA**

1. Baada ya kikao chao cha siri, mitume na wazee walikusanyika pamoja kujadili mambo haya muhimu sana.
2. Baada ya mabishano makubwa, Petro aliinuka kuzungumza na kanisa.
3. Petro alibainisha mambo yafuatayo:
   a. Mst.7 Mungu alimchagua Petro kunena injili kwa Mataifa ili wapate kuamini. (Angalia kwamba imani ya Mataifa jinsi ilivyowafikia):
      (1) Wala si kwa njia ya kimiujiza Roho Mtakatifu akifanya kazi mioyoni mwao!
      (2) Bali kwa njia ya kusikia neno la injili iliyohubiriwa na Petro (linga. Rum. 10:17)!
   b. Mst.8 Mungu alionyesha kuwa Mataifa walipaswa kupokea injili wakati Roho Mtakatifu atakaposhuka juu yao kama vile alivyoshukia juu ya mitume (linga.11:17,18).
   c. Mst.9 Wala hakufanya tofauti kati ya wenye asili ya Kiyahudi na wale wenye asili ya Mataifa.
   d. Mst.9 Hakufanya tofauti kwa kuruhusu mioyo ya makundi yote kutakaswa kwa imani (linga. 1 Pet.1:22).
      (1) Tafadhali angalia mioyo yao haikutakaswa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, bali kwa imani iliyohai, yenye utii, yenye matunda.
   e. Mst.10 Kwa nini basi mnawatwisha mizigo ("kongwa juu ya shingo") juu ya Wakristo Mataifa (k.m., kongwa la kutaka kushika Sheria ya Musa kikamilifu).
      (1) Petro alibainisha kuwa hata baba zao wenye asili ya Kiyahudi, wala kizazi chake hawakuweza kuubeba mzingo huo.
      (2) Zaida sana, alisema ikiwa walilazimisha mzingo huo katika Mataifa wakati Mungu hakufanya hivyo, "walimjaribu" Mungu, ndiyo kusema, wangemkasirisha Mungu.

f. Mst.11 Alihatimisha kwa hao wenye asili ya Kiyahudi na wale wa Mataifa wangeokolewa kwa njia ya neema ya Yesu Kristo (linga. Efe.2:2-10).
   (1) Wala si kwa kushika Sheria ya Musa!

### c. (15:12) PAULO NA BARNABA WANANENA

1. Makutano wakawasikiliza Paulo na Barnaba wakielezea jinsi Mungu alivyowaruhusu watende miujiza mingi kati ya Mataifa.
2. Kama tulivyojifunza, jambo hilo ilikuwa kuthibitisha kwamba walikuwa wakinena kwa mamlaka ya Mungu (linga. Mk.16:20).

### d. (15:13,14) YAKOBO AKUBALIANA NA PETRO

1. Kwa wasikilizaji hao wenye asili ya Kiyahudi, kusingelikuwa na uthibitisho bora zaidi kuliko maelezo ya Yakobo mst.13,14 kuliko ule wa kutoka maadiko ya Agano la Kale.
2. Na hilo ndilo alilofanya Yakobo. Alinukuu kutoka Amosi 9:11,12!
3. Pia, Yakobo alisema manabii walitabiri hayo aliyosema Petro, k.m., kwamba Mungu angewaleta Mataifa katika familia yake ya kiroho.
4. Kubainisha zaidi, katika unabii wa Agano la Kale, Mungu alitabiri wakati angeiinua tena magofu ya maskani ya hekalu la Daudi.
   a. Hilo lingefanyika ili wanadamu wote, k.m., Mataifa waweze kumtafuta Bwana.
   b. Hilo lingefanyika kwa kila mtu wa Mataifa ambayo yangeitwa kwa jina la Mungu.
   c. Na ni Mungu aliyetabiri mambo haya ya ajabu, wala si wanadamu ("asema Bwana")!
5. Sasa, Yakobo alikuwa akisema kwa uvuvio kwamba unabii wa Amosi ulitimia wakati Petro alipokwenda kuhubiri injili kwa Mataifa ili waweze kuamini na kufanyika watoto wa Mungu!
6. Kwa mara nyingine tena, tunakuomba uangalie jinsi ilivyosahihi na bayana alivyotimiza unabii huu katika Mwanawe Yesu Kristo, na katika kanisa lake!
   a. 13:23,24 Yesu alitoka katika ukoo wa Daudi, ambaye Mungu aliahidi kumwinua Mwokozi kutoka katika yeye.
   b. 2:30-36 Yesu ndiye Masihi, Mwokozi ambaye Baba:
      (1) Alimfufua kutoka kwa wafu, kama ilivyotabiriwa kupitia Daudi.
      (2) Alimwinua kuketi mkono wake wa kuume, kama alivyotabiriwa na Daudi.
      (3) Aliketishwa katika kiti cha enzi cha Daudi mbinguni kutawala kama mfalme katika ufalme wake, kanisa.
      (4) Alimfanya kuwa Bwana na Kristo.
   c. 10:1-4 Kornelio alikuwa mtu aliyemcha Mungu Mmataifa ambaye kwa hakika alimtafuta Bwana, lakini alihitaji kusikia maneno kutoka kwa Mungu ili amuriwe mambo ya kufanya ili aokolewe.
   d. 10:9-16 Mungu alimwonyesha Petro maono kumfundisha kwamba Mataifa wangepokea ujumbe wa wokovu.
   e. 10:44-46 Mungu alimwaga Roho Mtakatifu juu ya mataifa kama alivyofanya kwa Wayahudi, kama ishara kwamba waliwataka wapokee ujumbe wa wokovu.
   f. 10:47,48 Baada ya hapo, Petro aliamuru Kornelio na nyumba yake kubatizwa ili kupata msamaha wa dhambi.
   g. 11:17,18 Basi, Mataifa waliruhusiwa kutubu na kupata maisha mapya ya kiroho.
   h. Ru.6:3,4; Gal.3:26,27 Hakika, walibatizwa ili kuenenda katika upya wa uzima, kama watoto wa Mungu, washiriki wa familia ya kiroho!
   i. 11:26 Kama matokeo, wanafunzi hao wa Mataifa waliitwa kwa jina la Mungu, Wakristo, kwanza katika Antiokia!
   j. Efe.2:11-22 Hakika, hao wenye asili ya Mataifa walifanywa kuwa pamoja na hao wenye asili ya Kiyahudi kwa njia ya damu ya msalaba wa Yesu!

(1) Jambo hilo limetendeka katika mwili mmoja, kanisa la Bwana wetu Yesu Kristo!
k. 1 Kor.3:16,17 Hilo ndilo hekalu la Mungu!
7. Ukiwa na maandiko haya akilini mwako, hakuna shaka kabisa kwamba unabii wa Amosi ulitimia karne ya kwanza katika Yesu na katika bibi-arusi yake wa thamani, kanisa1
a. Ni jambo la ajabu, lenye kuleta imani, nguvu za kuimarisha roho ndani ya neno lake!

### f. (15:18-21) YAKOBO ATOA HATIMISHO

1. Katika mst.18 Yakobo alibainisha kwamba tangu milele Mungu alijua kila kitu kwamba angefanya (hata mambo makubwa kama vile Amosi 9:11,12)!
   a. Maana yake kwa kusema hivyo ni kuonyesha kwamba yaliyokuwa yakitendeka ya Mungu kuwakubali Mataifa halikuwa jambo la bahati nasibu!
   b. Badala yake, lilikusudiwa na Mungu mwenyezi na lisingefanikiwa kukataliwa au kupingwa na mwanadamu mnyonge!
2. Hatimisho la Yakobo juu ya Mataifa waliokuwa wakimgeukia Mungu ilikuwa wasisumbuliwe isipokuwa kuwaambia wajiepushe na mambo manne yafuatayo:
   a. Uchafu wa sanamu, k.m., vitu vilivyoambatana na ibada ya sanamu, kama vile aina mbalimbali za nyama.
      (1) Paulo alieleza bayana kuwa si dhambi kula nyama iliyotolewa kwa sanamu (1 Kor.8).
      (2) Walakini, baadhi ya Wakristo wenye asili ya Kiyahudi walidhania kuwa ni dhambi kula nyama kama hiyo (1 Kor.8:7).
      (3) Basi, hili lilikuwa kizuizi kikihatarisha ushirika baina ya makundi haya mawili kipindi hiki cha uchanga wa kanisa.
      (4) Kwa hiyo, swala la Kristo ilikuwa kujizua kula nyama iwapo ingelimkwanza ndugu (1 Kor.8:9-13).
      (5) Basi, Yakobo alisema kwamba upendo wa Mkristo upande wa Mataifa waliongolewa ungehamasisha kujizuia katika vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu.
      (6) Hakika, lilikuwa jambo la "muhimu" kufanya hivyo (mst.28).
   b. Jambo la pili ambalo walipaswa kujizuia ilikuwa kufanya uasherati.
   c. Jambo la tatu lilikuwa kula vitu vilivyosongolewa ( kwa sababu damu haikutoka katika mnyama).
   d. Na la nne ilikuwa kula damu.
3. Kusema ukweli, vitu vingine vilikatazwa na Mungu, bila kujali mtu ni Mataifa au mweye asili ya Kiyahudi.
4. Jambo hili ni kweli kwa kuwa dhambi imebainishwa na Mungu kama uasi wa sheria yake, wala si tu vitu hivyo vinne (1 Yoh.3:4)!
5. Basi kwa nini vitu hizi vinne vilitajwa na Yakobo?
6. Inaonekana vilitajwa hivi vinne kwa sababu ndizo dhambi ambazo ilikuwa kawaida kati ya Mataifa.
   a. Hakika, vitu hivyo ni vitu ambavyo Mataifa hawakufikiri kuwa ni dhambi, basi, maelezo haya ya kubainisha yalihitajika.
7. Kwa nyongeza, vilikuwa ni vizuizi vikubwa sana kwa umoja wa Wakristo wenye asili ya Kiyahudi na Mataifa.
8. Pia, kutokana na mst.21, vitu hivyo ni kati ya vitu ambavyo watu wenye asili ya Kiyahudi walisikia kila sabato.
9. Hata hivyo, vitu hivyo havikukatazwa tu na Sheria ya Musa.
   a. Kwa mfano, hata Nuhu alieleza dhambi ya kula damu na kwamba ilikuwa kabla ya Mungu kutoa Sheria kupitia Musa (Mwa.9:3,4).
   b. Pia, kabla ya Sheria ya Musa kutolewa, Mungu alianzisha sheria ya ndoa kuwa mahali pekee mtu anaweza kufanya tendo la ndoa ni kati ya mume na mke, ni hivyo kufanya uasherati kuwa dhambi (Mwa.2).

10. Mwisho, tunapaswa kujadili jambo moja la mwisho juu ya makatazo hayo manne na kutambua kama makatazo hayo tunaweza kuyatumia siku hizi.
11. Ebu na tuangalia makatazo hayo yote manne:
    a. Kwanza, unajisi wa sanamu.
        (1) Hapana shaka kwamba Mungu amekataza aina zote za sanamu (linga.Gal.5:20).
        (2) Walakini, kula nyama iliyotolewa kwa sanamu inakubaliwa kuliwa kama haiharibu dhamiri ya ndugu mpendwa katika Kristo n(angalia maelezo yetu ya awali katika 1 Kor.8).
    b. Pili, kula damu.
        (1) Kama tulivyobainisha hapo awali, katazo hili liliamuriwa na Mungu tangu mwanzo, hata kabla ya Sheria ya Musa (linga. Mwa.9:3,4).
        (2) Basi, ni dhahiri hii ni moja ya kanuni za milele, kama vile kukatazwa kuua, kama Mungu alivyokataza daima (Mwa.4:8-15).
        (3) Kwa nyongeza, hakuna katika Agano Jipya panapoondoa amri hii iliyoamuriwa katika mistari hii.
        (4) Hivyo basi, tunahatimisha kuwa makatazo ya Mungu juu ya kula vitu vilivyosongolewa na damu bado yanafanya kazi leo!

### g. (15:22-29) PAULO, BARNABA, YUDA, NA SILA WATUMWA KWENDA KWA WAKRISTO MATAIFA WAKIWA NA BARUA

1. Mitume, wazee, na kanisa zima liliamua kuwatuma watu wawili, Yuda na Sila pamoja na Paulo na Barnaba.
2. Kusudi lilikuwa kupeleka barua kwa Wakristo wa Mataifa Antiokia, Shamu, na Kilikia.
3. Katika barua hiyo walieleza mambo makubwa yafuatayo:
    a. Walisikia kwa hao walifika huko kutoka Yerusalem na kusumbua roho za hao Wakristo Mataifa kwa kusema wanapaswa kutahiriwa na kushika Sheria ya Musa.
    b. Mitume hawatoa agizo lolote kwa watu hao kufundisha mambo haya.
    c. Waliwasifia Paulo na Barnaba kama wapendwa wao, na ambao walihatarisha maisha yao kwa ajili ya Yesu.
    d. Walisema Yuda na Sila walitumwa ili wanene binafsi kuthibitisha mambo ambayo aliandikwa katika waraka huu.
    e. Ni maoni ya pamoja ya mitume, wazee, kanisa, na Roho Mtakatifu ili makatazo yakutiliwa mkazo ni manne tu.
    f. Tafadhali angalia, kutaja kwao Roho Mtakatifu, mitume na wazee walikuwa wakisema kwa uvuvio wa Mungu!

### h. (15:30-35) WANALITAARIFU KANISA LA ANTIOKIA

1. Barua iliposomwa kwa Wakristo Mataifa katika Antiokia, iliwafurahisha na kuwatia moyo!
2. Kwa nyongeza, Yuda na Sila waliwahamasisha na kuwatia nguvu ndugu wa Antiokia.
3. Yuda akarejea kwa mitume, akiwapelekea salaam kutoka kwa ndugu wa Antiokia.
4. Walakini, Sila alibaki pamoja na Paulo na Barnaba kufundisha na kuhubiri neno la Mungu, pamoja na wengine wengi.
5. Kabla hatujaendelea kujifunza zaidi safari ya pili ya umisionari, tunapenda kwa mhutasari kujadili baadhi ya watu katika ulimwengu wa dini walivyoharibu mkutano huu katika Yerusalem.
6. Watu wengi katika dini huendea sura hii na mkutano wa Yerusalem kutaka mamlaka ya kuanzisha makao makuu, bodi ya wakuu wa dini ambao wana mamlaka juu ya makusanyiko yote ya madhehebu hayo.
    a. Mifano watahusisha taasisi hizo kama baraza, sinodi, mkutano, n.k.

7. Hata hivyo, taasisi kama hizo kuwa juu ya kusanyiko la mahali pamoja hazijaruhusiwa katika sura hii, ama mahali pengine popote katika Agano Jipya!
8. Tafadhali angalia sababu zifuatazo kwa nini maelezo hayo ni sahihi:
   a. Kwanza, swala hili lilikuwa ni maombi ya kusanyiko moja kwa viongozi wa kanisa lingine juu ya swali au mabishano.
      (1) Basi, jambo hili siyo mkutano wa "maaskofu" au wajumbe toka sehemu zote, au makusanyiko mengi katika eneo hilo, kama inavyofanyika katika ulimwengu wa dini leo.
      (2) Kwa nyongeza, hapakuwa na uchaguzi au wawakilishi au kupiga kura juu ya swali lililojadiliwa, kama inavyofanyika leo!
   b. Pili, hili lilikuwa ombi kwa watu waliovuviwa, wala si kwa watu wasiovuviwa kama inavyoonekana katika vikundi vya dini vyenye makao makuu leo.
      (1) Lk.22:30 Kristo aliwapa mamlaka mitume kuketi katika viti vya enzi wakitawala Israeli ya kiroho, kanisa.
      (2) Yoh.14-16 Aliwaahidi na kuwapatia Roho Mtakatifu kwa kipimo cha miujiza kuwaongoza katika neno la Mungu lote.
      (3) 2 Pet.1:21 Walinena kama walivyoongozwa na Roho Mtakatifu.
      (4) Mdo.15:28 Walitaja wakibainisha uongozi wa Roho Mtakatifu katika kuamua na kutangaza maamuzi yao katika waraka.
   c. Kama tulivyoona katika somo letu awali, hakuna mtu anayeishi leo mwenye uwezo wa kimiujiza kutoka kwa Mungu.
   d. Kinyume chake, kupitia mitume na watu wengine waliovuviwa, aliandika maongozi yake na hekima katika Agano Jipya la Mwanawe mpendwa Yesu Kristo.
   e. Hicho ndicho kiini cha Mungu ambacho tunakitumia siku hizi kutatua matatizo na kujibu maswali yote!
   f. Na hakuna mahali katika kiini hicho cha Mungu tunaona mamlaka kwa kikundi fulani kuwa juu ya kusanyiko la mahali pamoja!
   g. Basi, mabaraza, sinodi, mikutano, mitaguso, vyuo vya makardinali, na vikundi vingine vyovyote vinavyolingana na hivyo kutawala juu ya kusanyiko la mahali pamoja ni dhambi ya kuongeza katika neno la Mungu!

## 2. (15:36-18:22) SAFARI YA PILI YA UMISIONARI

### a. (15:36-38) MABISHANO JUU YA YOHANA MARKO

1. Paulo alitoa maoni kwa Barnaba kwamba wangewatembelea ndugu zao wapendwa ambao waliongolewa katika safari ya kwanza ya umisionari kuona walikuwa wakiendelea vipi.
   a. Kwa njia ya kutendea kazi haya, inatuonyesha umuhimu wa kuwapenda na kudumu kufanya kazi pamoja na Wakristo wapya baada ya kuongolewa kwao.
   b. Linga. 28:20.
2. Barnaba akaazimu kumchukua Marko pamoja naye kama walivyofanya katika safari yao ya kwanza.
   a. Tafadhali kumbuka kilichotokea safarini, Yohana Marko aliwaacha Paulo na Barnaba Perge na kurejea Yerusalem (linga.13:13).
3. Paulo aliazimia kutomchukua Yohana Marko kwa sababu aliwaacha awali na hakwenda kufanya kazi pamoja nao.

### b. (15:39-41) PAULO/SILA NA BARNABA/MARKO WANATENGANA

1. Kutoelewana kwa Paulo na Barnaba ilikuwa jambo kubwa hata wakaamua kutengana na kuelekea njia tofauti tofauri.
   a. Barnaba alimchukua Yohana Marko na wakatweka kwenda Kipro.
   b. Na Paulo akamchagua Sila.

(1) Utakumbuka kwamba Sila alitumwa na mitume hapo nyuma kwenda Antiokia kupeleka waraka kwa Wakristo wa Mataifa pamoja na Paulo, Barnaba, na Uyahudi (linga. mst.22,32,34).

c. Paulo na Sila wakaelekea maeneo ya Shamu na Kilikia na kuyaimarisha makanisa.

2. Kuna mambo kadhaa muhimu ambayo tunapaswa kuyatilia mkazo katika somo letu ya tukio hili lenye kufurahisha katika historia ya kanisa.
   a. Kwanza, ni muhimu kutambua kwamba Paulo na Barnaba hawakutofautiana katika maswala ya mafundisho.
      (1) Kinyume chake, hawakukubaliana katika maswala ya maamuzi au maoni, k.m., ama kumchukua Marko pamoja nao.
      (2) Jambo hili ni muhimu sana kutambua kwa sababu ndugu wanaposhindwa kukubaliana katika maswala ya mafundisho na hao waliokosea kukataa kutubu baada ya uvumilivu mwingi juu yao, Bwana anaamuru hatua maalum ya kuchukua (linga. Rum.16:17,18; 2 Yoh.9-11; Tit.3:10,11; 1 Tim.6:3-5).
   b. Pili, ikiwa ndugu wa upendo wa dhati kwa Bwana, kazi yake, na roho zilizopotea, ni jambo linalowezekana kufikia hatua ya kutokukubaliana juu ya maswala ya maamuzi na maoni.
      (1) Kwa mfano, katika swala hili, watu wanne walitengana wakaenda njia mbili wakieneza injili.
      (2) Hakika, wangewafikia watu wengi zaidi kwa jinsi hii kuliko watu watatu kwenda njia moja.
   c. Tatu, hata ingawa hawakuelewana katika maswala ya maamuzi, ndugu wanapaswa kupendana na kutaka kufanya kazi pamoja kwa ajili ya Bwana siku zilizofuata.
      (1) Katika swala hili, Paulo baadaye alimtaja Barnaba katika hali ya kumkubali (1 Kor.9:6).
      (2) Na alifanya vivyo hivyo kwa kumtaja Yohana Marko kama mtenda kazi pamoja naye, mfariji wa Paulo, na anayefaa kwa utumishi (Kol.4:10,11; 2 Tim.4:11; Flm.24).

### c. (16:1-5) KATIKA DERBE / LISTRA – TIMOTHEO ATAHIRIWA

1. Paulo na Sila wakaenda tena katika mji wa Derbe, kisha Listra ambako Paulo na Barnaba walihubiri katika safari ya kwanza.
2. Katika Listra walimkuta kijana Mkristo aliyeitwa Timotheo.
3. Ni dhahiri kwamba Paulo alimfundisha Timotheo injili katika safari yake ya kwanza eneo hilo na kwamba Timotheo alitii injili (linga. 1 Tim.1:2).
4. Luka anatupatia ukweli ufuatao juu ya Timotheo katika mistari hii.
   a. Alikuwa "mwanafunzi", Mkristo, mwana wa Mungu.
   b. Mama yake alikuwa Myahudi kwa asili ("mwanamke Myahudi aliyeamini").
   c. Baba yake alikuwa Mmataifa ("Myunani").
   d. Timotheo alishuhudiwa mambo mema kati ya ndugu eneo hilo ("alishuhudiwa vema").
   e. Paulo alitaka kumchukua Timotheo pamoja naye safarini.
   f. Paulo alimtahiri.
   g. Alifanya hivyo kwa ajili ya Wayahudi walikuwepo eneo hilo.
5. Wengine wanadhani kwamba Paulo hakufanya vyema jinsi alivyowatendea Timotheo na Tito kwa swala la tohara.
   a. Paulo na Barnaba walimchukua Tito kwenda Yerusalem katika mkutano, hakika kabisa Paulo alikataa kumshurutisha Tito kutahiriwa (linga. Gal.2:1-5).
   b. Walakini, katika swala hili, Paulo binafsi alimtahiri Timotheo.
6. Ukweli ni kwamba, hakuyumba kabisa kwa namna alivyomtenda Tito na Timotheo juu la swala la tohara.
   a. Paulo alipompeleka Tito Yerusalem, wengine walidai Wakristo wa Mataifa lazima kutahiriwa ili wapate kuokoka (15:1)!

        (1) Paulo na Barnaba hawakukubalina kabisa na swala hili hata wakalileta swala hili kwa ndugu Yerusalem.
        (2) Kama Paulo angekuwa alimlazimisha Tito kutahiriwa, angekuwa anapinga jambo ambalo yeye na Barnaba walilolipinga kuwa ni mafundisho ya uongo.
        (3) Kwa maneno mengine, Paulo angekuwa kwa njia fulani anakubaliana na waalimu wa uongo kwa ni lazima kutahiriwa ili kupata wokovu.
        (4) Hiyo ndiyo sababu Paulo hakumshurutisha Tito kutahiriwa.
    b. Kwa upande mwingine, swala la Timotheo lilikuwa tofauti sana.
        (1) Kama tulivyoona, Paulo alimtaka Timotheo aende naye kuhubiri injili.
        (2) Lakini, Paulo alitambua kwamba kwa kuwa mama yake Timotheo alikwa kwa asili ni Myahudi na baba yake Mmataifa, ingelikuwa ni kikwazo kwa watu walio Wayahudi kwa asili iwapo Timotheo asingetahiriwa.
        (3) Ukiwa na hilo katika akili, Paulo akamtahiri Timotheo ili kwamba asiwe kikwazo.
        (4) Basi, Timotheo alitahiriwa kuondoa kikwazo ambacho kingekuwa kuwa kizuizi kwa mafanikio ya mahubiri yake ya injili, wala si alitakiwa kufanya hivyo ili apate kuokoka!
    c. Ukiwa na ukweli huo akilini mwako, tunaweza kuona bayana Paulo hakuyumba kwa jinsi alivyomtendea Tito na Timotheo juu ya swala la tohara!

### d. (16:6-10) KATIKA TROA - MAKEDONIA

1. Paulo na Sila baada ya kuhubiri katika maeneo ya Frigia na Galatia, Roho Mtakatifu akawakataza wasihubiri tena katika Asia.
2. Hivyo wakasafiri kwenda katika jimbo la Misia na wakajaribu kuingia katika Bithinia, lakini Roho Mtakatifu hakuwapa ruhusa waende.
3. Kwa hiyo, wakafika Troa, ambapo Paulo alipokea maono usiku.
4. Katika maono, mtu wa Makedonia alimsihi Paulo kuvuka kwenda Makedonia kuwasaida watu katika maeneo hayo.
5. Paulo na wale alioambatana nao walifikia uamuzi kutokana na maono hayo Bwana aliwaita kuhubiri injili katika kwa watu wa Makedonia.
6. Tafadhali angalia katika mst.10 Luka alisema, “tukataka kutoka kwenda Makedonia …”
    a. Kama tulivyoona katika somo letu katika utangulizi, hili ni dhahiri kwamba Luka alijiunga na Paulo na kundi lake hapa Troa.

### e. (16:11-40) KATIKA FILIPI
#### (1) (16:11-15) UONGOFU WA LIDIA

1. Wakang’oa nanga toka Troa, wakafika Samothrake, Neopoli, na kisha Filipi, ambao ulikuwa mji mkubwa eneo hilo la Makedonia.
2. Katika Filipi, walikwenda mahali palipotumika kwa ajili ya sala, na wakahubiri injili kwa baadhi ya wanawake walikutanika hapo.
3. Miongoni mwa wanawake hao alikuwa Lidia, aliyetajwa kama mcha Mungu.
    a. Basi, ni dhahiri Lidia alikuwa mtu aliyempenda Mungu akilini mwake.
4. Katika mst.14 tunajifunza Bwana akafungua moyo wa Lidia (k.m., akili zake) asikilize na kutii mambo ambayo Paulo alinena.
    a. Watu wengine katika ulimwengu wa dini wanatumia vibaya fungu hili kwa kusema Bwana alifungua akili za Lidia kwa namna fulani ya kimiujiza moja kwa moja, kisiri akifanya kazi kwa njia ya Roho Mtakatifu juu ya akili ya Lidia.
    b. Lakini, tumeona katika tayari katika masomo kadhaa yaliyopita Roho Mtakatifu hafanyi kazi moja kwa moja katika akili za watu, hata karne ya kwanza wakati miujiza ilitendeka.
    c. Kinyume chake, alifanya kazi katika akili za watu akitumia chombo chake, upanga wa Roho, neno la Mungu (linga. Efe.6:17 na somo letu katika 2:37).

d. Na hivyo ndivyo Bwana alifungua akili za Lidia katika tukio hili, alitumia neno lake, kama lilivyohubiriwa na mnenaji wake, Paulo!
e. Kuna njia mbili tunaweza kutambua kwamba Bwana alitumia neno lake kufungua akili za Lidia.
   (1) Kwanza, kutokana na mazingira ya fungu hili.
      (a) Mst.13 Lidia alizoelea kusali kwa Mungu, k.m., alikuwa mtu ambaye aliamua kuwa na moyo wa adili na mnyofu na alikuwa akimtafuta Bwana.
      (b) Mst.14 Alikuwa mtua alizoelea kumwabudu Mungu, k.m., alikuwa mtu wa dini na mnyenyekevu.
      (c) Mst.14 Paulo alinena mbele ya Lidia na wanawake wengine waliokutana pamoja kwa sala.
      (d) Mst.14 Lidia alisikia maneno yaliyosikiwa na Paulo.
      (e) Mst. 15 Baada ya kusikiliza maneno hayo, Lidia alizingatia na kutii, kwa kubatizwa.
      (f) Hivyo basi, kutokana na mazingira haya, tunahatimisha kuwa Bwana alifungua akili za Lidia kupitia neno la Mungu alilolinena Paulo!
   (2) Pili, kuzingatia mazingira ya mafungu mengine ya Biblia.
      (a) Zab.19:7,8.
      (b) Zab.119:104, 105
      (c) Zab.119:105
      (d) Kutoka mistari hii, tunaona Bwana akitumia upanga wa Roho, neno la Mungu:
         1. Kuongoa nafsi.
         2. Kuwafanya watu wasio elimika kuwa na ufahamu.
         3. Hutia nuru katika macho.
         4. Huwapatia ufahamu watu wake.
         5. Hufanya kazi kama taa na nuru inayomulika njia zetu za uzima.
         6. Kutia nuru na ufahamu na kutoa ufahamu kwa watu wake.
         7. Haya yanalingana na jinsi mambo yalivyotukia kwa Lidia siku hiyo!
            a. Kama alivyosikiliza maneno ya Mungu yenye nguvu, akili zake zikapata hekima, zilitiwa nuru, akapata kuelewa, na akaongolewa.
            b. Basi, imani ya kwamba Mungu alifungua akili za Lidia kupitia mahubiri ya neno lake, inalingana na mazingira ya fungu hili, kadhalika na Biblia nzima!

5. Katika mst.5 tunamwona Lidia na nyumba yake walitii injili kwa kubatizwa.
   a. Kwa roho hizo zilizotii injili, tunaona mwanzo wa kanisa hili katika Filipi.
   b. Wakristo hao walikuwa furaha ya Paulo daima (linga. kitabu cha Wafilipi).
6. Wengine katika dini wanadhani na kufundisha kwamba kwa kuwa Lidia na nyumba yake walibatizwa, basi lazima ni pamoja na watoto wachanga.
7. Kwa hiyo, wanahatimisha katika fungu hili, na mengine katika kitabu cha Matendo ambayo yametaja ubatizo pamoja na watu wa nyumbani, yana mamlaka ya kubatiza watoto wachanga.
8. Ukweli ni kwamba, wala si fungu hili ama mafungu mengine katika kitabu cha Matendo, au sehemu zilizobaki za Agano Jipya zinaamuru kubatiza watoto wachanga!
9. Ni kweli hilo kwa sababu watoto wachanga hawawajibiki katika ubatizo wa kimaandiko kwa sababu zifuatazo:
   a. Hakuna mfano hata mmoja wa ubatizo wa watoto wachanga katika Agano Jipya.
   b. Hakuna haja ya ubatizo wa watoto wachanga kwa sababu hawana hatia ya dhambi (Mt.18:1-13).
   c. Mtoto mchanga hawezi kutekeleza masharti ambayo ni lazima kutekelezwa kabla ya mtu hajatii ubatizo wa kimaandiko, k.m., kusikia, kuamini, kutubu, na kumkiri Kristo.

    d. Kwa maelezo ya nyongeza, tafadhali angalia notisi zetu katika 2:38, pamoja somo maalum katika ubatizo wa watoto wachanga.
10. Nyongeza katika ukweli huo wa kibibila, uchunguzi wa karibu wa mafungu hayo mbayo ubatizo pamoja na watu wa nyumbani ni msaada pia sana.
11. Tafadhali angalia maelezo yafuatayo ambayo yanaonyesha wazi kwamba watu wa nyumba nzima walipobatizwa, watoto hawakujumuishwa:
    a. Kornelio na nyumba yake (sura 10 na 11).
        (1) Kornelio na nyumba yake (sura 10 na 11).
        (2) 10:33.
        (3) 10:44.
        (4) 10:46.
        (5) 10:48.
        (6) Ni dhahiri basi, hao walikuwa nyumbani mwa Kornelio hawakuwa watoto wachanga, kwa sababu walifanya mambo hayo yote ambayo mtoto mchanga hawezi kufanya!
    b. Mlinzi wa gereza wa Filipi na nyumba yake (16:27-34).
        (1) 16:31.
        (2) 16:32.
        (3) 16:33.
        (4) 16:34.
        (5) Tena, ni dhahiri kabisa hao nyumbani kwa mlinzi wa gereza waliobtizwa hawakuwa watoto wachanga!
    c. Nyumbani kwa Stephana (1 Kor.16:16)..
        (1) 1 Kor.16:15 Hao wa nyumbani mwake walikuwa na umri wa kutosha, "wamejitia katika kazi ya kuwahudumia watakatifu"!
        (2) Mara nyingine, ni dhahiri kabisa hao waliokuwemo nyumbani mwa Stefana waliobatizwa hawakuwa watoto wachanga!
12. Ukiwa na maelezo ya kweli haya ya Biblia akilini, hakika hakuna shaka kwamba ubatizo uliohusisha nyumba nzima hauna maana watoto wachanga!

## (2) (16:16-18) PAULO AMTOA PEPO MSICHANA MTUMWA

1. Msichana huyu mtumwa mwenye pepo mchafu alikutana na Paulo na hao aliambatana nao.
2. Inadhihirika pia katika mazingira haya kwamba msichana huyu mtumwa aliwapatia faida nyingi mabwana zake kwa sababu ya kuagua kwake.
3. Msichana alimfuata Paulo na kundi lake kuzidi kusema kwamba walikuwa watumishi wa Mungu aliye juu wenye kuhubiri njia ya wokovu.
4. Paulo akasumbuliwa sana kwa jambo hili, akaamuru pepo mchafu amtoke kwa mamlaka ya Yesu Kristo, na pepo akamtoka.
5. Tukio linaonyesha dhahiri uweza wa mwenyezi Mungu juu ya Ibilisi na mapepo.
6. Lakini, kwa nini Paulo alimtoa pepo msichana huyo wakati alikuwa akisema ukweli kwamba Paulo na hao wengine walikuwa watumishi wa Mungu?
7. Kujibu swali hili, tafadhali chunguza ukweli ufuatao:
    a. Msichana huyu mtumwa na mabwana zake walikuwa wakidai uwezo wa kutabiri mambo yajayo (kuagua).
    b. Alikuwa na pepo mchafu.
    c. Basi, hata ingawa alikuwa akinena ukweli, Paulo hakutaka ukweli kutangazwa na kuhusishwa na huyo mtu mwenye pepo.
    d. Kama Paulo angeruhusu hili kuendelea, watu wangeshawishika kwamba kulikuwa na uhusiano kati ya watumishi wa Mungu na hao wa Shetani.
    e. Hili lingesababisha sifa njema ya Yesu na mitume wake kumwendea msichana mwenye pepo na bwana zake.
    f. Kwa nyongeza, ingepelekea sifa mbaya za mapepo kwenda kwa Yesu na mitume wake.

g. Hakika, hili lingeleta madhara makubwa katika kazi ya Bwana na ingesaidia kazi ya Shetani.
h. Ili kuzuia hali hiyo mbaya, Paulo alimtoa pepo kutoka kwa msichana mtumwa huyo ili kwamba ukweli usihubiriwe na pepo wachafu.

### (3) (16:19-24) BWANA ZAKE WAWAPIGA PAULO NA SILA NA KUWATIA GEREZANI KWA MASHITAKA YA UONGO

1. Bwana zake msichana huyo walipoona tumaini la faida yao limetoweka, waliwapeleka Paulo na Sila mbele ya wakuu wa mji wakiwashitaki kwa uongo.
2. Kama matokeo Paulo na Sila walipigwa kwa bakora na kutiwa gerezani chumba cha ndani (kwa usalama zaidi).
3. Kwa nyongeza mlinzi wa gereza alitii amri kwa kuwafunga miguu kwa mikatale.
4. Mambo yanapokuwa mabaya kama haya, tunapaswa kukumbuka (2 Tim.3:12).

### (4) (16:25-30) MLINZI WA GEREZA AULIZA, "YANIPASA KUFANYA NINI NIPATE KUOKOKA?"

1. Katikati ya hali hii mbaya sana, Paulo na Sila waliomba na kuimba nyimbo mbele za Mungu (linga. Flp.4:4)!
2. Angalia pia wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza (linga. Flp.2:15,16)!
3. Ghafula kukatukia tetemeko la ardhi, milango ikafunguka na vifungo vya wafungwa vikalegezwa.
4. Mlinzi wa gereza alipoamka na kuona milango imefunguka, alidhania kuwa wafungwa waliondoka na akataka kujiua.
5. Paulo akampazia sauti mlinzi wa gereza na akimshauri asijidhuru mwenyewe kwa kuwa wafungwa wote walikuwemo ndani.
6. Mlinzi wa gereza basi akauliza swali muhimu mno kwa vizazi vyote – "Bwana zangu, yanipasa nifanye nini ili nipate kuokoka?"
   a. Swali hili linabainisha mlinzi wa gereza aliamini kilichotokea na kwamba Paulo na Sila walikuwa watu wa Mungu.
   b. Pia tunaelezwa mlinzi wa gereza alitambua alihitaji kitu fulani kufanya ili aokoke kutoka katika dhambi!

### (5) (16:31-34) MLINZI WA GEREZA ALITII INJILI

1. Katika kujibu swali la mlinzi wa gereza, Paulo na Sila walimweleza kuwa amwamini Bwana Yesu na angeokoka.
   a. Kama tulivyoona katika masomo yetu kadhaa, hili swala halikuwa imani tu, au imani peke yake, imani iliyo hai, yenye matendo, na utiifu iliyotenda kazi kwa upendo (Yak.2:14-26; Gal.5:6)!
2. Hiyo siyo imani tu au imani peke yake inayookoa ambayo tumeona katika mst.32,33.
3. Katika mistari hiyo ukweli wa msingi kabisa umefunuliwa:
   a. Baada ya kumweleza mlinzi wa gereza hitaji la kuamini, Paulo na Sila walinena zaidi neno la Mungu mbela zake na nyumba yake.
   b. Kama matokeo ya mahubiri ya mitume, mlinzi wa gereza alifanya mambo mawili:
      (1) Akawaosha mapigo ambayo Paulo na Sila waliyapata.
         (a) Kwa kufanya hivyo, mlinzi wa gereza alikuwa akionyesha toba.
      (2) Alibatizwa pamoja na watu wa nyumbani mwake.
4. Swali muhimu ambalo tunapaswa kujiuliza na kujibiwa ni, "Ni wapi mlinzi wa gereza alijifunza juu ya hitaji la kubatizwa?"

5. Jibu ni dhahiri – alijifunza hitaji la kubatizwa kwa Paulo na Sila walipomweleza neno la Bwana!
6. Basi, katika kujibu swali la mlinzi wa gereza la mambo aliyopaswa kufanya ili aokoke, tunajua kwamba, ni dhahiri kabisa, Paulo na Sila walimweleza kuamini na kubatizwa!
7. Hili linalingana na ukweli tulioona kupitia somo letu hili lote la Matendo.
8. Ukweli huo kwamba imani na ubatizo ni kati ya mambo ambayo Mungu anataka mwanadamu afanye ili aokoke toka dhambini (linga. 2:38; 3:19; 8:35ff, 10:47,48).
9. Katika mst.34 tunaelezwa kwamba baada ya ubatizo wake, mlinzi wa gereza aliwalisha Paulo na Sila na akafurahi (hakika kwa sababu ya dhambi zake kutakaswa kupitia damu ya Kristo)!
10. Pia, ni muhimu kufahamu mwishoni mwa mst.34 kwamba nyumba ya mlinzi wa gereza pia ikamwamini Mungu.
    a. Kwa maneno mengine, watu wa nyumbani kwa mlinzi wa gereza haikubatizwa kwa sababu ya imani ya mlinzi katika Mungu.
    b. Kinyume chake, walibatizwa kwa sababu ya imani yao katika Mungu.

**(6) (16:35-40) PAULO NA SILA WALIACHIWA HURU TOKA GEREZANI**

1. Makadhi wa mji wakatuma ujumbe Paulo na Sila waachiwe huru.
2. Walakini, Paulo hakutaka aachiwe namna hiyo.
3. Kwa kufanya hivyo, alibainisha kama ifuatavyo:
    a. Watumishi walisababisha Paulo na Sila kupigwa hadharini (k.m., mbele ya umati mkubwa).
    b. Walifanya hivyo bila kujali ukweli kwamba Paulo na Sila walikuwa raia wa Rumi ambao hawakushitakiwa kihalali na hukuma.
    c. Waliwatia gerezani Paulo na Sila isivyo haki.
4. Nidhahiri Paulo alikuwa akitoa hoja hizi kuonyesha kwamba makadhi walifanya makosa makubwa kwa kuvuruga fursa yao ya kuwa raia wa Rumi.
5. Kwa msingi wa ukweli huo, Paulo alikataa kuachiwa huru kwa siri.
    a. Alikataa kwa sababu hilo lingewafanya watu kuamini kwamba Paulo na Sila walikuwa na hatia kama walivyoshutumiwa.
    b. Hilo lingeleta madhara makubwa kwa kazi yao ya kuhubiri injili.
6. Basi, Paulo alitaka moja kwa moja makadhi waje wenyewe na kuwatoa hadharani.
    a. Lingedhihirika hadharani kwa upande wa makadhi kwamba walifanya makosa.
    b. Ingekuwa pia dhahiri kwamba Paulo na Sila hawakuwa na hatia kwa mashitaka ya uongo waliyoshutumiwa.
7. Makadhi waliposikia Paulo na Sila walikuwa raia wa Rumi waliogopa sana, kwa sababu waligundua walifanya makosa!
8. Kama matokeo, makadhi waliwaachia huru Paulo na Sila na kuwaomba watoke katika mji.
9. Paulo na Sila wakaelekea nyumbani kwa Lidia, wakawaimarisha ndugu, na kuondoka Filipi.

**f. (17:1-9) KATIKA THESALONIKE**

**(1) (17:1-4) PAULO ALIMHUBIRI YESU KATIKA SINAGOGI**

1. Kutoka Filipi, Paulo na Sila wakapita Amfipoli na Apolonia na kisha Thesalonike, ambapo palikuwa na sinagogi.
2. Katika sinagogi hilo Paulo alijadiliana nao kutoka katika maandiko sabato tatu.
3. Katika mst.3 mafundisho ya Paulo yanafupishwa kwa kusema alidhihirisha mambo mawili muhimu:
    a. Ilimpasa Kristo kuteseka na kufufuka kutoka kwa wafu.
    b. Yesu huyo Paulo aliyemhubiri ndiye Kristo!
4. Matokeo ya mahubiri hayo ya mitume ilikuwa baadhi ya Wayahudi waliamini, na kadhalika makutano ya Mataifa wenye kumcha Mungu.

5. Basi, kanisa la Bwana likaanzishwa katika mji wa Thesalonike.
   a. Kama tunavyoona katika Nyaraka 1 na 2 Wathesalonike, hili kusanyiko likaeneza injili daima likawa pia kundi la Wakristo wenye juhudi katika kazi (linga. 1 Thes.1:2-10).

### (2) 17:5-9 (BAADHI YA WAYAHUDI WAKAFANYA GHASIA JUU YA WAKRISTO)

1. Baadhi ya Wayahudi wenye wivu wakaleta taabu, kama ifuatavyo:
   a. Wakakusanya baadhi ya watu waovu ili kupata kundi.
   b. Wakafanya ghasia katika mji.
   c. Wakaivamia nyumba ya mtu aliyeitwa Yasoni.
   d. Walijaribu kuwaleta Paulo na Sila katika mkutano.
2. Wayahudi waliposhindwa kumwona Paulo na Sila, waliwakokota Yasoni na baadhi ya ndugu wakawapeleka mbele ya wakuu wa mji.
3. Waliwashikati Wakristo kwa mambo mawili makubwa:
   a. "Walioupindua ulimwengu."
      (1) Hili ilikuwa namna ya kusema Wakristo walisababisha ghasia au matatizo kila mahali walipokwenda.
      (2) Kama tulivyoona, mashitaka hayo ni ya uongo, kwa sababu ni Wayahudi waliosababisha ghasia, na wala si Wakristo!
      (3) Wakristo walihubiri tu, wakafundisha, na kuishi maisha ya utukufu wa injili ya Kristo!
      (4) Je, si jambo la ajabu iwapo watu kwa uongo wanatushutumu kwa kuupindua ulimwengu kwa sababu tumekuwa waaminifu na juhudi ya kuhubiri, kufundisha, na kuishi maisha ya injili katika kila jamii zetu!
   b. Jambo la pili waliowashitaki ni kwamba Yesu alikuwa mfalme mwingine mbali na Kaisaria.
      (1) Hakuna shaka kwamba Paulo na wengine walifundisha kuwa Yesu ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana (linga. 1 Tim.6:15).
      (2) Walakini, kama Yesu mwenyewe, Paulo hakuwahi kudai kuwa Yesu alikuwa mfalme wa duniani akitafuta kutawala mahali pa Kaisari (linga. Yoh.18:36)!
      (3) Basi, Wayahudi hawa walikuwa wakigeuza mambo ya kweli kuwa kitu fulani ambacho ni uongo!
4. Katika mst.9 tunajifunza makadhi waliwatoza "dhamana" Yasoni na wenzake na kuwaachia huru.
   a. Ni dhahiri Yasoni alitoa kitu fulani cha dhamana, pengine fedha, kwamba Paulo na Sila wangeenenda sawasawa na sheria.

### f. (17:10-15) KATIKA BEROYA
### (1) (17:10-12) WABEROYE WAUGWANA WAAMINI

1. Ndugu wa Thesalonike wakawapeleka Paulo na Sila Beroya, ambapo waliingia katika sinagogi la Wayahudi na kuhubiri neno la Mungu.
2. Watu wa Beroya walitajwa kuwa wenye busara au waungwana kuliko wale wa Thesalonike kwa sababu mbili:
   a. Walilipokea neno la Mungu kwa uelekevu wote wa moyo, k.m.' walisikiliza kwa makini, kwa bidii, na kicho (linga. Zab.119:97)!
   b. Walichunguza maandiko kila siku ili kuona mambo hayo waliyosema kuwa yalikuwa kweli (linga. Yoh.5:39; 1 Yoh.4:1).
3. Ni tabia njema ajabu watu hawa walivyokuwa juu ya Bwana na neno lake la ajabu!
   a. Tunahitaji watu zaidi wa tabia kama hiyo siku hizi!
4. Kutokana na nia zao njema ajabu, watu wengi katika Beroya walimwamini Bwana!

### (2) (17:13-15) WAYAHUDI WA THESALONIKE WAKAFANYA GHASIA TENA

1. Kwa bahati mbaya, Wayahudi wenye wivu walitoka Thesalonike walikwenda Beroya kufanya ghasia pia.
2. Kama matokeo, ndugu walimchukua Paulo kwenda Athene, Sila na Timotheo wakabakia Beroya.
3. Paulo akawatuma hao waliompeleka Athene kwenda Beroya kuwaamuru Sila na Timotheo kufika haraka Athene.

### h. (17:16-34) KATIKA ATHENE

#### (1) (17:16-21) PAULO ATOA HOJA KTK SINAGOGI/ WANAFALSAFA WAONA SHAUKU KUHUSU MAFUNDISHO

1. Wakati Paulo aliwagonjea Sila na Timotheo wafike Athene, alikasirishwa na ibada za sanamu zilizoenea kwa sehemu kubwa katika mji huo.
2. Kama matokeo, alikwenda katika maeneo makubwa mawili kuhojiana na watu wa Athene.
   a. Sinagogi, kukabiliana na waabudu Wayahudi na Mataifa.
   b. Mahali pa soko, kukabiliana na hao waliotokea kuwa hapo.
   c. Kwa maneno mengine, Paulo alikwenda mahali ambapo alitambua kuwa kungekuwa na kundi kubwa la watu ambao wangelisikia injili.
3. Paulo alipofanya kazi kwa jinsi hii, Paulo alikabiliana na makundi ya wanafalsafa.
   a. Mwanafalsafa ni mtu anayejishughulisha kwa ujumla na sababu na kanuni za vitu.
   b. Kwa wakati huo, Athene ulikuwa mji mkuu wa falsafa za mwanadam.
   c. Kinyume kabisa na falsafa za kibinadamu hizi, Paulo alinena kwa uvuvio wa Mungu!
4. Katika mst.18 makundi mawili ya falsafa hizi za kibinadamu yametajwa:
   a. Waepikureo. Watu hawa waliamini mambo makuu yafuatayo:
      (1) Walimkana Mungu kuumba ulimwengu.
      (2) Walipinga majaliwa (providence) ya Mungu.
      (3) Walidai kwamba roho ni kitu (material) na inaangamia inapokufa.
      (4) Msemo (motto) wao ulikuwa, “Kula, kunywa, na ufurahi”.
   b. Kundi la pili la wanafalsafa hawa ilikuwa Wastoiko. Watu hawa waliamini katika mambo makubwa yafuatayo:
      (1) Kwamba dunia iliyokuwepo hii ndio Mungu.
      (2) Kwamba roho hufa.
      (3) Wema una malipo yake.
      (4) Mabaya yana adhabu yake.
      (5) Msemo (motto) wao ulikuwa, “Jikane mwenyewe.”
5. Baadhi ya wanafalsafa hawa walisema Paulo ni mtangaza habari za miungu migeni kwa sababu alimhubiri Yesu na ufufuo.
6. Walakini, kwa kuwa Wathene walipenda kusikia mambo mageni, walileta Paulo katika Areopago na kumwomba abainishe mafundisho yake.
7. Areopago ni kilima kilitazamana na Athene ambapo mashitaka yalifanyika na hotuba zilitolewa mara nyingi.

#### (2) (17:22-31) PAULO ALIMHUBIRI “MUNGU ASIYEJULIKANA”

##### (a) (17:22,23) PAULO ALIMTAMBULISHA MUNGU WA KWELI AMBAYE WALIMWABUDU BILA KUMJUA

1. Paulo alisema alitambua Wathene walikuwa watu wa dini sana kwa sababu kati ya vitu vingi walivyoabudu hata akaona madhabahu kwa ajili “Mungu asiyejulikana”.
2. Paulo basi alitaka amhubiri huyo Mungu huyo waliyemwabudu bila kumjua.

### (b) (17:24-29) PAULO ALIBAINISHA MUNGU MMOJA WA KWELI NA KUTOFAUTISHA NA MIUNGU WA UONGO

1. Tunapochanganua ujumbe wa Paulo, tunapaswa kukumbuka alikuwa akizungumza mbele ya wasikilizaji tofauti.
   a. Watu hawa walikuwa hawamwamini Mungu wa kweli aliye hai.
   b. Inawezekana hawakuwa na ujuzi wa maandiko, pengine kabisa.
   c. Basi hivyo, Paulo alianza kwa kubainisha Mungu wa kweli aliye hai, ili kuunda imani ndani yao.
2. Ukiwa na mawazo hayo akilini, ebu na tutazame jinsi kwa uzuri na nguvu alivyomwelezea Mungu huyo wa kweli aliye hai.
   a. Mst.24 Mungu aliumba ulimwengu huu na vitu vyote vilivyomo.
   b. Mst.24 Mungu ni Bwana (ruler) wa mbingu na nchi na hivyo basi hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono ya wanadamu.
   c. Mst.25 Mungu hahitiji ibada ya mwanadamu ili apate kuishi (survive).
   d. Mst.25 Kinyume na kuhitaji ibaya ya jinsi hiyo, Mungu ndiye chimbuko la uzima, pumzi, na vitu vyote anavyohitaji mwanadamu kiumbe chake!
   e. Mst.26 Ukweli ni kwamba, Mungu wa kweli aliye hai aliwaumba wanadamu wote "katika mmoja" (one blood).
   f. Mst.26 Siyo hivyo tu, bali Mungu akamweka mwanadamu duniani na kwa majaliwa yake ndiye anayeongoza miisho (destiny) na mipaka ya mataifa.
   g. Mst.27 Wanadamu wote wanawajibika kumtafuta kwa bidii Mungu na kumwona Mungu huyu wa kweli aliye hai.
   h. Mst.27 Hakika, hayuko mbali nasi, k.m., anapatikana kila mahali, eneo lolote lile kwa wakati wowote ule (omnipresent).
   i. Mst.28 Ni ndani ya Mungu huyu mmoja mwanadamu anaishi, anatembea, na kuwa na uhai wetu, k.m. mwanadamu kwa ujumla wake anamtegemea Mungu.
   j. Mst.28 Kweli kabisa, mwanadamu ametajwa kuwa uzao wa Mungu, na mshahiri Myunani ambaye Paulo alimnukuu alikubali hivyo!
   k. Mst.29 Kwa hiyo, kwa kuwa mwanadamu ni uzao wa Mungu, hatupaswi kufikiri kwamba Mungu wa kweli ni mfano wa mtu au kitu kilichoundwa na kuchongwa na mwanadamu, kama vile fedha, dhahabu, mawe, n.k.
      (1) Kwa maelezo hayo, tafadhali chunguza alichowabainishia Paulo, hata kunukuu kutoka kwa mshairi wao.
         (a) Mwanadamu ni uzao wa Mungu.
         (b) Lakini miungu iliyoabudiwa na Wathene ilikuwa mawe, fedha, dhahabu, n.k. vitu vilivyofanywa na wanadamu.
         (c) Kwa hiyo, juu ya mtazamo wao kuhusu Mungu, mwanadamu ni uzao wa mawe, fedha, dhahabu, n.k.!
      (2) Kwa maneno mengine, Paulo alikuwa akisema kuwa ibada ya vitu na miungu ya uongo haileti maana yoyote – si swala la kimantiki na kweli.
      (3) Kumbuka Paulo alizungumza na watu waliopenda kuchunguza, mantiki, na wanafalsafa!

### (c) (17:30,31) PAULO ATANGAZA WAJIBU WA MWANADAMU KWA MUNGU

### (3) (17:32-34) UREJEO KUFUATIA MAHUBIRI YA PAULO

1. Paulo alihatimisha kwa kusema kwamba zamani, Mungu alijifanya kama haoni ujinga huu (sanamu).
2. Ni jambo la msingi kutambua kwamba Paulo hakusema kuwa Mungu alisamehe au kukubali ibada hizo za sanamu.

a. Badala yake, alitoa uhuru tu kwa wanadamu wa kuchagua nani wamwabudu na jinsi ya kuishi (linga. 14:16,17; Rum.1:18-31).
b. Hata hivyo, watu hao walijua kwamba mshahara ya kuabudu sanamu na matendo mengine maovu ni mauti, k.m., kutengana milele na Mungu (Rum.1:32)!

3. Sasa, Mungu anaamuru kila mtu wa kila mahali kutubu (linga. somo letu katika 2:38 juu ya maana na umuhimu wa toba)!
4. Sababu moja watu wote wa kila mahali wanapaswa kutubu ni kwa Mungu amechagua siku atakayouhukumu ulimwengu kwa haki (linga. Ebr.9:27).
   a. Na kwamba hukumu hiyo atahukumu mwanadamu, Kristo Yesu.
   b. Linga. 2 Kor.5:10,11.
   c. Sababu nyingine wanadamu wanapaswa kutubu ni wema wa Mungu (linga. Rum.2:4-10).
5. Na Mungu ametuhakikishia kuja kwa kwa siku ya hukumu kwa kumfufua Yesu kutoka kwa wafu!

### j. (18:1-17) KATIKA KORINTHO

#### (1) (18:1-3) PAULO AKIWA NA AKILA NA PRISILA

1. Paulo akaondoka Athene na kwenda Korintho, ambako alimkuta Akila na Prisila walikuwa kazi yao ilikuwa kutengeneza hema kama vile Paulo.

#### (2) (18:4-6) PAULO ATOA HOJA KATIKA SINAGOGI – AKATALIWA NA WAYAHUDI

1. Katika Korintho Paulo akatoa hoja zake katika sinagogi kila Sabato na kuwashawishi Wayahudi na Mataifa.
2. Sila na Timotheo walipofika kutoka Thesalonike wakajiunga na Paulo, alisongwa katika roho kumhubiri Yesu kwa Wayahudi kwamba ni Kristo.
3. Walakini, Wayahudi walimpinga Paulo na kunena maneno maovu juu yake.
4. Paulo aliwajibu kuwa walikuwa wawajibike kwa makosa yao ("damu yenu na iwe juu yenu").
5. Tena, kama matokeo ya Wayahudi kuikataa injili, Paulo aliwaeleza kuwa sasa wangewageukia Mwataifa (linga. 13:46).

#### (3) (18:7-11) KRISPO NA WAKORINTHO WENGINE WAONGOKA

1. Kama matokeo ya mahubiri ya Paulo ya injili, Krispo, ambaye alikuwa mkuu wa sinagogi alimwamini Bwana.
2. Kwa nyongeza, Wakorintho wengi wakisikia ujumbe wa injili wakaamini na wakabatizwa!
   a. Hiki ni kielelezo ambacho tumekiona mara kwa mara katika kitabu hiki cha uongofu!
3. Katika mst.9,10 Bwana akanena na Paulo katika maono, akimhakikishia kama ifuatavyo:
   a. Usiogope (linga. Rum.8:31).
   b. Nena (neno).
   c. Niko pamoja nawe hakuna mtu atakayekushambulia ili kukudhuru (linga. Ebr.13:5,6).
4. Paulo aliendelea kukaa katika Korintho kwa miezi 18 na kufundisha neno la Mungu kati ya Wakorintho.

#### (4) (18:12-17) GALIO AKANA MADAI YA UONGO JUU YA PAULO

1. Wayahudi wakampeleka Paulo mbele ya liwali wa Rumi, aliyeitwa Galio.
2. Walimshitaki Paulo kwamba anawashawishi watu kumwabudu Mungu kinyume na Sheria.
3. Galio hakutaka kujihusisha kwa kuwa Paulo hakufanya kosa lolote la jinai.

4. Badala yake, aliwaambia Wayahudi kulishughulikia swala hilo wao wenyewe na akawafukuza waondoke katika kiti cha hukumu ambapo jambo hili lilifanyika.
5. Kisha Wayunani wakampiga mkuu wa sinagogi mbele ya kiti cha hukumu.

### (5) (18:18-22) PAULO AREJEA ANTIOKIA

1. Paulo akapitia Shamu (ambako Antiokia ipo) na akamchukua Prisila na Akila pamoja naye.
2. Katika mst.18 Luka alitaja kuwa Paulo alikata nywele zake kwa sababu alikuwa na nadhiri.
   a. Ingawa hatujui ni nadhiri ya jinsi gani Paulo aliiweka, na inaonekana kuwa ni aina ya viapo vya Kiyahudi vinavyoendana na Sheria ya Musa.
   b. Lakini, kwa kuwa sheria ya Musa iligogomelewa msalabani (Kol.2:14), kwa nini Paulo aliweka nadhiri na kunyoa kichwa chake kama ilivyoamuru sheria?
   c. Hakika, hii ni moja ya matukio kadhaa ambapo Paulo alifanya mambo kulingana na Sheria ya Musa baada ya kuondolewa (mst.21; 21:17-26).
   d. Ni jinsi gani Paulo alijiona sawa kufanya matendo hayo baada ya Sheria kupigiliwa msalabani, wakati akipinga kila jitihada kufunga sehemu zozote za Sheria kwa Wakristo wa Mataifa (15)?
   e. Jibu linaonekana kuwa kulikuwa na kipindi cha wakati kuanzia msalaba hadi kuanguka kwa taratibu za Kiyahudi katika kuangushwa kwa Yerusalem.
   f. Kupitia kipindi hicho, inadhihirika kuwa Wayahudi (wala si Mataifa) ambao walikuwa chini ya Sheria walishika baadhi ya maagizo.
   g. Maoni haya pengine yanathibitishwa zaidi katika Ebr.8:13.
   h. Kwa maelezo zaidi, tafadhali angalia mwishoni mwa notisi (Appendix M) katika notisi zilizochapwa.
3. Katika mst.19 Paulo akaenda Efeso akiwa na Akila na Prisila na akahojiana na Wayahudi katika sinagogi.
4. Walimwomba Paulo azidi kukaa kwa muda, lakini alikataa, akisema alipaswa afike Yerusalem.
5. Walakini, aliwaahidi kuwarejea iwapo yalikuwa mapenzi ya Bwana (Yak.4:15).
6. Kisha akang'oa nanga toka Efeso, akafika Kaisaria, na akashukia Antiokia alikoanzia safari hii ya pili ya umisionari.
7. Hapa ndipo mwiso wa safari ya pili ya umisionari.

### C. (18:24-19:41) SAFARI YA TATU YA UMISIONARI
### 1. (18:23) KATIKA GALATIA NA FRIGIA

1. Baada ya Paulo kukaa kwa muda fulani katika Antiokia, akarejea katika jimbo la Galatia na Frigia akiwaimarisha wanafunzi.

### 2. (18:24-19:41) KATIKA EFESO
#### a. (18:24-28) AKILA NA PRISILA WAMREKEBISHA APOLO

1. Mtu Myahudi aliyeitwa Apolo alifika Efeso.
2. Tafadhali angalia maelezo mazuri ya Luka anavyomwelezea mtu huyu:
   a. Mtu wa elimu.
   b. Hodari katika maadiko.
   c. Alifundishwa njia ya Bwana.
   d. Roko yake ilikuwa ikimwaka.
   e. Alinena na kufundisha kwa usahihi habari za Yesu.
   f. Isipokuwa alijua tu ubatizo wa Yohana (Mbatizaji).
3. Kutokana na maelezo haya, tunaweza kuhatimisha kuwa Apolo alikuwa mtu muhimu sana!
4. Lakini, alikuwa kihubiri ubatizo wa Yohana Mbatizaji na wala si ule wa Bwana Yesu Kristo.

   a. Ubatizo wa Yohana ulikuwa kwa ondoleo la dhambi, lakini ulikuwa maandalizi kwa ule wa Bwana Yesu (linga.19:4; Mk.1:4).
   b. Basi, ulipoanza kufanya kazi ubatizo wa Yesu, ubatizo wa Yohana haukuwa na kazi tena.
   c. Tangu ubatizo wa Yesu uanze siku ya Pentekoste (2:37-41), ubatizo wa Yohana hakuwa na kazi tena.
   d. Kwa hiyo, kwa kuhubiri ubatizo wa Yohana baada Pentekoste, Apolo hakufundisha ukweli katika somo hilo.
5. Akila na Prisila walipomsikia Apolo anafundisha ubatizo wa Yohana, wakamchukua kando na kumfundisha njia ya Mungu kwa usahihi zaidi.
6. Kutoka mst.27,28, ni dhahiri kwamba Apolo alikubali ukweli kama ulivyofundishwa na Akila na Prisila.
7. Baadaye, Apolo alitaka kwenda Akaya, ndugu wakamwandikia barua ya kutaka akaribishwe, na kwa kiwango kikubwa aliwasaidia Wakristo katika Akaya.
8. Pia aliwapinga kwa ujasiri Wayahudi hadharani kwa kuwaonyesha maandiko kwamba Yesu ni Kristo!

### b. (19:1-7) PAULO AWAKUTA WANAFUNZI 12 WALIOBATIZWA UBATIZO WA YOHANA

1. Paulo aliporejea tena Efeso, aliwakuta wanafunzi 12 na akawauliza iwapo walipokea Roho Mtakatifu walipoamini.
   a. Kwa kuwa walikuwa wanafunzi wa Bwana, Paulo alidhania kuwa walibatizwa kuingia katika Kristo na hivyo kupokea kwa kawaida Roho Mtakatifu kukaa ndani yao (linga. 2:38).
   b. Basi, Paulo alipouliza kama walimpokea Roho Mtakatifu, alikuwa akiuliza kama walimpokea Roho Mtakatifu katika kuwawezesha kutenda miujiza (linga. notisi zetu 8:17).
2. Wanafunzi walipojibu kwamba hawakuwahi hata kusikia Roho Mtakatifu, Paulo alitambua kwamba hawakupata ubatizo wa Ukristo.
3. Lakini, ni jinsi gani Paulo aliunganisha ukweli kwamba watu hawa hawakuwahi kusikia Roho Mtakatifu na ukweli wa kwamba hawakubatizwa kwa ubatizo wa Ukristo?
   a. Kwa sababu ubatizo wa Ukristo ni katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu na watu hawa walipaswa kufundishwa hivyo kabla ya kubatizwa kuingia katika Kristo (Mt.28:19).
   b. Kwa kuwa ubatizo wa Ukristo unasababisha mtu kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu (kukaa kwa hali ya kawaida), na watu hao walipaswa kufundishwa hivyo kabla hawajabatizwa kuingia katika Kristo (2:38)!
4. Ni swala la kawaida Paulo kuwauliza, “Mlibatizwa kwa ubatizo gani?”
5. Wanafunzi waliposema kuwa walibatizwa ubatizo wa Yohana, Paulo alifafanua ubatizo wa Yohana uliashiria kuja kwa Bwana Yesu Kristo.
6. Kutoka katika majibu ya Paulo na tulichojifunza katika mst.18:24-28, ni dhahiri kwamba wanafunzi hawa walibatizwa kwa ubatizo wa Yohana baada ya ule wa Yesu tayari ulikuwa ukitenda kazi!
7. Kwa hiyo, ubatizo wao haukuwa na kazi tena.
8. Wanafunzi walipotambua hilo, walibatizwa kwa ubatizo wa Yesu (jina/mamlaka ya Yesu).
9. Kisha Paulo akaweka mikono yake juu yao, kuwawezesha kunena kwa lugha na kutabiri.
   a. Mara nyingine tena, tunaona kuwa kwa kuwekewa mikono ya mitume uwezo wa kutenda miujiza alihamishwa kwenda kwa watu wengine (linga.8:14).

### c. (19:8-10) PAULO AHOJIANA KATIKA SINAGOGI NA KUFUNDISHA KATIKA SHULE

1. Kwa miezi mitatu, Paulo alinena kwa ujasiri katika sinagogi, akitoa hoja kuhusu mambo ya ufalme wa Mungu.
2. Walakini, wengine walipoifanya mioyo yao kuwa migumu na kukataa kuamini, Paulo na Wakristo wenzake wakaondoka katika sinagogi.
3. Ni jambo la kufurahisha kutambua mst.9 kwamba Ukristo umetajwa kama "Njia" (linga. mst.23; Yoh.14:6).
4. Baada ya miezi hiyo mitatu, Paulo alifundisha katika shule ya Tirano kwa miaka miwili.
5. Ni jambo la kuvutia sana kuona matokeo mazuri ya kufundisha neno la Mungu, kama ilivyohatimishwa mwishoni mwa mst.10!

### d. (19:11,12) PAULO AFANYA MIUJIZA

1. Katika mistari hii, tunajifunza Mungu alifanya miujiza isiyo ya kawaida kupitia Paulo, pamoja na magonjwa na pepo machafu wakiwatoka watu Paulo alipotuma leso na nguo kwao!
2. Utakumbuka kwamba Mungu alitenda miujiza hiyo hiyo kupitia Petro. Watu waliponywa walipoguswa kwa kivuli cha Petro (5:15).

### e. (19:13-16) WADANGANYIFU WALIIGIZA MIUJIZA LAKINI WALISHINDWA

1. Katika mst.13 Luka alitaja baadhi ya Wayahudi wapunga pepo wenye kutangatanga (k.m., waliodai kutoa pepo).
2. Wadanganyifu hao walijaribu kutoa pepo kutoka kwa watu kwa mamlaka ya Yesu, ambaye alihubiriwa na Paulo.
3. Katika mst.15 pepo mchafu alisema alimtambua Yesu na Paulo, lakini siyo hao wadanganyifu!
4. Kisha huyo mtu aliyepagawa na roho chafu aliwashinda wadanganyifu hao na wakakimbia wakiwa wamejeruhiwa.

### f. (19:17-20) YESU ATUKUZWA NA BAADHI YA WAKRISTO WATUBU

1. Habari za jambo hilo zilienea Efeso yote, zikileta hofu katika watu na kumtukuza Yesu!
2. Kwa nyongeza, Wakristo wengi waliungama matendo yao ya kale ya dhambi (mst.18).
3. Pia, nao waliotumia mambo ya uganga wakavichoma vitabu vyao mahali ambapo watu wote wangeona.
4. Uwezo wa neno la Mungu limedhihirika katika mst.20 likazidi na kushinda (k.m., lilishinda juu ya hao wadanganyifu, waganga, na juu ya vikwazo vyote)!

### g. (19:21,22) TIMOTHEO NA ERASTO WATUMWA MAKEDONIA

1. Paulo aliazimu kwenda Makedonia, Akaya, Yerusalem, na Roma.
   a. Kama utani Paulo baadaye alifika Rumi, pengine lakini si katika njia aliyoikusudia awali.
2. Bila shaka ili aitayarishe safari, Paulo akamtuma Timotheo na Erasto kwenda Makedonia, lakini alikaa katika Asia kwa muda kitambo.

### h. (19:23-29) DEMETRIO AHAMASISHA WAFUA VYUMA KUFANYA GHASIA NA UASI

1. Katika mistari hii Demetrio ametajwa kuwa ni mfua fedha ambaye aliwapatia faida mafundi wengi kwa kutengeneza mungu wa fedha mke Diana.
2. Katika mst.25-27 Demetrio aliwaita wafua vyuma hao na kusema mambo yafuatayo:

a. Paulo amewageuza watu wengi kwa kuwaeleza kwamba vitu vilivyofanywa kwa mikono si miungu!
b. Kama matokeo yake, biashara yao ya kufanya miungu ilikuwa katika hatari ya kuangamia.
c. Na wala si hivyo tu, lakini hekalu la Diana litadharaulika.

3. Watu waliposikia hayo, walijaa ghadhabu na mji ukajaa mfadhaiko.
4. Kwa nyongeza, wakawakamata Gayo na Aristarko, watu walisafiri nao Paulo, na kuwaleta mahali pa michezo.
   a. Paulo alimbatiza Gayo Korintho na alikuwa mwenyeji wa Paulo (1 Kor.1:14; Rum.16:23).
   b. Aristarko baadaye alifungwa pamoja na Paulo Rumi (Kol.4:10).

### i. (19:30-34) PAULO ATAKA KUNENA KATIKA MKUTANO, LAKINI WANAFUNZI WAKAMZUIA

1. Paulo alitaka kuingia katika ukumbi ili kuzungumza na watu, lakini wala si Wakristo wenzake ama watumishi wa Asia waliokuwa marafiki zake wangemruhusu.
3. Kundi moja likapiga kelele hizi na lingine zingine hata watu wengi hawakutambua kilichofanya mkutano huo1
4. Na mtu aliyeitwa Iskanda alitaka kuzungumza katika kuwatetea Wayahudi.
5. Hata hivyo, mkutano ulipotambua kuwa alikuwa Myahudi, wakapaza sauti kwa pamoja, “Artemi ni mkuu wa Waefeso” kwa kipindi cha masaa mawili.

### j. (19:35-41) KARANI WA MJI AKATULIZA MKUTANO

1. Mistari hii tunajifunza karani wa mji alituliza ghasia za mkutano.
2. Alifanya hivyo kwa kubainisha mambo matano:
   a. Mst.35,36 Hakuna mtu atakayepinga kwamba mji wa Efeso ni mtuzaji wa hekalu la Diana; hivyo basi, walipaswa kutulia na kutofanya mambo kwa pupa.
   b. Mst.37 Paulo na wenzake hawakuiba katika hekalu au kumtukana mungu wao.
   c. Mst.38 Kama yalikuwa mashitaka halali, Demetrio alipaswa kuwapeleka katika baraza lililoamuriwa.
   d. Mst.39 Kama wana madai mengine, yafanyiwe kazi katika mikutano halali.
   e. Mst.40 Walikuwa katika hatari na serikali ya Rumi kwa kukusanyika isivyo halali.
3. Baada ya kusema mambo hayo, karani wa mji akauvunja mkutano.

### 2. (20:1-5) KATIKA MAKEDONIA

1. Baada ya ghasia kukoma, Paulo akawaonya wanafunzi na akaondoka kwenda Makedonia, ambako alihamasisha Wakristo wenzake kwa maneno mengi.
2. Kisha akaenda Uyunani, ambako alikaa miezi mitatu.
3. Wayahudi walipomfanyia vitimvi huko, akaazimu kung’oa nanga kwenda Shamu, akipitia Makedonia kwanza.
4. Watu wengine waliotajwa katika mst.4 walikwenda na Paulo Asia.

### 4. (20:6-12) KATIKA TROA – CHAKULA CHA BWANA/ EUTIKE AFUFULIWA KUTOKA KWA WAFU

1. Paulo Paulo na watu alikuwa nao wakasafiri toka Filipi hata Troa, ambako walikaa siku saba.
2. Tafadhali chunguza mst.7 kwamba Wakristo walikusanyika pamoja kumwabudu Bwana siku ya kwanza ya juma.
   a. Siku ya kwanza ya juma ni Jumapili.

   b. Hili linatueleza kuwa Wakristo wanapaswa kukusanyika pamoja kumwabudu Bwana siku ya kwanza ya juma, na wala si Jumamosi, ambayo ni siku ya saba ya juma.
3. Wakristo walipokusanyika pamoja siku ya kwanza ya juma, walimega mkate (mst.7).
   a. Hapa mkate unalenga Chakula cha Bwana kuzingatia mazingira
   b. Hii ni kwa sababu moja ya mambo ambayo Wakristo wanafanya wanapokusanyika pamoja Jumapili ni kushiriki mkate unaowakilisha mwili wa Yesu na mzao wa mzabibu unaowakilisha damu yake.
   c. Linga. 2:42; 1 Kor.10:16; 11:20-29.
4. Jambo lingine Wakristo hawa walifanya kama moja ya ibada Jumapili ilikuwa mahubiri, mafundisho, na kusoma neno la Mungu. Paulo akahubiri hata usiku wa manane.
5. Paulo alipokuwa akihubiri, mtu mmoja aliyeitwa Eutiko akalemewa na usingizi, akaanguka orofa ya tatu dirishani, akafa.
6. Walakini, Paulo akamfufua kutoka kwa wafu na hilo likawafariji mno Wakristo.
7. Kabla hatujaondoka katika mistari hii, ni muhimu mno kwetu kutambua mfano wa mitume uliotolewa hapa.
8. Ni dhahiri kutokana na mfano huu na kutokana na ukweli kwamba Paulo alisubiri siku saba Troa kwamba Pauli alitambua Wakristo wa awali walikusanyika kila Jumapili.
   a. Lakini tumeona moja ya mambo waliyofanya walipokusanyika pamoja Jumapili ilikuwa "kumega mkate", k.m., kushiriki Chakula cha Bwana.
   b. Hivyo basi, tunaweza kuhatimisha bayana na sahihi kabisa kwamba Wakristo hao wa awali walifuata kielelezo hicho cha mitume katika kushiriki Chakula cha Bwana kila Jumapili (wala si kwa mwezi, robo mwaka, au kwa mwaka, n.k.).
   c. Hatimisho hilo huzidi kuwa na nguvu zaidi tunapoangalia baadhi ya mafungu mengine ya maandiko:
      (1) 1 Kor.16:2.
      (2) Kut. 20:8.

**5. (20:13-38) KATIKA MILETO**

**(a) (20:13-16) SAFARI KUELEKEA MILETO**

1. Paulo alitembea kwa miguu toka Troa hadi Aso, wakati wengine walisubiri merikebu.
2. Kutoka huko wakang'oa nanga kwenda Mitilene, Kio, Samo, Trogilio, na kisha Mileto.
3. Katika mst.16 tunajifunza Paulo aliazimu kupita Efeso merikebuni akitaka kuwahi Yerusalem Siku ya Pentekoste.

**b.c, (20:17-21) PAULO ALITUMA WAITWE WAZEE TOKA EFESO NA KUWAKUMBUSHA KAZI YAKE KWAO**

1. Kwa kuwa Paulo hakuwa na muda wa kwenda Efeso, aliwaita Wazee kutoka kanisa la Efeso kukutano naye Mileto.
2. Wazee walipokutana naye aliwakumbusha kazi yake mbele yao kwa kubainisha mambo yafuatayo kuhusu juhudi yake:
   a. Mst. 19.
   b. Mst. 19.
   c. Mst. 19 .
   d. Mst. 20.
   e. Mst. 20.
   f. Mst. 20.
   g. Mst. 21.

**d. (20:22-25) KWENDA YERUSALEM KUMALIZA MBIO ZAKE NA HUDUMA KWA FURAHA – BILA KUJALI MAONYO YA KUDHURIWA**

1. Katika mistari hii Paulo aliwaeleza wazee walikusudia kwenda Yerusalem, hata ingawa hakujua haswa jambo ambalo lingempata huko.
2. Alijua, hata hivyo, kwamba Roho Mtakatifu alimshuhudia kufungwa ("vifungwa") na dhiki vilikuwa vikimgojea.
3. Katika mst.24 tuna moja ya maelezo juu ya imani kubwa ya Paulo na upendo wa Bwana.
4. Tafadhali chunguza alichosema Paulo katika utabiri huu wenye kuogofya.
   a. Hakuna hata jambo moja lilimbabaisha (k.m., hayakumwogopesha na hayakumzuia kufanya alichokusudia).
   b. Hakuhesabu maisha yake mwenyewe kuwa kitu (alikuwa ni heri kufa kwa ajili ya Bwana Yesu) (linga. Flp.1:21).
   c. Alitaka kumaliza mbio zake za Ukristo kwa furaha (linga. Ebr.12:1-4).
   d. Na kumaliza huduma hii ya kuhubiri injili ya Kristo.
5. Angalia mwishoni mwa mst.24 Paulo aliitaja injili kama injili ya neema ya Mungu.
   a. Fungu hili, mst.32, na mafungu mengine mengi kama haya huharibu hoja zinazotumika na baadhi kwamba kwa kuwa tupo chini ya neema, hatupaswi kujali juu ya sheria za Mungu.
   b. Mafungu haya yanaonyesha kuwa hauwezi kutenganisha injili ya ajabu ya Mungu (k.m., sheria yake) kutoka katika neema yake ya ajabu!
6. Katika mst.25 Paulo aliwavunja moyo kwa kweli kwamba asingewaona tena ndugu hao katika maisha haya.

### e. (20:26,27) PAULO KUTOKUWA NA HATIA KWAKE

1. Katika mst.26 Paulo alitoa hoja ya nguvu kwamba alikuwa hana hatia kwa damu ya mtu yeyote (k.m., alikuwa hana hatia juu ya mtu yeyote aliyemhubiria).
2. Alisema kuwa aliweza kutoa maelezo hayo kwa sababu hakujiepusha kuwahubiria habari ya kusudi zima la Mungu.
3. Kwa maneno mengine, Paulo alisema alihubiri kwa ujasiri mapenzi ya Mungu yote kwa wasikilizaji wake, hata ingawa hawakutaka kusikia (linga. 13:46; 18:6).
4. Hili ni jukumu lisiloepukika la kila mzee, mhubiri, mwalimu, na kila Mkristo, k.m., kuhubiri kusudi zima la mapenzi ya Mungu katika kila somo.
5. Linga. 2 Tim.4:1,2; 1 Pet.4:11; Eze.3:16-21.

### f. (20:28-32) PAULO ALIWAONYA WAZEE JUU YA KUJA KWA UKENGEUFU

1. Katika mistari hii Paulo alitoa maonyo makali kwa wazee wa Efeso na kuwafundisha wazee kipindi hicho na kuendelea.
2. Paulo alianza katika mst.28 kwa kuwaeleza wazee kujitunza wenyewe kuwa makini sana ("jituzeni nafsi zenu").
   a. Kwa maneno mengine, wazee wameamuriwa kujilinda wao wenyewe kuhakiki kwamba maisha yao wenyewe yanastahili ofisi hiyo ya juu ambayo wanatumika.
   b. Wanapaswa kuwa makini sana kwamba wanaongoza kwa kuishi maisha yanayostahili injili ya Kristo ili wawe mfano bora wa maisha kwa wengine (1 Pet.5:3).
   c. Walipaswa kujilinda na majaribu ya kiburi, tamaa ya madaraka, uchu, n.k.
   d. Kama wahubiri, wazee wanapaswa kujitunza wenyewe na mafundisho yao (linga. 1 Tim.4:16).
3. Tena, Paulo alisema wazee walihitajika kujitunza au kwa bidii kukesha na lile "kundi lote".
   a. Katika Agano Jipya, "kundi" hurejea kondoo, ambayo ni njia ya Mungu ya upole kuwataja Wakristo, kanisa (linga. Yoh.10:1ff; 21:15-17).
   b. Basi, wazee wana jukumu makini la kukesha kwa hizo roho za washiriki wa kusanyiko la mahali pamoja ambalo wanatumika (linga. Ebr.13:17).

4. Tena, Pauloa alisema Roho Mtakatifu aliwafanya wazee hao wa Efeso kuwa “waangalizi”.
   a. Ni neno lilo hilo ambalo linatafsiriwa “askofu” katika mafungu kama 1 Tim.3:1.
   b. Tunabainishwa kuwa maneno askofu, mzee, na mwangalizi yote yanalenga ofisi moja katika kanisa la Bwana (linga. Tit.1:5-7).
   c. Neno lililotafsiriwa mwangalizi au askofu linamaanisha “mtu aliyekabidhiwa jukumu la kuangalia mambo kuwa yanafanywa na wengine barabara, mlinzi au msimamizi yeyote yule” (Thayer).
   d. Basi, ofisi ya mzee, askofu, mwangalizi, inahusu mamlaka waliyokabidhiwa na Mungu kwa watu hawa wenye sifa (linga. 1 Thes.5:12; Ebr.13:7, 17).
   e. Leo, Roho Mtakatifu anachagua waangalizi kwa namna ambayo amefunua sifa maalum ambazo watu ni sharti wawe nazo katika 1 Tim.3:1-7 na Tito 1:5-14.
   f. Basi, wanaume wanapofanya kazi kwa miaka mingi hukuza vipaji hivi vilivyotolewa na Roho Mtakatifu katika Biblia na ndugu katika kusanyiko la mahali pamoja huzitambua sifa hizo na huchagua wanaume hao kufanya kazi kama wazee, hivyo basi Roho Mtakatifu amewafanya kuwa waangalizi kwa njia hiyo isiyo ya moja kwa moja!
5. Bado katika mst.28 Pauli alisema kazi nyingine ya wazee ni “kulichunga” (shepherd – NKJV), au “kulilisha” (feed – KJV, ASV) kanisa.
   a. Neno lililotafsiriwa kwa jinsi hii lilitumika kurejea kazi za wachungaji kwa kondoo ambazo walikuwa na majukumu juu yake.
   b. Kazi hiyo ni pamoja na kulisha kondoo, kusimamia shughuli zao kwa ajili ya mema yao, nidhamu, kulinda kondoo na maadui, kuzituza kondoo zenye maradhi, na kuzirejesha kundini zile zilizopotea.
   c. Hivyo basi, katika kutumia neno, Mungu alikuwa akitoa picha nzuri ya majukumu ya wazee kama wachungaji wa kondoo wa Mungu, k.m., kwa washiriki wa kusanyiko.
   d. Basi, majukumu ya wazee katika kusanyiko inajumuisha mambo kama:
      (1) Kuhakikisha kwamba mafundisho sahihi ya neno la Mungu yanapatikana kama chakula cha kiroho (linga. Tit.1:9).
      (2) Kuangalia shughuli za kusanyiko kwa kutumia neno la Mungu sawasawa (linga. 1 Pet.5:2).
      (3) Kutoa nidhamu pale inapohitajika (linga. 2 Thes.3:6,14,15).
      (4) Kulinga kusanyiko na maadui kiroho (linga. mst.29-31; Tit.1:9-14).
      (5) Kuwatunza hao walio wagonjwa kiroho (linga. 1 Thes.5:12-14).
      (6) Kuwarejesha kundini hao walipotoka toka katika imani ya injili (linga. Tito 1:9-14).
6. Katika mst.29 Paulo alionya kwamba watu wenye nguvu, wakali, hatari (“mbwa mwitu wakali”) wangeinuka kati yao wazee wakijaribu kuharibu makusanyiko ya makanisa ya Bwana.
7. Zaidi sana, katika mst.30, Paulo alitahadharisha hatari nyingine kwa kanisa kama ifuatavyo:
   a. Watu wangeinuka miongoni mwa wazee.
   b. Wangenena mapotofu, k.m., mambo ya kuharibu, kugeuza, kuangamiza ukweli wa Mungu.
   c. Kusudi lao lilikuwa kuwageuza watu wawaandamie wao (badala ya Bwana Yesu Kristo).
   d. Kwa bahati, tunapojifunza historia ya kanisa inafunua ukweli huu juu mambo yaliyolipata kanisa la awali.
   e. Watu walinuka kutoka katika wazee kudai mamlaka zaidi na zaidi juu yao wenyewe hata mtu mmoja alidai kuwa na mamlaka juu ya wengine wote na cheo chake kama “papa” katika 606 B.K.
   f. Ingawa hatuna muda wa kutosha kujifunza mambo haya ya kusikitisha na huzuni kukengeuka kutoka katika Ukristo wa karne ya kwanza, tunakusihi ujifunze kwa maelezo zaidi ama katika kozi ya historia ya kanisa ilitolewa na “World Video Bible School.”
8. Katika mst.31 Paulo aliwaonya wazee kuwa makini kwa hatari hizi na zingine katika kusanyiko la kanisa la Bwana (linga. 1 Pet.5:8).

9. Paulo pia aliwakumbusha wazee jinsi alivyowaonya na ndugu wengine juu ya mambo haya hapo nyuma.
10. Angalia maelezo ya Paulo bora katika juhudi yake kama kielelezo kwa wahubiri wote wa neno la Mungu:
    a. Kwa miaka mitatu, hakuacha kumwonya kila mmoja wao.
        (1) Hakika, Paulo alikuwa mvumilivu katika juhudi yake kufundisha na kuwaonya ndugu (linga. 2 Tim.4:2; 2:24-26).
    b. Usiku na mchana.
        (1) Kazi ya mhubiri haiwezi kuisha; lazima awe tayari wakati ufaao na wakati usiofaa (linga. 2 Tim.4:2).
    c. Kwa machozi.
        (1) Mhubiri mwaminifu hafurahii kuwakemea watu wengine kwa kuhubiri neno la Mungu; badala yake, huhuzunika watu wanaoshindwa kumtii Bwana (linga. Zab.119:136)!
11. Katika mst.32 Paulo aliwaeleza wazee jinsi ya kulichunga na kulilinda kusanyiko la kanisa la Bwana.
12. Njia pekee ya kufanya hivyo ni kwa neno la Mungu, ambalo kupitia hilo neema yake ya ajabu hupatikana.
13. Pia, tafadhali angalia nguvu ya ajabu ya neno la Mungu ilivyobainishwa na Paulo katika mstari huu:
    a. Laweza kuwajenga, k.m., kuimarisha, kuwatia nguvu (linga. 1 Yoh.2:14)!
    b. Linaweza kuwapa urithi wa uzima wa milele kupitia maneno ambayo, tukitii, litatuongoza hata uzima wa milele (1 Pet.1:3,4; Yoh.6:68).
    c. Jambo hili linawezekana kwao waliotakaswa.
        (1) Kutakaswa maana yake ni kutengwa mbali na ulimwengu na kujitoa wakfu kwa ajili ya Bwana.
        (2) Hao tu waliotengwa mbali na ulimwengu na kujitoa wakfu kwa Bwana watapokea uzima wa urithi wa uzima wa milele.
        (3) Na njia pekee mtu anaweza kutakaswa au kutengwa ni kupitia kusoma, kutafakari, na kulitii neno la Mungu (linga. Yoh.17:17).

### g. (20:33-38) KUACHANA, SALA, NA HUZUNI

1. Katika mistari hii Paulo aliwakumbusha wazee hakuwa na hatia ya kutamani mali za watu wengine.
2. Ukweli ni kwamba, alifanya kazi kwa mikono yake kwa ajili ya mahitaji yake na wale walikuwa pamoja naye.
3. Kwa kufanya hivyo, alionyesha kwamba Wakristo lazima wawasaidia wanyonge na kwamba, kama Yesu alivyosema, ni heri kutoa kuliko kupokea (linga. 2:44,45; 4:34-36).
4. Baada ya Paulo kunena maneno hayo yenye mvuto, alipiga magoti na kusali pamoja nao.
5. Baada ya sala hiyo, walikuwepo hapo wakalia sana na kumbusu Paulo.
6. Walihuzunika sana kwa sababu Paulo aliwaambia wasingeonana tena naye.
7. Picha hii yenye kuguswa na upendo mwingi wa Wakristo hao kwa kila mmoja wao (ambao tunapaswa kupendana leo kila mmoja wetu) (linga. Yoh.13:34,35; Kol.2:2)!
8. Mwisho, wazee na wale walioambatana na Paulo wakaambatana na Paulo kuelekea katika merikebu mahali alikuwa aondokee.

## 6. (21:1-6) KATIKA TIRO – PAULO ALIONYWA ASIENDE YERUSALEM

1. Paulo na hao aliokuwa nao baada ya kusimama katika Patara wakang’oa nanga wakaacha kufika Kipro wakafika Tiro.
2. Katika Tiro waliwakuta baadhi ya Wakristo na wakakaa nao kwa siku saba.

3. Wakristo hao wakamwonya Paulo alipande Yerusalem.
4. Baada ya siku saba Wakristo wakamsindikiza Paulo kwenda katika merikebu, alipinga magoti pamoja nao, na wakasali.

**7. (21:7-14) KATIKA KAISARIA – AGABO AMWONYA PAULO KUHUSU YERUSALEM – MAJIBU YAKE**

1. Baada ya kutua katika Tolemai kwa siku moja, Paulo na wenzake wakafika Kaisaria na wakakaa pamoja na Filipo mwinjilisti, ambaye ni mmoja wa wale saba waliochaguliwa kwa ajili ya kazi ya kuhudumu mezani katika sura 6.
2. Katika mst.9 tunajifunza Filipo alikuwa na binti wanne ambao walitabiri.
   a. Inadhihirika kuwa wanawake hao walipokea uwezo wa kimiujiza wa kutabiri (linga. 1 Kor.12:4-10; 14:3).
   b. Swala hili ni utimilifu wa ahadi ya Mungu kumwaga Roho Mtakatifu juu ya "mabinti" (2:17).
   c. Hata hivyo, tunatambua kuwa wanawake hawa hawakuvunja amri ya Mungu ya kutofundissha na kuwatawala wanaume (linga. 1 Tim.2:11,12; 1 Kor.14:34).
3. Katika mst.10,11 nabii aliyeitwa Agabo alitabiri kuwa Paulo angefungwa na Wayahudi Yerusalem na kupelekwa katika mikono ya Mataifa.
4. Wenzake na Paulo waliposikia unabii huu, walimsihi asipande kwenda Yerusalem.
5. Paulo alijibu kwa kutoa mambo mazuri mawili:
   a. Aliuliza kwa nini walikuwa wakilia na kumvunja moyo.
   b. Alisema kwamba si tu alikuwa tayari kufungwa, bali pia kufa Yerusalem kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo (linga.20:24; Flp. 1:20-24)!
6. Walipoona nia Paulo haikubadilika wakasema, "Mapenzi ya Bwana yatendeke."
7. Hili linahatimisha safari ya tatu ya umisionari.
8. Katika safari hii ya kusisimua na kuvutia, tumeona kazi ya imani ya kujitoa na kazi ya upendo ya Paulo na alioambatana nao wakihubiri injili, kuongoa roho, na kuwaimarisha Wakristo katika maeneo yafuatayo:
   a. 18:23 Galatia na Frigia
   b. 18:24-19:41 Efeso
   c. 20:1-5 Makedonia.
   d. 20:6-12 Troa.
   e. 20:13-38 Mileto.
   f. 21:1-6 Tiro
   g. 21:7-14 Kaisaria
9. Hili sasa linatupeleka katika sehemu kubwa ya mwisho ya kielelezo chetu.

**D. (21:15-28:31) PAULO KATIKA MIKONO YA MAADUI**

**1. (21:15-23:23) KATIKA YERUSALEM**

**a. (21:15-17) PAULO AWASILI YERUSALEM NA APOKELEWA KWA FURAHA**

1. Ni dhahiri kutoka sehemu zingine za Agano Jipya kwamba Paulo alipeleka msaada kwa Wakristo katika Yudea.
2. Msaada huo ulikuwa kwa jinsi ya changizo kutoka kwa ndugu zao Wakristo wa Makedonia na Akaya.
3. Kabla ya kuwasili kwake Yerusalem, Paulo alidhania kwamba Wakristo katika Yudea wenye asili ya Kiyahudi wasingepokea zawadi kutoka kwa Wakristo wa Mataifa (linga. Rum.15:26-31).
4. Basi, kupokelewa kwa furaha kwa Paulo alipowasili Yerusalem hilo lazima lilimfurahisha.

### b,c. (21:18-22) PAULO AKUTANA NA YAKOBO NA WAZEE, YAKOBO ATAMBUA TATIZO

1. Paulo alikutana na Yakobo na wazee na kuwaeleza kwa kiina mambo Mungu aliyowatendea Mataifa kupitia huduma yake Paulo.
2. Yakobo na wazee wakamtukuza Bwana waliposikia habari hizo njema.
3. Kisha wakamweleza Paulo mambo ambayo Wakristo wengi wenye asili ya Kiyahudi wenye juhudi katika Sheria ya Musa walisikia alichokuwa akifundisha.
4. Kubainisha zaidi, walisikia kwamba Paulo akifundisha yafuatayo:
   a. Wayahudi wanapaswa kumwacha Musa, k.m., kwamba walipaswa kuiacha Sheria ya Musa.
   b. Hawakutakiwa kuwatahiri watoto wao.
   c. Wasizifuate desturi, k.m., desturi zinazoambatana na Sheria ya Musa.
5. Baada ya kutoa taarifa ya mambo hayo, Yakobo na wazee waliuliza jambo la kufanya kwa kuwa Wayahudi wangekusanyika pamoja kwa sababu walisikia kuwa Paulo yupo Yerusalem.

### d,e. (21:23-26) MAONI YA YAKOBO NA MAJIBU YA PAULO

1. Yakobo alimshauri Paulo ajitakase pamoja na watu wanne waliofanya nadhiri na kulipa gharama zao ili kwamba wanyoe vichwa vyao, ikiashiria hatima ya nadhiri yao.
2. Hakika, nadhiri hizi ni viapo vinavyoelezwa katika Sheria ya Musa (linga. Hes.6:3-20).
3. Yakobo alisema jambo hili lilikuwa lifanyike ili kwamba wote wapate kuona kuwa mambo waliyosikia kuhusu Paulo hayakuwa ya kweli.
4. Kisha, katika mst.25, Yakobo alirudia kwamba Wakristo wa Mataifa hawakupaswa kushika desturi hizo, isipokuwa mambo manne tuliyojifunza awali, katika sura 15.
5. Mwisho, katika mst.26, Paulo alifanya mambo aliomshauri Yakobo.
6. Basi, kama ilivyokuwa katika 18:18, Paulo alishika sehemu ya Sheria hata ingawa iligongomelewa msalabani (linga. Kol.2:14).
   a. Kama tulivyoona katika somo la 18:18, kipindi hicho baadhi ya mambo katika Sheria yalitendwa na hao Wakristo wenye asili ya Kiyahudi.
   b. Walakini, mambo hayo yalichukuliwa kama mambo ya hiari, kufaa (expediency), au kujali (indifference), ambayo hayakuhitajika kwa wokovu.
   c. Hilo lilikuwa kweli kwa sababu hakuna mtu angehesabiwa haki au kuokolewa kwa kushika Sheria za Kale (Rum.3:20, 28).
   d. Basi, Paulo alitenda mambo hayo si kwa sababu alipaswa kufanya, wala si kwamba aokoke, bali asiwe kikwazo kwa Wakristo wenye asili ya Kiyahudi.
7. Mwisho, katika kuzingatia kile walichosema kuwa kilifundishwa na Paulo kwamba Wayahudi hawakupaswa kuwatahiri watoto, tunajua kwamba dai hilo si kweli!
   a. Kwa mfano, alimtahiri Timotheo ambaye mamaye alikuwa mwenye asili ya Kiyahudi (linga. 16:13).
   b. Walakini, Paulo aliweka bayana hili kwamba mtu hakutakiwa atahiriwe ili aokoke (15:1,2; linga. Gal.5:6; 6:15).

### f. (21:27-30) WAYAHUDI ASHUTUMIWA NA KUKAMATWA ILI AUAWE

1. Paulo alipokuwa hekaluni, baadhi ya Wayahudi kutoka Asia wakataharakisha watu, wakamkamata Paulo, na kumshitaki.
2. Walimshitaki kwa uongo kama ifuatavyo:
   a. Anafundisha watu wote kila mahali kinyume “taifa letu”, k.m., Wayahudi.
   b. Kinyume na torati.
   c. Kinyume na hekalu.
   d. Akiwaleta Mataifa ndani ya hekalu, akilinajisi (kulichafua).

3. Katika mst.29 Luka alibainisha kwamba mashitaka yao juu ya kuleta Mataifa hekaluni ilikuwa dhana tu walizofikiri.
   a. Hili linaonyesha hatari ya kudhania na kurukia hatimisho kabla ya kuwa na ukweli wote!
   b. Hakika tunapaswa kufikiri mema kuhusu ndugu zetu hata wanapothibitika kwa namna nyingine za mafundisho au tabia (1 Kor.13:4ff).
4. Kuzingatia mashitaka hayo ya uongo, watu wakamkamata Paulo nje ya hekalu.

**h. (21:31-36) WATUMISHI WA RUMI WAMKAMATA PAULO**

1. Wayahudi walipojaribu kumwua Paulo, jemadari wa askari wa Rumi alisikia kuhusu ghasia na kupeleka askari eneo hilo.
2. Wayahudi walipoona maaskari, walimwacha kumpiga Paulo.
3. Jemadari akaamuru Paulo afungwe kwa minyororo na kumwulia jina lake na alichofanya.
4. Kwa kuwa umati ulipiga kelele kwa mambo mbalimbali kuhusu Paulo, jemedari hakupata hakika ndipo akaamuru Paulo apelekwe ndani ya ngome.
5. Maskari wakambeba Paulo kwa sababu ya vurugu za umati, waliokuwa wakipiga kelele, "mwondoe huyo," (linga. Yoh.19:15 – ndivyo walivyosema juu ya Yesu)!

**i. (21:37-39) PAULO ALIOMBA RUHUSA AZUNGUMZE MBELE YA UMATI**

1. Paulo alimwomba jemedari kuzungumza naye ambaye alifikiri kuwa Paulo ni Mmisri ambaye aliongoza uasi wa wauaji 4,000.
2. Paulo alimweleza jemedari alikuwa Myahudi kutoka katika mji muhimu wa Tarso.
3. Kwa maneno mengine, Paulo alisema hakuwa mwuaji kama jemedari alivyomdhania.
4. Paulo alimsihi jemedari ampe ruhusa kunena na mkutano.

**l. (21:40-22:21) PAULO APEWA RUHUSA NA KUANZA KUNENA**
**(1) (21:40-22:5) HISTORIA YA KUWA MWEBRANIA**

1. Jemadari alitoa ruhusa kwa Paulo kuzungumza na mkutano.
2. Paulo alipowakabili kwa heshima na kunena nao katika lugha ya Kiebrania, wakanyamaza kimwa.
   a. Paulo angeweza kuchangua kunena katika Kiyunani.
   b. Walakini, alichagua kunena kwa Kiebrania kama heshima ya utaifa wake wa Kiyahudi.
   c. Hilo likanyamzisha kundi.
3. Paulo aliwaeleza makutano alilelewa kiusahihi katika imani ya Kiyahudi.
4. Katika mst.4 na 5 hata akasema aliwatesa watu wa "Njia hii", k.m., Ukristo.
5. Jambo hili ni pamoja na kuwaua na kuwatia gerezani.

**(2) (22:6-10) MAONO YAKE JUU YA YESU ALIYEFUFUKA AKIWA NJIANI KWENDA DAMESKI**

1. Katika mistari hii Paulo alirudia kusimulia maono yake juu ya Yesu akiwa njiani kwenda Dameski (linga. somo letu 9:3ff).
2. Katika mst.9 angalia Paulo alisema wale aliokuwa nao akiwa njiani kwenda Dameski hawakusikia sauti ya huyo aliyezungumza na Paulo.
3. Wengine wanadai kuwa maelezo haya yanapingana na habari katika 9:7, ambapo panadai kwamba hao waliokuwa na Paulo walisikia sauti.
   a. Bila shaka, hakuna kupingana kabisa!
   b. Neno lililotafsiriwa "sikia" linaweza kutafsiriwa kwa namna mbili:
      (1) Tendo la kusikia sauti kimwili.
      (2) Si kusikia tu, bali pia kuelewa.

c. Basi, katika sura 9, Luka aliandika kwamba hao waliokuwa pamoja na Paulo walisikia sauti ya maneno yaliyozungumzwa na Bwana.
d. Sasa, katika sura 22, Luka aliandika kwamba watu waliosikia sauti, hawakuelewa maneno yaliyonenwa na Bwana.

4. Basi, kama tulivyoona mara kadhaa katika somo letu la kitabu cha Matendo, hakuna kupingana katika neno la Mungu, bila kujali "wasomi" na wadadisi wanavyodai!

### (3) (22:11-16) ANANIA AKAMFIKIA PAULO DAMESKI NA KUMWELEZA MAMBO YA KUFANYA

1. Mistari hii ina maelezo ya msingi kama tulivyoona katika somo letu 9:8-19.
2. Lakini, kuna maelezo muhimu kidogo yaliyofunuliwa katika mst.16.
   a. Katika mstari huo, Mungu alifunulia kile Anania alimweleza Paulo kufanya ili aokoke kutoka katika dhambi zake!
   b. Baada ya Paulo kumwamini Bwana na kufunga na kuomba kwa siku tatu, alikuwa angali katika dhambi!
   c. Alitakiwa kufanya jambo fulani ili dhambi zake hizo ziweze kusafishwa nafisini mwake.
   d. Anania alimwuliza Paulo kwa nini alikuwa akikawia na akamweleza kusimama na kubatizwa ili aoshwe dhambi zake!

### (4) (22:17-21) MAONO YA PAULO YERUSALEM

1. Hapa Paulo aliuambia umati mambo yaliyotokea aliporejea Yerusalem kutoka Dameski.
2. Alipokuwa akiomba hekaluni, Bwana alimweleza katika ndoto kuondoka Yerusalem mara moja kwa kuwa wasingepokea ushududa wake hapo.
3. Katika ndoto, Paulo aliitikia alivyoambiwa na Bwana kwamba Wayahudi walitambua Paulo aliwatesa Wakristo, pamoja na kuunga mkono na kushuhudia kifo cha Stefano mfia imani.
   a. Hakika, Paulo alilileta hili kwa Bwana akififikiri kuwa pengine Wayahudi wasingemsikiliza kwa sababu aliwatesa Wakristo hapo nyuma.
4. Walakini, Bwana alimwamuru kwenda kwa Mataifa.

### j. (22:22,23) WAYAHUDI WALIVYOPOKEA HOTUBA YA PAULO

1. Wayahudi walimsikiliza kwa makini Paulo hata alipotamka neno "Mataifa."
2. Waliposikia neno hilo wakapaza sauti zao wakidai kuwa Paulo hakustahili kuishi.
3. Mtazamo huu mbaya unadhihirisha chuki ya ukabila, isiyo na utaua ambayo Mungu anaipinga waliyokuwa nayo (Gal.3:28,29; Yak.2:1-13).

### k.(22:24-29) PAULO ADAI KUWA NI RAIA WA RUMI

1. Jemedari wa Rumi aliamuru Paulo achunguzwe sababu ya kumpigia mijeledi ili ajue kwa nini walimpigia kelele namna hiyo.
2. Kama askari walivyomfunga Paulo, alimwuliza akida kama ilikuwa halali kumpiga raia Mrumi ambaye hajahukumiwa bado.
3. Yule akida alipotambua kuwa alikuwa raia wa Rumi, alimwendea jemedari mara moja na kumshauri awe makini na alichofanya kwa sababu Paulo alikuwa raia wa Rumi.
4. Jemedari alimwuliza Paulo kama alikuwa kweli ni raia wa Rumi na akimwonyesha kuwa aliununua uraia wa Rumi kwa gharama kubwa.
5. Paulo alipojibu kuwa alizaliwa raia wa Rumi, jemedari aliongopa kwa kuwa alimfunga raia wa Rumi.

### l. (22:30-23:11) PAULO APELEKWA MBELE YA BARAZA

### (1) (22:30-23:5) KUKABILIANA KWAKE NA KUHANI MKUU

1. Kwa kuwa jemedari alitaka kujua sababu gani Paulo alishutumiwa na Wayahudi, alimpeleka Paulo katika baraza (Sanhedrin).
2. Paulo alizungumza mbele ya baraza kwa heshima na akasema kuwa aliishi mbele za Mungu kwa dhamiri safi hata sasa.
   a. Dhamiri ni utu wetu wa ndani ambao ama unatushutumu tunapofanya mabaya, au kutoa udhuru kwa yale tuliyofanya kuwa ni sawa (linga. Rum.2:15).
   b. Lakini, Paulo alikuwa amesema kuwa aliwaua Wakristo na kuwatia gerezani (matendo yote mabaya)1
   c. Hili linatufundisha sisi kuwa dhamiri siyo ndiyo kiongozi wa kutolea maamuzi.
   d. Kwa nyongeza, dhamiri inaweza kukataliwa au kutiwa muhuri kwa chuma cha moto kama tunaamua kufanya hivyo (linga.1 Tim.1:19; 4:2).
   e. Basi, dhahiri zawadi kubwa kutoka kwa Mungu, lakini ni sharti ifunzwe katika neno la Mungu ili iwe na matunda kama Mungu alivyoikusudia.
3. Katika kujibu madai ya Paulo, kuhani mkuu aliamuru waliokuwa karibu naye kumpiga kinywa chake Paulo.
4. Paulo, bila kujua ni nani aliyetoa amri hiyo kuwa ni kuhani mkuu, alitabiri kuwa Mungu angempiga aliyetoa amri hiyo.
5. Paulo alisema kuwa kwa sababu alitambua yeyote aliyeamuru apigwe kinywa bila ya kusikiliza swala lake ilikuwa ni kuvunja Sheria ya Musa (linga. Kumb.25:1,2).
6. Walipomweleza Paulo kwamba alinena maneno hayo juu ya kuhani mkuu, Paulo akaomba msamaha, akinukuu katika Sheria ya Musa (Kut.22:28).

### (2) (23:6-9) PAULO ALIGAWANYA BARAZA

1. Paulo alitambua kulikuwepo Mafarisayo na Masadukayo  katika baraza.
   a. Kama tulivyojifunza awali, Mafarisayo waliamini ufufuo, malaika, na roho, wakati Masadukayo hawakuamini hata moja ya hayo (linga. mst.8).
2. Ukiwa na ukweli huo akilini, Paulo alitangaza kuwa alikuwa Farisayo na alihukumiwa juu ya tumaini la ufufuo wa wafu.
   a. Alitambua kuwa maelezo hayo yangeligawa baraza.
3. Na hilo haswa ndilo lililotokea – baraza liligawanyika makundi mawili yanayopingana.
4. Hivyo wengine wakasema hatuoni baya lolote katika Paulo na kama malaika au roho alinena naye, baraza lisishindane na Mungu.

### (3) (23:10,11) JEMEDARI WA RUMI AMWOKOA PAULO NA BWANA ANENA NAYE

1. Jemedari alipoona kuwa Paulo anaweza kuraruriwa vipande vipande, Wayahudi wakorofi, aliwataka maaskari kumleta Paulo ndani ya ngome.
2. Usiku uliofuata, Bwana akamwambia Paulo awe na moyo mkuu kwa sababu alikuwa aende amshuhudie Bwana Rumi, kama alivyofanya Yerusalem.

### m. (23:12-15) BAADHI YA WAYAHUDI WAKAFANYA NJAMA ZA KUMWUA PAULO

1. Baadhi ya Wayahudi wakakusudia kumwua Paulo, wakajifunga kwa kiapo kwamba hawatakula ama kunywa hata wamemwua.
2. Watu hawa wakamwendea mkuu wa makuhani na wazee na walishauri kwamba walimwombe jemedari wa Rumi.
3. Maoni hayo yalikuwa waombe ruhusa ili Paulo aletwe mbele ya baraza (Sanhedrin) ili kumhoji zaidi maswali.

4. Bali kusudi lao haswa ilikuwa kumwua Paulo kabla hajakaribia Sanhedrin.

**n. (23:16-22) PAULO ALITAMBUA MBINU HIZO NA ALITAFUTA MSAADA TOKA KWA JEMEDARI WA RUMI**

1. Paulo alijufunza kuotea kwao toka kwa mpwa wake na akamwomba mmoja wa maakida kumpeleka mpwawe kwa jemedari.
2. Mpwawe Paulo akafunua mpango mzima kwa jemedari wa Rumi, ambaye akamwacha kijana aende, akiamuru asimweleze mtu yeyote kwamba alimweleza habari hizo.

**o. (23:23-30) JEMEDARI AMPELEKA PAULO KWA FELIKI LIWALI KATIKA KAISARI**

1. Jemedari akaamuru maaskari 200, wapanda farasi 70, na wenye mikuki 200 kumchukua Paulo kwa Feliki liwali usiku.
2. Katika mst.26 tunajifunza jina la jemedari wa Rumi aliitwa Klaudio Lisia na kwamba alituma barua pamoja na Paulo na maaskari.
3. Katika waraka huo, Klaudio Lisia akimfahamisha kuwa Paulo hakuwa na hatia ya kustahili kuuawa au kufungwa, bali alishitakiwa kufuatana na maswala ya sheria ya Kiyahudi.
4. Jemedari pia aliandika kwamba washitaki wake Paulo wakaeleze mashitaka yao mbele ya Feliki.

**2. (23:31-26:32) AKIWA KAISARIA**
**a. (23:31-35) PAULO ATUMWA KWA FELIKI**

1. Askari wakamkabidhi Paulo na barua kwa Feliki Kaisaria.
2. Feliki akamhifadhi Paulo katika nyumba ya uliwali ya Herode hata watakapofika washitaki wake Kaisaria.

**b. (24:1-9) WASHITAKI WA PAULO WAWAKILISHA MASHITAKA MBELE YA FELIKI**

1. Baada ya siku tano kuhani mkuu na wazee wakashuka huko wakiwa na msemi mmoja (haswa yaani wakili) aliyeitwa Tertulo ili kuwakilisha ushahidi mbele ya liwali juu ya Paulo.
2. Tertulo akimsifia Feliki kwa uongo (flatter), kisha akamwomba asikilize maneno machache toka kwake.
3. Turtulo alisema mambo yafuatayo kuhusu Paulo:
   a. Alikuwa pigo (plague).
   b. Mwanzilishi wa fitina katika Wayahudi wote.
   c. Ni kichwa cha madhhebu ya Wanazorayo.
   d. Alijaribu kulitia hekalu unajisi (kulifanya chafu au kuliharibu).
4. Kisha Tertulo alidai kwamba Wayahudi walimkamata Paulo na kunuia kuamua kwa sheria yao, lakini Lisia akaja na kumtoa Paulo katikati ya ghasia.
5. Tertulo alimalizia hoja zake kwa kusema Feliki angetambua mambo hayo kwa kumdadisi Paulo.
6. Wayahudi walikubaliana mambo hayo kuwa ni kweli.

**c. (24:10-21) PAULO AJIBU MADAI HAYO**
**(1) (24:10-13) ALISEMA HASINGEWEZA KUTHIBITISHA MADAI HAYO**

1. Paulo alibanisha kuwa si zaidi ya siku kumi na mbili tangu apande kwenda Yerusalem kuabudu.

   a. Kwa kusema hivi, alikuwa akithibitisha kwamba hakuwepo Yerusalem muda wa kutosha hata kuunda fitina baina ya Wayahudi kama walivyomshitaki.
2. Zaidi, Paulo alisema kwamba alipokuwa hapo, Wayahudi hawakumkuta akifanya mambo haya yafuatayo:
   a. Mjadala na mtu yeyote hekaluni.
   b. Kuhamasisha mkutano kufanya ghasia, ama hekaluni au mjini.
3. Paulo alihatimisha kwa kusema wasingeweza kuthibitisha madai yao juu yake.

**(2) (24:14-16) ALITOA MUHTASARI WA IMANI NA MAMBO AYAFANYAYO**

1. Paulo alikiri kumwabudu Mungu na kuamini kilichoandikwa katika Agano la Kale.
2. Pia alieleza kuwa na tumaini katika Mungu kwamba kungelikuwa na ufufuo wa wafu.
3. Zaidi sana, ufufuo huo ungejumuisha walio haki na wasio haki (linga. Yoh.5:28,29).
4. Kisha Paulo alibainisha kuwa alijaribu wakati wote kuishi kwa dhamiri safi mbele za Mungu na wanadamu (lengo la kuheshimiwa)!

**(3) (24:17-21) PAULO ALIELEZA KILE AMBACHO HASWA ALIKUWA AKIFANYA YERUSALEM ALIPOSHITAKIWA**

1. Paulo alieleza kuwa sababu haswa ya kufika Yerusalem ilikuwa kupeleka msaada wa mpendo kwa taifa lake.
2. Pili, Paulo alisema baadhi ya Wayahudi kutoka Asia walimkuta hekaluni, pasipo umati, na wala bila ya usumbufu wowote aliosababisha!
3. Kisha Paulo alitoa changamoto kwa Wayahudi wote waliokuwepo watoe ushahidi wowote kwa maandishi ni nini kibaya alichoshitakiwa na baraza la Sanhedrin.
4. Mwisho, Paulo alieleza kwamba kitu pekee walichokuwa kinyume nami ni maelezo yake mbele ya baraza kwamba alikuwa mbele yao kwa sababu ya imani ya ufufuo.

**d. (24:22-27) FELIKI AAHIRISHA KIKAO / PAULO AKATOA HOJA MBELE YAKE / FESTO AKACHUKUA NAFASI YA FELIKI**

1. Feliki alaahirisha kikao, akisema angemsubiri hata jemedari Lisia aje hata atoe waamuzi.
2. Feliki alimpatia Paulo uhuru fulani ikiwa pamoja na marafiki zake kumhudumia na kumtembelea.
3. Baadaye, Feliki na mkewe Myahudi Drusila walituma watu kumleta Paulo ili kusikia juu ya imani katika Kristo.
4. Paulo alijadiliana nao kuhusu masomo makubwa matatu:
   a. Haki –
      (1) Haki katika mahusiano ya baina ya mtu na Mungu.
   b. Kuwa na kiasi –
      (1) Mwanahistoria Josephus alitoa habari kwamba Feliki na Drusila walikuwa wakiishi katika uzinzi.
      (2) Basi, kuwa na kiasi lilikuwa somo sahihi kwa Paulo kulileta ili watafakari!
   c. Hukumu inayokuja –
      (1) Wanaume na wanawake kila mahali wanapaswa kukumbuka siku ile ambayo tutasimama mbele za Bwana kutoa hesabu kwake (linga. 17:30,31; Mhu.12:13,14; Rum.14:12)!
5. Paulo alipozungumza maneno hayo makali, Feliki aliogopa (linga. 2 Kor.5:10,11)!
6. Tafadhali tulia kwa muda kidogo na fikiria kuhusu moyo mkuu wa Paulo kuzungumza maneno haya makali kwa Feliki.
   a. Feliki alikuwa na uwezo wa kumwachilia Paulo au kumfunga.

b. Kwa wengi wetu leo, jaribu lingekuwa kujaribu kumpendeza Feliki kwa kunena maneno laini na rahisi, ujumbe usiokwaza.
c. Paulo alimpenda Bwana na Feliki zaidi kuliko kusema hivyo!
d. Mfano bora kwa wazee, wahubiri, waalimu, na kila Mkristo leo (Efe.4:15; Gal.4:16)!

7. Hata hivyo, Feliki alimweleza Paulo kwamba angemwita muda wake mwafaka!
8. Baada ya siku hiyo, Feliki alizungumza na Paulo mara nyingi, akitarajia kupewa fedha na Paulo (rushwa)!
9. Baada ya miaka miwili, Porkio Festo alimbadili Feliki kama liwali.
10. Feliki alitaka kuwapendeza Wayahudi, hivyo akamwacha Paulo gerezani.

### e. (25:1-5) FESTO AKAENDA YERUSALEM NA KUWAOMBA WAYAHUDI WAPELEKE MASHITAKA JUU YA PAULO KAISARIA

1. Wayahudi walikwenda Kaisaria na kutoa malalamiko makubwa juu ya Paulo ambayo hawakuweza kuyathibitisha.
2. Katika mst.8 Paulo alijibu kwa kukana kutenda jambo lolote baya juu ya mambo yafuatayo:
   a. Sheria ya Wayahudi.
   b. Hekalu.
   c. Kaisaria.
3. Kwa sababu Festo alitaka kuwapendeza Wayahudi, alimwuliza Paulo kwenda Yerusalem kuhukumiwa katika baraza (Sanhedrin) mbele ya Festo ("ukahukumiwe huko mbele yangu").
4. Paulo alijibu kwa kutoa mambo yafuatayo:
   a. Alikuwa akisimama katika kiti cha hukumu cha Kaisari ambapo angehukumiwa.
   b. Hakuwakosea jambo lolote baya Wayahudi, kama Festo alivyotambua.
   c. Alikuwa tayari kufa kama alifanya jambo lolote lililostahili kufa.
   d. Kama hakuwakosea Wayahudi, hakuna mtu angeweza kumpeleka huko kwao kihalali.
   e. Alitaka rufani kwa Kaisari (jambo ambalo lilikuwa halali kwa raia wa Rumi).
5. Festo alisema kwa kuwa Paulo alikata rufani kwa Kaisari, angepelekwa huko kwake.

### f. (25:13-22) FESTO AJADILI KESI YA PAULO NA MFALME AGRIPA, AMBAYE ALIKUBALI KUMSIKILIZA PAULO

1. Wakati fulani Mfalme Agripa na Bernike walimtembelea na akawaeleza kuhusu Paulo.
2. Katika mst.15-19 Festo aliipitia kesi ya Paulo mbele ya Agripa.
3. Festo alifupisha kesi hiyo kwa kusema kulikuwa na baadhi ya maswali kuhusu dini ya Kiyahudi na mtu anayeitwa Yesu ambaye alikufa lakini Paulo anadai kuwa yu hai.
4. Kisha Festo akamweleza Agripa kuhusu rufani ya Paulo kwa "Augusto" (Kaisari).
5. Agripa aliomba amsikilize Paulo, na Festo akaahidi kufanya hivyo siku iliyofuata.

### g. (25:23-27) PAULO ALETWA MBELE YA FESTO NA AGRIPA

1. Siku iliyofuata Festo alimleta Paulo mbele ya Agripa, maakida wakuu, na watu wakuu wa mji na kwa ufupi akasimulia tena kesi yake mbele yao.
2. Kisha Festo alikubali kuwa hana jambo la hakika kumwandikia Kaisaria hivyo alikuwa akitarajia Agripa angemchunguza Paulo na kuona kitu chochote cha kumwandikia Kaisaria.
3. Festo alitambua kuwa si sahihi kumtuma mfungwa Rumi bila kuonyesha bayana mashitaka juu yake.

### h. (26:1-32) PAULO ANAJITETEA MBELE YA AGRIPA

1. Paulo alimsihi Agripa kumsikiliza kwa uvumilivu kwa kuwa alikuwa anafahamu desturi za Wayahudi.

2. Paulo alibainisha kwamba kuanzia ujana wake aliishi kama Myahudi, ikiwa pamoja na umishi wake uliofuata katika madhehebu yenye msimamo mkali, Mafarisayo (linga. 23:3).

### (2) (26:6-8) IMANI YAKE NDIYO SABABU HASWA YA KUSHITAKIWA

1. Paulo alieleza kuwa alihukumiwa kwa tumaini lile la ahadi ya Mungu lililotolewa kwa baba zao Israeli, k.m., tumaini la ufufuo wa wafu toka kwa watu.
2. Kisha Paulo alimwuliza Agripa na wengine kwa nini walifikiri ni swala lisiloaminika kwamba Mungu anafufua toka kwa wafu.

### (3) (26:9-11) MATESO YAKE YA AWALI ALIYOFANYA KWA UKRISTO

1. Katika mistari hii Paulo alirudia habari yake ya kutesa Ukristo (linga. 22:4,5, 19).
2. Katika mst.11 jambo moja aliongeza katika habari hii ni kwamba aliwashurutisha Wakristo kukufuru, k.m., kunena mabaya juu ya Bwana.

### (4) (26:12-18) MAONO YAKE YA YESU ALIYEFUFUKA AKIWA SAFARINI KWENDA DAMESKI

1. Katika mst.12-15 Paulo alirudia habari ya maono yake ya Yesu akiwa safarini kwenda Dameski (linga. 9:3-8; 22:6-11).
2. Katika mst.16-18 Paulo alifunua taarifa zingine ambazo hazipatikana katika sehemu zingine mbili.
3. Kwanza, sababu tatu zilitolewa za Bwana kumtokea Paulo, kama ifuatavyo:
   a. Kumfanya awe mtumishi.
   b. Kumfanya awe shahidi wa mambo aliyoyaona.
   c. Kumfanya awe shahidi wa mambo ambayo Yesu angeyafunua kwake.
4. Pili, kwamba Yesu angemwokoa Paulo kutoka kwa Wayahudi na Mataifa, na angemtuma aende kwa Mataifa.
5. Yesu alikuwa na sababu tatu za kumtuma Paulo aende kwa Mataifa, kama ifuatavyo:
   a. Kufumbua macho yao (kwa njia ya kuhubiri injili).
   b. Kuwageuza waache giza (dhambi) kuelekea nuru (haki), na
   c. Wazianche na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu.
6. Sababu mbili za kufumbua macho yao na kuwageuza ili waweze:
   a. Kupokea msamaha wa dhambi.
   b. Kupokea urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani katika Kristo.
      (1) Urithi ni uzima wa milele uliohifadhiwa mbinguni (1 Pet.1:3,4).
7. Tafadhali kumbuka kwamba njia ambayo Mungu huwatakasa watu (kuwatenga kando) ni kupitia neno lake la ajabu (linga. Yoh.17:17).
8. Tunapoona maelezo haya kutoka kwa Yesu kwenda kwa Paulo, tunatakiwa kuvutiwa na hitaji, ubora, na fursa kubwa ya kueneza injili kwa maneno na matendo.
9. Hizo ndizo njia pekee ambazo zitageuza watu kutoka katika maisha maovu na kuwa watumishi wa Mungu, na hivyo kupokea msamaha na urithi!

### (5) (26:19-23) UTIIFU WAKE KWA YALE MAONO

1. Paulo alimwambia Agripa kwamba alitii mara mora wito wa Yesu kuhubiri ujumbe wake wenye utukufu wa wokovu.
2. Katika mst.20 tunaona kwamba miongoni mwa mambo aliyohubiri Paulo ni hitaji la kufanya mambo yafuatayo:
   a. Toba, k.m., kuzingatia huzuni iliyo ya jinsi ya Mungu, kugeuza akili (linga. 2:38).

   b. Kumwelekea Mungu (hili ni pamoja na kugeuka toka katika maisha ya dhambi ya kale pia pamoja na msamaha wa dhambio (linga. 3:19).
   c. Kufanya mambo yanayolingana na toba, k.m., kama tumetubu kweli, watu wataweza kutambua kabisa mabadiliko yetu katika matendo, mabadiliko katika maisha yetu (linga. Mt.3:8; Kol.3:1-23).
3. Katika mst.21 Paulo kwa ujasiri alieleza kwamba mahubiri yake ya ujumbe huo ndiyo sababu haswa iliyowafanya Wayahudi wamkamate hekaluni na kujaribu kumwua.
4. Walakini, kwa msaada wa Mungu, Paulo alipona na ameweza kuhubiri mambo ambayo Musa na manabii wengine walisema kuwa yangetimia.
5. Mambo hayo ni pamoja na:
   a. Kristo angeteseka (Lk.24:26, 44-46; Isa.53).
   b. Angekuwa wa kwanza kufufuka toka kwa wafu, na
   c. Angetangaza nuru kwa Wayahudi na Mataifa.
6. Maelezo kwamba Kristo angefufuka kwanza kutoka kwa wafu ni ya kufurahisha!
7. Ni kweli hilo kwa sababu Kristo hakika si wa kwanza kufufuka toka kwa wafu kwa mpangilio wa wakati.
8. Kwa mfano, Yesu alimfufua Lazaro toka kwa wafu kabla ya Yesu mwenyewe kufufuka toka kwa wafu.
9. Basi, maelezo kwamba Kristo angekuwa wa kwanza kufufuka toka kwa watu yana maana gani haswa?
10. Inamaanisha tu kwamba yeye alikuwa wa kwanza katika cheo, nguvu, na ofisi ambaye angefufuka kutoka kwa wafu.
    a. Angekuwa moja ya mtu muhimu, mkuu, kichwa cha hao waliofufuka toka kwa wafu.
    b. Alifufuka kutoka kwa wafu, asife tena!
    c. Linga. Kol.1:18; Ufu.1:18.

#### i. (26:24-32) FESTO ATAFSIRI / PAULO AMWELEKEZA AGRIPA

1. Kufikia hapa Festo alimtafsiri Paulo na kusema alikuwa hivyo kwa sababu ya kusoma kwake kwingi kulimfanya kuwa na wazimu!
2. Paulo alijibu kuwa hakuwa na wazimu. Bali alikuwa akinena maneno ya kweli na ya maana na Agripa alijua mambo hayo kwa sababu yalifanyika peupe.
3. Kisha Paulo akamwuliza Agripa iwapo anaamini manabii na bila shaka alisema kwamba aliamini.
4. Agripa alijibu kwa kusema Paulo, kwa maneno machache unadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo!
5. Paulo alieleza nia yake kubwa kwamba si tu Agripa, bali kila mmoja alikuwepo pale angekuwa kama yeye (k.m., Paulo kama Mkristo) isipokuwa kwa “vifungo” (kufungwa).
6. Baada ya Paulo kusuma, Agripa, Festo, na wengine waliokuwepo wakasimama na kuzungumza wao kwa waoi.
7. Walikubaliana kuwa Paulo hakufanya jambo lolote lililostahili kufa ama kufungwa na kusema kama asingekata rufani kwa Kaisari, angeachiwa huru.

### (3) (27:1-28:15) PAULO AENDA ROMA

#### (a) (27:1-8) WAKISAFIRI KATIKA UPEPO WA MBISHO KUELEKEA BANDARI NZURI

1. Iliamuriwa kumpeleka Paulo Italia pamoja na wafungwa wengine chini ya usimamizi wa akida Yulio.
2. Waliokuwa pamoja na Paulo ni Aristarko wa Thesalonike (linga. 20:4) na Luka (tuka…).
3. Kulingana na mst.3 kituo chao cha kwanza kilikuwa Sidoni ambako Yulio amlimfadhili Paulo vizuri kwa kumruhusu kuwaona rafiki zake na wakamtunza.

4. Kutoka huko, waling'oa nanga kuelekea kaskazini mwa Kipro na kutua katika mji wa Mira katika jimbo la Likia.
5. Katika Mira akida aliiona merikebu ikielekea Italia na akawapandisha Paulo na wengine ndani.
6. Walisafiri polepole, kwa shida wakafika Nido, kisha wakapita chini (under the shelter) ya kisiwa cha Krete, wakapita Salmone hata mahali palipoitwa Bandari Nzuri (Fair Heavens).

### b. (27:9-13) ONYO LA PAULO JUU YA HATARI LAPUUZWA

1. Katika mst.9 marejeo yametaja "kufunga" kulipokwisha.
   a. Marejeo haya ni wazi kwamba kufunga wakati wa Siku ya Upatanisho.
   b. Ni karibia na mwezi wa Oktoba.
   c. Kusafiri kwa merikebu kipindi hicho ilikuwa hatari sana.
2. Ukizingatia hatari hiyo, Paulo alimwonya akida na wengine kama ifuatavyo:
   a. Safari yao ingekuwa na madhara makubwa.
   b. Wangepoteza shehena nyingi.
   c. Pia kupotelewa na maisha ya watu wengi.
3. Akida alidharau maonyo ya Paulo, akaamua kumsikiliza mmiliki wa merikebu na nahodha kinyume chake.
4. Kwa kuwa Bandari Nzuri haikufaa kukaa majira ya baridi, waliamua kujaribu kung'oa nanga kwenda bandari ya Foinike, wakielekea karibu na kisiwa cha Krete.

### c. (27:14-20) UPEPO MKALI UKASUKUMA MERIKEBU, NA KUKATA TAMAA MIONGONI MWA WASAFIRI

1. Katika mst.13-17 tunajifunza kwamba muda mfupi baada ya kuondoka Bandari Nzuri wakakabiliana na upepo mkali sana ulioitwa "Eurakilo" ambao uliishinda merikebu.
2. Katika mst.18,19 merikebu ilipigwa sana na tufani wakaamua kupunguza uzito wa mizigo kwa kutupa shehena baharini.
3. Katika mst.20 baada ya kutoliona jua ama nyota kwa siku tatu wakakata tamaa ya kuokoka.

### d. (27:21-26) UNABII WA PAULO WA KUVUNJIKIWA NA MERIKEBU PASIPO WATU KUPOTEZA MAISHA

1. Baada ya kukosa chakula kwa siku nyingi, Paulo aliwakemea kwa kutomsikia alipowaonya mara ya kwanza.
2. Kisha, katika mst.22-26, aliwaambia kuwa na moyo mkuu kwa sababu hapana nafsi ingepoteza uhai, isipokuwa merikebu.
3. Aliwaeleza jinsi malaika wa Mungu alivyomweleza:
   a. Usiogope.
   b. Huna budi kusimama mbele ya Kaisari.
   c. Mungu amekupa watu wote waliokuwa wakisafiri pamoja naye.
4. Katika mst.25 na 26 Paulo alithibitisha imani juu ya yale aliyomweleza malaika, walakini, hatuna budi kupwelea katika kisiwa fulani.

### e. (27:27-32) BAADHI YA ABIRIA WALIJARIBU KUKIMBIA BILA MAFANIKO

1. Usiku wa kumi na nne baharia walidhani kuwa wamekaribia nchi kavu fulani.
2. Walipopima kina cha maji, wakatambua kuwa kina kilikuwa kikipunga zaidi na zaidi, kuelekea nchi kavu.
3. Ili kuzuia watu kukimbilia nchi kavu, wakatupa nanga nne za tezi na kuomba kuche.

4. Baada ya hapo, baadhi ya baharia walijaribu kukimbia kutoka katika merikebu, kwa kutumia madhua ndogo.
5. Walakini, Paulo akamweleza akida kama baharia hawatabakia ndani, hawataweza kuokoka.
6. Kama matokeo ya maonyo ya Paulo, maaskari wakakata kamba, wakifanya mashua kuangukia majini, ili kuzuia baharia wasitui hizo mashua kukimbia.

### f. (27:33-37) PAULO ALIWASHAURI WOTE KULA NA KUWAKUMBUSHA KWAMBA HAKUNA ATAKAYEUMIA

1. Baada ya kutokula kwa siku kumi na nne, Paulo aliwatia moyo kula ili waweze kupona, kwa kuwa hakuna hata mmoja wao angaangamia katika tufani.
2. Kisha Paulo akamshukuru Mungu mbele ya watu wote na kula chakula.
3. Hilo likawatia moyo wengine kula chakula.
4. Katika mst.37 Luka alifunua kuwa walikuwa 276 ndani ya merikebu.

### g. (27:38-44) WAKAONA NCHI / MERIKEBU IKAFIKA NCHI KAVU / WATU WOTE WAKAFIKA NCHI KAVU SALAMA (MALTA)

1. Walipokuwa wote wamekula vya kutosha, wakapunguza shehena zaidi, pamoja na ngano waliyoichukua.
2. Kulipopambazuka, waliiona nchi na kujaribu kukimbilia nchi kavu.
3. Walakini, walifikia mahali palipokutana bahari mbili kabla ya kufikia nchi kavuna merikebu ikaanza kuvunjika kwa nguvu za mawimbi.
4. Katika mst.42 tunajifunza kuwa askari walitaka kuwaua wafungwa wote ili wasitoroke.
5. Lakini, akida akitaka kumwokoa Paulo, hivyo akazuia wasifanye kama walivyokusudia.
6. Hivyo akida akawaambia wenye uwezo wa kuogolea wajitupe baharini na kufika nchi kavu.
7. Nao waliosalia wakasafiri kwa vipande vya bahari.
8. Kama matokeo ya matendo hayo, wote wakafika salama salimini nchi kavu, kama vile Paulo alivyotabiri!

### h. (28:1-6) KUPOKELEWA KWA UKARIMU NA WENYEJI / PAULO ANG'ATWA NA NYOKA

1. Walipofika katika kisiwa salama salimini, wakatambua kuwa kisiwa kiliitwa "Melita."
2. Wenyeji wakawafanyia fadhili zisizo za kawaida kwa kufanya mambo mawili:
   a. Ili wajisikie wamekarimiwa.
   b. Kuwawashia moto ili kuwatia joto kwa sababu mvua ilikuwa ikinyesha na palikuwa na baridi.
3. Walakini, Paulo alipokuwa akiweka kuni motoni, nyoka mwenye sumu ya kufisha akamzonga-zonga mkononi.
4. Wenyeji walipoona hivyo, walisema kwamba Paulo alikuwa mwuaji aliyekuwa akitendewa haki na hakuwa na sababu ya kuishi.
5. Walitarajia Paulo kuvimba na ghafula kuanguka na kufa.
6. Lakini Paulo akamsukutia nyoka katika moto na hakudhirika kabisa, wenyeji wakabidilisha mtazamo wao juu yake.
7. Wakamtazama kwa muda mrefu na walipohakikisha kwamba hakuna baya lililomfika waliamini kuwa alikuwa mungu!
8. Huu ni utimilifu mkubwa wa Mk.16:17,18.
   a. Kwa nia njema na upendo wote, tunauliza hao wanadai kuwa wana uwezo wa kutenda miujiza hawawezi kufanya hivi leo.
   b. Wanadai kuwa na uwezo sawasawa na Paulo na wengine waliokuwa karne ya kwanza.

c. Wanadai kuweza kufanya mambo mengine katika mistari hii miwili ambayo ni rahisi kuiiga.
d. Walakini, hawawezi kunywa vitu vya kufisha na kung'atwa na nyoka bila ya kudhurika.
e. Sababu inayowafanya wasiweze kufanya hivyo ni dhahiri na rahisi.
f. Hawana vipawa vya miujiza vya Roho Mtakatifu na madai yao ni uongo kabisa!

### i. (28:7-10) WEMA ZAIDI UNADHIHIRIKA

1. Katika mistari hii tunajifunza kwamba Publio, mmoja wa wakuu wa wenyeji wa kisiwa hicho, aliwafadhiri Paulo na wenzake kwa uangalifu kwa siku tatu.
2. Paulo alipotambua kwamba baba yake Publio alikuwa mgonjwa wa homa na kuhara, akaomba, akamwekea mikono juu yake, na kumponya.
3. Kisha wengine waliokuwa na maradhi wakamjia Paulo na wakaponywa.
4. Kuonyesha shukurani zao, wenyeji wakamheshimu Paulo na wenzake na kuwapatia vitu vingu muhimu walipoondoka hapo.

### j. (28:11-15) KUTWEKA KUELEKEA RUMI, WALITUA KATIKA PUTEOLI

1. Baada ya miezi mitatu Paulo aliondoka Melta na kuelekea Rumi.
2. Kwanza wakatua Sirakusa, kisha Regio, na kisha Putelio ambako waliwakuta ndugu ambayo waliwaalika kukaa siku saba.
3. Tena, walivyokuwa wakielekea Rumi, walikutana na ndugu kutoka mbali walifika kuwalaki mpaka Soko la Apio na Mikahawa Mitatu (Taverns).
4. Kabla ya kuondoka sehemu hii, tafadhali zingatia maelezo mazuri mwishoni mwa mst.15. Paulo alipoona ndugu zake, akamshukuru Mungu na akatiwa moyo!
   a. Huu ni mfano mkubwa wa furaha tunayopaswa kuwa nayo kuwaona na kukutana na ndugu katika Kristo, hata ingawa hatujawahi kukutana nao hapo kabla.
   b. Ni faraja na amani ya moyo kiasi gani kuweza kusafiri dunia nzima na kukutana washiriki wenzetu ambao famili ya Mungu!
   c. Tunafurahia, wamefarijika, na kuwa na amani ya moyo kwa sababu zifuatazo:
      (1) 2 Pet.1:1.
      (2) Yuda 3.
      (3) 1 Yoh.3:1.
      (4) Rum.8:16,17.
      (5) Rum.12:5,15; 1 Kor.12:26.
      (6) 1 Thes.5:11.
      (7) Ebr.10:24.
      (8) Kol.2:2.
      (9) Yoh.13:34,35.
      (10) 1 Yoh.3:16.
   d. Sababu kama hizi ndizo zilimpekea Paulo kumshukuru Mungu na kutiwa moyo alipowakuta ndugu zake wapendwa katika Kristo.

### 4. (28:16-31) PAULO ALIHUBIRI GEREZANI KWA MIAKA MIWILI

#### a. (28:16-22) PAULO AWASILI RUMI / ALIZUNGUMZA NA VIONGOZI WAYAHUDI WALIOTAKA KUSIKIA MAONI YAKE

1. Walipowasili Rumi akida aliwakabidhi wafungwa wengine kwa mkuu wa kikosi, lakini Paulo alindwe na askari mmoja tu.
   a. Jambo hili lilikuwa linaonyesha heshima kubwa aliyopewa Paulo na imani aliyokuwa nayo akida juu yake.

2. Baada ya siku tatu Paulo alikutana na viongozi wa Kiyahudi na kuzungumza nao.
3. Aliwahakikishia kwamba hakufanya jambo lolote kinyume na "watu wetu" (Wayahudi).
4. Kisha akaelezea jinsi alivyoletwa mbele ya watumishi wa Rumi ambao hawakuona jambo lolote baya lililostahili kifo.
5. Walakini, Wayahudi walivyopinga uamuzi huo, Paulo akaamua akate rufani kwa Kaisari kwa usalama wake mwenyewe, wala si kwamba anawashitaki Wayahudi kwa lolote.
6. Tena, katika mst.20, Paulo aliwaarifu Wayahudi kwamba alifungwa kwa minyonyoro kwa sababu ya "tumaini la Israeli."
   a. Haya ni marejeo dhahiri kwa tumaini la muda mrefu la Israeli juu ya Masihi ambaye alikuwa aje duniani.
   b. Basi, Paulo alikuwa akisema kwa sababu ya kumhubiri Yesu kama Masihi ndicho kilichofanya awe mfungwa.
   c. Ndiyo maana Paulo mara nyingi alijitambulisha mwenyewe kuwa "mfungwa wa Bwana" (Efe.3:1; 4:1)!
7. Katika kujibu, Wayahudi walisema hawakuona lolote baya juu ya Paulo kutoka kwa ndugu zao Wayahudi.
8. Kwa nyongeza, walitaka kusikia alichotaka kusema kwa sababu "madhehebu hiyo" (k.m., Ukristo) ulinenwa kinyume kila mahali.

### b. (28:23-29) PAULO ANENA TENA, AKINUKUU MAANDIKO / KUTOKUPATANA WAO KWA WAO

1. Wayahudi wakachagua siku ambayo wengi wangemjia Paulo kumsikiliza.
2. Kwa wakati huo Paulo akawashawishi juu ya ufalme (kanisa) wa Mungu na Yesu.
3. Na akafanya hivyo kwa kunukuu katika Sheria ya Musa na manabii kuanzia asubuhi hata jioni.
   a. Kwa bahati nzuri, kinyume na baadhi na wazee, wahubiri, na waalimu wa leo, Paulo aliamini katika kuhubiri na kufundisha kwa kunukuu maandiko (linga. 1 Pet.4:11; Isa.8:20; 2 Tim.4:1ff)!
4. Kama ilivyo kawaida, wengine walipomsikia Paulo wakaamini kuwa maneno yake ni kweli na wengine wakachagua kutokuamini.
5. Kabla hawajaondoka, Paulo akasema kwamba Roho Mtakatifu alinena vyema kupitia Isaya maneno yaliyoandikwa Isa.6:9,10 juu ya taifa la Israeli.
6. Tafadahli uangalia hoja za nguvu zifuatazo zinazopatikana katika unabii huu wa ajabu:
   a. Watu wangesikia, lakini wasingeelewa.
   b. Watu wangeona, lakini wasingetambua (k.m., wasitathimini haswa katika fahamu zao).
   c. Mioyo yao imepumbaa (k.m., wala wasiingize ndani waliyokuwa wakipokea; kushupaa).
   d. Walifanya masikio yao kuwa magumu kusikia.
   e. Walifumba macho yao wasije wakaona.
   f. Kama matokeo, hawakuweza kuona tena, kusikia, au kuelewa ili wasije wakamgeukia Bwana (kutubu na kutii) wapate kuponywa.
7. Mambo ya ajabu yanayowabainisha Wayahudi wengi kipindi hiki cha Paulo, kama tulivyoona mara nyingi katika somo letu katika Matendo!
8. Paulo alihatimisha kwa kuwaeleza Wayahudi kwamba kwa kuwa walifanya mioyo yao kuwa migumu, wokovu wa Mungu aliupeleka kwa Mataifa – na wangesikia!
9. Waliposikia maneno haya, Wayahudi wakaondoka na wakashindana sana kati yao wenyewe.

### c. (28:30,31) KWA MIAKA MIWILI, PAULO ALIHUBIRI UFALME WA MUNGU

1. Paulo alikuwa katika nyumba yake aliyopanga na kuwakaribisha watu wote waliomwendea.

2. Na katika mst.31 tunaona mwisho mzuri wa kitabu hiki kizuri ajabu katika shughuli ya Paulo ilibainishwa kama ifuatavyo:
   a. Alihubiri kuhusu ufalme (kanisa) wa Mungu.
   b. Alihubiri mambo kuhusu Bwana Yesu Kristo.
   c. Alifanya hivyo kwa ujasiri mkubwa (linga. 2 Tim.1:12).
   d. Na hakuna mtu yeyote alithubutu kumkataza (linga. 20:23,24)!